

Maarifa ya Uislamu  
Darasa la Watu Wazima

Juzuu ya 3  
(Toleo la pili)

Historia ya kushushwa Qur-an 96:1 - 5, inatukumbusha na kutufunza kuwa Mtume (s.a.w) alianza kushushiwa wahy kwa kupewa amri ya kusoma. Hivyo, hapana shaka kabisa kuwa Elimu ndiyo Faradhi ya kwanza inayopaswa kutekelezwa na kila Muislamu tangu zama za Mtume (s.a.w) hadi sasa.

Kusoma au kutafuta elimu kumefanywa kuwa Faradhi ya kwanza ili kumuwezesha mja kumjua Mola wake na kumpatia ujuzi wa kutosha juu ya kanuni na sheria alizoiweka Allah (s.w) zikifuatwa katika kila kipengele cha maisha ya kila siku, hupatikana uadilifu na amani ya kweli katika jamii.

Hii ni juzuu ya tatu ya maarifa ya Uislamu katika mfululizo wa juzuu 7 za masomo kwa Darasa la Watu Wazima unaokusudia kumuwezesha mja na jamii kufikia kilele hicho.

Mfululuzo huu wa masomo katika juzuu 7 ni:

1. Lengo la Maisha ya Mwanadamu
2. Nguzo za Uislamu
3. Qur-an na Sunnah
4. Familia ya kiislamu
5. Jamii ya Kiislamu
6. Historia ya Kuhuisha Uislamu
7. Kuhuisha Uislamu katika Jamii

Qur-an na Sunnah Juzuu ya 3 (Toleo la pili)

# Qur-an na Sunnah



Islamic Propagation Centre

Maarifa ya Uislamu

Darasa la Watu Wazima

Juzuu 3

# **Qur' an na Sunnah**

Toleo la Pili

Islamic Propagation Centre

© Islamic Propagation Centre

Maarifa ya Uislamu  
Darasa la Watu Wazima

Juzuu ya Tatu: **Qur-an na Sunnah**  
Toleo la Pili

Toleo la kwanza, 23 Desemba, 2003  
Nakala 1000  
Toleo la Pili, Oktoba, 2007  
Nakala 1000

Kimeandikwa na **Islamic Propagation Centre**  
P.O.BOX 55105, simu 022-2450403  
Dar es Salaam,  
**Tanzania.**

Kimechapwa na **Afroplus Industries (Ltd)**  
P.O.BOX 32427, Tel: 022 - 2773751  
Dar es Salaam, Tanzania.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## Neno la awali la toleo la Pili

Sifa zote njema anastahiki Allah (s.w) aliye Bwana Mlezi wa walimwengu wote. Rehema na amani zimwendee Mtume Muhammad (s.a.w) na ahli zake pamoja na wale wote wanaofuata mwenendo wake na kuliendea kwa hima lengo la kuletwa kwake la kuufanya Uislamu utawale mifumo yote ya maisha ya jamii.

Tunamshukuru Allah (s.w) kwa kutuwezesha kutoa toleo hili la pili la juzuu ya tatu (Qur'an na Sunnah ) katika mlolongo huu wa utoaji wa maarifa ya Uislamu kwa "Darasa la watu wazima". Toleo hili limeboreshwa zaidi na sura zake zimepangwa kama ifuatavyo:

- . Utangulizi
- . Qur'an
- . Mafunzo maalumu ya sura zilizochaguliwa
- . Mafunzo ya sura zilizochaguliwa katika juzuu Amma
- . Sunnah na Hadith
- . Mwenendo wa muislamu

Matarajio ni kwamba toleo hili litawawezesha wasomaji kwa tawfiq ya Allah (s.w) kukiendea kila kipengele cha maisha yao kwa mujibu wa Qur'an na sunnah hatimaye kuweza kusimamisha Uislamu katika jamii.

Kwa kuzingatia kuwa kazi ya binaadamu haiwezi kuepokana na mapungufu, tunawaomba wasomaji wa juzuu hizi wavumilie mapungufu yale yanayovumilika na watoe masahihisho, maoni na mapendekezo yao kwa lengo la kuboresha mafunzo haya ili lengo tarajiwa liweze kufikiwa kwa wepesi na kwa ufanisi.



Pia tunachukua fursa hii kuwashukuru na kuwaomba dua wale wote waliochangia na wanaoendelea kuchangia utoaji na uboreshaji wa mafunzo haya. Allah (s.w) awalipe kheri nyingi hapa duniani na akhera.



رَبَّنَا آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا  
مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٠﴾

*Mola wetu! Tupe rehema zinazotoka kwako na tutengenezee uongofu katika kila jambo letu (18:10)*



# YALIYOMO

Neno la Awali. ....	(i)
Utangulizi. ....	(vii)

<b>Sura ya kwanza:</b> .....	1
Qur'an .....	1
Qur'an na majina yake. ....	1
Orodha ya sura na zilimoshuka. ....	7
Wanaongozowa na Qur'an. ....	11
Historia ya kushka Qur'an .....	14
Sura za Makkah na Madina. ....	19
Orodha ya Sura za Makkah. ....	20
Orodha ya Sura za Madina. ....	23
Madai ya Makafiri dhidi ya Qur'an. ....	24
Namna ya Kuiendea Qur'an. ....	104
Zoezi la kwanza .....	109

<b>Sura ya Pili.</b> .....	111
Mafunzo maalumu. ....	111
Sifa za waumini. ....	111
Sifa za wanafiki. ....	153
Maadili na malezi ya jamii. ....	179
Wajibu wa waumini katika jamii. ....	236
Maandalizi ya mwanaharakati wa kiislamu. ....	309
Zoezi la Pili. ....	327

<b>Sura ya Tatu.</b> .....	329
Mafunzo sura zilizochaguliwa katika juzuu amma. ....	329
Suratul Fatiha. ....	331
Suratul A'ala. ....	343
Suratudh dhuhaa. ....	352

Suratun Nashrah. . . . .	359
Suratut Tyn. . . . .	366
Suratul Bayyinah. . . . .	372
Suratut Takaathur. . . . .	377
Suratul Asr. . . . .	381
Suratul Humazah. . . . .	388
Suratul Fyl. . . . .	392
Suratul Quraysh. . . . .	400
Suratul Ma'un. . . . .	404
Suratul Kawthar. . . . .	408
Suratul Kaafiruun. . . . .	412
Suratul Nasr. . . . .	416
Suratul Lahab. . . . .	422
Suratul Ikhlaas. . . . .	427
Suratul Falaq. . . . .	432
Suratun Naas. . . . .	439
<b>Sura ya Nne. . . . .</b>	<b>444</b>
Sunnah na Hadith. . . . .	444
Maana ya Sunnah. . . . .	444
Maana ya Hadith. . . . .	445
Nafasi ya Sunnah katika Uislaam. . . . .	446
Historia fupi ya Uandishi wa Hadith. . . . .	450
Tanzu za Hadith. . . . .	462
Aina za Hadith. . . . .	466
Zoezi la Nne. . . . .	467
<b>Sura ya Tano. . . . .</b>	<b>468</b>
Mwenendo wa Muislamu. . . . .	468
Dhikri wakati wa kuamka. . . . .	468
Dhikri ya kuleta wakati wa kuvaa nguo. . . . .	469
Dua ya Kuvua Nguo. . . . .	470

Dua ya Kuingilia Chooni. . . . .	470
Dua ya Kutoka Chooni. . . . .	470
Dhikri wakati wa kutoka Nyumbani. . . . .	470
Dhirki wakati wa Kurejea nyumbani. . . . .	471
Dua ya Kuingia Msikitini. . . . .	471
Dua ya Kutoka Msikitini. . . . .	472
Dhikri za Kuleta Asubuhi na Jioni. . . . .	472
Kumswalia Mtume Asubuhi na Jioni. . . . .	477
Kuomba Msamaha na Kutubia. . . . .	478
Dhikri ya kuleta baada ya kupatwa na janga au balaa. . . . .	479
Unapokutana na adui au mtawala dhalimu. . . . .	479
Dua ya Kulipa Deni. . . . .	480
Dua anayoleta yule aliyefikwa na jambo gumu.. . . . .	480
Dua ya kuomba unapotokewa na jambo usiloliridhia au unaposhindwa kufanya jambo. . . . .	480
Dua ya Kumuomba mgonjwa wakati wa kumtembelea. . . . .	481
Dua anayoomba mgonjwa aliyekata tamaa na kupona . . . . .	481
Dua ya kuomba mvua. . . . .	482
Dua ya kuleta wakati unapovuma upepo. . . . .	482
Dua ya kuleta wakati mvua inanyesha. . . . .	482
Dua ya kuleta baada ya mvua kunyesha . . . . .	482
Dua ya kusema unapoanza kula. . . . .	483
Dua ya kushukuru baada ya kula. . . . .	483
Dua ya mgeni kumuomba mwenyeji aliyemlisha chakula. . . . .	483
Dua ya kuleta baada ya kupiga chafya. . . . .	484
Dua ya kuwaomba maharusi (walio oana). . . . .	484
Dua ya kuleta unapoanza kufanya tendo la ndoa. . . . .	485
Dua ya kuleta unapopandwa na hasira. . . . .	485
Dua ya kuleta mwisho wa kikao(mkutano). . . . .	485
Dua kumuomba yule aliyekufanyia jambo zuri. . . . .	486
Dua ya kuomba kuepushwa na shirk. . . . .	486

Dua ya kupokelea Sadaq ai zawadi. . . . .	486
Dua ya kupanda mnyama/ chombo cha usafiri. . . . .	487
Dua ya Safari. . . . .	487
Dua ya kupokea habari ya kufurahisha. . . . .	488
Dua kupokea habari ya kuhuzunisha . . . . .	488
Dua ya kuingia sokoni . . . . .	488
Uboza wa kusalimiana. . . . .	489
Kumtukuza Allah wakati wa mapumziko. . . . .	489
Dhikri ya kuleta wakati wa kulala. . . . .	491
Zoezi la Tano. . . . .	493

# بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## Utangulizi

### **Qur-an na Sunnah**

Kuwa na ujuzi wa yakini juu ya Qur-an na Sunnah ni jambo muhimu mno kwa mwanaadamu, hususan Muislamu; Qur-an na Sunnah ndio chimbuko la elimu sahihi ya Uislamu.

**Qur-an** ni ujumbe sahihi kutoka kwa Allah (s.w) wenye lengo la kumuongoza binaadamu katika njia sahihi ya maisha itakayo muwezesha kuishi kwa furaha na amani hapa duniani na kuwa na makazi mema na furaha ya milele huko akhera. Katika kuongoza kwake, Qur-an humuwezesha binaadamu kujitambua kuwa yeye ni nani na kumfahamisha lengo la maisha yake hapa duniani na namna ya kulifikia. Pia Qur-an inamuweka wazi binaadamu kuwa ataishi hapa duniani maisha ya dhiki yenye kuzingirwa na hofu na huzuni na katika maisha ya akhera atakuwa na dhiki kubwa zaidi na huzuni ya kudumu endapo ataihalifu Qur-an kama tunavyokumbushwa katika aya zifuatazo:

وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنْكًا وَنَحْشُرُهُ  
يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى ﴿١٢٤﴾ قَالَ رَبِّ لِمَ حَشَرْتَنِي أَعْمَى وَقَدْ كُنْتُ  
بَصِيرًا ﴿١٢٥﴾ قَالَ كَذَلِكَ أَتَتْكَ آيَاتُنَا فَنَسَيْتَهَا ۖ وَكَذَلِكَ الْيَوْمَ  
نُنَسِي ﴿١٢٦﴾ وَكَذَلِكَ نَجْزِي مَنْ أَسْرَفَ وَلَمْ يُؤْمِنْ بِآيَاتِ رَبِّهِ  
وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَشَدُّ وَأَبْقَى ﴿١٢٧﴾

*“Na atakayejeipusha na mawaidha yangu (Qur-an), basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na siku ya kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu. Aseme: “Ee Mola wangu!*

*Mbona umenifufua kipofu, hali nilikuwa nikiona?” (Allah atasema, “Ndiyo vivyo hivyo. Zilikujia aya zetu ukazisahau (ukazipuuzwa) na kadhalika leo utasahauliwa (utapuuzwa). Na hivi ndivyo tutakavyomlipa kila apitaye kiasi (anayepundukia mipaka) na asiyeamini aya za Mola wake, na bila shaka adhabu ya akhera ni kali zaidi na iendeleayo sana.” (20:124-127).*

**Sunnah** ni maelekezo na mwenendo wa Mtume (s.a.w) ambaye ndiye aliyeshushiwa Qur-an na kuifasiri katika maisha ya kila siku ya kibinafsi na kijamii, yeye mwenyewe akiwa kiigizo chema. Tunavyojifunza katika Qur-an na katika historia ya maisha ya Mtume Muhammad(s.a.w) ni kuwa maelekezo na mwenendo wa Mtume Muhammad(s.a.w) ni ule wa kuifuata Qur-an kama ilivyo na kufanya kila jambo kwa kufuata maelekezo ya Allah(s.w) kama tunavyokumbushwa katika Qur-an:

وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ۗ (٣) إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ۗ (٤) عَلَّمَهُ شَدِيدٌ الْقُوَىٰ (٥)

*“Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake). Hayakuwa haya anayosema (na kutenda) ila ni wahyi uliofunuliwa (kwake Muhammad). Amemfundisha (Malaika) mwenye nguvu (mwenye cheo) sana (mbele ya Allah (s.w)). (53:3-5)*

Pamoja na kutufahamisha haya, Allah (s.w) anatufahamisha pia kuwa Muhammad (s.a.w) ni mwenye tabia njema kabisa:

وَإِنَّكَ لَعَلَّ خُلِقْتَ عَظِيمٌ (٤)

*“Na bila shaka una tabia njema kabisa.” (68:4)*

Ni katika msingi huu, Allah (s.w) anatumrisha tumtii Mtume (s.a.w) na tumfanye kiigizo chetu kama Allah (sw) anavyosema:

(viii)

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ

الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٦١﴾

*“Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na kumtaja Mwenyezi Mungu sana.” (33:21)*

فَلْ إِن كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ  
وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٦٢﴾ فَلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا إِلَهُ

لَا يُجِبُّ الْكٰفِرِينَ ﴿٦٣﴾

*“Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni; (hapo) Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye maghfira, mwenye Rehema” Sema: “Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume (wake). Na mkikengeuka (Mwenyezi Mungu atakuadhibuni) kwani Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri.” (3:31-32)*

Hivyo, kutokana na mafunzo ya aya hizi tulizozinukuu, hatuwezi kuwa Waislamu bila ya kufuata kwa ukamilifu sunnah ya Mtume Muhammad(s.a.w).



## Sura ya Kwanza

# QUR-AN

### **Qur-an na majina yake**

Qur-an ni wahy (ufunuo) kwa Mtume Muhammad (s.a.w) kutoka kwa Allah (s.w) kupitia kwa Malaika Jibril (a.s). Qur-an kama vitabu vingine vya Allah (s.w), imeshushwa kwa lengo la kuwaongoza wanaadamu katika kila kipengele cha maisha ya kila siku ya kibinafsi na kijamii. Lengo la Qur-an linabainishwa katika aya ifuatayo:

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ  
وَالْفُرْقَانِ.....

*"Ni mwezi wa Ramadhani ambamo imeshushwa Qur-an ili iwe mwongozo kwa watu na hoja zilizo wazi na upambanuzi (baina ya haki na batili)....." (2:185)*

Katika kuendea lengo lake hili, Qur-an humuongoza mwanaadamu kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii na hutoa hoja zenye mashiko dhidi ya wapinzani wake.

Katika kuonesha uwezo wake katika kumuongoza mwanaadamu katika kila kipengele cha maisha yake, Qur-an imeitwa (imesifiwa) kwa majina yafuatayo:

### **1. Al-Qur-an**

Maana yake ni "Chenye kuunganishwa pamoja" au "chenye kusomwa. "Yaani Qur-an ni kitabu kilichofumwa na herufi, silabi, maneno, aya na sura, kinachosomwa mara kwa mara. Kitabu hiki kimeitwa kwa jina hili la "Al-Qur-an" kwa sababu ni mkusanyiko wa mafunzo ya msingi ya maisha ambayo mtu hanabudi kuyarejea mara

kwa mara. Qur-an ndio Mwongozo sahihi pekee wa maisha ya mwanadamu hivi sasa.

## **2. Kalamullah:**

Maneno ya Allah (s.w). Qur-an yote ni maneno ya Allah (s.w) yenye kutoa mwongozo kwa walimwengu wote kupitia kwa Mtume Muhammad (s.a.w) kwa njia ya Wahy kupitia kwa Malaika Jibril (a.s).

## **3. Al-Mus-haf:**

Mkusanyiko wa kurasa. Hili ni jina mashuhuri lililotumiwa na maswahaba wa Mtume (s.a.w) baada ya Qur-an kukamilika kushuka na kuwekwa katika sura ya kitabu kikubwa.

## **4. Al-Kitaab:**

Kitabu pekee (Unique book). Qur-an ni kitabu kikamilifu kisicho na upogo wala dosari yoyote wala hakina mfano wa kitabu chochote kimuundo, maudhui na uwasilishaji wa maudhui hayo. Qur-an yenyewe imeliweka hili wazi katika aya ifuatayo:

ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾

*"Hiki ni kitabu pekee (Al-Kitaab) kisicho na shaka ndani yake na ni mwongozo kwa wamchao Mwenyezi Mungu." (2:2)*

## **5. Al-Furqaan:**

Kipambanuzi cha Haki na Batili au ukweli na uwongo. Yaani Qur-an ndio kipimo cha Haki na Batili au Zuri na Baya au Jema na Ovu, Tawhiid na Shiriki, Uislamu na Ukafiri

## **6. Adh-Dhikru:**

Mawaidha au ukumbusho. Qur-an ni mawaidha yenye kumkumbusha kila mwenye kusoma na kuzingatia.

## 7. At-Tanzil:

Mshuko au wahy kutoka kwa aliye juu. Jina hili linasisitiza kuwa Qur-an ni kitabu cha Allah (s.w) kilichoshushwa kwa njia ya wahy kwa Mtume Muhammad(s.a.w) kupitia kwa malaika Jibril(a.s) ili awaongoze walimwengu kwacho.

## 8. Al-Hukmu:

Kitabu pekee kinachostahiki kumuhukumu mwanaadamu. Hukumu yoyote kinyume na Hukumu ya Qur-an ni upinzani na uasi dhidi ya Allah (s.w) na ni dhulma dhidi ya wanaadamu kama inavyosisitiza Qur-an yenyewe:

.... وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٤٤﴾

“...Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.” (5:44)

.... وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٤٥﴾

“....Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu.” (5:45)

... وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٤٧﴾

“.... Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio wasi (mafasiki).” (5:47)

Neno “wasiohukumu” hapa limetumika kwa maana ya wanaoendesha maisha yao kinyume na yale aliyoteremsha Allah au wale wasioendesha maisha yao kwa mujibu wa Qur-an

## 9. Al-Hikma:

Kitabu pekee chenye Hikima isiyo kikomo. Ni kitabu cha Allah (s.w) ambaye ndiye chimbuko (source) la Elimu na Hekima. Hekima

ni jambo la sawa sawa lililofanywa kwa namna ya sawa sawa katika mazingira na wakati wasa wasa ili kufukia lengo tarajiwa. Qur'an ni Hikma na humuuongoza binaadamu aishi maisha ya Hikma.

### 10. Ash-Shifau:

Ponyo au dawa pekee. Qur-an imeitwa kwa jina hili la "**Ponyo pekee**" kwa sababu Qur-an ndio dawa pekee ya kuponya maradhi ya "nafsi". Maradhi makubwa ya nafsi ni Ukafiri, Ushirikina, Unafiki na Uasi wa kila aina. Qur-an imejizatiti katika kuyaelezea magonjwa haya ili kila mtu mwenye akili timamu ayafahamu bayana na imeelekeza kwa ufasaha namna ya kuyatibu.

### 11. Ar-Rahmat:

Rehema kwa watu. Vipawa vinavyomfanya binaadamu atofautiane na wanyama ni akili na elimu. Vipawa hivi vikitumika bila ya kufuata mwongozo kutoka kwa Allah (s.w) humpelekea binaadamu kufanya uharibifu katika ardhi kuliko mnyama yoyote yule. Binaadamu akitumia akili yake na elimu aliyotunukiwa kwa kufuata mwongozo wa Qur-an huwa juu na bora kuliko viumbe vyote.

### 12. Al-Khayr:

Qur-an ni kheri pekee. Yaani Qur-an ndio chanzo cha kheri zote. Kheri hupatikana kwa kufuata Qur-an vilivyo.

### 13. Ar-Ruuhu:

Qur-an ni roho ya maisha. Yaani mtu asiyeishi kwa kufuata Qur-an ni kama maiti japo anaishi. Allah (s.w) anawaasa waumini wasiwakumbatie wapinzani wa Qur-an (makafiri) kwani wao ni kama maiti walio makaburini.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ قَدْ يَيسُوا مِنْ

الْآخِرَةِ كَمَا يَيسُ الْكُفَّارُ مِنْ أَصْحَابِ الْقُبُورِ ﴿١٣﴾

*"Enyi mlioamini! Msifanye urafiki wa ndani na watu ambao Mwenyezi Mungu amewakasirikia na wamekata tamaa ya akhera kama walivyokwisha kata tamaa makafiri waliozikwa makaburini." (60:13)*

#### **14. Al-Bayaana:**

Qur-an ni kitabu pekee chenye maelezo ya wazi na kinachofafanua aya zake kwa uwazi kwa kutumia mifano iliyozoeleka katika mazingira ya watu kwa nyakati zote za historia. Hivyo, kila mwenye akili timamu anao uwezo wa kuelewa Qur-an na ikamuongoza.

#### **15. An-Nuur:**

Qur-an ni nuru pekee. Qur-an ni mwanga unaomuonesha binaadamu njia sahihi ya maisha itakayomfikisha kwenye lengo la kuumbwa kwake. Kuishi bila ya kufuata Qur-an ni sawa na mtu anayetembea katika giza nene na matokeo ya kutembea kwenye giza nene yanafahamika kwa kila mwenye akili timamu. Qur-an inatukumbusha:

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ آمَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ  
وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى  
الظُّلُمَاتِ أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

*"Allah ni kiongozi wa walioamini. Huwatoa kwenye giza na kuwaingiza katika nuru (mwanga). Lakini waliokufuru viongozi wao ni Matwaghuti huwatoa katika nuru na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa motoni, humo watakaa milele." (2:257)*

#### **16. Al-Burhan:**

Hoja pekee iliyowazi. Qur-an ni kitabu kinachotoa hoja zilizo wazi kwa wasomaji wake. Kwa mfano Qur-an inatoa hoja zilizo wazi, kuwa lazima pawe

na Muumba mmoja wa ulimwengu na vyote vilivyomo mwenye ujuzi na Hekima. Pia Qur-an pamoja na kutoa hoja maridhawa juu ya kumuamini Allah (s.w) na nguzo nyinginezo za imani , huonesha lengo la kumuabudu Allah (s.w) na umuhimu na hekima ya kufuata Qur-an na Sunnah kama mwongozo pekee wa njia sahihi ya maisha ya binaadamu.

### **17. Al-Haqq:**

Qur-an ni Haki. Qur-an ni haki kwa sababu ni maneno ya Allah (s.w) ambaye ni mjuzi wa kweli aliyepukana na upungufu wa aina yeyote. Qur-an humuongoza binaadamu kwenye njia ya haki na huhukumu kwa waki.

### **18.Ahsan-ul-Hadith:**

Maneno mazuri au maelezo mazuri kuliko yote kwa kuwa yanatoka kwa Allah (s.w), Mjuzi, mwenye hekima.

Kitabu hiki cha Allah (s.w), kilichosifiwa kwa majina haya, kina aya 6,236 zilizogawanywa katika sura 114 (Rejea jedwali 1). Pia kitabu cha Qur-an (Al-Mas-haf) kimegawanywa kwenye juzuu au mafungu (30) yaliyo sawa sawa.

## Jedwali 1: Orodha ya sura na zilimoshuka:

<i>Nambari ya Sura katika Msahafu</i>	<i>Jina la Sura</i>	<i>Nambari ya Sura kwa mpangilio wa kushuka</i>	<i>Mahali iliposhuka</i>
1.	Al-Fatihah	5	Makka
2.	Al-Baqarah	87	Madina
3.	Al-Imran	89	Madina
4.	An-Nisaa	92	Madina
5.	<i>Al-Maidah</i>	112	Madina
6.	Al-An-'am	55	Makka
7.	Al-A'araf	39	Makka
8.	Al-Anfal	88	Madina
9.	At-Tawbah	113	Madina
10.	Yunus	51	Makka
11.	Hud	52	Makka
12.	<i>Yusuf</i>	53	Makka
13.	Ar-Ra'ad	96	Madina
14.	Ibrahim	72	Makka
15.	Al-Hijr	54	Makka
16.	An-Nahal	70	Makka
17.	Bani-Israil	50	Makka
18.	Al-Kahf	69	Makka
19.	Maryam	44	Makka
20.	Twaaha	45	Makka
21.	Al-Anbiyaa	73	Makka
22.	Al-Hajj	103	Madina
23.	Al-Mu'minuun	74	Makka
24.	An-Nuur	102	Madina
25.	Al-Furqan	42	Makka
26.	Ash-Shu'araa	47	Makka
27.	An-Naml	48	Makka

<i>Nambari ya Sura katika Msahafu</i>	<i>Jina la Sura</i>	<i>Nambari ya Sura kwa mpangilio wa kushuka</i>	<i>Mahali iliposhuka</i>
28.	Al-Qasas	49	Makka
29.	Al-Ankabuut	85	Makka
30.	Ar-Ruum	84	Makka
31.	Luqman	57	Makka
32.	As-Sajdah	75	Makka
33.	Al-Ahzab	90	Madina
34.	Sabai	58	Makka
35.	Fatir	43	Makka
36.	Yasin	41	Makka
37.	As-Saaffat	56	Makka
38.	Sad	38	Makka
39.	Az-Zumar	59	Makka
40.	Al-Mu'min	60	Makka
41.	HaMliim Sajdah	61	Makka
42.	Ash-Shura	62	Makka
43.	Az-Zukhruf	63	Makka
44.	Ad-Dukhan	64	Makka
45.	Al-Jathiyah	65	Makka
46.	Al-Ahqaaf	66	Makka
47.	Muhammad	95	Madina
48.	Al-Fat-h	111	Madina
49.	Al-Hujurat	106	Madina
50.	Qaf	34	Makka
51.	Adh-Dhaariyat	67	Makka
52.	At-Tur	76	Makka
53.	An-Najm	23	Makka
54.	Al-Qamar	37	Makka
55.	Ar-Rahmaan	97	Madina
56.	Al-Waqi'ah	46	Makka
57.	Al-Hadid	94	Madina



<i>Nambari ya Sura katika Msahafu</i>	<i>Jina la Sura</i>	<i>Nambari ya Sura kwa mpangilio wa kushuka</i>	<i>Mahali iliposhuka</i>
58.	Al-Mujadilah	105	Madina
59.	Al-Hashr	101	Madina
60.	Al-Mumtahinah	91	Madina
61.	As-Saff	109	Madina
62.	Al-Jumu'ah	110	Madina
63.	Al-Munafiquun	104	Madina
64.	At-Taghaabun	108	Madina
65.	At-Talaq	99	Madina
66.	At-Tahrim	107	Madina
67.	Al-Mulk	77	Makka
68.	Al-Qalam	2	Makka
69.	Al-Haqqah	78	Makka
70.	Al-Ma'arij	79	Makka
71.	Nuh	71	Makka
72.	Al-Jinn	40	Makka
73.	Al-Muzzammil	3	Makka
74.	Al-Muddaththir	4	Makka
75.	Al-Qiyamah	31	Makka
76.	Ad-Dahr	98	Madina
77.	Al-Murasaalat	33	Makka
78.	An-Nabaa	80	Makka
79.	An-Nazi'at	81	Makka
80.	'A basa	24	Makka
81.	At-Takwyr	7	Makka
82.	Al-Infitar	82	Makka
83.	Al-Mutaffi'in	86	Makka
84.	Al-Inshiqaq	83	Makka
85.	Al-Buruuj	27	Makka
86.	At-Tariq	36	Makka
87.	Al-A'laa	8	Makka

<i>Nambari ya Sura katika Msahafu</i>	<i>Jina la Sura</i>	<i>Nambari ya Sura kwa mpangilio wa kushuka</i>	<i>Mahali iliposhuka</i>
88	Al-Ghaashiyah	68	Makka
89	Al-Fajr	10	Makka
90	Al-Balad	35	Makka
91	Ash-Shams	26	Makka
92	Al-Layl	9	Makka
93	Adh-Dhuha	11	Makka
94	An-Nashrah	12	Makka
95	At-Tin	28	Makka
96	Al-'Alaq	1	Makka
97	Al-Qadr	25	Makka
98	Al-Bayyinah	100	Madina
99	Az-Zilzal	93	Madina
100	Al-'Adiyat	14	Makka
101	Al-Qari'ah	30	Makka
102	At-Takaathur	16	Makka
103	Al-'Asr	13	Makka
104	Al-Humazah	32	Makka
105	Al-Fiil	19	Makka
106	Quraysh	29	Makka
107	Al-Ma'un	17	Makka
108	Al-Kawthar	15	Makka
109	Al-Kaafiruun	18	Makka
110	An-Nasr	114	Madina
111	Al-Lahab	6	Makka
112	Al-Ikhlās	22	Makka
113	Al-Falaq	20	Makka
114	An-Nas	21	Makka

## Wanaongozwa na Qur-an:

Lengo la kushushwa Qur-an kama ilivyobainishwa katika Qur-an yenyewe ni kuwaongoza binaadamu wote katika njia iliyonyooka. Njia iliyonyooka ni njia sahihi ya maisha itakayomuwezesha binaadamu kufikia lengo la kuumbwa kwake. Pamoja na Qur-an kuwa muongozo kwa watu wote, haiwaburuzi kwa nguvu kwenye uongofu bila ya wao wenyewe kudhamiria kuongoka. Qur-an huongoza wacha-Mungu tu kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ  
وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٣﴾ وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنزِلَ  
إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ وَبِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾ أُولَٰئِكَ عَلَىٰ هُدًى  
مِّن رَّبِّهِمْ ۗ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥﴾

*"Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake, ni uwongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu. Ambao huyaamini yasiyoonekana (maadam yamesemwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake) na husimamisha Swala na hutoa katika yale Tuliowapa. Na ambao wanaamini yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako na wanaamini (kuwa iko) Akhera. Hao wako juu ya uongozi utokao kwa Mola wao, na hao ndio wenye kufaulu." (2:2-5)*

Kwa mujibu wa aya hizi wanaongozwa na Qur-an ni wacha-Mungu wenye sifa zifuatazo:

- Waumini wa kweli wa vipengele vyote vya nguzo za Imani.
- Wasimamishaji Swala. (Rejea juzuu ya pili).
- Wanaotoa yale aliyowaruzuku Allah (s.w) kwa ajili ya kuwahurumia wanaadamu wenye kuhitajia msaada na katika kusimamisha Dini ya Allah(s.w). Aliyoturuzuku Allah (s.w)ni kila tulichonacho ikiwa ni pamoja na mali, elimu, afya, nguvu, vipaji na kadhalika.

## Wasioongozwa na Qur-an:

Tunajifunza katika Qur-an kuwa makundi mawili ya watu **Makafiri** (na washirikina) na **Wanafiki** hawataongozwa na Qur-an. Kuhusu **makafiri** na **washirikina** tunafahamishwa:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ ءَأَنذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾ خَتَمَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ وَعَلَى سَمْعِهِمْ وَعَلَى أَبْصَارِهِمْ غِشْوَةً وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٧﴾

*Hakika wale waliokufuru ni sawa kwao ukiwaonya (kwa hii Qur-an) au usiwaonye; hawataamini. (Kama kwamba) Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao; na juu ya macho yao pana vifuniko; basi watakuwa na adhabu kubwa. (2:6-7)*

Pamoja na Qur-an kuwa na sifa ya ukweli na uwazi kama majina yake yanavyodhihirisha, haiwezi kuwaongoza wapinzani (makafiri) wa wazi wa Mwenyezi Mungu(sw) na ujumbe wake. Haiwezi kwa sababu binaadamu amepewa uhuru na Mola wake wa kuamua na kufanya atakavyo. Akiamua kutii anaweza na akiamua kuasi anaweza. Hivyo mtu aliyeamua kuukataa mwongozo huu kwa makusudi huna namna ya kumuongoza.

Kuhusu **wanafiki** tunafahamishwa:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾ يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَمَا يُخَدِّعُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ فَزَادَهُمُ اللَّهُ مَرَضًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ ﴿١٠﴾

*"Na katika watu, wako (wanafiki) wasemao "Tumemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho" na hali ya kuwa si wenye kuamini. Wanataka kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale*

walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao, nao hawatambui. Nyoyoni mwao mna maradhi, na Mwenyezi Mungu amewazidisha maradhi. Basi watakuwa na adhabu iumizayo kwa sababu ya kule kusema kwao uongo.(2:8-10)

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿١١﴾  
 أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِن لَّا يَشْعُرُونَ ﴿١٢﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ ءَامِنُوا  
 كَمَا ءَامَنَ النَّاسُ قَالُوا أَنُؤْمِنُ كَمَا ءَامَنَ السُّفَهَاءُ ۗ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ السُّفَهَاءُ  
 وَلَكِن لَّا يَعْلَمُونَ ﴿١٣﴾

Na wanapoambiwa msifanye uharibifu ulimwenguni Husema "Sisi ni watengenezaji." Hakika wao ndio waharibuji, lakini hawatambui. Na wanapoambiwa: "Aminini kama walivyoamini watu," husema "Oh! Tuamini kama walivyoamini wapumbavu?" Hakika wao ndio wapumbavu lakini hawajui.(2:11-13)

وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَالُوا ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَوْا إِلَىٰ شَيْطَانِهِمْ قَالُوا  
 إِنَّا مَعَكُمْ إِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِءُونَ ﴿١٤﴾ اللَّهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَمُدَّهُمْ  
 فِي طُعَيْنِهِمْ يَعْزَمُونُ ﴿١٥﴾ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الضَّلَالَةَ بِالْهُدَىٰ  
 فَمَا رَبِحَت تِّجَارَتُهُمْ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿١٦﴾

Na wanapokutana na walioamini husema, "Tumeamini," na wanapokuwa peke yao kwa mashetani wao husema: "Hakika sisi tu pamoja nanyi, tunawacheza shere tu." Na Mwenyezi Mungu atalipa shere yao na kuwawacha katika upotofu wao wakitangatanga ovyo. Hao ndio waliokhiari upotofu kuliko uongofu, lakini biashara yao haikupata faida wala hawakuwa wenye kuongoka." (2:14-16)

Wanafiki pamoja na kujiiita Waislamu na pengine wakawa ni wanachuoni wa Qur-an walio mahiri katika kuifasiri Qur-an kwa

kutumia balagha, mantiq, sarfu, n.k; hawataongozwa na Qur-an maadamu wamekhiari maslahi ya dunia kinyume na mwongozo wa Mwenyezi Mungu(sw). Si tu hawa wasomi wa Qur-an wenye sifa hizo zilizoainishwa katika aya hizi hawataongozwa na Qur-an bali pia Allah (s.w) amewafananisha na mbwa katika aya zifuatazo:

وَأَنْزَلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ الَّذِي آتَيْنَاهُ آيَاتِنَا فَانْسَلَخَ مِنْهَا فَاتَّبَعَهُ الشَّيْطَانُ  
فَكَانَ مِنَ الْغَاوِينَ ﴿١٧٥﴾ وَلَوْ شِئْنَا لَرَفَعْنَاهُ بِهَا وَلَنُكَلِّمَهُهُ أَهْلَ الدَّارِ إِلَى  
الْأَرْضِ وَأَتَّبَعَهُ هَوْنَهُ فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ الْكَلْبِ إِنْ تَحْمِلُ عَلَيْهِ يَلْهَثُ أَوْ  
تَتْرُكُهُ يَلْهَثُ ذَلِكَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا فَاقْضِ  
الْقِصَصَ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١٧٦﴾

*"Na wasomee (Ewe Muhammad) habari za wale tuliowapa Aya zetu (kuzijua), kisha wakajivua nazo (wasizifuata). Na shetani akawaandama na, wakawa miongoni mwa waliopotea. Na kama tungelitaka tungeliwanyanyua kwazo, lakini wao waligandamana na ardhi (kutaka maslahi ya kidunia wakayapuuzwa ya Akhera) na wakayafuata matamania yao. Basi hali yao ni kama hali ya mbwa; ukimpigia kelele (hukimbia na huku) anahema, na ukimwacha pia huhema. Hiyo ndio hali ya watu waliokadhibisha Aya zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari." (7:175-176)*

Hivyo, kwa mujibu wa Aya hizi, mnafiki hata akiwa ni A'alim (Sheikh) wa Qur-an na Hadith, kamwe hawezi kuongozwa na Qur-an.

### **Historia ya Kushuka Qur-an:**

Qur-an ilianza kumshukia Mtume Muhammad (s.a.w) mwaka 610 A.D. alipokuwa na umri wa miaka 40. Mtume Muhammad (s.a.w) alianza kushushiwa Qur-an akiwa pangoni katika mlima Hira (Jabal Hira) katika usiku wa mwezi wa Ramadhani kama Qur-an yenyewe inavyotufahamisha:

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ.....

*Ni mwezi wa Ramadhani ambamo imeteremshwa hii Qur-an..... (2:185)*

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ ﴿١﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا لَيْلَةُ الْقَدْرِ ﴿٢﴾ لَيْلَةُ الْقَدْرِ

خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ ﴿٣﴾ تَنزِيلُ الْمَلَكِ وَالرُّوحُ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ مِّن

كُلِّ أَمْرٍ ﴿٤﴾ سَلَامٌ هِيَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ الْفَجْرِ ﴿٥﴾

*"Hakika Tumeiteremsha (Qur-an) katika Laylatul-Qadr (usiku wenye hishima kubwa). Na jambo gani litakujulisha (hata ukajua) ni nini huo usiku wenye hishima kubwa? Huo usiku wa hishima ni bora kuliko miezi elfu. Huteremka Malaika na roho (Jibriil) katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao kwa kila jambo. Ni amani (usiku) huo mpaka mapambazuko ya alfajiri." (97:1-5)*

Tunajifunza kutokana na aya hizi kuwa mwezi wa Ramadhani umetukuzwa kutokana na Qur-an kuanza kushuka katika mwezi huu. Pamoja na funga kufaradhishwa kwa umma za Mitume wote wa Allah (s.w); kwa ummat Muhammad (s.a.w),funga imefaradhishwa iwe katika mwezi wa Ramadhani ili iwe ni pamoja na kusherehekea kushuka kwa Qur-an na kilele cha sherehe hii kinakuwa katika usiku wa hishima (Laylatul-Qadr) ambamo Qur-an ilianza kushuka. Mtume (s.a.w) alikuwa akizidisha kusoma Qur-an katika mwezi huu na alikuwa akikaa Itiqaf katika kumi la mwisho la Ramadhani ili aweze kudiriki kilele cha sherehe. Usiku wenye hishima (Laylatul-Qadr) ulifichwa kwa Mtume (s.a.w) lakini alifunuliwa na Mola wake kuwa unapatikana katika kumi la mwisho la Ramadhani. Ni sunnah kwa Waislamu kuzidisha kusoma Qur-an katika mwezi mzima wa Ramadhani na kukaa Itiqaf katika kumi la mwisho, ili kushiriki kikamilifu katika sherehe ya kumbu kumbu ya kuanza kushuka Qur-an.

Historia ya kuanza kushuka Qur-an kwa Mtume Muhammad (s.a.w) kupitia kwa Malaika Jibril (a.s) inasimuliwa vyema katika Hadith ya bibi 'Aisha (r.a) ifuatayo:

*Bibi 'Aisha (r.a) amesema:" Kilichoanza katika Wahyi wa Mtume (s.a.w) ni ndoto za kweli. Alikuwa Mtume (s.a.w) haoti chochote isipokuwa kilitokea kama alivyoota. Kisha akaona ni bora kujitenga. Akawa anakwenda Jabal Hira kujilinda na maovu. Basi alikuwa anakwenda Jabal Hira akifanya ibada masiku mengi na alichukua masurufu kwa ajili hiyo. Masurufu haya kila yalipokwisha alirudi tena kwa Bibi Khadija, aliyemtayarishia masurufu kama yale (ya kwanza) mpaka ikambainikia haki akiwa pangoni Hira. Basi akamjia Malaika (Jibril) humo pangoni akamuamrisha kusoma, Mtume (s.a.w) alijibu: "Sijui kusoma". Alinibana kwa nguvu mpaka nikahisi taabu. Kisha akaniachia na kuniamrisha tena kusoma na nikajibu: Sijui kusoma: Kisha akanibana tena kwa nguvu kwa mara ya pili mpaka nikahisi taabu. Kisha akaniachia na kuniamrisha tena kusoma. Nilijibu tena, "sijui kusoma". Akanikumbatia tena kwa nguvu kwa mara ya tatu mpaka nikahisi mashaka, kisha akaniachia na akasema:*

أَقْرَأُ بِأَسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ① خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ② أَقْرَأُ وَرَبُّكَ  
 الْأَكْرَمُ ③ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ④ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ⑤

*"Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba. Amemuumba mwanaadamu kwa pande la damu. Soma na Mola wako ni Karimu sana. Ambaye amefundisha kwa msaada wa kalamu. Amemfundisha mwanaadamu mambo aliyokuwa hayajui." (96:1-5)*

Mtume wa Mwenyezi Mungu alirejea na Wahy huu, huku akitetemeka kwa khofu aliyokuwa nayo. Alikwenda kwa mkewe Khadijah na akamhadithia yale yote yaliyomtokea kisha akasema;



"Nakhofia kuwa kitu kinaweza kunitokea". Khadijah alijibu: "Hapana! Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu hataku fedhehesha. Unakaa vizuri na kuwafanyia wema ndugu na jamaa zako, unawasaidia masikini na fukara, unawakirimu wageni na unawasaidia waliokabiliwa na matatizo." Kisha Bibi Khadijah alimchukua Mtume (s.a.w) mpaka kwa bin-ami yake, Waraqa bin Naufal bin Asad bin Abdul Uzza, ambaye alikuwa Mkristo. Waraqa wakati huo alikuwa mzee sana na alikuwa hawezi kuona tena. Khadijah alimuambia Waraqa "Sikiliza hadithi ya mpwa wako, Ewe Bin-ami yangu" Waraqa aliuliza, "Ewe Mpwa wangu umeona nini?" Mtume wa Mwenyezi Mungu alimuhadithia habari yote kama alivyoona. Waraqa akasema: "Huyu ni yule mtunza siri (Malaika Jibril) ambaye Mwenyezi Mungu alimtumia kwa Mussa. Natamani ningelikuwa kijana na kuishi mpaka wakati huo watu wako watakapokukataa na kukufukuza." Mtume wa Mwenyezi Mungu akauliza: "Watanifukuza?" Waraqa akajibu kuwa watafanya hivyo na akasema, "Yeyote aliyekuja na kitu kama hicho ulichokuja nacho alifanyiwa uadui na watu wake, na ningejaliwa kubakia hai mpaka siku hiyo watu wako watakapokufukuza, ningelikusaidia kwa hali na mali." Lakini baada ya muda mfupi Waraqa alifariki na Wahyi mwingine ulikawia kuja kwa kipindi kirefu. (Sahih Bukhari)

Tunajifunza kutokana na Hadith kuwa kabla Mtume (s.a.w) hajaanza kushushiwa Qur-an kupitia kwa Malaika Jibril (a.s) alikuwa akipata Wahy kwa njia ya ndoto.

Qur-an yote kwa ujumla imehifadhiwa katika ubao mtukufu wa Allah (s.w) ulio katika Arshi yake kama tunavyofahamishwa katika Qur-an:

بَلْ هُوَ قُرْءَانٌ مَّجِيدٌ ﴿٦١﴾ فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ ﴿٦٢﴾

"Bali hii ni Qur-an tukufu iliyotolewa katika Lawhi Mmahfuudh (huo ubao uliohifadhiwa)." (85:21-22)

Kisha kutoka **Lawhi Mmahfuudh** Qur-an ilishushwa mpaka wingu wa kwanza. Kisha kutoka humo ikashushwa kidogo kidogo kwa Mtume (s.a.w) kupitia kwa Malaika Jibril (a.s) kwa kipindi chote cha Utume cha miaka 23.

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿١٩﴾ ذِي قُوَّةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ ﴿٢٠﴾

*"Kwa hakika hii (Qur-an) ni kauli (aliyokuja nayo) Mjumbe Mtukufu (Jibril), Mwenye nguvu na cheo cha hishima kwa Mwenyezi Mungu. (81:19-20)*

Kama tunavyojifunza katika Hadith, aya za mwanzo kumshukia Mtume (s.a.w) ni aya tano za mwanzo za suratul-'Alaq. Aya zilizofuatia katika sura hii (96:6-19) zilishuka siku za baadaye.

Aya ya mwisho kumshukia Mtume (s.a.w) alipokuwa katika Hija ya kuaga (Hijjatul Wadaai) ni aya ya tatu ya suratul Maida (5:3) ambayo imeashiria mwisho wa wahy wa Qur-an katika sehemu ifuatayo:

الْيَوْمَ يَئِسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِ الْيَوْمَ  
أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيْتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

*... ..Leo waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu, basi msiwaogope, bali niogopeni mimi. Leo nimekukamilishieni dini yenu, na kukutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini yenu..... (5:3)*

Pia tunajifunza kutokana na historia ya kushuka Qur-an kuwa sura ya kwanza kushuka nzima (ikiwa na aya zote) ni Suratul-Fatiha (Al-hamdu) na imekuwa ndio sura ya kwanza katika msahafu. Katika mtiririko wa kushuka suratul-Fatiha ni Wahy wa tano. Sura ya mwisho kushuka ikiwa nzima ni Suratun-Nasr, sura ya 114 katika utaratibu wa kushuka (rejea Jedwali 2 na 3).

## **Sura za Makka na Madina**

Kutokana na historia ya kushuka kwake sura za Qur-an zimegawanywa katika makundi mawili - sura za **Makka** na sura za **Madina**.

**Sura za Makka** ni zile zilizomshukia Mtume (s.a.w) katika kipindi cha Utume cha Makka kilichodumu kwa miaka 13. **Maudhui** ya sura za Makka kwa kiwango kikubwa yamejikita katika kujenga imani za watu kwa kutoa hoja madhubuti zilizozingatia mazingira ya wakazi wa Makka wa kipindi hicho. **Muundo** wa sura za Makka ni ule wa kishairi. Nyingi ya sura za Makka zimeundwa na aya fupi zenye kufikisha ujumbe moja kwa moja kwa mtindo wa kishairi uliozingatia mazingira ya watu wa Makka wa wakati ule.

Katika siku za mwanzo za kushuka kwa Qur-an, watu wa Makka walidhania kuwa Qur-an ni mashairi aliyotunga Muhammad (s.a.w), lakini baada ya kupitia aya zake kwa makini, kama alivyofanya bingwa wa washairi wa wakati huo, Labiid bin Rabiha, na baada ya kushindwa kutoa angalau sura moja mithili ya sura ya Qur-an, kimaudhui na kimuundo, ilidhihiri wazi kuwa Qur-an si mashairi bali ni Wahy kutoka kwa Allah (s.w).

## Jedwali 2: Orodha ya Sura za Makka

<i>Nambari ya Sura katika kushuka</i>	<i>Jina la Sura</i>	<i>Nambari ya Sura katika msahafu</i>	<i>Idadi ya aya</i>	<i>Juzuu</i>
1.	Al-A'laq	96	19	30
2.	Al-Qalam	68	52	29
3.	Al-Muzzammil	73	20	29
4.	Al-Muddaththir	74	56	29
5.	Al-Fatiha	1	7	1
6.	Al-Lahab	111	5	30
7.	At-Tak-wir	81	29	30
8.	Al-A'laa	87	19	30
9.	Al-Layl	92	21	30
10.	Al-Fajr	89	30	30
11.	Ah-Dhuha	93	11	30
12.	Alam-Nashrah	94	8	30
13.	Al-'Asr	103	3	30
14.	Al-Aadiyat	100	11	30
15.	Al-Kawthar	108	3	30
16.	At-Takaathur	102	8	30
17.	Al-Ma'un	107	7	30
18.	Al-Kafiruun	109	6	30
19.	Al-Fyl	105	5	30
20.	Al-Falaq	113	5	30
21.	An-Nas	114	6	30
22.	Al-Ikhlās	112	4	30
23.	An-Najm	53	62	27
24.	'Abasa	80	42	30
25.	Al-Qadr	97	5	30
26.	Ash-Shams	91	15	30
27.	Al-Buruj	85	22	30
28.	At-Tin	95	8	30
29.	Quraysh	106	4	30

<i>Nambari ya Sura katika kushuka</i>	<i>Jina la Sura</i>	<i>Nambari ya Sura katika msahafu</i>	<i>Idadi ya aya</i>	<i>Juzuu</i>
30.	Al-Qaariah	101	11	30
31.	Al-Qiyamah	75	40	29
32.	Al-Humazah	104	9	30
33.	Al-Mursalaat	77	50	29
34.	Qaf	50	45	26
35.	Al-Balad	90	20	30
36.	At-Twariq	86	17	30
37.	Al-Qamar	54	55	27
38.	Saad	38	88	23
39.	Al-A'raf	7	206	8/9
40.	Al-Jinni	72	28	29
41.	Yasin	36	83	22/23
42.	Al-Furqan	25	77	18/19
43.	Fatir	35	45	22
44.	Maryam	19	98	16
45.	Twaha	20	135	16
46.	Al-Waqi'ah	56	96	27
47.	Ash-Shu'ara	26	227	19
48.	An-Naml	27	93	19/20
49.	Al-Qasas	28	88	20
50.	Bani-Israil	17	111	15
51.	Yunus	10	109	11/12
52.	Hud	11	123	11/12
53.	Yusuf	12	111	12/13
54.	Al-Hijr	15	99	14
55.	Al-An'am	6	165	7/8
56.	As-Saffat	37	182	23
57.	Luqman	31	34	21
58.	Sabai	34	54	22
59.	Az-Zumar	39	75	23/24

<i>Nambari ya Sura katika kushuka</i>	<i>Jina la Sura</i>	<i>Nambari ya Sura katika msahafu</i>	<i>Idadi ya aya</i>	<i>Juzuu</i>
60.	Al-Mu'min	40	85	24
61.	HaMim Sajdah	41	54	24/25
62.	Ash-Shura	42	53	25
63.	Az-Zukhruf	43	89	25
64.	Ad-Dukhan	44	59	25
65.	Al-Jathiyah	45	37	25
66.	Al-Ahqaaf	46	35	26
67.	Adh-Dhariyat	51	60	26/27
68.	Al-Ghaashiyah	88	26	30
69.	Al-Kahf	18	110	16
70	An-Nahl	16	128	14
71	Nuh	71	28	29
72	Ibrahim	14	52	13
73	Al-Anbiyaa	21	112	17
74	Al-Mu'minuun	23	118	18
75	As-Sajdah	32	30	21
76	At-Tur	52	49	27
77	Al-Mulku	67	30	29
78	Al-Haqqah	69	52	29
79	Al-Ma'arij	70	44	29
80	An-Nabaa	78	40	30
81	An-Nazi'at	79	46	30
82	Al-Infitar	82	19	30
83	Al-Inshiqaq	84	25	30
84	Ar-Ruum	30	60	21
85	Al-Ankabuut	29	69	20/21
86	Al-Mutaffi'in	83	36	30

**Sura za Madina** ni zile zilizomshukia Mtume (s.a.w) baada ya kuhamia Madina katika kipindi cha pili cha Utume wake kilichodumu kwa miaka 10.

Maudhui ya sura za Madinah yamejikita kwenye kuunda na kuendesha Dola ya Kiislamu. Nyingi ya sura za Madina zina aya ndefu zenye kufafanua mambo kwa uwazi ili kuwawezesha Waislamu kutekeleza wajibu wao katika kusimamisha na kuhami dola ya Kiislamu. Pia aya nyingi za Madina zimeshehenezwa na maamrishi na makatazo mbali mbali ili kuunda jamii imara itakayoweza kusimamisha Ukhalifa katika ardhi.

### **Jedwali 3: Orodha ya Sura za Madina**

<i>Nambari ya Sura katika kushuka</i>	<i>Jina la Sura</i>	<i>Nambari ya Sura katika msahafu</i>	<i>Idadi ya aya</i>	<i>Juzuu</i>
87.	Al-Baqarah	2	286	1-3
88.	An-Anfaal	8	75	9-10
89.	Al-Imraan	3	200	3-4
90.	Al-Ahzab	33	73	21/22
91	Al-Mumtahinah	60	13	28
92	An-Nisai	4	176	4-6
93	Az-Zilzal	99	8	30
94	Al-Hadid	57	29	27
95	Muhammad	47	38	26
96	Ar-Raad	13	43	13
97	Ar-Rahmaan	55	78	27
98	Ad-dahr	76	31	29
99	At-Talaq	65	12	28
100	Al-Bayyinah	98	8	30
101	Al-Hashir	59	24	28
102	An-Nur	24	64	18
103	Al-Hajj	22	78	17

<i>Nambari ya Sura katika kushuka</i>	<i>Jina la Sura</i>	<i>Nambari ya Sura katika msahafu</i>	<i>Idadi ya aya</i>	<i>Juzuu</i>
104	Al-Munaafiquun	63	11	28
105	Al-Mujaadilah	58	22	28
106	Al-Hujuraat	49	18	26
107	At-Tahrim	66	12	28
108	At-Taghaabun	64	18	28
109	As-Saff	61	14	28
110	Al-Jum'ah	62	11	28
111	Al-Fat-h	48	29	26
112	Al-Maidah	5	120	6/7
113	At-Tawbah	9	129	10/11
114	An-Nasr	110	3	30

## **Madai ya Makafiri dhidi ya Qur-an**

Waislamu wanaamini pasi na tone la shaka kuwa Qur-an ni kitabu cha Allah (s.w) neno kwa neno kama mwenyewe anavyohibitisha:

ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾

*"Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake, ni uongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu." (2:2)*

Pamoja na uthibitisho huu, makafiri wa zama za kale na za sasa wameibuka na upinzani dhidi ya Qur-an na kudai kuwa kitabu hiki amekitunga mwenyewe Mtume Muhammad (s.a.w):

*"Au ndio wanasema kuwa hii Qur-an ameitunga (Muhammad)? Bali wao hawaamini lolote." (52:33)*

Dai hili la kumpa Mtume (s.a.w) utunzi wa Qur-an limewakilishwa katika sura mbali mbali na makafiri wa zama mbali mbali. Kwa ujumla makafiri wamedai kuwa Qur-an ni:



- (i) Mashairi aliyotunga Mtume Muhammad (s.a.w).
- (ii) Zao la njozi za Muhammad (s.a.w) zilizovurugika
- (iii) Zao la mwenye kujidhania kupata ufunuo
- (iv) Zao la mwenye kifafa na aliyepagawa na shetani.
- (v) Aya za shetani
- (vi) Uandishi wa Muhammad (s.a.w) kwa msaada wa Mayahudi na Wakristo.
- (vii) Utunzi wa Muhammad (s.a.w) ili kuleta umoja na ukombozi wa Waarabu.
- (viii) Utunzi wa Muhammad (s.a.w) ili kurekebisha tabia ya Waarabu.
- (ix) Utunzi wa Muhammad (s.a.w) ili ajinufaishe kiuchumi.
- (x) Utunzi wa Muhammad (s.a.w) ili kuwania madaraka na ukubwa.

Qur-an yenyewe inakanusha madai haya katika aya mbali mbali kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

فَلَا أَقْسِمُ بِمَا تُبْصِرُونَ ﴿٣٨﴾ وَمَا لَا تُبْصِرُونَ ﴿٣٩﴾ إِنَّهُ لَقَوْلُ  
 رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿٤٠﴾ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ قَلِيلًا مَّا تُوْمَنُونَ ﴿٤١﴾ وَلَا  
 يَقُولُ كَاهِنٍ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ﴿٤٢﴾ تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٣﴾  
 وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضُ الْأَقَاوِيلِ ﴿٤٤﴾ لَأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿٤٥﴾ ثُمَّ  
 لَقَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِينَ ﴿٤٦﴾

*Basi naapa kwa mnavyoviona. Na msivyoviona. Kwa hakika hii ni kauli iliyoletwa na Mjumbe (wa Mwenyezi Mungu) mwenye hishima (kubwa). Wala si kauli ya mtunga mashairi (kama mnavyosema). Ni machache sana mnayoyaamini. Wala si kauli ya mchawi (kama mnavyodai). Ni kidogo kabisa kuwaidhika kwenu. Ni mteremsho utokao kwa Mola wa viumbe vyote. Na kama*

(Mtume) angelizua juu yetu baadhi ya maneno tu, bila shaka tungalimshika kwa mkono wa kuume, (wa kulia). Kisha kwa hakika tungalimkata mshipa mkubwa wa moyo (69:38-46).

فَمَا مِنْكُمْ مِّنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَدِثِينَ ﴿٤٧﴾ وَإِنَّهُ لَتَذَكَّرَةٌ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٤٨﴾

وَإِنَّا لَتَعْلَمُونَ أَنَّ مِنْكُمْ مُّكَذِّبِينَ ﴿٤٩﴾ وَإِنَّهُ لَحَسْرَةٌ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٥٠﴾

وَإِنَّهُ لَحَقُّ الْيَقِينِ ﴿٥١﴾ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٥٢﴾

Na hapana yeyote katika nyie angeweza kutuzuia naye. Kwa hakika hii (Qur-an) ni mawaidha kwa wanaomcha Mwenyezi Mungu. Na kwa yakini tunajua kuwa miongoni mwenu wamo wanaokadhibisha. Na itakuwa ni sikitiko, (majuto) juu ya wanaokanusha. Na hakika hii ni haki ya yakini. Basi litukuze jina la Mola wako aliye Mkuu. (69:47-52)

Pamoja na aya hizi na nyingine nyingi zinazokanusha madai ya makafiri dhidi ya utunzi wa Qur-an bado Allah (s.w) ametoa changa moto kwa makafiri wa zama zote tangu ianze kushuka Qur-an hadi leo, kuwa:

وَإِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّمَّنْ

مِثْلِهِ وَادْعُوا شُهَدَاءَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٣﴾

"Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyomteremshia Mtumwa Wetu (kuwa hakuteremshiwa na Mwenyezi Mungu) basi leteni sura moja iliyofanywa na (mtu) aliye mfano wake, na muwaite waungu wenu bighairi ya Mwenyezi Mungu (wakusaidieni), ikiwa mnasema kweli." (2:23)

Pamoja na changamoto hii ya Qur-an, hebu tuangalie kwa undani kidogo udhaifu wa hizi hoja kumi za makafiri dhidi ya Qur-an:

**(i)Dai kuwa Qur-an ni Mashairi aliyotunga  
Muhammad (s.a.w):**

Dai hili lilitolewa na Makuraishi katika enzi hizo za kushuka kwa Qur-an pia linaendelea kutolewa na makafiri wa karne hizi. Kwa mfano Stober, baada ya kusoma tafsiri ya Qur-an alidai kuwa itakuwa imeandikwa na Mwarabu ambaye ni mweledi wa historia ya Mayahudi na mila za nchi yake ambaye pia ni mshairi mzuri.

**Udhaifu:**

Wasomaji wa mashairi ya Kiarabu wanafahamu kuwa mashairi hayo yana mizani, beti na vina na yanaimbika kwa kiasi kwamba wakati mwingine inabidi hata maana au sarufi viwekwe pembeni alimradi tu shairi liimbike. Hivi sivyo kabisa ulivyo mfumo wa Qur-an. Qur-an si mashairi bali ni ujumbe wenye maana kamili ulioandikwa katika fasihi ya hali ya juu kwa kuzingatia sarufi na miiko yote ya lugha hai.

Historia imeshuhudia kuwa Qur-an si mashairi. Ilikuwa kawaida ya washairi wakati ule wa Mtume (s.a.w) kubandika mashairi yao kwenye mlango wa Ka'aba kama changa-moto kwa washairi wengine. Ilitokea siku moja mshairi mashuhuri wa wakati huo, Labbiib ibn Rabiah, akabandika shairi lake kwenye mlango wa Ka'aba ili kutoa changamoto kwa washairi wengine. Shairi lake lilikuwa limetungwa kwa utaalumu mkubwa sana na lilikuwa zuri mno kiasi cha kutohubutu mtu yeyote kupambanisha shairi lake na hilo. Lakini baada ya kubandikwa kipande cha Sura ya Qur-an karibu na shairi lake, Labbiid mwenyewe (ambaye alikuwa Mshirikina) baada ya kusoma mistari michache ya sura hiyo alinaswa na mvuto wake na kuamini dini iliyofunuliwa kutoka kwa Allah (s.w) na kubandua shairi lake

**(ii)Dai kuwa Qur-an ni zao la njozi za Mtume (s.a.w)  
zilizovurugika:**

Katika miaka ya 1960 waandishi wawili, Anderson na Watt, walikuja na dai kuwa Qur-an ni zao la dhana (Wishful Thinking).

Walidai kuwa maneno na maelezo ya habari mbalimbali yaliyomo katika Qur-an yametokana na mawazo ya Mtume (s.a.w) aliyoyotoa kwa dhana tu. Watt, kwa kutumia njia za kisasa za kuchunguza fasihi alihitimisha kuwa angelifanya makosa makubwa sana kama angeliadini kuwa Qur-an ni ujumbe wa Allah (s.w) kwani: "Kila kinachoonekana kinatoka nje ya fikra za mwanaadamu, kwa kweli hutokana na mawazo yake ya kinjozi ambayo hutokea bila ya kufikiri." Kwa hiyo alieleza Watt kuwa Qur-an ni zao la dhana (Creative Imagination)

**Udhaifu wa Dai hili:**

Nadharia ya Anderson na Watt haina nguvu yoyote kwa sababu katika historia nzima ya mwanaadamu hapajatokea mawazo ya kinjozi hata yawe yamebuniwa kwa uhodari kiasi gani yakaunda kitabu mithili ya Qur-an au hata angalau sura moja iliyo mithili na sura yoyote ya Qur-an. Hata hivyo, jambo la kukumbuka ni kwamba dai hili la Anderson na Watt na makafiri wengine wa kisasa wenye mawazo kama hayo, si geni bali ni dai kongwe lililotolewa na jamii ya Mtume (s.a.w) mwenyewe kama tunavyofahamishwa katika Qur-an:

بَلْ قَالُوا أَضْغَثُ أَحْلَمَ بَلْ أَفْتَرْتَهُ بَلْ هُوَ شَاعِرٌ فَلْيَأْتِنَا بِآيَةٍ كَمَا أُرْسِلَ  
 الْأَوْلُونَ ﴿٥﴾

*"Lakini (Makafiri) walisema: "(Hayo anayosimulia) ni ndoto zilizovurugika. Bali ameyabuni (mwenyewe). Bali huyu ni mtunga mashairi tu. Basi atuletee Muujiza kama walivyotumwa (Mitume) wa kwanza." (21:5)*

**(iii)Dai la Kujidhanja Kupata Wahy (Self Revelation)**

Bwana E. Birmngham katika kitabu chake anadai kuwa, kwa sababu Muhammad (s.a.w) alikuwa mkweli na mwadilifu alichukia sana moyoni mwake kwa jinsi uovu na ufidadi ulivyoshamiri katika jamii yake. Kutokana na mwangaza aliokuwa nao yeye mwenyewe

binafsi akaona kuwa ipo haja ya kuijenga upya jamii hiyo. Huenda pia alisikia juu ya kitabu cha Wayahudi na Wakristo lakini hakupendezwa na mafundisho ya Utatu Mtakatifu (Trinity). Na yawezekana alisikia kuwa atakuja nabii kutoka katika eneo hilo. Mambo hayo yakawa yanazunguka ndani kabisa ya nafsi yake, hadi kufikia kuamini kuwa yeye ni mtume na ndipo akaanza kupata fikra za kimazezeta kuwa Malaika wanamsemesha.

**Udhaifu:**

Endapo kama chimbuko la Qur-an ni hisia za ndani za nafsi ya Muhammad (s.a.w) (subconsciousness), basi Qur-an itakuwa inatokana na elimu na mazingira yake. Lakini ukiiangalia Qur-an kwa makini utaona kuwa imetoa taarifa nyingi sana ambazo itakavyokuwa vyovyote haziwezi kuwa zimetoka katika nafsi ya Muhammad (s.a.w).

Kwa mfano Qur-an inaeleza matukio ya kihistoria au matukio yatakayotokea baadaye ambayo Muhammad(s.a.w) hakuyajua na wala hakuwa na namna ya kuyajua. Kwa mfano:

(1)Sura ya 18 ya Qur-an, Al-Kahf iliteremka baada ya Muhammad (s.a.w) kuulizwa maswali matatu na makafiri wa Makka ili kumjaribu. Maswali hayo waliyauliza baada ya kushauriana na watu wa Kitabu (Mayahudi). Maswali hayo yalikuwa:

- (i) Ni kipi kisa cha vijana wa pangoni?
- (ii) Ni kipi kisa cha Al-Khidhr?
- (iii) Unajua nini juu ya Dhul-qarnain?

Kwa kuwa maswali haya yalifungamana na historia ya Wakristo na Wayahudi, na habari zake hazikujulikana Hijaz, yalikusudiwa kumpima Mtume (s.a.w) kuwa kweli alikuwa Mtume wa Allah (s.w) aliyekuwa akipokea wahy kutoka kwake au ni mzushi tu.

Alipoulizwa maswali hayo Muhammad (s.a.w) alisema, "Nitakujibuni kesho" lakini hakusema, 'Inshaa-Allah'. Siku iliyofuata alikuwa bado hajapata wahy, hivyo walipokuja makafiri kusikiliza majibu, akawaambia waje siku iliyofuata. Walipokuja hakuwa na majibu. Hali ikaendelea hivyo kwa muda wa siku 15. Makafiri wakaanza kumkejeli na kumdhihaki. Muhammad (s.a.w) akahuzunika sana kwa kutopata wahy alioutazamia. Hatimaye Jibril (a.s) akamletea wahy akafahamishwa majibu ya maswali yote. Kule kuchelewa kuja kwa wahy kulikuwa ni fundisho kwake:

وَلَا تَقُولَنَّ لِشَايٍ إِنِّي فَاعِلٌ ذَٰلِكَ غَدًا ﴿٢٣﴾ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ ۗ وَأَذْكُرْ رَبَّكَ

إِذَا نَسِيتَ وَقُلْ عَسَىٰ أَنْ يَهْدِيَنِّي رَبِّي لِأَقْرَبَ مِنْ هَٰذَا رَشَدًا ﴿٢٤﴾

*Wala usiseme kamwe kwa lolote lile kuwa: "Nitalifanya kesho." Isipokuwa (uongeze) Ishaa-Allah. Na umkumbuke Mola wako unaposahau, na useme "Asaa Mola wangu ataniongoza njia iliyo karibu zaidi na uongofu kuliko hii" (18:23-24)*

Ingawa kuchelewa kwa kuja wahyi kulimsononesha sana Muhammad (s.a.w) ilikuwa ni ushahidi kuwa Qur-an haikutungwa na yeye. Laiti angelikuwa mtunzi wa Qur-an angeliyatoa majibu yale kesho yake ili kuepuka fedheha iliyompata.

Kuhusiana na hili la fikra za kimazezeta jambo la kuzingatia hapa ni kwamba Muhammad (s.a.w) aliulizwa maswali kuhusiana na matukio maalum,. Ni vigumu sana kuona jinsi ambavyo fikra za kimazezeta ya kidini zingeweza kumsaidia kujibu kwa usahihi maswali aliyoulizwa. Majibu ambayo yaliwatosheliza na kuwanyamazisha makafiri.

Na miongoni mwa mambo yanayojitokeza katika kisa hiki ni namna ulivyowasilishwa muda wa vijana waliokaa pangoni. Qur-an inasema:

وَلَيْسُوا فِي كُفْرِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةِ سِنِينَ وَأَرْبَادًا وَسَعًا ﴿٢٥﴾

*Na walikaa katika pango yao miaka mia tatu, na ongeza tisa.  
(18:25)*

Kwa nini aya haikusema moja kwa moja "miaka mia tatu na tisa" na badala yake ikasema "mia tatu na ongeza tisa?" Hii ni kwasababu vijana hao walikaa miaka 300 kwa kufuata kalenda ya jua (solar calendar) na ni miaka 309 kwa kufuata kalenda ya kuandama mwezi (lunar calendar). Sababu yake ni kuwa mwaka wa kuandama kwa miezi ni mfupi kwa siku 11 ukilinganishwa na ule wa jua. Hivyo  $11 \times 300/365 = 9$ . Yaani siku 11 mara 300 kugawanywa kwa 365 ni miaka 9. Hivyo basi madai kuwa mahesabu hayo sahihi yanatokana na kujidhania au mauzauza yaliyompanda Muhammad (s.a.w) hayana nguvu. Mfano mwingine tunaukuta katika sura ya 89 ya Qur-an ambayo ina aya inayoutaja mji wa kale sana wa Iram:

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦﴾ إِرْمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٧﴾ الَّتِي لَمْ يُخْلَقْ

مِثْلُهَا فِي الْبِلَادِ ﴿٨﴾

*Je! Hukuona jinsi Mola wako alivyowafanya Adi, wa (mji wa) Iram, wenye majumba marefu marefu ambayo hawakuumbwa mfano wao katika mji (mwingine) ." (89:6-8)*

Jina la mji huu lilikuwa halijulikani vizuri hata wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w). Kwa sababu hiyo kulikuwa na utatanishi mkubwa juu ya ni ipi Jiografia ya mji huo.

Hata hivyo utafiti uliochapishwa katika jarida la chama cha Jiografia huko Marekani liitwalo The National Geographic toleo la December 1978 umeonesha kuwa Iram ni jina la mji. Mwaka 1975 Dk. Paolo Mathiae wa chuo Kikuu cha Roma aligundua huko Syria maktaba ya kale sana iliyokuwa na vigae 15,000 vyenye maandishi. Miongoni mwa maelezo yaliyokuwamo katika vigae

hivyo ilikuwa ni taarifa kuwa watu wa mji wa Ebla walikuwa wakifanya biashara na watu wa mji wa Iram.

Ni vigumu sana kuona ni kwa vipi fikra za kizezeta zingeweza kumwongoza Muhammad (s.a.w) kutoa taarifa sahihi juu ya majumba yaliyoharibiwa miaka 3,000 kabla yeye hajazaliwa!

Isitoshe Qur-an imetamka katika sehemu kadhaa kuwa Muhammad na watu wake hawakuvijua baadhi ya visa vilivyotajwa katika Qur-an:

تِلْكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهَا إِلَيْكَ مَا كُنْتَ تَعْلَمُهَا أَنْتَ وَلَا قَوْمُكَ مِنْ  
قَبْلِ هَذَا فَاصْبِرْ ۗ إِنَّ الْعُقُوبَةَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٤٩﴾

*Hizi ni katika habari za ghaibu tunazokufunulia. Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii (Qur-an kuteremshwa). Hakika mwisho mwema ni wa wamchao Mwenyezi Mungu(11:49)*

Yafaa kuzingatia hapa kuwa hakuna hata mtu mmoja aliyejitokeza na kusema, "Ewe Muhammad, hayo uyasemayo si kweli. Mimi ni Mwarabu kama wewe na nilizijua habari hizi kabla ya huu wahy wako. Si hivyo tu, bali pia kama Muhammad (s.a.w) angekuwa ndiye mtunzi wa Qur-an asingethubutu kuitamka aya hii, au kama angeitamka basi angekuwa amejitia katika patapotea ya hatari kabisa kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, hata kama tukisema mathalan kuwa Muhammad (s.a.w) kwa hakika alizijua habari hizo kabla lakini hapa anasingizia tu, basi hapana shaka yeye hatakuwa mtu pekee anayezijua. Hivyo asingeweza kusema kwa ujasiri kiasi hiki juu ya kutokujua kwa wengine. Atakuwa na uhakika gani kuwa watu wote wengine hawazijui?



**Pili**, hata kama ni kweli kuwa watu wengine hawakujua habari hizo, maadui na wapinzani wake wangeweza kusingizia kuwa wao kwa hakika walikuwa wanazijua habari hizo hasa hasa ilivyokuwa kauli hiyo imetamkwa katika Qur-an baada ya kumaliza kukisimulia kisa chenyewe. Lakini pamoja na yote hayo hakuna mtu aliyeitumia fursa hiyo. Muhammad (s.a.w) angeweza kujua kuwa hakuna mtu atakayeitumia fursa hiyo?

**(iv) Dai kuwa Qur-an ni zao la Mwenye Kifafa na Aliyepagawa na Shetani:**

Waandishi kadhaa wa kikafiri katika maandishi yao wamedai bila kutoa ushahidi wowote unaotokana na historia kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa mwenye kifafa na mwenye kupagawa na Shetani na maneno yake alipokuwa katika hali ya ugonjwa ndiyo yaliyonukuliwa na kuunda Kitabu cha Qur-an!

**Udhaifu:**

Udhaifu wa dai hili tunaweza kuuona kwa kujiuliza maswali yafuatayo: Je, kifafa, ugonjwa mbaya kama tunavyofahamu, umewahi kumtokea mtu katika historia ya mwanaadamu na bado akawa mtu mwenye kutoa sheria za kufuatwa na umati wa watu wengi zaidi ya robo ya dunia? Je, historia ya mwanaadamu imewahi kumshuhudia mgonjwa wa kifafa au mwenye kupagawa na shetani kuwa na hadhi na uwezo mkubwa kuliko mtu yeyote ulimwenguni kama ilivyokuwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w)? Kama mgonjwa wa kifafa ndiye aliyeandika Qur-an, inakuwaje maandishi hodari wenye akili timamu na wanafalsafa wakubwa washindwe kuandika kitabu mithili ya angalau sura moja ya Qur-an na kukabili changa moto iliyotolewa na Qur-an karne nyingi zilizopita:

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَيْنَاهُ قُلْ فَاتَّبِعُوا سُورَةَ مِثْلِهِ ۖ وَادْعُوا مَنِ اسْتَلْعَتُمْ مِّنْ

دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾

*"Je! Ndiyo wanasema ameitunga? Sema: "Hebu (tungeni na nyie) mlete sura moja mfano wake na waiteni muwezao (kuwapata waje).- isipokuwa Mwenyezi Mungu - (wa kuwasaidieni) kama nyinyi mnasema kweli (kuwa haya ameyazua Muhammad)." (10:38)*

Kitaalam inafahamika kuwa ugonjwa wa kifafa baada ya muda humfanya mgonjwa kuwa taahira (punguani). Pia ugonjwa wa kifafa humdhoofisha mgonjwa na hutisha wauguzaji na wenye kumuangalia mgonjwa wakati ameshikwa na kifafa. Hapana ushahidi wowote katika historia ya Mtume (s.a.w) ambayo iko bayana mno kuliko historia ya mtu yeyote, kuwa alikuwa mwenye kifafa au mwenye kupagawa na shetani.

### **(v) Dai kuwa Qur-an ni aya za Shetani**

Katika mwaka 1988 Salman Rushdie, Muingereza mwenye asili ya kihindi, aliandika kitabu chake alichokiita "**Satanic Verses**" (yaani aya za Shetani) ambamo amemtukana Mtume (s.a.w), Uislamu na Qur-an kwa kuiita "aya za Shetani."

Katika kitabu chake hicho, Rushdie amedai kuwa hapakuwa na wahy wowote uliomshukia Muhammad (s.a.w) bali alikuwa akidai tu kuwa anashushiwa Wahy. Aidha Rushdie anadai kuwa Muhammad (s.a.w) alikuwa ni mtu aliyekuwa akifuata matashi yake mwenyewe akiongozwa na shetani na kwa hiyo yote yaliyomo ndani ya Qur-an ni maneno ya shetani.

Pia Rushdie katika kitabu chake hicho amedai kuwa Mtume (s.a.w) hakuwa na uwezo wa kutofautisha wahy kutoka kwa Malaika au wahy kutoka kwa shetani.

Vile vile Salman Rushdie amedai kuwa Mtume (s.a.w) hakuwa na kumbukumbu ya kile alichowasomea waandishi wake na wala hakuweza kutambua hata kile ambacho waandishi hao wamekiongeza kichini-chini. Amepiga mfano wa mwandishi

mmoja wa Kifursi kuwa alisomewa na Mtume aandike "Mwenye kusikia, mwenye kujua kila kitu" lakini yeye akaandika "Mwenye kujua na Mwenye hikma" na Mtume hakung'amua mabadiliko hayo!

### Udhaifu wa madai ya Salman Rushdie

Kwanza, ujumbe wa Qur-an umeteremshwa ili kumtoa binaadamu kutokana na hadaa zote za shetani. Shetani katika Qur-an ameelezwa wazi pamoja na vitimbi vyake na watu anaowatumia ili wanaadamu wasiweze kupotezwa naye. Hebu turejee aya chache zifuatazo:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيْطَانِ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَى بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ ﴿١١٢﴾

"Na namna hii tumemfanyia kila Nabii maadui, (nao ni) mashetani katika watu na (mashetani) katika majini. Baadhi yao wanawafunulia wenzao maneno ya kupamba pamba ili kuwadanganya. Na Mola wako angelipenda wasingelifanya hayo. Basi waache na uongo wao." (6:112)

يَدْبِينِ آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمُ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُم مِّنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْءَٰنَهُمَا إِنَّهُ يَرَئِكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِن حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيْطَانَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٢٧﴾

"Enyi wanaadamu! Shetani (Iblisi) asikutieni katika matata, kama alivyowatoa wazee wenu katika Pepo akawavua nguo zao ili kuwaonesha tupu zao. Hakika yeye pamoja na kabila yake wanakuoneni na hali ya kuwa hamuwaoni." Bila shaka sisi tumewajaalia mashetani kuwa marafiki wa wale wasioamini." (7:27)

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ  
 أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٦﴾

*"Kwa yakini Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni adui (yenu; kwa hivyo msimtii) kwani anaita (analiita) kundi lake liwe katika watu wa Motoni." (35:6)*

Kama Qur-an ni maneno ya Shetani, inakuwaje tena shetani mwenyewe ajidhihirishe kiasi hicho ili watu wamkimbie?

**Pili**, Allah (s.w) anasema kuwa laiti ingelikuwa hii Qur-an inatoka kwa mwingine asiye kuwa Yeye au kama ingekuwa ina waandishi wawili tofauti ambao wana malengo yanayopingana mmoja anavutia kwenye mema na mwingine kwenye uovu pangelikuwa na khitilafu nyingi (Qur-an 4:82). Je, uko mgongano wowote katika maneno ya Qur-an? Haupo, bali maneno yote ya Qur-an ni yenye kusadikishana. Hivyo haiwezekani Qur-an kuwa na mchanganyiko wa maneno ya shetani na ya Allah (s.w) kwa pamoja.

**Tatu**, Qur-an yenyewe imekataa kuwa Qur-an si maneno ya shetani.

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ ﴿٢٥﴾

*"Wala hii si kauli ya shetani aliyefukuzwa (katika rehema za Mwenyezi Mungu.) (81:25)*

**Nne**, Sote tunamfahamu shetani kuwa ni kiumbe dhaifu pamoja na kuwa hatumuoni. Sasa ikiwa shetani ameleta maneno na ujumbe mzito uliomo ndani ya Qur-an, kwanini na mashetani wengine nao hawakai pamoja kujibu zile changamoto zilizotolewa? "Mahound" kama alivyomwita Rushdie ni shetani mmoja tu, je

pamekuwa na uzito gani kwa wanaadamu pamoja na majini wakichanganyika kuleta mfano wa angalau sura moja ya Qur-an? Qur-an imetoa changamoto hiyo tangu kuanza kushuka kwake:

قُلْ لِّئِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَن يَأْتُوا بِمِثْلِ هَٰذَا الْقُرْآنِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ ۗ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴿٨٨﴾

*"Sema "Hata wakijikusanya watu (wote) na majini kuleta mfano wa hii Qur-an basi hawangaliweza kuleta mfano wake, hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao." (17:88)*

**(vi)Madai Kuwa Mtume (s.a.w) Aliandika Qur-an kwa Msaada wa Mayahudi na Wakristo:**

Tunakutana na madai mengine kuwa Mtume (s.a.w) aliandika Qur-an baada ya kusoma Biblia au wengine wanadai kuwa alifundishwa na Mayahudi na Wakristo ndio naye akaandika Qur-an kwa kuzingatia wakati na watu aliokuwa nao. Makafiri wa karne hii sio tu walioanzisha madai haya bali madai haya ni makongwe kama ilivyo kongwe Qur-an yenyewe.

Pametolewa madai mengi ya namna hii kuanzia karne hizo za kushushwa Qur-an kwa Mtume (s.a.w) mpaka hivi leo. Hebu tuangalie dai hili la baadhi ya makafiri wa karne hizi za usoni ambalo limegawanyika katika sehemu zifuatazo:

**(a)Dai la Kufundishwa na Padri Bahira:**

Baadhi ya makafiri wanadai kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) alijifunza Uyahudi na Ukristo katika safari zake mbili za biashara alizofanya Sham (Syria), hasa katika safari yake ya kwanza alipokutana na Padri Bahirah, alipokuwa na umri wa miaka 12. Tunavyojifunza katika historia ni kuwa Bahirah alikutana na Mtume (s.a.w) njiani na kuashiria kwa Ami yake Abutwalib, kuwa anamkisia kijana wake (Muhammad) ana sifa za yule mtume aliyetabiriwa katika Injili (Rejea Qur-an 61:6). Je, inamkinika kuwa mazungumzo haya ya njiani ya muda mfupi yawe ndiyo

yaliyompelekea Mtume (s.a.w) kuandika Qur-an miaka 28 baada ya makutano hayo? Ikumbukwe kuwa Mtume (s.a.w) alianza kushushiwa wahy wa Quran alipokuwa na umri wa miaka arobaini ambapo alikutana na Bahirah akiwa na umri wa miaka kumi na mbili.

Safari ya pili ya Mtume (s.a.w) kwenda Syria kwa biashara ni pale alipokodiwa na Bibi Khadijah alipokuwa na umri miaka ishirini na tano. Katika kumbukumbu za historia, Mtume (s.a.w) hakufanya mkutano wowote na Wakristo wala Mayahudi kabla ya Utume.

### **(b)Dai la Kunakili Biblia**

Aidha wengine wanasema Muhammad alinakili mafundisho ya biblia na halafu akadai kuwa yanatoka kwa Allah (s.w). Lakini inadaiwa kuwa hakunakili kila kitu bali alichagua sehemu fulani fulani alizoziona nzuri. Ushahidi wanaoutoa ni kuwa zipo sehemu katika Qur-an ambazo zinafanana na zile zilizomo katika Biblia. Hivyo, kwa kuwa ilitangulia Biblia kabla ya Qur-an ni wazi kuwa Qur-an ndiyo iliyochota kutoka katika Biblia. Madai haya ni dhaifu kwa sababu zifuatazo:

- (i) Muhammad (s.a.w) alisema na kusisitiza kuwa Qur-an imetoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w).
- (ii) Muhammad hakujua kusoma wala kuandika.
- (iii) Nakala ya kwanza ya Agano la Kale (Old Testament) kufasiriwa kwa lugha ya Kiarabu ilipatikana mwaka 900 A.D. Wakati huo ilikuwa imekwishapita miaka 200 tangu Muhamad kutawafu. Ama Agano Jipya (New Testament) lilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 1616, miaka elfu baada ya Muhammad (s.a.w) kufariki dunia!
- (iv) Qur-an (4:82) imesema kuwa lau kama hii Qur-an ingetoka kwa asiye kuwa Allah ingekuwa na khitilafu nyingi. Hivyo mtu mwenye shaka na aitumie fursa hiyo kutafuta khitilafu katika Qur-an.

- (v) Isitoshe, ikiwa kuna tungo mbili au vitabu viwili vimefanana, kufanana huko peke yake si ushahidi wa kutosha kuwa kitabu kimoja kimenakili kutoka katika kitabu cha kwanza kuandikwa. Hii ni kwa sababu yawezekana pia kuwa vitabu vyote viwili vikawa vimetegemea au kunakili kutoka katika kitabu cha tatu ambacho sisi hatukijui. Ilivyo ni kuwa Taurati, Injili na Quran ni vitabu vya Mwenyezi Mungu. Hivyo ni wazi kuwa kama Biblia imenukuu aya halisi za Tourati na Injili lazima aya hizo zitafanana na aya za Qur-an, kwa vile zote zinatokana na Allah(s.w).

Isitoshe utafiti uliofanywa na baadhi ya wanazuoni umeonesha kuwa amri kumi za Mungu zilizomo katika Agano la Kale kwa mfano, zimekuwemo katika vitabu vya Wahindu kabla ya kuja kwa Agano hilo la kale. Je, tuseme biblia ilinakili amri hizo kutoka kwa Wahindu? Si lazima iwe hivyo.

Pamoja na kufanana huko katika baadhi ya sehemu bado kimsingi Biblia na Qur-an zimetofautiana kiasi kikubwa.

### **Tofauti za Kimsingi Kati ya Qur-an na Biblia**

- (1) Biblia si kitabu kimoja bali ni mkusanyiko wa vitabu 73 kwa mujibu wa madhehebu ya Wakatoliki au vitabu 66 kwa mujibu wa madhehebu ya Waprotestanti. Vitabu hivyo viliandikwa na waandishi wasiopungua 40. Qur-an ni kitabu kimoja kilichotoka kwa Mwenyezi Mungu na aya zake zote ziliandikwa mara tu baada ya kushuka.
- (2) Biblia ni kitabu chenye mchanganyiko wa maneno ya Mwenyezi Mungu, Mitume na maoni ya wanahistoria. Qur-an ni neno la Allah (s.w) tu peke yake. Hata maneno ya Muhammad (s.a.w) hayamo katika Qur-an.

- (3) Katika Agano la Kale na Jipya yapo maelezo juu ya historia ya maisha ya Mitume. Kumbukumbu la Torati siyo tu ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watu bali pia historia ya maisha ya nabii Mussa (a.s). Injili ya Mathayo, Luka, Marko na Yohana zinaelezea historia ya Yesu kama ilivyosimuliwa na wanafunzi wake. Qur-an inataja habari za mitume waliopita ili kutoa mafundisho kwa watu lakini sio kama sira (biography) za mitume hao.
- (4) Biblia inavyo vitabu kadhaa ambavyo viliandikwa miaka mingi sana baada ya kutawafu mitume hao. Ndio maana wanazuoni Wakikristo hupata matatizo sana katika uchambuzi wa maandiko hayo kwani hushindwa kumjua nani mwandishi na aliandika lini. Kwa mfano katika Biblia iliyotolewa na **Collins** iitwayo: **Revised Standad Version ya 1971** uk. 12-17 imeandikwa kuwa Mwandishi wa 1 Samweli hajulikani, pia hajulikani mwandishi wa kitabu cha 2 Samweli, 1 Wafalme, 1 Mambo ya Nyakati, Esta, Ayubu, Yona na Habakuki. Hali kadhalika mpaka leo kuna wasiwasi kama kitabu cha Waebrania kiliandikwa na Paulo au na mtu mwingine. Na **Encyclopaedia Britannica** inakiri kuwa mpaka hivi hatuna uhakika jinsi au wapi vitabu 4 vya Injili vilizuka. Kinyume chake Qur-an yote iliandikwa wakati wa uhai wa Muhammad (s.a.w) na ikahifadhiwa vifuani na mamia ya watu.
- (5) Injili 4 zilizomo katika Agano Jipya siyo Injili zote zilizoandikwa. Zilikuwapo Injili nyingine nyingi. Ilifanyika Sinodi (mkutano wa wawakilishi wa makanisa) mwaka 325 ili kuamua Injili zipi zichukuliwe na zipi zikataliwe. Injili ya Barnabas ilikataliwa. Na katika historia ya Kanisa viko vitabu vilivyokubaliwa na baadaye kukataliwa na kinyume



chake. Ni binaadamu waliokuja baadaye ndio waliokuwa na uwezo wa kuamua lipi liwe neno la Mungu na lipi lisiwe. Katika Uislamu hakukuwa na Ijtimai yoyote iliyokaa kuamua sura ipi iwe Qur-an ama isiwe.

**(c)Dai la Kufundishwa na Jabir na Yasir:**

Makafiri wengine wanadai kuwa Mtume (s.a.w) alifundishwa na Jabir na Yasir waliokuwa watumwa kutoka Ethiopia (Uhabeshi) na wakasilimu mbele ya Mtume (s.a.w). Wanadai hivyo kwa kuwa bwana wao aliyekuwa akiwatesa sana kwa sababu ya kusilimu kwao alikuwa akiwapiga sana na kuwaambia: "Mnamfundisha Muhammad?" na walikuwa wakijibu "Kwa jina la Allah hatumfundishi bali ndiye anayetufundisha na kutuongoza".

Bila ya kuangalia majibu ya Jabir na Yasir, wameshikilia swali alilouliza bwana wao kuwa ndio ushahidi wao kuwa Mtume (s.a.w) alifundishwa Qur-an na watu hao.

Makafiri wengine wamedai kuwa Mtume (s.a.w) aliandika Qur-an kwa kusaidiwa na Salman aliyekuwa Mfursi (Persian). Salman alikuwa Mzoroastian kabla ya kuwa Mkristo huko Sham (Syria). Baadaye Salman alisafiri kwenda Madina ambapo alikutana na Mtume (s.a.w) na kusilimu.

Madai haya ni dhaifu kwa sababu mbili. Kwanza, karibu theluthi mbili ya Qur-an ilishuka Makka kabla Mtume (s.a.w) hajahamia Madina ambapo alikutana na Salman. Pili, fasihi ya lugha iliyotumika katika Qur-an ni ya hali ya juu mno kiasi ambacho wanafasihi mashuhuri wa Kiarabu walijaribu kwa miaka mingi kuigiza Qur-an bila ya mafanikio yoyote, itakuwaje Mfursi awe ndiye aliyeandika?

Madai haya yamerejewa kwenye Qur-an kama tunavyosoma katika aya ifuatayo:

وَلَقَدْ نَعَلْنَا أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ لِّسَانُ الَّذِي يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ  
 أَعْجَبِي ۗ وَهَذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُّبِينٌ ﴿١٠٣﴾

*"Na bila shaka tunajua kwamba wanasema: "Yuko mtu anayefundisha," (lakini) lugha ya yule wanayemuelekezea (kuwa anamfundisha Mtume) ni ya kigeni na hii (lugha iliyotumika katika Qur-an) ni lugha ya Kiarabu fasaha (bulbul)." (16:103)*

Madai yote haya pamoja na madai mengine mengi ambayo yamekuwa yakitolewa katika muda wote wa historia tangu ishuke Qur-an mpaka hivi leo, ni madai dhaifu mno ambayo hayana ushahidi wowote wa kiakili au wa kihistoria kuwa mwandishi (mtunzi) wa Qur-an ni mwengine asiye kuwa Allah (s.w).

Historia ya Mtume (s.a.w) imeandikwa na kuhifadhiwa vema kuliko historia ya mtu yeyote ulimwenguni, lakini hatuoni katika historia hiyo mahali popote tunapofahamishwa kuwa alikaa kitako kwa mtu yeyote kujifunza chochote. Kwani kama Muhammad (s.a.w) angelikuwa amesoma kwa Makasisi na Mapadri wa Kiyahudi na Kikristo au kwa mtu yeyote yafuatayo yangelijitokeza.

- (a) Muhammad (s.a.w) hangelificha kueleza hayo kwani alikuwa mashuhuri katika maisha yake yote kwa kuhubiri na kusema ukweli. Aliitwa As-swadiq - Mkweli. Ndani ya Qur-an yenyewe yamezungumzwa mambo yake ya ndani lakini bado hakuyaficha bali aliyadhahirisha kama yalivyo.
- (b) Hangelifundisha imani iliyo tofautiana sana na Ukristo na Uyahudi hasa kuhusu misingi ya dini hizo. Lakini imani ya Kiislamu ni mbali na ni kinyume kabisa na imani ya Kikristo na Kiyahudi.

- (c) Yeyote yule aliyemfundisha angeliweza kuandika kitabu mfano wa Qur-an angalau sura moja. Lakini hakutokea mtu yeyote mwenye uwezo huo.
- (d) Mayahudi ambao katika Qur-an wameitwa **"Ahlul-Kitaabi"** au wana wa Israil (Bani Israil) wamekuwa katika muda wote wa utume wake wakimhoji-hoji Mtume Muhammad (s.a.w) na kumcheza shere na walikuwa wakimficha Mtume vitabu vyao. Kunawezekanaje watu hawa kama ndio waliomfundisha Mtume Qur-an wawe wanamhoji hoji tena juu ya Qur-an? Kama wangalikuwa wamemfundisha Mtume chochote, kwa nini wasingelikuwa watu wa kwanza kutangaza kwa watu kuwa wao ndio waliomfundisha ili kuonesha uongo wa utume wake?
- (e) Mtume Muhammad (s.a.w) asingelikuwa mkweli katika utume wake na mwaminifu katika kutoa ujumbe aliotumwa autowe kwa watu, wafuasi wake wasingelikuwa wanyenyekavu kwake kiasi hicho na wasingelijizatiti katika kusimamisha mafundisho yake kiasi hicho katika mazingira magumu ya kufa na kupona. Historia inaonesha kuwa Waumini waliomfuata hawakumsaliti hata chembe.

### **Qur-an Inasadikisha Ukweli:**

Sifa ya Qur-an ni kuwa inasadikisha yaliyo ya kweli katika vitabu vilivyopita. Hivyo Muislamu anaweza kujua kwa urahisi kabisa lipi ni sahihi katika Biblia na lipi si sahihi. Lolote lililomo katika vitabu vilivyotangulia ambalo linawafikiana na Qur-an ni sahihi. Na lolote linalokwenda kinyume na Qur-an ni batili.

Jambo la kusisitiza hapa ni kuwa kuhusu vitabu vilivyotangulia Qur-an imevitaja kuwa ni Suhf, Zabur, Taurat na Injili. Muislamu anayevikana vitabu hivi katika asili yake anakoma kuwa Muislamu.

Kama tulivyokwishasema Biblia inavyo kwa uchache vitabu 66. Agano la Kale lina vitabu 39 na Jipya inavyo 27. Katika vile 39 vya Agano la Kale ni vitano tu ndivyo vinavyoitwa Taurati ya Musa.

Qur-an inapotaja Taurati haikusudii Biblia au vitabu 39 vya Agano la Kale wala hivyo vitano vinavyodaiwa kuwa viliandikwa na Musa. Qur-an imeitaja Taurati kama ni ufunuo kutoka kwa Allah. Lakini tunaona kitabu cha Mwanzo ambacho kina taarifa za zamani sana kabla ya yeye (Musa) kuzaliwa. Hatuna uhakika kama kitabu hicho cha Mwanzo ilikuwa ni sehemu ya ufunuo alioupata kwenye mlima Sinai.

Isitoshe nusu ya kitabu cha Kutoka inazungumzia habari za kutoka kwa Wayahudi Misri. Hayo pia yalitokea kabla ya Musa kupata Taurati. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati ambacho inadaiwa kiliandikwa na Musa kimeandikwa pia habari za kufariki kwa Musa:

*Basi Musa, mtumishi wa BWANA, akafa huko, katika nchi ya Moabu, kukabili Beth-peori; lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo. Musa alikuwa mtu wa miaka mia na ishirini alipokufa; jicho lake halikupofuka, wala nguvu za mwili wake hazikupunguka. Wana wa Israeli wakamwombolezea Musa katika uwanda wa Moabu siku thelathini; basi siku za maombolezo ya matanga ya Musa zikaisha. (Kumbukumbu la Torati 34:4-12)*

Ni dhahiri kuwa upo wasiwasi kama Nabii Musa (a.s) ndiye mwandishi wa kitabu hiki kwa sababu asingeweza kusimulia habari ya kifo chake na matanga yake mwenyewe.

**(vii) Dai kuwa Muhammad (s.a.w) alitunga Qur-an ili kuleta Umoja na Ukombozi wa Waarabu:**

Wako baadhi ya watu wanaodai kuwa Muhammad(s.a.w) aliitunga Qur-an ili awaunganishe na kuwakomboa Waarabu. Dai hili pia halina nguvu kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, lau dai hilo lingekuwa la kweli basi hapana shaka kuwa Qur-an ingetia msisitizo mkubwa sana katika mada ya umoja na ukombozi wa Waarabu. Kwa hakika hakuna aya hata moja katika Qur-an nzima inayolingania umoja na ukombozi wa taifa la Kiarabu. Itayumkinikaje basi Muhammad (s.a.w) atunge Kitabu kwa lengo la kujenga utaifa wa Waarabu na kusiweko katika kitabu hicho hata aya moja juu ya suala hilo?

**Pili**, msingi wa umma (taifa) unaofundishwa na Qur-an umejengwa juu ya itikadi ya haki na Qur-an inapinga hisia zote za utaifa kwa kufuata misingi ya rangi au kabila. Kila anayekubali itikadi ya Uislamu anakubalika katika umma wa Waislamu bila ya kujali rangi au kabila, au damu. Umoja uliodhihiri Arabia baada ya kushamiri kwa Uislamu ulikuwa umejengwa juu ya misingi ya Uislamu na siyo utaifa wa Kiarabu.

**Tatu**, lau umoja wa Waarabu ungekuwa ndilo jambo lililomsukuma Muhammad (s.a.w) hapana shaka angekubali kuwa mfalme wa Waarabu ili atumie fursa hiyo kujenga umoja wa taifa la Waarabu.

Lakini tunaona alikataa ufalme pale wakuu wa Kikuraysh walipotaka kumrubuni ili aache kuutangaza Uislamu.

**Nne**, zipo aya katika Qur-an zinazolikanusha dai hilo. Aya mojawapo ya Qur-an yasema:

وَإِذْ قَالَتِ الْمَلَأِيكَةُ يَمْرُؤِمُ إِنَّ اللَّهَ أَصْطَفٰكَ وَطَهَّرَكَ وَأَصْطَفٰكَ عَلٰى

نِسَاءِ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٤٧﴾

*"Na (kumbuka) Malaika waliposema: Ewe Maryamu! Kwa hakika*

*Allah amekuchagua na kukutakasa na kukutukiza kuliko wanawake wa ulimwengu (wote)." (3:42)*

Aya hii inamzungumzia Maryamu, mama yake Nabii Isa (a.s). Maryamu alikuwa ni Myahudi. Na Wayahudi walikuwa wanadharau Waarabu kuwa ni taifa duni. Muhammad (s.a.w) alikuwa ni Mwarabu na Qur-an imeshuka kwa lugha ya Kiarabu na watu wa mwanzo kusomewa hii Qur-an walikuwa Waarabu.

Swali ni hili: Ikiwa Muhammad (s.a.w) alitaka kukuza hisia za utaiifa wa Waarabu vipi basi aweke katika Qur-an aya hii inayomsifu mwanamke wa Kiyahudi kuwa amechaguliwa, ametakaswa na kutukuzwa na Allah(s.w) kuliko wanawake wote? Kwa nini asimsifie mama yake au mwanamke mwingine yeyote wa Kiarabu?

Aya nyingine ni hii ifuatayo:

يٰۤاَيُّهَا اِسْرٰٓءِيْلَ اذْكُرُوْا نِعْمَتِيَ الَّتِيْ اَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَاَنْتُمْ فَضَلْتُمْ عَلٰى

الْعٰلَمِيْنَ ﴿٤٧﴾

*Enyi kizazi cha Israili (Mayahudi)! Kumbukeni neema zangu nilizokuneemesheni, na nikakutukuzeni kuliko viumbe wengine. (2:47)*

Mifano hii yaonesha kuwa haiingii akilini kuwa Muhammad (s.a.w) awe ametunga Qur-an kwa lengo la kuleta umoja na utukufu wa taifa la Waarabu halafu ndani ya hiyo hiyo Qur-an akasifia kwa sifa za kipeo cha juu kabisa watu walio maadui wa Waarabu!

### **(viii) Dai la Kurekebisha Tabia ya Waarabu:**

Miongoni mwa wale wanaosema kuwa Muhammad (s.a.w) ndiye aliyetunga Qur-an wapo wanaodai kuwa Muhammad (s.a.w) alifanya hivyo kwa nia nzuri ya kutaka kujenga tabia na mwenendo mzuri miongoni mwa ndugu zake Waarabu. Yaani, Muhammad (s.a.w) alichukizwa sana na tabia mbaya walizokuwa nazo

Waarabu wa zama zake na hivyo akaona lazima ajitahidi kuziondoa. Na ili afanikishe lengo lake hilo akaona atunge Qur-an na asingizie kuwa inatoka kwa Allah (s.w). Dai hili pia halina nguvu kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, kujenga mwenendo mzuri wa tabia za watu ni jambo jema ambalo laweza kutekelezwa pasi na kutumia udanganyifu na uovu mwingine. Ni kipi kilichomfanya Muhammad (s.a.w) atumie uwongo na udanganyifu ili awafundishe watu kuwa wa kweli na waaminifu?

**Pili**, Qur-an imeitaja dhambi ya kuzua uwongo kuwa ni miongoni mwa madhambi makubwa:

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ قَالَ أُوحِيَ إِلَيَّ وَلَمْ يُوحَ إِلَيْهِ شَيْءٌ وَمَنْ قَالَ سَأُنزِلُ مِثْلَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمْرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُو أَيْدِيهِمْ آخِرِ جُودًا أَنْفُسَكُمْ أَيُّكُمْ أَلْيَوْمَ تُجْرَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ وَكُنْتُمْ عَنْ آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٩٣﴾

"Na nani dhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye uwongo Allah au mwenye kusema: "Nimeletewa wahyi," na hali hakufunuliwa chochote; na yule asemaye: "Nitateremsha (ufunuo) kama ule aliouteremsha Allah." Na kama ungewaona madhalimu watakapokuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyooshea mikono yao (na kuwaambia): "Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Allah pasipo haki na kwa vile mliyokuwa mkizifanyia kiburi Aya zake." (6:93)

Aya hii inasema hakuna dhalimu mkubwa kuliko yule mtu ambaye atamzulia uwongo Allah au atakayesingizia kuwa amepata

wahyi kutoka kwa Allah na ilhali hakupata. Halafu aya hii inataja jinsi watu wa aina hiyo watakvoyofedheheshwa na jinsi watakvoyopapatika wakati wa kutolewa roho zao.

Lau kama Muhammad (s.a.w) angekuwa ndiye aliyeitunga halafu akamsingizia Allah (s.w), asingeiweka aya kama hii katika Qur-an kwa sababu angehisi kuwa anajitukana mwenyewe na kujilaani mwenyewe. Pia kwa kuhofia kuwa yaweza kutokezea siku ambayo watu watamgundua angehakikisha kuwa anaiandika aya hii kwa namna ambayo haitamfedhehesha hapo atakapojulikana.

Angeweza kwa mfano kusema: "Hapana lawama kwa wale ambao, ikiwa hapana budi kusema uwongo kwa ajili ya Allah." St. Paulo kwa mfano ameandika hivi katika Biblia:

*Lakini ikiwa kweli ya Mungu imezidi kudhihirisha utukufu wake kwa sababu ya uongo wangu, mbona mimi ningali nahukumiwa kuwa ni mwenye dhambi." (Warumi 3:7)*

Aidha madai kuwa Muhammad (s.a.w) alitunga Qur-an ili aitumie katika kurekebisha mwenendo wa tabia za watu pia yanatenguliwa na ukweli kwamba Qur-an haikushuka yote mara moja bali ililetwa kidogo kidogo kwa muda wa miaka 23. Na katika kipindi hicho Qur-an ilitoa ahadi ya kujibu maswali yote yatakayoulizwa wakati Qur-an bado inashuka.

..... وَإِنْ تَسْأَلُوا عَنْهَا حِينَ يُنَزَّلُ الْفُرْقَانُ تَبَدَّ لَكُمْ.....

*.....Na kama mtayauliza, maadam inateremshwa Qur-an mtabainishiwa....." (5:101)*

Watu waliitumia fursa hiyo iliyotolewa na Qur-an kuuliza maswali mbali mbali kama vile juu ya ulevi, kamari, hedhi, ngawira, roho na hata juu ya watu kama Dhur-qarnain. Katika kuyajibu maswali hayo



Qur-an imetumia msemu "Wanakuuliza juu ya jambo kadhaa. Sema: Lipo namna kadhaa." Kwa mifano halisi tazama Qur-an 2:189, 2:215, 2:217, 2:219, 2:220, 2:222, 5:4, 7:187, 8:1, 17:85, 18:83, 20:105 na 79:42.

Tatizo linalojitokeza hapa ni kwamba Muhammad (s.a.w) asingeweza kujua kuwa maswali aliyowaruhusu watu kuuliza yatakuwa yanahusu marekebishi ya mwenendo na tabia za watu. Kwani inadaiwa kuwa haitakuwa jambo la busara kwa rais anayetaka kuzungumzia hali ya chakula nchini mwake kuwaita maandishi wa habari na kuwaruhusu waulize maswali yoyote yanayowatatiza. Rais huyo atakuwa na hakika gani kuwa watauliza juu ya hali ya chakula na siyo juu ya wafungwa wa kisiasa?

### **(ix)Dai kuwa Muhammad Alitunga Qur-an ili Ajinufaishe Kiuchumi**

Baadhi ya watu wanasema kuwa Muhammad (saw) ndiye mtunzi wa Qur-an na alifanya ili ajinufaishe kiuchumi. Wanasema kuwa yawezekana kuwa Muhammad (s.a.w) aliitunga Qur-an lakini akasema imetoka kwa Allah ili ajipatie manufaa makubwa zaidi. Kama tunazungumzia uwezekano, ni kweli kuwa uwezekano kama huu unaweza kuwepo. Swali la kujuliza ni hili:Ni manufaa gani hasa ambayo Muhammad (s.a.w) tuseme alikuwa akiyawania? Manufaa hayo yanaweza kuwa ni wasaa wa mali, mamlaka, au ufalme. Hebu tuyafuatilie zaidi madai haya.

### **Muhammad hakuwa tajiri baada ya Utume**

Kusema kuwa Muhammad (s.a.w) aliitunga Qur-an ili ajinufaishe maana yake ni kuwa Muhammad (s.a.w) alikuwa mrongo aliposema Qur-an inatoka kwa Allah (s.w). Madai kuwa Muhammad (s.a.w) alikuwa mwongo yanakwenda kinyume na ushahidi wa historia ya maisha yake. Hata hivyo kwa sababu za kutaka kuendeleza mjadala na utafiti wetu, hebu na tuuweke kando ukweli na uaminifu wa Muhammad (s.a.w) na tuchunguze alijinufaishaje kwa kudai kuwa Qur-an ni neno la Allah(s.w).

Tukianza na hali yake kiuchumi tunaona kuwa alikuwa na hali nzuri kabla kuliko baada ya kupata utume. Kabla ya kupata utume, alipokuwa na umri wa miaka 25 alimwoa bibi Khadija ambaye alikuwa ni mfanyabiashara tajiri sana. Muhammad (s.a.w) aliishi naye kwa wasaa mkubwa na pasi na dhiki yoyote. Baada ya kupata utume hali yake kiuchumi ilikuwa ngumu kwa kuwa karibu mali yote ilitumika kuwasaidia Waislamu wachache waliokuwa wakiteswa na kubughudhiwa na makafiri wa Makka. Na hata baada ya kusimama dola ya Kiislamu hali ya kiuchumi ya Muhammad (s.a.w) ilikuwa ndio ngumu zaidi.

### **Baadhi ya mifano ya hali yake kiuchumi**

Katika kitabu cha Hadith cha An-Nawawi, mmoja wa wakeze Mtume (s.a.w) Bibi Aisha (r.a) amesema kuwa wakati mwingine ulipita mwezi mzima au hata miezi miwili pasi na moto kukokwa katika nyumba ya Mtume (s.a.w) kwa sababu hakukuwa na cha kupika. Walikuwa wakiishi kwa kula tende na kunywa maji. Wakati mwingine walipata maziwa ya mbuzi kutoka kwa watu wa Madina.

Katika kitabu cha maisha ya Muhammad (s.a.w) kilichoandikwa na Martin Lingas<sup>1</sup> imeelezwa kuwa Mtume (s.a.w) na familia yake walikuwa wanaishi katika hali ngumu sana kiuchumi. Wakati mwingine hawakupata japo hizo tende za kutosha.

Hali hii haikuwa ni matatizo ya kupita tu bali ilikuwa ndio mwenendo wa kudumu wa maisha. Mtume (s.a.w) aliishi katika hali hiyo wakati ambao angeweza kuishi kama mfalme kama angetaka. Kwa hakika ni kutokana na kuamua kwa makusudi kuishi maisha hayo pamoja na kuwa angeweza kuishi maisha ya anasa ndipo wakeze Mtume (s.a.w) wakaja juu. Kwa nini waendeleo kuishi maisha ya dhiki na hali wanaweza kuishi kwa wasaa? Mtume alitatizwa na manung'uniko hayo ya wakeze.

---

1. *Muhammad His Life Based on the Earliest Sources*

Allah(sw) akamteremshia wahyi uliomwamuru awaambie wakeze ama wamchague Allah(s.w) na Mtume wake au starehe ya kupita ya ulimwengu huu:

يَتَأْتِيهَا اللَّيْلُ قُلُوبًا لِأَزْوَاجِكَ إِنْ كُنْتُمْ تُرِيدُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا  
 وَزِينَتَهَا فَتَعَالَيْنَ أُمَتِّعْكَنَّ وَأَسْرِحْ كُنَّ سَرَّاحًا جَمِيلًا ﴿٢٨﴾ وَإِنْ كُنْتُمْ  
 تُرِيدُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالذَّارَ الْآخِرَةَ فَإِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْمُحْسِنَاتِ مِنْكُمْ  
 أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾

*Ewe Mtume! Waambie wake zako. "Ikiwa mnapenda maisha ya (hii) dunia na uzuri wake, njooni, nitakupeni kitoka*

*nyumba, na kukuacheni muwachano mzuri. Na kama mnamtaka Allah na Mtume wake na nyumba ya Akhera, basi Allah amewaandalia wafanyao mema hayo, miongoni mwenu, malipo makubwa." (33:28-29)*

Kuhusiana na jinsi chumba cha Mtume kilivyokuwa Umar (r.a) anasema:

*Niliona kuwa mali yote iliyokuwa chumbani mwake ilikuwa ni vipande vitatu vya ngozi na fungu dogo la shayiri lililokuwa katika koa. Nikaangaza huku na huko lakini sikuona kitu kingine chochote. Nikaanza kulia. Akaniuliza: Kwanini unalia? Nikajibu: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Kwanini nisilie? Naona alama ya mkeka katika mwili wako, na naangalia pia mali yote uliyo nayo katika chumba hiki. Ewe, Mjumbe wa Allah! Mwambie Allah atuzidishie riziki, Waajemi na Warumi ambao hawana imani ya kweli na ambao hawamwabudu Allah bali wafalme wao - akina Kaizari - wanaishi katika mabustani yanayopita mito kati yao, lakini Mjumbe mteule na mja wa Allah akaishi katika umasikini kama huu!' Mtume*

*alikuwa amejipumzisha hali ya kuwa amelalia mto, lakini aliponisikia nikisema hivyo, akaketi na kusema; 'Ewe Umar! Je, bado una shaka juu ya jambo hili? Raha na starehe za akhera ni bora kuliko raha na starehe za ulimwengu huu. Makafiri wanafaidi starehe zao zote hapa duniani na sisi tutakuwa na starehe zetu zote huko akhera.' Nikamwomba Mtume kwa kusema: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Niombe msamaha kwa Allah. Kwa hakika nilikosea.'*

Alipoulizwa juu ya kitanda cha Mtume (s.a.w) kilivyo, Bibi Aisha alijibu: 'Ni ngozi iliyojazwa magome ya mitende.'

Ikumbukwe kuwa Muhammad (s.a.w) aliishi maisha ya namna hiyo kwa hiari yake kwa sababu kila alipopata zawadi aliigawa yote kwa mafakiri pasi na yeye mwenyewe kuchukua chochote. Safari moja alipewa na Chifu wa Fidak zawadi zilizobebwa na ngamia wanne, lakini alizigawa zote.

Wakati wa kutawafu kwake Muhammad (s.a.w) hakuwa na hata senti moja mfukoni. Alikuwa na dinari saba karibu ya kufariki kwake lakini akazigawa kwa maskini kabla ya kufariki. Isitoshe alipofariki, pamoja na ushindi mkubwa alioupata katika vita na pamoja na kuwa alikuwa ndiye kiongozi wa dola ya Kiislamu, Muhammad (s.a.w) alikuwa akidaiwa na ngao yake ilikuwa mikononi mwa Myahudi mmoja wa Madina kama rehani ya deni hilo.

Ipo mifano mingine mingi inayoonesha kuwa katika kipindi chake chote cha utume, Muhammad (s.a.w) aliishi katika maisha ya kujinyima. Kutokana na ushahidi huu unaotokana na historia ya maisha yake, ni wazi kuwa madai kuwa Muhammad (s.a.w) aliitunga Qur-an ili apate kujinufaisha kiuchumi hayana msingi.

**(x) Dai kuwa Muhammad (s.a.w) aliitunga Qur-an ili Kuwania Madaraka na Ukubwa:**

Aidha, fikra kuwa huenda Muhammad (s.a.w) aliitunga Qur-an kwa sababu aliwania ukubwa na madaraka pia ni vigumu sana kuithibitisha, kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, Muhammad (s.a.w) alijulikana sana ulimwengu mzima kama kiongozi aliyefanikiwa sana katika historia ya binaadamu. Mtu mwenye sifa kama hizo angeweza kuchukua uongozi na madaraka bila hata kudai kwanza utume. Kwa hakika kufanya hivyo kungekuwa rahisi zaidi kwake kama alikuwa anataka madaraka kuliko kudai utume kwanza.

**Pili**, Qur-an imetamka wazi wazi kuwa hakuna mtu yeyote ikiwa ni pamoja na Muhammad (saw) mwenyewe awezaye kuleta mfano wake. Kama lengo lake lilikuwa kupata utukufu miongoni mwa watu angejitapa kuwa ndiye mtunzi wa kitabu hiki kinachovishinda vitabu vyote.

Hata hivyo tabia yake haikuonesha dalili zozote za mtu anayepigania madaraka au utukufu. Kupenda madaraka na utukufu kwa kawaida kunajionesha kwa mtu kutaka majumba ya fahari ya kifalme, nguo za kipekee, kutaka kusifiwa na kuabudiwa na watu, n.k. Muhammad (s.a.w) alionesha mfano wa ajabu kabisa wa unyenyekevu. Pamoja na amana kubwa ya unabii aliyokuwa nayo na dhamana kubwa sana ya kuongoza dola ya Kiislamu, Muhammad (s.a.w) alikuwa akisaidia kufanya kazi ndogo ndogo za nyumbani. Akishona nguo zake na kuripea viatu vyake na akimkama mbuzi wake. Alikuwa akimsikiliza kwa makini kila aliyemwendea, kiasi ambacho Qur-an imesema makafiri walikuwa wakilalamika kwanini anawasikiliza hata wanyonge (Qur-an 9:61).

Wakati fulani Waislamu walikuwa wanasimama walipotaka kumwamkia kama ishara ya heshima. Lakini aliwakataza na kuwaambia, “Msisimame kama Waajemi wanavyofanya, baadhi yao kuwatukuza wengine.”

Mifano mingine ya unyenyekevu wake ni ile iliyotajwa na mwanachuoni maarufu Dk. Gamal Badawi:

*Siku moja Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa akisafiri pamoja na baadhi ya maswahaba wake ambao njiani walipiga kambi na kuanza kupika chakula kwa kugawanya kazi za kufanya. Muhammad (s.a.w) alichagua kazi ya kutafuta kuni. Maswahaba wake wakamwambia asifanye kazi yoyote kwani wao watamfanyia. Muhammad (s.a.w) akawajibu, "Najua kuwa mnaweza kunifanyia lakini nachukia kupewa nafuu kuliko nyinyi."*

Mfano mwingine ni huu:

*Mtu mmoja alimwendea Mtume (s.a.w) huku akitetema kwa kumheshimu. Muhammad (s.a.w) alimwomba mtu yule amsogelee na akamkumbatia na kumpigapiga mgongoni kwa huruma kubwa, halafu akamwambia, 'Tulia ndugu yangu, mimi ni mtoto wa mwanamke aliyekuwa anakula mkate mkavu.'*

Aidha imeripotiwa kuwa baadhi ya watu walimwendea Mtume (s.a.w) na wakamsifu kwa kusema: "Ewe Mjumbe wa Allah(sw), wewe u-mbora kuliko sote na wewe ni mtoto wa mbora wetu, wewe ni kiongozi wetu na ni mtoto wa kiongozi wetu. Jibu lake lilikuwa:

*Enyi watu, semeni lile mlilolisema mwanzo (yaani "Ewe Mjumbe wa Allah,") na msikubali shetani awapotezeni. Mimi ni Muhammad, mja wa Allah na Mjumbe wake. Sipendi nyinyi muiinue daraja yangu kuliko ile daraja ambayo Allah (s.w) amenipa.*

Vile vile ilisadifu kwamba kifo cha mwana mpenzi wa Muhammad (s.a.w) aliyeitwa Ibrahim kilitokea na jua likapatwa. Watu wakasema huo ni mwujiza utokao kwa Allah unaoonesha kuwa mbingu na ardhi zina majonzi kuhusiana na kifo cha Ibrahim.

Aliposikia maneno hayo, Muhammad (s.a.w) alikasirika sana akasema: "Jua na mwezi ni dalili mbili miogoni mwa dalili nyingi za Allah (s.w). Jua na mwezi havipatwi kwa sababu ya kufa au kuzaliwa mtu yeyote."

Mifano yote hii inaonesha kuwa madai kwamba Muhammad (s.a.w) aliitunga Qur-an ili ajipatie madaraka na utukufu pia hayana nguvu.

Kwa nini kwa mfano, atunge kitabu kinachomwamuru yeye mwenyewe awatangazie watu wote kuwa yeye hana uwezo wowote wala hana elimu ya ghaibu na kwamba lau angekuwa nayo angejizidishia heri zote na shari isingemgusa(Qur-an 7:188)?

Au kwanini aandike kitabu kinachomwamuru aseme kwamba hakuja na itikadi mpya na kwamba hata hakutazamia kuwa kitabu kama hiki kingefunuliwa kwake na hivyo awaambie watu kuwa yeye ni mtu kama watu wengine? (Qur-an 46:9, 28:86, 8:110 na 6:50).

**Pili**, hisia za Muhammad (s.a.w) baada ya kupata wahy mwanzo zaonyesha kuwa hakuwa anawania ukubwa kisiri siri. Baada ya yaliyomtokea katika pango la Hira alirejea haraka kwa mkewe hali ya kuwa anatetemeka kwa hofu kana kwamba alikuwa na homa kali. Akamwomba mkewe amfunike nguo nzito. Baada ya hofu kumwondoka akamsimulia mkewe yote aliyoyaona kisha akasema: 'Ewe Khadijah, ni lipi linalotaka kunisibu?'Ni dhahiri kuwa kama kusingizia kupata wahy ilikuwa ni mbinu tu ya kujipatia ukubwa Muhammad (s.a.w) asingehofia chochote. Ushahidi uliopo unaonesha kuwa hakupanga apate wahy wala hakutegemea kupata wahy. Alijistukia tu analetewa wahy. Na juu ya jambo hili Qur-an yasema:

وَمَا كُنْتَ تَرْجُو أَن يُلْقَىٰ إِلَيْكَ الْكِتَابُ إِلَّا رَحْمَةً مِن رَّبِّكَ <sup>ط</sup>

*Nawe hukuwa unatumai ya kwamba utaletewa Kitabu, lakini ni rehema ya Mola wako. (28:86)*

**Tatu** Jambo jingine linalozidi kudhihirisha kuwa Muhammad (s.a.w) hakuwania ukubwa na utukufu ni kule kukataa kwake alipopewa pendekezo hilo na Maquraishi.

Wakati ambapo Waislamu walikuwa wakibughudhiwa na kuteswa, Machifu wa Maquraishi wa Makka walimtaka Muhammad (s.a.w) aache kuhubiri dini ya Uislamu na wao watampatia alitakalo miongoni mwa yafuatayo:

- (1) Kama anataka mali watampatia mali nyingi hadi awe tajiri kuliko watu wote.
- (2) Kama anataka utukufu, watamfanya bwana wao na hawataamua lolote bila ridhaa yake.
- (3) Kama anataka ufalme, watamfanya awe mfalme wao, na
- (4) Kama amepagawa na pepo na ameshindwa kumwondoa mwilini mwake wao watamtafuta mganga atakayemtibu kwa gharama yoyote.

Lakini Muhammad (saw) aliyakataa yote hayo na badala yake akamsomea mjumbe aliyetumwa kumletea mapendekezo hayo, Utbah ibn Rabia, aya ya 1-38 ya Sura ya 41.

### **Uthibitisho kuwa Qur-an ni neno la Allah (s.w)**

Baada ya kuona madai mbali mbali yaliyotolewa kupinga kuwa Qur-an si kitabu cha Allah (s.w) na baada ya kuona udhaifu wa madai hayo, ni vyema sasa kuonesha hoja madhubuti zinazothibitisha kuwa Qur-an ni kitabu cha Allah (s.w). Katika kuthibitisha kuwa Qur-an ni kitabu cha Allah (s.w), tuna vigezo viwili (a) Qur-an yenyewe na (b) Historia ya kushuka kwake.

#### **(a)Uthibitisho Kutokana na Qur-an Yenyewe:**

Vipengele vinavyothibitisha kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah (s.w) kutokana na Qur-an yenyewe ni hivi vifuatavyo:

- (i) Kutojua kusoma na kuandika kwa Mtume Muhammad (s.a.w).
- (ii) Qur-an yenyewe inajieleza kuwa ni Kitabu cha Allah (s.w).



- (iii) Hali aliyokuwa nayo Mtume katika kupokea wahyi.
- (iv) Qur-an kushushwa kidogo kidogo kwa kipindi cha miaka ishirini na tatu (23).
- (v) Kukosolewa kwa Mtume katika Qur-an.
- (vi) Kutokea kweli yale yaliyotabiriwa katika Qur-an.
- (vii) Mpangilio wa Qur-an.
- (viii) Maudhui ya Qur-an na mvuto wa ujumbe wake.
- (ix) Wanaadamu kushindwa kuandika kitabu mithili ya Qur-an.

Hebu tuangalie jinsi kila kipengele kinavyothibitisha kuwa Qur-an ni neno la Allah (s.w).

**(i)Mtume Muhammad (s.a.w) Kutojua Kusoma na Kuandika:**

Iwazi mno katika historia yake kuwa Mtume (s.a.w) hakujuza kusoma wala kuandika. Ukweli huu wa historia unathibitishwa na aya za Qur-an zifuatazo:

قُلْ يَتَّيْبُهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ  
 وَالْأَرْضِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ النَّبِيِّ الْأُمِّيِّ  
 الَّذِي يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَكَلِمَاتِهِ وَاتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٥٨﴾

"Sema (Wewe Nabii Muhammad): Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Allah kwenu nyinyi nyote, (Allah) ambaye ana ufalme wa mbingu na ardhi, hapana aabudiwaye (kwa haki) ila Yeye, Ndiye ahuishaye na ndiye afishaye. Basi mwaminini Allah na Mtume wake, aliye Nabii Ummy, (asiyejua kusoma wala kuandika), ambaye humwamini Allah na maneno yake na mfuateni yeye ili mpate kuongoka." (7:158)

وَمَا كُنْتَ تَتْلُو مِنْ قَبْلِهِ مِنْ كِتَابٍ وَلَا  
 تَخُطُّهُ بِيَمِينِكَ إِذًا لِأَنَّكَ لَمُبْطَلُونَ ﴿٤٨﴾

"Na hukuwa mwenye kusoma kitabu chochote kabla ya hiki,

*wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume, ingekuwa hivyo wangepanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki)."*  
(29:48)

Sababu ya Mtume (s.a.w) kutojua kusoma wala kuandika imebainishwa wazi katika aya hii ya (29:48) kuwa angelijua kusoma na kuandika watu wakaidi wasio tayari kumwamini Mtume na kuamini Qu-ran kwa sababu si maneno ya Allah(s.w) bali ni maneno aliyoyatunga Mtume (s.a.w) au ni maneno aliyoyanakili kutoka kwenye vitabu vya kale au ni maneno aliyofundishwa na watunga mashairi mashuhuri na kuyanukuu kwenye kitabu. Mtume (s.a.w) angalijua kusoma na kuandika ingalikuwa vigumu sana kuonesha udhaifu wa madai haya. Lakini kutojua kusoma wala kuandika kwa Mtume (s.a.w) kumewafanya wapinzani wengi wakose hoja ya uwazi ya kukataa kuwa Qur-an si Kitabu cha Allah (s.w).Hata hivyo, pamoja na ukweli wa historia kuwa Mtume (s.a.w) hakuwa ni mwenye kujua kusoma wala kuandika, walitokea watu waliojitia upofu na kudai kuwa Qur-an ni maneno ya Muhammad (s.a.w). Ili kuwahuzunisha na kuwaonesha kuwa ni waongo katika madai yao hayo, Allah (s.w) aliwawekea watu hao na walimwengu kwa ujumla changa moto ambayo tutaiona katika kipengele cha (ix).

Kwa hiyo Mtume Muhammad (s.a.w) kutojua kwake kusoma wala kuandika na bado akawasilisha kwa watu ujumbe mzito wenye hekima kubwa na wenye kumuongoza mwanaadamu kwa usahihi katika kila kipengele cha maisha yake, ujumbe ambao hapana yeyote anayeweza kuleta mfano wake ni ushahidi mkubwa kuwa Qur-an yote kama ilivyo ni maneno ya Allah (s.w).

## **(ii)Qur-an Yeneyewe Inajieleza kuwa ni Ufunuo**

### **Kutoka kwa Allah (s.w) :**

Ukiisoma Qur-an kwa makini utakuta kuna aya nyingi zinazojieleza kuwa Qur-an imeshushwa kutoka kwa Allah, kama inavyodhihirika katika aya chache zifuatazo:

لَكِنَّ اللَّهَ يَشْهَدُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ أَنْزَلَهُ بِعِلْمِهِ ۗ وَالْمَلَائِكَةُ يَشْهَدُونَ  
وَكَفَى بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿١١٦﴾

*Lakini Allah anayashuhudia kuwa aliyokuteremshia (kuwa ni haki) ameyateremsha kwa ilimu yake, na Malaika (pia) wana shuhudia. Na Allah anatosha kuwa shahidi. (4:166).*

تَنْزِيلِ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾ أَمْ يَقُولُونَ  
أَفْتَرَيْنَاهُ بَلْ هُوَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ لِتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أَتَتْهُمْ مِنْ نَذِيرٍ مِّنْ  
قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ ﴿٣﴾

*"Uteremsho wa Kitabu hiki hauna shaka kuwa umetoka kwa Muumba wa ulimwengu. Je, wanasema: "Amekitunga mwenyewe". (Sivyo hivyo). Bali hicho ni haki itokayo kwa Mola wako ili uwaonye watu wasiojiwa na muonyaji kabla yako. Huenda wakaongoka." (32:2-3)*

وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ هُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ إِنَّ اللَّهَ  
بِعِبَادِهِ لَخَبِيرٌ بَصِيرٌ ﴿٣١﴾

*Na Kitabu tulichokuletea kwa wahyi ndicho cha haki, kinasadikisha (vitabu) vilivyokuwa kabla yake. Bila shaka Allah kwa waja wake ni Mwenye kuwajua vyema na kuwaona vizuri." (35:31)*

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا  
Ni mwenye kuleta baraka (kweli kweli) yule aliyeteremsha Qur-an kwa mja wake, ili awe muonyaji kwa walimwengu wote. (25:1)

تَنْزِيلِ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ

*Uteremsho wa Kitabu hiki umetoka kwa Allah, mwenye nguvu, na mwenye hikima. (45:2)*

Aya zote hizi na nyingi nyinginezo kama hizi zilizomo ndani ya

Qur-an hujieleza wazi wazi kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah (s.w) alichowashushia wanaadamu kupitia kwa Mtume Muhammad (s.a.w). Pangelikuwa na haja gani Mtume kuandika kitabu kisha adai kuwa kinatoka kwa Allah (s.w) tukikumbuka kuwa yeye amekuwa mwaminifu na mkweli katika historia yote ya maisha yake.

**(iii)Jinsi Mtume Muhammad (s.a.w) alivyoipokea Qur-an:**

Tumejifunza kuwa Allah (s.w) huwasiliana na wanaadamu kwa njia ya Wahyi (ufunuo) kwa kutumia njia za mawasiliano zifuatazo:

- Il-hamu.
- Kutumwa Malaika.
- Kuongelehwa nyuma ya pazia.
- Maandishi (yaliyoandikwa tayari).
- Ndoto za kweli.

Qur-an ilishushwa kwa Mtume (s.a.w) kwa njia hii ya wahyi kupitia kwa Malaika Jibril.

Kuonesha kuwa Qur-an ni neno la Allah (s.w) na wala si tungo za Mtume Muhammad (s.a.w) ni ile hali aliyokuwa nayo wakati wa kupokea wahyi. Wakati wa mwanzo mwanzo wa kuanza kushushiwa wahyi Mtume (s.a.w) alikuwa akiyarudia haraka haraka yale aliyokuwa anasomewa na Malaika Jibril kwa wasi wasi kuwa atasahau. Ndipo Allah (s.w) akamtoa wasi wasi huo kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

لَا تَحْرِيكَ بِهِ لِسَانَكَ لِتَتَعَجَّلَ بِهِ ۖ ﴿١٦﴾ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ۖ ﴿١٧﴾  
 فَإِذَا قَرَأْنَاهُ فَاتَّبِعْ قُرْآنَهُ ۖ ﴿١٨﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ۖ ﴿١٩﴾

*Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka.Wewe sikiliza tu. Usiseme kitu). Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha (kukukusanyia na kukusomesha). Wakati*

*tunapokusomea, basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu yetu kuubainisha (kukubainishia). (75:16-19)*

سَنُقَرِّئُكَ فَلَا تَنْسَى ۝ إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفَى ۝

*Tutakusomesha (tutakusomea) wala hutasahau. Ila Akipenda Mwenyezi Mungu; Yeye anajua yaliyodhahiri na yaliyofichikana. (87:6-7)*

Kwa hiyo kutokana na aya hizi Qur-an si maneno ya Mtume Muhammad (s.a.w) aliyoyotoa kichwani mwake. Kwani yangelitoka kichwani mwake asingelikuwa na wasi wasi wowote kuwa atakuja yasahau. Alikuwa na wasi wasi kwa sababu yeye akiwa ni Mtume wa Allah(s.w) alijua fika kuwa jukumu lake kubwa ni kuufikisha ujumbe wa Allah kwa watu kama ulivyo bila ya kupunguza au kuzidisha hata chembe.

#### **(iv)Qur-an Kushuka Kidogo Kidogo kwa Kipindi cha Miaka 23:**

Historia inatuthibitishia kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) hakuanza kuufundisha Uislamu na kuutangaza ulimwengu mzima kwa kurejea Qur-an kama Kitabu tulicho nacho hivi sasa bali aya za Qur-an zilikuwa zikimshukia kidogo kidogo kulingana na haja na wakati kwa kipindi chote cha Utume wake cha miaka 23. Kwa maana nyingine Qur-an imeshuka kidogo kidogo katika kipindi chote cha utume kuanzia mwanzo wa Utume 610 A.D. mpaka siku chache kabla ya kutawafu Mtume(saw), 632 A.D. Kuhusu Qur-an kushuka kidogo kidogo tunafahamishwa katika aya zifuatazo:

وَقُرْءَانًا فَرَقْنَاهُ لِتَقْرَأَهُ عَلَى النَّاسِ عَلَى مُكْتَبٍ وَنَزَّلْنَاهُ تَنزِيلًا ۝

*Na Qur-an tumeigawanya sehemu mbali mbali ili uwasomee watu kwa kituo, na tumeiteremsha kidogo kidogo. (17:106)*

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ الْقُرْآنُ جُمْلَةً وَاحِدَةً

كَذَلِكَ لِنُثَبِّتَ بِهِ فُؤَادَكَ وَرَتَّلْنَاهُ تَرْتِيلاً

*Na wakasema wale waliokufuru; Mbona hakuteremshiwa Qur-an yote kwa mara moja? Kama hivi (mnavyoona, tumeiteremsha kidogo kidogo) ili tuuthibitisha, (tuutie nguvu), moyo wako (kwa hizo aya mpya mpya zinazoteremshwa wakati baada ya wakati) na tumeipanga kwa uzuri. (25:32)*

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ تَنزِيلًا

*Hakika sisi tumekuteremshia Qur-an sehemu sehemu (kidogo kidogo). (76:23).*

Kama inavyoonekana katika aya hizi. Qur-an imeshushwa kidogo kidogo ili iwe wepesi kwa Mtume Muhammad (s.a.w) kuufikisha ujumbe uliotangulia kwa ukamilifu kinadharia na kimatendo kabla ya ujumbe mwingine uliofuata.

Kwa upande mwingine Qur-an imeshuka kidogo kidogo ili kuwawezesha waumini wa mwanzo kuihifadhi Qur-an kwa wepesi, kuyaelewa fika mafundisho yake kinadharia na kuwawezesha kuitekeleza Qur-an katika kila kipengele cha maisha yao ili wawe jamii bora ya kuigwa na jamii zitakazofuatia.

Kushuka Qur-an kidogo kidogo kwa muda wa miaka 23 ni hoja nyingine kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah (s.w). Kwa yeyote yule anayeisoma Qur-an kwa makini na akajua mpangilio wake wa aya na sura kama vile sura moja kuwa na mchanganyiko wa aya za mwanzo na zilizoshushwa mwishoni lakini bado kunapatikana mtiririko mzuri wa maudhui na mpangilio wa sura usiofuata mtiririko wa kushuka, utaona kuwa haiyumkiniki kuwa Qur-an ni Kitabu kilichoandikwa na Mtume Muhammad (s.a.w) kama wanavyodai makafiri.

Pia Qur-an ingelikuwa imeandikwa na Mtume Muhammad (s.a.w) isingelichukua muda wote huo, bali ingelibidi aiandike yote kwa muda mfupi ili aweze kuitumia katika kazi yake ya kuwaongoza watu. Ni kawaida kuwa ili kufanikiwa katika utekelezaji wa jambo lolote ni lazima kwanza pawe na nadharia nzuri inayoelekeza namna ya utekelezaji. Halikadhalika, Mtume Muhammad (s.a.w) aliyekuwa kiongozi wa Dola ambaye mfano wake haujapatikana, asingeliweza kufanya kazi nzito na kubwa kiasi hicho bila ya kuwa na nadharia ya kumwongoza. Hivyo, kwa kutokuwa na Qur-an yote mkononi mwake ili kuitumia katika kila hatua ya kazi yake, inadhihirisha kuwa alikuwa akiletewa mwongozo kutoka kwa Allah(sw) katika kila hatua ya kazi yake mpaka alipoikamilisha.

**(v)Kukosolewa Mtume (s.a.w) katika Qur-an ni Ushahidi Mwingine kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah (s.w):**

Hoja nyingine inayotufanya tuamini pasi na tone la shaka kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah (s.w) ni kule kukosolewa Mtume (s.a.w) ndani ya Qur-an. Si jambo la kawaida kwa mwanaadamu yeyote mwenye akili timamu kutangaza aibu zake na kujikosoa kwa namna Mtume (s.a.w) alivyokosolewa katika Qur-an, katika Kitabu chake mwenyewe. Atakalolifanya mwandishi mkweli na muadilifu ni kuacha tabia mbaya au udhaifu aliokuwa nao na kuwapa wengine ujumbe kuwa waache udhaifu huo. Lakini katika Qur-an tunaona kuwa pale Mtume Muhammad (s.a.w) alipoonesha kidogo udhaifu wa kibinaadamu na akaenda kidogo nje ya utendaji anaouridhia Allah (s.w) pale pale Allah (s.w) alimkosoa na kumrejsha katika njia iliyo sawa. Kwa mfano Mtume Muhammad (s.a.w) alipohisi ugumu katika kutekeleza amri ya Allah(sw) ya kumuoa Zainabu bint Jahsh baada ya kuachwa na Zaidi bin Harith, aliyekuwa mtoto wake wa kulea kwa kuchelea Uislamu kutukanwa na kupakwa matope na makafiri na wanafiki, Allah (s.w) alimzindua katika aya zifuatazo:

وَإِذْ تَقُولُ لِلَّذِي أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَأَنْعَمْتَ عَلَيْهِ أَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ وَاتَّقِ  
 اللَّهَ وَتُخْفِي فِي نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ  
 تَخْشَاهُ فَلَمَّا قَضَى زَيْدٌ مِنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنَاكَهَا لِكَيْ لَا يَكُونَ عَلَى  
 الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَزْوَاجِ أَدْعِيَائِهِمْ إِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ وَطَرًا وَكَانَ أَمْرُ  
 اللَّهِ مَفْعُولًا ﴿٣٧﴾

*Na(wakumbushe)ulipomwambia yule ambaye Mwenyezi Mungu amemneemesha (kwa kumuafikia Uislamu) na wewe ukamneemesha kwa kumpa uungwana. naye ni Bwana Zaid bin Haritha ulipomwambia): “Shikamana na mkeo na umche Mwenyezi Mungu(usimuache)” na ukaficha katika nafsi yako aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyatoa(Nayo ni kuwa Mwenyezi Mungu amekuamrisha umuoe wewe huyo mkewe atakapomuacha ili iondoke ile itikadi iliyokuwa ikiitakidiwa ya kuwa mtoto wa kulea ni kama mtoto wa kumzaa), na ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye haki zaidi ya kumchelea. Basi alipokwisha Zaidi haja yake na mwanamke huyo, Tulikuoza wewe ili isiwe taabu kwa Waislamu kuwaoa wale wa watoto wao wa kupanga wanapokuwa hawana haja nao. na amri ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutekelezwa (33:37)*

Mfano mwingine ni pale Mtume (s.a.w) aliposusa kula asali ili kuwaridhisha wake zake ambapo Allah (s.w) alimwonya kama aya ifuatayo inavyotufahamisha:

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ لِمَ تُحَرِّمُ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكَ تَبَتَّغِي مَرَضَاتِ أَرْوَاجِكَ وَاللَّهُ  
 غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٦١﴾

*Ewe Mtume! Mbona (kwa nini) unaharamisha alichokuhahalishia Allah? Unatafuta radhi za wake zako ndiyo maana ukafanya hivi! Na Allah ni mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu. (66:1)*

Mfano mwingine ni ule wa kukosolewa Mtume (s.a.w)



katika Qur-an ni pale alipomkasirikia sahaba kipofu aliyetaka kupata mawaidha mapya na badala yake akawaelekea wakubwa wa makafiri kwa matumaini kuwa watasilimu na kuleta nafuu kubwa katika kazi ya kuusimamisha Uislamu. Kitendo hiki hakukiridhia Allah (s.w) na akamkosoa Mtume wake katika aya zifuatazo:

عَمَسَ وَتَوَلَّى ۝١ أَن جَاءَهُ الْأَعْمَى ۝٢ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّهُ وَّيَّرَكَ ۝٣ أَوْ  
يَذْكُرُ فَتَنْفَعَهُ الذِّكْرَى ۝٤ أَمَّا مَنِ اسْتَعْتَنِي ۝٥ فَأَنْتَ لَهُ وَصَدِّي ۝٦  
وَمَا عَلَيْكَ أَلَّا يَزْكِي ۝٧ وَأَمَّا مَنِ جَاءَكَ يَسْعَى ۝٨ وَهُوَ يَخْشَى ۝٩  
فَأَنْتَ عَنْهُ تَلَهَّى ۝١٠ كَلَّا إِنَّهَا تَذْكِرَةٌ ۝١١ فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ۝١٢

*Alikunja (Mtume) paji akageuza uso, kwa sababu alimjia kipofu, na nini kilichokujulisha (kuwa huyo sahaba pofu hahitaji mawaidha mapya) labda atatakasika (akisikia mawaidha mapya), au atakumbuka (aliyoyasahau) ukumbusho huo upate kumfaa, ama ajionaye hana haja (ya dini), wewe ndiye unayemshughulikia! Na si juu yako kama hakutakasika, lakini anayekukimbilia - naye anaogopa, wewe unampuza (usifanye hivyo). Sivyoo! Hakika hii (Qur-an) ni nasaha (mawaidha), basi kila apendaye atawaidhika (asiyetaka basi muachilie mbali). (80:1-12).*

Ni dhahiri kuwa kama Mtume (s.a.w) asingelikuwa Mtume wa Allah(s.w) na kama ndiye yeye aliyeandika Qur-an, kamwe asingelithubutu kudhihirisha aya hizo katika kitabu chake. Kwa aya hizi na nyingine kama hizi kubakia katika Qur-an na Mtume (s.a.w) kuzitangaza kwa watu kama zilivyo kwa muda wote wa maisha yake ya Utume, ni hoja nyingine kuwa Qur-an si maneno ya Mtume Muhammad (s.a.w) bali ni maneno matukufu ya Allah (s.w).

**(vi)Kutokea Kweli Matukio yaliyotabiriwa  
katika Qur-an:**

Ushahidi mwingine unaonesha kuwa Qur-an ni neno la Allah (s.w) ni kutokea mambo kama yalivyotabiriwa hapo awali na Qur-an. Katika mwanzo wa kushuka Qur-an kuna mambo mbali mbali ambayo Mtume (s.a.w) aliahidiwa pamoja na Waislamu kuwa yatatokea hapo baadaye. Pamoja na kuonekana kwa watu kutokuwa na uwezekano kutokea hayo yaliyotabiriwa kulingana na hali halisi iliyokuwapo wakati huo ukweli ni kwamba yalitokea. Kwa mfano, katika siku za mwanzo za Utume, Mtume (s.a.w) na Waislamu waliahidiwa na Allah (s.w) kuwa pamoja na ugumu uliokuwa ukiwakabili na pamoja na udhaifu wa mali na uwezo waliokuwa nao, hali yao itazidi kuwa nzuri siku hadi siku na baadaye watafarijika na kuwa juu ya maadui zao. Ahadi hizi tunazikuta katika aya zifuatazo:

وَلِلْآخِرَةِ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ ۖ وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ﴿٤﴾

*Na bila shaka wakati ujao utakuwa ni bora kwako kuliko uliotangulia, na Mola wako atakupa mpaka uridhike. (93:4-5)*

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٥﴾ إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٦﴾

*Na kwa hakika baada ya dhiki (huja) faraja. Hakika baada ya dhiki (huja) faraja. (94:5-6)*

Tukiangalia maisha ya Mtume na maswahaba wake, ahadi zote hizi zilitimia. Waislamu waliongezeka siku hadi siku na Uislamu ulisimama na kuwa juu ya Dini zote (njia zote za maisha) katika kipindi kifupi cha miaka 23 tu. Mfano wa pili wa utabiri wa Qur-an ulitokea kweli baada ya kipindi kifupi tu ni ule uliotolewa katika suratur-Ruum katika aya zifuatazo:

غَلَبَتِ الْأَرُومُ ﴿٢﴾ فَمِنَ الْأَرْضِ وَالْهُم مِّنْ  
 بَعْدِ غَلَبِهِمْ سَتِيلُونَ ﴿٣﴾ فِي بَضْعِ سِينِينَ لِلَّهِ الْأَمْرُ مِنْ قَبْلُ  
 وَمِنْ بَعْدُ وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٤﴾ بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ  
 يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٥﴾ وَعَدَّ اللَّهُ لَا يُخْلِفُ اللَّهُ وَعْدَهُ  
 وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦﴾

*Warumi wameshindwa katika nchi iliyo karibu (na nchi ya Bara Arabu, nayo ni Sham) nao baada ya kushindwa kwao watahinda, katika miaka michache: Amri hii ni ya Allah kabla (yake) na baada (yake) na siku hiyo Waislamu watafurahi kwa nusra ya Allah (Atakayowapa wao. Nayo ni kuwashinda Makuraishi siku hiyo) (Allah) Humnusuru amtakaye; naye ni Mwenye Nguvu; Mwenye Rehma. Hii ni ahadi ya Allah, Allah havunji ahadi yake lakini watu wengi hawajui. (30:2-6)*

Katika mwaka wa sita au saba wa Utume, palikuja habari Makka kuwa Warumi ambao ni watu wa Kitabu (Ahlal-Kitab) wameshindwa vita na Waajemi ambao walikuwa ni washirikina kama washirikina wa Makka. Tukio hili liliwafurahisha sana washirikina wa Makka na kuwaambia Waislamu: "Wakristo, watu wa Kitabu kama nyinyi, wameshindwa na washirikina wenzetu, na hii ni ishara kuwa na sisi hivi karibuni tutakushendeni." Ndipo Quran ikatangaza katika aya hizi bishara mbili; bishara ya kwanza ni kuwa katika muda wa miaka tisa Waajemi watahinda na Warumi na ya pili ni kuwa Waislamu siku hiyo nao watafurahi na kuwacheka Washirikina wa Makka, yaani makafiri wa Makka nao watahinda vibaya sana na Waislamu. Hivi ndivyo ilivyotokea, kwani katika mwaka 624 A.D. Warumi waliwashinda Waajemi na mwaka huo huo Waislamu 313 walishinda jeshi la makafiri wa Makka lililokuwa na askari 1000 katika vita vya Badr, kwa hiyo ahadi ya Allah(s.w) aliyoitoa

katika Qur-an ilitimia. Je hii haithibitishi kuwa Qur-an ni maneno ya Allah (s.w), Mjuzi wa yote yaliyopita na yajayo?

Hebu tuangalia tena mfano mwingine unaoonesha kutokea kweli ahadi alizozitangaza Allah(s.w) katika Qur-an. Katika suratul-Fat-h tunafahamishwa:

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ﴿٤٨﴾

*Bila shaka Tumekwisha kupa kushinda kuliko dhahiri. (48:1)*

Katika mwaka wa 6 A.H. Mtume (s.a.w) na baadhi ya Maswahaba wake walitoka kwenda Makka kufanya Umra (Hija ndogo) lakini walipokaribia kuingia Makka makafiri waliwakatalia kata kata wasiende kufanya ibada hiyo.

Waislamu walikasirika sana mpaka kukaribia kupigana ndipo Allah (s.w) akawateremshia utulivu na wakakubaliana kufanya mkataba wa (Hudaibiya), kisha Allah (s.w) akawaahidi kupata ushindi baada ya muda mfupi. Ndivyo ilivyotokea.

Baada ya miaka miwili tu, na baada ya makafiri wenyewe kuvunja ule mkataba wa amani, Waislamu waliuteka mji wa Makka na kuwa mwisho wa kuabudiwa miungu mingine pamoja na Allah(s.w) katika Nyumba Takatifu (Al-Kaaba) na katika muda mfupi huo watu wengi walisilimu. Je, kutimia kwa bishara hii ambayo iko wazi mno katika historia, haioneshi kuwa haikutolewa na yeyote ila ni yule mwenye elimu ya hakika juu ya yote yaliyopita na yajayo?

### **(vii)Mpangilio wa Qur-an:**

Ukiuchunguza msahafu kwa kina utagundua kuwa si kitabu cha kawaida kama vile wanavyo vitunga wanaadamu. Qur-an pamoja na aya zake kufumwa na maneno ya Kiarabu, pametumika ujuzi usio na mfano katika uchaguzi na mpangilio wa maneno. Maneno yamechaguliwa na kupangiliwa kwa kiasi kwamba

huwianisha habari zote zilizoelezwa ndani ya Kitabu na kuufikisha ujumbe kwa wepesi. Mifano michache ifuatayo itatupa picha ya mpangilio wa ajabu wa Qur-an:

**Kwanza**, kutokana na uchunguzi uliofanyika kwa kutumia **kompyuta** imedhihirika kuwa sura zile zilizoanza na herufi kama

**Qaf** ( ق ) zina idadi kubwa zaidi ya herufi hiyo ukilinganisha na herufi nyingine katika sura hizo.

**Pili**, Kuna sura 114 katika msahafu na kila sura imeanza kwa "Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim" isipokuwa Suratut Tawba. Hi huifanya idadi ya "Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim" kuwa 113. Lakini katika Suratun-Naml kuna "Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim" iliyoletwa katikati ya sura.

إِنَّهُ مِنْ سُلَيْمَانَ وَإِنَّهُ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٣٠﴾

*Imetoka kwa Suleimani, nayo ni: Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu." (27:30)*

Hivyo huifanya idadi ya "Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim" kuwa 114 sawa na idadi ya sura zote katika msahafu. Je, hii imetokea kwa bahati tu au ni mpangilio wa Mjuzi, Mwenye Hikma.

**Tatu**, kutokana na uchunguzi imedhihirika kuwa maneno mbali mbali katika Qur-an yamerudiwa kwa kuzingatia idadi maalum. Kwa mfano neno "**Sema**" ( قُلْ ) limerudiwa mara 332 katika msahafu na neno "**Alisema**" ( قَالَ ) limerudiwa mara hizo hizo 332. Pia katika Qur-an zimetajwa "**Mbingu Saba**" ( سَبْعَ سَمَوَاتٍ ) na maneno haya yamerudiwa mara saba tu katika msahafu mzima.

Kuna miezi kumi na mbili katika mwaka mmoja na neno "**Shahr**"( شَهْرٌ ) lenye maana ya mwezi limetajwa mara 12 katika

Qur-an. Neno "Yaum" (يَوْمٌ) katika Qur-an limetajwa mara 365 sawa na idadi ya siku za mwaka mmoja katika mwendo wa jua!

**Nne**, Qur-an inapofananisha jambo fulani na lingine, idadi ya utajo wa mambo hayo kitabuni humo pia huwiana. Kwa mfano katika sura ya 3 aya 59 Qur-an inasema:

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ خَلَقَهُ مِن تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ وَاكُنْ

فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾

*Bila shaka hali ya Issa mbele ya Allah ni kama ile ya Adam. Alimuumba kwa udongo, kisha akamwambia kuwa na akawa. (3:59).*

Adam(a.s) ametajwa mara 25 katika Qur-an. Issa(a.s) vile vile ametajwa mara 25 katika Qur-an. Zaidi ya hivyo katika sura 3:59, Adam ametajwa kwa **mara ya saba** vivyo hivyo Issa nae ametajwa kwa **mara ya saba** katika aya hiyo.

Adam(a.s) ametajwa katika aya zifuatazo:

2:31, 2:33, 2:34, 2:35, 2:37, 3:33, 3:59 (mara ya saba), 5:27, 7:11, 7:26, 7:31, 7:35, 7:35, 7:172, .17:61, 17:70, 18:50, 19:58, 20:115, 20:116, 20:117, 20:120, 20:121, 36:60.

Issa(a.s) ametajwa katika aya zifuatazo:

2:87, 2:136, 2:253, 3:45, 3:52, 3:55, 3:59 (mara ya saba), 3:84, 4:157, 4:163, 4:171, 5:46, 5:78, 5:110, 5:112, 5:114, 5:116, 6:85, 19:34, 33:7, 42:13, 43:63, 57:27, 61:6 na 61:14.

Mfano mwingine ni ule wa sura ya 7 aya ya 176. Qur-an inawalinganisha watu wanaoifuata matamania ya nafsi zao

kinyume na aya za Mwenyezi Mungu, kuwa hao ni sawa na mbwa (Kalb).

فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ الْكَلْبِ

"Hali yao ni sawa na ile ya mbwa:

Tamko:"Wale wanaokanusha aya zetu (الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا) limerejewa mara 5 katika Qur-an, na neno "mbwa"( الْكَلْبِ ) limetajwa mara 5:

**Tamko:**"Wale wanaokadhibisha aya zetu limetajwa katika aya zifuatazo:7:176 (mara ya kwanza),7:177,21:77, 25:36 na 62:5 (mara ya tano).

Neno mbwa (kalb) limetajwa katika aya zifuatazo:

7:176 (mara ya kwanza), 18:18, 18:22

Aidha Qur-an inaposema jambo au kitu hiki si kama kile idadi ya mambo au vitu hivyo haiwiani katika kutajwa kwake ndani ya Qur-an.<sup>2</sup>

Kutokana na mifano hii michache ni muhali mwanaadamu kuweza kuandika kitabu chenye mfumo wa maneno, aya na sura mithili ya Qur-an.

### **(viii)Maudhui ya Qur-an na Mvuto wa Ujumbe Wake**

Ukiisoma Qur-an na kuizingatia kwa makini na ukawa unaijua lugha yake vizuri utakiri kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah (s.w) kwani ujumbe wake hupenya katika moyo hata wa yule anayeipinga.

Tunafahamishwa katika historia kuwa Waarabu waliopinga Qur-an walikuwa wakipiga kelele na kuziba masikio ili wasipate ujumbe wake wakati ilipokuwa ikisomwa. Kwani kila mwenye kuielewa vizuri lugha ya Qur-an aliathiriwa na ujumbe wake.

Mfano wa athari ya kupenyeza kwa Qur-an katika nyoyo za wanaadamu ni ule wa Labiid ibn Rabiha aliyesilimu kutokana na changa moto ya aya za Qur-an dhidi ya shairi lake. Kwa kuwa yeye alikuwa mwanafasihi mashuhuri na aliyejamini mno katika fani ya mashairi, baada ya kusoma aya chache za sura ya Qur-an alikiri kuwa Qur-an si mashairi na wala haiwezi kuwa zao la mwanaadamu. Ilibidi akiri kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah (s.w) na akasilimu mbele ya Mtume (s.a.w)

Mfano mwingine ni ule wa 'Umar bin al-Khattab. Akiwa bado mmoja wa viongozi wa Washirikina waliokuwa katika harakati za kumpiga vita Mtume Muhammad (s.a.w) na dini aliyokuwa akiitangaza. 'Umar alichukia sana aliposikia kuwa dada yake amesilimu. Baada tu ya kupata habari ya kusilimu kwa dada yake aliharakisha kwenda nyumbani kwa dada yake kwa hasira na upanga mkononi. Alikuta nyumbani kwa dada yake ikisomwa Qur-an iliyoandikwa katika kipande cha karatasi ambacho alidai apewe. Dada yake alikataa kumpa mpaka alipokubaliana na masharti yake. Baada ya kusoma na kurudia aya chache za Surat-Twaha (sura ya 20) alipoa na kuondoka moja kwa moja kwenda kwa Mtume Muhammad (s.a.w) na kusilimu.

Baada ya kusilimu, 'Umar ibn al-Khattab alikuwa ngao ya kuutetea Uislamu kwa hali na mali kwa muda wote wa maisha yake na alikuwa Khalifa wa pili wa Mtume (s.a.w) na kiongozi wa Kiislamu aliye mashuhuri katika historia ya ulimwengu.

Hebu turejee aya chache za sura hii zilizokuwa ndio sababu ya kusilimu 'Umar kutokana na mvuto wake:



طه ﴿١﴾ مَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لِتَشْقَى ﴿٢﴾ إِلَّا تَذِكْرَةً لِمَنْ يَحْشَى ﴿٣﴾  
 تَنْزِيلًا مِمَّنْ خَلَقَ الْأَرْضَ وَالسَّمَوَاتِ الْعُلَى ﴿٤﴾ الرَّحْمَنُ عَلَى الْعَرْشِ  
 اسْتَوَى ﴿٥﴾ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَمَا تَحْتَ  
 الثُّرَى ﴿٦﴾ وَإِنْ تَجَهَّرَ بِالْقَوْلِ فَإِنَّهُ يَعْلَمُ السِّرَّ وَأَخْفَى ﴿٧﴾

*Twaaha! Hatukukuteremshia Qur-an ili upate mashaka. Bali iwe mawaidha kwa wenye kunyenyekea. Kiteremsho kinacho toka kwa Yule aliyeyumba ardhi na mbingu zilizo inuka juu. Ndiye Mungu mwenye rehema. Aliyetawala juu ya kiti cha Enzi. Ni vyake (tu peke yake) vyote vilivyomo Mbinguni na vilivyomo ardhini na vilivyo baina yao na vilivyomo chini ya ardhi. Na ukinena kwa sauti kubwa (au ndogo ni sawa sawa) kwani hakika Yeye anajua yaliyosiri na yaliyofichikana zaidi. Mwenyezi Mungu hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye. (20:1-7)*

Je, unaonaje ujumbe wa aya hizi za mwanzo ambazo hasa ni utangulizi wa sura hii? Utaona kuwa namna Qur-an inavyowasilisha ujumbe wake kwa watu ni tofauti kabisa na uwasilishaji wa ujumbe katika uandishi wa mwanaadamu.

Si tu kuwa ujumbe wa Qur-an unanasa kwa kila mwenye kuijua lugha yake, bali hukuti udhaifu wowote katika uandishi wake kama vile kuwa na maneno yanayopingana pamoja na kwamba uandishi wake mpaka kufikia kwenye msahafu huu tulionao ulichukua miaka 23 na mpangilio wa aya na sura ni tofauti kabisa na utaratibu wa kushuka kwake. Qur-an yenyewe inathibitisha hili katika aya zifuatazo:

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِنْدِ غَيْرِ اللَّهِ لَوَجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا  
 كَثِيرًا ﴿٨٧﴾

*Hawaizingatii nini hii Qur-an? Na kama ingelitoka kwa asiye kuwa Allah bila shaka wanalikuta ndani yake hitilafu nyingi. (4:82).*

اللَّهُ نَزَّلَ أَحْسَنَ الْحَدِيثِ كِتَابًا مُّتَشَابِهًا مَّثَانِيَ تَقْشَعِرُّ  
مِنْهُ جُلُودُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ثُمَّ تَلِينُ جُلُودُهُمْ وَقُلُوبُهُمْ  
إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ ذَٰلِكَ هُدَىٰ اللَّهِ يَهْدِي بِهِ ۗ مَن يَشَاءُ ۗ وَمَن يُضْلِلِ اللَّهُ فَمَا  
لَهُ مِن هَادٍ ﴿٢٣﴾

*Mwenyezi Mungu ameteremsha hadithi nzuri kabisa; Kitabu chenye maneno yanayowafikiana na yanayokaririwa; (bila kuchosha) husisimka kwayo ngozi za wale wanaomuogopa Mola wao; kisha ngozi zao na nyoyo zao huwa laini kwa kumkumbuka Mola wao. Huo ndio uongofu wa Allah; kwa huo humuongoza Amtakaye, na anayeachiwa na Allah kupotea basi hakuna wa kumuongoa. (39:23)*

Pamoja na kuona kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah(s.w) kutokana na mvuto wake na ukamilifu wake, hebu tuangalie maudhui ya aya mbali mbali za Qur-an ambazo zinaonekana wazi kuwa haziwezekani zikawa zimetungwa na Mtume Muhammad (s.a.w) na wala hapana yeyote miongoni mwa wanaadamu aliyemfundisha:

خَلَقَ السَّمَوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ۗ وَأَلْقَىٰ فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيَ أَن تَمِيدَ  
بِكُمْ

*"Ameziumba mbingu pasipo nguzo, mzionazo na ameiweka milima katika ardhi ili (ardhi) isikusukesukeni (isikutetemesheni)..." (31:10)*

Aya hii inatufahamisha kuwa maumbile mbali mbali katika anga ikiwa pamoja na dunia yameshikiliwa na nguvu ya uvutano

(gravitational force) ambayo hatuioni kwa macho yetu. Kama aya hii ilitungwa na Muhammad (s.a.w) miaka mingi kabla ya ugunduzi wa kuwepo kwa nguvu ya uvutano kati ya dunia, jua na sayari nyingine na kabla ya maendeleo ya sayansi yaliyopo hivi leo juu ya ulimwengu (universe) kwa ujumla kwa nini akaongeza neno "mzionazo" badala ya kusema tu "ameziumba mbingu pasipo nguzo?" Yeye alijuaje kwamba kuna nguvu ya uvutano na haionekani? Zaidi ya hivyo Mtume (s.a.w) angelijuaje kabla ya ugunduzi wa sayansi wa karne ya 19/20 A.D kuwa kuwepo kwa milima katika sehemu zake ni muhimu sana katika kuithubutisha dunia na kuifanya isiyumbe yumbe wakati ikizunguka kwa kasi sana katika muhimili wake, na kuzuia tetemeko? Imegundulika hivi karibuni kuwa milima ina mizizi.

Ujumbe wa aya hii wenye maelezo ya kisayansi yaliyotolewa na wanasayansi wa karne hizi za usoni hauwezi kuwa umetolewa na Mtume (s.a.w) katika karne ya Saba wakati uvumbuzi huu haujafahamika kwa mtu yeyote. Kwa hiyo ujumbe wa aya hii ni hoja tosha kuwa Qur-an ni neno linalotoka kwa Mjuzi wa yote.

وَإِنَّ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةً ۚ نُسْتَفِيكُمْ مِمَّا فِي بُطُونِهِ ۚ مِنْ بَيْنِ فَرْثٍ وَدَمٍ

لَبَنًا خَالِصًا سَائِغًا لِلشَّرْبِ بَيْنَ ۝۱۱

*"Na bila shaka katika wanyama muna mazingatio makubwa kwa ajili yenu. Tunakunywesheni katika vile vilivyomo matumboni mwao baina ya choo na damu, (Tumekunywesheni) maziwa safi (na) mazuri kwa wanywao." (16:66)*

Ukweli kwamba maziwa katika wanyama hutengenezwa katika "mammary glands" kutokana na chakula kilichochunjwa kutoka tumboni na kikasafirishwa katika mikondo ya damu ni ugunduzi wa kisayansi wa hivi karibuni katika karne ya ishirini (20). Sasa Muhammad (s.a.w) angelipata wapi utaalamu huu kama kweli yeye ndiye mwandishi wa Qur-an?

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ سُلَالَةٍ مِّن طِينٍ ﴿١٣﴾ ثُمَّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ  
مَّكِينٍ ﴿١٤﴾ ثُمَّ خَلَقْنَا النَّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً فَخَلَقْنَا الْمُضْغَةَ  
عِظْمًا فَكَسَوْنَا الْعِظْمَ لَحْمًا ثُمَّ أَنْشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ فَتَبَارَكَ اللَّهُ  
أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ ﴿١٥﴾

"Na kwa yakini tulimuumba mwanaadamu kwa udongo uliosafi, kisha tukamuumba kwa tone la manii lililowekwa katika makao yaliyohifadhika. Kisha tukalifanya tone hilo kuwa pande lenye kuning'inia, kisha Tukalifanya kuwa pande la nyama kisha tukalifanya kuwa mifupa na mifupa tukaivisha nyama, kisha tukamfanya kiumbe mwingine. Basi Ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa Waumbaji." (23:12-14)

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ نُطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا  
"Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai (uzazi) iliyochanganyika (ya mwanamume na mwanamke) ili Tumfanyie mtihani, kwa hiyo Tukamfanya ni mwenye kusikia (na) mwenye kuona." (76:2)

Kama Mtume Muhammad (s.a.w) ndiye mwandishi wa aya hizi, angelijua je au ni nani angelimfundisha wakati ule uhakika huu wa kisayansi juu ya hatua za kukua mtoto katika mfuko wa uzazi tokea kwenye mbegu za uzazi hadi kuwa mwanaadamu kamili? Hebu tumalizie mifano kwa kuzingatia tena aya zifuatazo:

﴿ وَهُوَ الَّذِي مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ هَذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ وَهَذَا مِلْحٌ

أَجَاحٌ وَجَعَلَ بَيْنَهُمَا بَرْزَخًا وَحِجْرًا مَّحْجُورًا ﴿٥٣﴾

"Naye (Mwenyezi Mungu) Ndiye anayeziunganisha bahari mbili hii ni tamu inayoondosha kiu, na hii ni yenye chumvi kali; na akaweka kinga kati yao na kizuizi kizuiacho." (25:53)

مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ يَلْتَقِيَانِ ﴿١٩﴾ بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لَا يَبْغِيَانِ ﴿٢٠﴾

*"Amezikutanisha bahari mbili. Baina yao kuna kizuizi, haziingiliani (hazichanganyiki)." (55:19-20)*

Aya hizi na aya nyinginezo za Qur-an zinatufanya tuzidi kuwashangaa wale wanaodai kuwa mtunzi wa Qur-an ni Muhammad (s.a.w). Ni hivi karibuni tu, 1983, mtaalamu mmoja wa Ufaransa, Capitain Jecques Constan, amegundua kuwa maji ya bahari mbili hayachanganyiki jambo lililoelezwa katika Qur-an karne 14 zilizopita. Mtaalamu huyu aliposoma aya hizi za Qur-an ilibidi akiri:

*"Nimeshuhudia kuwa Qur-an ni maneno ya Allah (s.w). Sayansi yetu ya leo inathibitisha tu yale yale yaliyoelezwa na Qur-an karne 14 zilizopita."*<sup>3</sup>

Aya hizi tulitozinukuu kama mifano na nyingine nyingi kama hizi zinatufahamisha juu ya utalaamu wa hali ya juu, juu ya maumbile ambao ndio tu umegunduliwa katika karne hizi za 19/20 kutokana na utafiti wa kisayansi. Yapo mambo mengi yaliyoelezwa katika Qur-an juu ya maumbile ambayo mpaka hivi sasa mwanaadamu hajaweza kuyatolea maelezo ya kisayansi.

Kwa hiyo ukiichunguza Qur-an kwa makini na kuifanyia utafiti kwa kiwango cha utalaamu kilichofikiwa hivi sasa utaona kuwa Qur-an ni

Kitabu kinachoweka bayana na kuelezea kila kitu kinachohitajika katika kuleta ufanisi wa maisha ya mwanaadamu hapa ulimwenguni na huko Akhera. Qur-an yenyewe inadhihirisha hili katika aya zifuatazo:

الرَّءِيسَ تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ وَقُرْءَانَ مُبِينٍ ﴿١﴾

---

3. Habari hizi zimenukuliwa kutoka: ISLAMIC HORIZONS Vol. IX  
Na.3, March -April 1983/Jamad 1, 1403A.H

"Alif Lam Raa, Hizi ni aya za Kitabu kilichokusanya kila yanayohitajiwa na kikayadhihirisha kwa vizuri." (15:1)

تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿٢﴾

"Hizi ni aya za kitabu kielezacho (kila linalohitajiwa)." (26:2)

طس تِلْكَ آيَاتُ الْقُرْآنِ وَكِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿١﴾

"Twa Sin. Hizi ni aya za Qur-an, (Kitabu kilichojaa kila yenye faida) na kitabu kielezacho (kila linalohitajika)." (27:1)

وَمَا عَلَّمْنَاهُ الشِّعْرَ وَمَا يَنْبَغِي لَهُ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ وَقُرْآنٌ مُّبِينٌ ﴿١٤﴾

لِيُنذِرَ مَنْ كَانَ حَيًّا وَيَحِقُّ الْقَوْلُ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٧﴾

"Wala hatukumfundisha (Muhammad) mashairi, wala haiwi kwake (kuwa mtunga mashairi). Haikuwa (Qur-an) ila ni ukumbusho na Kitabu kibainishacho (kila yanayohitajiwa). Ili amwonye aliye hai na ihakikike kauli (ya kuadhibiwa) juu ya makafiri." (36:69-70)

حَمِّ ﴿١﴾ وَالْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿٢﴾

Haa Miim. "Naapa kwa Kitabu (hiki) kinachobainisha (kila linalohitajika)." (44:2)

Aya zote hizi zinatufahamisha kuwa Qur-an imetubainisha kwa uwazi na kwa lugha nyepesi kila linalohitajika katika kuendesha maisha yetu ya kila siku kwa ufanisi. Anashuhudia ukweli huu kila mwenye kuisoma Qur-an kwa mazingatio. Kwa hiyo, ni muhali kabisa Qur-an kuwa kitabu kilichotungwa na mwanaadamu bali ni lazima mwandishi wake awe ni yule aliye mjuzi wa mambo yote yaliyo nyuma na mbele ya maisha ya mwanadamu na mwenye ujuzi huo si mwingine ila Allah (s.w).

S

## (ix)Wanaadamu kushindwa Kuandika Kitabu S Mithili ya Qur-an:

Ushahidi mkubwa na wa uwazi zaidi ni hii changa moto iliyonadiwa kwa wanaadamu wote katika Qur-an yenyewe. Ni kwamba, watu waliokufuru wa nyakati zote za historia ya Qur-an wanadai kuwa Qur-an si kitabu cha Allah(s.w) bali ni kitabu kinachotokana na kazi ya mwanaadamu, hususan Mtume Muhammad (s.a.w). Baadhi ya madai yao tumeshayaona katika kurasa za nyuma. Baada ya kutoa madai yao haya yasiyo na ushahidi wowote au fununu yoyote ya ukweli, Allah (s.w), aliye Mjuzi na Mwingi wa hekima, Alitoa changamoto si kwa hawa wapinzani tu bali kwa wanaadamu wote ili baada ya hapo kila mwenye akili timamu ashuhudie kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah (s.w). Allah (s.w) alitoa wito kwa wapinzani wote wa Qur-an kuwa wakusanyike pamoja na washirikiane na wataalamu wote wa ulimwengu walio na uzoefu na uhodari katika sanaa ya uandishi kisha katika ushirikiano wao huo watoe kitabu mfano wa Qur-an. Historia nzima inatuonesha kuwa hakuna aliyefua dafu. Hebu turejee changa moto hii katika aya ifuatayo:

قُلْ لِّسِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَنْ يَأْتُوا بِمِثْلِ هَذَا الْقُرْآنِ لَا  
يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴿٨٨﴾

*Sema: "Hata wakijikusanya watu (wote) na majini ili kuleta mfano wa hii Qur-an basi hawangaliweza kuleta mfano wake, hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao." (17:88)*

Baada ya kushindwa kutoa kitabu mfano wa Qur-an, Allah (s.w) aliwapa makafiri tahfifu ili wazidi kutanabahi na kuhuzunika kwa kuwanadia kuwa waandike mfano wa sura kumi tu za Qur-an badala ya sura 114, kama tunavyofahamishwa katika aya ifuatayo:

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَيْنَاهُ قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوْرٍ مِّثْلِهِ مُفْتَرِيَاتٍ وَادْعُوا

مَنْ اسْتَطَعْتُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٣﴾

*Ndiyo kweli wanasema kuwa: "Ameitunga mwenyewe (Muhammad hii Qur-an)?" Sema: "Basi leteni sura kumi za uwongo zilizotungwa mfano wa hii, na waiteni muwawezao (kuwaita) badala ya Allah (waje wakusaidieni kutunga hivyo) ikiwa mnasema kweli." (11:13)'*

Hakuna aliyethubutu kutoa sura hizo kumi mfano wa Sura za Qur-an kwa wakati wote wa historia ya Qur-an. Allah (s.w) Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ujuzi na Hekima, alitoa tena tahfifu nyingine kwa kuwataka wale wote wanaodai kuwa Qur-an ni kitabu cha Mtume Muhammad (s.a.w) nao waandike angalau sura moja tu mfano wa sura za Qur-an kwa ufasaha wa lugha, mantiki, mtiririko wa maudhui na ukamilifu wa ujumbe. Hebu turejee aya zifuatazo:

وَإِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا فَأْتُوا بِسُوْرَةٍ مِّن

مِّثْلِهِ وَادْعُوا شُهَدَاءَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٣﴾

*"Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyomteremshia mtumwa wetu, (kuwa hakuteremshiwa na Allah), basi leteni sura moja iliyofanywa na (mtu) aliye mfano wake, na muwaite miungu yenu bighairi ya Allah (wakusaidieni) ikiwa mnasema kweli." (2:23)*

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَيْنَاهُ قُلْ فَأْتُوا بِسُوْرَةٍ مِّثْلِهِ وَادْعُوا مَنْ اسْتَطَعْتُمْ مِّنْ

دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٨﴾

*Je, ndiyo wanasema ameitunga? Sema: "Hebu (tungeni na nyie) mlete sura moja mfano wake na waiteni muwezaao (kuwapata waje) isipokuwa Allah (wa kuwasaidieni) kama nyinyi mnasema kweli (kuwa haya ameyazua Muhammad)" (10:38)*



Kama Muhammad (s.a.w) ndiye mwandishi wa Qur-an angelithubutu kweli kutoa changa moto hii kwa walimwengu wote wa nyakati zote? Mtume (s.a.w) angaliwezaje kutamka kwa uhakika kiasi hicho kuwa walimwengu wote hata wakishirikiana pamoja hawawezi kuandika kitabu mithili ya Qur-an uhakika ambao umebakia mpaka hivi leo? Kwa hiyo kushindwa kwa wanaadamu wa enzi zote za historia ya Qur-an kuleta mfano wa Qur-an angalau sura moja ni hoja tosha kuwa Qur-an ni Kitabu cha Allah (s.w).

Aidha Qur-an pia imewajibu wale watu wanaosema kuwa Muhammad (s.a.w) ndiye aliyeandika Qur-an kwa kuwataka watu hao wazingatie mawili: Kwanza Muhammad aliishi nao kwa muda wa miaka 40 na hakuonesha dalili zozote za kuwa mwandishi wala mshairi. Imekuwaje ghafla mtu huyo akaweza kuandika aya ambazo hakuna awezaye kuleta mfano wake? Pili, Muhammad angewezaje kuandika Qur-an na ilhali hakujua kusoma wala kuandika? Hoja hizo zinapatikana katika aya zifuatazo za Qur-an:

قُلْ لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا تَلَوْتُهُ وَعَلَيْكُمْ وَلَا أَدْرَنَكُمْ بِهِ ۗ فَقَدْ لَبِثْتُ فِيكُمْ  
عُمُرًا مِّن قَبْلِهِ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٦﴾

"Sema: Kama Allah angelitaka nisingalikusomeeni hii (Qur-an), wala asingalikujulisheni (hiyo Qur-an). Nalika baina yenu umri (mwingi) kabla ya haya; (hamkunisia kusema kitu). Basi hamfahamu (kuwa haya si yangu mwenyewe kwa nafsi yangu)? (10:16)

وَمَا كُنْت تَتْلُو مِن قَبْلِهِ ۗ مِن كِتَابٍ وَلَا  
تَخْطُهُ ۗ بِيَمِينِكَ ۗ إِذَا لَارْتَابَ الْمُبْطِلُونَ ﴿٤٨﴾

"Na hukuwa mwenye kusoma chochote kabla ya hiki, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume, (ingekuwa hivyo) wangepanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki). (29:48)

## **(b)Uthibitisho kutokana na Historia (Hadith)**

Historia ya kushuka Qur-an na namna Mtume (s.a.w) alivyoipokea ni ushahidi mwingine unaotuthibitishia kuwa Qur-an si kitabu alichokitunga Muhammad (s.a.w). Kuna maelezo kadhaa ya kihistoria tunayojifunza katika Hadith juu ya namna Mtume (s.a.w) alivyoipokea Qur-an. Hebu turejee hadithi zifuatazo:

- (1) Hadithi ya bibi Aysha (r.a) iliyopokelewa na Imamu Bukhari inatufahamisha namna Mtume (s.a.w) alivyopokea wahyi wa kwanza wa Qur-an alipokuwa katika pango la Jabal Hira. Kama tulivyojifunza katika hadithi hiyo Mtume (s.a.w) alistushwa sana na tukio lile la kujiwa na Malaika Jibril (a.s) na kumuamrisha kusoma kinyume na uwezo wake. Tukio lile lilimhofisha sana Mtume (s.a.w) na kumfanya arejee nyumbani kwake akiwa anatetemeka. Tukio la Jabal Hira ni ushahidi mwingine tosha kuwa Qur-an si maneno ya Muhammad (s.a.w) bali ni ujumbe kutoka kwa Allah (s.w) uliofikishwa kwake kwa njia ya wahyi kupitia kwa Malaika Jibril.
- (2) Mtume (s.a.w) alikuwa akibadilika haiba yake na kutokwa na jasho wakati wa kupokea wahyi kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Bibi aysha (r.a) amesimulia: Kwa hakika nimemuona Mtume akiteremshiwa wahyi siku ya baridi kali na baada ya kumaliza kile kipindi cha kuteremshiwa wahyi aliminikwa na jasho jingi kichwani mwake." (Malik)*

*Amesimulia Aysha (r.a), "Al-Harith bin Hisham (r.a) alimuuliza Mtume wa Allah, 'Ee mtume wa Allah! Ni vipi wahyi unakuja?' Mtume wa Allah alijibu, "Wakati mwingine ulifunuliwa kwangu kwa sauti mithili ya mlio wa kengele, wahyi ulioletwa kwa namna hii ulikuwa mgumu sana kuliko aina nyingine zote (za wahyi), kisha hali hii ilikwisha baada ya kukidhibiti kile kilichofunuliwa. Wakati mwingine Malaika*

*(Jibril) alikuja katika umbile la binaadamu na kuzungumza nami, ambapo nilikidhibiti (nilikichukua) chochote kile alichosema." Aysha (r.a) aliendelea kusema: Hakika nilimuona Mtume (s.a.w) wakati anateremshiwa wahyi siku ya baridi kali na kuona jasho likitiririka usoni mwake." (Bukhari)*

Hadithi hizi nazo zinatuthibitishia kuwa Qur-an si utunzi wa Muhammad (s.a.w) kabisa, bali ni ujumbe wa Allah (s.w) uliopitia kwake kwa njia ya wahy.

### **Kuhifadhiwa kwa Qur-an**

Tofauti na vitabu vingine vya Allah (s.w) vilivyotangulia, Qur-an ina ahadi ya Allah (s.w) ya kuhifadhiwa kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿١٥٩﴾

*"Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya (hii Qur-an) na hakika sisi ndio tutakaoyalinda". (15:9)*

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ ۗ تَنْزِيلٌ مِّنْ

حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

*"Haitakifikia batili mbele yake wala nyuma yake, kimeteremshwa na Mwenye Hikima ahimidiwaye." (41:42)*

Kutokana na aya hizi, Qur-an iko vile vile kama ilivyoteremshwa na haijabadilika hata kidogo. Kila aya zilivyoshuka zilihifadhiwa kwa njia tatu zifuatazo:

**Kwanza**, alihifadhiwa Mtume (s.a.w) na kuahidiwa na Mola wake kuwa hatasahau kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

سَتُنْفَرُكَ فَلَا تَنْسَى ۚ ﴿٦﴾ إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفَى ﴿٧﴾

"Tutakusomesha wala hutasahau ila akipenda Mwenyezi Mungu. Yeye anajua yaliyodhahiri na yaliyofichikana." (87:6-7)

لَا تُحَرِّكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ۚ ﴿١٦﴾ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ﴿١٧﴾

فَإِذَا قَرَأْنَاهُ فَاتَّبِعْ قُرْآنَهُ ﴿١٨﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ﴿١٩﴾

"Usitikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi. Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha. Wakati tunapokusomea basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu yetu kuubainisha." (75:16-19)

**Pili**, Waislamu walihifadhi Qur-an vifuani mwao baada ya kusomewa na Mtume (s.a.w).

**Tatu**, Qur-an ilihifadhiwa katika maandishi chini ya usimamizi wa Mtume (s.a.w) mwenyewe. Kila aya ya Qur-an iliposhuka iliandikwa wakati ule ule katika karatasi maalumu za ngozi (Qur-an 52:3) na waandishi wa Mtume (s.a.w) chini ya uangalizi na usimamizi wake kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Uthman bin Affan (r.a) amesimulia: "Wakati wowote Mtume wa Allah alipoteremshiwa wahyi humuita mmoja wa watu waliochaguliwa kuandika." (Tirmidh)*

Naye Zaid bin Thabit mmoja wa waandishi wa Qur-an anasema:

*"Nilikuwa jirani na Mtume wa Allah, kwa hiyo kila alipoteremshiwa wahyi ilikuwa kawaida yake kuniita nami niliandika aliyoniamuru." (Abu Daud)*

Idadi ya waandishi wa Qur-an aliowateua Mtume (s.a.w) ilifikia hadi 42. Miongoni mwa waandishi wa Mtume (s.a.w) ni pamoja na Makhalifa wake wanne - Abu bakr, Umar, 'Uthman na Ally (r.a). Waandishi wengine waliokuwa mashuhuri ni Zaid bin Thabit, Abdullah bin Mas-'ud, Ubayyi bin Ka'ab, na Khalid bin Walid.

Mtume (s.a.w) baada ya kuwaamuru waandishi wake wa Qur-an waandike kile alichowasomea, pia aliwaamuru wamsomee walichoandika na alifanya marekebisho pale walipokosea kama tunavyojifunza katika hadith ifuatayo:

*Zaidi bin Thabit amesema: "... Kila nilipomaliza kuandika (Wahyi) Mtume aliniamuru nisome nilichoandika na nilikuwa ninamsomea. Kama palikuwa na kosa alilisahihisha kisha aliwapa watu (kunakili na kuhifadhi vifuani).*

Pia Mtume (s.a.w) ndiye aliyewaelekeza waandishi wake wa Qur-an wazipange aya na sura kama zilivyo katika msahafu tulionao hivi leo kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*'Uthman bin Affan (r.a) ameeleza: "Ilikuwa kawaida ya Mtume wa Allah kila aliposhushiwa aya za sura mbali mbali (za Qur-an) au kila aya iliposhuka alimuita mmoja wapo wa waandishi wa Qur-an na kumwambia, "Andika aya hizi katika Sura kadhaa baada ya aya kadhaa."*

Pamoja na Hadithi hii kuna hoja kadhaa za kihistoria zinazothibitisha kuwa Qur-an iliandikwa na kukusanywa katika msahafu tulionao hivi leo chini ya usimamizi na uangalizi wa Mtume (s.a.w) mwenyewe. Baadhi ya hoja hizo ni hizi zifuatazo:

**Kwanza** Anas (r.a) aliyekuwa miongoni mwa masahaba wa Mtume (s.a.w) ameeleza kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) aliwaamuru waigawanye Qur-an katika mafungu saba baada ya Suratul-Fatiha (sura ya ufunguzi). Fungu la kwanza katika haya

lilikuwa na sura tatu, kisha likafuatiwa na fungu la sura tano, kisha la sura saba, kisha la sura tisa, kisha la sura kumi na moja, kisha la sura kumi na tatu na mwishowe sura zote zilizobakia ziliwekwa katika fungu moja. Fungu hili la mwisho limeanza na Suratul Qaaf. Ukihesabu sura zote pamoja na sura ya ufunguzi (Suratul-Fatiha) utakuta Suratul-Qaaf inakuwa ni sura ya hamsini (50). Sura hii pia ni ya 50 katika Msahafu tulionao hivi leo kuthibitisha kuwa mpango wa sura katika msahafu ulioelekezwa na Mtume Muhammad (s.a.w) haujabadilika mpaka hivi leo.

**Pili** Katika Hadithi ya Abu Daud, Hudhaifa (r.a) anasimulia kuwa amemuona Mtume (s.a.w) akisoma sura ya Al-Baqara, Al-Imran, An-Nisaa, Al-Maida na Al-An-'am katika mfuatano huo. Mpango wa sura hizi kama zilivyotajwa katika Hadithi hii ni kama ziivyo kwenye msahafu baada ya sura ya ufunguzi ambayo pia imebakia sura ya kwanza katika msahafu tangu alivyoiweka Mtume(s.a.w) katika nafasi ilipo. Hii inaonesha kuwa mpango wa sura lazima uwe umepangwa na Mtume(saw) mwenyewe kama alivyoongozwa na Allah (s.w).

**Tatu** Imam Tirmidh katika kitabu chake cha Hadithi anatufahamisha hadithi ifuatayo:

*"Mtu mmoja aliuliza: "Ewe Mtume wa Allah! Tendo lipi ambalo Allah hulipenda kuliko yote?" Akajibu (Mtume) ("Tendo) la yule analizaye safari na kisha akaendelea nayo". Pakaulizwa: "Nini maana ya kumaliza safari na kuanza nyingine?" Mtume alijibu: "Mwenye kuisoma Qur-an anaisoma tangu mwanzo hadi mwisho na amalizapo anarudia mwanzo na kusoma tena hadi mwisho na hufanya hivi kuwa kawaida yake; yaani kila amalizapo anaanza upya" (Darmi).*

Suala la kusoma Qur-an tangu mwanzo hadi mwisho ni hoja tosha ya kuwepo kwa mpango wa sura ya kwanza hadi mwisho.

## **Je Qur-an ilikusanywa na kuandikwa katika msahafu wakati wa uongozi wa Abu-Bakr(r.a)**

Kwa muda mrefu imekuwepo nadharia kuwa Qur-an katika umbo lake la Msahafu au kitabu imeanza wakati wa Khalifa Abu Bakr baada ya kushauriwa na 'Umar ibn Khattab(r.a). Na inavyosemekana ni kwamba kwanza Abu Bakr (r.a) alikataa ushauri huo kwa kuwa jambo hilo Mtume(s.a.w)hakufanya. Baada ya kuona kuwa ni kweli Qur-an itaweza kupotea maadamu wale waliokuwa wamehifadhi wanakufa, Abubakar alikubali ushauri wa Umar.

Tunaambiwa kuwa Khalifa Abu Bakr(ra) alimchagua Zaid bin Thabit kuifanya kazi ya kuandika Msahafu. Kazi hii ilifanyika kwa kukusanya mifupa, mawe, makozi ya mitende pamoja na ngozi ambamo inasadikiwa kuwa ndimo Qur-an ilimokuwa imeandikwa wakati wote wa miaka 23 ya Utume. Hebu turejee Hadith iliyopokelewa na Imam Bukhari, na kusimuliwa na Zaid bin Thabit (ra) kuwa:

*"Abu Bakr alinitumia mtu kuja kuniita wakati watu wa Yamama walipouliwa (masahaba walipopigana na Musailama). (Nilikwenda) na nilimkuta 'Umar bin Khattab amekaa pamoja naye, Abu Bakr akaniambia: "'Umar amenijia na akaniambia kuwa siku ya Yamama, mauaji mengi yametokea kwa mahafidhi wa Qur-an na nahofia kuwa huenda mauaji yakatokea tena kwa mahafidhi katika vita vingine jambo ambalo linaweza kupelekea sehemu kubwa ya Qur-an kupotea. Hivyo nakushauri (wewe Abu Bakr) kuwa uamrishe kuwa Qur-an ikusanywe." Nikamwambia 'Umar: "Vipi nitafanya jambo ambalo Mtume wa Allah hajalifanya?" 'Umar akaniambia kuwa: "Wallahi; kufanya hivyo ni jambo zuri", na hakuacha kunitaka kufanya hivyo mpaka Allah akaondosha uzito kifuani mwangu na nikaanza kuona uzuri wa mawazo aliyoyaona Umar. Kisha Abu Bakr akaniambia (mimi Zaid): "Wewe ni mtu mwenye akili na hatuna wasi wasi nawe, na wewe ulikuwa ukimuandikia wahyi Mtume (s.a.w).*

*Hivyo vitafute vipande vya Qur-an na uvikusanye'. Wallah! (anasema Zaidi kuwa) lau kama wangeniamrisha kuondoa mmojawapo wa milima, basi lisingelikuwa jambo gumu (zito) kuliko kuikusanya Qur-an. Kisha nikamuuliza Abu Bakr: "Vipi utafanya kitu ambacho Mtume wa Allah hakukifanya?" Abu Bakr alijibu: "Wallahi; kufanya hivyo ni jambo zuri", na akaendelea kunitaka nifanye hivyo mpaka Allah akanipa wepesi kifuani mwangu kama alivyofanya kwa Abu Bakr na 'Umar. Hivyo nikaanza kuitafuta Qur-an (iliyokuwa imetapanyika vipande vipande) katika makozi ya mitende, mawe na mahafidhi na kuikusanya mpaka nikaipata aya ya mwisho ya Suratul-Tawbah kwa Abi Khuza'ymal Ansari; na sikuikuta aya hii kwa yoyote isipokuwa yeye **'Amekujieni Mtume aliye jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni...'** mpaka mwisho wa aya (9:128-129). Kisha nakala ya Msahafu ikabakia kwa Abu Bakr mpaka alipofariki, kisha ikabaki kwa 'Umar mpaka mwisho wa maisha yake na hapo tena kwa binti yake Hafsa. (Bukhari).*

Hadithi hii pamoja na kuwa imepokelewa na Imam Bukhari bado inatupa maswali mengi sana ya kujiuliza kwani kwanza inapingana na Qur-an yenyewe, pili inapingana na ushahidi wa kihistoria pamoja na hadithi nyingine na tatu haikubaliki hata kiakili (kimantiki).

### **(a)Kupingana na Qur-an:**

Hadithi hii inayosimulia kuwa Qur-an ilikusanywa na Zaid bin Thabit(r.a) kutoka kwenye makozi ya mitende na mawe na kutoka kwa mahafidhi inapingana na Qur-an kwa sababu zifuatazo:

- (i) Mwenyezi Mungu (s.w) ameikusudia Qur-an iwe kitabu hata kabla ya kuumbwa chochote katika maumbile yake aliyoyaumba. Kama inavyoashiriwa katika aya mbali mbali kwamba Qur-an ilikuwako kwenye Lawhil Mahfudh hata kabla ya kuteremshwa kwa Mtume (s.a.w) kulingana na matukio



mbali mbali yalivyotokea:

إِنَّهُ لَقُرْءَانٌ كَرِيمٌ ﴿٧٧﴾ فِي كِتَابٍ مَّكْنُونٍ ﴿٧٨﴾

"Bila shaka hiki (mnachosomewa) ni kitabu kilichokusanya kila yanayohitajiwa na chenye heshima. Kimetolewa katika hicho kitabu kilichohifadhiwa kweli kweli." (56:77-78).

بَلْ هُوَ قُرْءَانٌ مَّجِيدٌ ﴿٢١﴾ فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ ﴿٢٢﴾

"Bali hii ni Qur-an tukufu. (Iliyotolewa) katika huo ubao uliohifadhiwa (wa Allah)." (85:21-22).

Aidha Mwenyezi Mungu katika aya mbali mbali amekuwa akiishiria Qur-an na akiita kitabu:

ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾

"Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu." (2:2).

Vile vile rejea 3:3, 7; 7:2; 10:1; 13:1; 14:1, n.k

Kutokana na marejeo hayo haiwezekani kuwa pawe hapana kitu cha aina hiyo lakini bado Mwenyezi Mungu arudie namna hiyo. Kweli, neno "kitab" linatumika kwa vitu mbali mbali vilivyoandikwa kama mikataba au hata barua lakini bado katika Qur-an neno hili limetumika kurudia kitabu katika maana halisi hasa ya kitabu. Chukua mfano, aya ya 7 ya Suratul Al-Imran:

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ  
وَأُخَرٌ مُتَشَابِهَاتٌ

"Yeye ndiye aliyekuteremshia Kitabu. Ndani yake zimo aya Muhkam (nyepesi kufahamika) ambazo ndizo msingi (asili ya Kitabu). Na ziko nyingine Mutashabihat..." (3:7)

Hivyo Allah(s.w) alipotaja neno Al-Kitab kwa kuirudia Qur-an alikuwa na maana hiyo na ndiyo maana Mtume(s.a.w) alipokuwa katika Hija yake ya kuaga alisema nimekuachieni vitu viwili - Kitabu cha Allah na Mwendo wangu. Mtume(s.a.w) asingelisema hivyo kama kitabu hicho hakikuwepo.

(ii)Hadith hiyo pamoja na kuwa imepokelewa na Imam Bukhari bado inakataa aya zifuatazo za Qur-an:

وَكِتَابٍ مَّسْطُورٍ ﴿٢﴾ فِي رَقٍّ مَّنْشُورٍ ﴿٣﴾

*Na (Naapa) kwa Kitabu kilichoandikwa katika karatasi ya ngozi (iliyo safi na) kikakunjuliwa (kisomwe)." (52:2-3).*

Katika aya hii Allah (s.w) anatuambia wazi wazi kuwa Qur-an ni Kitabu kilichoandikwa katika karatasi za aina fulani ambazo zilikuwa zikitumika wakati wa zama hizo. Ni karatasi za aina hiyo hiyo, kama tutakavyoona baadaye, ambazo Mtume(s.a.w) alizitumia kuandikia barua zake na kuwatumia wafalme mbali mbali na kutumiwa na baadhi ya Masahaba kuandikia vitabu vyao.

Kabla hatujaendelea kufafanua zaidi hoja hii ni vyema kunukuu maneno ya mwanazuoni - Qutubi alivyofafanua aya hizo:

*"... Na ameapa (Mwenyezi Mungu) kwa "Kitabu manshurin" (kitabu kilichoandikwa) yaani kilichoandikwa nacho ni Qur-an wanayoisoma Waislamu katika Masahafu na wanayoisoma Malaika katika Lawhul Mahfudh. Na pia inasemwa kuwa (Allah) ameviapia vitabu vingine vyote vilivyoteremshwa kwa Mitume kwani kila kitabu kilikuwa katika karatasi (ya ngozi) wakikunjuliwa watu wake wakisome. Ama "Arraqqu" ni ile iliyotengenezwa kwa ngozi ili iandikiwe".<sup>4</sup>*

---

4. Imenukuliwa katika Safwatut-Tafsiri ya Sheikh Muhammad 'Ali Sabuni, uk. 262, Vol. III, Darul Qur-anil Karim, Beirut 1981.

Lawhul Mahfudh ambao ni ubao uliohifadhiwa hautegemewi kuwa karatasi za ngozi kwani hii ni teknolojia ya mwanaadamu ambayo Mtume(s.a.w) alikutana nayo. Hivyo makusudio ya aya ni Qur-an au Msahafu.

Kutokana na ufafanuzi huo hatuwezi kusema Qur-an ilikuwa imeandikwa katika mifupa wala makozi ya mitende kwani itapingana na aya hii ambayo iko wazi. Haitakuwa na nafasi hata ikipokelewa na maimamu wote kwani kigezo kikuu cha Hadithi ni kutopingana na aya yeyote ya Qur-an. Na kwa nini Zaid(r.a) aone uzito wa kukusanya Qur-an ambayo imeashiriwa na Allah(s.w) kuwa ni kitu kilichopo? Na uzito wenyewe uwe ni zaidi ya kuusogeza mlima!

Kusema hivyo ni kukana aya nyingine za Qur-an pale Allah (s.w) aliposema kuwa kazi ya kuikusanya Qur-an ni yake. Turejee aya zifuatazo:

﴿١٦﴾ لَا تُحَرِّكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ﴿١٧﴾ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ﴿١٨﴾

*"Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka).Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha." (75:16-17)*

Hapa aya inasema wazi kuwa kazi ya kuikusanya Qur-an siyo kifuani mwa Mtume(s.a.w) tu bali kuhakikisha kutoharibiwa kwake pamoja na kuteremka kwake kidogo kidogo ni ya Allah(s.w) kinyume chake Hadith inasema kazi hiyo aliifanya Zaid(r.a)!

### **(b)Kupingana na Ushahidi wa Kihistoria**

Hadith hii pia inapingana na ushahidi wa kihistoria kwa sababu:

- (i) Katika hadithi maarufu sana iliyopokelewa na Imam Muslim toka kwa Ibnu Mas-'ud, Mtume amesema katika Hijja yake ya kuaga kuwa:

*"Na nimewaachieni vitu wili ambavyo mkishikamana navyo hamtapotea kamwe baada yangu - Kitabu cha Allah na Sunnah yangu." (Musilim)*

Hadith hii kiakili haiashirii kitu ambacho hakijulikani kilipo na chenye ugumu kupatikana kama alivyoeleza Zaid (r.a) bali ni kitu ambacho kila mmoja anatarajiwa kukifikia pasipo na ugumu wowote. Wala Hadith hii haishirii kitu ambacho kimetawanyika katika mawe na mifupa ambayo pa kupatikana hapafahamiki bali ni kitu kilichokusanywa na kuhifadhiwa mahala maalumu.

(ii)Ukiacha hadithi hiyo, kuna hadithi nyingine ambayo ameipokea mwenyewe Imamu Bukhari ambayo inasema wazi kabisa kuwa Mtume ameacha Msahafu:

*'Abdul'-Aziz bin Rufai(ra) ameeleza kuwa: "Mimi na Shaddad bin Ma'aqil tuliingia kwa Ibnu "Abbas. Shaddad akamuuliza: Je Mtume (s.a.w) ameacha chochote?" akajibu (Ibn 'Abbas) "Hakuacha chochote isipokuwa (hiki) kilichopo baina ya magamba mawili (ya Qur-an)." Baadaye tulimtembelea Muhammad bin Al-Hanafiyya na akamuuliza suala (lile lile). Akajibu (Al-Hanafiyya), Mtume hakuacha kitu isipokuwa (hiki) kilichopo baina ya magamba mawili (ya Qur-an)."*

Hadithi hii, **kwana**, inaisadikisha Qur-an kuwa ni kitabu (masahafu) ambacho kimeandikwa katika kurasa na kuwekewa magamba (bindings or covers) ili kihifadhike.

**Pili**, Hadithi hii inaisadikisha Hadith tuliyoirejea juu miongoni mwa vitu ambavyo Mtume ameviacha. Hapa tunaambiwa alichocha ni kile kilicho baina ya magamba mawili - la mwanzo na mwisho - yaliyokuwa yamehifadhi Qur-an ambayo hapana shaka ilikuwa ndani ya karatasi za aina yake na siyo ndani ya mawe au mifupa.

**Tatu**, Hadith hii inathibitisha kuwa kweli Allah (s.w) aliikusanya Mwenyewe Qur-an na akaihifadhi katika muundo wa kitabu kupitia kwa Mtume wake.

(iii) Inapingana na Hadith iliyotolewa na Maimamu Tirmidhi na Darimi kuwa Mtume(s.a.w) amesema kwamba msafiri mzuri ni yule anayeianza Qur-an upya kila anapomaliza kuisoma na kwamba hili ndilo tendo analolipenda Allah. Wakati wa Mtume(s.a.w) tunaambiwa kuwa masahaba wengi walikuwa wamehifadhi Qur-an yote lakini bado walipatikana wengine ambao hawakufikia hatua hiyo. Na kwa namna tunavyowafahamu masahaba ambao walikuwa wakishindana katika kufanya mambo mazuri ni lazima wawe ambao huirudia tena na tena kama alivyoashiria Mtume (s.a.w). Sasa watu hawa walikuwa wakiipata wapi Qur-an ambayo ilikuwa imetawanyika kiasi cha aya nyingine kutojulikana zilipo na kugundulikana baadaye kama zilivyokuwa aya za Suratut-Tawbah?

Mitume wa Allah(s.w) siku zote waliwafundisha wafuasi wao vitu wanavyoweza kuvitekeleza na vipo katika mazingira yao, hivyo Mtume (s.a.w) naye alipoongea hivyo aliashiria kitu cha aina hiyo. Tunasoma katika historia kwamba hata baadhi ya masahaba ambao walikuwa mahafidhi wa Qur-an walikuwa wakisoma ile iliyoandikwa. Khalifa 'Uthman bin 'Affan aliuawa wakati akisoma Mas-hafu yake. Hii inawezekana kabisa kuwa ilikuwa ni desturi ya masahaba wengi na ndivyo Mtume (s.a.w) alivyoashiria.

(iv) Mpangilio wa sura zote zilizomo Msahafuni ukilinganishwa na kushuka kwake umeonekana ni tofauti. Mpangilio huu ni ule ambao Mtume (saw) mwenyewe aliuelekeza kama alivyoelekezwa na Allah (s.w). Fikiria aya 6666 ambazo zimeshuka kwa kipindi cha miaka 23 na hazifahamiki zilipowekwa (nani alikuwa mtunzaji) katika hayo mawe na mifupa ni vipi Mtume(s.a.w) angeweza kuashiria kwa maandishi wake kuwa aya hii iwekeni baada ya aya fulani na sura hii baada ya sura fulani?

Tukizingatia maneno ya Zaid(r.a) utakuta kuwa jambo hilo lisingeliwezekana kwani tangu kufariki Mtume(s.a.w) na alipoanza hiyo kazi haukuwa umepita hata mwaka mmoja na waandishi wa Mtume(s.a.w) wote walikuwepo bado. Lakini bado anasema aya moja hakuwa nayo yeyote yule zaidi ya Abu Khuzaymal Ansari ambaye hatuambiwi kuwa alikuwa ni mwandishi wa Mtume! Hadith hii inakataana na hali halisi kama tunavyoendelea kuona.

(v)Tumeona kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa na pupa ya kuhifadhi wahyi ili asiye akasahau kiasi Allah(s.w) akamwambia asifanye hivyo:

لَا تُحَرِّكُ بِهِ لِسَانَكَ لِتَتَّعَلَ بِهِ ۗ

*"Usitikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka)." (75:16)*

وَلَا تَتَّعَلْ بِالْقُرْآنِ مِّنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ إِلَيْكَ وَحْيُهُ ۗ

*"Wala usiifanyie haraka (hii) Qur-an (kwa kusoma), kabla haujamalizika wahyi (ufunuo) wake." (20:114).*

Sasa Mtume(s.a.w) ambaye alikuwa na pupa kiasi kama hicho cha kuhakikisha amehifadhi kila alicholekwa na Jibril(a.s) na kuhakikisha anaandikwa kila aya inayoteremka, iweje tena kuandika kwenyewe kuwe ndani ya mawe, makozi ya mitende na mifupa kiasi kwamba alipofariki haijulikani ameiweka wapi hiyo mifupa! Mtume(s.a.w) kulingana na khofu hiyo kabisa asigeliandika Qur-an mahala kama humo halafu asiweke mtu wa kuitunza bali iwe pata-potea. Hapana shaka huku ni kumsingizia Mtume(s.a.w) kuwa alikuwa hajali Qur-an:

(vi)Swali jingine la kujiuliza, kwa nini Mtume atumie mawe, mifupa na makozi ya mitende kuandikia maneno matukufu ya Allah(s.w) na wakati karatasi zilikuwepo na zikitumika? Qur-an yenyewe inathibitisha kuwa wakati ule karatasi zilikuwepo:

وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ كِتَابًا فِي قِرْطَاسٍ فَلَمَسُوهُ بِأَيْدِيهِمْ لَقَالُوا الَّذِيْنَ كَفَرُوا

إِنْ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٧﴾

*"Na lau tungelikuteremshia maandishi katika karatasi(kama wanavyotaka) na wakayagusa (wakakigusa hicho kitabu) kwa mikono yao, bila shaka wale waliokufuru wangelisema: "Haya si chochote ila ni uchawi dhahiri." (6:7)*

Historia (tarekh) inatuambia kuwa Mtume (s.a.w) ametumia karatasi kuandikia:

- Katiba yake iliyoandikwa mara tu baada ya kuingia Madina.
- Sulhu ya Hudaybia.
- Barua alizowatumia wafalme mbali mbali.

Je kusema kuwa Mtume(s.a.w) ametumia mawe na mifupa kuandikia Qur-an haionekani kuwa Mtume(s.a.w) amethamini zaidi maandishi mengine kuliko maneno ya Mwenyezi Mungu? Haiwezekani iwe hivyo bali ni visa vilivyobuniwa kuudhoofisha ukweli na Hadhi ya Qur-an.

Huenda pia ikadhaniwa kuwa, kwa sababu ya ugumu wa kupatikana karatasi ndiyo Mtume akawa anatumia mawe na mifupa. Dhana hii vile vile haina msingi kwani tunaambiwa kuwa masahaba mbali mbali walikuwa na vitabu vyao wakiandika mafunzo ya Uislamu. Hebu turejee Hadith zifuatazo:

*Abu Hurayrah(ra) amesema: "Hapana hata mmoja katika masahaba wa Mtume ambaye amesimulia Hadith nyingi zaidi kuliko mimi ukimtoa (isipokuwa) 'Abdullah bin 'Amr ambaye alikuwa anaandika wakati mimi sikufanya hivyo." (Bukhari).*

*"Abu Hudhaifa(ra) amesema: Nilimuuliza Ali je muna kitabu chochote kile (zaidi ya Qur-an)? Ali alisema hapana isipokuwa kitabu cha Mwenyezi Mungu au uwezo wa ufahamu ambao amepewa Muislamu au hiki kilichomo katika upande huu wa karatasi (sahifa)..." (Bukhari).*

Hivyo suala la ugumu wa karatasi halipo kwani hapana hata sahaba mmoja ambaye angekataa kutoa karatasi ya kuandikia Qur-an kama angetakiwa kufanya hivyo.

(vii)Suala la karatasi kuwepo tena kwa wingi linaonekana hata kwa Mayahudi na Wakristo ambao walikuwa na vitabu vyao vinavyobebeka siyo vya mifupa wala mawe.Hebu turejee Hadith ifuatayo: 'Abdallah bin 'Umar amesema:

*"Mayahudi walikwenda kwa Mtume na kueleza kwamba mwanamke na mwanamume mmoja wao amezini Mtume akawauliza: 'Je katika Tawrat hakuna sheria ya kupiga mawe mpaka kufa?' Wakajibu: 'Tunawafedhehesha kisha tunawapiga bakora!' 'Abdullah bin Salaam akasema: "Waongo kwa hakika ndani ya Tawrat imo habari ya kupiga mawe hadi kifo. "Wakalete Tawrat isomwe na mmoja wao akaifunika ile aya ya kupiga mawe kwa mkono wake na badala yake akasoma aya ya juu na chini. 'Abdallah bin Salaam akamwambia: "Ondoa mkono wako." Akaondoa na mara ikaonekana aya ya kupiga mawe. Akasema "Muhammad amesema kweli kweli kwani imo aya ya kupiga mawe..." (Bukhari na Muslim).*

Huo ni ushahidi wa vitabu vilivyokuwepo. Na hata katika Qur-an tunaambiwa kuwa imeandikwa katika karatasi (52:2-3) jambo ambalo limejitokeza wakati aliposilimu Umar bin Khatab. Tunaambiwa kuwa kilichomsilimisha ni suhufa - ukurasa wa karatasi ya wakati ule ambao ulikuwa umeandikwa Surat Taha.



### **(c)Hoja za Kiakili (mantiki - logic)**

Kimantiki vile vile Hadith ya Zaid haina nguvu kwa sababu:

(i)Katika masahaba ambao Mtume (s.a.w) aliwachagua kama waandishi wake wa wahyi hatumkuti mtu anayeitwa Abu Khuzaymal Ansari. Ukiwatoa makhalifa wanne na baadhi ya Muhajiriin tunawapata Ansari wachache sana ambao walishughulikia uandishi wa wahyi wakati wa Mtume(s.a.w). Jambo la kushangaza na kutia wasi wasi katika simulizi hii ni kuwa wale waandishi wote wa Mtume (s.a.w) walioteuliwa maalum kuandika wahyi hawakuwa na aya hizo isipokuwa sahaba huyu ambaye hakuwemo! Hivyo ni kweli, Mtume(s.a.w) ambaye kila unapoteremka wahyi hata usiku huwafuata waandishi wake ili wauandike leo hii waandishi hao ambao walikuwa majirani zake wa pua na mdomo wasiwe na aya hizo mbili bali awe nazo mtu wa mbali ambaye ni mmoja tu? Haiwezekani kabisa.

Tatizo jingine la simulizi hii ni kupingana na Hadithi nyingine au tukio lingine ambalo vile vile ni lenye kutia wasi wasi. Katika simulizi nyingine aliyoitwa Anas bin Malik na kupokelewa na Imam Bukhari tunaambiwa kuwa Khalifa 'Uthman baada ya kupata habari kuwa Qur-an inatamkwa kinyume kabisa alivyoitamka Mtume(s.a.w) aliamrisha kuandikwa nakala sanifu kwa ajili ya marudio ya watu wote. Kazi hii ya kuinakili Qur-an kutoka Msahafu unaodaiwa wa Hafsa ambao uliandikwa wakati wa Abu Bakr walikabidhiwa:

- Zaid bin Thabit. (r.a)
- Abdallah bin Zubery.(r.a)
- Sa'id bin Al'As.(r.a)
- Abdulrahman bin Harith bin Hisham.(r.a)

Katika kunakili huku Msahafu wa Hafsa kulionekana kuwa aya moja ilikosekana na mara hii ilikuwa ni:

مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ

*"Wapo watu miongoni mwa walioamini waliotimiza ahadi walioahidiana na Mwenyezi Mungu..." (33:23)*

Aidha aya hii ilipatikana kwa Khuzayma bin Thabit al-Ansari! Hivyo ni kweli kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi na mbili kitabu cha Allah(s.w) kiwe kimepungua aya na watu wote wasijue pamoja na kuwepo mahafidhi chungu nzima? Msahafu huo unaoambiwa kuwa umeandikwa wakati wa Abu Bakr(r.a) ulikuwa ndio rejea ya watu wote, je kama mtu atasema kuwa Qur-an haikuwa imetimia kwa kipindi kile atakuwa na makosa? Watu wote walirejea msahafu huo pungufu, je ahadi ya Allah(s.w) ya kuihifadhi Qur-an iko wapi wakati Msahafu pekee uliokuwapo ulikuwa na kasoro ya aya moja? Hivyo, ni visa vya kubuni tu.

(ii)Inavyofahamika ni kuwa Zaid bin Thabit (r.a)ni mtu wa Madina (Ansar) sasa vipi ilikuwa hali ya Makka ambapo yeye alikuwa hayupo? Bila shaka palikuwa pana waandishi wengine ambao walimtangulia kwenye kazi hiyo na akashirikiana nao walipokuwa Madina. Mtume(s.a.w) alikuwa na kikundi chake cha waandishi wa wahyi na maandishi mengine kama vile mikataba. Je, ni jambo lenye kuingia akilini kuwa watu wote hao ambao inasadikiwa kufika 42 waikose aya hiyo na badala yake awe nayo mtu wa mbali? Je waandishi hao walikuwa na kazi gani ikiwa kuna aya ambazo hawakuziandika? Desturi ya masahaba ilikuwa ni ya kusubiri wahyi mpya kama vile watu wanavyosubiri taarifa ya habari siyo wajue tu bali watekeleze. Masahaba walikuwa wanapangiana zamu za kwenda kukaa kwa Mtume ili kujua jambo lolote jipya linalowahusu wao binafsi au jamii. Simulizi hii inatuambia pamoja na kusikilizwa mahafidhi bado aya hii ilipatikana kwa mtu mmoja! Je tuseme kwa kipindi chote hicho tangu alipofariki Mtume hadi kuanza kuandikwa wakati wa 'Uthman watu walihifadhi msahafu wenye upungufu? Haiwezekani bali simulizi ni ya uzushi.

(iii) Simulizi hii vile vile inatupa wasi wasi zaidi kwani haiwezi kujibu maswali ya fuatayo: Kwa nini Zaid(r.a) aisake mifupa na mawe ambayo yametumika kuandikia Qur-an na siyo kwenda kuyachukua mahali fulani tu? Je ni sahaba gani aliyekuwa dhamana ya kulinda mifupa na mawe hayo? Wakati Mtume alipohama Makka, mawe yale na mifupa ilichukuliwa? makozi ya mitende katika kipindi cha miaka 13 hayaozi tu?!, Usafiri gani walitumia kubebea mawe, mifupa na makozi yaliyokuwa na aya za Qur-an? Kwa kusaidia kujibu maswali hayo ni kwamba lazima mawe au mifupa hiyo ingelikuwa imekusanywa katika mojawapo ya nyumba za Waislamu hivyo pasingekuwa na haja ya kusakwa. Iliyokuwa hizo ni aya za Allah (sw), Mtume(s.a.w) asingethubutu kuwaachia makafiri wazichezee, hivyo lazima ingesimuliwa ni vipi alizihamisha, lakini hatuna habari kama hiyo. Ukizingatia idadi ya aya za Qur-an kuwa ni 6,236 ni lazima mawe na mifupa hiyo mikubwa ingekuwa imeshindiliwa katika magunia jambo ambalo siyo kweli. Hivyo maswali hayo na majibu yanatuthibitishia kuwa hiki ni kisa cha kubuni ambacho hakiingii akilini.

(iv) Al-Bukhariy ni binaadam, pamoja na udhibitifu mkubwa aliokuwa nao Al-Bukhary katika ukusanyaji, uchambuzi na uandishi wa Hadith bado yeye ni binaadam na anayomadhaifu, hakuwa akipokea wahy wowote hivyo ubinaadamu wake yatosha yeye kukosea kunakili jambo kama hili katika sahihi yake, kwani pia zipo Hadith nyingi tu dhaifu zinazopatikana katika sahihi yake. Pia inamkinika maadui wa Uislamu wakapachika Hadith hii katika kitabu chake. Tukikumbuka kuwa vitabu vya Hadith havina hivadhi ya Allah kama ilivyo Qur'an(15:9)

## Lugha ya Qur-an:

Lugha iliyotumika katika Qur-an ni Kiarabu sanifu kama tunavyojifunza katika Qur-an yenyewe:

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِّتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا  
وَتُنذِرَ يَوْمَ الْجَمْعِ لَا رَيْبَ فِيهِ فَرِيقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ

*"Na namna hii tumekufunulia Qur-an kwa Kiarabu ili uwaonye watu wa Makka na walio pembezoni mwake. Na uwaonye siku ya mkutano, siku isiyo na shaka. Kundi moja litakuwa Peponi na kundi jingine Motoni....."* (42:7)

## Kwa nini Qur-an Imeshushwa kwa Lugha ya Kiarabu?

Walimwengu walio wengi wakiwemo baadhi ya Waislamu wanaitakidi kuwa lugha ya Kiislamu ni Kiarabu na Uislamu ni dini ya Waarabu. Bila shaka mawazo haya yamejitokeza kutokana na kutoujua Uislamu kwa upeo wake. Uislamu ni Dini ya Walimwengu wote wa nyakati zote na ni Dini iliyofundishwa na Mitume wote. Je, Mitume wote walikuwa Waarabu au watu wote waliolinganiwa na Mitume hao na kuwafuata walikuwa Waarabu? Bila shaka jibu litakuwa "hapana". Bali tunajifunza katika Qur-an yenyewe kuwa Allah (s.w) amewajaalia walimwengu kuzungumza lugha mbali mbali na ni katika ishara ya Uungu wake na utukufu wake.

وَمِنْ آيَاتِهِ خَلْقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَخْتِلَافَ اللَّسَانِ وَالْوَالِدَاتِ

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّلْعَالَمِينَ ﴿٢٢﴾

*"Na katika Ishara zake (zinazoonyesha uwezo wake) ni kuumba mbingu na ardhi, na kuhitilafiana lugha zetu na rangi zenu. Kwa yakini katika haya zimo ishara kwa wenye ujuzi."* (30:22)

Kwa nini Qur-an imeshushwa kwa lugha ya Kiarabu? Jibu lake linapatikana ndani ya Qur-an yenyewe:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ رَسُولٍ إِلَّا بِلِسَانِ قَوْمِهِ لِيُبَيِّنَ لَهُمْ فَيُضِلُّ اللَّهُ مَنْ يَشَاءُ  
وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٤﴾

*"Na hatukumpeleka Mtume yeyote isipokuwa kwa lugha ya watu wake ili apate kuwabainishia. Kisha, Mwenyezi Mungu anamuacha kupotea amtakaye (kwa kuwa hataki kufuata ujumbe uliomfikia wazi wazi) na humuongoza amtakaye. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye Hekima." (14:4)*

Aya hii inatufahamisha kuwa kila Mtume alishushiwa Wahyi kwa lugha ya watu wake ili yeye mwenyewe apate kuwabainishia vizuri na wao wapate kumuelewa vizuri. Kwa kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa Mwarabu wa kabila la Kiquraishi na kwa kuwa Maquraish na Waarabu kwa ujumla ndio watu wake wa mwanzo kuwalingania Uislamu ili wamsaidie kuufikisha ulimwengu mzima. Qur-an ilibidi ishushwe kwa lugha ya Kiarabu cha Kiquraish kilichokuwa fasaha kuliko vilugha vyote vya Kiarabu. Watu wake wasingemuelewa kabisa kama Mtume (s.a.w) angewaligania kwa lugha isiyokuwa ya Kiarabu:

وَلَوْ جَعَلْنَاهُ قُرْءَانًا أَعْجَمِيًّا لَقَالُوا لَوْلَا فُصِّلَتْ آيَاتُهُ ؕ أَعْجَمِيٌّ وَعَرَبِيٌّ

*"Na lau kama tungaliifanya Qur-an lugha isiyo ya Kiarabu wangelisema: Kwa nini aya zake hazikupambanuliwa? Lo! Lugha isiyokuwa ya Kiarabu na (Mtume) Mwarabu! (Mambo gani hayo)?....." (41:44).*

وَلَوْ نَزَّلْنَاهُ عَلَىٰ بَعْضِ الْأَعْجَمِينَ ﴿١٩٨﴾ فَقَرَأَهُ عَلَيْهِمْ مَا

كَانُوا بِهِ مُؤْمِنِينَ ﴿١٩٩﴾

*"Na lau tungaliiteremsha juu ya mmoja wa wasiokuwa Waarabu, na akawasomea (kwa ufasaha) wasingalikuwa wenye kuamini." (26:198-199)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa:

- (i) Ni desturi ya Allah (s.w) kumtuma mjumbe wake kwa lugha ya watu wake anaowafikishia.
- (ii) Qur-an imeteremshwa kwa lugha ya Kiarabu kwa kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa Mwarabu na wale aliowalingania mara ya kwanza walikuwa ni Waarabu.
- (iii) Waarabu wa mwanzo kulinganiwa Uislamu na Mtume (s.a.w) wasingeliukubali ujumbe kama Mtume asingelikuwa Mwarabu na kama angelingania kwa lugha nyingine isiyokuwa ya Kiarabu.
- (iv) Kama Mtume (s.a.w) angelingania kwa lugha nyingine isiyokuwa Kiarabu, ujumbe wake usingelifahamika na watu wake wasingelazimika kuufuata kwa kuwa hawauelewi.

### **Ujumbe wa Qur-an Utawafikiaje Wale wasio Waarabu au wale Wasiojua Kiarabu?**

Si jambo zuri na si hekima mtu kufikisha ujumbe kwa Kiarabu wakati wasikilizaji wake hawafahamu lugha hiyo. Ni kweli kuwa Kiarabu ni lugha ya Qur-an na lugha aliyoitumia Mtume (s.a.w) kufundishia yale aliyoteremshiwa kutoka kwa Allah (s.w). Hivyo ni lugha ambayo inampasa kila Muislamu ajitahidi kujifunza. Pamoja na umuhimu wa kuifahamu lugha ya Kiarabu, haina maana kuwa anayekijua Kiarabu ndiye Muislamu na yule asiyekijua ni Muislamu mwenye kasoro.

La muhimu ni kuujua ujumbe wa Qur-an na kuendesha maisha ya kila siku kwa mujibu wa ujumbe huo. Ujumbe wa Qur-an unaweza kumfikia kila Muislamu pasina shaka yoyote kwa lugha yake kwa kusoma tafsiri na sherehe ya Qur-an ambayo kwa Rehema ya Allah (s.w) imetolewa katika lugha mbali mbali na wanachuoni wacha Mungu ambao ni mashuhuri katika uliwengu wa Waislamu. Tukumbuke kuwa Qur-an imeshushwa kwa ajili ya walimwengu wote

ambao Allah (s.w) amewajaalia kuzungumza lugha zinazotofautiana (rejea Qur-an (39:22). Naye Mtume (s.a.w) pia ameletwa kwa ajili ya walimwengu wote. Hivyo ili ujumbe wa Qur-an na Sunnah uwafikie walengwa wote, hauna budi kufasiriwa kwa lugha za walengwa wote. Kazi ambayo kwa Rehema ya Allah (s.w) imeshafanyika. Leo hii hapana udhuru kwa mtu yeyote ulimwenguni wa kutoufahamu ujumbe wa Qur-an kwa sababu si Mwarabu au hajui Kiarabu.

### **Haja ya Kujifunza Lugha ya Kiarabu kwa Waislamu:**

Ipo haja kubwa kwa Waislamu kujifunza lugha ya Kiarabu kuliko ile haja tunayoitambua ya kujifunza lugha za kigeni na za Kimataifa kama vile Kiingereza, Kifaransa, n.k. Kwa mfano hapa Tanzania tunajifunza lugha ya Kiingereza (English) ili tuweze kufaidika kitaaluma, kiuchumi, na kisiasa n.k. Tukijifunza lugha ya Kiarabu tunafaidika na hayo yote pamoja na ziada ifuatayo:

- (i) Tutaufahamu ujumbe wa Qur-an na mafundisho ya Mtume (s.a.w) kwa lugha yake ya asili. Daima tafsiri haikosi upungufu japo kidogo.
- (ii) Tutaweza kufahamu maana ya undani ya dua na dhikiri mbali mbali tunazoleta katika ibada maalum kama vile swala ambapo haturuhusiwi kutumia lugha nyingine isiyokuwa Kiarabu. Kufahamu maana ya yote tuyasemayo katika swala hutupelekea kuwa na khushui inayotakikana.
- (iii) Lugha ya Kiarabu ni chombo cha kuwaunganisha waislamu wote ulimwenguni ili wadumishe udugu na umoja wao kama wanavyotakiwa wawe. Kama Waislamu wanavyoshikamana katika swala kwa kutumia lugha moja ndivyo wanavyotakiwa waelewane na kushikamana katika ibada zote zinazofanywa kimataifa kama vile Ibada ya Hija.

## Namna ya Kuiendea Qur-an

Pamoja na kujifundisha kuisoma Qur-an kwa kuzingatia hukumu zake na kuwafundisha watoto wetu hivyo, hatuna budi kuisoma Qur-an kwa mazingatio ili kufikia lengo la kushushwa kwake. Qur-an imeshushwa ili iwe mwongozo wa maisha yetu yote ya binafsi na ya jamii. Mtume (s.a.w) alipoamrisha katika mwanzo wa Utume wake "Warattilil-Qur-an tar-tiilaa" - "na soma Qur-an vilivyo" haikuwa na maana ya kumtaka Mtume(s.a.w) kuisoma Qur-an kwa tajwidi kama wasomaji wa tajwid wanavyoghani, bali ni amri ya Allah (s.w) iliyomtaka Mtume(s.a.w) na wafuasi wake, wote wa ulimwengu mzima, waisome Qur-an kwa mazingatio ili waupate kwa uwazi ujumbe uliomo na waweze kuufuata vilivyo katika maisha yao ya kila siku. Wale wanaosoma aya za Qur-an bila ya kuzizingatia na kuziingiza katika utendaji Allah (s.w) amewalinganisha na punda', mbwa, viziwi na vipofu

مَثَلُ الَّذِينَ حُمِلُوا التَّوْرَةَ ثُمَّ لَمْ يَحْمِلُوهَا كَمَثَلِ الْحِمَارِ يَحْمِلُ  
أَسْفَارًا بِئْسَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَبُوا بِعَاثِرِ اللَّهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ  
الظَّالِمِينَ ﴿٥﴾

*Mfano wa wale waliopewa Taurati kisha hawakuichukua, ni kama mfano wa punda aliyebeba vitabu. Ni mfano mbaya kabisa wa watu waliokadhibisha aya za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu. (62:5).*

فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ الْكَلْبِ إِنْ تَحْمِلْ عَلَيْهِ يَلْهَثْ أَوْ تَتْرُكْهُ يَلْهَثْ  
..Basi mfano wake ni kama mfano wa mbwa, ukimkimea anahema, ukimwacha anahema..(7:176).

صُمِّمْتُ بِكُمْ عَمَىٰ فَهُمْ لَا يَرُوعُونَ ﴿١٨﴾

*"Viziwi, mabubu, vipofu, kwa hivyo hawatarejea (katika uongofu)." (2:18)*



Kwa namna nyingine, Allah (s.w) anatufahamisha kuwa, waja wake anaowapenda atakaowaongoza katika njia iliyonyooka hapa ulimwenguni na kuwalipa ghorofa za Peponi na makazi mazuri kabisa, ni pamoja:

﴿٧٣﴾ وَالَّذِينَ إِذَا ذُكِرُوا بِعَآيِنِ رَبِّهِمْ لَمْ يَخِرُّوْا عَلَيْهَا صُمًّا وَعُمْيَانًا

*"Na wale ambao wanapokumbushwa aya za Mola wao hawaziangukii kwa uziwi na upofu." (25:73)*

Kwa kuzingatia maelezo haya, ili tuweze kuongozwa na Qur-an hatuna budi kufanya yafuatayo:

- (i) Tupitie kwa makini maelezo ya kitabu hiki ili tuwe na yakini kuwa Qur-an ni kitabu cha Allah (s.w) kisicho na shaka hata kidogo.
- (ii) Kwa kuwa na yakini kuwa Qur-an ni ujumbe kutoka kwa Allah (s.w), hatuna budi kuisoma kwa mazingatio na kujitahidi kupata ujumbe unaotokana na kila aya.
- (iii) Ili kuupata kwa uwazi ujumbe wa kila aya au kila sura ya Qur-an hatunabudi kusoma tafsiri na shereheza wanazuoni mbali mbali waliojitahidi kuitafsiri(kuifasili) Qur-an katika lugha tunayoimudu. Qur-an imetafsiriwa katika lugha mbali mbali kikiwemo Kiswahili na Kiingereza.
- (iv) Baada ya kuupata kwa uwazi ujumbe wa Qur-an hatuna budi kuyaingiza maagizo ya Mola wetu katika utendaji huku tukimfanya Mtume (s.a.w) kiigizo chetu na huku tukizingatia msisitizo wa aya zifuatazo:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُمِئَةٍ إِذَا قَضَىٰ اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ

الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

*"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata*

shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotofu ulio wazi (kabisa)." (33:36)

﴿٤٤﴾ وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ

"Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri." (5:44)

﴿٤٥﴾ وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu (5:45)

﴿٤٧﴾ وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

"Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio mafasiki(5: 47)

(v)Ili kuiingiza Qur-an yote katika maisha yetu ya kila siku na kujipamba na tabia ya Qur-an lazima kujenga tabia ya kuwa wasafiri wa Qur-an wa kudumu kwa kuipitia kwa mazingatio kuanzia sura ya mwanzo (Al-Faatiha) mpaka ya mwisho (An-Naas) na iwe ni ada yetu mpaka tutakapokufa. Kufanya hivyo Mtume (s.a.w) amefananisha na mtu kufanya safari ya kheri isiyokatika, ambayo ina malipo makubwa mbele ya Allah (s.w). Kuipitia Qur-an yote mara kwa mara kwa mazingatio humfanya muumini aweze kuishi katika mipaka ya Allah (s.w) katika kila kipengele cha maishayake.

(vi)Tuwe na tabia ya kuirejea Qur-an kila tunapokwama au tunapokabiliwa na tatizo lolote la kibinafsi au la kijamii. Tusiridhike kujifanyia au kufuata mkumbo katika kuendea mambo ya kibinafsi au ya kijamii bila ya kuangalia kwanza Allah (s.w) kasema nini au kaagiza nini juu ya jambo hilo

au Mtume wake (s.a.w) ambaye ndiye mfasiri wa Qur-an, ameliendeaje jambo hilo. Katika kusesitiza nukta hii tuzingatie agizo la Mtume (s.a.w) alilolitoa mwezi 9 Dhul-Hajj, 10 A.H. (633 A.D) katika uwanja wa Arafah katika Hija ya kuaga (Hijjatul-Wadaa) pale aliposema:

*"Nimekuachieni vitu viwili ambavyo mkikamatana navyo hamtapotea abadan, navyo ni kitabu cha Allah (Al-Qur-an) na Sunnah ya Mtume wake."*

(vii) Tufanye juhudi ya kusimamisha Uislamu katika jamii kwa mali zetu na nafsi zetu, ili tuweze kuufuata Uislamu wote katika kila kipengele cha maisha ya binafsi na ya jamii kama Qur-an yenyewe inavyo sisitiza:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا ادْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَآفَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ

الشَّيْطَانِ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٢٠٨﴾

*"Enyi mliaoamini! Ingieni katika hukumu zote za Uislamu, wala msifuute nyayo za shetani, kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri." (2:208)*

Ni dhahiri kwamba pale ambapo Uislamu haujashika hatamu za Uongozi wa jamii, Waislamu watakuwa hawana namna ya kutofuata nyayo za shetani katika siasa, uchumi, utamaduni na katika kila nyanja ya maisha ya jamii. Pale ambapo Uislamu haujasimama katika jamii, Waislamu watakuwa wanaswali huku chakula chao na kivazi chao kinatokana na uchumi haramu unaotokana na uzinzi, kamari, riba, ulevi, rushwa utapeli na mengineyo. Watakuwa wanafunga huku futari na daku yao inatokana na uchumi haramu, watakuwa wanatoa zakat na kuhiji kwa mali inayotokana na uchumi haramu; watakuwa wanamuabudu Mwenyezi Mungu wakiwa misikitini na wanapotoka misikitini hufuata sera na sharia zilizotungwa na matwaghati

mabungeni. Hivyo, ni wazi kuwa pale ambapo Uislamu haujasimama katika jamii, Qur-an haitapewa nafasi na kuwaongoza Waislamu katika kila kipengele cha maisha yao, jambo ambalo inabidi Waislamu waingie katika jihadi ili kupigania uhuru wao wa kuongozwa na Qur-an. Kama Waislamu watapuuza suala hili la jihadi na wakaridhika kuishi maisha ya mseto ya kutumikia miungu wawili - Allah (s.w) katika swala, zakat, saum, n.k na Twaghuti katika uchumi, siasa, sheria, n.k. wajue kuwa hawana ridhaa ya Allah (s.w) bali hali yao halisi ni ile inayoelezwa katika aya zifuatazo:

أَفْتُوْمُونَ بَبْعُضِ الْكُتُبِ وَتَكْفُرُونَ بِبَعْضِ فَمَا جَزَاءُ مَن يَفْعَلُ ذَٰلِكَ مِنكُمْ إِلَّا خِزْيٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يُرَدُّونَ إِلَىٰ أَشَدِّ الْعَذَابِ

"... Je! Mnaamini baadhi ya kitabu na kukataa baadhi (yake)? Basi hakuna malipo kwa mwenye kufanya haya katika nyinyi ila ni fedheha katika maisha ya dunia, na siku ya Kiyama watapelekwa katika adhabu kali..." (2:85)

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أُولَئِكَ هُمُ الظُّلُمَاتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

"Mwenyezi Mungu ni mlinzi (kiongozi) wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika nuru. Lakini waliokufuru walinzi (viongozi) wao ni matwaaghuti. Huwatoa katika nuru na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa motoni, humo watakaa milele. (2:257)

## Zoezi la Kwanza

1. (a) Chemchem ya mafundisho ya Uislamu ni \_\_\_\_\_  
na \_\_\_\_\_
  - (b) Qur-an ni \_\_\_\_\_
  - (c) Lengo la kushushwa Qur-an ni \_\_\_\_\_
  - (d) Ili kudhihirisha uwezo wake katika kumuongoza binaadamu, Qur-an imesifiwa kwa majina yafuatayo:
    - (i) \_\_\_\_\_
    - (ii) \_\_\_\_\_
    - (iii) \_\_\_\_\_
    - (iv) \_\_\_\_\_
    - (v) \_\_\_\_\_
    - (vi) \_\_\_\_\_
    - (vii) \_\_\_\_\_
    - (viii) \_\_\_\_\_
    - (ix) \_\_\_\_\_
    - (x) \_\_\_\_\_
  - (e) Toa maelezo mafupi juu ya kila jina la Qur-an uliloliorodhesha katika swali 1(d).
  - (f) Qur-an huongoza wacha-Mungu wenye sifa zifuatazo:
    - (i) \_\_\_\_\_
    - (ii) \_\_\_\_\_
    - (iii) \_\_\_\_\_
    - (iv) \_\_\_\_\_
  - (g) Wasioongozwa na Qur-an ni \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_
2. (a) Eleza kwa muhtasari historia ya kushushwa Qur-an:
  - (b) Tofautisha sura za Makka na zile za Madinah.

3. (a) Orodhesha madai kumi (10) wanayotoa makafiri dhidi ya Qur-an:  
 (b) Onesha udhaifu wa madai matano (5) dhidi ya Qur-an.
  
4. Kwa kuirejea Qur-an yenyewe na Historia ya kushuka kwake, toa hoja kumi (10) kuthibitisha kuwa Qur-an ni ufunuo kutoka kwa Allah (s.w).
  
5. *“Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya (hii Qur-an) na hakika sisi ndio tutakaoyalinda”. Onesha namna Qur-an ilivyohifadhiwa wakati wa Mtume (s.a.w).*
  
6. Kwa mujibu wa Qur-an, hekima ya Qur-an kushushwa kwa lugha ya Kiarabu ni:
  - (a) \_\_\_\_\_
  - (b) \_\_\_\_\_
  - (c) \_\_\_\_\_
  - (d) \_\_\_\_\_
  
7. Ili Qur-an ituongoze kwenye njia iliyonyooka hatunabudi kufanya mawili yafuatayo:
  - (a) \_\_\_\_\_
  - (b) \_\_\_\_\_

## Sura ya Pili

# MAFUNZO MAALUMU

### Utangulizi:

Katika sura hii tumechagua sura au aya mbali mbali za Qur-an zenye kuainisha:

1. Sifa za Waumini.
2. Sifa za wanafiki.
3. Maadili na malezi ya jamii.
4. Wajibu wa waumini katika jamii.
5. Maandalizi ya mlinganiaji Uislamu katika jamii.

Tarajio ni kwamba baada ya wasomaji kuupitia na kuutafakari kwa makini ujumbe wa sura hizi wataweza kuwa waumini wa kweli walioepukana mbali na unafiki, watakaoweza kujipamba na maadili mema na kuchukua nafasi yao ya kuwa umma bora (Qur-an 3:110) katika jamii.

Pia tunatarajia kuwa pamoja na kupata ujumbe utokanao na aya hizi, wasomaji watapata uzoefu wa kuchanganua na kuingiza katika utendaji ujumbe wa Qur-an pale watakapokuwa wanaipitia (Qur-an) katika usomaji wao wa kila siku wakitekeleza amri ya Allah (s.w):

.....وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلاً ﴿٤﴾

"..... Na soma Qur-an vilivyo (kwa mazingatio)" (73:4)

### 1. Sifa za waumini

Sifa za waumini zimeainishwa katika aya mbali mbali za Qur-an, lakini katika sura hii tutapitia sifa za waumini zilizoainishwa katika sura za Qur-an zifuatazo:

## 1. Al-Anfal (8:2-4) na Al-Hujurat (49:15)

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ  
ءَايَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢﴾ الَّذِينَ يُبَيِّمُونَ  
الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٣﴾ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا لَهُمْ  
دَرَجَاتٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَمَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٤﴾

*"Hakika wanaoamini kweli ni wale ambao anapotajwa Allah nyoyo zao hujaa khofu; na wanaposomewa aya zake huwazidishia imani na wanamtegemea Mola wao tu basi." Ambao husimamisha swala na wanatoa katika yale tuliyo wapa. Hao ndio wanaoamini kweli kweli, wao wana vyeo (vikubwa) kwa Mola wao, na msamaha na riziki bora kabisa". (8:2-4)*

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا وَجَاهَدُوا  
بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

*"Wenye kuamini kweli kweli ni wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake kisha wakawa si wenye shaka na wanaopigania dini ya Allah kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio wenye kuamini kweli kweli." (49:15)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa waumini wa kweli ni wale wenye sifa zifuatazo:

### (i)Wana yakini kuwa Allah (s.w) yupo

Waumini wa kweli huwa na yakini nyoyoni mwao juu ya kuwepo Allah (s.w) na Mtume wake. Yaani wanashuhudia kwa dhati nyoyoni mwao kuwa Allah (s.w) ni Mola wao pekee na Muhammad (s.a.w) ni Mtume wake wa mwisho na katika matendo yao yote huishi kwa kufuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na daima hukumbuka msisitizo wa aya ifuatayo:



وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا لِمُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ  
 الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

*“Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri wawe na hiari katika shauri lao. na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotofu ulio wazi (kabisa).” (33:36)*

**(ii)Humcha Allah (s.w) kwa kutekeleza amri zake**

Anapotajwa Mwenyezi Mungu au wanapokumbushwa juu ya maamrishi na makatazo ya Mwenyezi Mungu, nyoyo zao hunyenyekea na kufuata kama walivyokumbushwa. Hufanya hivyo kwa kukhofu ghadhabu za Mwenyezi Mungu na kutarajia radhi zake.

**(iii)Huongezeka Imani yao kwa Kusoma na kufuata Qur-an**

Wanaposoma aya za Mwenyezi Mungu huwazidishia imani kwa maana nyingine, waumini wa kweli hufuata mwongozo wa Allah (s.w) katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Hawako tayari kufanya jambo lolote kinyume na mwongozo wa Allah (s.w). Imani huongezeka kwa kutenda inavyostahiki kwa mujibu wa maelekezo ya Allah (s.w).

**(iv)Humtegemea Mwenyezi Mungu peke yake**

Hawamuogopi au kumtegemea yeyote kinyume na Mwenyezi Mungu. Wanamsimamo thabiti na hawayumbishwi na yeyote katika kutekeleza wajibu wao kwa Mola wao. Wanayakini kuwa aliyeenusuriwa na Allah (s.w) hakuna wa kumdhuru na aliyeandikiwa kupata dhara na Allah (s.w) hakuna wa kumnusuru.

### **(v)Husimamisha Swala**

Husimamisha swala katika maisha yao yote. Huswali swala zote za faradhi na swala za Sunnah kwa kadiri ya uwezo wao kwa khushui (unyenyekevu) huku wakizingatia masharti na nguzo za swala. Na kwahiyo hufikia lengo la swala kwa kutojijhusisha kabisa na mambo machafu na maovu. Pia husimama kidete kuondoa maovu na machafu yaliyopo katika jamii.

### **(vi)Husaidia wenye matatizo katika jamii**

Huwa wepesi wa kutoa msaada wa hali na mali kwa wanaadamu wenzao wanaohitajia msaada. Pia hutoa mali zao na nguvu zao kwa ajili ya kuendeleza Uislamu na kuusimamisha katika jamii.

### **(vii)Hupigania Dini ya Allah (s.w)**

Wanafanya jitihada za makusudi kwa kutumia mali zao na kujitoa muhanga nafsi zao ili kuhakikisha kuwa dini ya Allah inasimama katika jamii. Yaani wanajitahidi kwa jitihada zao zote ili kuzitafanya sharia za Allah (s.w) ziwe ndizo zinazotawala harakati zote za maisha ya jamii. Lengo lao kuu la maisha ni kuutawalisha Uislamu katika jamii.

## **2. Ar-Raad (13:19-26)**

Katika suratur-Raad, sifa za waumini zimewasilishwa kama ifuatavyo:

﴿ أَفَمَن يَعْلَمُ أَنَّمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ أَعْمَىٰ ۗ

إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿١٩﴾

*Je, anayejua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako ni haki (akayafuata, basi) ni kama aliyekipofu? Wenye akili ndio wanaozingatia." (13:19).*

﴿ الَّذِينَ يُوفُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَلَا يَنْقُضُونَ الْمِيثَاقَ ﴿٢٠﴾

(Nao ni hawa) ambao wametimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu wala hawavunji ahadi za (wanaadamu wenzao)." (13:20)

وَالَّذِينَ يَصِلُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِ أَنْ يُوصَلَ وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ وَيَخَافُونَ

سُوءَ الْحِسَابِ ﴿٢١﴾

"Na ambao huyaunga aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe na humuogopa Mola wao, na huiiogopa hisabu mbaya (itakayowapata wabaya huko Akhera). (13:21)

وَالَّذِينَ صَبَرُوا ابْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَنفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ

سِرًّا وَعَلاَنِيَةً وَيَدْرَءُونَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ أُولَئِكَ لَهُمْ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢٢﴾

"Na ambao husubiri (wakastahimilia wenziwao) kwa kutaka radhi ya Mola wao na wakasimamisha swala na wakatoa katika vile Tulivyowapa wakavitoa kwa siri na dhahiri na wakayaondoa maovu kwa mema. Hao ndio watakaopata malipo (mema) ya nyumba (ya Akhera)." (13:22)

جَنَدْتُمْ عَدُنِ يَدْخُلُونَهَا وَمَنْ صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ

وَالْمَلَائِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ ﴿٢٣﴾ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ

فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢٤﴾

Mabustani ya milele watayaingia wao (pamoja) na waliofanya mema miongoni mwa wazee wao na wake zao na kizazi chao. Na malaika watawaingilia katika kila mlango, (wanawaambia): Salaam alaykum (iwe amani juu yenu) kwa sababu mlisubiri. Basi ni mema yaliyoje matokeo ya nyumba (ya Akhera kwa wanaomcha Mwenyezi Mungu)." (13:23-24)

وَالَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ  
 اللَّهُ بِهِ أَنْ يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ أُولَٰئِكَ لَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ  
 سُوءُ الدَّارِ ﴿٧٥﴾

"Na wale waliovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu (na za wanaadamu wenzao) baada ya kuzifunga, na wakakata aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe, na wamefanya uharibifu katika nchi, hao ndio watakaopata laana, na watapata nyumba mbaya (ya akhera). (13:25)

اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ وَفَرِحُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَا الْحَيَاةُ  
 الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا مَتَنَعٌ ﴿٧٦﴾

"Mwenyezi Mungu hukunjua riziki kwa amtakaye na Huidhikisha (kwa Amtakaye). Na wamefurahia maisha ya dunia. Na uhai wa dunia kwa mkabala wa akhera si kitu ila ni starehe ndogo tu." (13:26)

### **Mafunzo:**

Mwanzo mwa aya hizi, Allah (s.w) anavuta fikra zetu kwa kutuuliza swali kuwa, "Je, yule aliyeyakinisha kuwa Qur-an ni kitabu cha Allah (s.w) alichoshushiwa Mtume Muhammad (s.a.w) na akakifuata kikamuongoza katika maisha ya **nuru** (furaha na amani) ni sawa na yule aliyekataa kuongozwa na Qur-an na kuishi maisha ya **giza** (upofu)? Baada ya swali hili Allah (s.w) anahitimisha kuwa wenye akili ndio wanaozingatia. Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa wenye akili ni **Waumini** wenye sifa zifuatazo:

### **(i)Wanaotimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu**

Ahadi kuu ambayo sote binaadamu tumeichukua mbele ya Mola wetu ni ile ya kumuabudu yeye pekee kama anavyotukumbusha:

وَإِذْ أَخَذَ رَبُّكَ مِن بَنِي آدَمَ مِن ظُهُورِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَأَشْهَدَهُمْ  
 عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ قَالُوا بَلَىٰ شَهِدْنَا أَن تَقُولُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ  
 إِنَّا كُنَّا عَنْ هَذَا غَافِلِينَ ﴿١٧٢﴾ أَوْ تَقُولُوا إِنَّمَا أَشْرَكَ آبَاؤُنَا مِن قَبْلُ  
 وَكُنَّا ذُرِّيَّةً مِّن بَعْدِهِمْ أَفَتُهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ الْمُبْطِلُونَ ﴿١٧٣﴾

*"Na (kumbuka) Mola wako Alipowaleta katika wanaadamu kutoka migongoni mwao kizazi chao, na akawashuhudisha juu ya nafsi zao (akawaambia): "Je, Mimi siye Mola wenu?" Wakasema: "Ndiye; tunashuhudia (kuwa wewe ndiye Mola wetu)." (Akawaambia Mwenyezi Mungu): Msije mkasema siku ya Kiyama kuwa sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo (hatujui); au mkasema: "Baba zetu ndio walioshirikisha zamani, nasi tulikuwa kizazi nyuma yao, basi utatuangamiza kwa sababu ya yale waliyoyafanya waovu?" (7:172-173)*

Wengi wa wafasiri wa Qur-an wanakubaliana kuwa ahadi hii ilichukuliwa na Adamu na mkewe Hawwah na roho zote za kizazi chao kabla hawajafika hapa duniani. Kwa hiyo kila nafsi ya mwanaadamu imechukua ahadi hii.

Ahadi hii kuu pia tunaikariri katika shahada mara kwa mara kwamba tutamuabudu Allah (s.w) peke yake kwa kufuata mwongozo aliotuletea kupitia Qur-an na Sunnah ya Mtume wake Muhammad (s.a.w). Kila umma uliikariri shahada hii kupitia kwa Mtume wao. Hivyo binaadamu atakapoacha kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo atakuwa amevunja ahadi hii kuu aliyoitoa mbele ya Mola wake.

**(ii) Wanaotimiza ahadi wanazozitoa kwa binaadamu wenzao**

Katika Qur-an tunahimizwa kutekeleza ahadi zote tunazozitoa kwa binaadamu wenzetu katika mambo ya kheri.

.....وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُولًا ﴿٣٤﴾

".....Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa." (17:34)

Waumini hawafungiki na ahadi zinazovunja ahadi kuu. Bali tunalazimika kuvunja ahadi yoyote ile inayotupelekea kumuasi Allah (s.w) na Mitume wake. Qur-an inatupa dira juu ya mashirikiano na binaadamu wenzetu katika Qur-an:

.....وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ

وَأَتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢٧﴾

"... Saidianeni katika wema na ucha-Mungu wala msisaidiane katika uovu na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu." (5:2)

### **(iii)Wanaounga yale aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe.**

Kuunga yale aliyoamuru Mwenyezi Mungu ni kuufuata Uislamu vilivyo katika kila kipengele cha maisha ikiwa ni pamoja na kuwafanyia wema wazazi, ndugu, jamaa, marafiki, jirani na binaadamu wote kwa ujumla. Kuwa na huruma kwa maskini, yatima na wote wenye shida. Kuwa mkarimu kwa ujumla na kuwa mstari wa mbele katika kujenga mahusiano mema na watu kwa kuzingatia kanuni na misingi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

### **(iv)Wanaomuogopa Mwenyezi Mungu na kuiogopa Hisabu mbaya huko akhera**

Kumuogopa Mwenyezi Mungu ni kuogopa kukasirikiwa na Mwenyezi Mungu. Kwani kila atakayekasirikiwa na Allah (s.w) atastahiki kupata adhabu yake ambayo ni kali isiyoyana na mfano wake:

فَيَوْمَئِذٍ لَا يُعَذِّبُ عَذَابَهُ أَحَدٌ ﴿٢٥﴾ وَلَا يُوثِقُ وَتَأْفَهُهُ أَحَدٌ ﴿٢٦﴾

"Basi siku hiyo hataadhibu yoyote namna ya kuadhibu kwake

*(Mwenyezi Mungu). Wala hatafunga yoyote jinsi ya Kufunga kwake (Mwenyezi Mungu)." (89:25-26)*

Kumuogopa Mwenyezi Mungu kiutendaji ni kujitahidi kufanya mema au yale yote aliyoamrisha Allah (s.w) kwa kutarajia kupata radhi yake na kujitahidi kuacha yale yote aliyoakataza kwa kuhofia kughadhibikiwa na yeye.

**(v)Wanaosubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao**

Wanaosubiri kwa ajili ya kupata radhi za Allah (s.w) ni wale:

- (a) Wanaofanya wema na kudumu mpaka mwisho wa maisha yao.
- (b) Wanaojiepusha na maovu na kudumu katika kujiweka mbali na maovu mpaka mwisho wa maisha yao.
- (c) Wanaostahimili juu ya misuko suko mbali mbali inayowafika katika maisha ya kila siku na wakawa ni wenye kumtegemea Allah (s.w).
- (d) Wanaostahamili maudhi wanayofanyiwa na bianaadamu wenzao katika mchakato wa maisha ya kila siku.
- (e) Wasiotoa maamuzi haraka haraka bila kuyapima vya kutosha katika kuendea mambo yao.
- (f) Wasiotarajia kupata haraka haraka matunda ya Harakati za kusimamaisha Uislamu katika jamii. Suala la kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii na kuuhami usiangushwe ni suala la kufanywa kwa uhai wote wa maisha ya muumini.

Allah (s.w) anawabashiria malipo makubwa wenye kusubiri kuwa:

أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٧﴾

*"Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na rehema; na ndio wenye kuongoka." (2:157)*

### **(vi)Wanaosimamisha Swala**

Kusimamisha swala ni kudumu katika kuswali swala zote kama alivyozitekeleza Mtume (s.w) kuanzia kwenye faradhi ya Qiyamullailiy (Tahajjud), swala tano za faradh na swala nyingine zote za Sunnah kwa kufuata barabara masharti yake, nguzo zake na kuwa na khushui wakati wa kutekeleza swala hizi. Kiutendaji swala itakuwa imesimama pale itakapomwezesha mwenye kuswali kuepukana na mambo maovu na machafu na kumwezesha kufanya jitihadi za makusudi za kuondoa maofu na machafu katika jamii.

### **(vii)Wanaotoa katika vile alivyowapa Mwenyezi Mungu**

Kila tulichonacho ikiwa ni pamoja na mali na neema mbali mbali zilizotuzunguka pamoja na vipawa mbali mbali tulivyonavyo, ikiwa nguvu, siha nzuri, elimu, fikra, n.k. ameturukuzu Allah (s.w). Muumini anatakiwa avitumie vitu hivi kwa ajili ya kujinufaisha yeye na wale wanaomtegemea kwa mahitaji ya lazima na ziada aitoa kwa ajili ya kusimamisha dini ya Allah (s.w) na kuwasaidia binaadamu wenzake wanaohitajia msaada kwa kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s.w).

### **(viii)Wanaoondoa maovu kwa wema**

Kuondoa maovu kwa wema kuna maana mbili;

(a)Baada ya mtu kufanya maovu, hurejea haraka haraka kwa Mola wake kwa kuleta toba ya kweli; kisha kuzidisha kufanya wema kwa kuleta dhikri nyingi, kuzidisha kufunga, kutoa sadaqa, n.k.:

﴿ وَمَنْ تَابَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَإِنَّهُ يَتُوبُ إِلَى اللَّهِ مَتَابًا ﴾

*"Na aliyetubia na kufanya wema, basi kwa hakika yeye anatumbea kweli kweli kwa Mwenyezi Mungu." (25:71)*

(b)Baada ya mtu kufanyiwa uovu au kuudhiwa na mtu



mwingine, huzuia hasira na kuwa mwepesi wa kumpa aliye mnyima, kumsamehe aliyemkosea, kumchangamkia aliyemnunia, kumrudishia maneno mazuri aliyemtukana, n.k. Hekima ya kujipamba na sifa hii inabainishwa katika aya ifuatayo:

وَلَا تَسْتَوِي الْحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ادْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ  
فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿٢٤﴾

*"Mambo mabaya na mazuri hayawi sawa. Ondosha ubaya unaofanyiwa kwa wema, tahamaki yule ambaye baina yako na baina yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia uchungu". (41:34)*

Mwisho, baada ya kufahamishwa hizi sifa za waumini zilizo rodheshwa, tunafahamishwa malipo wata kayostahiki kuyapata katika nyumba ya Akhera ambayo ni kuishi Peponi milele pamoja na wazee wao na watoto wao ambao nao walijipamba na sifa hizi za waumini.

### 3. Al-Mu'uminun (23:1-11)

Pia sifa za Waumini zinabainishwa katika Suratul-Muuminun katika aya zifuatazo:

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ ﴿٢﴾

*Hakika wamefuzu waumini ambao katika swala zao huwa wanyenyekevu. (23:1-2)*

وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِلرَّكَّوَةِ فَاعِلُونَ ﴿٤﴾

*Na ambao hujiepusha na Lagh-wi (mambo ya upuuzi). Na ambao (nguzo ya) Zaka wanaitekeleza. (23:3-4)*

وَالَّذِينَ هُمْ لِأُزْوَاجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٥﴾ إِلَّا عَلَىٰ أَرْوَاحِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ

أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٦﴾

*Na ambao tupu zao wanazihifadhi isipokuwa kwa wake zao au kwa (wanawake) wale iliyomiliki mikono yao ya kuume. Basi hao ndio wasiolaumiwa. (23:5-6)*

فَمَنْ أَبْتَغَىٰ وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعَادُونَ ﴿٧﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمْتِنَتِهِمْ

*Lakini anayetaka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka. Na ambao amana zao na ahadi zao wanaziangalia. (23:7-8).*

وَالَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَوَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٨﴾ أُولَٰئِكَ هُمُ الْوَارِثُونَ ﴿١٠﴾

*Na ambao swala zao wanazihifadhi. Hao ndio warithi. (23:9-10)*

الَّذِينَ يَرِثُونَ الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١١﴾

*Ambao watarithi Firdaus (Pepo ya daraja ya juu wakae humo milele. (23:11)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa, waumini wa kweli waliofuzu na watakaostahiki kupata Pepo ya Firdaus, (ya daraja ya juu kabisa) ni wale wanaojipamba na sifa zifuatazo:

### **(i)Wenye Khushui katika Swala**

Waumini wa kweli waliofuzu huwa na khushui (unyenyekavu) katika swala. Yaani huswali kwa kutulizana kimwili, kimoyo na kifikra, huku wakizingatia yale wayasemayo mbele ya Mola wao wakiwa na yakini kuwa anawaona na anawasikia.

### **(ii)Wenye Kuhifadhi Swala**

Waumini wa kweli waliofuzu huhifadhi swala kwa kutekeleza kwa ukamilifu sharti zote za swala, nguzo zote za swala na huswali kama alivyoswali Mtume (s.a.w) na hudumu na swala katika maisha yao yote. (Qur-an 70:23)

### **Zingatia:**

Swala husimama kwa kuhifadhiwa na kuswaliwa kwa khushui na kudumu na swala katika maisha yote.

### **(iii)Wenye kuepuka Lagh-wi**

Waumini wa kweli waliofuzu hujiepusha na Lagh-wi. Laghwi ni mambo ya upuuzi yanayomsahaulisha mtu kumkumbuka Mola wake, yanayosababisha ugomvi au bughudha baina ya watu na yanayomsahaulisha mtu kuswali (Qur-an 5:91). Mahala ambapo Allah (s.w) hakumbukwi, shetani huchukua nafasi. michezo yote ni lagh-wi isipokuwa ile tu inayochezwa kwa kuchunga mipaka yote ya Allah (s.w) kwa lengo la kukuza ukakamavu na siha ili kuwa imara katika kusimamisha Uislamu katika jamii.

### **(iv)Hutoa Zakat na Sadakat**

Waumini wa kweli waliofuzu hutoa Zakati wakiwa na mali na hutoa misaada na huduma waziwezazo kwa wanaadamu wenziwe kwa kadiri ya haja ilivyojitokeza. Asiyejali binaadamu wenzake, huku ana uwezo si Muumini. Rejea Qur-an (107:1-3).

### **(v)Wenye kujiepusha na Zinaa na Tabia za Kizinifu.**

Waumini wa kweli waliofuzu hujihifadhi na zinaa au hujiepusha kufanya jimai nje ya mipaka aliyoiweka Allah (s.w). Hatua ya kwanza ya kujilinda na zinaa ni kujiepusha na vishawishi vyote vinavyokurubisha watu kwenye zinaa. Muumini wa kweli hutekeleza pasina kusita ile amri ya Allah (s.w) ya katazo kuwa:

وَلَا تَقْرَبُوا الزَّيْنَىٰ إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

*Wala usiikaribie zinaa; kwa hakika huo ni uchafu na ni njia mbaya kabisa. (17:32)*

### **(vi)Huwa Muaminifu**

Waumini wa kweli waliofuzu huchunga amana. Hutunza amana aliyopewa na kuirejesha au kuitumia kwa mujibu wa maelekezo ya mwenyewe. Amana kuu aliyopewa mwanaadamu na Mola wake ni kule kufadhilishwa kwake kuliko viumbe vingine vyote (Qur-an (17:70),(95:4) ili asimamishe Ukhalifa (utawala wa

Allah) katika ardhi kama tunavyokumbushwa katika Qur-an:

إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَنْ يَحْمِلْنَهَا  
وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا وَحَمَلَهَا الْإِنْسَانُ إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا ﴿٧٢﴾

*"Kwa yakini Sisi tulidhihirisha amana kwa mbingu, ardhi na milima, vikakataa kuichukua na vikaiogopa, lakini mwanaadamu aliichukua. Bila shaka yeye ni dhalimu mkubwa, mjinga sana." (33:72)*

### **(vii)Wenye Kutekeleza Ahadi**

Hutekeleza ahadi zao wanapoahidiana na wanaadamu wenziwao maadamu ni katika mipaka ya Allah (s.w). Ahadi kubwa wanayotoa Waislamu mbele ya Allah (s.w) ni **Shahada**; pale wanapoahidi kuwa hawatamshirikisha Allah (s.w) na chochote na kwamba wataishi maisha yao yote kwa kufuata mwongozo wa Allah (s.w) kupitia kwa Mtume wake, Muhammad (s.a.w).

### **4.Al-Furqaan (25:64-76)**

Katika Suratul-Furqaan sifa za Waumini zinabainishwa tena kama ifuatavyo:

وَعِبَادُ الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ  
الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا ﴿٦٤﴾

*"Na waja wa Rahmaan; Ni wale wanaokwenda ulimwenguni kwa unyenyekevu; na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu (maneno ya) salama. (25:63)*

وَالَّذِينَ يَبِيتُونَ لِرَبِّهِمْ سُجَّدًا وَقِيَامًا ﴿٦٥﴾ وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا اصْرِفْ  
عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿٦٥﴾

*Na wale wanaopitisha baadhi ya saa za usiku kwa ajili ya Mola wao kwa kusujudu na kusimama. na wale wanaosema:*

"Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahannam, bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea. (25:64-65)

إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٦٦﴾ وَالَّذِينَ إِذَا أَنْفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا  
وَلَمْ يَقْتُرُوا وَكَانَ بَيْنَ ذَلِكَ قَوَامًا ﴿٦٧﴾

Hakika hiyo (Jahannamu) ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa". Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanaokuwa katikati baina ya hayo. (25:66-67)

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ  
إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا يَزْنُونَ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَامًا ﴿٦٨﴾

Na wale wasiomuomba Mungu mwingine pamoja na Allah, wala hawaiui nafsi aliyoiharamisha Allah ila kwa haki, wala hawazini; na atakayefanya hayo atapata madhara (papa hapa ulimwenguni). (25:68).

يُضَاعَفْ لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَيَخْلُدْ فِيهِ مُهَانًا ﴿٦٩﴾

Na atazidishiwa adhabu siku ya Kiyama na atakaa humo kwa kufedheheka milele. (25:69)

إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَالِحًا فَأُولَئِكَ يُبَدِّلُ  
اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٧٠﴾

Ila yule atakayetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri, basi hao ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa kurehemu. (25:70)

وَمَنْ تَابَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَإِنَّهُ يَتُوبُ إِلَى اللَّهِ مَتَابًا ﴿٧١﴾

Na aliyetubia na kufanya wema, basi kwa hakika yeye anatubu kweli kweli kwa Mwenyezi Mungu. (25:71)

وَالَّذِينَ لَا يَشْهَدُونَ الزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا ﴿٧٣﴾

*Na wale ambao hawashuhudii shahada za uwongo, na wanapopita penye upuuzi, hupita kwa hishima (yao). (25:72)*

وَالَّذِينَ إِذَا دُكِرُوا بِعَائِدَتِ رَبِّهِمْ لَمْ يَخِرُّوا عَلَيْهَا صُمًّا وَعُمْيَانًا ﴿٧٤﴾

*Na wale ambao wanapokumbushwa aya za Mola wao hawaziangukii kwa uziwi na upofu. (25:73).*

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا

لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا ﴿٧٥﴾

*Na wale wanaosema: "Mola wetu! Tupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho (yetu) (nyoyo zetu), na Utujaalie kuwa waongozi kwa wamchao (Mungu). (25:74)*

أَوْ لَكَ يَجْزُونَ الْعُرْفَةَ بِمَا صَبَرُوا وَيُلَقَّوْنَ فِيهَا تَحِيَّةً وَسَلَامًا ﴿٧٥﴾

*Hao ndio watakaolipwa ghorofa (za Peponi) kwa kuwa walisubiri, na watakuta humo hishima na amani. (25:75)*

خَالِدِينَ فِيهَا حَسَنَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٧٦﴾

*Wakae humo milele; kituo kizuri na mahali pazuri (kabisa pa kukaa). (25:76)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa sifa za Waumini ambao hapa wameitwa "**Waja wa Rahman**" ni pamoja na:

### **(i)Kuishi na watu kwa Wema**

Waumini wa kweli huishi na watu kwa wema kwa kuwathamini na kuwaheshimu; kujizuia na kuwafanyia watu kibri, kujizuia na kujikweza na kujitukuza mbele ya wengine, kujizuia na kuwadhalilisha watu na kuwavunja heshima. Kutembea katika ardhi kwa unyenyekevu ni pamoja na kuchungua barabara mipaka ya Allah(s.w) na mtume wake(s.a.w)

## **(ii)Huepukana ugomvi na Mabishano**

Waumini wa kweli huepuka kabisa tabia ya ugomvi na mabishano. Waumini hufahamu fika kuwa kwenye ugomvi na mabishano shetani huwepo na huchochea faraka baina ya ndugu. Namna ya kuepukana na wagomvi kwa salama inaelekezwa katika Qur-an (41:36)

## **(iii)Hudumu katika Kuswali Tahajjud**

Kuamka usiku na kuswali swala ya "Tahajjud" (kisimamo cha usiku - Qiyamullayl) kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w) na Rehema zake. Swala hii huswaliwa usiku wa manane hususan katika theluthi ya mwisho ya usiku inayokaribiana na Al-fajiri. Swala hii ni lazima kwa kila Muislamu mwenye azima ya kuulingania Uislamu na kuusimamisha katika jamii. Ukirejea Historia ya kushuka Qur-an, amri ya kwanza aliyopewa Mtume (s.a.w) kwa niaba ya umma wake ni Kusoma kwa ajili ya Allah (s.w) - Qur-an (96:1-5); amri ya pili ikiwa swala ya Tahajjud (Qur-an 73:1-5) ili iwe maandalizi ya kukabili shughuli nzito ya kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii. Msisitizo wa Qiyamullayl tunaupata vizuri katika aya ifuatayo:

أَمَّنْهُوَ قَدِيتْ عَانَءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا يَحْذَرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُو رَحْمَةَ رَبِّهِ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٩﴾

*"Je, afanyaye ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa akhera na kutarajia rehema ya Mola wake (ni sawa na asiyefanya hivyo)? Sema: "Je wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?" Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu." (39:9)*

## **(iv)Huogopa adhabu ya Allah (s.w)**

Waumini wa kweli huogopa adhabu ya Allah (s.w) aliyowaandalia watu waovu huko akhera kwa kujitahidi kutenda

mema na kujiepisha na maovu na kila mara kuomba:

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا اصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿١٥﴾ إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿١٦﴾

"Nawale wanaosema: Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahannam, bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea. Hakika hiyo (Jahannamu) ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa." (25:65-66)

### (v) Hutumia Neema kwa Insafu

Waumini wa kweli hutumia neema walizopewa na Allah (s.w) kwa insafu. Hawafanyi ubadhirifu au israfu wa neema kama vile kutumia vibaya mali, wakati, vipaji na ujuzi. Waumini daima huzingatia kuwa Allah (s.w) hawapendi waja wanaofuja neema walizotunukiwa na Allah (s.w). Wasiotumia neema kwa insafu, ni wafuasi wa shetani.

وَعَاتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمَسْكِينِ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلَا تُبَذِّرْ تَبْذِيرًا ﴿٢٦﴾

"Na wape jamaa wa karibu haki zao, na mayatima (vile vile) na masikini, wala usifanye ubadhirifu." (17:26)

إِنَّ الْمُبَذِّرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيْطَانِ ط وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِرَبِّهِ كَفُورًا

Hakika wafanyao ubadhirifu ni marafiki wa shetani, na shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake. (17:27)

### (vi) Hawamshirikishi Allah (s.w)

Waumini wa kweli hawamshirikishi Allah (s.w). Hujiepisha na aina zote za shirk. Shirk katika dhati, shirk katika sifa, shirk katika hukumu na shirk katika mamlaka ya Allah (s.w). Kufanya shirk ni dhambi kubwa ya daraja la kwanza. Qur-an inaonya na kutahadharisha kuwa:



إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ وَمَنْ يُشْرِكْ

بِاللَّهِ فَقَدْ أَفْتَرَىٰ إِثْمًا عَظِيمًا ﴿٤٨﴾

*Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi (dhambi ya) kushirikishwa na kitu na husamehe yasiyokuwa haya kwa amtakaye. Na anayemshirikisha Allah bila shaka amebuni dhambi kubwa. (4:48).*

Pia rejea Qur-an (4:116) na (39:65)

### **(vii)Hulinda na kutetea haki ya Uhai wa Nafsi**

Waumini wa kweli hulinda na kutetea haki ya uhai wa kila nafsi yenye haki ya kuishi. Hivyo, hujitahidi kujiepusha na ushiriki wa kusababisha au kufanya mauwaji ya nafsi ambayo kwa mujibu wa mwongozo wa Allah (s.w) hustahiki kuishi. Ulinzi wa utetezi huu wa haki ya uhai wa nafsi unatokana na mwongozo wa Allah katika Qur-an kuwa:

مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ كَتَبْنَا عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُ مَن قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ

فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ

جَمِيعًا وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ إِنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ بَعَدَ ذَلِكَ فِي

الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ ﴿٣٢﴾

*Mwenye kuiwa nafsi pasina nafsi hiyo iliyouliwa kuuwa au kufanya fisadi katika ardhi, itakuwa kana kwamba ameuwa watu wote. Na atakayelinda nafsi hiyo, atakuwa kana kwamba amelinda uhai wa watu wote. (5:32)*

### **(viii)Hawafanyi Uzinzi**

Waumini wa kweli hawaikaribii zinaa wala kufanya uzinifu. Na zaidi hawashawishi wala kushiriki kwa namna yoyote ile katika

mambo yanayosababisha zinaa kufanyika.

وَلَا تَقْرَبُوا الزِّنَىٰ إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

*"Wala usikaribie zinaa. Hakika hiyo ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kabisa)." (17:32)*

### **(ix)Husema Kweli daima**

Waumini wa kweli husema kweli daima. Hawatowi ushahidi wa uongo au kutetea batili. Wanapowajibika kutoa ushahidi juu ya jambo, husema ukweli hata kama ni dhidi ya nafsi zao wenyewe au watu wao wa karibu. (Rejea Qur-an 4:135, 5:8)

### **(x)Hawavutiwi na mambo ya Kipuuzi**

Waumini wa kweli ni wale ambao hawavutiwi na mambo ya kipuuzi ambayo wafuasi wa Ibilisi huyatumia katika kuwavutia watu kwa lengo la kuwapumbaza na kuwateka akili zao. Muumini huwa hana muda wa kupoteza au fursa ya kuikabidhi akili yake kwa twaghuti aichezee. Hivyo, kwenye mambo ya kipuuzi waumini hupita haraka kwa heshima zao, na ikibidi kuweka jambo m-badala lenye maana na manufaa kwa jamii.

### **(xi)Humwitikia Allah (s.w) anapowaita**

Waumini wa kweli humwitikia Allah (s.w) anapowaita kwa makatazo na maamrisha yake katika Qur-an. Hivyo hutii kwa unyenyekevu maagizo ya Allah (s.w) kila wanapokumbushwa kwa kusomewa au Kusoma wenyewe aya za Kitabu cha Allah (s.w) na Allah (s.w) ananadi katika Qur-an kuwa:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ

فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾

*Na waja wangu wanapokuuliza kuhusu mimi, basi (waambie) hakika Mimi nipo karibu najibu maombi ya mwombaji pindi anaponiomba. Basi na waniitikie na waniamini Mimi ili wapate kuongoka. (2:186)*

## (xii)Hujenga Familia za Kiislamu

Waumini hujitahidi kujenga familia za Kiislamu kwa kumuongoza mke na kuwalea watoto na wale wote waliochini ya mamlaka yake katika mipaka ya Ucha-Mungu kwa kuwaamrisha kutenda mema na kuwakataza maovu. Pamoja na jitihada hiyo huomba msaada wa Allah (s.w) kwa kuleta dua ifuatayo:

رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَرْوَاجِنَا وَذُرِّيَّتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا

لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا ﴿٧٤﴾

“.....Mola wetu! Tupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho (yetu) (nyoyo zetu), na Utujaalie kuwa waongozi kwa wamchao (Mungu). (25:74)

Kwa ujumla waumini wa kweli ni wale wanaojipamba na tabia njema kama iliyoelekezwa katika Qur-an na Sunnah na hao ndio watakao stahili kuingia peponi.

## (5)As-Sajdah (32:10-22)

وَقَالُوا أَإِذَا ضَلَلْنَا فِي الْأَرْضِ أَأَنَّا لَفِي خَلْقٍ جَدِيدٍ بَلْ هُمْ

بِلِقَاءِ رَبِّهِمْ كَافِرُونَ ﴿١٠﴾ قُلْ يَتَوَفَّنَكُم مَّلَكُ الْمَوْتِ الَّذِي وُكِّلَ

بِكُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١١﴾

*Nao husema (kwa maskhara): "Je, tutakapotea katika ardhi, (tukageuka mchanga) ndio tutarudishwa katika umbo jipya?" (Ndio).Bali wao hawakiri kwamba watakutana na Mola wao! Sema: Atakufisheni Malaika wa mauti aliyewakilishwa kwenu, kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu." (32:10-11)*

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا رُءُوسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ  
رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا إِنَّا مُوقِنُونَ ﴿١٣﴾ وَلَوْ  
شِئْنَا لَآتَيْنَا كُلَّ نَفْسٍ هَدْيَهَا وَلَكِنْ حَقَّ الْقَوْلُ مِنِّي لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ

مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١٣﴾

*Na ungaliwaona waovu wakiinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao, (na kusema) "Mola wetu! Tumekwisha kuona na tumekwisha kusikia, basi turudishe, tutafanya vitendo vizuri; hakika (sasa) tumeyakinisha." Na Tungalitaka Tungempa kila mtu uwongofu wake, lakini imihakikika kauli iliyotoka Kwangu: Kwa yakini Nitaijaza Jahannamu kwa wote hawa; majini na watu (ambao ni wabaya).(32:12-13)*

فَذُوقُوا بِمَا نَسِيتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَذَا إِنَّا نَسِينَاكُمْ وَذُوقُوا عَذَابَ  
الْحُلْدِ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾ إِنَّمَا يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا الَّذِينَ إِذَا ذُكِرُوا بِهَا  
خَرُّوا سُجَّدًا وَسَبَّحُوا بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ﴿١٥﴾

*Basi ionjeni (adhabu) kwa sababu ya kusahau makutano ya siku yenu hii; na Sisi Tutakusahauni (Motoni), na onjeni adhabu idumuyo kwa yale mliyokuwa mkiyatenda. Hakika wanaoziamini aya Zetu ni wale tu ambao wanapokumbushwa huanguka kusujudu na humtukuzwa Mola wao kwa sifa Zake, nao hawatakabari.(32:14-15)*

تَتَجَافَىٰ جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا وَطَمَعًا  
وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿١٦﴾ فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّا أُخْفِيَ لَهُم مِّن  
قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

*Huinua mbavu zao kutoka vitandani wakati wa usiku ili*

*kumuabudu Mola wao kwa kuogopa Moto na kutaraji Pepo; na hutoa (zaka na sadaka) katika yale tuliyowapa. Nafsi yoyote haijui yaliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho (huko Peponi): ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya.(32:16-17)*

أَفَمَنْ كَانَ مُؤْمِنًا كَمَنْ كَانَ فَاسِقًا لَا يَسْتَوِينَ ﴿١٦﴾ أَمْ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ جَنَّاتُ الْمَأْوَىٰ نُزُلًا بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

*Je! Mwislamu kamili atakuwa sawa na yule aliye fasiki? Hawawi sawa. Wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri watakuwa na Mabustani ya makazi mazuri. Ni andao lao kwa yale waliyokuwa wakiyatenda.(32:18-19)*

وَأَمْ الَّذِينَ فَسَقُوا فَمَأْوَاهُمُ النَّارُ كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا أُعِيدُوا فِيهَا وَقِيلَ لَهُمْ ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنْتُمْ بِهِء تَكْذِبُونَ

*Na wale waliofanya uovu, makazi yao ni Motoni, watakapotaka kutoka humo watarudishwa mumo humo na wataambiwa: "Onjeni tu adhabu ya Moto ambayo mlikuwa mkiikadhibisha." (32:20)*

## **Mafunzo**

Mafunzo tuyapatayo kutokana na aya hizi ni kuwa:

**Kwanza**, makafiri kwa kuzugwa na maisha ya dunia huacha kutumia akili zao na vipawa vyao vya tafakuri walivyotunukiwa na Allah (s.w) na kujitia upofu, uziwi na ububu kuwa dunia hii haina muumba na kuwa binaadamu hatarejeshwa kwa Muumba huyo na kuulizwa juu ya matendo yake yote aliyoyafanya katika mgongo huu wa ardhi. Hivyo kwa dhana yao hii makafiri huishi kwa jeuri katika ardhi na kufisidi watakavyo. Ni kutokana na tabia yao hii Allah (s.w) amewaandalia adhabu kali ya moto kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ الْجِنِّ وَالإِنسِ لَهُمْ قُلُوبٌ لَا يَفْقَهُونَ بِهَا  
 وَلَهُمْ أَعْيُنٌ لَا يُبْصِرُونَ بِهَا وَلَهُمْ آذَانٌ لَا يَسْمَعُونَ بِهَا أُولَئِكَ كَالْأَنْعَامِ  
 بَلَّغْنَا لَهُمُ آيَاتِنَا وَلَٰكِن لَّا يُفْقَهُونَ ﴿١٧٩﴾

*"Na bila shaka tumewaumbia moto wa Jahannamu wengi katika majini na wanaadamu (kwa sababu hii). Nyoyo wanazo, lakini hawafahamu kwazo (hawataki kufahamu kwazo) na macho wanayo, lakini hawaoni kwayo na masikio wanayo lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walioghafilika." (7:179)*

**Pili**, Makafiri pamoja na kukanusha kwao kuwepo kwa Allah (s.w) na Siku ya Mwisho, watakapofishwa na kurejeshwa mbele ya Mola wao, ukweli utadhihiri na uongo utajitenga na watayakinisha kuwa wao walikuwa waovu. Hivyo watajuta juu ya uovu wao na watamuomba Mola wao, awarudishe tena duniani ili wawe waumini watenda mema. Haya ni majuto yasiyo na manufaa, kwani walitahadharishwa juu ya maisha ya Akhera lakini walikanusha na kufanya maskhara:

وَقَالُوا أَإِذَا ضَلَلْنَا فِي الْأَرْضِ أَإِنَّا لَفِي خَلْقٍ جَدِيدٍ بَلْ هُمْ  
 بِلِقَاءِ رَبِّهِمْ كَافِرُونَ ﴿١٨٠﴾

*"Na husema:Je, tutakapopotea katika ardhi (tukageuka mchanga) ndio tutarudishwa katika umbo jipya? (Ndio) Bali wao hawakiri kwamba watakutana na mola wao!" (32:10).*

**Tatu**, Allah (s.w) hatakuwa anawadhulumu makafiri atakapowaadhibu, bali watakuwa wamejidhulumu wenyewe nafsi zao. Allah (s.w) aliwaumba na kuwapa akili na uhuru wa kuchagua maisha yakuwa Muumini au Kafiri baada ya kufahamishwa wazi kuwa waumini wataishi maisha ya **nuru** hapa duniani na kulipwa neema za Peponi huko akhera na kuwa makafiri wataishi maisha

ya **gizani** hapa duniani na kustahiki adhabu kali ya motoni huko akhera kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ فَمِنْكُمْ كَافِرٌ وَمِنْكُمْ مُؤْمِنٌ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

"Yeye (Allah) ndiye aliyekuumbeni (nyote). Na kuna wengine wenu ni makafiri na wengine wenu ni waumini. Na Allah anayaona (yote) mnayoyafanya." (64:2)

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ آمَنُوا يُخْرِجُهُمْ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُمْ مِنَ النُّورِ إِلَى

الظُّلُمَاتِ أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

"Allah ni mlinzi (kiongozi) wa wale walioamini. Huwatoa katika **giza** na kuwaingiza katika **nuru**. Lakini waliokufuru walinzi (viongozi) wao ni matwaghuti (mashetani). Huwatoa katika **nuru** na kuwaingiza katika **giza**. Hao ndio watu wa motoni humo watakaa milele." (2:257)

**Nne**, Tofauti na makafiri ambao hungojea kujuta kwa makosa yao pale watakapoona adhabu ya Allah(s.w) huko akhera, waumini siku zote na nyakati zote katika maisha yao hapa duniani huhofia ghadhabu za Allah (s.w) na kujitahidi kumuelekea Mola wao katika sura hii sifa za waumini zimeorodheshwa kama ifuatavyo:

- (i) Wanapokumbushwa kwa aya za Allah(s.w) hunyenyekea kwa kusujudu. Kiutendaji inamaana kuwa waumini wanapopewa maagizo na Mola wao humtii mara moja na kuingia katika utendaji.
- (ii) Humtukuza Mola wao kwa kutaja sifa zake (tukufu) na hawatakabari.
- (iii) Huinua mbavu zao kutoka vitandani wakati wa usiku (wa manane) ili kumuabudu Mola wao kwa kuswali (Qiyamullayl) kwa kuogopa moto na kutaraji pepo.

(iv) Hutoa katika yale aliyo waruzuku Mola wao kwa ajili ya kusimamisha Uislamu na kuwahurumia wanaadamu wenziwao.

Pamoja na waumini kufanya haya na mema mengineyo, daima huomba dua ifuatayo:

رَبَّنَا أَصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ إِنَّ

عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿١٥﴾ إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿١٦﴾

".....Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahannamu, bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea. Hakika hiyo (Jahannamu) nikituo kibaya na mahali (pabaya kabisa)pakukaa" (25:65-66)

**Tano**, Waumini wa kweli (Waislamu kamili) ni bora kuliko watu wengine wote kwa sababu ndio pekee kwa kufuata mwongozo wa Allah (s.w) wanaoweza kuiongoza jamii kwa haki na uadilifu na kuleta furaha na amani ya kweli katika jamii..

**Sita**, Dhalimu mkubwa kuliko madhalimu wote ni yule anayekumbushwa aya za Mola wake kisha akazikataa. Kukataa aya za Allah (s.w) si lazima utamke kuwa umezikataa bali kutozitekeleza kwa makusudi ndio hasa kuzikataa. Hivyo, wale tunaajiita waumini lakini tunaendesha maisha yetu kinyume na aya za Allah (s.w), tujue kuwa tu madhalimu wakubwa kama wale walioikanusha Qur-an kwa uwazi na Mtume (s.a.w) akalalamika juu yao:

وَقَالَ الرَّسُولُ يَا رَبِّ إِنَّ قَوْمِي اتَّخَذُوا هَذَا الْقُرْآنَ مَهْجُورًا

Na Mtume alikuwa akisema: "Ee, Mola wangu! Hakika watu wangu wameifanya Qur-an hii kuwa ni kitu kilichohamwa.(25:30)



Kuihama Qur-an ni kutoisoma kwa mazingatio na kutoiingiza katika utendaji wa maisha ya kila siku.

**(6)Al-Ahzab (33:35-36)**

إِنَّ الْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَالْقَانِتِينَ وَالْقَانِتَاتِ  
 وَالصَّادِقِينَ وَالصَّادِقَاتِ وَالصَّابِرِينَ وَالصَّابِرَاتِ وَالْخَاشِعِينَ  
 وَالْخَاشِعَاتِ وَالْمُتَصَدِّقِينَ وَالْمُتَصَدِّقَاتِ وَالصَّالِحِينَ وَالصَّالِحَاتِ  
 وَالْحَافِظِينَ فُرُوجَهُمْ وَالْحَافِظَاتِ وَالذَّاكِرِينَ اللَّهَ كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ  
 أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٥﴾

*Bila shaka wanaume wenye kufuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanawake wanaozifuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanaume wanaoamini vizuri nguzo za Imani, na wanawake wanaoamini vizuri nguzo za Imani, na wanaume wanaotii, na wanawake wanaotii, na wanaume wasemao kweli, na wanawake wasemao kweli, na wanaume wanaosubiri, na wanawake wanaosubiri, na wanaume wanaonyenyekea na wanawake wanaonyenyekea, na wanaume wanaotoa (Zaka na) sadaka, na wanawake wanaotoa (Zaka na) sadaka, na wanaume wanaofunga, na wanawake wanaofunga, na wanaume wanaojihifadhi tupu zao, na wanawake wanaojihifadhi, na wanaume wanaomtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi, na wanawake wanaomtaja Mwenyezi Mungu (kwa wingi) Mwenyezi Mungu amewaandalia msamaha na ujira mkubwa.(33:35)*

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا لِمُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ  
 الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

*Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke*

*aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotofu (upotevu) ulio wazi (kabisa). (33:36).*

## **Mafunzo**

Kutokana na aya hizi tunapata mafunzo yafuatayo:

**Kwanza**, Muumini wa kweli ni yule anayejitahidi kwa kadiri ya uwezo wake kutekeleza yale yote yaliyoorodheshwa katika aya (33:35) na kutekeleza maamrisha mengine yote ya Allah (s.w) na Mtume wake pamoja na kuacha makatazo yote ya Allah (s.w) na Mtume wake. Kwa muhtasari sifa za waumini zilizoorodheshwa katika aya hizi ni hizi zifuatazo.

- (i) Wenye kutoa shahada ya kweli kwa kutekeleza vilivyo maamrisha yote ya Allah(s.w) na kuacha makatazo yake yote.
- (ii) Wenye kuziingiza katika matendo nguzo zote za imani.
- (iii) Wenye kumtii Allah (s.w) na Mtume wake ipasavyo katika kukiendea kila kipengele cha maisha na kuwatii wenye mamlaka juu yao kwa mujibu ya maelekezo ya Allah (s.w) na Mtume wake.
- (iv) Wenye kusema na kusimamia ukweli
- (v) Wenye kujipinda katika kufanya subira katika kuendesha maisha yao ya kila siku na katika kusimamisha Uislamu katika jamii.
- (vi) Wenye kujiepusha na kibri, majivuno, majigambo, n.k. katika kuhusuhubiana na watu katika mchakato wa maisha ya kila siku.
- (vii) Wenye kutoa yale Allah(s.w) aliyowaruzuku kwa ajili ya kuwahurumia wenye kuhitajia na pia kwa ajili ya kuundeleva Uislamu na kuusimamisha katika jamii.
- (viii) Wenye kuleta mara kwa mara funga za sunnah baada ya kuikamilisha funga ya Ramadhani na funga za kafara kwa yule aliyelazimika kwazo. Yaani wenye kuwa katika swaumu angalu siku tatu kwa kila mwezi.
- (ix) Wanaojihifadhi na zinaa na kujiepusha na vishawishi vyote vya zinaa.

(x) Wenye kumtaja na kumbumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi.

**Pili**, katika Uislamu waumini wanaume na waumini wanawake wana haki sawa mbele ya Allah (s.w). anayeheshimiwa zaidi mbele ya Allah ni yule aliye mchaji zaidi kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ  
لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقَنُّكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

*"Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja, Adamu) na (yule yule) mwanamke (mmoja, Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu). Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye Allah zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Allah ni mjuzi mwenye habari (za mambo yote)." (49:13)*

### (7) Ashu-Shuura (42:36 - 43)

فَمَا أوتيتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَمَتَّعِ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ  
لِلَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٣٦﴾

*"Basi vyote hivi mlivyopewa ni starehe ya maisha ya dunia tu, lakini kilicho kwa Mwenyezi Mungu ni bora na cha kudumu (milele). Watatahiki wale walioamini na wakawa wanamtegemea Mola wao." (42:36)*

وَالَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَبِيرَ الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ وَإِذَا مَا غَضِبُوا  
هُمْ يَغْفِرُونَ ﴿٣٧﴾

*"Na wale wanaojiepusha na madhambi makubwa na mambo mabaya na ambao wanapokasirika husamehe". (42:37)*

وَالَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَمْرُهُمْ شُورَى بَيْنَهُمْ

وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٣٨﴾

*Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa kila amri zake) na wakasimamisha swala na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku." (42:38)*

وَالَّذِينَ إِذَا أَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُونَ ﴿٣٩﴾

*"Na wale ambao jeuri inapowafikia huzitetea nafsi zao." (42:39)*

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِثْلُهَا فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ لَا

يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿٤٠﴾ وَلَمَنْ آتَصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهِ فَأُولَئِكَ مَا عَلَيْهِمْ مِنْ

سَبِيلٍ ﴿٤١﴾ إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ

بِغَيْرِ الْحَقِّ أُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٢﴾ وَلَمَنْ صَبَرَ وَغَفَرَ إِنَّ

ذَلِكَ لَمِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿٤٣﴾

*"Na malipo ya ubaya ni ubaya uliosawa na (ubaya) huo; lakini anayesamehe na kusuluhisha ugomvi; ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu; bila shaka yeye hawapendi madhalimu. Na wanaolipiza kisasi baada ya kudhulumiwa, hao hakuna njia ya kulaumiwa. Bali lawama iko juu ya wale waliodhulumu na wakawafanyia jeuri katika ardhi pasipo haki; hao ndio watakaopata adhabu iumizayo. Na anayesubiri na kusameme (atalipwa wema wake). Bila shaka hilo ni katika mambo makubwa ya kuazimiwa kufanywa (na kila Muislamu)"(42:40-43)*

## **Mafunzo:**

Kutokana na aya hizi (42:36-43) tunajifunza kuwa,

**Kwanza**, neema zote tulizopewa hapa duniani ikiwa ni pamoja na vitu mbali mbali vya thamani tunavyovipenda na

vinavyotushughulisha sana katika kuvisaka, tunafahamishwa na Mola wetu Muumba kuwa ni kwa ajili tu ya matumizi ya maisha ya hapa duniani. Vitu hivi havina thamani yoyote katika maisha maisha ya akhera. Historia ya mwanaadamu, ni ushahidi tosha kuwa hapana mtu yeyote, hata wale waliokuwa wafalme na matajiri wa kupindukia, aliyeondoka na chochote katika safari yake ya akhera. Katika kushajihisha kipengele hiki, Allah (s.w) anatumkumbusha tena na tena juu ya starehe za maisha ya dunia ukilinganisha na maisha ya akhera katika aya zifuatazo:

رُزِيَ لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوَاتِ مِنَ النِّسَاءِ وَالْبَنِينَ وَالْقَنَاطِيرِ الْمُقَنْطَرَةِ مِنَ  
 الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ وَالْخَيْلِ الْمُسَوَّمَةِ وَالْأَنْعَامِ وَالْحَرْثِ ذَلِكَ مَتَاعُ الْحَيَاةِ  
 الدُّنْيَا وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْنُ الْمَقَابِ ﴿١٤﴾ \* قُلْ أَوْفَيْتُكُمْ بِخَيْرٍ مِّنْ ذَلِكَمُ  
 لِلَّذِينَ اتَّقَوْا عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا  
 وَأَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللَّهِ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ ﴿١٥﴾

*"Watu wametiwa huba ya kupenda wanawake na watoto na mirundi ya dhahabu na fedha, na farasi wanaotunzwa vizuri, na wanyama na mashamba. Na hayo ni matumizi katika maisha ya dunia, na kwa Mwenyezi Mungu ndiko kwenye marejeo mazuri. Sema: "Nikwambieni yaliyo bora kuliko hivyo?" Kwa ajili ya wamchao Mungu ziko bustani kwa Mola wao, zipitazo mito mbele yake. Watakaa humo milele na wake (zao) waliotakaswa (na kila uchafu na kila ubaya). Na wana radhi ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu anawaona (wote) waja (wake). (3:14-15)*

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ وَإِنَّمَا تُوَفَّقُونَ أُجُورَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ  
 فَمَنْ رُحِخَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا  
 مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿١٥﴾

*Kila nafsi itaonja mauti. Na bila shaka mtapewa ujira wenu kamili siku ya Kiyama. na aliyewekwa mbali na moto na akaingizwa Peponi, basi amefuzu (amefaulu kweli kweli). Na maisha ya dunia (hii) si kitu ila ni starehe idanganyayo (watu). (3:185)*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ أَنْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ  
 أَتَأْقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ أَرْضَيْتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَتَّعَ  
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٣٨﴾

*Enyi mlioamini! Mna nini mnapoambiwa "Nendeni (kupigana) kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu", mnajitia uzito katika ardhi? Je, mumekuwa radhi na maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kwa (mkabala wa maisha ya) akhera ni kidogo tu. (9:38)*

اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ وَفَرِحُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَا الْحَيَاةُ  
 الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا مَتَّعٌ ﴿٣٨﴾

*"Mwenyezi Mungu hukunjua riziki kwa amtakaye na huidhikisha (kwa amtakaye). Na wamefurahia maisha ya dunia (kuliko ya Akhera). Na uhai wa dunia kwa mkabala wa Akhera si kitu ila ni starehe ndogo tu. (13:26)*

وَأَضْرَبَ لَهُم مَّثَلَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَا ءَأَنزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ  
 بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ فَأَصْبَحَ هَشِيمًا تَذْرُوهُ الرِّيحُ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ  
 شَيْءٍ مُّقْتَدِرًا ﴿٤٥﴾

*Na wapigie mfano wa maisha ya dunia: (Maisha ya dunia) ni kama maji tunayoyateremsha kutoka mawinguni; kisha huchanganyika nayo (maji hayo) mimea ya ardhi (ikastawi), kisha (baadaye) ikawa (mimea hiyo) majani makavu yaliyokatikatika ambayo upepo huyarusha huku na huko. Na Mwenyezi Mungu Ana uweza juu ya kila kitu. (18:45)*

أَعْلَمُوا أَنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌّ وَلَهُمْ وَرَبُّنَا وَقَدْحُهُمْ بَيْنَكُمْ وَتَكَاتُرُهُمْ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ كَمَثَلِ غَيْثٍ أَعْجَبَ الْكُفَّارَ نَبَاتُهُ ثُمَّ يَهِيجُ فَتَرَاهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَكُونُ حُطَمًا وَفِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ شَدِيدٌ وَمَغْفِرَةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٌ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿٢٠﴾

*Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo na upuuzi na pambo na kufaharishana baina yenu (kwa nasaba), na kufaharishana kwa mali na watoto. (Na hali ya kuwa vyote hivi hamdumu navyo. Mfano wake) ni kama mvua ambayo huwafurahisha (wakulima) mazao yake, kisha yanakauka ukayaona yamepiga umanjano (badala ya kupiga uchanikiwiti), kisha yanakuwa mabuwa (hayana chochote). Na Akhera kuna adhabu kali (kwa wabaya); na (pia) msamaha wa Mwenyezi Mungu na radhi (Yake kwa wema). Na hayakuwa maisha ya dunia ila ni starehe idanganyayo; (mara huondoka). (57:20)*

بَلْ تُؤْثِرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿١٦﴾ وَالْآخِرَةَ خَيْرٌ وَأَبْقَى ﴿١٧﴾

*"Bali nyinyi mna penda zaidi maisha ya dunia, hali ya kuwa ya akhera ni bora (zaidi kabisa) na yenye kudumu". (87:16-17)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa hapa duniani si uwanja wa kustarehe bali ni uwanja wa kutafutia starehe za kudumu milele za maisha ya akhera. Hivyo wale watakao kanusha maelekezo haya ya Mola wao, badala yake wakaifanya dunia kuwa ni sehemu ya kustarehe na wakatumia vipaji vyao na umri wao wote katika harakati za kutafuta starehe hizo, watakuwa wamekhasirika kweli kweli.

**Kwanza** starehe hawataiona kwa vile umbile la binaadamu la hapa duniani si lenye kuhimili starehe halisi. Kwa mfano mtu mwenye wasaa wa kula na kunywa vizuri mara hunenepa na

kuandamwa na magonjwa chungu nzima - ugonjwa wa moyo, presha, kisukari, n.k. **Pili**, hata wale watakaojidhania na kujidanganya kuwa wanastarehe, starehe hizo ni za muda mchache mno. Hata kama tukijaalia kuwa kuna mtu aliyepata starehe kwa saa 24 za kila siku katika umri wake wote, bado ukilinganisha umri wa maisha ya dunia na umri wa milele wa maisha ya akhera, ni starehe isiyokuwepo. Ndiyo maana Allah (s.w) anatufahamisha kuwa starehe ya maisha ya dunia ni **starehe idanganyayo** na ni **mchezo na upuuzi**.

**Pili**, starehe hasa ni starehe ya maisha ya akhera ambamo mtu atakuwa katika starehe katika kila pumzi ya maisha yake ya milele. Watakaostahiki starehe hizi ni **waumini** wenye sifa zifuatazo:

- (i) Wanaomtegemea Mola wao, ambao hawamchelei yoyote katika kutekeleza wajibu wao kama walivyoamrisha na Mola wao, wakijua kuwa hapana hila wala uwezo ila kutoka kwa Allah (s.w). Wanayakini kuwa aliyenusuriwa na Allah (s.w) hapana mwenye uwezo wa kumdharau na aliyeandikiwa kudhurika hapana wa kumnusuru.
- (ii) Wanaojiepusha na madhambi makubwa na mambo mabaya, yaani wanajitahidi kwa kadiri ya uwezo wao kujiepusha na mambo maovu yaliyobayana. Pia mara kwa mara huleta stighfari (kuomba msamaha wa Allah) kwa pale walipomkosea bila ya kujitambua kutokana na udhaifu wa kibinaadamu
- (iii) Ambao wanaopokasirika husamehe. Yaani pamoja na kukasirika baada ya kukasirishwa, huwa tayari kusamehe baada ya kuombwa msamaha au hata bila ya kuombwa msamaha. Kwa ufupi ni wale wanaojitahidi kuzuia hasira na kuwasamehe binaadamu wenzao.



- (iv) Wanaomuitikia Mola wao, yaani wanaomtii Mola wao ipasavyo kwa kutekeleza kila alilowaamrisha na kuacha kila alilowakataza kwa unyenyekevu. Kwa maana nyingine, wale wanaomuabudu Allah (s.w) ipasavyo katika kukiendea kila kipengele cha maisha yao.
- (v) Wanaosimamisha Swala, yaani wanaodumu na ibada ya swala katika maisha yao yote kama alivyoitekeleza Mtume (s.a.w). kwa kuchunga masharti na nguzo za swala na kuswali kwa khushui.
- (vi) Wanaoshauriana katika mambo yao. Yaani wale ambao wanapokuwa na jambo juu ya kuupeleka Uislamu mbele na kuusimamisha katika jamii, hulijadili na kila mtu akatoa ushauri na maoni yake na hatimaye hufikia muafaka na kuazimia kulitekeleza kwa kutegemea msaada wa Allah (s.w)
- (vii) Wanaotoa katika yale waliyoruzukiwa na Allah (s.w). Yaani hutoa mali zao, nguvu zao, elimu zao, muda wao, na kila walichoruzukiwa na Allah (s.w) kwa ajili ya kuwahudumia na kuwasaidia binaadamu wenzie wanaohitajia msaada na kwa ajili ya kuusimamisha Uislamu, kuuendeleza na kuulinda.
- (viii) Wale wanaotetea nafsi zao baada ya kufanyiwa jeuri. Yaani wale ambao hawakubali kudhulumiwa haki zao kirahisi, bali hufanya juhudi za makusudi za kupambana na dhalimu mpaka wapate haki zao.

## (8)Al-Ma'arij (70:19-35)

﴿٢١﴾ إِذَا مَا سَأَلَ لَشْرًا جَزُوعًا ﴿٢٠﴾ وَإِذَا مَسَّهُ  
الْخَيْرُ مَنُوعًا ﴿٢١﴾ إِلَّا الْمُصَلِّينَ ﴿٢٢﴾ الَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ  
﴿٢٣﴾ وَالَّذِينَ فِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ﴿٢٤﴾

*Kwa hakika binaadamu ameumbwa, hali ya kuwa mwenye papatiko. Inapomgusa shari huwa mwenye fadhaa. Na inapomgusa kheri huwa anaizuilia. Ila wanaosali; (hao hawana sifa mbaya). Ambao wanadumisha Sala zao. Na ambao katika mali zao iko sehemu maalumu. (70:19-24)*

لِلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿٢٥﴾ وَالَّذِينَ يُصَدِّقُونَ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٢٦﴾ وَالَّذِينَ هُمْ  
مِنَ عَذَابِ رَبِّهِمْ مُشْفِقُونَ ﴿٢٧﴾ إِنَّ عَذَابَ رَبِّهِمْ غَيْرُ مَأْمُونٍ ﴿٢٨﴾ وَالَّذِينَ  
هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٢٩﴾

*Kwa ajili ya aombaye na anayejizuilia kuomba (japo muhitaji). Na ambao wanasadiki siku ya Malipo. Na ambao wanaiogopa adhabu (itokayo) kwa Mola wao. Hakika adhabu ya Mola wao si ya kusalimika nayo mtu (mbaya). Na ambao wanahifadhi tupu zao.(70:25-29)*

إِلَّا عَلَىٰ أَرْوَاحِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٣٠﴾ فَمَنْ  
أَبْتَغَىٰ وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعَادُونَ ﴿٣١﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمْتِنَتِهِمْ  
وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ﴿٣٢﴾ وَالَّذِينَ هُمْ بِشَهَادَتِهِمْ قَائِمُونَ ﴿٣٣﴾ وَالَّذِينَ  
هُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٣٤﴾ أُولَٰئِكَ فِي جَنَّاتٍ مُّكْرَمُونَ

*Isipokuwa kwa wake zao au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, basi hao hawalaumiwi. Lakini wanaotaka kinyume cha haya, basi hao ndio wanaoruka mipaka. Na ambao wanaangalia*

*amana zao na ahadi zao . Na ambao ni imara katika ushahidi wao. Na ambao wanazihifadhi Swala zao Hao ndio watakaokuwa katika Mabustani wakihishimiwa.(70:30-35)*

## **Mafunzo**

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa:

**Kwanza**, binaadamu ameumbwa na udhaifu mwingi. Miongoni mwa udhaifu alionao ni kuwa anapofikwa na jambo lolote la shari hushikwa na huzuni kubwa na kukata tamaa; lakini akipata kheri kidogo, hujivuna na kuwa bahili.

**Pili**, mwanaadamu ataepukana na udhaifu mwingi alionao ambao humdunisha na kumshusha chini kuliko vilivyo chini, pale tu atakapokuwa Muumini wa kweli anayefanya vitendo vizuri ikiwa ni pamoja na:

- (i) Kusimamisha swala kwa **kuzihifadhi(kuteleleza vilivyo sharti na ngozo zake), kuziswali kwa unyenyekevu na kudumu nazo katika maisha yote.**
- (ii) Kutoa mali na kuwasaidia wanaadamu wenziwe wanaohitajia baada ya kupatwa na shida mbali mbali.
- (iii) Kusadikisha au kuwa na yakini kuwa atarejea kwa Mola wake.
- (iv) Kuogopa adhabu ya Allah(sw) kwa kujiepusha na yale yote yanayomghadhibisha Allah(sw) na kuomba mara kwa mara kuepushwa na moto (25:65 - 66)
- (v) Kuhifadhi tupu kwa kujiepusha mbali na zinaa na vishawishi vyake vyote.
- (vi) Kuchunga amana zote na amana kuu ikiwa ni ile ya Ukhalifa aliyotunukiwa na Allah (s.w) kama tunavyokumbushwa katika aya ifuatayo:

إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَنْ يَحْمِلْنَهَا  
 وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا وَحَمَلَهَا الْإِنْسَانُ إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا ﴿٧٦﴾

*"Kwa yakini tulitoa amana (ya Ukhalifa) kwa mbingu na ardhi na milima vikakataa kuichukua na vikaogopa, lakini mwanaadamu akaichukua. Bila shaka yeye ni dhalimu mkubwa (kwa kuhini amana aliyopewa na Mola wake) mjinga sana." (33:72)*

- (vii) Kuchunga ahadi zote anazotoa kwa watu na kwa Allah (s.w). Ahadi kuu aliyoitoa muumini kwa Allah (s.w) ni ile ya "shahada mbili" pale anapoahidi kuwa hatamshirikisha Allah (s.w) na mungu yeyote na kuwa ataishi kwa kufuata sunnah ya Mtume Muhammad (s.a.w).
- (viii) Kuwa imara katika ushahidi au katika kusimamia haki. Muumini wa kweli ni yule asiyehofu chochote katika kusimamia haki.

## **Muhtasari wa sifa za waumini**

Lengo tarajiwa la Muhtasari huu ni kutuwezesha kuzibaini fika sifa za Waumini zilizoainishwa katika Qur'an, kisha kujipamba nazo ili tuwe waja wema watakaorehemewa na kuridhiwa na Allah (s.w).

### **1. Al-Anfal (8:2-4).**

- (i) Anapotajwa Allah (s.w) nyoyo zao hujawa na khofu.
- (ii) Wanaposomewa aya za Allah (s.w) huwazidishia Imani.
- (iii) Wanamtegemea Mola wao tu basi katika kila jambo lao.
- (iv) Wanasimamisha swala.
- (v) Wanatoa katika yale walioruzukiwa na Mola wao ikiwa ni pamoja na Zakat, Sadaqaat, n.k. kwa ajili ya Allah (s.w).

## **2. Ar-Raad (13:19-24)**

- (i) Huamini na kuyafuata yaliyotoka kwa Allah (mafundisho ya Qur'an na Sunnah).
- (ii) Hutimiza Ahadi ya Allah (s.w) (6:162:163), (7:172-173), (33:72-73).
- (iii) Hawavunji ahadi za wanadamu wenzao kwa hali yoyote ile.
- (iv) Huyaunga aliyoamuru Allah (s.w) yaungwe .
- (v) Humuogopa Mola wao kwa kuzingatia uwezo wake, nguvu zake, na mamlaka yake yasiyo na kikomo.
- (vi) Huiogopa siku ngumu ya Hesabu na Hesabu mbaya ikawa sababu ya kuyakimbia maovu na kuyaendea mema na mazuri.
- (vii) Ambao pia huwa na subira na uvumilivu katika mazito yanayowakabili katika maisha.
- (viii) Husimamisha swala.
- (ix) Hutoa katika vile walivyoruzukiwa na Allah (s.w) kwa siri na dhahiri.

## **3. Al-Mu'uminuuna (23:1-11).**

- (i) Huwa wanyenyekevu katika swala zao.
- (ii) Hujiepusha na mambo ya upuuzi (laghwi) - Upuuzi ni jambo lolote ambalo humtoa mtu katika lengo la kumuabudu Allah (s.w) na kusimamisha Ukhalifa katika jamii.
- (iii) Hutoa katika yale waliyoruzukiwa na Allah (s.w).
- (iv) Huhifadhi tupu zao kwa kusitiri uchi na kujiepusha na zinaa.
- (v) Huchunga amana zao.
- (vi) Hutekeleza ahadi zao.
- (vii) Huhifadhi swala zao.

#### **4. Al-Furqaan (25:63-77).**

- (i) Huwa ni wanyenyekevu (walioepukana na kibri, majivuno,(n.k.) na wenye nidhamu katika kuendesha maisha yao ya kila siku.
- (ii) Watu wajinga (wasio na nidhamu wala ustaarabu katika maisha yao) wakiwakorofisha huwasiliana nao kwa njia ya amani (husema nao maneno ya salama).
- (iii) Hupitisha baadhi ya saa zao za usiku kwa ajili ya Mola wao kwa kusujudu na kusimama (kuswali Tahajjud/Qiyaamullayl).
- (iv) Humuomba Mola wao awaepushe na adhabu ya Jahannam kwa kujua kwamba ni pahala pabaya pa kukaa Mja.
- (v) Wanapotumia hawafanyi Israaf (kutumia kwa fujo) wala hawatumii kwa ubakhili bali hutumia kwa kadiri ( kati kwakati).
- (vi) Hawamuombi mungu mwingine pamoja na Allah(s.w) na hawamshirikishi Allah (s.w) katika aina zote za shiriki.
- (vii)Hawau nafsi iliyoharamishwa kuuawa ila kwa haki.
- (viii)Hawakaribii zinaa wala kuzini.
- (ix)Huwa na tabia ya kuleta toba ya kweli kila wanapokosea kosa dogo au kubwa kwa kufuata masharti yake ambayo ni (1) Kumuamini Allah (s.w) ipasavyo, (2) Kudumu katika kutenda vitendo vizuri, (3) Kujutia dhambi waliyofanya, (4) Kuchukuwa ahadi na azma ya kutorejea tena dhambi hiyo (5) Kurejesha haki kwa wenyewe (6) Kisha kumuelekea Mola na kumuomba msamaha kwa khushui.
- (x)Hawashuhudii shahada za uongo (hawatoi ushuhuda wa uongo) hata kama ni juu ya nafsi zao au watu wao wa karibu.
- (xi)Wanapopita penye upuuzi, hupita kwa heshima zao.
- (xii)Wanapokumbushwa Aya za Mola wao hawaziangukii kwa uziwi na upofu (huziingiza katika utendaji).
- (xiii)Humuomba Mola wao awape wake wema na watoto wema.
- (xiv)Humuomba Allah (s.w) awajaalie kuwa viongozi wa wamchao yeye (Allah) ambao ni wapesi kuelekea katika njia

iliyonyooka.

### **5. As-Sajdah (32:12-20).**

- (i) Wanapokumbushwa Aya za Mwenyezi Mungu huzitii na kuzitekeleza ipasavyo
- (ii) Humtukuzwa Mola wao kwa sifa zake tukufu (huleta mara kwa mara tasbihi, tahmid, tahlili, takbir, n.k.)
- (iii) Hawafanyi kiburi katika ardhi (Hawatakabari).
- (iv) Huinua mbavu zao usiku kutoka vitandani mwao kwa ajili ya kuswali Tahajjud, kwa kuogopa **Moto** na kutaraji **Pepo**.
- (v) Hutoa katika vile walivyoruzukiwa na Mola wao.

### **6. Al-Ahzaab (33:35-36)**

- (i) Husimamisha nguzo za Uislamu ipasavyo.
- (ii) Huamini nguzo zote za Imani ipasavyo kimatendo.
- (iii) Ni watiifu kwa Allah (s.w) ipasavyo katika kuendesha maisha yao ya kila siku.
- (iv) Husema kweli na kusimamia ukweli.
- (v) Huwa na subira.
- (vi) Ni wanyenyekevu kwa Allah (s.w) katika kuendesha maisha yao.
- (vii) Hutoa vile walivyoruzukiwa na Allah (s.w) kuwapa wanaostahiki.
- (viii) Hufunga swaumu ya mwezi wa Ramadhani na funga za Sunnah.
- (ix) Huhifadhi tupu zao na hujiepusha na zinaa.
- (x) Humkumbuka Allah (s.w) kwa wingi na kumtaja kwa wingi.
- (xi) Hawawi na khiyari katika mashauri ambayo Allah (s.w) na Mtume wake wameshapitisha hukukumu juu yake (yaani hutii bila ubishi au bila kuhoji).

### **7. Ash-Shu'ura (42:30-43).**

- (i) Wanamuamini Allah (s.w) na Mtume wake na nguzo zote za Imani.

- (ii) Humtegemea Mola wao katika kila jambo lao.
- (iii) Wanajiepusha na Madhambi makubwa na hujiepusha na mambo mabaya.
- (iv) Wanapokasirika husamehe.
- (v) Huitikia amri za Mola wao kila wanapoamrisha.
- (vi) Husimamisha swala.
- (vii) Hushauriana katika mambo yao.
- (viii) Hutoa katika vile walivyoruzukiwa na Mola wao.
- (ix) Jeuri inapowafikia huzitetea nafsi zao.
- (x) Husuluhisha ugomvi baina yao.
- (xi) Hulipiza kisasi baada ya kudhulumiwa.
- (xii) Huwa na Subira.

### **8. Al-Maarij (70:19-35).**

- (i) Husimamisha swala.
- (ii) Hudumisha sala zao.
- (iii) Katika Mali zao iko sehemu maalumu ya kuwapa wanaostahiki.
- (iv) Husadiki siku ya Malipo.
- (v) Huogopa adhabu itokayo kwa Mola wao.
- (vi) Huhifadhi tupu zao.
- (vii) Huzichunga amana zao.
- (viii) Huziangalia ahadi zao.
- (ix) Wako Imara katika Ushahidi wao (husimamia ushahidi vilivyo).

### **9. Al-Hujuraat (49:15).**

- (i) Humuamini Allah na Mtume wake ipasavyo kwa kufuata kwa unyenyekevu maamrisha yao yote na kuacha kwa unyenyekevu makatazo yao yote.
- (ii) Hupigania dini ya Allah kwa mali zao na nafsi zao.



## 2. Sifa za Wanafiki

Sifa za wanafiki zimebainishwa kwa uwazi katika sura zifuatazo:

### (1) Al-Baqara (2:8-20)

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ آمَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾  
يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَالدِّينَ ءَامَنُوا وَمَا يَخْدَعُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ  
﴿٩﴾ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ فَزَادَهُمُ اللَّهُ مَرَضًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا  
يَكْذِبُونَ ﴿١٠﴾

*Na katika watu, wako (wanafiki) wasemao: "Tumemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho"; na hali ya kuwa wao si wenye kuamini. Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao; nao hawatambui. Nyoyoni mwao mna maradhi, na Mwenyezi Mungu amewazidishia maradhi. Basi watakuwa na adhabu iumizayo kwa sababu ya kule kusema kwao uwongo. (2:8-10)*

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿١١﴾  
أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِن لَّا يَشْعُرُونَ ﴿١٢﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ ءَامِنُوا  
كَمَا ءَامَنَ النَّاسُ قَالُوا أَنُؤْمِنُ كَمَا ءَامَنَ السُّفَهَاءُ ۗ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ السُّفَهَاءُ  
وَلَكِن لَّا يَعْلَمُونَ ﴿١٣﴾

*Na wanapoambiwa: "Msifanye uharibifu ulimwenguni." Husema "Sisi ni watengenezaji." Hakika wao ndio wahaaribuji, lani hawatambui. Na wanapoambiwa: "Aminini kama walivyoamini watu" Husema "Oh! Tuamini kama walivyoamini wale wapumbavu?" Hakika wao ndio wapumbavu lakini hawajui. (2:11-13)*

وَإِذَا نَقُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَالُوا ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَوْا إِلَىٰ شَيَاطِينِهِمْ قَالُوا  
 إِنَّا مَعَكُمْ إِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِءُونَ ﴿١٤﴾ اللَّهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَمُدُّهُمْ  
 فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١٥﴾ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الضَّالَّةَ بِالْهُدَىٰ  
 فَمَا رَبِحَت تِّجَارَتُهُمْ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿١٦﴾

*Na wanapokutana na walioamini husema: "Tumeamini"; na wanapokuwa peke yao kwa mashetani wao husema: "Hakika sisi tu pamoja nanyi, tunawacheza shere tu." Mwenyezi Mungu atawalipa shere yao na kuwawacha katika upotofu wao wakitangatanga ovyo. Hao ndio waliokhiari upotofu kuliko uongofu; lakini biashara yao haikupata faida wala hawakuwa wenye kuongoka. (2:14-16)*

مَثَلُهُمْ كَمَثَلِ الَّذِي اسْتَوْقَدَ نَارًا فَلَمَّا أَضَاءَتْ مَا حَوْلَهُ ذَهَبَ اللَّهُ  
 بِنُورِهِمْ وَتَرَ كَهْمُ فِي ظُلْمَةٍ لَا يُبْصِرُونَ ﴿١٧﴾

*Mfano wao (hawa wanafiki) ni kama mfano wa wale (wasafiri waliokumbwa na kiza) wakakoka moto, (na) ulipowaonyesha yaliyo pembezoni mwao, Mwenyezi Mungu aliiondoa nuru yao hiyo na kuwawacha katika viza; hawaoni. (2:17)*

ضُمُّكُمْ عُمَّيْ فَهَمْ لَا يَرِ جِعُونَ ﴿١٨﴾

*Viziwi, mabubu, vipofu; kwa hivyo hawatarejea. (2:18)*

أَوْ كَصَيْبٍ مِّنَ السَّمَاءِ فِيهِ ظُلُمَاتٌ وَرَعْدٌ وَبَرْقٌ يَجْعَلُونَ  
 أَصْبَعَهُمْ فِتًىٰ ءَاذَانِهِمْ مِّنَ الصَّوَاعِقِ حَذَرَ الْمَوْتِ ۗ وَاللَّهُ مُحِيطٌ  
 بِالْكَافِرِينَ ﴿١٩﴾

*Au (mfano wao pia) ni kama mvua kubwa itokayo mwinguni; ndani yake mkawa mna viza na radi na umeme; wakawa*

wakitia vidole vyao masikioni mwao kwa ajili ya mingurumo, kwa kuogopa kufa; (na kufanya hivyo hawakusaidii kitu). Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema hao makafiri. (2:19)

يَكَادُ الْبَرْقُ يَخْطَفُ أَبْصَارَهُمْ كُلَّمَا أَضَاءَ لَهُمْ مَشْوَءٌ فِيهِ  
وَإِذَا أَظْلَمَ عَلَيْهِمْ قَامُوا وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَذَهَبَ بِسَمْعِهِمْ وَأَبْصَرِهِمْ إِنَّا

اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٠﴾

Unakaribia umeme huo kunyakua macho yao; kila unapowaangazia huenda ndani yake na unapowafanyia giza husimama. Na Mwenyezi Mungu angependa angaliondoa kusikia kwao na kuona kwao. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kuweza juu ya kila kitu. (2:20)

Kutokana na aya hizi tunajifunza sifa za wanafiki zifuatazo:

- (i) Kuonesha imani ya uongo. Katika vinywa vyao wanadai kuwa ni waumini lakini katika nafsi zao na matendo yao wanaikanusha imani yao.
- (ii) Wanauchukia Uislamu nyoyoni mwao, na wanazidi kuuchukia kila Uislamu unavyosonga mbele.
- (iii) Hufanya uharibifu katika nchi huku wakidai kuwa wanatengeneza.
- (iv) Huwabeza waumini wa kweli wanaofuata Uislamu vilivyo.
- (v) Hawana msimamo. Wanataka wapate maslahi ya Uislamu na wakati huo huo wawe pamoja na makafiri.
- (vi) Wanawacheza shere Waislamu.
- (vii) Kwa mujibu wa mfano uliopigwa katika aya ya 17 (2:17) wamekhiyari kupotea baada ya kujiwa na mwongozo (nuru).
- (viii) Kwa sababu wamedhamiria upotevu badala ya uongofu kwa ajili ya maslahi ya dunia, hata ukiwaita kwenye uongofu hawawezi kuja. Wamefananishwa na watu wenye vilema vitatu kwa pamoja vya uziwi, ububu na upofu. Hivyo hawawezi kusikia neno la mwenye kuadhini wala la mwenye kukimu.

Kwa mujibu wa mfano uliopigwa katika aya ya 19 na 20 (2:19-20), wanafiki wanatamani matunda yatokanayo na kusimama kwa Uislamu katika jamii lakini hawako tayari kukabiliana na changamoto zinazotokana na mchakato mzima wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Wanafurahia matunda yanayotokana na mvua nzuri za masika lakini hawako tayari kukabiliana na radi, ngurumo na umeme vinavyoandamana na mvua hizo.

**(2)Al-Imraan (3:167-169)**

وَلْيَعْلَمَ الَّذِينَ نَافَقُوا وَقِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا قَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ ادْفَعُوا  
 قَالُوا لَوْ نَعْلَمُ قِتَالًا لَاتَّبَعْنَاكُمْ هُمْ لِلْكَفْرِ يَوْمَئِذٍ أَقْرَبُ مِنْهُمْ لِلْإِيمَانِ  
 يَقُولُونَ بِأَفْوَاهِهِمْ مَا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ وَاللَّهُ أَغْلَمُ بِمَا يَكْتُمُونَ

*Na kuwapambanua wale waliokuwa wanafiki. Nao waliambiwa: "Njooi mpigane katika njia ya Mwenyezi Mungu au mzuie (maadui pamoja na sisi)" Wakasema: "Tungejua kuwa kuna kupigana bila ya shaka tungelikufuateni." Wao siku ile walikuwa karibu na ukafiri kuliko na Uislamu (japokuwa siku zote wakidhihirisha Uislamu wa uwongo). Wanasema kwa midomo yao yasiyokuwa nyoyoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anajua vyema (yote) wanayoyaficha.(3:167)*

الَّذِينَ قَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوا لَوْ أَطَاعُونَا مَا قَاتَلُوا قُلْ فَادْرَءُوا عَن  
 أَنْفُسِكُمْ أَلَمْ تَمُوتْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٦٨﴾

*Wale waliosema juu ya ndugu zao - na (wao wenyewe) wamekataa kwenda (hawakwenda) vitani: "Wangalituti wasingeuawa." Sema: "Jiondoleeni mauti (nyinyi) wenyewe msife maisha ikiwa mnasema kweli." (3:168)*

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ

رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ ﴿١٦٩﴾

*"Wala usiwadhani wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu (maiti). Bali wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao." (3:169).*

Kutokana na aya hizi tunapata sifa za wanafiki zifuatazo:

- (i) Hawako tayari kujitua muhanga kupigania dini ya Allah (s.w) isimame katika jamii au kuihami isiangushwe baada ya kusimama kwake.
- (ii) Wanasema kwa midomo yao yasiyokuwa nyoyoni mwao. Baada ya mapambano dhidi ya maadui wa Dini ya Allah (s.w) kwisha, wanafiki hujikosha kwa kusema uwongo kuwa hawakuwa na taarifa juu ya mapambano ya Waislamu dhidi ya maadui zao, vinginevyo wangelikuwa Pamoja katika vita hivyo hali ya kuwa walijificha wasiende vitani kwa kuogopa kufa.
- (iii) Huwabeza na kuwalaumu wale wanaouliwa au kupata misuko suko katika kuupigania Uislamu.

Katika aya ya 168 na 169 (3:168-169), Allah (s.w) anawasuta wanafiki na kuwakatisha tamaa kuwa mtu hafi kwa kuwa amepigania dini ya Allah (s.w), bali kila mtu atakufa kwa ajali yake aliyopangiwa:

*"... Sema: (uwaambia wanafiki): "Jiondosheeni mauti (nyinyi wenyewe msife milele) ikiwa mnasema kweli."*

Pia Allah (s.w) anawakatisha tamaa wanafiki na kuwatumainisha waumini kuwa hapana jambo lililozuri na bora kwa mtu kuliko kufa katika njia ya Allah (s.w) (kufa shahidi).

### (3)An-Nisaa (4:60-63, 88, 138-145)

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ  
وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ وَقَدْ أُمِرُوا  
أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿١٠﴾

*Huwaoni wale wanaodai kwamba wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako? Nao wanataka wakahukumiwe kwa njia ya twaghuuti; na hali wameamrisha kukataa njia hiyo. Na Shetani anataka kuwapoteza upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki).(4:60)*

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَإِلَىٰ الرَّسُولِ رَأَيْتَ الْمُتَنَفِّقِينَ  
يَصُدُّونَ عَنْكَ صُدُودًا ﴿١١﴾ فَكَيْفَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ

أَيْدِيهِمْ ثُمَّ جَاءُوكَ يَحْلِفُونَ بِاللَّهِ إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا إِحْسَانًا وَتَوْفِيقًا ﴿١٢﴾

*Na wanapoambiwa "Njoooni katika yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, na (njooni) kwa Mtume," utawaona wanafiki wanajiweka mbali nawe kabisa. Basi itakuwaje utakapowafikia msiba kwa sababu ya yale iliyotanguliza mikono yao? Kisha wakakujia wakiapa "Wallahi! Hatukutaka ila wema na mapatano." Hao ndio wale ambao Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi waachilie mbali, (lakini) uwape mawaidha na uwaambie maneno yenye taathira yatakayoingia katika nafsi (nyoyo) zao. (4:61-63)*

﴿ فَمَا لَكُمْ فِي الْمُتَنَفِّقِينَ فَتَتَيْنِ وَاللَّهِ أَرَأَيْتُمْ بِمَا كَسَبُوا آثَرَ يَدُونَ

أَنْ تَهْتَدُوا مِنْ أَضَلِّ اللَّهُ وَمَنْ يُضِلِّ اللَّهُ فَلَنْ تَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴿٨٨﴾

*Imekuwaje nyinyi kuwa makundi mawili katika khabari ya wanafiki, na hali Mwenyezi Mungu amewageuza kwa sababu ya*

yale (mabaya) waliyoyachuma? Je! Mnataka kumwona mwongofu ambaye Mwenyezi Mungu amemhukumu kuwa kapotea? Na aliyemhukumu Mwenyezi Mungu kuwa amekwisha potea hutampatia njia (ya kuambiwa mwongofu). (4:88)

بَشِّرِ الْمُنَافِقِينَ بِأَنَّ لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٣٨﴾ الَّذِينَ يَتَّخِذُونَ الْكَافِرِينَ  
 أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ أَبِئْتَهُمْ الْعِزَّةَ فَإِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا  
 ﴿١٣٩﴾ وَقَدْ نَزَّلَ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتَابِ أَنْ إِذَا سَمِعْتُمْ آيَاتِ اللَّهِ يُكْفَرُ بِهَا  
 وَيَسْتَهْزَأُ بِهَا فَلَا تَتَعَدُوا مَعَهُمْ حَتَّى يَخُوضُوا فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِ إِنَّكُمْ  
 إِذَا مَثَلْتُمْ<sup>ظ</sup> إِنَّ اللَّهَ جَامِعُ الْمُنَافِقِينَ وَالْكَافِرِينَ فِي جَهَنَّمَ جَمِيعًا ﴿١٤٠﴾

Waambie wanafiki kwamba watapata adhabu inayoumiza. (Wanafiki) ambao huwafanya makafiri kuwa marafiki badala ya Waislamu. Je! Wanataka wapate utukufu kwao? Basi utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu. (Hauko katika mkono wa mtu). Naye amekwisha kuteremshieni katika Kitabu (hiki) ya kwamba mnaposikia Aya za Mwenyezi Mungu zinakataliwa na kufanyiwa stihzai, basi msikae pamoja nao, hata waingie katika mazungumzo mengine. (Mtakapokaa) mtakuwa kama wao. Hakika Mwenyezi Mungu atawakusanya wanafiki na makafiri wote pamoja katika Jahannam.(4:138-140)

الَّذِينَ يَتَرَبَّصُونَ بِكُمْ فَإِنْ كَانَ لَكُمْ فِتْحٌ مِّنَ اللَّهِ قَالَُوا أَلَمْ نَكُنْ مَعَكُمْ  
وَإِنْ كَانَ لِلْكَافِرِينَ نَصِيبٌ قَالُوا أَلَمْ نَسْتَحْوِذْ عَلَيْكُمْ وَنَمْنَعَكُم مِّنَ  
الْمُؤْمِنِينَ فَآلَهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ  
عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا ﴿١٤١﴾ إِنَّ الْمُتَنَفِقِينَ لِيُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِيعُهُمْ  
وَإِذَا قَامُوا إِلَى الصَّلَاةِ قَامُوا كُسَالَى يُرَاءُونَ النَّاسَ وَلَا يَذْكُرُونَ اللَّهَ  
إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٤٢﴾

(Wanafiki) ambao wanakungojeni (mpate msiba): basi mkipata kushinda kunakotoka kwa Mwenyezi Mungu, husema (kukwambieni): "Je! Hatukuwa pamoja nanyi?" (Na kama makafiri wamepata sehemu (ya kushinda) husema: (kuwaambia makafiri),"Je, hatukukurubia kukushindeni (tulipokuwa katika jeshi la Waislamu), tukakuzuilieni na (kudhuriwa na hao). Waislamu?" Basi Mwenyezi Mungu atahukumu baina yenu siku ya Kiyama. Na Mwenyezi Mungu hatawajaalia makafiri njia ya kuwashinda Waislamu (kabisa kabisa mpaka waiondoshe dini yao. Hawatajaaliwa kupata hayo). Wanafiki hutaka kumdanganya (hata) Mwenyezi Mungu. Naye atawaadhibu kwa sababu ya kudanganya kwao (huko). Na wanaposimama kusali husimama kwa uvivu, wanaonyesha watu (kuwa wanasali) wala hawamtaji Mwenyezi Mungu ila kidogo.(4:141-42)

مُذَبِّبِينَ بَيْنَ ذَلِكَ لَا إِلَى هَتُولَاءِ وَلَا إِلَى هَتُولَاءِ وَمَنْ يُضْلِلِ اللَّهُ فَلَنْ  
تَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴿١٤٣﴾ يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ  
مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ أَتُرِيدُونَ أَنْ تَجْعَلُوا لِلَّهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَنًا مُّبِينًا  
﴿١٤٤﴾ إِنَّ الْمُتَنَفِقِينَ فِي الدَّرَكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ وَلَنْ تَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا



*Wanayumbayumba baina ya huku (kwa Waislamu na huku kwa makafiri). Huku hawako wala huku hawako. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemhukumu kupotea, huwezi kumpatia njia (ya kuhisabika kuwa mwongofu). Enyi mlioamini! Msiwafanye makafiri kuwa marafiki badala ya Waislamu. Mnataka awe nayo (Mtume wa) Mwenyezi Mungu hoja dhahiri juu yenu (ya kuwa nyinyi wabaya)? Bila shaka wanafiki watakuwa katika tabaka la chini kabisa katika moto. Hutamkuta kwa ajili yao msaidizi (yo yote). (4:143-145)*

Katika aya hizi sifa za wanafiki zinaainishwa kama ifuatavyo:

- (i) Wanapendelea kuhukumiwa kwa sheria za Kitwaghuut kuliko kuhukumiwa kwa sheria za Allah (s.w)
- (ii) Hawako tayari kuishi kwa kufuata Qur-an na Sunnah.
- (iii) Hutumia sana viapo katika kuficha uovu wao dhidi ya Uislamu na Waislamu.
- (iv) Huwafanya makafiri kuwa marafiki badala ya Waislamu.
- (v) Hujikomba kwa makafiri kwa kutaraji kupata vyeo au kuonekana wa maana kwao.
- (vi) Wanashirikiana na makafiri katika kuzifanyia stihizai aya za Allah (s.w) na Uislamu kwa ujumla.
- (vii) Waislamu wakishinda, hujikomba kuwa pamoja nao na hujinakshi (hujigamba) kuwa wao ndiwo waliosababisha kupatikana kwa ushindi.
- (viii) Makafiri wakishinda hujikomba kwao na kujinakshi kuwa ndio waliowawezesha kushinda.
- (ix) Hawana msimamo. Kwa Waislamu hawapo na kwa makafiri hawapo. Hivyo hawaaminiki kote kote.
- (x) Wanaposimama kuswali, husimama kwa uvivu.
- (xi) Hufanya amali kwa riya (kwa kuonyesha watu).
- (xii) Hawamtaji Mwenyezi Mungu ila kidogo tu.

#### (4) At-Tawbah (9:43-68)

عَفَا اللَّهُ عَنْكَ لِمَ أَذْنَتْ لَهُمْ حَتَّىٰ يَتَّبِعِنَ لَكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَتَعْلَمَ

الْكَذِبِينَ ﴿٤٣﴾

*Mwenyezi Mungu amekuwia radhi (amekusamehe). Kwa nini umewapa ruhusa? (Ungengoja) mpaka wanaosema kweli wakupambanukie, na uwajue waongo (9:43).*

لَا يَسْتَعِذُكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أَنْ يُجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ

وَأَنْفُسِهِمْ ۗ وَاللَّهُ عَلَيْهِمُ بِالْمُتَّقِينَ ﴿٤٤﴾

*Hawatakuomba ruhusa wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. (Hawatakutaka ruhusa) kutoipigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu anawajua wanaomcha. (9:44)*

إِنَّمَا يَسْتَعِذُكَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَارْتَابَتْ قُلُوبُهُمْ

فَهُمْ فِي رَيْبِهِمْ يَتَرَدَّدُونَ ﴿٤٥﴾

*Wanakuomba ruhusa wale wasiomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na nyoyo zao zina shaka; kwa hivyo wanasitasita kwa ajili ya shaka yao. (9:45)*

﴿٤٦﴾ وَلَوْ أَرَادُوا الْخُرُوجَ لَأَعَدُّوا لَهُ عُدَّةً وَلَكِن كَرِهَ اللَّهُ انبِعَاتَهُمْ

فَشَبَّطَهُمْ وَقِيلَ لَهُمْ قَاعِدُوا مَعَ الْقَاعِدِينَ ﴿٤٦﴾ لَوْ خَرَجُوا فِيكُمْ مَا زَادُوكُمْ

إِلَّا خَبَالًا وَلَا وُضِعُوا خِلَالَكُمْ يَبْغُونَكُمُ الْفِتْنَةَ وَفِيكُمْ سَمَّاعُونَ

لَهُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلَيْهِمُ بِالظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾ لَقَدْ ابْتِغَوْا الْفِتْنَةَ مِنْ قَبْلِ

وَقَلَّبُوا لَكَ الْأُمُورَ حَتَّىٰ جَاءَ الْحَقُّ وَظَهَرَ أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ كَرِهُونَ

*Na kama wangelitaka kutoka (kwenda vitani) bila shaka*

wangaliandalia maandalio yake (lakini hawakufanya lolote, ni alama kuwa hawakuwa na nia ya kwenda huko vitani). Mwenyezi Mungu hakupenda kutoka kwao (kwenda huko vitani). Na kwa hivyo akawazuia na ikasemwa (na Shetani) "Kaeni pamoja na wanaokaa." Kama wangelitoka pamoja nanyi wasingalikuzidishieni ila mchafuko, na wangekwenda huku na huku baina yenu kukutakieni fitina (kukugombanisheni). Na miongoni mwenu wako wanaowasikiliza (watu wabaya hao). Na Mwenyezi Mungu anawajua madhalimu. Tangu zamani walitaka kukutilieni chokochoko (na fitina) na wakakupindulia mambo chini juu, mpaka ikafika haki na kudhihirika amri ya Mwenyezi Mungu; juu ya kuchukia kwao. (9: 46-48)

وَمَنْهُمْ مَّنْ يَقُولُ أَخَذْنَا لِي وَإِنَّا تَفَتَّتِيَّ وَلَا تَفَتَّتِيَّ إِلَّا فِي الْفِتْنَةِ سَقَطُوا وَإِن جَهَنَّمَ  
 لَمَحِيطةٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿٤٦﴾ إِن تُصِيبَكَ حَسَنَةٌ فَسُؤْهُمْ وَإِن تُصِيبَكَ مُصِيبَةٌ  
 يَقُولُوا قَدْ أَخَذْنَا أَمْرَنَا مِن قَبْلُ وَتَوَلَّوْا وَهُمْ فَرِحُونَ ﴿٤٧﴾ قُل لَّن  
 يُصِيبَتَا إِلَّا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَنَا هُوَ مَوْلَانَا وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ

Na miongoni mwao yuko anayesema (kumwambia Mtume): "Niruhusu (nisije vitani) wala usinitumbukize katika fitina (kwa kuona wanawake wa huko nikafitinika nao)." Hakika wao wamekwishatumbukia katika fitina. Na kwa yakini Jahannamu itawazunguka makafiri (wasiwe na pa kutokea). Ukikufikia wema (wewe Mtume na Masahaba) unawachukiza; na ukikufikia msiba husema: "Tuliangalia vizuri tangu zamani mambo yetu (kwa hivyo hatukufikwa na balaa hii)," na hugeuka wanakwenda zao nao wamefurahi. Sema: "Halitatusibu ila alilotuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye ni Mola wetu." Basi Waislamu nawamtegemee Mwenyezi Mungu tu. (9:49-51)

قُلْ هَلْ تَرَبَّصُونَ بِنَا إِلَّا إِحْدَى الْأَحْسَنِينَ ۗ وَنَحْنُ نَتَرَبَّصُ بِكُمْ أَنْ يُصِيبَكُمْ اللَّهُ بِعَذَابٍ مِّنْ عِنْدِهِ أَوْ بِأَيْدِينَا فَتَرَبَّصُوا إِنَّا مَعَكُمْ مُتْرَبِّصُونَ ﴿٥٦﴾ قُلْ أَنْفِقُوا طَوْعًا أَوْ كَرْهًا لَّن يُتَقَبَلَ مِنْكُمْ إِلَّا أَنْتُمْ كُنْتُمْ قَوْمًا فَاسِقِينَ ﴿٥٧﴾ وَمَا مَنَعَهُمْ أَنْ تُقَبَلَ مِنْهُمْ نَفَقَتُهُمْ إِلَّا أَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۗ وَلَا يَأْتُونَ الصَّلَاةَ إِلَّا وَهُمْ كُسَالَىٰ وَلَا يُنْفِقُونَ إِلَّا وَهُمْ كَارِهِونَ ﴿٥٨﴾

Sema: "Nyinyi hamtutazamii sisi ila (kupata) moja katika mema mawili (ima kushinda tukapata ngawira au kuuawa tukapata Pepo). Na sisi tunakutazamieni kuwa Mwenyezi Mungu akufikishieni adhabu itokayo kwake au (inayopatikana) kwa mikono yetu. Basi ngojeni, nasi tunangoja pamoja nanyi." Sema: (kuwaambia hawa wanafiki): Toeni (mali yenu) kwa kupenda au kwa kutopenda, hakutakubaliwa kwenu (kutoa huko). Hakika nyinyi ni watu maasi." Na haikuwazuilia ikubaliwe kwao michango yao, ila kwa sababu walimkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala hawafiki mahala pa kusali ila katika hali ya uvivu. (9:52-54)

فَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ أَنْفُسُهُمْ وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٥٥﴾ وَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ إِنَّهُمْ لَمِنْكُمْ وَمَا هُمْ مِنْكُمْ وَلَكِنَّهُمْ قَوْمٌ يَفْرُقُونَ ﴿٥٦﴾ لَوْ يَجِدُونَ مَلْجَأًا أَوْ مَعْرَاطًا أَوْ مَدَّخَلًا لَّوَلَّوْا إِلَيْهِ وَهُمْ يَجْمَحُونَ ﴿٥٧﴾

Wala hawatoi (hivyo wanavyovitoa) ila kwa kuchukua. Yasikufurahishe mali yao wala watoto wao. Anataka Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa hayo katika maisha ya dunia, na zitoke roho zao, na hali ya kuwa ni makafiri. Na

wanaapa kwa (jina) la Mwenyezi Mungu kwamba wao ni pamoja nanyi. Wala wao si pamoja nanyi. Bali wao ni watu wanaoogopa (ndio maana wanasema uwongo huku kwa Waislamu na huko kwa makafiri). Kama wanalipata pa kukimbilia au mapango au mahali (pengine) pa kuingia, (bila shaka) wangekimbia mbio huko, wanakwenda shoti (kama farasi waliochafuka). (9:55-57)

وَمِنْهُمْ مَّن يَلْمِزُكَ فِي الصَّدَقَاتِ فَإِنْ أُعْطُوا مِنْهَا رَضُوا وَإِنْ لَمْ يُعْطُوا مِنْهَا إِذَا هُمْ يَسْخَطُونَ ﴿٥٨﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ رَضُوا مَا آتَيْنَهُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ سَيُؤْتِينَا اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَرَسُولُهُ إِنَّا إِلَى اللَّهِ رَاغِبُونَ ﴿٥٩﴾

Na miongoni mwao (hao wanafiki) wako wanaokusema katika (kugawa kwako) sadaka. Wanapopewa katika hizo (Sadaka na Zaka) huridhika; na wakitopewa katika hayo wanakasirika. Na kama wangeparidhia yale aliyowapa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na wakasema: "Anatutoshea Mwenyezi Mungu, karibuni Mwenyezi Mungu atatupa katika fadhila zake, na Mtume wake (pia); hakika sisi tunaelekea kwa Mwenyezi Mungu." (9:58-59)

﴿ إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسْكِينِ وَالْعَمِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغُرَمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِّنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾ وَمِنْهُمْ الَّذِينَ يُؤْذُونَ النَّبِيَّ وَيَقُولُونَ هُوَ أذُنٌ قُلُّ أذُنٌ خَيْرٌ لَّكُمْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِينَ وَرَحْمَةٌ لِلَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ رَسُولَ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦١﴾

*Sadaka hupewa (watu hawa): - Mafakiri na masikini na wanaozitumikia na wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya Uislamu) na katika kuwapa Uungwana watumwa na katika Kuwasaidia wenye madeni na katika mambo aliyoamrisha Mwenyezi Mungu na katika (kupewa) Wasafiri (walioharibikiwa). Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima. Na miongoni mwa (hao wanafiki) wako wanaomuudhi Mtume na kusema: "Yeye ni sikio tu" (yaani anasikia maneno bila ya kuyapima. Waongo wakubwa). Sema "Sikio la kheri kwenu"; anamuamini Mwenyezi Mungu na anawasadiki wanaoamini. Na ni rehema kwa wale wanaoamini miongoni mwenu. Na wanaomuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu watakuwa na adhabu inayoumiza (9:60-61)*

يَحْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ لِيُرْضَوْكُمْ وَاللَّهُ وَرَسُولُهُ أَحَقُّ أَنْ يُرْضَوْهُ إِنْ كَانُوا مُؤْمِنِينَ ﴿١٢﴾ أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّهُ مَن يُحَادِدِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَأَنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا فِيهَا ذَلِكَ الْخِزْيُ الْعَظِيمُ ﴿١٣﴾

*Wanakuapieni Mwenyezi Mungu ili kukuridhisheni (japo wanamuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume), hali ya kuwa Mwenyezi Mungu - na Mtume wake (pia) - ana haki zaidi ya kuwa wao wamridhishe, ikiwa wao ni wanaoamini. Je, hawajui ya kwamba anayeshindana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi yeye atapata moto wa Jahannamu kukaa humo daima? Hivyo ndiyo hizaya kubwa (udhalilifu inayowangojea). (9:62-63)*

يَحْذَرُ الْمُنَافِقُونَ أَنْ تُنزَلَ عَلَيْهِمْ سُورَةٌ تُنَبِّئُهُمْ بِمَا فِي قُلُوبِهِمْ قُلْ أُسْتَهْزِئُ وَإِنِ اللَّهُ مُخْرِجٌ مَا تَحْذَرُونَ ﴿١٤﴾ وَلَئِنْ سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ ﴿١٥﴾ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ إِن نَّعَفُ عَن طَآئِفَةٍ مِّنْكُمْ نَعَذِّبُ طَآئِفَةً بِأَنَّهُمْ كَانُوا مُجْرِمِينَ ﴿١٦﴾

*Wanafiki wanaogopa kuteremshiwa sura itakayowatajia (unafiki wao) uliomo katika nyoyo zao. Sema: "Fanyeni tu mzaha, hakika Mwenyezi Mungu atayatoa nje hayo mnayoyaogopa." Na kama ukiwauliza (kwa nini waifanyia mzaha dini) wanasema: "Sisi tulikuwa tukizungumzazungumza na kucheza tu." Sema: "Mlikuwa mkimfanyia mzaha Mwenyezi Mungu na Aya zake na Mtume wake?" Msitoe udhuru (wa uwongo); umekwisha kudhihiri ukafiri wenu baada ya kule kuamini kwenu (kwa uwongo). (9:64-66)*

الْمُنَافِقُونَ وَالْمُنَافِقَاتُ بَعْضُهُمْ مِّنْ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمُنْكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمَعْرُوفِ وَيَقْبِضُونَ أَيْدِيَهُمْ نَسُوا اللَّهَ فَنَسِيَهُمْ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿١٧﴾ وَعَدَّ اللَّهُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْكُفَّارَ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا هِيَ حَسْبُهُمْ وَلَعْنَةُ اللَّهِ وَاللَّهُ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿١٨﴾

*Wanaume wanafiki na wanawake wanafiki, wote ni hali moja; huamrisha yaliyo mabaya na huyakataza yaliyo mazuri, na kuizuilia mikono yao (hawasaidii mambo ya kheri); wamemsahau Mwenyezi Mungu (wamepuza amri Zake); na*

*Yeye pia amewasahau (amewapuzi). Hakika wanafiki ndio wavunjao amri. Mwenyezi Mungu amewaahidi wanafiki wanaume na wanafiki wanawake na makafiri, moto wa Jahannamu kukaa humo daima. Huo unawatosha (kuwaadhibu); na Mwenyezi Mungu amewalaani; nao wana adhabu itakayodumu. (9:67-68)*

Sifa za Wanafiki zilizoainishwa katika aya hizi ni hizi zifuatazo:

- (i) Huepa jukumu la kupambana na maadui wa Uislamu kwa kutoa nyudhuru za uongo.
- (ii) Nyoyo zao zina shaka, kwa hivyo wanasita sita kwa ajili ya shaka yao.
- (iii) Huchochea fitna baina ya Waislamu.
- (iv) Wanachukia mafanikio ya Waislamu.
- (v) Waislamu wanapopatwa na msiba hufurahia.
- (vi) Huendea swala kwa uvivu.
- (vii) Wanapotakiwa watoe mali kwa ajili ya Allah (s.w), hutoa kwa kuchukia.
- (viii) Huapa kwa jina la Allah kuwa wapo pamoja na Waislamu. Kihalisia hawapo pamoja na Waislamu bali wao ni maadui wa Waislamu.
- (ix) Ni waoga. Wanaogopa kufa.
- (x) Mgao wa zakat na sadaqat ukiangukia kwao hufurahia lakini ukienda kwa wengine wanaostahiki zaidi kuliko wao hukasirika na kunung'unika.
- (xi) Wanamuudhi Mtume (viongozi) kwa kumtukana na kumkejeli.
- (xii) Wanaogopa kudhihirishwa uovu wao waliouficha vifua ni mwao.
- (xiii) Humfanyia mzaha Mwenyezi Mungu na Mtume wake.
- (xiv) Huamrisha mabaya na kukataza mema.



## (5)Al-Ahzab (33:12-20)

وَإِذْ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ  
إِلَّا غُرُورًا ﴿١٢﴾ وَإِذْ قَالَتْ طَآئِفَةٌ مِّنْهُمْ يَا أَهْلَ يَثْرِبَ لَا مُقَامَ لَكُمْ  
فَارْجِعُوا وَيَسْتَأْذِنُ فَرِيقٌ مِّنْهُمُ النَّبِيَّ يَقُولُونَ إِنَّ بُيُوتَنَا عَوْرَةٌ وَمَا هِيَ  
بِعَوْرَةٌ إِنْ يُرِيدُونَ إِلَّا فِرَارًا ﴿١٣﴾ وَلَوْ دَخَلَتْ عَلَيْهِمْ مِّنْ أَقْطَارِهَا ثُمَّ  
سَأَلُوا الْفِتْنَةَ لَآتَوْهَا وَمَا تَلَبَّثُوا فِيهَا إِلَّا بَسِيرًا ﴿١٤﴾

*Na waliposema wanafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao, "Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawakutuahidi ila udanganyifu tu." Na taifa moja miongoni mwao liliposema "Enyi, wenyeji wa Yathribu (Madina)! Hamna mahali pa kukaa nyinyi, basi rudini Na kundi jingine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa Mtume kwa kusema: "Hakika nyumba zetu ni tupu, (hapana watu, tunakwenda zetu)," lakini hazikuwa tupu, hawakutaka ila kukimbia tu. Na lau kama yaliingia (Majeshi ya makafiri) juu yao katika pande zote , kisha wakaombwa kufanya vita (juu ya Waislamu) wangevifanya, na wasingelika humo (Madina tena) ila muda kidogo tu (33:12-14)*

وَلَقَدْ كَانُوا عَاهِدُوا اللَّهَ مِنْ قَبْلُ لَا يُؤَلُّونَ الْأَدْبَرَ وَكَانَ  
عَهْدُ اللَّهِ مَسْئُولًا ﴿١٥﴾

*Na kwa yakini walikwishafanya ahadi na Mwenyezi Mungu zamani ya kwamba hawatageuza migongo ; na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni yenye kuulizwa.(33:15)*

قُلْ لَنْ يَنْفَعَكُمْ الْفِرَارُ إِنْ قَرَرْتُمْ مِنَ الْمَوْتِ أَوْ الْقَتْلِ وَإِذَا لَا تُمْتَعُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٦﴾ قُلْ مَنْ ذَا الَّذِي يَعْصِمُكُمْ مِنَ اللَّهِ إِنْ أَرَادَ بِكُمْ سُوءًا أَوْ أَرَادَ بِكُمْ رَحْمَةً وَلَا يَجِدُونَ لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿١٧﴾ ﴿١٧﴾ قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الْمَعْوِفِينَ مِنْكُمْ وَالْقَائِلِينَ لِإِخْوَانِهِمْ هَلُمَّ إِلَيْنَا وَلَا يَأْتُونَ الْبَأْسَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٨﴾ ﴿١٨﴾

*Sema: "Kukimbia hakutakufaeni kama mkikimbia mauti au kuuawa, na kwa hivyo, hamtastareheshwa ila kidogo tu, (kisha mara mtakufa)." Sema: "Ni nani ambaye aweza kukulindeneni na Mwenyezi Mungu kama (Mungu) akikutakieni uovu, au akikutakieni rehema?" Wala hawatapata mlinzi wala msaidizi kinyume cha Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu anawajua wale wanaojizuia miongoni mwenu (wasende vitani pamoja na Mtume) na wawaambiao ndugu zao; "Njooi kwetu (wala msende kwa Muhammad);" wala hawendi katika mapigano ila kidogo tu (ili kuwadanganya Waislamu). (33:16-18)*

أَشْحَةً عَلَيْكُمْ ۖ فَإِذَا جَاءَ الْخَوْفُ رَأَيْتَهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ تَدْوِيرًا ۖ أَعْيَبُهُمْ كَالَّذِي يُغْشَىٰ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۖ فَإِذَا ذَهَبَ الْخَوْفُ سَلَقُواكُمْ بِالْسِنَةِ ۖ جَدَادِ أَشْحَةً عَلَى الْخَيْرِ ۚ أُولَٰئِكَ لَمْ يُؤْمِنُوا ۖ فَأَحْبَطَ اللَّهُ أَعْمَالَهُمْ ۖ وَكَانَ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿١٦﴾ يَحْسَبُونَ الْأَحْرَابَ لَمْ يَذْهَبُوا ۗ وَإِن يَأْتِ الْأَحْرَابَ يَوَدُّوا لَوْ أَنَّهُمْ بَادُونَ فِي الْأَعْرَابِ يَسْأَلُونَ عَنْ أَنْبَائِكُمْ ۖ وَلَوْ كَانُوا فِيكُمْ مَا قَاتَلُوا إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٧﴾ ﴿١٧﴾

*Wakakufanyieni choyo (kukusaidieni) lakini inapokuja hofu, utawaona wanakutazama, macho yao yanazungukazunguka*

*kama yule aliyezimia kwa mauti; lakini hofu inapoondoka, wanakuudhini kwa ndimi zao kali, wanaifanyia choyo kheri, (hawataki kusaidia). Hao hawakuamini, kwa hivyo Mwenyezi Mungu ameviondoshea thawabu vitendo vyao; na hayo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu. (Mpaka sasa kwa woga wao) Wanafikiri yale makundi (ya maadui) hayajaondoka. Na kama makundi hayo yangekuja (tena), wangependa laiti wangekua wako jangwani pamoja na Mabedui, wakiuliza tu habari zenu. Na kama wangalikuwa pamoja nanyi wasingalipigana ila kidogo tu. (Mara wangelikimbia kwa woga wao). (33:19-20)*

Sifa za wanafiki zilizoainishwa katika aya hizi ni hizi zifuatazo:

- (i) Humdhania Mwenyezi Mungu na Mtume wake dhana mbaya. Walisema wakati ule wa Mtume (s.a.w):  
"Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawakutuahidi ila udanganyifu tu."
- (ii) Huwahofisha na kuwakatisha tamaa waumini ili warudi nyuma wasipambane na maadui wa Uislamu.
- (iii) Hutoa nyudhuru za uwongo ili kuepa majukumu ya kuuhami Uislamu na kuuendeleza.
- (iv) Huvunja ahadi kila wanapoahidi.
- (v) Hawako tayari kupata misukosuko kwa ajili ya Uislamu na huogopa kufa. Hivyo hujitenga mbali na mapigano dhidi ya maadui wa Uislamu.

**(6)Al-Hashr (59:11-17)**

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَئِنْ أُخْرِجْتُمْ لَتَخُرَّجَنَّ مَعَكُمْ وَلَا تُطِيعُ فِيكُمْ أَحَدًا أَبَدًا وَإِنْ قُوتِلْتُمْ لَنَنْصُرَنَّكُمْ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿١١﴾  
لَئِنْ أُخْرِجُوا لَا يَخْرُجُونَ مَعَهُمْ وَلَئِنْ قُوتِلُوا لَا يَنْصُرُونَهُمْ  
وَلَئِنْ نَصَرُوهُمْ لَيُوَلِّنَنَّ الْأُذُنُ ثُمَّ لَا يَنْصُرُونَ ﴿١٢﴾

*Huwaoni wale wanafiki wanawaambia ndugu zao walio makafiri miongoni mwa watu waliopewa Kitabu (kabla yenu) Mayahudi (Wanawaambia): "Kama mkitolewa, (mkifukuzwa hapa) tutaondoka pamoja nanyi, wala hatutamtii yoyote kabisa juu yenu. Na kama mkipigwa vita lazima tutakusaidieni." Na Mwenyezi Mungu anashuhudia ya kuwa wao ni waongo. Kama wakifukuzwa hawataatoka pamoja nao, na kama wikipigwa hawatawasaidia; na kama wakiwasaidia kwa yakini watageuza migongo (wende mbio); kisha hawatanusuriwa.(59:11-12)*

﴿ لَأَنْتُمْ أَشَدُّ رَهَبَةً فِي صُدُورِهِمْ مِنَ اللَّهِ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ

*Hakika nyinyi (Waislamu) mnaogopwa zaidi katika nyoyo zao kuliko wanavyomuogopa Mwenyezi Mungu; maana wao ni watu wasiofahamu (lolote).(59:13)*

لَا يَقْبَلُونَكُمْ جَمِيعًا إِلَّا فِي قُرَى مُحَصَّنَةٍ أَوْ مِنْ وَرَاءِ جُدُرٍ  
بَأْسُهُمْ بَيْنَهُمْ شَدِيدٌ تَحْسَبُهُمْ جَمِيعًا وَقُلُوبُهُمْ شَتَّى ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا  
يَعْقِلُونَ ﴿١٤﴾ كَمَثَلِ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ قَرِيبًا ذَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ وَلَهُمْ  
عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٥﴾ كَمَثَلِ الشَّيْطَانِ إِذْ قَالَ لِلْإِنْسَانِ اكْفُرْ فَلَمَّا كَفَرَ  
قَالَ إِنِّي بَرِيءٌ مِنْكَ إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦﴾

*Hawatapigana nanyi kwa mkusanyiko isipokuwa katika vijiji vyao vilivyohifadhiwa, au nyuma ya kuta. Vita vyao baina yao vikubwa. Utawadhani kuwa wako pamoja; kumbe nyoyo zao ni mbali mbali. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili. Hali yao (hawa Mayahudi wa Kibanu Nadir) ni kama ya wale (Mayahudi wa Bani Qaynuqai) waliowatangulia (kufikwa na baa) hivi karibuni; walionja ubaya wa mambo yao; na watapata adhabu (nyingine) iumizayo (vile vile). Ni kama Shetani anapomwambia mtu: "Kufuru;" na anapokufuru akamwambia: "Mimi si pamoja nawe, hakika namuogopa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu."(59:14-16)*

فَكَانَ عَنقِبَتَهُمَا أَنَّهُمَا فِي النَّارِ خَالِدَيْنِ فِيهَا وَذَٰلِكَ جَزَاؤُ الظَّالِمِينَ

*Basi mwisho wa wote wawili hao ukawa waingie Motoni kukaa humo daima; na hiyo ndiyo jaza ya madhalimu. (59:17)*

Sifa za wanafiki zilizoainishwa katika aya hizi ni hizi zifuatazo:

- (i) Hushirikiana na kusaidiana na makafiri katika kuuhujumu Uislamu na Waislamu.
- (ii) Wanawaogopa watu kuliko wanavyo muogopa Allah (s.w)
- (iii) Wanaonekana kuwa wamoja lakini kiutendaji kila mmoja yuko na lake. Umoja wao ni kama ule wa inzi, likitupwa jiwe kila mmoja hutawanyika kikwake tofauti na mshikamano ule wa kundi la nyuki ambao wakichozwa

hushambulia kwa pamoja mpaka kumkibiza adai  
**(7)Al-Munaafiqun (63:1-8)**

إِذَا جَاءَكَ الْمُنَافِقُونَ قَالُوا نَشْهَدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّهِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ  
 لَرَسُولُهُ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَكَاذِبُونَ ﴿١﴾

*Wanapokujia wanafiki, husema: "Tunashuhudia ya kuwa kwa yakini wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu." Na Mwenyezi Mungu anajua kuwa wewe ni Mtume wake na Mwenyezi Mungu anashuhudia ya kuwa hakika wanafiki ni waongo, (wanasema wasiyoyasadiki).(63:1)*

أَتَّخَذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢﴾  
 ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ ءَامَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا فَطُبِعَ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ ﴿٣﴾  
 وَإِذَا رَأَوْا تَعْجِيبَكَ أَعْجَبَهُمْ وَإِنْ يَقُولُوا تَسْمَعُ لِقَوْلِهِمْ ﴿٤﴾  
 كَانَهُمْ خَشَبٌ مُسْتَدَدٌ يَحْسَبُونَ كُلَّ صَبْحَةٍ عَلَيْهِمْ هُمُ الْعَدُوُّ فَاحْذَرْهُمْ  
 قَدْ تَلَّهْمُ اللَّهُ أَنَّهُ يُؤْفِكُونَ ﴿٥﴾

*Wamevifanya viapo vyao ndizo ngao za kujikingia, wakajikinga na kupitishwa njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa hakika ni mabaya kabisa waliyo kuwa wakifanya. Na hayo ni kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hivyo muhuri umepigwa juu ya nyoyo zao; kwa hivyo hawafahamu lolote. Na unapowaona, miili yao inakupendeza, na kama wakisema, unasikiliza usemi wao (kwa vile unavyopendeza); lakini wao ni kama boriti zilizoegemezwa; (wamekaa magogo tu hapo, hawafahamu lolote); wanadhani kila kishindo (kinachozuka) ni juu yao, (ni cha kuwatafuta wao). Hao ni maadui, jihadhari nao. Mwenyezi Mungu awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki! (63:2-4)*

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ رَسُولُ اللَّهِ لَوَّأُ رُءُوسَهُمْ وَرَأَيْتَهُمْ  
يَصُدُّونَ وَهُمْ مُسْتَكْبِرُونَ ﴿٥﴾ سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ  
تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ لَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٦﴾  
هُمُ الَّذِينَ يَقُولُونَ لَا تُنْفِقُوا عَلَى مَنْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ حَتَّى يَنْفَضُوا  
وَلِلَّهِ خَزَائِنُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَفْقَهُونَ

*Na wanapoamabiwa: "Njooi ili Mtume wa Mwenyezi Mungu akuombeeni msamaha (kwa makosa yenu mliyoyafanya), huvigeuza vichwa vyao (kwa kuonyesha kuwa hawataki); na unawaona wanajizua na wakijiona wakubwa. Ni sawa kwao ukiwatakia msamaha au usiwatakie msamaha, Mwenyezi Mungu hatawasamehe; hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu maasi (wenye kutoka katika taa yake). Hao ndio wanaosema: "Msitoe mali kwa ajili ya wale walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ili waondokelee mbali (hapa nchini kwetu, Madina)." Na hazina za mbingu na ardhi ni za Mwenyezi Mungu; lakini wanafiki hawafahamu. (63:5-7)*

يَقُولُونَ لَيْنَ رَجَعْنَا إِلَى الْمَدِينَةِ لِيُخْرِجَنَا الْأَعْرَابُ مِنْهَا الْأَذَلَّ وَلِلَّهِ الْعِزَّةُ

وَلِرَسُولِهِ ۚ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٨﴾

*Wanasema: "Tukirudi Madina, Mwenye utukufu atamfukuza mnyonge." Na utukufu hasa ni wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wa Waislamu; lakini wanafiki hawajui. (63:8)*

Sifa za wanafiki zilizoainishwa katika aya hizi ni hizi zifuatazo:

- (i) Wanasema wasiyoyasadikisha katika nyoyo zao. Katika aya ya kwanza (63:1), Allah (s.w) amewaita wanafiki waongo kwasababu, pamoja na kudai kuwa wanashuhudia kuwa Muhammad (s.a.w) ni Mtume wa Allah (s.w), wanamkanusha Mtume

nyoyoni mwao na katika matendo yao. Hawakuwa tayari kuufuata Uislamu ule aliofundisha Mtume Muhammad (s.a.w).

- (ii) Hufanya viapo vyao kuwa blanketi la kufichia maovu wanayoyafanya dhidi ya Uislamu na Waislamu.
- (iii) Huonesha Uislamu wao katika mavazi na maneno, lakini katika utendaji wako mbali kabisa na Uislamu.
- (iv) Huishi kwa wasiwasi wakikhofia kuwa uovu wao waliouficha utafichuliwa.
- (v) Wanazuia watu wasitoe sadaqa zao kuusaidia Uislamu na Waislamu wanaostahiki kusaidiwa.
- (vi) Hawako tayari kurejea kwa Mwenyezi Mungu kwa makosa yao.
- (vii) Wanaendekeza ubaguzi wa kikabila/ na cha warangi

Kwa kuhitimisha sehemu hii ya "sifa za wanafiki" tumejifunza kuwa wanafiki ni wale watu wanaodai kuwa ni Waislamu, na ilihali vitendo vyao katika maisha ya kila siku ni kinyume kabisa na Uislamu.

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾

*"Na katika watu wako wasemao "Tumeamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na hali ya kuwa wao si wenye kuamini." (2:8)*

Si wenye kamini kwa sababu tabia na mwenendo wao katika mchakato wa maisha yao kila siku katika ngazi ya binafsi na ya



jamii ni sawa na tabia na mwenendo wa makafiri wanaomkanusha Allah (s.w) na siku ya mwisho. Mnafiki hajiiti mnafiki wala hana alama yoyote katika mwili wake ya kuonesha unafiki wake, bali huwa mnafiki kutokana na tabia yake hata kama atadai kuwa ni Muislamu kwa mavazi, kuswali, Kufunga, kuhiji, n.k. Hivyo Muumini wa kweli hanabudi kuwa Muislamu mtendaji kwa mujibu wa Qur-an na Sunnah na hanabudi kujiepusha na tabia zote za kinafiki. Waislamu huangukia kwenye unafiki kutokana na moja ya sababu tatu zifuatazo:

- (i) Kutokuwa na Elimu sahihi juu ya Uislamu. Elimu sahihi ni ile inayomuwezesha mtu kujua lengo la kuwepo kwake hapa duniani na namna ya kulifikia.
- (ii) Kupupia maisha ya dunia kwa dhana kuwa dunia ni sehemu ya starehe.
- (iii) Khofu inayotokana na kuogopa kufa au kukabiliwa na magumu mbali mbali yanayosababishwa na maadui wa Uislamu.

### **Muhutasari wa sifa za wanafiki**

Kwa kuzingatia aya zote tulizozipitia juu ya wanafikitunaweza kutoa majumuisho ya sifa za wanafiki kama ifuatavyo:-

- (1) Hutenda kinyume cha imani wanaodai kuwa nayo.
- (2) Hujaribu kumdanganya Mwenyezi Mungu pamoja na waumini wakidhani kuwa yaliyo nyoyoni mwao hayajulikani.
- (3) Hufanya maovu katika ardhi huku wakidai kuwa wanatenda mema.
- (4) Huwona waumini wa kweli kuwa ni wajinga kwa kufuata kwao Uislamu inavyotakikana.
- (5) Huwacheza shere Waislamu.
- (6) Hujiona kuwa wao ni bora kuliko waumini

- (7) Hujikomba kwa viongozi wa kitwaaghuti.
- (8) Huwafanya makafiri na Washirikina kuwa marafiki zao wa ndani badala ya Allah(s.w) Mtume wake na waumini.
- (9) Huyapenda zadi maslahi ya dunia kuliko ya akhera.
- (10) Hukataa kuhukumiwa na sheria za Allah (s.w).
- (11) Hutumia viapo kama kifuniko cha maovu yao.
- (12) Huchanganya haki na batili, kufuru na Uislamu.
- (13) Huendea swala kwa uvivu.
- (14) Hawamtaji Allah ila kidogo sana.
- (15) Huwafitinisha Waislamu.
- (16) Huchukia Waislamu wanapofikwa na kheri na kufurahia wanapofikwa na msiba.
- (17) Hawako tayari kutoa mali zao katika njia ya Allah (s.w) na wakitoa chochote hutoa kwa ria
- (18) Huwazuia watu kutoka katika njia ya Allah.
- (19) Huzifanyia stihizai (shere) aya za Qur-an.
- (20) Huamrisha maovu na kukataza mema.
- (21) Husema uongo na kuvunja ahadi.
- (22) Huwa vunja moyo na kuwakatisha tamaa Waislamu wa kweli ili wabakie katika ukafiri sawa na wao.
- (23) Hufanya hiyana katika mambo ya kheri na kuchagua mambo mepesi mepesi.
- (24) Wanawaogopa na kuwachelea watu zaidi kuliko Allah (s.w).
- (25) Hushirikiana na maadui kuupiga vita Uislamu na Waislamu.

### 3. Maadili na malezi ya jamii

Qur-an, vile vile inatufunza mahusiano tunayotakiwa tuwe nayo ili kuondoa chuki na uadui na kupandikiza mapenzi miongoni mwa wanajamii kama tunavyojifunza katika sura zifuatazo:

#### 1. Bni Israil (17:23-40)

﴿ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۚ إِنَّمَا يُبَلِّغُنَّ عِنْدَكَ  
الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا أُفٍّ وَلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُلْ لَهُمَا  
قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾ وَأَخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَبِّ  
أَرْحَمُهُمَا كَمَا رَبَّيْتَانِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾ رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا فِي نُفُوسِكُمْ  
إِنْ تَكُونُوا صَالِحِينَ فَإِنَّهُ كَانَ لِلْأَوَّابِينَ غَفُورًا ﴿٢٥﴾

*Na Mola wako amehukumu kuwa msimuabudu yoyote ila Yeye tu. Na (ameagiza) kuwafanyia wema (mkubwa) wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee, (naye yuko) pamoja nawe, au wote wawili, basi usiwaambie hata Ah! Wala usiwakemee. Na useme nao kwa msemu wa hishima (kabisa). Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa (njia ya kuwaonea) huruma na useme: "Mola wangu! Warehemu (wazee wangu) kama walivyonyilea katika utoto." Mola wenu anajua sana yaliyo nyoyoni mwenu. Kama mkiwa wema (kwa wazee wenu daima; lakini mara moja mbili hivi mkapotea, basi atakusameheni) kwani Yeye ni Mwenye kuwaghufiria wenye kurejea (kwake). (17:23-25)*

وَعَاتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلَا تَبْذُرْ  
تَبْدِيرًا ﴿٢٦﴾ إِنَّ الْمُبْذِرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيْطَانِ وَكَانَ الشَّيْطَانُ  
لِرَبِّهِ كَفُورًا ﴿٢٧﴾

*Na umpe jamaa (yako) haki yake, na maskini na msafiri aliyeharibikiwa, wala usitawanye (mali yako) kwa ubadhirifu. Hakika watumiao kwa ubadhirifu ni ndugu wa mashetani (wanamfuata Shetani). Na Shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake. (17:26-27)*

وَإِمَّا تَعْرِضْنَ عَنْهُمْ أَبْيَعَاءَ رَحِمَةٍ مِّن رَّبِّكَ تَرْجُوهَا فَعَلَّ  
لَهُمْ قَوْلًا مَّيْسُورًا ﴿٢٦﴾ وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا  
كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿٢٧﴾

*Na kama unajipurukusha nao (sasa hivi kwa kuwa huna kitu) lakini unatafuta rehema ya Mola wako (riziki) unayoitumai, basi sema nao maneno laini (ya kuwapa waadi ya kuwa ukipata utawapa). Wala usifanye mkono wako (kama) uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjuje ovyo, utakuwa ni mwenye kulaumiwa (ukifanya hivyo) na kufilisika (ukiukunjua ovyo ovyo). (17:28-29)*

إِنَّ رَبَّكَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ إِنَّهُ  
كَانَ بَعَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿٢٨﴾

*Hakika Mola wako humkunjulia rikizi amtakaye na humdhikishia (amtakaye). Hakika Yeye kwa waja wake ni Mwenye kuwajua na kuwaona; (anajua yupi anayestahiki utajiri na yupi anayestahiki ufakiri). (17:30)*

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَاقٍ نَّحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ  
إِن قَاتَلْتُمُ كَانِ خَطَأً كَبِيرًا ﴿٢٩﴾ وَلَا تَقْرَبُوا الرِّزْقَ إِنَّهُ  
كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٠﴾

*"Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umasikini. Sisi ndio tunaowaruzuku wao na nyinyi (pia). Kwa yakini kuwauwa ni khatia kubwa. Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kabisa). (17:31-32)*

وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَمَنْ قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لَوْلِيَّيْهِ سُلْطٰنًا فَلَا يُسْرِفُ فِي الْقَتْلِ إِنَّهُ كَانَ مَنْصُورًا ﴿٣٣﴾

*Wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha (kuuliwa) isipokuwa kwa haki. Na mwenye kuuawa kwa kudhulumiwa, basi tumempa nguvu mrithi wake. Basi (mrithi) asifanye fujo katika kuua (kwa ajili ya huyo mtu wake aliyeuliwa). Hakika yeye atasaidiwa (na sharia maadam anayo haki). (17:33)*

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۗ وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ ۗ إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُولًا ﴿٣٤﴾ وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ۗ ذٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٣٥﴾

*Wala msiyakaribie (msiyaguse) mali ya yatima, isipokuwa kwa njia iliyo bora mpaka afike balebhe yake (huyo yatima akabidhiwe mwenyewe). Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa (Siku ya Kiama). Na timizeni kipimo mpimapo; na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na bora mwishoni (kwake). (17:34-35)*

وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ ۗ إِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ وَالْفُؤَادَ كُلُّ أُولٰٓئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْئُولًا ﴿٣٦﴾ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا ۖ إِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْأَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولًا ﴿٣٧﴾

*Wala usifuata usiyo na ilimu (ujuzi) nayo. Hakika masikio na macho na moyo; hivyo vyote vitaulizwa. Wala usitembee (usende) katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala huwezi kufikia urefu wa milima. (Basi unajivuna nini). (17:36-37)*

كُلُّ ذَٰلِكَ كَانَ سَيِّئُهُ ۗ عِنْدَ رَبِّكَ مَكْرُوهًا ﴿٣٨﴾

*Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola wako. (17:38)*

ذَٰلِكَ مِمَّا أَوْحَىٰ إِلَيْكَ رَبُّكَ مِنَ الْحِكْمَةِ ۗ وَلَا تَجْعَلْ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا

ءَاخَرَ فَتَلْقَىٰ فِي جَهَنَّمَ مَلُومًا مَّدْحُورًا ﴿٣٩﴾

*Haya ni katika yale aliyokufunulia Mola wako katika hikima (zake). Wala usimueke pamoja na Mwenyezi Mungu, Mungu mwengine, usije kutupwa katika Jahanamu hali ya kuwa mwenye kulaumiwa (na) mwenye kufukuzwa (huku na huku). (17:39)*

Aya hizi zinatufundisha kuwa ili tuweze kuishi vizuri katika jamii hatuna budi kushikamana na maamrishi kadhaa yaliyoainishwa na kujiepusha na makatazo kadhaa.

### **(i) Maamrishi ya kushikamana nayo**

Yale tunayoamrisha kushikamana nayo ni haya yafuatayo:

#### **(i) Kumuabudu Allah (s.w) Peke yake**

Kumuabudu Allah (s.w) peke yake ndilo jukumu la kwanza kwa Muumini na hasa ndio lengo la kuumbwa binaadamu (rejea Qur-an 51:56). Kumuabudu Allah (s.w), ni kumtii kwa unyenyekevu katika kukiendea kila kipengele cha maisha ya binafsi na ya jamii.

#### **(ii) Kuwafanyia wema na kuwahurumia wazazi**

Ni wajibu kwa Waumini kuwafanyia wema wazazi wao. Kuwafanyia wema wazazi ni pamoja na kuwafanyia yafuatayo:

- (a) Kuwatii katika yale yote yanayowafikiana na sharia ya Allah (s.w). Wazazi watakapowaamrisha watoto wao wafanye mambo ambayo ni kinyume na amri za Allah (s.w) na Mtume wake, hawatapaswa kuwatii, bali watoto waumini wanapaswa

kuwakatalia hao wazazi wao kwa adabu na heshima kubwa kwa kuwajibu kwa upole na kwa kauli nzuri.

- (b) Kuwaheshimu wazazi kwa kuongea nao kwa upole na kwa huruma. Pia ni pamoja na kujiepusha na kujibizana nao, hata tu kuwagunia au hata kuwapuuzwa kwa ishara.
- (c) Kuwahurumia wazazi kwa kuwapa msaada wowote wanaohitajia kwa kadiri ya uwezo wao, ila tu msaada huo uzingatie mipaka ya Allah (s.w) na Mtume wake.
- (d) Kuwausia wazazi wao kumcha Allah (s.w) na kuwaombea dua na msamaha kwa Allah (s.w) kama tunavyoelekezwa na Allah (s.w) katika Qur-an:

رَبَّنَا اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ الْحِسَابُ ﴿٤١﴾

"Mola wetu nighufirie mimi na wazazi wangu na wale wote wanaoamini siku ya Hisabu". (14:41)

وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا وَحَمْلُهُ وَفِصْلُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَبَلَغَ أَرْبَعِينَ سَنَةً قَالَ رَبِّ أَوْرِعْنِي أَنُ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ وَأَن أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ وَأَصْلِحْ لِي فِي ذُرِّيَّتِي إِنِّي تُبْتُ إِلَيْكَ وَإِنِّي مِنَ

الْمُسْلِمِينَ ﴿٤٥﴾

Na tumemuusia mwanaadamu afanye wema kwa wazazi wake. Mama yake amechukua mimba yake kwa taabu na akamzaa kwa taabu. Na kubeba mimba yake hata kumwachisha ziwa; (uchache wake) ni miezi thalathini. Hata anapofikia baleghe yake na akawa mwenye umri wa miaka arubaini, (mtoto mwema) husema: - "Ee Mola wangu! Niwezeshe nishukuru neema zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu na niwezeshe nifanye vitendo vizuri unavyovipenda, na unitengenezee watoto wangu; kwa yakini ninatubu kwako; na hakika mimi ni miongoni mwa waliosilimu (walionyenyekea)." (46:15)

### (iii) Kutoa mali katika kuwasaidia wanaohitajia

Muumini anawajibika kutoa msaada wa mali na hali kuwapa wanaohitajia. Katika utaratibu wa kutoa msaada utanza na jamaa zako wa karibu kisha ndio uwaangalie wahitaji wengine ikiwa ni pamoja na maskini, wasafiri walioharibikiwa na wengineo kama walivyoainishwa katika Qur-an (2:177), (4:36) na (51:19). Kama huna cha kutoa, angalau mliwaze huyo mwenye kuhitajia kwa kumpa maneno ya faraja na ya matumaini:

﴿قَوْلٌ مَّعْرُوفٌ وَمَغْفِرَةٌ خَيْرٌ مِّنْ صَدَقَةٍ يَتَّبِعُهَا أَذَىٰ وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَلِيمٌ﴾

*"Kauli njema na kusamehe ni bora kuliko sadaqa inayofuatishwa na udhia, na Mwenyezi Mungu ndiye Mkwasi na Mpole. (2:263)*

### (iv) Kutimiza vipimo

Waumini wanawajibika kuwa waadilifu wakati wa kuuziana kwa kukamilisha vipimo vya uzito, ujazo, urefu, n.k. Kufanya ujanja au ubabaishaji wowote katika vipimo ni katika makosa makubwa mbele ya Allah (s.w):

﴿وَاللَّمْطَفِّينَ﴾ ١ ﴿الَّذِينَ إِذَا أَكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ﴾ ٢ ﴿وَإِذَا

كَالَوْهُمْ أَوْ وَّرَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ﴾ ٣

*"Maangamizo yatawathubutikia wapunjao . Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili. Lakini wanapowapimia kwa (kipimo cha) vibaba au mizani (au vinginevyo) wao hupunguza. (831-3)*

﴿أَلَا يَظُنُّ أُولَٰئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ﴾ ٤ ﴿لِيَوْمٍ عَظِيمٍ﴾ ٥

*Je! Wao hawafikiri ya kwamba watafufuliwa; katika siku iliyo Kuu. (83:4-5)*

﴿يَوْمَ يَقُومُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ﴾ ١

*Siku watakaposimama watu (wote) mbele ya Mola wa walimwengu wote?" (83:6)*



## **(v) Kutimiza Ahadi**

Ahadi ni deni ambalo linamlazimu Muumini kulilipa. Asiyetimiza ahadi kwa mujibu wa Qur-an (17:34) atakuwa ni mkosaji na siku ya Hukumu atasimamishwa kizimbani mbele ya Mahakama ya Allah (s.w) aulizwe juu ya ahadi aliyovunja. Kuna aina mbili za ahadi; **ahadi kuu** na **ahadi za kawaida**.

Ahadi kuu ni ile iliyoichukua kila nafsi ya binaadamu kuwa itamuabudu Allah (s.w) peke yake bila ya kumshirikisha na chochote. Rejea Qur-an (7:172-173). Waumini kila mara wanaikariri ahadi hii katika shahada na katika kila swala, hasa pale wanaposoma suratul-Faatiha na kuahidi "**Wewe tu ndiye tunayekuabudu na Wewe tu ndiye tunayekuomba msaada**". (1:5)

**Ahadi za kawaida** ni zile tunazoahidiana na binaadamu wenzetu katika kutekeleza mambo ya kheri. Ahadi za kufanya mambo maovu ni batili na hatuna budi kuzivunja pale tunapotanabahi.

## **(2) Makatazo ya kujiepusha nayo**

Yale waumini wanayowajibika kujiepusha nayo kwa mnasaba wa aya tulizozipitia (17:23-40) ni haya yafuatayo:

### **(a) Kujiepusha na kumshirikisha Allah (s.w)**

Kumshirikisha Allah (s.w) ni kujaalia kuwa Allah (s.w) anao washirika wake wanaomsaidia katika kuendesha masuala mbali mbali katika mchakato mzima wa maisha ya dunia. Allah (s.w) hushirikisha **kinadharia** na **kiutendaji**.

Allah (s.w) hushirikishwa **kinadharia** kwa kujaalia kiumbe kisicho na uwezo wowote, kama vile sanamu, jiwe kubwa, mti mkubwa, majini, malaika, n.k.; kuwa ni mungu na kukielekea kwa maombi na kukitegemea kama apasavyo kuombwa na kutegemewa Allah (s.w). Hii ni shiriki katika **Dhati ya Allah (s.w)**. Pia Allah (s.w) hushirikishwa kinadharia, kwa kumnasibisha na kiumbe au kukipachika kiumbe sifa anazostahiki kusifiwa kwazo. Hii ni shiriki katika **sifa za Allah (s.w)**.

Allah (s.w) hushirikishwa kiutendaji kwa kutiwa kanuni na sharia na kufuatwa miongozo ya maisha iliyotungwa na watu kinyume na mwongozo wa maisha wa Allah (s.w) kupitia kwa Mitume wake na Vitabu vyake. Kumtii yeyote kinyume na kanuni na sharia za Allah (s.w) ni kumshirikisha Allah (s.w) katika **Mamlaka yake**. Na kupitisha hukumu yoyote kinyume na alivyohukumu Allah (s.w) ni kumshirikisha katika **Hukumu zake**. Shirk ndio kiini na chanzo kikuu cha maovu yote duniani na ndio msingi mkuu wa dhuluma (rejea Qur-an 31:13)

### **(b) Kujiiepusha na Ubadhirifu (israfu)**

Ubadhirifu ni utumiaji wa mali au kitu chochote kile chenye thamani kama vile muda, zaidi kuliko mahitajio. Pia kutoa mali au huduma na kuwapa watu wasiostahiki ni katika kufanya ubadhirifu. Vile vile kutumia mali au muda katika yale yaliyoharamishwa, ni katika israfu. Ubadhirifu wa aina zote umekatazwa katika Uislamu na afanyae ubadhirifu ni rafiki yake shetani.

### **(c) Kujiiepusha na ubakhili**

Ubakhili ni kinyume cha ubadhirifu. Ubakhili ni kitendo cha kuwanyima msaada wale wanaostahiki wakati uwezo wa kuwasaidia upo. Pia ni katika kufanya ubakhili kwa mtu kujinyima mahitaji muhimu ya maisha kama vile lishe bora, mavazi na makazi bora na huku anauwezo. Katika kutumia na kutoa misaada, Waumini wanatakiwa wawe kati na kati:

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا

كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿٢٩﴾

*"Wala usifanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjue ovyo ovyo, utakuwa ni mwenye kulaumiwa na kufilisika" (17:29)*

وَالَّذِينَ إِذَا أَنْفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ يَقْتُرُوا وَكَانَ بَيْنَ ذَلِكَ قَوَامًا ﴿١٧﴾

*"Na (katika waja wa Rahman ni) wale ambao wanapotumia hawatunii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa kati kati baina ya hayo." (25:67)*

**(d) Kujiepusha na kuua nafsi bila ya Haki.**

Kuua nafsi bila ya Haki, ni kuiua nafsi isiyo na kosa linalostahiki hukumu ya kifo. Hata kama mtu amefanya kosa la kustahiki kuuliwa, hatauliwa kwa mtu binafsi kuchukua sharia mkononi bali itabidi afikishwe mbele ya Kadhi na ahukumiwe kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu.

Si nafsi ya binaadamu tu iliyoharamishwa kuuliwa pasina haki bali hata nafsi za viumbe vingine vyote ikiwa ni pamoja na wanyama wakubwa na wadogo na mimea. Kwa mfano tunaruhusiwa kuwaua wanyama kwa ajili ya manufaa kutoka kwao au kwa ajili ya kujikinga na madhara yao dhidi ya binaadamu. Pia haturuhuswi kukata au kuteketeza mimea ovyo ovyo pasina haja maalumu na kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira.

..... وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ إِمْرَآئٍ

*"Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umasikini..."(17:31)*

Kiutendaji kuwaua watoto kwa kuogopa umasikini si lazima kuishia kwenye kuwaua watoto waliokwisha zaliwa bali hata kuzuia mimba isitokee, kutoa mimba au kufunga kizazi bila ya sababu ya msingi ya kiafya ni katika kuua watoto. Na katika aya hizi Allah (s.w) anatahadharisha:

..... إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا ﴿٣١﴾

*"... Kwa yakini kuwaua ni khatia kubwa". (17:31)*

### **(e) Kujiepusha na kukaribia zinaa**

Si zinaa tu iliyoharamishwa bali hata yale yote yanayotengeneza mazingira na kuchochea kufanyika kwa zinaa nayo pia yameharamishwa. Yanayochochea zinaa ni pamoja na mavazi yasiyozingatia sheria ya Kiislamu; michanganyiko ya wanaume na wanawake isiyozingatia sheria ya Kiislamu; michezo, miziki, ngoma, nyimbo na mengineyo yanayochochea zinaa.

*"... Hakika hiyo zinaa ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kabisa)" (17:32)*

Uchafu na ubaya wa zinaa unadhihirika wazi kwa wahusika binafsi na kwa jamii kwa ujumla katika maeneo yafuatayo:

- (i) Magonjwa ya zinaa ukiwemo UKIMWI, ambayo hudhoofisha afya na kuathiri kwa kiasi kikubwa uchumi na maendeleo ya jamii kwa ujumla.
- (ii) Kuporomosha maadili ya jamii. Watu wazinifu hawana haya, ni watovu wa nidhamu, walaghai, waongo, wabinafsi na wapupia machafu ya kila namna.
- (iii) Zinaa huondosha umuhimu na heshima ya ndoa.
- (iv) Kuvunja ndoa na kusababisha matatizo ya kifamilia.
- (v) Husababisha watoto wa mitaani na kuingiza jamii katika janga la wahuni, wala unga, matapeli, majambazi pamoja na kusababisha kundi kubwa la vijana wasio na uwezo wa kufanya lolote.

### **(f) Kujiepusha na kula mali ya Yatima**

Waumini wanawajibika kuwatunzia mayatima mali zao na kuwakabidhi wanapofikia baleghe yao baada ya kuwajaribu na kuthibitisha kuwa wanao uwezo wa kutunza mali zao - Rejea Qur-an (4:5-6).

Katika aya ya (17:34) tunakatazwa hata kukurubia mali ya yatima kwa maana ya kwamba tusithubutu kuchanganya mali zao na zetu kwa kisingizio chochote kile na tusizitumie hata kwa matumizi yao wenyewe iwapo tunao uwezo wa kuwalea pasina kuhitajia mali zao:

*"Na wapeni mayatima mali zao wala msibadilishe kibaya kwa kizuri. Wala msile mali zao pamoja na mali zenu. Hakika (yote) hayo ni jukumu kubwa." (4:2)*

*"Na waogope (Mawasii kuwadhulumu mayatima; na wakumbuke) kama na wao wangewacha nyuma yao watoto madhaifu wangukuwa na khofu juu yao; basi wamwogope Mwenyezi Mungu na waseme maneno yaliyo sawa (kwa hao mayatima waliousiwa kuwatazama). Hakika wale ambao wanakula mali ya mayatima kwa dhuluma, bila shaka wanakula moto matumboni mwao; na wataungua katika huo Moto (wa jahannam) uwakao." (4:9-10)*

### **(g) Kujipusha na kufuata mambo kwa kibubusa**

Waislamu wanakatazwa kufanya na kufuata mambo kwa kibubusa (kwa mkumbo) bila ya kuwa na ujuzi unaostahiki.

*"Wala usifuate usiyo na ilimu (ujuzi) nayo. Hakika masikio na macho na moyo; hivyo vyote vitaulizwa." (17:36).*

Kila mtu wa kawaida hana budi kutumia kipaji chake cha akili (moyo) na milango ya fahamu (macho, masikio, n.k.) katika kuchukua uamuzi sahihi na kufuata utaratibu wa maisha anaoridhia Allah (s.w). Na hasa kazi ya akili na kipaji cha elimu alichotunukiwa binaadamu, ni kumuwezesha kujitambua, kumtambua Mola wake na kumuabudu inavyostahiki.

Mtu atakayeishi kwa kufuata mambo kinyume na utaratibu anaoridhia Allah, ambao ni Uislamu, hatapaswa kumlaumu yeyote isipokuwa nafsi yake kwa matokeo mabaya yatakayomfika katika maisha ya dunia na akhera. Allah (s.w) anatumanaabahisha juu ya hili katika aya zifuatazo:

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأَوْا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ  
 الْأَسْبَابُ ﴿١١٦﴾ وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا لَوْ أَنَّا كَرِهْنَا فَنَتَّبِعَهُ مِنْهُمْ  
 كَمَا تَبَرَّءُوا مِنَّا كَذَلِكَ يُرِيهِمُ اللَّهُ أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ  
 وَمَا هُمْ بِخَيْرِ جِينٍ مِنَ النَّارِ ﴿١١٧﴾

*(Wakumbushe wakati) waliofuatwa watakapowakataa wale waliowafuata, na hali ya kuwa wamekwisha kuiona adhabu, na yatakatika mafungamano yao. Na watasema wale waliofuata, "Laiti tungeweza kurudi (duniani) tukawakataa kama wanavyotukataa." Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu atakavyowaonyesha vitendo vyao kuwa majuto yao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni." (2:166-167)*

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَنُؤْمِنَ بِهَذَا الْقُرْآنِ وَلَا بِالَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَلَوْ  
 تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ مَوْقُوفُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ الْقَوْلَ  
 يَقُولُ الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لَوْلَا أَنشَأَ لَكُم مَّوْمِنِينَ  
 ﴿٣١﴾ قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لِلَّذِينَ اسْتَضَعُّوا أَنَحْنُ صَدَدْنَاكُمْ عَنِ  
 الْهُدَىٰ بَعْدَ إِذْ جَاءَكُمْ بَلْ كُنْتُمْ مُجْرِمِينَ ﴿٣٢﴾

وَقَالَ الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ  
 وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُ  
 أَنْدَادًا وَأَسْرُوا الثَّمَامَةَ لَمَّا رَأَوْا الْعَذَابَ وَجَعَلْنَا الْأَغْلَالَ فِي أَعْتَاقِ  
 الَّذِينَ كَفَرُوا هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٣٣﴾

*Na wakasema wale waliokufuru: "Hatutaiamini Qur-an hii kabisa, wala Vile (vitabu) vilivyokuwa kabla yake." Na*

ungewaona madhalimu watakaposimamishwa mbele ya Mola wao, wakirudishiana maneno wao kwa wao, (ungeona mambo)! Wale wanyonge watawaambia wale waliojiona wakubwa: "Kama si nyinyi bila shaka tungekuwa Waislamu." Waseme wale waliojiona wakubwa kuwaambia wale wanyonge: "Oh!Sisi tulikuzuilieni uwongofu baada ya kukufikieni? (Siyu) Bali nyinyi wenyewe mlikuwa waovu." Na wale wanyonge waseme kuwambia wale waliojiona wakubwa: "Bali (mlikuwa mkifanya), vitimbi (hila) usiku na mchana (vya kutuzulia tusiamini); mlipotuamuru tumkufuru Mwenyezi Mungu na tumfanyie washirika." Nao wataficha majuto watakapoiona adhabu; na Tutaweka makongwa shingoni mwa wale waliokufuru; kwani wanalipwa mengine ila yale waliyokuwa wakiyatenda?" (34:31-33)

وَإِذْ يَتَحَاوُونَ فِي النَّارِ فَيَقُولُ الضُّعَفَاءُ لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا  
 إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ أَنتُمْ مُّعْتَدُونَ عَنَّا نَصِيبًا مِّنَ النَّارِ ﴿٤٧﴾  
 قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُلٌّ فِيهَا إِنَّ اللَّهَ قَدَّ حَكَمَ بَيْنَ الْعِبَادِ ﴿٤٨﴾  
 وَقَالَ الَّذِينَ فِي النَّارِ لِخِزْنَةِ جَهَنَّمَ ادْعُوا رَبَّكُمْ يُخَفِّفْ عَنَّا يَوْمًا  
 مِّنَ الْعَذَابِ ﴿٤٩﴾ قَالُوا أَوْ لِمَ تَدْعُوا رَبَّكُمْ رُسُلُكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ  
 قَالُوا بَلَىٰ قَالُوا فَادْعُوا وَمَا دَعَاؤُ الْكٰفِرِينَ إِلَّا فِي ضَلٰلٍ ﴿٥٠﴾

"Na (wakumbushe) watakapobishana katika Moto huo - wakati madhaifu watakapowaambia wale waliojitukiza: "Kwa yakini sisi tulikuwa wafuasi wenu, basi je, mnaweza kutuondolea sehemu kidogo ya Moto?" Waseme wale waliokuwa wakijitukiza: "Sisi sote tumo humu; Mwenyezi Mungu amekwishahukumu baina ya viumbe; (na tumekwishastahiki Moto, hatuna la kufanya." Na wale waliomo Motoni watawaambia walinzi wa Jahanamu; "Muombeni Mola wenu atupunguzie (alau) siku moja ya

*adhabu." (Walinzi) wawaambie: "Je, hawakuwa wakikujieni Mitume wenu kwa hoja zilizowazi?" Waseme: "Kwa nini? (Wakitujia lakini tuliasi)" Wawaambie: "Basi ombeni; na madua ya makafiri hayawi ila ni ya kupotea bure." (40:47-50)*

### **(h) Kujiepusha na maringo na majivuno**

Maringo, majivuno, majigambo, dharau ni vipengele vya kibri. Kwa mujibu wa Hadith sahihi kibri ni katika madhambi makubwa"

*"Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yule ambaye moyoni mwake mna punje ya kibri hataingia peponi." Sahaba mmoja akauliza: "Je, kama mtu anapenda nguo nzuri na viatu?" Mtume (s.a.w) akasema, "Allah (s.w) ni mzuri na anapenda vizuri. Kibri ni kukataa ukweli na kupuuza watu." (Muslim)*

Ili kuepukana na maringo na kibri Allah(s.w) anaturanabahisha:

*"... Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala huwezi kufikia urefu wa mlima." (17:37)*

*"Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu na hali mlikuwa wafu, akakuhuisheni; kisha atakufisheni; kisha atakuhuisheni (tena); kisha kwake mtarejeshwa." (2:28)*

Aliye bora mbele ya wengine ni yule aliyewazidi katika kumcha Mwenyezi Mungu - Rejea Qur-an (49:13)

### **2. An-Nuur (24:1-31, 58-61)**

*سُورَةٌ أَنْزَلْنَاهَا وَفَرَضْنَاهَا وَأَنْزَلْنَا فِيهَا آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ لِّعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ*

*"(Hii) ni sura tuliyoiteremsha; tukailazimisha (mambo mengi ndani yake) tukateremsha ndani yake Aya zilizo wazi kabisa ili mkumbuke." (24:1)*



Ukipitia kwa makini Suratun-Nuur aya za (24:1-31, 58-61) utapata mafunzo ya kimalezi na kimaadili kama ifuatavyo:

**(a) Makemeo juu ya Zinaa na Hukumu kwa Wazinifu.**

Tendo la zinaa ni tendo chafu kimaadili na Allah (s.w) amelikataza si tu kulitenda, bali hata kulikurubia.

*“Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kabisa)”. (17:32)*

Watakao kiuka amri hii ya Allah (s.w), jamii ya Waislamu inalazimika kuwaadhibu wawili hao kwa adhabu iliyo sawa sawa kama inavyo bainishwa katika aya (24:2)

*"Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mpigeni kila mmoja katika wao mijeledi (bakora) mia. Wala isiwashike kwa ajili yao huruma katika (kupitisha) hukumu hii ya Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi mnamuamini. Na lishuhudie adhabu yao (hii) kundi la waumini" (24:2)*

Adhabu hii ni kwa wale ambao hawajaoa au hawajaolewa. Adhabu ya wazinifu ambao wameoa au kuolewa ni kurujumiwa (kupigwa kwa mawe) mpaka wafe kama tunavyojifunza katika Hadithi.

*“Omar (r.a) amesimulia: "Hakika Allah (s.w) alimtuma Muhammad kwa haki, alimshushia kitabu (Qur'an). Katika aya alizoshusha Allah (s.w) palikuwa na aya ya kupiga mawe (wazinifu) mpaka wafe. Mtume wa Allah alihukumu kupigwa mawe (wazinifu) mpaka kufa na baada yake pia tuliwahukumu (Wazinifu) kupigwa mawe mpaka kufa. Na hukumu ya kupigwa mawe mpaka kufa katika kitabu cha Allah ni jambo la haki dhidi ya wanaume na wanawake waliozini wakiwa wameoa/wameolewa baada ya ushahidi kukamilika au baada ya kupata ujauzito au baada ya kukiri kufanya kitendo hicho" (Bukhari na Muslimu)*

*Jabir (r.a) ameeleza kuwa mtu alizini na mwanamke. Mtume (s.a.w) akapitisha hukumu dhidi yake na akachapwa viboko stahiki (100). Baadaye Mtume (s.a.w) alifahamishwa kuwa mtu yule alikuwa ameo. Hivyo, Mtume (s.a.w) alipitisha hukumu stahiki dhidi yake na akapigwa mawe mpaka kufa" (Abu Daud)*

Zinaa ni tendo la jimai lililofanywa baina ya mume na mke nje ya ndoa. Katika Uislamu na katika maadili mema ya kibinaadamu hapana ndoa inayokubalika baina ya jinsia moja, yaani ndoa ya mume kwa mume (ubasha) au mke kwa mke (usagaji). Pamoja na uovu wa zinaa, jimai baina ya jinsia moja, yaani Ubasha na Usagaji ni uovu uliokithiri. Watu waovu katika kaumu ya Nabii Lut (s.a) ikiwa ni pamoja na mkewe, waliangamizwa kutokana na kuzama kwao katika kutenda ovu hili.

*"Na (wakumbushe) Luti alipowaambia watu wake: "Je, mnafanya uchafu, na hali mnaona?"  
"Mnawaingilia wanaume kwa matamanio mabaya badala ya wanawake? Hakika nyinyi ni watu mfanyao ujinga kabisa."  
(27:54-55)*

Pamoja na nasaha walizopewa na Mtume wao, Lut (a.s), watu hawa hawakutaka kubabili tabia yao chafu.

*Basi haikuwa jawabu ya watu wake ila kusema: "Wafukuzeni wafuasi wa Luti katika mji wenu, hao ni watu wanaojitakasa, (basi wasikae na sisi wachafu)." (27:56)  
Wakasema: "Kama usipoacha, ee Luti (kutukataza haya), bila shaka utakuwa miongoni mwa wanaofukuzwa (katika nchi hii)." (26:167)*

Hukumu ya Allah (s.w) kwa watu hawa walionywa wasionyeke ilikuwa ni kuwaadhibu hapa hapa duniani na huko akhera wakiwa wanangojewa na adhabu kali.

*Basi ilipofika amri yetu, tuliifanya ; juu yake kuwa chini yake, na tukawateremshia mvua ya changarawe za udongo mgumu (wa Motoni uliokamatana).*

*(Changarawe) zilizotiwa alama kwa Mola wako (kila moja kuwa ya mtu fulani). Na (adhabu) hii haiko mbali na madhalimu (wengine kama hawa watu wa umma huu wanaofanya machafu haya). (11:82-83)*

Mtume (s.a.w) amelikemea vikali na kulitolea hukumu ya kifo tendo la kaumu Lut (ubasha) kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Jabir (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hakika jambo ovu la kutisha ninalokhofia umat wangu, ni tendo la kaumu Lut." (Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah)*

*Akramah kutoka kwa Ibn Abbas (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yeyote yule mtakayemshika kwa kosa la kufanya kitendo cha kaumu Lut, muueni yeye na yule aliyefanyiwa kitendo hicho." (Tirmidh, Ibn Majah)*

Pamoja na ukubwa wa uovu wa matendo haya ya Ubasha na Usagaji, uliobainishwa wazi katika Qur'an na Hadith Sahihi za Mtume (s.a.w), leo hii duniani kuna nchi zilizo halalisha ndoa za jinsia moja na kutoa uhuru kamili wa kufanya matendo ya zinaa, ubasha na usagaji. Hiki ndio kiwango cha kuporomoka kwa maadili duniani hivi leo. Lakusikitisha zaidi, ni kwamba nchi zilizoporomoka kimaadili kiasi hicho, ndizo zinazojikweza kwa ustaarabu na uungwana na nchi nyingine zikiwemo za Waislamu kuzifanya viigizo.

Maovu haya ya uzinzi na ubasha yametolewa hukumu kali kiasi hicho cha kuchapwa mijeledi 100 mbele ya hadhara au kuuawa ili kuiokoa jamii ya binaadamu na madhara makubwa yanayosababishwa na maovu haya.

**(b) Ni haramu kwa Waumini kuwaoa au kuolewa na Wazinifu, Washirikina na Mahabithi**

الرَّانِي لَا يَنْكِحُ إِلَّا زَانِيَةً أَوْ مُشْرِكَةً وَالزَّانِيَةُ لَا يَنْكِحُهَا إِلَّا زَانٍ أَوْ مُشْرِكٌ وَحُرِّمَ ذَلِكَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿٣١﴾

*Mwanamume mzinifu hafungamani ila na mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina; na mwanamke mzinifu hafungamani naye ila mwanamume mzinifu au mshirikina; na hayo yameharamishwa kwa waumini" (24:3)*

الْخَبِيثَاتُ لِلْخَبِيثِينَ وَالْخَبِيثُونَ لِلْخَبِيثَاتِ وَالطَّيِّبَاتُ لِلطَّيِّبِينَ وَالطَّيِّبُونَ لِلطَّيِّبَاتِ أُولَئِكَ مُبَرَّءُونَ مِمَّا يَقُولُونَ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٣٦﴾

*Wanawake habithi (wabaya) ni wa wanaume habithi na wanaume habithi ni wa wanawake habithi; na wanawake wema ni wa wanaume wema na waume wema ni wa wanawake wema ..... " (24:26)*

Aya hizi zinatuweka wazi kuwa ili kujenga jamii iliyoinkua kimaadili, waumini hawanabudi kuwa macho katika uchumba. Waumini wahakikishe kuwa katika ndoa ya kwanza binti muolewaji ni bikra na kijana muoaji ni bikra vile vile. Kadhalika katika ndoa ya pili, waumini wasiidhinishesha ndoa mpaka wawe na uhakika pasina tone la shaka, kuwa waoanaji wawili ni watwaharifu na wacha-Mungu. Mwanamume mzinifu ni mshirikina kwa mujibu wa Qur'an kwa kuwa ameyafanya matamania ya nafsi yake kuwa Mungu badala ya Allah (s.w)

أَرَأَيْتَ مَنْ اتَّخَذَ إِلَهَهُ هَوَاهُ أَفَأَنْتَ تَكُونُ عَلَيْهِ وَكِيلًا ﴿٤٣﴾

*"Je, umemuona yule aliyefanya matamania (ya nafsi) yake (kila anachokipenda), kuwa Mungu wake? Basi je, utaweza kuwa mlinzi wake (ukamhifadhi na hayo, na hali ya kuwa hataki)? (25:43)*

Kukiukwa kwa maagizo ya Allah (s.w), katika aya hizi (24:3, 26), imekuwa ni sababu kubwa ya mtafaruku katika familia nyingi za Waislamu na jamii kwa ujumla. Familia za waumini zitaishi kwa furaha na amani endapo ujumbe wa aya hizi utafuatwa vilivyo tangu mapema katika kuanzisha familia hizi.

**(c) Ushahidi juu ya kosa la Uzinifu**

Ushahidi wa kuthibitisha kutendeka kwa kosa la uzinifu unapatikana kwa namna tatu zifuatazo:

- (i) Kushuhudia tendo hilo likifanyika kwa wakati mmoja watu wanne Mukalafu (Walio balebhe na wenye akili timamu), wakiwa ni Waislamu waadilifu.
- (ii) Muhusika au wahusika kukiri kwa hiari yake/yao bila ya shinikizo au mazingira yanayopelekea shinikizo lolote.
- (iii) Mwanamke kupata ujauzito nje ya ndoa.

Nje ya ushahidi huu, mtu hatahukumiwa kwa kosa la uzinifu au ubasha pamoja na kuwepo mazingira ya kutatanisha. Sana sana atahukumiwa kukurubia zinaa na kupewa nasaha na maonyo stahiki. Ila ikitokea kwa mwanandoa kumkamata mwenziwe ugoni, bila ya mashahidi wanne au muhusika kukiri kosa kwa hiari yake, wanandoa hawa watalazimika kula kiapo mbele ya kadhi kama ilivyoelekezwa katika aya zifuatazo:

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ أَزْوَاجَهُمْ وَلَمْ يَكُن لَّهُمْ شُهَدَاءُ إِلَّا أَنفُسُهُمْ فَشَهَدَةُ أَحَدِهِمْ أَرْبَعُ شَهَدَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٦﴾  
 وَالْخَمْسَةَ أَنْ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَيْهِ إِنْ كَانَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٧﴾ وَيَدْرَأُ  
 عَنْهَا الْعَذَابَ أَنْ تَشْهَدَ أَرْبَعُ شَهَدَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمِنَ الْكَاذِبِينَ  
 ﴿٨﴾ وَالْخَمْسَةَ أَنْ غَضَبَ اللَّهِ عَلَيْهَا إِنْ كَانَ مِنَ الصَّادِقِينَ

*Na wale wanaowasingizia wake zao (kuwa wamezini) na hawana*

*mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa kushuhudia mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu: ya kwamba bila shaka yeye ni mmoja wa wanaosema kweli. Na mara ya tano (aape) kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa ni miongoni mwa waongo.*

*Na (mke) itamuondokea adhabu kwa kutoa shahada mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba (huyu mume) ni miongoni mwa waongo.*

*Na mara ya tano (aape) ya kwamba hasira ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kama (mumewe) yu miongoni mwa wanaosema kweli, (na yeye mke ndiye muongo)." (24:6-9)*

#### **(d) Uovu wa kumzulia Muumini Uzinifu na Maovu mengine na Hukumu dhidi ya Wazujaji**

Kumzulia mtu mtwahirifu kuwa amefanya tendo la zinaa pasina kuleta ushahidi stahiki ni tendo ovu mno mbele ya Allah (s.w). Kina cha Uovu wa tendo hili la kuwasingizia uzinifu watu watwahirifu kinadhihirishwa na adhabu kali inayotolewa dhidi ya wazushi hawa:

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْتَدُوا هُمْ  
ثَمَنِينَ جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

*“Na wale wanaowasingizia wanawake watahirifu (kuwa wamezini), kisha hawaleti mashahidi wanne, basi wapigeni mijeledi, (bakora) thamanini, na msiwakubalie ushahidi wao tena, na hao ndio mafasiki." (24:4)*

إِنَّ الَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ الْغَنِيَّاتِ الْمُؤْمِنَاتِ لُعِنُوا فِي الدُّنْيَا  
 وَالْآخِرَةِ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٢٣﴾ يَوْمَ تَشْهَدُ عَلَيْهِمْ أَلْسِنَتُهُمْ وَأَيْدِيهِمْ  
 وَأَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٤﴾ يَوْمَئِذٍ يُوقِفُهُمُ اللَّهُ دِينَهُمُ الْحَقَّ  
 وَيَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ الْمُبِينُ ﴿٢٥﴾

*"Bila shaka wale wanaowasingizia wanawake waliotakasika wasiojua (maovu), Waislamu; (wenye kuwasingizia watu hawa) wamelaaniwa katika dunia na akhera; nao watapata adhabu kubwa."*

*"Siku ambayo zitawashuhudia ndimi zao na mikono yao na miguu yao, kwa yale waliyokuwa wakiyafanya."*

*"Siku hiyo Mwenyezi Mungu Atawapa sawasawa malipo yao ya haki, na watajua kwamba Mwenyezi Mungu ndiye (Mwenye kulipa kwa) haki iliyo dhahiri."  
 (24:23-25)*

Pia aya ifuatayo inakemea kwa ujumla juu ya tabia mbaya ya kuwasingizia (kuwazulia) watu wema kuwa wamefanya uovu, ili tu kuwadhalilisha na kuwaaibisha mbele ya jamii:

إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَنْ تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِينَ ءَامَنُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ  
 فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٩﴾

*"Kwa yakini wale wannnaopenda uenee uovu kwa wale walioamini, watapata adhabu iumizayo katika dunia na akhera; na Mwenyezi Mungu ndiye Anayejua; na nyinyi hamjui." (24:19)*

Jambo la kuwasingizia uovu watu wema ni ovu mno mbele ya Allah (s.w) kwa sababu ndiyo silaha wanayotumia wanafiki na

washirika wao katika kudhoofisha Uislamu kwa kuwakatisha tamaa wanaharakati na kuisambaratisha jamii ya Waislamu kwa ujumla. Katika historia ya Uislamu, wakati wa Mtume (s.a.w) silaha hii waliitumia wanafiki wakiongozwa na mkubwa wao Abdullah bin Ubayy, walipomsingizia Bi Aisha (r.a), mkewe Mtume (s.a.w), kuwa amezini na Swafan bin Mu'attal Sulami, miongoni mwa maswahaba wema aliyeshiriki katika vita vya Badr. Allah (s.w) aliwatakaswa waja wake hawa na uzushi wa wanafiki kwa kushusha Sura hii hasa katika aya zifuatazo:

إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِّنْكُمْ لَا تَحْسَبُوهُ شَرًّا لَّكُم بَلْ هُوَ خَيْرٌ  
 لَّكُمْ لِكُلِّ أَمْرٍ مِّنْهُمْ مَا أَكْتَسَبَ مِنَ الْإِثْمِ وَالَّذِي تَوَلَّى كِبْرَهُ مِنْهُمْ  
 لَهُ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١١﴾ لَّوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ ظَنَّ الْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ  
 بِأَنفُسِهِمْ خَيْرًا وَقَالُوا هَذَا إِفْكٌ مُّبِينٌ ﴿١٢﴾ لَّوْلَا جَاءُوا عَلَيْهِ بِأَرْبَعَةِ  
 شَهَادَةٍ فَإِذْ لَمْ يَأْتُوا بِالشَّهَادَةِ فَآتَتْكَ مِنْهُ خَبْرًا فَكُذِّبُوا ﴿١٣﴾  
 وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ لَمَسَّكُمْ فِي مَا  
 أَفَضْتُمْ فِيهِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٤﴾ إِذْ تَلَقَّوْنَهُ بِأَلْسِنَتِكُمْ وَتَقُولُونَ  
 بِأَفْوَاهِكُمْ مَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ وَتَحْسَبُونَهُ هَيِّئًا وَهُوَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمٌ  
 ﴿١٥﴾ وَلَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ قُلْتُمْ مَا يَكُونُ لَنَا أَنْ نَتَكَلَّمَ بِهَذَا سُبْحَانَكَ  
 هَذَا بُهْتَانٌ عَظِيمٌ ﴿١٦﴾ يَعِظُكُمُ اللَّهُ أَنْ تَعُودُوا لِمِثْلِهِ أَبَدًا إِنْ  
 كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿١٧﴾ وَبَيِّنَ اللَّهُ لَكُمْ الْآيَاتِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٨﴾

*Hakika wale walioleta uwongo huo (wa kumsingizia Bibi Aisha - mkewe Mtume -kuwa amezini) ni kundi miongoni*



*mwenu, (ni jamaa zenu). Msifikiri ni shari kwenu, bali hiyo ni heri kwenu. Kila mtu katika wao atapata aliyoyachuma katika madhambi hayo. Na yule aliyejitwika sehemu yake kubwa miongoni mwao, atapata adhabu kubwa (zaidi)*

*Mbona mliposikia (habari) hii, wanaume Waislamu na wanawake Waislamu hawakuwadhania wenzao mema, na kusema "huu ni uzushi dhahiri?"*

*Mbona hawakuleta mashahidi wanne? Na walipokosa kuleta mashahidi, basi hao mbele ya Mwenyezi Mungu ni waongo.*

*Na kama isingalikuwa juu yenu fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema Yake katika dunia na akhera, bila shaka ingalikutepeni adhabu kubwa kwa sababu ya yale mliyoyashughulikia.*

*Mlipoupokea (uwongo huo mkawa mnautangaza) kwa ndimi zenu na mkasema kwa vinywa vyenu msiyoyajua, na mlifikiri ni jambo dogo, kumbe mbele ya Mwenyezi Mungu ni kubwa.*

*Na mbona, mliposikia, hamkusema: "Haitujazii kuzungumza haya: Utakatifu ni Wako (Mola wetu!) Huu ni uwongo mkubwa."*

*Mwenyezi Mungu Anakunasihini msirudie kabisa kufanya mfano wa haya, ikiwa nyinyi ni Waislamu kweli.*

*Na Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya (zake); na Mwenyezi Mungu ndiye Ajuaye, Mwenye hikima.' (24:11-18)*

**Kutokana na aya hizi tunajifunza yafuatayo:**

- (i) Waumini watakoposikia habari za uzushi dhidi ya watu wema, wasizikubali bali wadai ushahidi ulio wazi

unaothibitisha tuhuma hizo.

- (ii) Wazushi wakishindwa kuleta ushahidi, wachukuliwe moja kwa moja kuwa ni waongo na Waislamu wote wawe dhidi yao na kuwepo adhabu inayostahiki.
- (iii) Ni marufuku kwa waumini kudaka na kutangaza mambo ya uzushi dhidi ya watu wema ambayo hawana hakika nayo. Katika kuisisitiza hili Allah anatuasa:

*“Enyi mlioamini! Kama fasiki, (asiyekuwa wa kutegemewa) akikujieni na habari (yoyote ile msimkubalie tu) bali pelelezeni (kwanza), msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda.”(49:6)*

- (iv) Waislamu wanahimizwa wajenge tabia ya kuwa na dhana njema juu ya waumini wenzao kuwa haiwezekani kwa muumini kufanya tendo hilo chafu.

### **(e) Himizo la kuwasamehe waliotukosea**

وَلَا يَأْتَلِ أُولُو الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ أَنْ يُؤْتُوا أُولَى الْقُرْبَىٰ وَالْمَسْكِينِ  
وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلْيَعْفُوا وَلْيَصْفَحُوا أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ  
اللَّهُ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٢﴾

*“Na wasiape wale wakarimu na wenye wasaa miongoni mwenu, kujizuia kuwasaidia jamaa zao, maskini na wale waliohama kwa ajili ya Dini ya Allah; na wasamehe na waachilie mbali (wapuuze yaliyopita). Je, nyinyi hampendi Allah akusameheni? Na Allah ni msamehevu, mrehevu.”(24:22)*

Tukirejea historia, Bi 'Aisha (r.a) amesema kuwa baada ya kuteremshwa aya za (24:11-21) zilizomtakasa na uzushi wa wanafiki, baba yake, Abu Bakr (r.a) aliapa kuwa hatamsaidia tena kwa mali Mistah bin Uthatha, miongoni mwa watu waliokuwa mstari wa mbele katika kueneza uzushi dhidi ya Bi 'Aisha (r.a).

Katika kufanya kitendo cha kueneza uzushi, Mistah hakuonyesha kabisa kujali mahusiano wala ihsani ambazo Abu Bakar (r.a) daima alikuwa anamfanyia yeye na familia yake. Hili lilimkasirisha sana Abu Bakar mpaka kumfikisha kwenye kuchukua kiapo cha kusitisha msaada wake kwa Mistah. Baada ya kushushwa aya hii, Abu Bakar aliomba msamaha kwa Allah (s.w) na akaanza tena kumsaidia Mistah kwa moyo mkunjufu zaidi kuliko hata hapo awali.

Kwa mujibu wa 'Abdullah bin 'Abbas (r.a), waumini wengine miongoni mwa maswahaba pia waliapa kuwa hawatawasaidia tena wale wote walioshiriki katika kusambaza masingizio dhidi ya Bi 'Aisha (r.a). Lakini baada ya kuteremshwa aya hii, wote walivibatilisha viapo vyao, na uhasama wote uliosababishwa na hayo 'masingizio' ukaisha.

Kwa mujibu wa aya hii na maelezo haya ya kihistoria tunajifunza kuwa:

- (i) Katika maadili mema, hatuna budi kuendelea kuwafanyia wema wale waliotukosea, maadamu hatudhuriki tukiendelea kuwafanyia hivyo. Hekima ya kufanya hivyo Allah (s.w) anaibainisha katika aya zifuatazo:

وَلَا تَسْتَوِي الْحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ادْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ  
 فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿٣٤﴾ وَمَا يُلْقِنَهَا  
 إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا ذُو حِظٍّ عَظِيمٍ ﴿٣٥﴾

*"Mambo mazuri na mabaya hayawi sawa. Ondosha ubaya (unaofanyiwa) kwa wema, tahamaki yule ambaye baina yako na baina yake kuna uadui, anakuwa kama jamaa (yako) mwenye kukufia uchungu"*

*Lakini jambo hili hawatapewa ila wale wanaosubiri, wala hawatapewa ila wenye hadhi kubwa (Mbele ya Allah (s.w))."*  
 (41:34-35)

- (ii) Hatuna budi kuwa wepesi kuwasamehe wale walio tukosea ili iwe sababu na sisi kusamehewa makosa yetu na Allah (s.w)"

*Je, nyinyi hampendi Allah akusameheni? ..... " (24:22)*

**(f) Adabu ya kuingia katika nyumba za watu**

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّى تَسْتَأْذِنُوا وَتُسَلِّمُوا عَلَىٰ أَهْلِهَا ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٢٧﴾ فَإِن لَّمْ تَجِدُوا فِيهَا أَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوهَا حَتَّىٰ يُؤْذَنَ لَكُمْ وَإِن قِيلَ لَكُمْ ارْجِعُوا فَارْجِعُوا ۗ هُوَ أَزْكَىٰ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٢٨﴾ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَن تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ مَسْكُونَةٍ فِيهَا مَتَعٌ لَّكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا تَكْتُمُونَ ﴿٢٩﴾

*Enyi mlioamini! Msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka muombe ruhusa, (mpige hodi) na muwatolee salamu waliomo humo. Hayo ni bora kwenu; huenda mtakumbuka (mkaona ni mazuri haya mnyoambiwa).*

*Na kama hamtamkuta humo yeyote, basi msiingie mpaka mruhusiwe . na mkiambiwa "Rudini," basi rudini; hili ni takaso kwenu. Na Mwenyezi Mungu Anajua mnayoyaatenda. Si vibaya kwenu kuingia majumba yasiyokaliwa, (yasiyofanywa maskani: kama mahoteli, maktaba), (bila kupiga hodi), ambamo humo mna manufaa yenu; na Mwenyezi Mungu Anajua mnayoyadhihirisha na mna yoyaficha.(24:27-29)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza adabu za kuingia katika nyumba za watu kama ifuatavyo:

- (i) Hairuhusiwi mtu kuingia nyumba ya mtu bila ya kubisha hodi. Hata kama utaukuta mlango uko wazi, huruhusiwi kuangaza macho ndani. Hivyo wakati wa kubisha hodi unatakiwa uwe pembeni mwa mlango, kiasi kwamba hata kama mlango umefunguliwa usiweze kumuona mtu au vitu vilivyomo ndani. Vile vile hairuhusiwi kubisha hodi kupitia mlango wa uani au madirishani. Hekima ya amri hii ya kubisha hodi, ni kulinda haki ya faragha (privacy) ambayo ni haki ya msingi kwa binaadamu katika mambo mema.
- (ii) Hata baada ya kuruhusiwa kuingia katika nyumba za watu, hatutaingia mpaka kwanza tuwatolee salamu waliomo ndani.
- (iii) Kama mtu atabisha hodi mara tatu bila ya kuitikiwa, hata kama atakuwa anawasikia watu wakiongea ndani, asiingie bali aondoke aende zake bila kinyongo.
- (iv) Iwapo mtu ataitikiwa baada ya kubisha hodi na badala ya kukaribishwa ndani akaambiwa arudi, hanabudi kurudi kwa moyo mkunjufu bila ya manung'uniko yoyote.
- (v) Hatuhitajiki kubisha hodi kwenye nyumba zenye kutoa huduma za kijamii kama vile hoteli, maktaba, msikiti, n.k.

**(g) Adabu ya kukaa na kula katika nyumba za watu.**

لَيْسَ عَلَى الْأَعْمَى حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْأَعْرَجِ حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْمَرِيضِ حَرْجٌ  
وَلَا عَلَى أَنْفُسِكُمْ أَنْ تَأْكُلُوا مِنْ بُيُوتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ آبَائِكُمْ أَوْ بُيُوتِ  
أُمَّهَاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ إِخْوَانِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أَخَوَاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أَعْمَامِكُمْ  
أَوْ بُيُوتِ عَمَّاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ إِخْوَانِكُمْ أَوْ بُيُوتِ خَدَائِكُمْ أَوْ مَا مَلَكَتُمْ  
يَمَانِيَهُمْ أَوْ صَدِيقِكُمْ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَأْكُلُوا جَمِيعًا أَوْ أَشْتَاتًا  
فَإِذَا دَخَلْتُمْ بُيُوتًا فَسَلِّمُوا عَلَى أَنْفُسِكُمْ تَحِيَّةً مِّنْ عِنْدِ  
اللَّهِ مُبْرَكَةٌ طَيِّبَةٌ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٦١﴾

*"Si vibaya kwa kipofu, wala si vibaya kwa kiguru, wala si vibaya kwa mgonjwa, wala kwenu, kama mkila katika nyumba zenu, au nyumba za baba zenu, au nyumba za mama zenu, au nyumba za ndugu zenu, au nyumba za dada zenu, au nyumba za ami zenu, au nyumba za shangazi zenu, au nyumba za wajomba zenu, au nyumba za dada wa mama zenu, au za wale mliowashikia funguo zao, au rafiki zenu. Si vibaya juu yenu kama mkila pamoja au mbali mbali. Na mnapoingia katika majumba toleaneni salamu; (maamkio haya) ni zawadi itokayo kwa Mwenyezi Mungu, yenye baraka, na mema. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyokubainishieni Aya (zake) ili mpate kufahamu." (24:61)*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ إِلَّا أَنْ يُؤْذَنَ لَكُمْ إِلَى  
طَعَامٍ غَيْرٍ نَبْظِرِينَ إِنَّهُ وَلَئِكَ إِذَا دُعِيتُمْ فَأَدْخُلُوا فَإِذَا طَعِمْتُمْ  
فَاتَّشِرُوا وَلَا مُسْتَفْسِسِينَ لِحَدِيثٍ إِنَّ ذَٰلِكُمْ كَانَ يُؤْذَى النَّبِيُّ  
فَيَسْتَحْيِي مِنْكُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يَسْتَحْيِي مِنَ الْحَقِّ وَإِذَا سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَاعًا  
فَسْأَلُوهُنَّ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ ذَٰلِكُمْ أَطْهَرُ لِقُلُوبِكُمْ وَقُلُوبِهِنَّ ۗ وَمَا كَانَ  
لَكُمْ أَنْ تُؤْذُوا رَسُولَ اللَّهِ ۗ وَلَا أَنْ تَنْكِحُوا أَزْوَاجَهُ مِنْ بَعْدِهِ أَبَدًا  
إِنَّ ذَٰلِكُمْ كَانَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمًا ﴿٥٧﴾

*"Enyi mlioamini! Msiingie nyumba za Mtume ila mpewe ruhusa kwenda kula, pasipo (kwenda kukaa) kungojea kiivie. Lakini mtakapoitwa ingieni, na mnapokwisha kula tawanyikeni. Wala msiweke mazungumzo, maana jambo hili linamuudhi Mtume, naye anakuoneeni haya; lakini Mwenyezi Mungu Haoni haya kusema haki. Nanyi mnapowauliza (wakeze) waulizeni nyuma ya pazia. Kufanya haya kutasafisha nyoyo zenu na nyoyo zao. Wala haikupasieni (haitakikani) kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu. Wala kuwaoa wake zake baada yake; kabisa. Hakika jambo hilo ni (dhambi) kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. (33:53)*

Tukizingatia aya hizi tunapata maelekezo ya kimaadili yafuatayo:

- (i) Pamoja na kwamba Uislamu unahimiza ukarimu, haumuhusu kwa pande mmoja, kuingia na kula katika nyumba za watu pasi na mwaliko rasmi. Kuvamia chakula katika nyumba za watu ni kuvuruga utaratibu wa familia na kuleta kero, jambo ambalo halikubaliki katika Uislamu. Kwa upande mwingine, katika mafundisho ya Uislamu,

akija mgeni asiyerami (mgeni wa kupita) asitoke bila ya kumkirimu chochote, angalau maji ya kunywa; naye apokee lakini ahakikishe kuwa hawakalifishi wenyeji wake.

- (ii) Wanaoruhusika kula chakula watakacho kikuta ni wanafamilia wenyewe na jamaa wa karibu kama walivyotajwa katika aya (24:61). Marafiki walioainishwa katika aya hii ni wale marafiki wa ndani walioshibana na familia (rafiki ndugu).
- (iii) Wengine wanaoruhusika kula chakula katika nyumba za watu bila mwaliko rasmi ni wagonjwa, vilema, na wengine walioathirika kiuchumi wanaotambulika kisheria na wanaohitajia msaada wa Waislamu.
- (iv) Waislamu watakapopata mwaliko wa kwenda kula katika nyumba za watu, waje pale kwa wakati uliopangwa na baada ya kula waombe ruhusa ya kuondoka ili kuwapa wenyeji wao uhuru wa kufanya mambo yao mengine ya faragha (yanayohusu familia).

### **(h) Hijabu na kujikinga na zinaa**

Katika kutokomeza zinaa katika jamii, Uislamu hauanzii na kutoa adhabu kali ya kuwachapa wazinifu viboko 100 mbele ya hadhara au kuwapiga mawe mpaka wafe, bali umeanza na kukataza kuikurubia zinaa Qur'an (17:32) na kuweka mazingira yatakayopelekea kutoikurubia zinaa kwa kutoa maelekezo mbali mbali ya hijabu kama inavyodhihiri katika aya zifuatazo:

قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ يَغُضُّوْا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوْا فُرُوْجَهُمْ ذٰلِكَ

أَرْكَى لَهُمْ إِنَّ اللّٰهَ خَبِيْرٌۢ بِمَا يَصْنَعُوْنَ ﴿٣٠﴾

*“Waambie Waislamu wanaume wainamishe macho yao*



(wasiangalie kwa jicho la matamano), na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao; bila shaka Mwenyezi Mungu Anazo habari za (vote) wanayoyafanya." (24:30)

وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَعْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَائِهِنَّ أَوْ أَبْنَاؤَ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي أَخَوَاتِهِنَّ أَوْ نِسَائِهِنَّ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ أَوِ التَّابِعِينَ غَيْرِ أُولَى الْأَرْبَةِ مِنَ الرِّجَالِ أَوِ الطِّفْلِ الَّذِينَ لَمْ يَظْهَرُوا عَلَىٰ عَوْرَاتِ النِّسَاءِ وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ مِنَ زِينَتِهِنَّ وَتَوْبُوا إِلَى اللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهُ الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣١﴾

"Na waambie Waislamu wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe viungo vyao isipokuwa vinavyodhihirika (navyo ni uso na vitanga vya mikono - na wengine wanasema na nyayo). Na waangushe shungi zao mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe mapambo yao ila kwa wanaume zao, au baba zao, au baba za waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenziwao, au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, (watumwa wao), au wafuasi wanaume wasio na matamano (kwa wanawake) au watoto ambao hawajajua mambo yaliyohusu uke. Wala wasipige miguu yao ili yajulikane wanayoyaficha katika mapambo yao. Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waislamu ili mpate kufaulu." (24:31)

يٰۤاَيُّهَا النَّبِيُّ لَسْتُنَّ كَاٰحِدٍ مِّنَ النِّسَاءِ اِنَّ اَتَّقِيْتَنَّ فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ  
فَيَطْمَعَ الَّذِيْ فِيْ قَلْبِهِ مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا مَّعْرُوفًا ﴿٣٢﴾ وَقُرْنَ  
فِيْ بُيُوْتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْاُولٰٓئِؕ وَاَقِمْنَ الصَّلٰوةَ  
وَعَٰتِينَ الزَّكٰوةَ وَاَطِعْنَ اِلٰهَ وَرَسُوْلَهٗؕ اِنَّمَا يُرِيْدُ اِلٰهُ لِيُذْهَبَ عَنْكُمُ  
الرِّجْسَ اَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

*"Enyi wake wa Mtume, nyinyi si kama yeyote tu katika wanawake wengine. (Nyinyi wakeze Mtume). Kama mnataka (kufanya jambo la ) kumcha Mwenyezi Mungu, basi msiregeze sauti (zenu mnaposema na wanaume) ili asitamani mtu mwenye ugonjwa moyoni mwake (kufanya mabaya na nyiye) na semeni maneno mazuri."*

*"Na kaeni majumbani mwenu, wala msionyeshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionyesha mapambo yao wanawake wa zama za ujahili na simamisheni Sala na toeni Zaka, na Mtiini Mwenyezi Mungu na mtume Wake. Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa nyumba (ya Mtume), na (anataka) kukutakaseni kabisa kabisa." (33:32-33)*

يٰۤاَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لِّاَزْوَاجِكَ وِبَنَاتِكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِيْنَ يُدْنِيْنَ عَلَيْهِنَّ  
مِّنْ جَلْبَابِهِنَّ ذٰلِكَ اَدْنٰٓى اَنْ يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذِيْنَ وَاَنَّ اِلٰهَ غَفُوْرًا  
رَّحِيْمًا ﴿٥١﴾

*"Ewe Mtume! Waambie wake zako, na binti zako, na wanawake wa Kiislamu wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya Hivyo kutapelekea upesi wajulikane (kuwa ni watu wa hishima ili) wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu." (33:59)*

Kutokana na aya hizi tunapata maelekezo yafuatayo juu ya hijabu:

- (i) Ili kuepukana na zinaa wanaume na wanawake wameamrisha **kuinamisha macho** yao. **Kuinamisha macho** ni msembo wenye maana ya kutowaangalia wanawake (kwa upande wa wanaume) au wanaume (kwa upande wa wanawake) kwa jicho la matamano. Mara nyingi jicho la matamano limekuwa ndio chanzo cha fitna baina ya mume na mke wasio maharimu, yaani walio ajinabi (wanaoweza kuoana).
- (ii) Wanaume na wanawake pia wamehimizwa katika aya hizi kuwa wafanye jitihada za makusudi za **kulinda tupu zao**. Kulinda tupu ni kufanya jitihada za makusudi kujiepusha na maasia yote yanayosababishwa na utupu. Hili ni pamoja na kujiepusha na zinaa, ubasha, usagaji na kuchezea tupu ili kukidhi matashi ya ngono. Kukidhi matashi ya ngono ni halali tu ndani ya ndoa tena kwa kuliendea tendo hilo kama alivyoliruhusu Allah (s.w). Ubasha ni tendo oву na haramu hata kwa mtu na mkewe. Wanawake ambao kimaumbile na kisaikolojia ni kivutio (attractive) cha wanaume wamepewa maelekezo zaidi ya Hijabu katika aya za (24:31), (33:32-33) na (33:59) kama ifuatavyo:
- (iii) Wavae nguo inayofunika mwili mzima isipokuwa tu uso na viganja vya mikono (wengine wanasema na nyayo za miguu).
- (iv) Wavae Shungi (jalabibi) iliyoshuka vizuri kiasi cha kufunika kifua mpaka kutovuni.
- (v) Wavae vazi pana linaloshuka vizuri bila ya kubana kiasi cha kuonesha makunjo ya mwili.
- (vi) Vazi la baibui au kanzu liwe na mikono mirefu yenye

vifungo karibu na viganja vya mikono ili isitokee mwanya wa vazi hilo kuvuka na kuiacha mikono uchi wakati wa kufanya shughuli mbalimbali.

- (vii) Pamoja na wanawake kuruhusiwa kuvaa mapambo (kinyume na wanaume), hawaruhusiwi kudhihirisha mapambo yao ila kwa wale waliotajwa katika aya (24:31).
- (viii) Wanawake hawaruhisiwi hata kudhihirisha sauti ya mapambo yao. Pia wanawake hawaruhisiwe kudhihirisha hata harufu na rangi ya vipodozi vyao. Wanaruhisiwa kujipodoa kwa mafuta na manukato butu (yasiyo na harufu kali). Ni haramu kwa wanawake kujipaka rangi za midomoni, kuchani, viganjani na kwingineko penye kudhihirika.
- (ix) Ikibidi wanawake waongee na wanaume wasio maharimu zao, wanalazimika kuzikaza sauti zao. Wanawake kulegeza sauti zao mbele ya wanaume wasio maharimu ni miongoni mwa vichocheo vya zinaa.
- (x) Wanawake wamekatazwa kutoka ovyo majumbani mwao pasi na sababu za msingi. Na wakitoka kwa sababu za msingi wachunge miiko yote ya Hijabu iliyoelekezwa katika aya hizi pia wajiepushe na michanganyiko ya wanaume na wanawake isiyozingatia mipaka ya Uislamu. Ni haramu kwa mwanamume na mwanamke ajinabi kukaa faragha wakiwa wawili tu. Ikibidi wanaume na wanawake kukutana pamoja kwa ajili ya jambo la kheri wasiwe chini ya watu watatu.

Pamoja na maelekezo haya ya Hijabu, bado Uislamu umechukua hatua nyingine ya kuikinga jamii na zinaa na majanga yatokanayo kwa kuhalalisha na kuhimiza ndoa (rejea Qur'an 4:24, 5:5). Pia katika Hadithi ya 'Abdullah bin Mas'ud (r.a), Mtume (s.a.w) aliwausia vijana:

*“Enyi kongamano la vijana! Na aoe yule aliye na uwezo miongoni mwenu, Hakika kuoa **kunainamisha macho** na asiyeweza kuoa na afunge; hakika funga hukata matamano” (Bukhari na Muslim).*

Wanawake wa Kiislamu pamoja na washauri wao (mawalii wao) wanashauriwa watoze mahari kidogo kulingana na hali ya muoaji mtarajiwa, ili kurahisisha ndoa.

Hivyo, katika majumuisho ya sehemu hii tunajifunza kuwa Uislamu unatokomezwa zinaa katika jamii kwa kufuata hatua zifuatazo:

- (1) Kuwakataza watu kuikurubia zinaa na kuonesha ubaya wa zinaa (Qur'an 17:32)
- (2) Kutoa maelekezo ya Hijabu kwa wanaume na wanawake ambayo yakitiwa ipasavyo yanawawezesha watu kuepokana na zinaa.
- (3) Kuhimiza ndoa ambayo ndiyo njia pekee iliyo nzuri katika kutosheleza matashi ya kimaumbile ya ngono.
- (4) Kutoa adhabu kali kwa wazinifu ili iwe onyo kwao na kwa jamii nzima.

### **(i) Kubisha hodi katika nyakati za faragha katika familia**

*“Enyi mlioamini! Nawakupigieni hodi wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume, (ya kulia), na wale wasiofikia baleghe miongoni mwenu, mara tatu: kabla ya Sala ya Alfajiri na mnapovua nguo zenu Adhuhuri, na baada ya Sala ya Isha; hizi ni nyakati tatu za faragha kwenu. Si vibaya juu yenu wala juu yao baada ya nyakati hizo (kuingia bila ya kupiga hodi:) mnazungukiana nyinyi kwa nyinyi. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyokuelezeni Aya (zake); na Mwenyezi Mungu*

*ni Mjuzi, Mwenye hikima.*

*“Na watoto miongoni mwenu, watakapobaleghe basi nawapige hodi kama walivyopiga hodi wale wa kabla yao. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyokubainishieni aya zake, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hikima. (24:58-59)*

Katika aya hizi tunapewa maelekezo ya kinidhamu na kimaadili juu ya watoto na watumishi kuwatembelea wazazi wakiwa nyumbani mwao kama ifuatavyo:

- (i) Waumini wanatakiwa wawaelekeze watoto wao ambao hawajafikia baleghe kuwa wabishe hodi wanapotaka kuingia vyumbani katika nyakati tatu za faragha zilizoainishwa:
  1. Kabla ya Swala ya Al-fajiri
  2. Kabla ya Swala ya Adhuhuri wakati wa kujitayarisha kwa swala.
  3. Baada ya Swala ya Al-Ishaa.
- (ii) Mida mingine nje ya hii watoto wanaruhusika kuingia bila ya hodi. Kwa maana nyingine wazazi wawe katika hali ya sitara ambayo haitakuwa ni chukizo watakapokutwa na watoto.
- (iii) Watoto waliofikia baleghe hawaruhusiwi kuingia chumbani mwa wazazi wao pasina kubisha hodi katika nyakati zote.

### **(3) Luq-man (31:12-19)**

وَلَقَدْ آتَيْنَا لُقْمَانَ الْحِكْمَةَ أَنْ شَكَرَ لِلَّهِ وَمَنْ

يَشْكُرْ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿١٣﴾

*Na kwa yakini Tulimpa Luqmani hikima, tukamwambia Mshukuru Mwenyezi Mungu; na atakayeshukuru, kwa yakini*

*anashukuru kwa ajili ya nafsi yake; na atakaye kufuru, Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Asifiwaye, (hahitaji kushukuriwa na yeye).(31:12)*

وَإِذْ قَالَ لِقَمَرِن لَابْنِهِ وَهُوَ يَعِظُهُ وَيَدْبُرُن لَآ تَشْرِكُ  
بِاللَّهِ إِنَّ الشَّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿١٣﴾

*Na (wakumbushe), Luqmani alipomwambia Mwanawe; na hali ya kuwa anampa nasaha.Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu, maana kushirikisha ndiyo dhulma kubwa.(31:13)*

وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهَنًا عَلَى وَهْنٍ وَفِصْلَهُ فِي  
عَامَيْنِ أَنْ اشْكُرْ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَى الْمَصِيرِ ﴿١٤﴾

*Na tumemuusia mwanaadamu (kuwafanyia ihsani) wazazi wake - mama yake ameichukuwa mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na (kumnyonyesha na kuja) kumwachisha kunyonya katika miaka miwili - ya kwamba unishukuru Mimi na wazazi wako; marejeo yenu ni Kwangu.(31:14)*

وَإِنْ جَاهِدَاكَ عَلَى أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا  
وَصَاحِبَهُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا وَاتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَيَّ ثُمَّ إِلَيَّ  
مَرْجِعُكُمْ فَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

*Na (wazazi wako) wakikushurutisha kunishirikisha na (yale) ambayo huna ilimu nayo, usiwatii; lakini kaa nao kwa wema hapa duniani (maadamu ni wazee wako, ila usiwafuate tu mwendo wao mbaya); shika njia ya wale wanaoelekea Kwangu, kisha marejeo yenu ni Kwangu, hapo Nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda.(31:15)*

يَدْبِنَىٰ إِنَّهَا إِن تَكُ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ فَتَكُن فِي صَخْرَةٍ أَوْ فِي  
السَّمَوَاتِ أَوْ فِي الْأَرْضِ يَأْتِ بِهَا اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿١٦﴾

*Ewe mwanangu! Kwa hakika jambo lolote lijapokuwa na uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya jabali au mbinguni au katika ardhi, Mwenyezi Mungu Atalileta (amlipe aliyefanya); bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo yaliyofichikana, (na) Mjuzi wa mambo yaliyo dhahiri. (31:16)*

يَدْبِنَىٰ أَقِمِ الصَّلَاةَ وَآمُرْ بِالْمَعْرُوفِ وَانْهَ عَنِ الْمُنْكَرِ  
وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا أَصَابَكَ إِنَّ ذَلِكَ مِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿١٧﴾

*Ewe mwanangu! Simamisha Sala, na uamrishe mema, na ukataze mabaya, usubiri juu ya yale yatakatayokusibu (kwani mwenye kuamrisha mema na kukataza mabaya lazima zitamfika tu taabu); Hakika hayo ni katika mambo yanayostahiki kuazimiwa (na kila mtu). (31:17)*

وَلَا تَصْعِرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ  
مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿١٨﴾

*Wala usiwatazame (usiwafanyie watu jeuri), kwa upande mmoja wa uso, wala usende katika nchi kwa maringo; hakika Mwenyezi Mungu Hampendi kila ajivunae, ajifahirishaye. (31:18)*

وَأَقْصِدْ فِي مَشْيِكَ وَأَعْظُضْ مِنْ صَوْتِكَ إِنَّ أَنْكَرَ الْأَصْوَاتِ  
لَصَوْتُ الْحَمِيرِ ﴿١٩﴾

*Na ushike mwendo wa katikati, na uteremshe sauti yako; bila shaka sauti ya punda ni mbaya kuliko sauti zote (kwa makelele yake ya bure). (31:19)*

Mzazi wa Kiislamu mwenye hekima ni yule atakayekuwa mstari



wa mbele kutenda mema na kuwalea watoto wake wafuate nyayo zake pamoja na kuwausia na kujusia yeye mwenyewe kufanya yafuatayo:

**(a) Kuwa wenye shukurani mbele ya Allah (s.w)**

Mwanaadamu ametunukiwa neema mbali mbali na Mola wake kuliko viumbe wengine wote kama tuanvyojifunza katika aya mbali mbali za Qur'an.

❖ وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ

مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ﴿٧٠﴾

*"Na hakika tumewatukuza wanaadamu na tumewapa vya kupanda barani na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewatukuza kuliko wengi katika wale tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa (kabisa)." (17:70)*

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٩٤﴾

*"Bila shaka tumemuumba mwanaadamu kwa umbo lililo bora kabisa." (95:4)*

Pamoja na neema zilizoainishwa kwa upeo mpana katika aya (17:70), Mwanaadamu ameboreshwa kuliko viumbe wengine kwa kutunukiwa vipawa vya ziada vifuatavyo:

- ③ Akili inayomuwezesha kufikiri na kutafakari
- ③ Utambuzi wa ubinafsi unaomuwezesha kujitambua, kuyatambua mazingira yake na mahusiano yake na muumba na vile vyote Alivyoviumba
- ③ Kipawa cha elimu - uwezo wa kujielimisha na kuelimisha wengine.
- ③ Uhuru wa kuamua na kutenda.

Neema zote hizi ametunukiwa binaadamu ili aweze kufikia lengo la kuumbwa kwake ambalo ni kumuabudu Allah (s.w) katika

kila kipengele cha maisha yake (Qur'an 51:56) na kisha kuwa Khalifa katika jamii. Hivyo, binaadamu atakuwa ni mwenye kumshukuru Allah (s.w) iwapo atamuabudu Allah (s.w) ipasavyo katika kila kipengele cha maisha yake na atakuwa ni mwizi wa fadhila endapo atatakabari na kuwaabudu wengine kinyume na Allah (s.w).

Anaye shukuru kwa kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo anafanya hivyo kwa faida ya nafsi yake ya kuishi kwa furaha na amani katika maisha ya hapa duniani na kupata maisha bora zaidi huko akhera. Anayekufuru kwa kuacha kumuabudu Allah (s.w) iipasavyo, anaitia khasarani nafsi yake mwenyewe kwa kuishi maisha ya mashaka na khofu hapa duniani na kustahiki adhabu kali isiyo na mfano wake katika maisha ya akhera. Allah (s.w) hafaidiki kwa chochote kutokana na kushukuru kwetu na pia hapungukiwi na chochote kutokana na kukufuru kwetu. Allah (s.w) ameliweka hili wazi mara tu baada ya kutufahamisha lengo la kuumbwa kwetu.

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾ مَا أُرِيدُ مِنْهُمْ مِّن رِّزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَنْ يُطْعَمُوا ﴿٥٧﴾ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ ﴿٥٨﴾

*"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu. Sitaki kwao riziki wala Sitaki wanilishe. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ndiye Mtoaji wa riziki, Mwenye nguvu, Madhubuti". (51:56-58).*

### **(b) Kujiepusha na Shirk**

Shirki ni kitendo chochote cha kukipa kiumbe nafasi ya Allah (s.w) katika **dhati yake, Sifa zake, Mamlaka yake na Hukumu zake.**

Allah (s.w) aliyemuumba binaadamu na viumbe vyote vilivyo mzunguka kwa lengo, ndiye mwenye Haki na Uwezo pekee wa

kumuwekea mwanaadamu mwongozo wa maisha utakao muwezesha kuishi kwa furaha na amani katika maisha ya hapa duniani na maisha ya baadaye huko akhera.

Yeyote yule katika viumbe atakayechukua au kupewa nafasi ya Allah (s.w) katika kutoa kanuni, sheria na mwongozo wa maisha ya binaadamu katika jamii, atakuwa amechukua au amepewa mamlaka ambayo hana uwezo nayo na kwa vyovyote vile atakuwa ameitumbukiza jamii katika **Kiza** cha **Khofu** na **Huzuni** kinachosababishwa na **dhuluma** za aina mbalimbali. Allah (s.w) analiweka hili wazi katika aya zifuatazo:

لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ ۚ قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ ۚ فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ  
وَيُؤْمِنْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ لَهَا ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ  
عَلِيمٌ ﴿٢٥٦﴾ اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ آمَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ  
وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ  
إِلَى الظُّلُمَاتِ ۗ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

*"Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini. Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkataa shetani na akamwamini Mwenyezi Mungu, bila shaka yeye ameshika kishiko chenye nguvu kisichokuwa na kuvunjika. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia mwenye kujua.."*

*"Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa wale walioamini. Huwatoa katika **giza** na kuwaingiza katika **nuru**. Lakini waliokufuru, walinzi wao ni matwaghuti. Huwatoa katika **nuru** na kuwaingiza katika **giza**. Hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele." (2:256-257).*

Hivyo kwa mnasaba wa maelezo haya na aya tulizozirejea, tunajifunza kuwa chanzo cha dhuluma zote anazofanyiwa

binaadamu na binaadamu mwenziwe zimetokana na kumshirikisha Allah (s.w) ama katika Dhati yake, Sifa zake, Mamlaka yake au katika Hukumu zake.

**(c) Kuwafanyia Wema Wazazi**

Allah (s.w) anatuusia kuwafanyia wema wazazi wawili na hasa kuzidisha wema zaidi kwa mama kwa sababu za msingi ambazo Allah (s.w) mwenyewe anatukumbusha.

حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهَيَّأَ عَلَيَّ وَهَنًا وَفَصَلَّتْهُ فِي

عَامَيْنِ .....

“..... *Mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na (kumnyonyesha na kuja) kumwachisha kunyonya katika miaka miwili.....*” (31:14).

حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا

وَحَمَلُهُ وَفَصَلَّتْهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا

“.....*Mama yake amechukua mimba yake kwa taabu na akamzaa kwa taabu. Na kubeba mimba yake hata kumwachisha ziwa (uchache wake) ni miezi thelathini (30).....*” (46:15).

Namna ya kuwafanyia wema wazazi kumefafanuliwa vyema katika mafunzo ya Surat Bani Israil tuliyoyapitia nyuma.

**(d) Kutowatii Wazazi katika kumuasi Allah (s.w)**

*"Na (wazazi wako) wakikushurutisha kunishirikisha na (yale) ambayo huna ilimu nayo, usiwatii; lakini kaa nao kwa wema hapa duniani (Maadamu ni wazee wako, ila usiwafuate tu mwenendo wao mbaya); Shika mwenendo wa wale wanaoelekea kwangu, kisha marejeo yenu ni kwangu, hapo nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda."* (31:15).

Aya inabainisha wazi kuwa hatupaswi kuwatii wazazi wetu pale watakapotuamrisha kumuasi Allah (s.w). Tukiwatii tutakuwa tumemshirikisha Allah (s.w) kwa kuwafanya wazazi wetu miungu badala yake kama inavyo bainika katika Qur'an.

أَتَّخِذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرَهْبَنَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ .....

*"Mayahudi na Wakristo) wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Allah (s.w)...." (9:31)*

Iliposhushwa aya hii Adi bin Hatimu (r.a) ambaye alisilimu kutoka kwenye Ukristo, alimtaka Mtume (s.a.w) atoe ufafanuzi kwa sababu alidai kuwa kinadharia hawakuwa wanawafanya watawa wao miungu. Katika kufafanua, Mtume (s.a.w) alimuuliza Adi, "Je hawakuwa watawa wenu wanawahalalishia alivyo viharamisha Allah (s.w) na nyinyi mkawatii?" Alijibu Adi, "Ndiyo" Mtume (s.a.w) akamuuliza tena, "Je watawa wenu hawakuwa wanakuharamishieni alivyo halalisha Allah (s.w) na nyinyi mkawatii? Adi akajibu tena "Ndiyo." Basi Mtume (s.a.w) akasema, "Huko ndio kuwafanya miungu".

Hivyo, kumtii mzazi au kiongozi au yeyote yule katika kumuasi Allah (s.w) ni kumfanya mungu badala ya Allah (s.w). Pia ukitii matashi ya nafsi yako kinyume na amri au makatazo ya Allah (s.w) utakuwa umeifanya nafsi yako mungu badala ya Allah (s.w).

أَرَأَيْتَ مَنِ اتَّخَذَ إِلَهَهُ هَوَاهُ أَفَأَنْتَ تَكُونُ عَلَيْهِ وَاكِيلًا ﴿٤٣﴾

*"Je, umemuona yule aliyefanya matamania yake, (kile anachikipenda), kuwa Mungu wake? Basi je, utaweza kuwa mlinzi wake (ukamhifadhi na hayo, na hali ya kuwa hataki?)."(25:43).*

Lakini, tunaamrisha katika aya hii (31:15) kuwa pamoja na kutowatii wazazi wetu katika kumshirikisha Allah (s.w), tusiwe jeuri na fedhuli kwao, bali tuzungumze nao kwa upole kwa kauli njema

na tuendeleo kuwatii na kuwafanyia wema katika mambo yote ya halali.

Wakati mwingine wazazi wanaweza kutishia kuacha laana tutakapowakatalia kwa kauli nzuri kutowatii katika yale yatakayotupelekea kumuasi na kumshirikisha Allah (s.w). Tusiymbishwe na tishio hili kwa sababu marejeo yetu sote ni kwa Allah (s.w) na ni mjuzi kamili juu ya dhamira (nia) zetu na vitendo vyetu - "...kisha marejeo yenu ni kwangu, Hapo nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda" (31:15).

### **(e) Kutopupia dunia**

*"Ewe mwanangu! Kwa hakika jambo lolote lijapokuwa na uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya jabali au mbinguni au katika ardhi, Mwenyezi Mungu Atalileta (amlipe aliyefanya); bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo yaliyofichikana,(na) Mjuzi wa mambo yaliyo dhahiri"(31:16).*

Aya hii inatuhakikishia kuwa kila mtu amekadiriwa jambo lake na hapana yeyote na hila yoyote itakayomzuia mtu asipate kile alichokadiriwa kukipata au kumuwezesha mtu kupata kile ambacho hakukadiriwa. Pia aya ifuatayo inatuweka wazi zaidi:

﴿وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَىٰ آلِهِ

رِزْقُهَا.....﴾

*"Na hakuna mnyama yoyote (kiumbe chochote) katika ardhi ila riziki yake iko juu ya Mwenyezi Mungu....." (11:6)*

Kutokana na aya hii tunajifunza kuwa lengo la maisha yetu si kutafuta riziki na maslahi ya dunia bali vitu hivi ni vitendea kazi tu vyakutuwezesha kulifikia lengo kuu. Lengo letu kuu ni **kuusimamisha Uislamu katika jamii ili tuweze kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo** katika kila kipengele cha maisha yetu ya kibinafsi na ya kijamii ambalo ndilo lengo la kuumbwa kwetu.

Hivyo katika mchakato wa kuliendea lengo hili la **kusimamisha Uislamu katika jamii**, tusimchelee yeyote wala tusichelee kupoteza chochote kwani hamna mwenye uwezo wa kutupokonya au kutuzidishia chochote kile kinyume na alivyotukadiria Allah (s.w). Katika hili ni vyema tukazingatia pia aya ifuatayo:

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّنْ قَبْلِ أَنْ نَّبْرَأَهَا إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾

*Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwishaandikwa katika Kitabu (cha Mwenyezi Mungu) kabla Hatujaumba. Kwa yakini hili ni sahali kwa Mwenyezi Mungu." (57:22).*

**(f) Kusimamisha Swala**

Swala iliyosimamishwa vilivyo ndiyo nyenzo kuu ya kumtakasa Muislamu na kumpa sifa zinazomuwezesha kustahiki kufanya kazi takatifu ya **kusimamisha Uislamu katika jamii**. Swala ikisimamishwa vilivyo humuwezesha mja kumcha Allah (s.w) ipasavyo katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na pia ni msingi wa kumpelekea mja **kusimamisha Uislamu katika jamii**.

**(g) Kuamrisha mema na kukataza mabaya na kusubiri juu yale yatakayokusibu**

Kuamrisha mema na kukataza maovu ni masuala yanayohitaji mamlaka na nguvu (authority and power). Hata hivyo kuwa na mamlaka na nguvu sio lazima ianzie kileleni katika ngazi ya Dola, bali **mamlaka na nguvu** ya kuamrisha mema na kukataza mabaya huanzia kwa mtu binafsi, kisha kwa familia yake kisha kwa ndugu na jamaa zake wa karibu. Kuamrisha mema na kukataza maovu ni wajibu kwa waumini wote (Qur'an 3:104, 3:110, 8:25, n.k).

Kuamrisha mema na kukataza maovu ni suala la mapambano

hata katika ngazi ya mtu binafsi na katika ngazi ya familia. Ni shughuli inayohitajia kuwa na subira ya hali ya juu. Subira ina maana pana ikiwa ni pamoja na:

1. Wewe mwenye kubakia na msimamo wa kufanya mema na kujiepusha na maovu
2. Kuwahimiza na kuendelea kuwashupalia kufanya mema na kuacha maovu wale ambao unamamlaka juu yao.
3. Kuwa tayari kulaumiwa na yeyote atakayelaumu.
4. Kuwa tayari kukabiliana na magumu yoyote yatakayokufika.
5. Kutotarajia kupata matunda ya haraka haraka kutokana na kazi ya kuamrisha mema na kukataza mabaya.

### **(h) Kujiepusha na Kibri na Majivuno**

*"Wala usiwatizame watu kwa upande mmoja wa uso (usiwafanyie watu jeuri) Wala usiende katika nchi kwa maringo; Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye" (31:18)*

*"Wala usitembee (usiende) katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala huwezi kufikia urefu wa mlima. Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola wako" (17:37-38)*

Kibri ni tabia ya **kukataa ukweli na kuwadharau watu** kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:

*"Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa, Mtume wa Allah amesema, "Yule ambaye moyoni mwake mnachembe ya kibri hataingia peponi" Swahaba mmoja akauliza: "Je kama mtu anapenda nguo nzuri na viatu?" Mtume (s.a.w) akasema, "Allah (s.w) ni mzuri na anapenda vizuri. Kibri ni kukataa ukweli na kupuuza watu". (Muslimu)*

Vile vile **kibri** na **majivuno** ni tabia ya kishirikina kama



tunavyojifunza katika Hadithi nyingine ifuatayo:

*"Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema; Allah akasema; Utukufu ni nguo yangu na kibri ni kilemba changu. Yeyote atakaye shindania kimoja wapo katika hivi ataangamia."  
(Muslimu)*

Mtu mwenye kibri na majivuno daima atakuwa ni mpinzani wa harakati za kusimamisha Uislamu katika ardhi, kwani atapendelea utawala ule ambao utamfanya kuwa mungu katika jamii.

### **(i) Kushika mwenendo wa kati**

*"Na ushike mwenendo wa kati...." (31:19)*

Mwenendo wa kati ni mwenendo ulioepukana na **kibri** na **majivuno** kwa upande mmoja na ulioepukkana na **udhalili** na **unyonge** kwa upande mwingine. Kama ilivyo vibaya kwa mtu kujikweza na kujivuna mbele ya wengine ndivyo ilivyo vibaya kwa mtu kujidhalilisha na kujinyengesha mbele ya wengine. Muislamu anahaki ya kujidhalilisha na kujinyengesha kwa **mmoja** tu, ambaye ni **Allah (s.w)**. Hivyo kujinyengesha na kujidhalilisha kwa yeyote awaye ni **Shirk**.

### **(j) Kushusha sauti**

*'.....na uteremshe sauti yako; bila shaka sauti ya punda ni mbaya kuliko sauti zote" (31:19)*

Kushusha sauti ni kuzungumza kwa sauti ya heshima ambayo itawavuta wasikilizaji na kuwawezesha kupata ujumbe uliokusudiwa kwa dhana iliyo kusudiwa. Sauti ya punda ni sauti ya kufoka au kuonesha dharau, sauti ambayo haiwezi kufikisha ujumbe uliokusudiwa katika dhana iliyo kusudiwa. Pia katika kuzungumza na watu tunatakiwa tuchukue sauti ya kati na kati. Tusizungumze kwa kufoka au kupaza sauti kiasi cha kuwakera wasikilizaji, pia tusizungumze kwa sauti ndogo na ya kunyanyapaa

kiasi cha kuwafanya wasikilizaji wasisikie vizuri au kuelewa dhana halisi ya ujumbe uliokusudiwa kufikishwa. Mlinganiaji ujumbe, hanabudi kuifahamu vyema hadhira yake na kuifikishia ujumbe anaokusudia kwa heshima na kwa sauti ya wazi inayozingatia hadhira.

**(4). Al-ahqaaf (46:15-18)**

وَوَصَّيْنَا الْإِنسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا  
 وَحَمْلُهُ وَفِصْلُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَبَلَغَ أَرْبَعِينَ سَنَةً  
 قَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ وَأَنْ  
 أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ وَأَصْلِحْ لِي فِي ذُرِّيَّتِي إِنِّي تُبْتُ إِلَيْكَ وَإِنِّي مِنَ  
 الْمُسْلِمِينَ ﴿١٥﴾

*Na tumemuusia mwanaadamu afanye wema kwa wazazi wake. Mama yake amechukua mimba yake kwa taabu na akamza kwa taabu. Na kubeba mimba yake hata kumwachisha ziwa; (uchache wake) ni miezi thelathini. Hata anapofikia baleghe yake na akawa mwenye umri wa miaka arubaini, (mtoto mwema) husema: "Ee Mola wangu! Niwezeshe nishukuru neema zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na niwezeshe nifanye vitendo vizuri unavyovipenda, na unitengenezee watoto wangu; kwa yakini ninatubu kwako; na hakika mimi ni miongoni mwa waliosilimu (walionyenyekae)." (46:15).*

أُولَئِكَ الَّذِينَ نَتَقَبَّلُ عَنْهُمْ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا وَدَتَجَاوَزُ عَنْ سَيِّئَاتِهِمْ  
 فِي أَصْحَابِ الْجَنَّةِ وَعَدَّ الصِّدْقِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿١٦﴾

*Hao ndio tunaowakubalia vitendo vyao vyema walivyovifanya, na tunayapita kando makosa yao,*

(*tunayasamehe*); (*watakuwa*) miongoni mwa watu wa *Peponi*: miadi ya kweli waliyoahidiwa. (46:16).

وَالَّذِي قَالَ لِيَا وَيْلَيْهِ أَفٍ لَّكُمْ أَتَعِدَانِي أَنْ أُخْرَجَ وَقَدْ خَلَتِ الْقُرُونُ مِنْ

قَبْلِي وَهُمَا يَسْتَعْجِلَانِ اللَّهَ وَيْلَكَ ءَامِنٌ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ فَيَقُولُ مَا هَذَا

إِلَّا اسْتَطِيرَ الْأُولِينَ ﴿١٧﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي أُمَمٍ قَدْ

خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ إِنَّهُمْ كَانُوا خَسِرِينَ ﴿١٨﴾

*Na ambaye anawaambia wazazi wake: "Kefule nyi! Oh! Mnanitishia kuwa nitafufuliwa; na hali karne nyingi, (watu wengi) zimekwisha pita kabla yangu (wala hazikufufuliwa)?" Na hao (wazee wake) wawili huomba msaada wa Mwenyezi Mungu; (na humwambia mtoto wao:) "Ole wako! Amin (haya unayoambiwa). Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli." Lakini yeye husema: "Hayakuwa haya (mnayoyasema) ila ni visa vya watu wa kale (tu si maneno ya kweli)."*

*Hao ndio ambao imelazimika hukumu juu yao (ya kutiwa Motoni, pamoja na mataifa yaliyopita kabla yao ya majini na watu, hakika hao ndio waliojitia khasarani. (46:17-18)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa:

- (a) Hatunabudi kuwafanyia wema wazazi wawili na hasa mama ambaye anapata dhiki kubwa katika kutuzaa na kutunyonyesha mpaka kufikia umri wa miaka miwili.
- (b) Hatunabudi kumshukuru Allah (s.w) kwa kutuneemesha kwa neema mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuwapa wazazi wetu moyo wa huruma na mapenzi ya kutulea mpaka kufikia utu uzima.
- (c) Pamoja na kumshukuru Allah (s.w), hatunabudi kuwashukuru wazazi wetu kwa kutulea kwa huruma na

mapenzi. Shukrani zetu kwao tutazidihirisha kwa kuwatii, kuwafanyia ihsani na kuwaomba dua na maghfira kwa Allah (s.w).

- (d) Hatuna budi kujiepusha mbali na kuwafanyia wazazi wetu ufedhuli na jeuri. Tuisubutu hata kuwagunia.
- (e) Hatunabudi kuomba kizazi chema na kumuomba Allah (s.w) atuwezeshe kukilea vyema kizazi chetu.
- (f) Hatunabudi kufuatilia kwa makini usia mwema wanaotupa wazazi wetu.
- (g) Hatunabudi kuleta toba na kuomba maghfira mara kwa mara (angalau kila siku mara mia moja).

### (5) Al-Hujurat (49:1-13)

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيْ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۗ  
إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ  
فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ ۗ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ  
أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٢﴾

*Enyi mlioamini! Msitangulize (neni leni) mbele ya (neni la) Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na Mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. Enyi mlioamini! msipaze sauti zenu kuliko sauti ya Mtume wala msiseme naye kwa sauti ya nguvu kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikakosa thawabu, na hali hamtambui. (49:1-2)*

إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَٰئِكَ  
 الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِتَقْوَىٰ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ  
 ﴿٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِنْ وَرَاءِ الْحُجُرَاتِ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٧﴾  
 وَلَوْ أَنَّهُمْ صَبَرُوا حَتَّىٰ تَخْرُجَ إِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ  
 رَّحِيمٌ ﴿٨﴾

*Kwa hakika wale wanaoangusha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa kumuogopa Mwenyezi Mungu. Basi yatakuwa kwao maghufira na thawabu kubwa (kabisa). Wale wanaokwita nyuma ya nyumba; (uko ndani kwako, wanakuja kukugongea dirisha na kukwita); wengi wao hawafahamu (adabu). Na kama wangalingoja mpaka uwatokee, ingekuwa bora kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghufira (na) Mwenye rehema. (49:3-5)*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنْ جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَأٍ فَتَبَيَّنُوا أَنْ تُصِيبُوا  
 قَوْمًا بِجَهَنَّةٍ فَتُصِيبُوا عَلَىٰ مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِينَ ﴿١﴾ وَأَعْلَمُوا أَنَّ فِيكُمْ  
 رَسُولَ اللَّهِ لَوْ يُطِيعُكُمْ فِي كَثِيرٍ مِّنَ الْأَمْرِ لَعَنِتُّمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ حَبِيبٌ  
 إِلَيْكُمْ إِلَيْمَنَ وَرَيْتَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَتْ إِلَيْكُمْ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ  
 وَالْعِصْيَانَ أُولَٰئِكَ هُمُ الرَّاشِدُونَ ﴿٢﴾

*Enyi mlioamini! Kama fasiki, (asiyekuwa wa kutegemewa) akikujieni na habari (yoyote ile msimkubalie tu) bali pelelezeni (kwanza), msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda. Na jueni ya kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko pamoja na nyiye. (Basi msikilizeni yeye anavyokuambieni). Lau yeye angekutiini katika mambo mengi (mnaoyasema) bila shaka*

*mngetaabika. Lakini Mwenyezi Mungu ameupendezesha kwenu Uislamu na ameupamba nyoyoni mwenu, na amekufanyeni mchukie ukafiri na ufasiki na uasi. Hao ndio walioongoka.(49:6-7)*

فَضْلًا مِّنَ اللَّهِ وَنِعْمَةً وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٨﴾ وَإِنْ طَائِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ  
 اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا فَإِنْ بَغَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَى فَقْتُلُوا الَّتِي  
 تَبْغَى حَتَّى تَفِيءَ إِلَى أَمْرِ اللَّهِ فَإِنْ فَاءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ  
 وَأَقْسِطُوا إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٩﴾ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا  
 بَيْنَ أَخْوَيْكُمْ وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٠﴾

*Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na neema (zake mmpata haya). Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima. Na ikiwa makundi mawili katika waislamu yanapigana, basi fanyeni suluhu baina yao; na likiwa moja la hayo linamdhulumu mwenziwe, basi lipigeni lile linaloonea mpaka lirudie katika amri ya Mwenyezi Mungu. Na kama likirudi, basi yapataniheni baina yao kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaohukumu kwa haki. Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu; basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na Mcheni Mwenyezi Mungu, ili mrehemewe.(49:8-10)*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَسْخَرُونَ قَوْمًا مِّن قَوْمٍ عَسَىٰ أَن يَكُونُوا خَيْرًا  
 مِنْهُمْ وَلَا نِسَاءً مِّن نِّسَاءٍ عَسَىٰ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِنْهُنَّ وَلَا تَلْمِزُوا  
 أَنفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَرُوا بِاللِّقَابِ بئسَ الأَسْمُ الأَفْسُوقُ بَعْدَ الأَيْمَنِ وَمَن لَّمْ  
 يَتُوبْ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾

*Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao;*

*huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msitukanane kwa kabila, wala msiitane kwa majina mabaya (ya kejeli): Jina baya kabisa kuambiwa mtu ni asi baada ya kuwa ni Muislamu. (Na kufanya haya ni uasi) Na wasiotubu, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao).(49:11)*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ  
وَلَا تَجَسَّسُوا وَلَا يَغْتَب بَّعْضُكُم بَعْضًا أَيُحِبُّ أَحَدُكُمْ أَن يَأْكُلَ لَحْمَ  
أَخِيهِ مَيْتًا فَكْرِهُتُمُوهُ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ رَّحِيمٌ ﴿١٧﴾ يَتَأْتِيهَا  
النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا  
وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقَدُّكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ

*Enyi mlioamini! Jiepusheni sana na (kuwadhanja watu) dhana (mbaya) kwani (kuwadhanja watu) dhana (mbaya) ni dhambi. Wala msipeleleze (habari za watu).Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine. Je! Mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La, Hampendi; (Basi na haya msiyapende). Na Mcheni Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba (na) Mwingi wa kurehemu. Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja, Adamu) na (yule yule) mwanamke (mmoja; Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu basi; siyo mbaguane). Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari (za mambo yote). (49:12-13)*

## **Mafunzo**

Kutokana na aya tulizosisoma tunajifunza yafuatayo:

**Kwanza**, waumini wa kweli ni wale ambao hawafanyi jambo lolote kinyume na alivyo agiza Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

**Pili**, waumini wa kweli wanatakiwa wawe na adabu katika kuongea. Wakiongea na wakubwa zao ki-umri au kicheo, wanalazimika kushusha sauti zao.

**Tatu**, waumini wote ni ndugu moja na waislamu wameamrisha na Allah (s.w) kuudumisha udugu huu kwa kujizatiti katika kusuluhisha waliogombana wakiwa mmoja mmoja au katika kundi.

**Nne**, ili kudumisha udugu baina yao, waislamu wanaamrisha na Mola wao kujiepusha na uzushi, dharau, kutukanana, dhana mbaya, kusengenyana na kujiona na kujikweza.

**Tano**, waumini wanaaswa wasitoe hukumu dhidi ya watu kutokana na tetesi tu. Hawanabudi kufanya uchunguzi juu ya shutuma zilizokuja na kisha kutoa hukumu baada ya kupatikana ushahidi wa wazi

## **Muhtasari wa madili malezi ya jamii kama ilivyobainishwa katika Qur-an**

### **1. Bani-Israil (17:23-40)**

- (i) Kujiepusha na kumshirikisha Allah katika nyanja zote.
- (ii) Kuwafanyia wema wazazi na kusema nao kwa heshima.
- (iii) Kutowakemea wazazi, au kuonesha ishara ya ukaidi kwao, mfano kusema Ah!
- (iv) Kuwaonea huruma wazazi na kuwanyenyekea.



- (v) Kuwaombea dua wazazi.
- (vi) Kuwasaidia wenye shida.
- (vii) Kutotumia mali kwa ubadhirifu.
- (viii) Kujitaabisha katika kutafuta maisha ili kuwahudumia wazazi ipasavyo.
- (ix) Kujiepusha na ubakhili.
- (x) Kutowauwa watoto kwa kuhofia umasikini.
- (xi) Kujiepusha na zinaa kwani ni njia mbaya na ni uchafu.
- (xii) Kujiepusha na kula mali za yatima.
- (xiii) Kuchunga ahadi.
- (xiv) Kutimiza vipimo wakati wa kupima na kutumia mizani iliyo sawa au kipimo kilicho sawa.
- (xv) Kutofuata mambo usiyo na ilimu nayo, yaani kutofuata mambo kwa kibubusa

**2. An-Nuur (24:1-31,58-63)pamoja na (7:26),(33:32,59)**

- (i) Kujiepusha na zinaa.
- (ii) Tusifunge ndoa na wenza waovu.
- (iii) Kujiepusha kuwasingizia uovu waumini.
- (iv) Ni tabia njema kuwa mwenye kufanya toba mara kwa mara.
- (v) Tujiepushe na tuhuma mpaka tupate ushahidi.
- (vi) Kujitahidi kuwadhanja vyema waumini.
- (vii) Kujiepusha na kutangaza habari mbaya za watu.
- (viii) Kujiepusha na maovu na machafu (ni amali za shetani).
- (ix) Kujiepusha na jazba na viapo.
- (x) Kushikamana na kusamehe.
- (xi) Tusiingie majumba ya watu mpaka tupate ruhusa (tupige hodi).
- (xii) Tukiambiwa turudi tusingie basi turudi. Hakuna kupiga hodi kwenye majumba ya Ummah.
- (xiii) Kujiepusha na kutazama yale yaliyokatazwa na sheria ya Allah (s.w).
- (xiv) Kujiepusha na zinaa na kulinda tupu zetu.

- (xv)Kujisitiri kisheria na kuchunga mipaka ya mahusiano, sauti na mavazi.
- (xvi)Wanawake wakae na kujituliza majumbani kwao, wasitoke ila kwa dharura muhimu.
- (xvii)Kujitakasa kutokana na uovu na machafu.

### **3. Luqmaan (31:12-19)**

- (i) Kuwa na Hikma
- (ii) Kumshukuru Allah (s.w).
- (iii) Kutoa nasaha njema kwa watoto.
- (iv) Kutomshirikisha Allah (s.w), kwani ni dhambi kubwa.
- (v) Kuwafanyia wema (Ihsaan) wazazi wetu.
- (vi) Kutowatii wazazi kama wakitupeleka vibaya (wakitupelekea kumshirikisha Allah) lakini kukaa nao kwa wema.
- (vii)Kushika njia ya waja wema wanaoelekea kwa Allah.
- (viii)Kuwa na tahadhari katika kila jambo.
- (ix) Kuwa na yakini kuwa Allah (s.w), ndiye Mwenye kuruzuku na Mwenye kumlipa mja kile anachostahiki.
- (x) Kusimamisha swala.
- (xi) Kuamrisha mema.
- (xii)Kukataza mabaya.
- (xiii)Kuwa na subira katika yale yatakayotusibu.
- (xiv)Kutowatizama watu kwa dharau.
- (xv)Kutotembea katika ardhi kwa maringo.
- (xvi)Kujiepusha na majivuno na kujifaharisha.
- (xvii)Kushika mwendo wa kati na kati.
- (xviii)Kutopaza sauti, kujiepusha na tabia ya kupiga kelele.

### **4. Al-Ahqaaf (46:15-18)**

- (i) Kuwafanyia wema wazazi/walezi.
- (ii)Kumuomba Allah (s.w) atupe kizazi chema.
- (iii)Kufanya toba mara kwa mara.

- (iv) Kuwashukuru wazazi kwa kuwatii na kuwaombea dua na msamaha kwa Allah(s.w).
- (v) Kufuatilia kwa makini usia mwema wanaotupa wazazi.
- (vi)Kutowakaripia wazazi/walezi wetu au kuwafanyia mambo mabaya.

**5. Al-Hujurat (49:1-13) pamoja na (24:27-29),(33:53), (4:86)**

- (i) Kutotanguliza maneno/kauli mbele ya kauli ya Allah (s.w) na Mtume wake yaani tusifuute matashi yetu kinyume na maamrisha/matazo ya Allah(s.w) na mtume wake
- (ii) Tusipaze sauti zetu juu ya sauti za viongozi wetu.
- (iii) Kutowaita watu madirishani au kusema nao madirishani.
- (iv) Kufanyia uchunguzi taarifa yoyote kabla ya kuifanyia kazi.
- (v) Kupatanisha ndugu na jamaa kwa uadilifu.
- (vi) Kuunganisha udugu wa Kiislamu.
- (vii)Kujiepusha na dharau na kujiona (kujikweza).
- (viii)Kutoitana majina mabaya.
- (ix) Tusitukanane kwa makabila, rangi, taifa au vyeo n.k.
- (x) Kujiepusha na kuwadhania watu dhana mbaya.
- (xi) Kujiepusha na kupeleleza habari za watu.
- (xii)Kujiepusha na kusengenywa.
- (xiii)Kumcha Allah (s.w) ukweli wa kumcha).
- (xiv)Kupiga hodi majumba ya watu kabla ya kuingia na kuwatolea salamu wenyeji.
- (xv)Tunapokaribishwa majumbani mwa watu tushughulike na kile kilichotupeleka na tukimaliza tutawanyike.
- (xvi)Tukiongea na wanawake ambao si maharim zetu tuongee nao nyuma ya Pazia.

## Wajibu wa waumini katika jamii

Kutokana na mafunzo ya Qur'an, **wajibu mkuu** wa waumini ni **kuusimamisha Uislamu katika jamii** ili kuiwezesha jamii hiyo kuishi kwa furaha na amani na kuandaa mazingira yatakayo wawezesha waumini kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo katika kukiendea kila kipengele cha maisha yao ya kibinafsi na ya kijamii.

Ili kufikia lengo kuu la kusimamisha Uislamu katika jamii waumini wanawajibika kufanya mambo kadhaa kama yalivyoelekezwa katika Qur'an. Katika juzuu hii wajibu wa waumini katika jamii unaainishwa kupitia aya za Sura zifuatazo:

1. Al-Imran (3:100-120)
2. An-Nisaa (4:71-87)
3. Al-Anfal (8:59-66)
4. At-Tawba (9:1-29, 38-42, 111-112)
5. Al-Hajj (22:78)
6. As-Saaf (61:1-14)

### 1. Al-Imraan (3:100-120)

Tukipitia kwa makini aya hizi (3:100-120) tunajifunza kuwa ili tuweze kuusimamisha Uislamu katika jamii hatuna budi kufanya yafuatayo:

#### (a) Kujiepusha na kuwatii baadhi ya wale waliopewa kitaab

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَطِيعُوا فَرِيقًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ يَرُدُّوكُمْ

بَعْدَ إِيمَانِكُمْ كَافِرِينَ ﴿١٠٠﴾

*"Enyi mlioamini! Mkiwatii baadhi ya wale waliopewa Kitabu, watakurudisheni kuwa makafiri baada ya Uislamu wenu". (3:100)*

Aya hii inatuhadarisha waumini kuwa ikitokea **tukawatii** baadhi ya wale waliopewa Kitabu, wataturudisha kuwa Makafiri

baada ya kuwa waumini. Ili kuelewa vyema tahadhari hii anayoitoa Allah (s.w) hatunabudi kuliingia kwa undani zaidi hili suala la kuwatii **baadhi ya Ah-lalkitaab.**

Kwa mujibu wa Qur'an Ahlalkitaab ni Mayahudi na Wakristo. Wameitwa Ah-lalkitaab kwa sababu wanadai kuwa na wao wanafuata dini ya Allah (s.w) iliyoshushwa kupitia kwa Mitume wa Allah (s.w) na vitabu walivyoshushiwa. Mayahudi wanadai kuwa wanafuata Taurati iliyoshushwa kwa Nabii Musa (a.s) na Wakristo wanadai kuwa manafuata Injili iliyoshushwa kwa Nabii Isa (a.s).

Wote Mayahudi na Wakristo wanadai kuwa chimbuko la dini hizi mbili ni Nabii Ibrahim (a.s) ambaye wanaamini kwamba ndiye chimbuko la Mitume wote wa Bani Israil kupitia kwa Is-haqa (a.s), mtoto wa pili wa Nabii Ibrahim (a.s). Israil ni jina la utani la Nabii Yakuub (a.s), mtoto wa Is-haqa (a.s). Pia Mayahud na Wakristo wanajua kupitia vitabu hivyo wanavyodai kuvifuata kuwa Nabii Ibrahim (a.s) ni chimbuko la Utume wa Mtume Muhammad (s.a.w) kupitia kwa Nabii Ismail (a.s), mtoto wa kwanza wa Nabii Ibrahim (a.s). Pamoja na madai yao haya Allah (s.w) anawapa changamoto katika aya zifuatazo:

مَا كَانَ إِبْرَاهِيمَ يَهُودِيًّا وَلَا نَصْرَانِيًّا وَلَٰكِن كَانَ حَنِيفًا مُّسْلِمًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٧﴾ إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ بِإِبْرَاهِيمَ لَلَّذِينَ اتَّبَعُوهُ وَهَذَا النَّبِيُّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاللَّهُ وَلِيُّ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٨﴾

*“Ibrahim hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu, mtii; wala hakuwa katika washirikina.”*

*“Watu wanaomkurubia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeye (katika zama zake) na Mtume huyu (Muhammad) na waliomwamini (Mtume huyu). Na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa wenye kuamini”.(3:67-68)*

Aya hizi zinawaweka Mayahudi na Wakristo katika changamoto kuwa kama kweli wanadai kuwa Nabii Ibrahimu (a.s) ndiye Baba wa Mitume mbona yeye hakuwa Myahudi wala Mkristo, bali alikuwa Muislamu (Mnyenyekevu kamili) kwa Allah (s.w). Uyahudi na Ukristo, umeibukia wapi? Allah (s.w) mjuzi wa mambo yote ya siri na ya dhahiri, anatoa changamoto nyingine kwa Mayahudi na Wakristo katika aya ifuatayo:

أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ حَضَرَ يَعْقُوبَ الْمَوْتُ إِذْ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعْبُدُونَ مِن بَعْدِي قَالُوا نَعْبُدُ إِلَهَكَ وَإِلَهَ آبَائِكَ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِلَهًا وَاحِدًا وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿١٣٣﴾

*"Je; (nyinyi Mayahudi na Wakristo) mlikuwapo yalipomfikia Yaaquub mauti, alipowaambia wanawe. 'Je, mtamuabudu nani baada yangu'?"*

*Wakasema; "Tutamwabudu Mola wako na Mola wa baba zako, Ibrahim, Ismail na Is-haqa; Mungu mmoja tu, na sisi tunanyenyekea (tumejisalimisha) kwake." (2:133)*

Ukweli unaodhihirishwa na historia ni kwamba Uyahudi na Ukristo ni dini walizoziunda Mayahudi kwa ufundi kwa kubadilisha mafundisho halisi ya vitabu vya Allah (s.w) vya Taurati, Zaburi, Injili na Suhufi na mafundisho halisi ya Mitume husika, kwa lengo la kupata maslahi ya dunia ya **kiuchumi** na **kiutawala** kwa njia za batili zisizoafikiana na mafundisho ya Allah (s.w) kupita kwa vitabu vyake na Mitume wake. Allah (s.w) amekuwa akiwaasa Mayahudi na Wakristo wa zama zote juu ya uovu wao huu wa kupotosha ukweli kwa maslahi madogo ya kidunia katika aya mbalimbali za Qur'an ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:

يَدْبِنِي إِسْرَائِيلَ أَذْكَرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَوْفُوا بِعَهْدِي  
 أَوْفِ بِعَهْدِكُمْ وَإِنِّي فَأَرْهَبُونَ ﴿٤٠﴾ وَعَامِنُوا بِمَا أَنْزَلْتُ مُصَدِّقًا لِمَا  
 مَعَكُمْ وَلَا تَكُونُوا أُولَٰ كَافِرٍ بِهِ ۗ وَلَا تَشْتَرُوا بِعَائِدَتِي ثَمَنًا قَلِيلًا وَإِنِّي  
 فَاتِقُونَ ﴿٤١﴾ وَلَا تَلْبَسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ

*"Enyi kizazi cha Israili (Nabii Yaaqub! Yaani Enyi Mayahudi!) Zikumbukeni neema zangu nilizokuneemesheni; na tekelezeni ahadi yangu (ya kuwa akija Mtume mtamfuata), nitatekeleza ahadi yenu (ya kukupeni Pepo); na niogopeni mimi tu."*

*"Na aminini niliyoyateremsha (kwa Muhammad) ambayo yanasadikisha yaliyo pamoja nanyi, wala msiwe wa kwanza kuyakataa. Wala msiyauze maneno yangu kwa ajili ya thamani ndogo tu (ya kilimwenguni); na niogopeni Mimi tu".*

*"Wala msichanganye haki na batili, na mkaficha haki, na hali mnajua" (2:40-42)*

Waliofanya kazi hii ya kiufundi ya kubadili mafundisho halisi ya Mwenyezi Mungu na Mitume wake si Mayahudi wala Wakristo wa kawaida, bali ni wataalamu (wanazuoni) na viongozi wao. Wataalamu na wakubwa wa Kiyahudi waliunda dini (mifumo ya maisha) za Kiyahudi na Kikristo ambazo ziliwataka wafuasi wake wazifuate kibubusa (Dogmatically) bila kuhoji ili wawanyonye na kuwakandamiza kiuchumi na kisiasa kirahisi. Ni kwa msingi huu, Karl Marx kwa kuurejea Ukristo na Uyahudi, alishutumu dini kuwa ni vyombo vilivyoundwa kwa ajili ya kurahisisha unyonyaji na ukandamizaji wa watu katika jamii kiuchumi na kisiasa. Pia hili la kufuata wanazuoni na viongozi wa jamii kibubusa, Allah (s.w) anawashutumu Wakristo na Wayahudi wa kawaida kama ilivyo katika aya ifuatayo:

*“(Mayahudi na Wakristo) Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu.....” (9:31)*

Katika ufafanuzi wa sehemu hii ya aya Mtume (s.a.w) anatumfahamisha kuwa kuwafanya wanazuoni na watawa Miungu ni kuwatii au kuwafuata kinyume na maamrisha na makatazo ya Allah (s.w). Daima, viongozi wa Kiyahudi na Kikristo wakiwemo wanazuoni na watawa wao, wako mbioni na hawalali katika harakati zao za kuongeza wigo wa Uyahudi na Ukristo katika ulimwengu ili kufikia ndoto yao ya kuutawala ulimwengu kiuchumi na kisiasa. Hawatarajii watu wote Ulimwenguni, wakiwemo Waislamu, kuwa Wakristo au Mayahudi wanaingia "**Makanisani**" na kwenye "**Masinagogi**", wanachotaka ni kuwafanya watu wote, pamoja na kuwa na dini zao, wafuate mifumo ya Kiyahudi na Kikristo katika kukiendea kila kipengele cha maisha ya jamii. Yaani wafuate mifumo ya Kiyahudi na Kikristo katika elimu, utamaduni, siasa, uchumi na mambo yote ya kijamii kwa ujumla.

Wanazuoni na Viongozi wa Kikristo na Kiyahudi, wanafahamu vyema kuwa kikwazo cha kufikiwa ndoto yao ya kuutawala Ulimwengu kiuchumi na kisiasa ni **Waislamu** wanaofuata vilivyo Qur'an na Sunnah. Wanawachukia mwisho wa kuwachukia Waislamu hawa wanaowaita kwa lugha zao za kipropaganda, "Siasa kali" Islamic terrorists, Islamic radicalists, Islamic fascists, Islamic extremists, Islamists, Jihadists, n.k. kwa sababu wanajua vyema hila zao na vitimbi vyao katika kuwanyonya na kuwakandamiza watu wanyonge katika Ulimwengu.

Pia wanajua fika kuwa Waislamu hawa wanaofuata vilivyo mafundisho ya Qur'an na Sunnah ya Mtume Muhammad (s.a.w), ndio pekee watakapo uokoa Ulimwengu na unyonyaji na ukandamizaji wa kisiasa na kiuchumi unaosababishwa na wao.



Kutokana na historia vile vile, Mayahudi na Wakristo, hawana kifua cha kupambana na Waislamu kwa uwazi. Bali katika kipindi chote cha historia wamekuwa wakifanya hila za kichini chini ikiwa ni pamoja na kuwafanya Waislamu marafiki kinafiki. Katika urafiki huu wa kinafiki hupenyeza hila zao na tamaduni zao ambazo hatimaye huwaingiza Waislamu katika mifumo yao ya kijamii na kuwabakisha tu na Uislamu wa binafsi wa kuswali, kufunga, kuhiji na wa matendo mengine ya Ibada binafsi kama hizo. Kwa kuchelea hila hizi za kifundi sana wanazozifanya viongozi na wanazuoni wa Kiyahudi na Kikristo Allah (s.w) ametutahaddharisha katika aya hii (3:100) kuwa tuwe macho na hila hizi za kiyahudi na Kikristo, kwani lengo lao ni kutufanya tufuate mfumo wao wa maisha unaopingana na mfumo wa maisha aliouweka na kuuridhia Allah (s.w), mfumo wa Uislamu.

Tukiwafuata tutakuwa tumemkufuru Allah (s.w) kama wao, pamoja na kuwa kibinafsi tutabakia na Uislamu wa majina na wa kuswali, kufunga, kuhiji, n.k Kwa ghiliba ya Mayahudi na Wakristo mara nyingi Waislamu wamekuwa wakiwafanya watu hawa marafiki zao wa ndani kwa tarajio la kupata ridhaa yao na kusalimika na uadui wao. Lakini, Allah (s.w) anatufahamisha kuwa, Maadamu pamoja na urafiki huo, tutataka kubakia na Uislamu wetu kibinafsi na kijamii, Mayahudi na Wakristo hawataturidhia, hata tukiwabeba kwa mbeleko.

وَلَنْ تَرْضَىٰ عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَىٰ حَتَّىٰ تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ ۗ قُلْ  
 إِنَّ هُدَىٰ اللَّهِ هُوَ الْهُدَىٰ ۗ وَلَئِنِ اتَّبَعْتَ أَهْوَاءَهُمْ بَعْدَ الَّذِي جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ

مَا لَكَ مِنَ اللَّهِ مِن وَّلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١٠٠﴾

*“Hawatakiwa radhi juu yako Mayahudi wala Wakristo mpaka ufuate mila yao. Sema: "Hakika uwongozi wa Mwenyezi Mungu ndio uwongozi (khasa)." Na kama ukifuata matamano yao baada ya yale yaliyokufikia ya ujuzi (wa kweli) hautapata msaidizi yoyote wala mlinzi kwa Mwenyezi Mungu". (2:120)*

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa Mayahudi na Wakristo wakiongozwa na wanazuoni wao na watawa wao, ni maadui wa dhahiri wa Uislamu na Waislamu wanaofuata Uislamu vilivyo. Ahlal-kitaabi wamejenga chuki na Uadui dhidi ya waumini kwa sababu za msingi zifuatazo:

1. Allah (s.w) amebainisha wazi dhamira yao na hila zao katika Qur'an
2. Waumini kwa kujua vyema dhamira na hila zao katika kuufisidi ulimwengu, ndio pekee wenye uwezo wa kuwahibiti na kujenga ulimwengu wa uadilifu na amani ya kweli.

Hivyo, Waislamu, tunatahadharishwa, tena na tena katika Qur'an kuwa tusithubutu kamwe kuwafanya Mayahudi na Wakristo kuwa rafiki zetu na wasiri wetu kwa sababu za msingi anazoziainisha Allah (s.w) katika aya zifuatazo:

يَتَّيِّهُهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا بَطَانَةً مِّن دُونِكُمْ  
لَا يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُؤًا مَا عَيْتُهُمْ قَدْ بَدَتِ الْبَغْضَاءُ مِنْ  
أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ إِن كُنْتُمْ  
تَعْقِلُونَ ﴿١١٨﴾

*“Enyi mlioamini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasiokuwa katika nyinyi: hao hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yale yanayokudhuruni. Bughudha (yao juu yenu) inadhihirika katika midomo yao. Na yanayofichwa na vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekubainishieni dalili (zote) ikiwa nyinyi ni watu wa kufahamu.”(3:118)*

هَذَاذَمُّكُمْ أَوْلَاءِ تُحِبُّونَهُمْ وَلَا يُحِبُّونَكُمْ وَتُؤْمِنُونَ بِالْكِتَابِ كُلِّهِ  
وَإِذَا لَقُواكُمْ قَالُوا آمَنَّا وَإِذَا خَلَوْا عَضُّوا عَلَيْكُمُ الْأَنَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ قُلْ  
مُوتُوا بِغَيْظِكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١١٩﴾

*Oh! Nyinyi mnawapenda (maadui zenu hao), hali wao hawakupendeni! Nanyi mnaamini vitabu vyote (chenu na vyao). Na wanapokutana nanyi husema, "Tumeamini". Lakini wanapokuwa peke yao wanakuumieni vyanda kwa chungu. Sema: "Kufeni kwa chungu wenu (huo); hakika Mwenyezi Mungu anayajua (hata) yaliyomo vifuani." (3:119)*

إِنْ تَمَسَسَكُمْ حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ وَإِنْ نَصَبَكُمْ سَيِّئَةٌ يَفْرَحُوا  
بِهَا وَإِنْ نَصَبُوا وَتَتَّقُوا لَا يَضُرُّكُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا إِنَّ اللَّهَ  
بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿١٢٠﴾

*"Ikikupateni kheri huwasikitisha. Na ikikupateni shari wanaifurahia. Na kama nyinyi mkisubiri na mkamcha Mungu hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua vizuri yote wanayoyatenda." (3:118-120)*

Katika aya ya (3:101) Allah (s.w) anawatabahisha waumini:

وَكَيفَ تَكْفُرُونَ وَأَنْتُمْ تُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ آيَاتِ اللَّهِ وَفِيكُمْ  
رَسُولُهُ ۗ وَمَنْ يَعْصِمْ بِاللَّهِ فَقَدْ هَدَىٰ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٠١﴾

*"Na mnakanushaje, hali nyinyi mnasomewa aya za Mwenyezi Mungu, na Mtume wake yuko pamoja na nyiye? Na Mwenyekumshika Mwenyezi Mungu sawa sawa, basi yeye amekwisha ongozwa katika njia iliyo nyooka." (3:101)*

Aya hii inawatanabahisha waumini kuwa, inakuwaje mnafuata mwenendo wa Kiyahudi na Kikristo na kuwafanya maadui zenu hawa kuwa marafiki zenu wa ndani, na ili hali Allah (s.w) na Mtume wake wamewabainishia kwa uwazi uadui wao dhidi yenu? Basi atakayewafuata Mayahudi na Wakristo baada ya kubainikiwa na ukweli huu atakuwa pamoja nao katika ukafiri. Na atakaye mtii Allah (s.w) na Mtume wake ipasavyo, kwa kuwakhaliifu Mayahudi na Wakristo na kufuata utaratibu wa maisha aliouweka Allah (s.w), atakuwa anafuata njia ya sawa sawa yenye kuleta furaha na amani ya kweli katika maisha haya ya Dunia na ya huko akhera.

**(b) Kumcha Allah (s.w) ipasavyo**

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تَقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُمْ مُسْلِمُونَ

*"Enyi mlioamini! Mcheni Allah (s.w) kama iapasavyo kumcha wala msife mpaka mmekwisha kuwa Waislamu kamili". (3:102)*

Kumcha Allah (s.w) kama ipasavyo kumcha ni kitendo cha makusudi cha kumtii Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na ya kijamii kwa kufuata maamrishi yake yote na kuacha makatazo yake yote kwa kuzingatia kanuni na taratibu alizotuwekea kupitia kwa mitume wake na vitabu vyake. Kwa mfano katika kutekeleza amri ya kusimamisha swala, tutahesabika kuwa tumemcha Allah (s.w) kama ipasavyo kumcha, iwapo tutatekeleza lbada hiyo kama alivyotuelekeza Mtume (s.a.w) kuanzia kwenye kutekeleza sharti za swala, nguzo za swala na kuwa na khushui inayotakikana. Utii huu kwa Allah (s.w) isiwe katika mazingira au katika nyakati fulani fulani tu bali iwe katika mazingira yote na katika maisha yote mpaka nukta ya mwisho ya uhai wa muumini. Ni kwa msingi huu Mtume (s.a.w) anasema,

*"Yule ambaye kauli yake ya mwisho itakuwa, "laailaahailallah" (Hapana mola ila Allah) ataingia peponi". (Abu Daud).*

Ukweli ni kwamba Waislamu hawataweza kuusimamisha Uislamu katika jamii mpaka kila Muumini ausimamisha Uislamu katika nafsi yake kwa kumcha Allah (s.w) kama ipasavyo kumcha katika kila kipengele cha maisha yake ya binafsi kwa kudhamiria na kufanya juhudi za makusudi na kubakia na msimamo huo kwa maisha yake yote. Na Muumini hataweza kumcha Allah (s.w) kama ipasavyo kumcha katika maisha yake yote pasina kuwa na elimu sahihi juu ya Uislamu. Tukumbuke kuwa elimu sahihi juu ya Uislamu ni elimu inayomuwezesha mja kujua lengo la kuumbwa kwake na lengo kuu la maisha yake na kumpa hamu na hamasa ya kuliendea.

**(c) Kushikamana pamoja katika Dini ya Allah (s.w)**

وَأَعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا وَاذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا وَكُنْتُمْ عَلَىٰ شَفَا حُفْرَةٍ مِنَ النَّارِ فَأَنْقَذَكُمْ مِنْهَا كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٠٣﴾

*“Na Shikamaneni kwa kamba (Dini) ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu. (Zamani) mlikuwa maadui, Naye akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema yake mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la moto (wa Jahannam), Naye akakuokoeni nalo. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubaishieni aya zake ili mpate kuongoka.” (3:103)*

Katika aya hii tunajifunza kuwa waumini wanawajibika kushikamana pamoja kwa kamba (habli) ya Mwenyezi Mungu. Kamba (habli) ya Mwenyezi Mungu, kwa kurejea tafsiri ya Qur'an si jengine bali lengo la kusimamisha Uislamu katika jamii. Kwa maana nyingine waumini wanawajibika kushikamana pamoja katika kuusimamisha

Uislamu katika jamii. Msisitizo wa mshikamano huu tunaupata pia katika aya zifuatazo:

*".....na Shikamaneni pamoja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu....." (22:78)*

*"Kwa yakini Mwenyezi Mungu anawapenda wale wanaopigana katika njia yake, safu safu (mkono mmoja); kama kwamba wao ni jengo lililokamatana barabara." (61:4)*

Kamwe, Waislamu hawataweza kushikamana na kuwa kitu kimoja kama watakuwa na malengo tofauti na lile la **kuusimamisha** au **kuutawalisha Uislamu katika jamii**. Kama Waislamu watatofautiana kimalengo, kwa mfano wengine wakawa na lengo la kunusuru Sunnah za ndevu na kukata suruali; wengine kuhuisha na kunusuru Maulid, wengine kuhuisha na kunusuru twarika za masheikh zao, wengine kuhuisha na kufuata misimamo ya maimamu wao wa kifiq-h, kamwe hawawezi kushikamana pamoja. Hivyo, ili Waislamu washikamane pamoja na kuwa Umma mmoja wenye nguvu, hawanabudi kutekeleza masharti matatu ya msingi yafuatayo:

- (i) Kuwa na lengo moja tu la **kuusimamisha Uislamu katika jamii** ambalo ndilo lengo la kuletwa Mtume Muhammad (s.a.w) - rejea Qur'an (9:33, 61:9),(48:28)
- (ii) Kufanyiana mambo mema kwa kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s.w)
- (iii) Kujiepusha na kufanyiana mambo mabaya ambayo ni sumu ya upendo na mshikamano baina ya Waislamu binafsi na katika makundi.

Ukirejea kwenye historia ya Aus na Khazraj, Makabila ya Kiarabu yaliyoishi Madina kwa uadui na uhasama uliodumu kwa muda mrefu, yaliungana na kuwa kitu kimoja baada ya kusilimu na kuwa pamoja na Mtume (s.a.w) katika lengo la kusimamisha Dola ya Kiislamu.

Waislamu wenye lengo moja la kusimamisha Uislamu katika jamii, sana sana wanaweza **kuhitalifiana** lakini sio **kufarakana** kutokana na tofauti za kimaumbile na za kivipaji. Waislamu wanaweza kutofautiana katika kutafsiri mambo mbali mbali kiutendaji.

Wakati wa Mtume (s.a.w) Maswahaba walihitalifiana kwa nia njema kabisa katika kutekeleza maagizo aliyowapa na bado akawakubalia wote kuwa wamepatia. Kwa mfano, mara tu baada vita vya Ahzab, Mtume (s.a.w) alitoa agizo kwa maswahaba kuwa wasiswali swala ya Alasiri ila katika eneo la Bani Quraizah. Walipofika njiani katika kuelekea kwa Bani Quraizah, Maswahaba wakaona alasiri inakaribia kwisha. Wakashauriana kuwa waswali pale lakini wakatofautiana katika hili. Wengine wakabakia na kauli ya Mtume (s.a.w) kuwa wasiswali alasiri ila katika eneo la Bani Quraizah. Kundi lingine likawa na tafsiri nyingine kuwa kauli ile ya Mtume (s.a.w) ilikuwa ni kuwahimiza wawahi lakini si kupitisha wakati wa swala wakirejea Qur'an:

*“..... kwa hakika swala kwa waumini ni faradh iliyowekewa nyakati makhsusi” (4:103).*

Hivyo, wakatofautiana, kundi moja likaswali pale njiani na lingine likaahiriisha na kuiswali swala hiyo nje ya wakati katika eneo la Bani Quraizah. Mtume (s.a.w) alipofikishiwa habari hii, aliyakubalia makundi yote mawili kuwa yalipatia. Katika historia ya Mtume (s.a.w) na maswahaba kuna mifano mingi ya maswahaba kuhitalifiana katika kutafsiri maagizo ya Mtume (s.a.w) na Mtume (s.a.w) akawa anakubaliana na khitilafu hizo.

Pia ukirejea historia ya Maimamu wanne mashuhuri wa fiq-h, Abu Hanifa, Malik, Shafii na Hambal, walitofautiana katika kutoa baadhi ya fatwa za kifiqh kulingana na uelewa na uoni wao katika kutafsiri aya na Hadith kiutendaji kulingana na mazingira yaliyowazunguka. Maimamu hawa pamoja na kuhitalifiana katika

baadhi ya fatwa za kifiqh, waliheshimiana na kushikamana katika lengo moja la kuhisha Uislamu na kuusimamisha katika jamii kama alivyoiacha Mtume Muhammad (s.a.w).

Waumini hawanabudi kuumia magego suala la mshikamano baina ya Waislamu kwa kujitahidi kushikilia lengo kuu la kusimamisha Uislamu katika jamii na kusahau hitilafu ndogo ndogo zisizo athiri kufikiwa kwa lengo kuu. Kwa upande mwingine, waumini hawanabudi kuwa macho sana na juhudi za kuwafarakanisha Waislamu zinazofanywa na maadui wa Uislamu. Hivi leo Waislamu wanafarakanishwa kwa kutumiwa Qur'an na Sunnah. Tumfanye adui dhahiri wa kusimama kwa Uislamu katika jamii yeyote yule anayewagawa Waislamu na kuwafarakanisha, hatakama atakuwa anatomia Qur'an na Hadith sahihi katika kufanya hivyo. Hao si katika Waislamu hatakama watajipachika sifa ya "Ah-lal-Qur'an wa Sunnah" kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

إِنَّ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيَعًا لَسْتَ مِنْهُمْ فِي شَيْءٍ إِنَّمَا أَمْرُهُمْ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿١٥٩﴾

*“Hakika wale waliofarikisha dini yao na wakawa makundi, huna uhusiano nao wowote. Bila shaka shauri yao (ya kuwaadhibu) iko kwa Mwenyezi Mungu; kisha (hapo wakati wa kuwaadhibu) atawaambia yale waliyokuwa wakitenda”. (6:159)*

Fikiria kama utakuwa "Answari Sunnah" lakini huna uhusiano na Mtume (s.a.w), itakuwaje? Pia wanao farakanisha Waislamu wameitwa washirikina pamoja na kujinakshi kwa "Uislamu safi" katika aya zifuatazo:

﴿٣٧﴾ مِنَ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيَعًا كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ ﴿٣٧﴾

*“Nyenyekeeni kwake na Mcheni, na simamisheni Sala, wala*



*msiwe katika washirikina" "Katika wale walioitenga dini yao na wakawa makundi makundi; kila kikundi kinafurahia kilicho nacho". (30:31-32)*

﴿ شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى وَعِيسَى أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ كَبُرَ عَلَى الْمُشْرِكِينَ مَا تَدْعُوهُمْ إِلَيْهِ اللَّهُ يَجْتَبِي إِلَيْهِ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ يُنِيبُ ﴿١٣﴾ وَمَا تَفَرَّقُوا إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَعْيَا بَيْنَهُمْ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى لَفُضِيَ بَيْنَهُمْ وَإِنَّ الَّذِينَ أُورِثُوا الْكُتُبَ مِنْ بَعْدِهِمْ لَفِي شَكٍّ مِنْهُ مِرْيَبٍ ﴿١٤﴾

*“Amekupeni Sharia ya dini ile ile aliyomuusia Nuhu na tuliyokufunulia wewe na tuliyowausia Ibrahimu na Musa na Isa, kwamba simamisheni dini wala msifarikiane kwayo, ni ngumu kwa wenye kushirikisha (dini hii) unayowaitia; Mwenyezi Mungu humchagua Kwake amtakaye na humuongoza Kwake aelekeaye (Kwake)”.*

*“Na hawakutengana (wakawa mapote mbali mbali yasiyopatana) ila baada ya kuwajia ilimu. (Na kama isingalikuwa kauli iliyotangulia kutoka kwa Mola wako (ya kuwa kuadhibiwa ni) mpaka muda wake uliowekwa, hukumu ingalitolewa (sasa hivi baina yao). Na kwa yakini wale waliorithishwa Kitabu baada yao (hao waliopita), wanakitilia shaka inayowahangaisha.” (42:13-14)*

Hivyo, Allah (s.w) anawaonya waumini.

﴿ وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ تَفَرَّقُوا وَاخْتَلَفُوا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَاتُ وَأُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٥﴾

*“Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kukhitalifiana baada ya kuwafikia dalili zilizo wazi (za kuwakataza hayo). Na hao ndio watakaokuwa na adhabu kubwa.” (3:105)*

#### **(d) Kuwa na Vikundi vya Kiharakati**

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ

الْمُنْكَرِ ۚ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

*“Na wawepo katika nyinyi (kundi la) watu wanaolingania kheri (Uislamu), wanao amrisha mema na kukataza maovu. Na hao ndio watacao tengenekewa.” (3:104)*

Katika aya hii Allah (s.w) anatoa agizo kwa waumini la kuwepo vikundi vya kiharakati katika jamii ya Waislamu, vitakavyo kuwa chachu ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Vikundi hivi vya kiharakati vitakuwa na kazi kubwa tatu ambazo zitafanywa katika ushirikiano.

#### **(i) Kulingania Kheri**

Kuwalingania watu kheri (Yyad-u'una ila l-khayri) ni kuwafikishia watu ujumbe sahihi wa Uislamu utakao wawezesha kuufahamu Uislamu katika uhalisia wake na kuwapa hamu na hamasa ya kuutekeleza katika maisha yao yote ya kibinafsi na ya kijamii.

Hivyo, ili kazi hii ya kulingania ifanikiwe, mlinganiaji mwenyewe hanabudi **kwanza**, kuufahamu kwa usahihi wake huo Uislamu anaoulingania na **pili**, hanabudi kuuingiza katika matendo na kuwa kiigizo chema, kabla hajaanza kuulingania.

#### **(ii) Kuamrisha mema**

Mema ni yale yote mazuri anayo yaridhia Allah (s.w) na Mtume wake ambayo yakitekelezwa vilivyo hujenga mazingira ya

furaha na amani katika jamii. Miongoni mwa mambo mema ni pamoja na yale Allah (s.w) na Mtume (s.a.w) waliyoamrisha ya fanywe. Waislamu wanatakiwa wawe viigizo vyema vya kutenda wema katika jamii kabla hawajaanza kuwaamrisha wengine kufanya wema huo. Waislamu wanatakiwa wawe ni mfano wa kuigwa katika kutoa huduma za kijamii. Wasio Waislamu hawataweza kuuona uzuri wa uislamu kindharia pasina kuuona kimatendo.

**(iii) Kukataza Maovu**

Maovu ni yale yote mabaya aliyoyakataza Allah (s.w) na Mtume wake ambayo yakiachiwa huiathiri jamii na kuitumbukiza katika mazingira ya khofu na huzuni. Wanaharakati, ili wafanikiwe kuondoa maovu katika jamii hawanabudi wao wenyewe kuwa katika mstari wa mbele katika kujiepusha na maovu.

وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ﴿٥﴾

“Na mabaya yaepuke.” (74:5)

Haya mambo matatu ya kulingania kheri, kuamrisha mema na kukataza maovu, hayaanzii kwenye ngazi ya dola bali yanatakiwa yaanzie chini kwenye ngazi ya mtu binafsi, familia, ndugu na jamaa wa karibu, mtaani na hivyo hivyo hatua kwa hatua mpaka kwenye ngazi ya taifa na kimataifa.

**(e) Kusimamisha Uislamu katika Jamii**

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ  
عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَوْ آمَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ  
خَيْرًا لَهُمْ مِّنْهُمْ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿١١٠﴾

“Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishiwa watu (ulimwenguni) -mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza

*yaliyo maovu, na mnamwamini Mwenyezi Mungu. Na kama wale waliopewa Kitabu wangu aliadini (kama walivyoaamrisha) ingalikuwa bora kwao. (Lakini) miongoni mwao wako wanaoamini; na wengi wao wanatoka katika taa ya Mwenyezi Mungu." (3:110).*

Kwa mujibu wa aya hii Umma wa Waislamu hautakuwa bora kuliko umma nyingine katika jamii kwa kuongeza idadi ya misikiti na kutekeleza Ibada binafsi za Swala, Swaumu, Hija, n.k., bali utakuwa bora pale utakapo simamisha Uislamu katika jamii na kuwa na uwezo wa kuamrisha na kudumisha mema yatakayo boresha ustawi wa jamii na kujenga mazingira ya furaha na amani kwa wanajamii wote pasina ubaguzi wa aina yoyote.

Pia Umma wa Waislamu utakuwa bora pale utakapochukua dhima ya kuondoa na kuzuia maovu yasiendeke katika jamii.

Umma wa Waislamu utakapo simamisha Uislamu katika jamii hautakuwa bora tu juu ya Umma nyingine bali utakuwa bora hata mbele ya Allah (s.w) kwa kuwa utakuwa unamuaabudu kisawasawa katika kila kipengele cha maisha ya binafsi na ya jamii kama inavyo bainika katika aya ifuatayo:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي  
 الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي  
 ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي  
 شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٥٥﴾

*"Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioaamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia dini yao aliyowapedelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu*

yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo; basi hao ndio wavunjao amri zetu". (24:55).

## **2. An-Nisaai (4:71-87)**

Tukipitia kwa makini aya hizi (4:71-87) tunapata ujumbe kuwa ili waumini waweze kusimamisha Uislamu katika jamii hawanabudi kuzingatia na kufanya yafuatayo:

### **(a) Kushika tahadhari juu ya Maadui**

..... يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا خُذُوا حِذْرَكُمْ

*"Enyi mlioamini! Shikeni hadhari yenu (juu ya Maadui zenu, Msihadaike)..." (4:71)*

Aya hii inawaamrisha waumini wachukue tahadhari juu ya Maadui zao. Kuchukua tahadhari ni pamoja na kufanya yafuatayo:

### **(i) Kuwajua Maadui wa Uislamu na Waislamu**

Maadui wa Uislamu na Waislamu walioainishwa katika Qur'an na waliojitokeza katika muda wote wa historia ya binaadamu ni hawa wafuatao:

- Shaitwaani
- Makafiri na Washirikina
- Mayahudi na Wakristo (Ah-lal-kitaab)
- Wanafiki

### **(ii) Kujua mbinu na hila za Maadui hao sita**

Mbinu na hila za maadui hao zimeainishwa vyema katika Qur'an. Hila na mbinu za maadui hawa pia zinatudhihirikia kila uchao na hasa pale waumini wanapodhamiria kusimamisha Uislamu katika jamii.

### (iii) Kutowafanya maadui hawa marafiki wa ndani.

Allah (s.w) anatutahadharisha kuwa maadui hawa wanatuhadaa kwa kutufanya marafiki ili waweze kutujua vyema na kutuzunguka kwa kirahisi. Allah (s.w) anatutahadharisha:

﴿يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَمَن يَتَوَلَّهُمْ مِنكُمْ فَإِنَّهُ مِنَّهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ

الظَّالِمِينَ ﴿٥١﴾

*“Enyi Mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa marafiki (wa kuwapa siri zenu); wao kwa wao ni marafiki. Na miongoni mwenu atakayefanya urafiki huo nao, basi huyo atakuwa pamoja nao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi (njia ya kheri) watu madhalimu.” (5:51)*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَكُمْ هُرُوعًا وَلَعِبًا  
مِّنَ الَّذِينَ ءَاثَرُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَالْكَفَّارَ أَوْلِيَاءَ وَاتَّقُوا اللَّهَ

إِن كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾

*“Enyi Mlioamini! Msiwafanye marafiki wale walioifanyia mzaha na mchezo dini yenu miongoni mwa wale waliopewa kitabu kabla yenu na miongoni mwa makafiri (wengine). Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini.” (5:57)*

### (iv) Kuwa Wasiri

Waumini wanatakiwa wajitahidi kuficha mipango na mikakati yao ya kuupeleka Uislamu mbele isiwafikie wasiohusika mpaka utakapofika muda wa kuliweka jambo hilo wazi. Siri za mipango na mikakati ya kuupeleka Uislamu mbele, zinatakiwa zibakie katika vifua vya wachache wanaohusika na upangaji na utekelezaji wa mipango hiyo katika hatua mbali mbali. Mipango na mikakati ifahamike tu pale itakapofikia kilele cha kuihusisha jamii.

### **(v) Kuwa Wasalama na Walinzi**

Kila mara Waislamu wanatakiwa wawe hadhiri kuwa wanao maadui wanaofuatilia harakati za Kiislamu usiku na mchana na muda wote wanapanga njama za kuwahilikisha Waislamu na Uislamu kama anavyotufahamisha Allah (s.w):

*“Wanataka kuzima Nuru ya Mwenyezi Mungu (ya Uislamu) kwa vinywa vyao; na Mwenyezi Mungu ataikamilisha Nuru yake japo kuwa makafiri watachukiwa”. (61:8)*

Hivyo Waislamu daima wanatakiwa wafuatilie miondoko ya maadui na wachukue tahadhari kubwa zaidi juu ya wanafiki ambao ni maadui wa ndani wa Uislamu na Waislamu. Waislamu wasichukue kila neno na kulifanyia kazi bila kulipima.

### **(vi) Kujiandaa kimazoezi na kisilaha**

Katika kuchukua tahadhari, waumini wanatakiwa waone kuwa wakati wowwote wanaweza kuvamiwa kwa kushitukizwa na maadui zao. Hivyo muda wote waumini wanatakiwa wafanye mazoezi ya kimwili wawe na siha nzuri na waweze kujihami pindi watakapo shambuliwa. Pia waumini wanaamrisha na Mola wao kujiandaa kwa silaha na mazoezi ya kivita vya kisasa (rejea Qur'an 8:60).

**(b) Kupigana vita na maadui pale inapobidi**

❖ فَلْيُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يَشْرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا بِالْآخِرَةِ وَمَنْ

يُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيُقْتَلْ أَوْ يَغْلِبْ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٧٤﴾

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ

وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ

أَهْلُهَا وَأَجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا وَأَجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ نَصِيرًا

*“Basi nawapigane katika njia ya Mwenyezi Mungu wale wanaouza maisha (yao) ya dunia kwa (kununua) ya Akhera. Na anayepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha akauawa au akashinda, tutampa ujira mkuu.”*

*Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu (katika kuwaokoa) wale walio dhaifu katika wanaume na wanawake na watoto ambao husema: “Mola wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu, na tujaalie tuwe tuna mlinzi anayetoka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anayetoka kwako.” (4:74-75)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa Waislamu wanalazimika kuingia vitani kwa sababu zifuatazo:

**(i) Kuwaokoa wanyonge wanaodhulimiwa katika jamii na mifumo kandamizi ya kitwaghuti.**

Hebu fikiria ukandamizaji ulipo ulimwenguni hivi sasa katika ngazi ya taifa na kimataifa! Hebu fikiri jinsi wananchi wenye uchumi duni wanavyo nyonyolewa na watoza kodi bila ya kupata huduma yoyote ya kijamii kwa manufaa ya kikundi kidogo cha watu! Hebu fikiria tena jinsi mataifa makubwa, Marekani, Uingereza, n.k.



yanavyonyonya na kukandamiza nchi maskini za Afrika, Latini Amerika, Mashariki ya kati, n.k, na jinsi mataifa haya yanapokataa kunyonywa na kukandamiza, yanavyo vamiwa kijeshi na kupigwa kama ilivyo tokea kwa Afghanistan, Iraq, n.k.

Katika mazingira haya Allah (s.w) anawashangaa Waumini:

*“Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu katika kuwaokoa wale walio dhaifu, katika wanaume, wanawake na watoto.....” (4:75)*

### **(ii) Kujihami na Maadui wa Uislamu**

*“Basi pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hukalifishwa ila nafsi yako. Nawahimize Waislamu. Huenda Mwenyezi Mungu akazuia mashambulio ya waliokufuru. Na Mwenyezi Mungu ndiye mkali wa kushambulia na mkali wa kuadhibu.” (4:84)*

Kawaida ya Allah (s.w), ni kwamba atawanusuru waumini pale watakapofanya jitihada za makusudi za kuinusuru Dini yake. Hivyo Waislamu wanaposhambuliwa na maadui zao na maadui wa Allah (s.w) wasirudi nyuma bali wapambane nao, na Allah (s.w) ameahidi kuwapa Waislamu ushindi. Pia Allah (s.w) anatumiza kupigana ili kujihami na maadui katika aya zifuatazo:

وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يُقْتُلُونَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ

الْمُعْتَدِينَ ﴿١٩٠﴾

*“Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, wala msipindukie mipaka (mkawapiga wasiokupigeni). Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi warukao mipaka.” (2:190)*

وَقَدِّلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةً وَيَكُونَ الدِّينُ لِلَّهِ فَإِنِ اٰنْتَهُوْا فَلَا

عُدُوْنَ اِلَّا عَلٰى الظَّالِمِيْنَ ﴿١٩٣﴾

*“Na piganeni nao mpaka kusiwe na mateso (wao kuwatesa Waislamu bure), na dini iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Na kama wakiacha basi usiweko auadui ila kwa madhalimu.” (2:193)*

### (iii) Kupigania Uhuru wa kuabudu

وَقَدِّلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةً وَيَكُونَ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ فَإِنِ اٰنْتَهُوْا

فَاِنَّ اِلٰهَ مَا يَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿٢١٤﴾

*“Na piganeni nao (makafiri) mpaka yasiweko mateso (nyinyi kuteswa na wao kwa ajili ya dini kama wanavyokuteseni sasa); na dini iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (asitaaradhiwe mtu kuabudu dini anayoitaka). Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyatenda.” (8:39)*

Kupigana vita vya jihadi kwa sababu hizi tatu za kuwawezesha Waislamu kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo, kusimamisha uadilifu katika jamii na kuuhami Uislamu usiporomoshwe baada ya kusimama, ni katika amali bora yenye malipo makubwa mbele ya Allah (s.w) kama tunavyojifunza katika Qur'an:

﴿ فَلْيُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللّٰهِ الَّذِيْنَ يَشْرُوْنَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا بِالْآخِرَةِ وَمَنْ

يُقَاتِلْ فِي سَبِيْلِ اللّٰهِ فَيَقْتُلْ اَوْ يَغْلِبْ فَسَوْفَ نُؤْتِيْهِ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿٧٤﴾

*“Basi nawapigane katika njia ya Mwenyezi Mungu wale wanaouza maisha (yao) ya dunia kwa (kununua) ya Akhera. Na anayepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha akauawa au akashinda, tutampa ujira mkuu.” (4:74)*

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ ﴿١٦٤﴾ فَرِحِينَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَيَسْتَبْشِرُونَ بِالَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُوا بِهِمْ مِنْ خَلْفِهِمْ أَلَّا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٦٥﴾ \*يَسْتَبْشِرُونَ بِنِعْمَةِ اللَّهِ وَفَضْلٍ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٦٦﴾

*“Wala usiwadhani wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu (maiti). Bali wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao.”*

*“Wanafurahia aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila Zake; na wanawashangilia wale ambao hawajajiunga nao, walio nyuma yao, (wako ulimwenguni, bado hawajafa); ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.”*

*“Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa wanaoamini.”*  
(3:169-171)

Chujio kubwa la kuwabainisha waumini na wanafiki ni kupigania Uislamu kwa mali na nafsi. Katika mambo mepesi mepesi wanafiki wanaweza kujiparagua na kuwepo na Waislamu pale ambapo wanaona hawapotezi lolote. Lakini pale penye mapambano halisi na penye uwezekano wa kupoteza maisha au maslahi ya dunia ambayo ndiyo lengo lao la maisha, wanafiki kamwe hawawezi kubakia. Allah (s.w) anatufahamisha:

الَّذِينَ آمَنُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ الطَّاغُوتِ فَقَاتِلُوا أَوْلِيَاءَ الشَّيْطَانِ إِنَّ كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا ﴿٧١﴾

“Wale walioamini wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini waliokufuru wanapigana katika njia ya Shetani. Basi piganeni na marafiki wa Shetani. Hakika hila za Shetani ni dhafu.” (4:76)

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ قِيلَ لَهُمْ كُفُّوا أَيْدِيَكُمْ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ  
وَأَتُوا الزَّكَاةَ فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ إِذَا فَرِيقٌ مِنْهُمْ يَخْشَوْنَ النَّاسَ  
كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً وَقَالُوا رَبَّنَا لِمَ كَتَبْتَ عَلَيْنَا الْقِتَالَ لَوْلَا  
أَخَّرْتَنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ ۗ قُلْ مَتَّعْتُكُمْ الدُّنْيَا قَلِيلًا وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لِّمَنِ اتَّقَىٰ  
وَلَا تُظَلَّمُونَ فِتْيَالًا ﴿٧٧﴾

“Huwaoni wale walioambiwa: “Izuieni mikono yenu (na kupigana na makafiri mpaka ije amri ya kupigana)? Na (sasa) simamisheni Sala, na toeni Zaka (tu).” Na (baadae) walipolazimishwa kupigana, mara kundi moja katika wao liliogopa watu (makafiri) kama kumwogopa Mungu au kwa khofu zaidi. Na wakasema: “Mola wetu! Kwa nini umetulazimisha kupigana? Lau ungetuakhirisha mpaka muda kidogo hivi (ingekuwa vizuri).” Sema “Starehe ya dunia ni ndogo. Akhera ni bora zaidi kwa hao wenye kumcha Mungu. Wala hamtadhulumiwa hata uzi ulio katika uwazi wa kokwa ya tende.” (4:77)

أَيُّنَمَا تَكُونُوا يُدْرِكُكُمْ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشِيدَةٍ وَإِن  
تُصِبْهُمْ حَسَنَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَإِن تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَقُولُوا  
هَذِهِ مِنْ عِنْدِكَ قُلْ كُلٌّ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ فَمَالِ هَٰؤُلَاءِ الْقَوْمِ لَا يَكَادُونَ  
يَفْقَهُونَ حَدِيثًا ﴿٧٨﴾

“Po pote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome

*madhubuti.* "Na kama ukiwafikia wema (wale wanafiki na makafiri) wanasema: "Huu umesababika kwa ajili yako (wewe Muhammad)." Sema: "Yote yametoka kwa Mwenyezi Mungu." Basi wamekuwaje watu hawa? Hawawezi kufahamu maneno? (4:78)

### **(c) Kumtii Allah (s.w), Mtume (s.a.w) na Viongozi wa Harakati**

مَنْ يُطِيعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ وَمَنْ تَوَلَّى  
فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا ﴿٨٠﴾

*"Mwenye kumtii Mtume amemtii Mwenyezi Mungu (kwani anayoyaamrisha Mtume yametoka kwa Mwenyezi Mungu). Na anayekengeuka (anajidhuru mwenyewe). Hatukukupeleka wewe kuwa mlinzi juu yao" (4:80)*

Siri ya mafanikio katika harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii iko kwenye kushikamana na kumtii Allah (s.w) na Mtume wake ipasavyo, kisha kuwatii vilivyo viongozi wa harakati pale wanapotuelekeza kusimamisha Uislamu kwa mujibu wa maongozi ya Qur'an na Sunnah. Hili la kuwatii viongozi wa kiharakati linasisitizwa katika Qur'an.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولَى  
الْأَمْرِ مِنْكُمْ فَإِن تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن  
كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

*Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenyemamlaka juu yenu, walio katika nyie (Waumini wenzenu). Na kama mkikhitalifana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hiyo ndiyo kheri, nayo ina matokeo bora kabisa." (4:59).*

Matokeo ya kumuasi Mtume (s.a.w) katika vita vya Uhud yaliyopelekea Waislamu kupata kipigo na kibano wasichokitarajia, hayataacha kuwafika Waislamu pale watakapo waasi viongozi wao baada ya kuwapa maelekezo halali ya kiharakati. Hivyo kumtii Allah (s.w) na Mtume wake ipasavyo pamoja na kuwatii viongozi wetu katika yale yote yanayowafikiana na Qur'an na Sunnah ni wajibu kwa waumini wenye lengo la kusimamisha Uislamu katika jamii.

### 3. Al-Anfal (8:59-66)

Tukipitia kwa makini aya hizi (8:59-66) tunajifunza kuwa ili waumini waweze kuusimamisha Uislamu katika jamii na kuudumisha, wanawajibika kufanya yafuatayo:

#### (a) Kujiandaa kimapambano dhidi ya Maadui zao

وَلَا يَحْسِبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَبَقُوا إِنَّهُمْ لَا يُعْجِزُونَ ﴿٥٩﴾ وَأَعِدُوا لَهُمْ مَا  
 اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهَبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ  
 وَآخَرِينَ مِنْ دُونِهِمْ لَا تَعْلَمُونَهُمُ اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي  
 سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ﴿٦٠﴾

*Wale wale waliokufuru wasifikiri kwamba wao wameshatangulia (mbele, Mwenyezi Mungu hawapati)ila, wao hawatamshinda (Mwenyezi Mungu)*

*"Basi waandalieni (wawekeeni tayari) nguvu (silaha) mziwezao, na mafarasi yaliyofungwa tayari tayari (mipakani), ili kwazo (nguvuhizi) muwaogopeshe maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, (mnaowajua) na pia(maadui zenu) wengineo wasiokuwa wao, msiowajua nyinyi (lakini) Mwenyezi Mungu anawajua. Na chochote mtakachokitoa katika njia ya Mwenyezi Mungu (kama hii*

*misaada ya vita vya Jihadi) mtarudishiwa kamili wala hamtadhulumiwa." (8:59-60)*

Kwa upande mmoja Allah (s.w) anawakatisha tamaa makafiri na kwa upande mwingine anawapa moyo waumini kuwa makafiri pamoja na hatua kubwa waliyoifikia ya teknolojia ya vita na silaha za kisasa wasiwe na dhana kuwa watazuia dini ya Allah (s.w) isisimame pale waumini wa kweli watakapokuwa tayari kutekeleza wajibu wao wa kuisimamisha kwa mali zao na nafsi zao. Lakini ilivyo kawaida ya Allah (s.w), hatausimamisha Uislamu kwa miujiza, bali anawataka waumini wafanye jitihada ya kujiandaa mwisho wa uwezo wao kulingana na mazingira na wakati uliopo kama wanavyojiandaa maadui zao. Kisha katika mapambano waumini wamtegemee Allah (s.w) na Allah (s.w) ameahidi kuleta nusura yake na kuwapa Waislamu ushindi. Kwa mfano katika vita vya Badr, ambapo Waislamu waliokuwa wachache (300 tu hivi) na silaha duni pamoja na uchache wa mahitaji ya kivita; walipambana na Makafiri wa Kiquraish waliokuwa wengi (1'000) pamoja na zana nzuri na nyingi za kivita na Allah (s.w) aliwasaidia Waislamu kuwashinda Makafiri kwa kishindo. Allah (s.w) aliwasaidia Waislamu kwa kuwashushia jeshi la Malaika na kujalia gauo la mchanga alioutupa Mtume (s.a.w) (kwa amri yake Allah) uingie katika macho ya kila adui na kumuwasha kuliko pili pili kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo.

إِذْ يُوحِي رَبُّكَ إِلَى الْمَلَائِكَةِ أَنْ يَأْتِيَنَّكُمْ فَتَنَبَّأُوا  
الَّذِينَ آمَنُوا سَأَلْتَنِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا أَلرُّعْبَ فَاضْرِبُوا  
فَوْقَ الْأَعْنَاقِ وَاضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ ﴿١٣﴾

*(Kumbukeni) Mola wako alipowafunulia Malaika (akawaambia): "Hakika Mimi ni pamoja nanyi, basi watieni nguvu wale walioamini; nitatia woga katika nyoyo za makafiri. Basi wapigeni juu ya shingo (zao) na kateni kila*

ncha za vidole vyao." (8:12)

فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ  
رَمَىٰ وَيُغِيٓبُ الْمُؤْمِنِينَ مِنْهُ بَلَآءٌ حَسَنًا إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٧﴾

*Hamkuwaua nyinyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaua; na hukutupa wewe (Mtume ule mchanga wa katika gao la mkono wako), ulipotupa (ukawaingia wote machoni mwao); (hukufanya wewe haya) walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyetupa, (yaani ndiye aliyeufikisha katika macho yao wote yakawa yanawawasha kuliko pili pili, wakenda mbio) Alifanya haya Mwenyezi Mungu ili awape walioamini hidaya nzuri itakayo kwake. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Asikiaye na Ajuaye." (8:17)*

Tukumbuke kuwa sharti la kupata msaada wa Allah (s.w) katika kupambana na maadui wa Dini yake, ni sisi waumini kujiandaa na kujizatiti kivita kwa kadiri ya uwezo kulingana na mazingira yaliyopo.

Nguvu za msingi tuziwezazo hivi sasa kama tulivyoamrisha katika aya (8:60), kabla hatujafika kwenye silaha za kisasa za "nuklia" ni pamoja na hizi zifiatazo:

**(i) Elimu sahihi** - itakayowezesha kulifahamu vyema lengo la kuumbwa kwetu na lengo la maisha yetu hapa duniani na namna ya kufikia malengo haya.

Elimu sahihi itapatikana kwa kusoma elimu ya mazingira pamoja na elimu ya mwongozo kwa lengo la kuweza kusimamisha Uislamu katika jamii na kumuabudu Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na kijamii. Elimu hii ndiyo itakayopelekea kuandaa nguvu za "nuklia" katika siku za usoni.

**(ii) Imani thabiti** - itakayo wawezesha waumini kupigania



Uislamu kwa mali zao na nafsi zao kwa kutarajia pepo ya Allah (s.w) bila ya kujali lawama za yeyote mwenye kulaumu. Imani thabiti inapatikana kutokana na elimu sahihi ya mwongozo kupitia Qur'an na Hadithi sahihi za Mtume (s.a.w) na vitabu vya kiada vilivyoandaliwa kwa mrengo wa kusimamisha Uislamu katika jamii vilivyo andikwa na wanazuoni wa mrengo huo, kama akina Sayyid Qutub, A.A. Maudud, Hassan Al-Bannah, Juzuu saba (7) za Darasa la watu wazima n.k.vilivyoandikwa kwa marejeo ya Qur'an na Hadithi sahihi za Mtume (s.a.w).

**(iii) Tabia njema ya Utendaji** - itakayowawezesha waumini wawe ni viigizo katika jamii ambao mchango wao katika kuihudumia, kuinufaisha na kuistawisha jamii utaonesha umuhimu wa kuwepo kwao. Tabia njema ya kuitendaji itadhiri pale waumini watakapo jizatiti kuishi kwa kufuata vipengele vyote vya tabia njema vilivyo amrisha na kusisitizwa katika Qur'an na Hadith sahihi za Mtume (s.a.w), ikiwa ni pamoja na kujitahidi kujiepusha na vipengele vyote vya tabia mbaya vilivyoainishwa na kukatazwa katika Qur'an na Hadith sahihi za Mtume (s.a.w); katika kusuhubiana na wanajamii katika mchakato mzima wa maisha.

**(iv) Mshikamano wa Waislamu** - utakao wawezehsa waumini kuwa nanguvu moja ya kumdhoofta na kumshinda adui. Nguvu hii anaidhirisha Allah (s.w) katika aya ifuatayo:

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ  
 تَرَاهُمْ رُكْعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا سِيمَاهُمْ فِي  
 وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثَرِ السُّجُودِ ذَلِكَ مَثَلُهُمْ فِي التَّوْرَةِ وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ  
 كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْئَهُ فَكَازَرَهُ فَاسْتَغْلَظَ فَاسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِ يُعْجِبُ  
 الزُّرَّاعَ لِيغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ وَعَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ  
 مِنْهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾

*Muhamad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu (pamoja), wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi (yake). Alama zao zi katika nyuso zao, kwa taathira, (athari) ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili (umetajwa hivi): Kuwa (wao) ni kama mmea uliotoa matawi yake; kisha (matawi hayo) yakautia nguvu; ukawa mnene ukasimama sawasawa juu ya kigogo chake, ukawafurahisha walioupanda; ili awakasirisha makafiri kwa ajili yao. Mwenyezi Mungu amewaahidi walioamini na kutenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa." (48:29)*

Waislamu wataweza kushikamana na kuwa na nguvu ya kuwakasirisha na kuwashinda maadui zao kama mfano huu uliopigwa katika aya hii (48:29) endapo watajizatiti kufanya matatu yafuatayo:

**Kwanza,** Wote kulielewa na kuwatayari kuliendea lengo la kuletwa Mtume (s.a.w) la kuutawalisha Uislamu katika jamii kama lilivyodhihirishwa katika Qur'an (9:33, 61:9) ambalo ndilo lililowawezesha maswahaba kushikamana na hatimaye kulifikia kama ilivyo dhihirika katika aya ifuatayo:

*"Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi." (48:28)*

**Pili**, Kupendana na kufanyiana wema pamoja na kushirikiana pamoja katika utekelezaji wa lbada maalumu za faradh kama vile Swala, Saumu, Zakat na Hija.

**Tatu**, Kutofanyiana mambo mabaya ambayo ni sumu ya kuvunja udugu na upendo. Waislamu wakizingatia na kutekeleza kwa dhati haya matatu, Allah (s.w) anatoa ahadi ya kuunganisha nyoyo zao.

*"Na akaziunga nyoyo zao (wakapendana wote hao Masahaba zako); hata kama ungalitoa vyote vilivyomo ardhini usingaliweza kuziunga nyoyo zao, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaunganisha. Hakika yeye ni mbora na Mwenye hikima." (8:63)*

### **(b) Kuelekea katika amani**

﴿وَأِنْ جَاحُوا لِلْسَّلَامِ فَأَجْزَحْ لَهَا وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ﴾<sup>(11)</sup>

*"Na kama (hao maadui) wakielekea katika amani, nawe pia ielekee na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika yeye ndiye asikiaye (na) ajuaye." (8:61)*

﴿وَإِنْ يُرِيدُوا أَنْ يَخْدَعُوكَ فَإِنَّ حَسْبَكَ اللَّهُ هُوَ الَّذِي أَيَّدَكَ بِنَصْرِهِ وَبِالْمُؤْمِنِينَ﴾<sup>(12)</sup>

*"Na kama wakitaka kukukhadaa basi Mwenyezi Mungu atakutoshelezea. Yeye ndiye aliyekusaidia kwa nusura yake na kwa waliokuamini." (8:62)*

Uislamu ni Dini yenye makusudio ya kuleta **utulivu** na **amani** ya kweli katika jamii na yenye makusudio kwa upande mwingine kutokomezwa yote yenye kuleta **khofu** na **mashaka** katika jamii ya binaadamu. Waislamu wanalazimika kuingia vitani kwa lengo hili la kuondosha khofu na kusimika amani. Hivyo, maadui wa amani watakaposalimu **amri** na kuitaka **amani** Waislamu wanawajibika kusitisha mapigano na kuelekea amani. Wala Waislamu wasisite kutoa amani kwa kuwadhania maadui zao kuwa wanataka kuwahadaa ili wawageuke kwa kuwashutukiza. Waislamu wasiwe na wasiwasi huo, kama aya inavyowatoa wasiwasi.

*"Na kama wakitaka kukuhadaa basi Mwenyezi Mungu atakutoshelezea. Yeye ndiye aliyekusaidia kwa nusura yake na kwa waliokuamini." (8:62)*

Hata hivyo, Waislamu wakati wote wanatakiwa wawe macho na kuchukua tahadhari juu ya maadui zao kama tulivyoona himizo hilo katika Qur'an (4:71).

**(c) Kumtegemea Allah (s.w)**

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ حَسْبُكَ اللَّهُ وَمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٤﴾

*"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mwenyezi Mungu anakutoshelezea wewe na wale waliokufuata katika hao walioamini." (8:64)*

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ حَرِيضَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَى الْقِتَالِ إِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ عَشْرُونَ  
صَبْرُونَ يَغْلِبُوا مِائَتِينَ وَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ مِائَةٌ يَغْلِبُوا أَلْفًا مِّنْ

الَّذِينَ كَفَرُوا بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ ﴿١٥﴾

*"Ewe Mtume (wa Mwenyezi Mungu)! Wahimize walioamini wende vitani. Wakipatikana kwenu watu ishirini wanaosubiri wataashinda mia mbili. Na kama wakiwa watu mia moja kwenu*

watawashinda elfu moja ya wale waliokurufu, maana hao ni watu wasiofahamu (uhai wa Akhera). (8:65)

الَّذِينَ خَفَّفَ اللَّهُ عَنْكُمْ وَعَلِمَ أَنَّ فِيكُمْ ضَعْفًا فَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ مِائَةٌ صَابِرَةٌ يَغْلِبُوا مِائَتَيْنِ وَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ أَلْفٌ يَغْلِبُوا أَلْفَيْنِ بِإِذْنِ اللَّهِ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿١١﴾

*“Sasa Mwenyezi Mungu amekuhafifishieni, maana anajua ya kwamba kuna udhaifu (sasa) kwenu (kwa kuwa vita vimeendelea kwa muda mrefu). Kwa hivyo wakiwa watu mia moja kwenu wenye subira nawawashinde watu mia mbili kwao; na kama wakiwa elfu moja miongoni mwenu nawawashinde elfu mbili; kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri.” (8:66)*

Waislamu pamoja na kutekeleza wajibu wao wa kujizatiti kwa mapambano dhidi ya maadui wa Uislamu na Waislamu kwa kadiri ya uwezo wao, bado wanao wajibu mkubwa sana wa kumtegemea Allah (s.w). Ukirejea historia nzima ya mapambano ya Waislamu dhidi ya maadui zao utaona Waislamu wachache wenye silaha duni waliweza kuwashinda maadui zao wenye uwezo mkubwa wa kijeshi kwa idhini na msaada wa Allah (s.w). Tumeona kuwa jeshi dogo la Waislamu katika vita vya Badr, liliweza kushinda la Makafiri wa Kiquraishi lililokuwa kubwa mara tatu zaidi kwa idhini na msaada wa Allah (s.w). Vile vile Allah (s.w) anatumkumbusha ushindi wa jeshi dogo la waumini lililoongozwa na Twalut dhidi ya jeshi kubwa la Jalut, aliyekuwa amiri jeshi wa jeshi la Makafiri katika aya zifuatazo:

فَلَمَّا فَصَلَ طَالُوتُ بِالْجُنُودِ قَالَ إِنَّ اللَّهَ مُبْتَلِيكُمْ بِنَهَرٍ فَمَنْ شَرِبَ مِنْهُ  
فَلَيْسَ مِنِّي وَمَنْ لَمْ يَطْعَمْهُ فَإِنَّهُ مِنِّي إِلَّا مَنِ اعْتَرَفَ غُرْفَةً بِيَدِهِ  
فَشَرِبُوا مِنْهُ إِلَّا قَلِيلًا مِنْهُمْ فَلَمَّا جَاوَزَهُ هُوَ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ قَالُوا لَا  
طَاقَةَ لَنَا الْيَوْمَ بِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ قَالَ الَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلَاقُوا اللَّهَ  
كَمْ مِنْ فِئَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةً بِإِذْنِ اللَّهِ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٢٤٩﴾

وَلَمَّا بَرَزُوا لِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ قَالُوا رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَثَبِّتْ  
أَقْدَامَنَا وَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٥٠﴾ فَهَزَمُوهُمْ بِإِذْنِ اللَّهِ  
وَقَتَلَ دَاوُدُ جَالُوتَ وَءَاتَاهُ اللَّهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَهُ مِمَّا يَشَاءُ  
وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ لِلنَّاسِ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَفَسَدَتِ الْأَرْضُ وَلَكِنَّ اللَّهَ ذُو  
فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٢٥١﴾

*Basi Talut alipoondoka na majeshi, alisema: "Mwenyezi Mungu atakufanyieni mtihani kwa mto (mtakaokutana nao njiani huko mnakokwenda). Basi atakayekunywa humo si pamoja nami, na asiyekunywa atakuwa pamoja nami; ila atakayeteka kwa kiasi cha kujaza kitanga cha mkono wake (akanywa hayo tu, huyo hana makosa)." Lakini walikunywa humo isipokuwa wachache tu miongoni mwao. Basi alipouvuka yeye na (wakauvuka) wale walioamini pamoja naye, walisema: "Leo hatumwezi Jaluti na majeshi yake." Wakasema wale wenye yakini ya kukutana na Mola wao: "Makundi mangapi madogo yameshinda makundi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wafanyao subira."*

*Na walipotoka kupambana na Jalut na majeshi yake, walisema hao watu wa Taluti: "Mola wetu! Tumiminie subira, na uithibitisha miguu yetu, na utusaidie juu ya watu hawa makafiri." Basi (hao watu wa Taluti) wakawaendesha mbio (hao maadui zao) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu; na Daudi akamwua Jaluti, na Mwenyezi Mungu akampa (huyu Daudi) ufalme na hikima (Utume) na akamfundisha aliyoyapenda. Na kama Mwenyezi Mungu asingalizuia watu, baadhi yao kwa wengine, kwa yakini ardhi ingeliharibika. Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila (kubwa) juu ya walimwengu wote. (2:249-251)*

Hivyo, waumini watakapo mtegemea Allah (s.w) baada ya kutekeleza wajibu wao wa kujiandaa na kujikusanyia nguvu waziwezazo, Allah (s.w) atawawezesha kuwa na nguvu yenye uwiano wa Muumini mmoja kupambana na maadui wawili (1:2) hadi kufika uwiano wa muumini mmoja kupambana na makafiri kumi (1:10) na wakati mwingine uwiano huu huongezeka kama ilivyokuwa katika vita vya **Muttah** vilivyopiganwa katika mwaka wa 7 A.H, baina ya jeshi la Mtume (s.a.w) la watu 3'000 na jeshi la Gavana wa Warumi lililokuwa na askari 200'000 (ambapo uwiano ulikuwa  $3'000:200'000 = 1:67$ ) na jeshi la Warumi likaingia mitini na kuwapa Waislamu ushindi.

Katika historia tunajifunza kuwa, pale Waislamu walipoona kuwa hawana haja ya kumtegemea Allah (s.w) kwa kuwa wana askari wapiganaji wengi na silaha bora na za kutosha Allah (s.w) aliondoa msaada wake na kuwaacha watafute ushindi kwa kutegemea medani za kivita kama walivyokuwa wakitegemea makafiri. Katika vita vya Hunain, vilivyopiganwa katika mwaka wa 8 A.H baada ya Fat-h Makka, baina ya Jeshi la Mtume (s.a.w) na jeshi la Makabila ya Bani Hawaizin na Bani Thaqif ya Mji wa Taif, Waislamu walijifaharisha na kujitanganzia ushindi kwa kuwa walikuwa na uwezo mkubwa wa kijeshi, walikuwa na wapiganaji hodari elfu kumi na mbili (12'000). Kwa wakati huo hilo lilikuwa jeshi kubwa. Kwa kosa hili la kutarajia kupata ushindi nje ya

msaada wa Allah (s.w), Waislamu walipata kibano kama onyo, na kisha Allah (s.w.) akadhirisha msaada wake kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

لَقَدْ نَصَرَ كُمْ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُم مُّدْبِرِينَ ﴿٢٥﴾ ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَنْزَلَ جُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا وَعَذَّبَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَذَلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ

*Bila shaka Mwenyezi Mungu amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Huneyni (pia); ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni chochote, na ardhi ikawa dhiki juu yenu; ingawa ilikuwa yenye wasaa, kisha mkageuka mkarudi nyuma (mnakimbia).*

*Kisha Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu wake juu ya Mtume wake na juu ya walioamini. Na akateremsha majeshi (ya Malaika) ambayo hamkuyaona, na akawaadhibu wale waliokufuru; na hayo ndiyo malipo ya makafiri." (9:25-26)*

#### **4. At-Tawba (9:1-29, 38-41, 111-112)**

Ili tuweze kusimamisha Uislamu katika jamii na kuuhami usiangushwe baada ya kusimama, waumini tunawajibika kufanya mambo kadhaa kama yalivyo ainishwa katika aya za sura hii (9:1-29, 38-41, 111-112). Wajibu wa waumini katika aya hizi umeainishwa kama ifuatavyo:

##### **(a) Kuchunga Kanuni, Masharti na Sharia ya Mikataba**

Tukirejea aya (9:1-12) tunajifunza kuwa:

- (i) Waislamu wanalazimika kuheshimu Mikataba waliyowekeana na watu au nchi nyingine. Kutekeleza



ahadi kwa Waislamu ni amri ya Allah (s.w) - rejea Qur'an (17:34)

- (ii) Makarifi watakapo vunja mkataba wa amani waliowekeana na Waislamu, waumini waone kuwa hilo ni tangazo dhahiri la vita. Hivyo Waislamu wanawajibika nao kuvunja mkataba na kupambana nao kama maadui wengine wa Dini ya Allah (s.w).
- (iii) Maadui wa Waislamu watakapotubu na wakashilimu na wakawa wanasimamisha swala na kutoa zaka, Waislamu wanaamuriwa wasitisha vita dhidi yao kwani wao wamekwisha kuwa ndugu zao katika Dini kama aya zinavyo sisitiza:

..... فَإِن تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَعَآتُوا الزَّكَاةَ فَخَلُّوا

سَبِيلَهُمْ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٩﴾

*"...Lakini wakitubu na wakashimamisha swala na wakatoa Zakat, basi iacheni njia yao (waacheni). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa Kurehemu." (9:5)*

فَإِن تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَعَآتُوا الزَّكَاةَ فَإِخْوَانُكُمْ فِي

الَّذِينَ وَتَفَصَّلَ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿١١﴾

*"Kama wakitubu na wakashimamisha swala na wakatoa Zakat, basi ni ndugu zenu katika dini. Na tunazieleza Aya (vizuri) kwa watu wanaojua." (9:11)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa, mtu atakapo sema ni muislamu na akawa anatekeleza lbada ya kusimamisha Swala na akawa anatoa Zakat, haturuhusiwi kumpiga vita kwa namna yoyote hatakama anamapungufu mengi katika utekelezaji wa Uislamu kwa ujumla. Vile vile haturuhusiwi kumuita mnaifiki, kafiri au jina lingine lolote linaloashiria kumtoa katika Uislamu. Allah (s.w) anawaasa waumini juu ya kosa la kuwaita Waislamu majina mabaya katika aya ifuatayo:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَسْخَرُونَ قَوْمًا مِّن قَوْمٍ عَسَىٰ أَن يَكُونُوا خَيْرًا  
مِّنْهُمْ وَلَا نِسَاءً مِّن نِّسَاءٍ عَسَىٰ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ وَلَا تَلْمِزُوا  
أَنفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا بِاللِّقَابِ بَعْضُ الْأَسْمَاءِ فَسُقُبًا يَسُوقُ بَعْدَ الْإِيمَانِ وَمَن لَّمْ  
يَتُبْ فَأُولَٰئِكَ هُم الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾

*Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msitukanane kwa kabila, wala msiitane kwa majina mabaya (ya kejeli): Jina baya kabisa kuambiwa mtu ni asi baada ya kuwa ni Muislamu. (Na kufanya haya ni uasi) Na wasiotubu, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao)."* (49:11)

Ukweli ni kwamba mapungufu yetu mengi katika utekelezaji wa Uislamu katika kila kipengele cha maisha yetu, unatokana na uhaba wa elimu sahihi juu ya Dini yetu tulionao. Uhaba huu umetokana na kazi kubwa wanayoifanya maadui wa Uislamu, hasa Mayahudi, katika mchakato mzima wa kutaka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu. Ulimwengu wa Waislamu bila kujitambua, wamewekewa mitaala inayo bagua elimu ya **dini** na **dunia**. Na hiyo elimu inayoitwa ya dini, ikawekewa mitaala ambayo inatoa wataalamu (Masheikh, Wanazuoni, n.k), ambao hawana uoni kabisa juu ya lengo la kuletwa Mtume Muhammad (s.a.w) la kuutawalisha Uislamu katika jamii (Qur'an 9:33, 61:9, 48:28) ambalo ndilo lengo la kuletwa Mitume wote kama linavyo bainishwa katika aya ifuatayo:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ  
لِيَتَّقُوا النَّاسَ بِالْقِسْطِ وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنْفَعٌ لِلنَّاسِ  
وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢٥﴾

*“Kwa hakika tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili wazi wazi na Tukaviteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu. Na tukateremsha (Tumekiumba) chuma, chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu; na ili Mwenyezi Mungu ajulishe anayemnusuru na Mitume yake, na hali ya kuwa hawamuoni Mwenyezi Mungu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda” (57:25)*

Aya hii inaonyesha wazi kuwa lengo la kuletwa Mitume wote ni kusimamisha Uadilifu katika jamii. Yaani kuweka mazingira ya uadilifu ambapo jamii itaweza kuishi kwa furaha na amani. Kazi hii si nyepesi, kwani wale wote wanaojihalalishia kuinyonya na kuifisidi jamii wanalindwa na nguvu za dola za kitwaghuti. Hivyo aya hii inaweka bayana kuwa nguvu ya chuma (silaha) haikushushwa kwa ajili ya Matwaghuti tu, bali na Waislamu nao pia wanawajibika kutumia "chuma chenye nguvu" katika kupambana na uongozi wa kitwaghuti ili kuweka uongozi wa Allah (s.w)

Jambo la kusikitisha sana ni kwamba wanazuoni wetu walioandaliwa na **Mitaala ya Kiyahudi**, hawana uoni huo wa kutumia "Chuma" ili kusimamisha Uislamu pale inapobidi. Badala yake wanazuoni wetu waliotakaraji katika vyuo vya Al-Azhar, Madinatil-Munawwar, Ummul-Qurah, n.k. wanapita Misikitini wakiwachochea Waislamu "waliomaamuma" kuwa wasifuate mafunzo ya wanazuoni wa kiharakati kama akina S. Qutub, A.A. Maududi, Shahiid Hassan Al-Bannah, Prof. M.H. Malik, n.k, wenye muelekeo wa kuziingiza katika utendaji aya tulizozirejea (9:33, 61:9, 48:28, 57:25). Pamoja na kueneza propaganda hizi zenye

lengo la kuzuia Uislamu usisimame katika jamii, wanazuoni hawa waliotokana na mitaala ya Kiyahudi, taaluma yao imeishia kuifasiri Qur'an kwa kutumia visa vya Kiyahudi (Israeliet), kuwagawanya Waislamu katika makundi ya Twarika, Answari Sunnah, Ahlal-Sunnah Waljamaa, Shia, Ahlal-Bidaa, Wahabi, n.k. yenye kuhasimiana na kukufurishana. Lengo la adui ni kuwafarakanisha Waislamu ili wapoteze nguvu zao katika kupambana wao kwa wao, huku maadui wakizidi kujijimarisha na kuitawala dunia **kitwaghut**. Ili Waislamu tujikomboe na makucha ya **Twaghut**, hatunabudi kuusoma Uislamu kwa usahihi wake kwa kufuata mtaala wa Mtume (s.a.w) aliourithisha kwa maswahaba wake waongofu, ambao kwa mtaala huo waliweza kuutawalisia Uislamu katika ulimwengu wa wakati huo. Rejea utawala wa Abu Bakar (r.a) 'Umar bin Khattab (Omar the Great) na nusu ya wakati wa utawala wa 'Uthman bin Affan (r.a). Nusu ya utawala wa 'Uthman na utawala Ally bin Abi Twalib uliathiriwa na kirusi kibaya cha Adui Myahudi (Abdullah bin Sabaah), kilicho sambaratisha utawala wa Kiislamu ulimwenguni mpaka hivi leo. Pamoja na historia hii chungu, wakati wowote Waislamu watakaporejea kwenye Qur'an na Sunnah kwa mrengo wa kusimamisha Uislamu katika jamii, wataweza kuchukua nafasi yao ya kuongoza tena ulimwengu.

**(b) Kupigana katika njia ya Allah (s.w)**

قَدْتَلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ  
 وَرَسُولُهُ وَلَا يَدِينُونَ دِينَ الْحَقِّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَتَّى يُعْطُوا  
 الْجِزْيَةَ عَن يَدٍ وَهُمْ صَاغِرُونَ ﴿٢٦﴾

*Piganeni na wale wasiomuamini Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho wala hawaharimishi alivyoviharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala hawashiki dini ya haki, miongoni mwa wale waliopewa Kitabu; (piganeni nao) mpaka watoe kodi kwa hiari yao hali wametii." (9:29)*

Ukirejea kwa makini aya hizi (9:13-29, 38-41) utajifunza kuwa Allah (s.w) anawashawishi na kuwachochea waumini wapigane na maadui zao katika kulipiza kisasi na kuihami dini ya Allah (s.w). Kwa ujumla katika aya hizi tunajifunza yafuatayo:

- (i) Waislamu wanaamrisha wapigane na maadui zao kwa sababu zilizo ainishwa katika aya zifuatazo:

أَلَا تَقْتُلُونَ قَوْمًا نَكَثُوا أَيْمَانَهُمْ وَهَمُّوا بِإِخْرَاجِ الرَّسُولِ وَهُمْ  
 بَدَءُوكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ أَتَخْشَوْنَهُمْ فَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَوْهُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ  
 ﴿١٣﴾ قَاتِلُوهُمْ يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْزِيهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ  
 عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُؤْمِنِينَ ﴿١٤﴾ وَيَذْهَبْ  
 غَيْظَ قُلُوبِهِمْ وَيَتُوبَ اللَّهُ عَلَى مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٥﴾

*Je, hamtapigana na watu waliovunja ahadi zao na wakafunga nia ya kumfukuza Mtume, nao ndio (pia) waliokuanzeni mara ya kwanza? Je, mnawaogopa? Basi Mwenyezi Mungu anastahiki zaidi mumuogope; ikiwa nyinyi mumeamini.*

*Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa mikono yenu, na awafedheheshe na akunusuruni juu yao, na avipoze vifua vya Waislamu (vifurahi).*

*Na aondoe joto la ghadhabu lililokuwa katika nyoyo zao; na Mwenyezi Mungu humwelekea kwa rehema amtakaye; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) mwenye hikima. (9:13-15)*

- (ii) Miongoni mwa sifa za waumini wa kweli, ni kupigania dini ya Allah (s.w) kwa mali na nafsi.

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تُتْرَكُوا وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَلَمْ يَتَّخِذُوا  
 مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَا رَسُولِهِ وَلَا الْمُؤْمِنِينَ وَلِيجَةً وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ

*Je, mnadhani kuwa mtaachwa, na hali Mwenyezi Mungu hakuwabainisha wale waliopigania dini miongoni mwenu na wasiwafanye rafiki wa moyo isipokuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Waislamu (wenzio)? Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayoyafanya. (9:16)*

(iii) Makafiri na maadui wengine wa Uislamu hatakama watajikomba kwa Waislamu kwa kuwajengea misikiti, kuwapa nafasi ya kufungua idhaa zao za television na redio kwa Qur'an Karim, kuwafanyia mipango ya Hija, n.k. na huku wameshikilia khatamu za uongozi wa jamii kinyume na uongozi wa Allah (s.w), Waislamu hawatawaona wa maana na kuridhika na uongozi wao wa kitwaghut kama aya zinavyo bainisha:

مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ أَنْ يَعْمُرُوا مَسْجِدَ اللَّهِ شَاهِدِينَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ  
 بِالْكَفْرِ أُولَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ وَفِي النَّارِ هُمْ خَالِدُونَ ﴿١٧﴾  
 إِثْمًا يَعْمُرُ مَسْجِدَ اللَّهِ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ  
 وَعَاتَىٰ الزَّكَاةَ وَلَمْ يَحْشَ إِلَّا اللَّهَ فَعَسَىٰ أُولَٰئِكَ أَنْ يَكُونُوا مِنَ  
 الْمُهْتَدِينَ ﴿١٨﴾ \* أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ وَعِمَارَةَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ كَمَنْ  
 ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَجَاهَدَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا يَسْتَوُونَ عِنْدَ اللَّهِ  
 وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٩﴾

*Haiwi kwa makafiri (kuhisabika) wanaamirisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu, hali wanajishuhudia kwa ukafiri. Hao (ndio ambao) vitendo vyao vyema vimeruka patupu, na katika Moto*

watakaa daima.

*Wanaoamirisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na kusimamisha Swala na kutoa Zaka na hawamuogopi yoyote ila Mwenyezi Mungu; basi hao ndio wanaotarajiwa kuwa miongoni mwa walioongoka.*

*Je, mnafanya kuwanyweshwa maji mahaji na kuuamirisha Msikiti Mtukufu ni sawa na (kazi ya) wale walioamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho na wakaipigania dini ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu." 9:17-19)*

Watu wenye hadhi mbele ya mbele ya Allah (s.w) na mbele ya waumini ni wale wanaobainishwa katika aya zifuatazo:

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ  
أَعْظَمَ دَرَجَةً عِنْدَ اللَّهِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٢١﴾ يُبَشِّرُهُمْ رَبُّهُمْ  
بِرَحْمَةٍ مِّنْهُ وَرِضْوَانٍ وَجَنَّتٍ لَّهُمْ فِيهَا نَعِيمٌ مُّقِيمٌ ﴿٢٢﴾ خَالِدِينَ  
فِيهَا أَبَدًا إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٢٣﴾

*Wale walioamini na wakahama na wakaipigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na kwa nafsi zao wana cheo kikubwa mbele ya Mwenyezi Mungu; na hao ndio watakaotengenekewa .*

*Mola wao anawabashiria (anawapa habari njema za) rehema zitokazo kwake, na radhi (zake) na mabustani ambayo humo watapata neema zitakazodumu.*

*Watakaa humu milele. Hakika Mwenyezi Mungu kwake kuna malipo makubwa kabisa." (9:20-22)*

- (iv)Waislamu wanakatazwa kumfanya rafiki yeyote awaye maadamu ni adui wa Uislamu na Waislamu kama aya ifuatayo inavyosisitiza:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا ءَابَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ ءَوْلِيَاءَ إِنِ اسْتَحَبُّوا

الْكَفَرَ عَلَى الْإِيمَانِ وَمَن يَتَوَلَّهُمْ مِنكُمْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٣﴾

*“Enyi mlioamini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi (vyenu) ikiwa wanastahabu (wanapenda) ukafiri kuliko Uislamu. Na katika nyinyi atakayewafanya hao kuwa ndio vipenzi vyake, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao).” (9:23)*

- (v) Pia waumini wanatakiwa wasimpende yeyote au kitu chochote, hata nafsi zao wasizipende kuliko Allah (s.w), Mtume wake na kupigania dini yake kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

قُلْ إِن كَانَ ءَابَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ

وَأَمْوَالٌ أُفْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِينُ تَرْضَوْنَهَا

أَحَبُّ إِلَيْكُمْ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّى يَأْتِيَ

اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٤﴾

*Sema: "Kama baba zenu na wana wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizochuma na biashara mnazoogopa kuharibikiwa, na majumba mnayoyapenda; (ikiwa viitu hivi) ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kupigania dini yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi (njia iliyonyooka).” (9:24)*

- (vi) Allah (s.w) anawataka waumini wasimuogope yeyote katika kupigania Dini yake, kwani yeye yuko pamoja na waumini na ameahidi kuwanusuru kama alivyowanusuru waumini waliopita katika mapigano mengi.



لَقَدْ نَصَرَ كُمْ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحَبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُمْ مُدْبِرِينَ ﴿٢٥﴾ ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَنْزَلَ جُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا وَعَذَّبَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَذَلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ

*Bila shaka Mwenyezi Mungu amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Huneyni (pia); ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni chochote, na ardhi ikawa dhiki juu yenu; ingawa ilikuwa yenye wasaa, kisha mkageuka mkarudi nyuma (mnakimbia).*

*Kisha Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu wake juu ya Mtume wake na juu ya walioamini. Na akateremsha majeshi (ya Malaika) ambayo hamkuyaona, na akawaadhibu wale waliokufuru; na hayo ndiyo malipo ya makafiri." (9:25-26)*

(vii) Allah (s.w) anawachochea na kuwahamasisha waumini waingie vitani kupambana na maadui zao kwa kauli nzito kama tunavyorejea katika aya zifuatazo:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ أَنْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَتَأْقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ أَرْضَيْتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَتَّعَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٣٨﴾ إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا وَيَسْتَبْدِلَ قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئًا وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٩﴾

*Enyi mlioamini! Mna nini mnapoambiwa "Nendeni (kupigana) kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu" mnajitia*

uzito katika ardhi? Je, mumekuwa radhi na maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kwa (mkabala wa maisha ya) Akhera ni kidogo tu.

*Kama hamtakwenda atakuadhibuni kwa adhabu inayoumiza, na atawaleta watu wengine badala yenu, wala hamatamdhuru (Mwenyezi Mungu) chochote (mkitopigania dini yake); na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu. (9:38-39)*

إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا  
ثَانِيًا أَتَيْنِي إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ  
مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا  
وَجَعَلَ لِكَلِمَةِ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَىٰ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ  
عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٠﴾ أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا وَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِكُمْ  
وَأَنْفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾

*Kama hamtamnusuru (Mtume), basi Mwenyezi Mungu alimnusuru walipomtoa wale waliokufuru; alipokuwa (mmoja tu na mwenziwe) wa pili wake, (peke yao); walipokuwa wote wawili katika pango; (Mtume) alipomwambia sahibu yake: "Usihuzunike, kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi." Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona, na akafanya neno la wale waliokufuru kuwa chini; na neno la Mwenyezi Mungu ndilo la juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayeshinda na ndiye Mwenye hikima.*

*Nendeni (vitani) mkiwa wepesi na mkiwa wazito (wazima au wagonjwa); na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu. Haya ni bora kwenu; mkiwa watu mnaojua (jambo)." (9:40-41)*

### (c) Kufanya Biashara na Allah (s.w)

Allah (s.w) anawapa motisha waumini ili wapigania Dini yake kwa moyo mkunjufu na kwa hima kubwa, kwa kuifananiha kazi hii na biashara inayofanywa baina yake na waumini. Ambapo waumini wanatoa bidhaa ya "**mali zao na nafsi zao**", Allah(s.w) naye anathaminisha bidhaa hizo kwa "**Pepo**" yake adhimu kama aya inavyobainisha.

﴿إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَىٰ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدًّا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبِشِرُوا بِبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ﴾

*“Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waislamu nafsi zao na mali zao (watoe nafsi zao na mali zao katika kupigania dini) ili na yeye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu; wanaua na wanauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati na Injili na Qur'an. Na ni nani atekelezaye zaidi ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye (Mwenyezi Mungu). Na huko ndiko kufuzu kukubwa.” (9:111)*

Lakini watakaokubaliwa na Allah (s.w) kuwa wafanyabishara wenzake ni wale tu watakaokuwa na sifa kama zilivyoainishwa katika aya ifuatayo:

﴿التَّائِبُونَ الْعَابِدُونَ الْحَامِدُونَ السَّابِحُونَ الرَّكَعُونَ السَّجِدُونَ  
الْآمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَالنَّاهُونَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَالْحَافِظُونَ لِحُدُودِ اللَّهِ  
وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ﴾

“(Hao waliahidiwa kupata haya ni wale) wanaotubia (wakikosa), wanaofanya ibada (kweli kweli), wanaomshukuru (Mwenyezi Mungu) wanaofunga, wanaorukuu, na kusujudu (yaani wanaosali), wanaoamrisha yaliyo mema, na wanaokataza yaliyo mabaya, na wanaohifadhi mipaka ya Mwenyezi Mungu; (hawaipindikii). Basi wape habari njema hao walioamini (hivi).” (9:112)

## 5. Al-Hajj (22:77-78)

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَرْكَعُوا وَاسْجُدُوا وَاعْبُدُوا رَبَّكُمْ وَأَفْعَلُوا الْخَيْرَ

لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٧٧﴾

Enyi mlioamini! (Salini) rukuuni na kusujudu na Mwabuduni Mola wenu na fanyeni mema, ili mpate kufaulu (kufuzu). (22:77)

وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ هُوَ اجْتَبَاكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ

مِنْ حَرَجٍ مِّلَّةَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ هُوَ سَمَّاكُمُ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلُ وَفِي هَذَا

لِيَكُونَ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ فَأَقِيمُوا

الصَّلَاةَ وَءَاتُوا الزَّكَاةَ وَاعْتَصِمُوا بِاللَّهِ هُوَ مَوْلَاكُمْ فَنِعْمَ الْمَوْلَى وَنِعْمَ

التَّصِيرُ ﴿٧٨﴾

Na ipiganieni dini ya Mwenyezi Mugu kama inavyostahiki (kupiganiwa). Yeye amekuchagueni (muwe uma ulio bora). Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini. (Nayo dini hii) ni mila ya baba yenu Ibrahimu; yeye (Mwenyezi Mungu) alikwiteni Waislamu tangu (katika vitabu vya zamani) huko; na katika (Qur'an) hii pia (mumeitwa jina hilo), ili awe Mtume shahidi juu yenu na nyinyi muwe mashahidi juu ya watu (waliotangulia). Basi simamisheni Sala na toeni Zaka na shikamaneni pamoja kwa ajili ya

*Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mola wenu. Mola Mwema aliyoje, na Msaidizi Mwema aliyoje! (22:78)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa waumini ili wafikie kilele cha lengo la kuumbwa kwao, hawanabudi kutekeleza kwa azma kubwa yafuatayo:

**(a) Kutekeleza Ibada za Kibinafsi kwa kadiri ya uwezo wao**

Ibada binafsi ni zile zinazoweza kutekelezeka bila ya kuwa na dola ya Kiislamu. Ibada hizi ni pamoja na utekelezaji wa nguzo tano za Uislamu; yaani kusimamisha **Swala**, kutoa **Zakat** na **Sadaqat**, **kufunga**, **kuhiji** na utekelezaji wa **Sunnah** zinazoambatana na nguzo hizi. Pia ni pamoja na utekelezaji wa amali nyingine mbalimbali zilizoainishwa katika Qur'an na Sunnah ambazo mtu binafsi anaweza kuzitekeleza bila ya kuhitajika nguvu za dola ikiwa ni pamoja na kujipamba na tabia njema.

Utekelezaji wa Ibada hizi za kibinafsi kama zinavyostahiki kutekelezwa na kudumu nazo ni jambo muhimu mno kwa waumini kwani ndio msingi wa kusimamisha Dola ya Kiislamu. Uislamu hautasimama katika jamii kama waumini hawataanza kuusimamisha katika nafsi zao kama Allah (s.w) anavyotukumbusha.

..... إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ ۗ .....  
.....

*“... Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyiko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao .....” (13:11)*

**(b) Kuziendea Ibada za Kijamii kwa kufanya juhudi za maksudi za kusimamisha Uislamu**

Ibada za kijamii ni zile ambazo hazitekelezeki kibinafsi pasina kuwa na dola ya Kiislamu. Kwa mfano Waislamu katika kiwango cha binafsi, hata wakiwa na ari kiasi gani, hawana namna ya kuwa

na uchumi wa Kiislamu Sheria na hukumu za Kiislamu, utamaduni wa Kiislamu, siasa na maongozi ya Kiislamu na kuwa na mifumo mingine ya Kiislamu chini ya dola ya kitwaghati. Kwa maana nyingine pale ambapo Uislamu haujasimama na kuchukua khatamu za dola, Waislamu hawana namna ya kuweza kumuabudu Mola wao inavyopasa katika masuala yote ya kijamii kama vile Uchumi, Siasa, Utamaduni, Sheria, Mahakama, n.k.

Hivyo ili Waislamu waweze kumcha Mola wao katika haki ya kumcha (Qur'an 3:102) au ili Waislamu waweze kufuata Uislamu wote kibinafsi na kijamii (Qur'an 2:208) hawanabudi kuingiza katika utendaji aya ya (22:78) ambayo inatupa mafunzo yafuatayo:

**(i) Waumini wanaamrisha kuipigania Dini ya Allah (s.w) kama ipasavyo kupiganiwa.**

Maana yake ni kwamba waumini wanawajibika kuipigania Dini ya Allah isimame katika jamii na kuihami isiporomoshwe chini baada ya kusimama kwa kupania na kuweka mikakati ya makusudi na sio kwa kubangaiza au kidharura dharura. Lengo kuu la waumini liwe ni kusimamisha Uislamu kama lilivyo kuwa lengo la kuletwa Mtume Muhammad (s.a.w) (Qur'an 9:33, 61:9). Waislamu walio wengi hivi leo, hata wale wanaojiita wanaharakati, wanautumikia Uislamu baada ya saa za kazi ya kutafuta maslahi ya maisha ya dunia (maisha binafsi) au baada ya kustaafu kazi yakutafuta ya maisha ya dunia. maslahi binafsi. Yaani, suala la kusimamisha Uislamu katika jamii limekuwa ni suala la "part time" kwa Waislamu waliowengi, tena wanaojiita wanaharakati. Sijui Waislamu tunaielewaje aya hii:

قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ  
وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِينُ تَرْضَوْنَهَا  
أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّى يَأْتِيَ  
اللَّهُ بِأَمْرٍ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٩٤﴾

*Sema: "Kama baba zenu na wana wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizochuma na biashara mnazoogopa kuharibikiwa, na majumba mnayoyapenda; (ikiwa vitu hivi) ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kupigania dini yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi (njia iliyonyooka). (9:24)*

Bila shaka aya hii inatuweka wazi kuwa kazi ambayo tunatakiwa tuipe kipaumbele kwa kutumia muda wetu, mali zetu, nguvu zetu, fursa zetu na vipaji vyetu vya akili, ni kazi ya kuutawalisha Uislamu katika jamii na kuudumisha katika utawala mpaka mwisho wa dunia.

## **(ii) Ubora wa Ummah wa Kiislamu**

Utadhihiri pale watakapotekeleza jukumu hili la kuusimamisha Uislamu katika jamii ambapo watakuwa na nguvu za dola za kuamrisha mema na kukataza mabaya, jambo ambalo litajenga mazingira ya Uadilifu yatakayo wezesha kupatikana kwa utulivu, ustawi na amani ya kweli. Dola ya Kiislamu ndiyo "Mkombozi" wa raia wanaodhulumika na kunyanyasika chini ya dola za kitwaghut za **mfumo nyonyaji** na **mfumo gandamizi**. Hivyo Waislamu wajue kuwa ndio wakombozi wa wanyonge katika jamii kama Allah (s.w) anavyotukumbusha.

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَدِّمُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ  
 وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أَهْلُهَا  
 وَأَجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا وَأَجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ نَصِيرًا ﴿٧٥﴾

*“Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu na (katika kuwaokoa) wale walio dhaiifu - katika wanaume na wanawake na watoto - ambao husema: "Mola wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu, na tujaalie tuwe tuna mlinzi anayetoka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anayetoka kwako." (4:75)*

Hivyo Umma wa Waislamu ni bora katika jamii kwa kuwa wanatoa huduma zinazostawisha jamii na wanaiweka jamii katika mazingira ya utulivu na amani ya kweli bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

### **(iii) Uislamu ni Dini nyepesi katika kuifuata**

Uislamu ni Dini nyepesi katika kuifuata kwa sababu inaendana na maumbile ya mwanadamu na maumbile yote yaliyomzunguka kama Allah (s.w) anavyotuthibitishia katika aya ifuatayo:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا  
 تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا  
 يَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

*“Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawasawa -ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu; (Yaani dini hii ya Kiislamu inawafikiana barabara na umbo la binadamu). Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini iliyo haki, lakini watu wengi hawajui.” (30:30)*



#### (iv) Uislamu ni Mila ya Nabii Ibrahim (a.s)

Kwa maana ya kwamba ni Dini ya kujisalimisha moja kwa moja (asilia mia kwa mia) kwa Allah (s.w) kama alivyojisalimisha Nabii Ibrahim (a.s) kiasi cha kutekeleza amri ya kumchinja Mwanawe mpendwa pekee kwa moyo mkunjufu kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

رَبِّ هَبْ لِي مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٠٠﴾ فَبَشَّرْنَاهُ بِغُلَامٍ حَلِيمٍ ﴿١٠١﴾ فَلَمَّا بَلَغَ  
مَعَهُ السَّعْيَ قَالَ يَدُبَّتْ إِيَّيَّيْ أَرَى فِي الْمَنَامِ أَنِّي أَذْبَحُكَ فَانظُرْ مَاذَا تَرَى  
قَالَ يَتَّابَتِ أَفْعَلُ مَا تُؤْمَرُ سَتَجِدُنِي إِن شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٠٢﴾ فَلَمَّا  
أَسْلَمَا وَتَلَّاهُ لِلْجَبِينِ ﴿١٠٣﴾ وَتَدَيَّنَّاهُ أَن يَتَّخِذَهُ إِبرَاهِيمَ ﴿١٠٤﴾ قَدْ صَدَّقْتَ  
الرُّءْيَا إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٠٥﴾ إِن هَذَا لَهُوَ الْبَلَاءُ الْمُبِينُ  
﴿١٠٦﴾ وَفَدَيْنَاهُ بِذَبْحٍ عَظِيمٍ ﴿١٠٧﴾ وَتَرَكَنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿١٠٨﴾  
سَلَامٌ عَلَى إِبرَاهِيمَ ﴿١٠٩﴾

*"Ewe Mola wangu! Nipe (mtoto awe) miongoni mwa watenda mema."*

*"Ndipo tukampa habari njema ya (kuwa atapata) mtoto mplele. (Basi akampata. Naye ndiye Nabii Ismaili)."*

*Basi alipofikia (makamu ya) kwenda na kurudi pamoja naye, alimwambia: "Ewe mwanangu! Hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja. (Na ndoto ya Mitume ni Wahyi). Basi fikiri, waonaje?" Akasema: "Ewe baba yangu! Fanya unayoamrisha, utanikuta Inshallah miongoni mwa wanaosubiri."*

*Basi wote wawili walipojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu), na akamlaza kifudufudi (amchinje). Pale pale tulimwita: "Ewe Ibrahim:"*

"Umekwishasadikisha ndoto. (Usimchinje mwanao)." Kwa yakini hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema. Bila shaka (Jambo) hii ni jaribia lililo dhahiri, (mtihani ulio dhahiri). Basi tukamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa mtukufu. Na tukamuachia (sifa nzuri) kwa (watu wote) waliokuja baadaye. Amani kwa Ibrahimu. (37:100-109)

Ni katika kiwango hicho cha utii, Allah (s.w) akampa heshima ya mwenendo au Mila yake kuwa kiigizo cha waumini.

وَمَنْ يَرْعَبْ عَن مِّلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَن سَفِهَ نَفْسَهُ وَلَقَدِ اصْطَفَيْنَاهُ فِي  
الدُّنْيَا وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٣٠﴾

"Na nani atajitenga na mila ya Ibrahimu (akaichukia dini hii ya Kiislamu) isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu? Na kwa yakini sisi tulimchagua (Ibrahimu) katika dunia; na kwa hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema (kabisa)." (2:130)

وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِّمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ وَاتَّبَعَ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ  
حَنِيفًا وَاتَّخَذَ اللَّهُ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا ﴿١٣٥﴾

"Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule ambaye ameuzelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye ni mwema, na anafuata mila ya Ibrahimu (kuwa Muislamu kweli kweli). Na Mwenyezi Mungu amemfanya Ibrahimu kuwa ni kipenzi chake." (4:125)

Hivyo kwa ufupi tunaweza kusema Uislamu ni Dini ya kumnyenyekea Allah (s.w) na kumtii kwa ukamilifu katika kukiendea kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na ya kijamii.

**(v) Waislamu wanatakiwa wabakie na utambulisho wa kuitwa "Waislamu"** na wajiepushe kabisa na kujita majina mengine ya kiitikadi au kitaasisi kama vile Answari Sunnah, Ahlul-

Sunnah Wal-Jamaat, Ahlul-Dhikri, Shi'a n.k. Kujiita majina haya ni kujitenga na Uislamu na kudhoofisha Ummah wa Kiislamu jambo linalompa adui mwanya wa kuwafarakanisha Waislamu na kuwatawala. Hili suala la kujigawa katika makundi yaliyofarakana na kupoteza nguvu zetu dhidi ya maadui zetu Allah (s.w) amelitahadharisha katika aya nyingi za Qur'an na miongoni mwa hizo ni hii:

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَا تَتَزَوَّجُوا فَتَفْشَلُوا وَتَذْهَبَ رِيحُكُمْ  
وَأَصْبِرُوا إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٤٦﴾

*“Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake wala msizozane (msigombane), msije mkaharibikiwa na kupoteza nguvu, na yumilieni (msitahamiliane). Bila shaka Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaovumilia.” (8:46)*

**(vi) Waislamu kuwa wamoja. Umoja wa waislamu** utapatikana tu pale Waislamu watakapo kuwa na lengo kuu moja la kusimamisha Uislamu katika jamii, wakajipa anuani moja ya kuitwa "Waislamu", wakahurumiana na kufanyiana wema na wakajiepusha na kubughudhiana na kuzozana.

**(vii) Waislamu kuwa Viyoo kwa Jamii**

Kama Mtume (s.a.w) alivyo kuwa kiigizo chetu katika kusimamisha Uislamu na kuleta ustawi wa jamii kwa faida ya watu wote bila ya ubaguzi wa kidini au kitaifa, ndivyo Waislamu tunavyotarajiwa tuwe kigezo kwa wengine katika jamii katika kufanya mema na kutoa huduma mbali mbali zinazostawisha maisha ya watu wote kwa ujumla katika jamii.

**6. As-Saaf (61:1-14)**

Sura hii nayo ni miongoni mwa Sura zinazo ainisha wajibu wa waumini katika jamii. Tukiipitia Sura hii kwa makini tunapata ujumbe

unaonesha wajibu wa waumini katika jamii katika maeneo yafuatayo:

**(a) Kumtukuza Allah (s.w) ipasavyo**

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦١﴾

*“Vinamtukuza Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.;(61:1)*

Mwanaadamu anapaswa kumuamini Allah (s.w) na kumtukuza ipasavyo kama vinavyomtukuza viumbe vyote vilivyomo mbinguni na ardhini, ikizingatiwa kuwa mwanaadamu ametukuzwa na Mola wake kuliko viumbe vingine kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

﴿وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ

مِّنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ﴿٧٠﴾

*“Kwa hakika tumewakirimu wanaadamu na tumewapa vya kupanda barani na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewatukuza kuliko wengi katika wale tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa (kabisa).” (17:70)*

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٩٥﴾

*“Bila shaka! Tumemuumba mwanaadamu kwa umbo lililo bora kabisa.” (95:4)*

Kwa takrima hii mwanaadamu anawajibika kumshukuru Allah (s.w) kwa kumtukuza na kumuabudu ipasavyo. Ni wazi kuwa mwanaadamu atakuwa ni mwizi wa fadhila na mkosa shukurani aliyekubuhu, pale atakapompuuza Mola wake Karimu na badala yake akavitukuza viumbe vyake.

Muumini wa kweli ni yule anayejiunga na viumbe wengine katika **kumsabihi** Allah (s.w) kwa kufuata mwongozo wa Qur'an na Sunnah na kisha kujizatiti katika kusimamisha Uislamu katika jamii

ili kujenga mazingira ya kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo katika kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na kijamii.

**(b) Kuwa Waumini watendaji**

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ  
أَنْ تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾

*Enyi mlioamini! Mbona, (kwa nini) mnasema msiyoyatenda? "Ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda."(61:2-3)*

Waumini wa kweli wanatakiwa wawe kioo kwa wengine katika tabia ya kiutendaji. Wawe wa kwanza kutekeleza mema kwa manufaa ya jamii kabla hawajawafahamisha na kuwaamrisha wengine kufanya hayo mema. Ikiwezekana waonyeshe mema kwa matendo kwa asilimia themanini (80%) na wamalizie kuyadhihirisha kwa watu kwa maneno kwa asilimia ishirini (20%) iliyobakia au chini ya hapo. Vivyo hivyo wajiepushe na maovu kabla hawajawakataza wengine kuacha hayo maovu.

Hivyo, dai'yah (Mlinganiaji) mzuri ni yule anayekuwa mfano wa kuufuata ujumbe wa Allah (s.w) na Mtume wake kwa wale anao walingania kama inavyo bainika katika aya ifuatayo:

وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا  
وَقَالَ إِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٣٣﴾

*Ni nani asemaye kauli bora zaid kuliko aitaye (viumbe) kwa Mwenyezi Mungu, na (mwenyewe) akafanya vitendo vizuri na husema (kwa maneno yake na vitendo vyake): "Hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu." (41:33)*

Ni unafiki wa wazi kwa mtu kuhimiza wengine kufanya mema na kuacha maovu na huku yeye mwenyewe anatenda kinyume

chake. Allah (s.w) anatutanabaisha juu ya tabia hii katika aya ifuatayo:

﴿ أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴾

*Je! Mnawaamrisha watu kutenda mema na mnajisahau nafsi zenu, hali mnasoma Kitabu (cha Mwenyezi Mungu kuwa kufanya hivyo ni vibaya)? Basi je, hamfahamu? (2:44)*

Mtume (s.w) anabainisha kina cha uovu wa mtu kusema asiyo yatenda katika Hadithi ifuatayo:

*“Usamah bin Zaid (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema, mtu ataletwa siku ya kiyama kisha atatumbukizwa Motoni, matumbo yake yatamwagika motoni na kusagwa sagwa (yawe kama unga) kisha wakazi wa huko motoni watamzunguka na kisha watamuuliza”Ewe mtu kitu gani kilichokusibu? Hukuwa unatuamrisha mema na kutukataza maovu?” Atajibu, "Nilikuwa nikikuamrishi mema ambayo mimi mwenyewe sikuwa nikiyafanya, na nilikukatazeni maovu ambayo mimi mwenyewe nilikuwa ninayafanya." (Bukhari na Muslimu).*

### **(c) Kuwa na mshikamano katika kupigania Dini ya Allah (s.w)**

﴿ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الَّذِينَ يُقْتَلُونَ فِي سَبِيلِهِ صَفًا كَانَتْهُمْ بُنْيَانٌ مَرُوضٌ ﴾

*"Kwa yakini Mwenyezi Mungu anawapenda wale wanaopigana katika njia yake, safusafu, (mkono mmoja); kama kwamba wao ni jengo lililokamatana bara bara." (61:4)*

Kama tulivyoona katika Al-Imraani (3:103) Waislamu wamewajibishwa kushikamana pamoja ili waweze kuwa na nguvu ya pamoja ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Mshikamano

unaohimizwa katika aya hii si ule wa **kitwariqa** au wa **kitaasisi** au wa **mapote mbali mbali ya Waislamu yenye malengo tofauti tofauti**. Bali mshikamano unaohimizwa katika aya hii ni ule unaowapelekea waumini kuliendea **lengo moja la kusimamisha Uislamu katika jamii**.

Hivyo ili Waislamu washikamane pamoja kama jengo lililokamatana barabara, kiasi cha kustahiki kupata ridhaa na upendo wa Allah (s.w), hawanabudi kutekeleza masharti matatu:

- (i) Kuwa na lengo moja la kuutawalisha Uislamu katika jamii, wakijua kuwa maadui wote wa Uislamu watachukia; ambalo pia ndilo lengo la kuletwa Mtume (s.a.w) - Qur'an (9:33, 61:9)
- (ii) Waumini kufanyiana mema yenye kupalilia upendo na udugu, kama yalivyo ainishwa katika Qur'an na Sunnah.
- (iii) Waumini kujiepusha na kufanyiana mabaya yanayo mkaribisha Sheitwani kuchochea chuki na uadui baina ya Waislamu, kama yalivyoainishwa katika Qur'an na Sunnah.

**(d) Kuntii Mtume Muhammad (s.a.w)**

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يَا قَوْمِ لِمَ تَعْبُدُونَ مَا لَا يَنْفَعُكُمْ شَيْئًا وَلَا يَضُرُّكُمْ ۗ إِنَّكُمْ تَعْبُدُونَ لِلشَّيْطَانِ وَهُوَ بَشَرٌ خَلَقَ كَمَا خَلَقَ آلَ آدَمَ ۚ فَاتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَكُونَ ۗ وَإِنَّ لَكُمْ فِي آلِ آدَمَ لَعَلَّةً كَمَا فِيكُمْ ۗ فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاغَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

*Na wakumbushe, (Nabii) Musa alipowaambia watu wake: "Enyi watu wangu! Mbona, (kwa nini) mnaniudhi, hali mnajua kuwa mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (niliyeletwa) kwenu?" Basi walipoendelea na uovu wao, Mwenyezi Mungu aliziachilia nyoyo zao zipotoke (kama walivyotaka wenyewe); na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu waovu (wenye kutoka katika taa yake)." (61:5)*

وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَدَّبُّنِي إِسْرَءِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدٌ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُبِينٌ

*Na (wakumbushe) aliposema (Nabii) Isa bin Mariamu (kuwaambia Mayahudi): "Enyi wana wa Israili! Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na kutoa habari njema ya Mtume atakayekuja nyuma yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad. (Muhammad) Na maana ya majina mawili yote haya ni moja. Maan yake Mwenye kushukuriwa kwa maneno yake mazuri na vitendo vyake vizuri na kila chake kwani vyake vyote ni vizuri. Lakini alipowajia kwa hoja zilizo wazi, walisema: "Huu ni udanganyifu uliyo dhahiri."*

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُوَ يُدْعَى إِلَى الْإِسْلَامِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

*"Na ni nani dhalimu mkubwa wa nafsi yake kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, na hali anaitwa katika Uislamu? Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu (wa nafsi zao)." (61:6-7)*

Katika aya hizi tunarejeshwa kwenye historia ya Nabii Musa (a.s) na Nabii Issa (a.s) Mitume waliotekeleza wajibu wao wa kufikisha ujumbe wa Allah (s.w) kwa watu waliotumwa kwao. Kwa ujumla kazi ya Mitume wote wa Allah (s.w) ilikuwa kuwafikishia watu wao kwa uwazi ujumbe wa Mola wao na kuwa viigizo vyema katika utekelezaji wa ujumbe huo katika maisha ya kila siku. Mitume hawakuwa na wajibu wa kuwalazimisha watu kuufuata ujumbe huo kwa nguvu, bali watu wao baada ya kuwafikishia kwa uwazi walikuwa na uhuru kamili wa **kuamini** au **kukufuru** ujumbe



huo. Wale walioamini Mitume walifuzu katika maisha ya dunia na wameahidiwa na Mola wao kufuzu kukubwa katika maisha ya akhera. Ama wale waliowakadhibisha Mitume wao walijudhulumu nafsi zao na kuhasirika katika maisha ya dunia na katika akhera wameahidiwa na Mola wao kupata adhabu kali katika Jahannam kama tunavyojifunza katika Qur'an:

لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ ۚ قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ ۚ فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ  
 وَيُؤْمِنْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ لَهَا ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ  
 عَلِيمٌ ﴿٢٥٦﴾ اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ  
 وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ  
 إِلَى الظُّلُمَاتِ ۗ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

*“Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini. Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkataa shetani na akamwamini Mwenyezi Mungu, bila shaka yeye ameshika kishiko chenye nguvu kisichokuwa na kuvunjika. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia mwenye kujua.”*

*“Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika nuru. Lakini waliokufuru, walinzi wao ni matwaghuti. Huwatoa katika nuru na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele.” (2:256-257)*

Halikadhalika, waumini wa leo ni wajibu wetu kumtii Mtume Muhammad (s.a.w) ipasavyo na kumfanya kiigizo chetu katika kuulingania Uislamu na kuusimamisha katika jamii. Hatunabudi kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa uwazi na kwa lengo stahiki kwa watu wote, sisi wenyewe tukiwa mfano wa utekelezaji wa ujumbe

huo bila ya kujali upinzani wa wale wanaokadhibisha ujumbe huo.

Dhalimu mkubwa, kwa mujibu wa aya (61:7) ni yule anayezua utaratibu mwingine wa maisha kinyume na ule uliofundishwa na Mitume wa Allah (s.w) kupitia katika vitabu vyake vitakatifu. Uislamu ni mfumo wa maisha ya jamii aliouweka Allah (s.w) kwa ajili ya binaadamu wote kupitia kwa Mitume wake na vitabu vyake.

Pia Uislamu ndio mfumo wa maisha unaofuatwa na maumbile yote yaliyo mbinguni na ardhini pasina hiari. Wanaadamu na Majini ndio pekee waliopewa uhuru na Mola wao wa kuamua kuufuata au kutoufuata na kubuni mifumo mingine kwa mujibu wa matamano ya nafsi zao. Kuamua kupingana na mfumo wa maisha unaoafuatwa na maumbile yote ni kitu cha kushangaza kama Allah (s.w) anavyotutanabalisha:

أَفَغَيْرَ دِينِ اللَّهِ يَبْتَغُونَ وَلَهُمْ أَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ

وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾

*Je! Wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii yeye, kikipenda kisipende? Na kwake watarejeshwa wote." (3:83)*

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ

الْخَاسِرِينَ ﴿٨٥﴾

*Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa)." (3:85)*

Mwanaadamu atakapotumia uhuru wake vibaya na akaamua kubuni mifumo mingine ya maisha inayopingana na Uislamu kwa kuchelea maslahi machache ya kidunia atakuwa amejidhulumu nafsi yake mwenyewe kwani atakuwa anapingana na mfumo wa maumbile yote yaliyomzunguka na atasababisha migongano mingi

katika ardhi. Hivyo makafiri watatastahiki adhabu kali kutokana na madhara na machafuko wanayo sababisha katika jamii kama Allah (s.w) anavyosisitiza:

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَا إِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِينَ مُنتَقِمُونَ ﴿٢٢﴾

*“Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayekumbushwa kwa aya za Mola wake kisha akazikataa? Hakika sisi ni wenye kuchukua kisasi kwa wale wabaya.” (32:22)*

**(e)Kutumchelea yeyote katika kupigania Dini ya Allah (s.w)**

يُرِيدُونَ لِيُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَاللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِ  
وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٨﴾

*“Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu (ya Uislamu) kwa vinywa vyao; na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafiri watachukiwa.”(61:8)*

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ  
وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٩﴾

*“Yeye ndiye aliyemtuma (aliyemleta) Mtume wake (Nabii Muhammad) kwa uwongofu na kwa dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote, ijapokuwa washirikinai watachukiwa.” (61:9)*

يَتَّبِعُهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا أَنْصَارَ اللَّهِ كَمَا قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ  
لِلْحَوَارِيِّينَ مَنْ أَنْصَارِي إِلَى اللَّهِ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ  
فَعَامَنَّا طَائِفَةٌ مِّنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَكَفَرَت طَّائِفَةٌ فَأَيَّدْنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا  
عَلَىٰ عَدُوِّهِمْ فَأَصْبَحُوا ظَاهِرِينَ ﴿١٤﴾

*Enyi mlioamini! Kuweni wasaidizi wa (kutanganza dini ya) Mwenyezi Mungu, kama alivyosema Isa bin Mariamu kuwambia wafuasi (wake maneno haya): Ni nani wasaidizi wangu kwa ajili ya (kutanganza dini ya) Mwenyezi Mungu?" Wafuasi wakasema: "Sisi ni wasaidizi wa (kutanganza dini ya) Mwenyezi Mungu." Basi taifa moja la wana wa Israili liliamini, na taifa jingine lilikufuru; basi tukawatia nguvu wale walioamini juu ya maadui zao na wakawa wenye kushinda." (61:14)*

Makafiri pamoja na kupania kuufuata Uislamu katika uso wa dunia kwa kutumia propaganda na nguvu za dola kubwa za dunia hawawezi kufikia lengo hili kwa ahadi ya Allah (s.w), kuwa waumini watakapo mtii Allah (s.w) na Mitume wake kisawasawa na wakasimama kidete kuutawalisha Uislamu katika jamii kwa mali zao na nafsi zao, atawapa ushindi dhidi ya maadui zao. Kutekelezwa kwa ahadi hii kukobayana katika historia ya Mitume wa Allah na maswahaba zao.

Tukichukua historia ya Mtume Muhammad (s.a.w) aliyeletwa kwa lengo lililobainisha katika aya (61:9), alianza kazi yake ya Utume akiwa mwenyewe pale pangoni katika Jabal Hira, kisha akaanza kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu wake wa karibu ikiwa ni pamoja na watu wa familia yake, rafiki zake na jamaa zake wa karibu ambao nao waliufikisha ujumbe huo kwa watu wao wa karibu. Baada ya miaka mitatu, Mtume akiwa bado na wafuasi wake wachache sana, aliamrisha na Mola wake atangaze ujumbe wa Uislamu kwa watu wote bila ya kuchelea upinzani mkali atakao upata kutoka kwa wakuu wa dola na vyombo vya dola vilivyowazunguka.

Historia inatuonesha kuwa Mtume (s.a.w) na maswahaba zake walipata kibano kikali kutoka kwa Dola ya Kikafiri ya Maquraishi kwa kipindi cha miaka 13. Hata baada ya kuhamia Madinah, ambapo Mtume alipata mazingira mazuri ya kuanzisha

dola changa ya Kiislamu, bado makafiri wa Kiquraishi walimfuata humo na pamoja nao wakaongezeka maadui wengine wane ambao ni Wanafiki, Mayahudi, Wakristo na Makabila mengine ya washirikina. Katika kipindi cha miaka kumi ya Madina, Mtume (s.a.w) na wafuasi wake walipambana na maadui hawa katika kuihami dola ya Kiislamu katika vita zaidi ya thelathini (30) yeye mwenyewe Mtume (s.a.w) akiwa ameongoza vita ishirini na saba (27).

Pamoja na upinzani huu mkubwa alioupata Mtume (s.a.w) na maswahaba zake katika mchakato mzima wa kuliendea lengo la kuutawalisha Uislamu katika jamii ya walimwengu wa wakati ule; Allah (s.w) alikamilisha nuru yake kupita mikono ya Waislamu. Dola ya Kiislamu iliinukia kuwa "Supper Power" baada ya kuiingiza mitini Dola ya Kirumi katika mwaka wa 7 A.H katika vitabu vya Muttah na 9 A.H katika eneo la Tabuuk, mpakani na Syria. Kabla ya vita hivi Warumi walikuwa ndio "Supper Power" katika ulimwengu wa wakati huo. Na Allah (s.w) analithibitisha hilo katika aya ifuatayo:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظَاهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ ۗ

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*“Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi.” (48:28)*

Hivyo wakati Mtume (s.a.w) anawaaga Waislamu wa ulimwengu wa wakati huo katika Hija ya kuaga 10 A.H, baada ya miaka 23 ya mapambano, hapa kuwa na nguvu yoyote ya makafiri iliyokuwa na tamaa ya kuwashinda Waislamu. Allah (s.w) an alithibitisha hili katika aya ya mwisho aliyomshushia mja wake na Mtume wake wa mwisho:

الْيَوْمَ يَئِسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِ الْيَوْمَ  
 أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

“...Leo waliokufuru wamekata tamaa katika Dini yenu, basi msiwaogope bali niogopeni mimi. Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na kukutimizieni neema yangu, na Nimekupendeleeni Uislamu uwe Dini yenu....” (5:3)

Uislamu kwa muumini utakamilika pale atakapoweza kumuabudu Mola wake ipasavyo katika kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii au pale atakapoweza kumtii Allah (s.w) katika amri ifuatayo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا ادْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَآفَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا

خُطُوتِ الشَّيْطَانِ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٢٨﴾

Enyi mlioamini! Ingieni katika hukumu za Uislamu zote, wala msifuata nyayo za Shetani; kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri." (2:208)

Chini ya Uongozi wa Twaaghut, tunaweza kwa kiasi fulani kujidanganya kuwa tunaweza kumuabudu Allah (s.w) kibinafsi kwa kuswali, kufunga, kutoa zaka, kuhiji na kufanya ibada nyingine za binafsi kama hizi. Lakini chini ya Twaaghut hatuwezi kumuabudu Allah (s.w) kijamii katika uchumi, siasa, utamaduni, sheria na katika mifumo mingine ya kijamii.

Ukweli ni kwamba hata hizo ibada binafsi tunazo zitekeleza haziswihi kwa sababu zinategemeana mno na mifumo ya kijamii. Kwa mfano swala ya mtu haitaswihi endapo ataswali na kivazi kilichotokana na mfumo haramu wa uchumi kwa ushahidi wa Hadith sahihi ifuatayo:

*"Ibn 'Umar (r.a) ameeleza, 'Atakayenunua nguo kwa dirhamu kumi ambayo diramu moja ni ya haramu, Allah (s.w) hataipokea swala yake pindipo anaitumia nguo hiyo kuswalia" Baada ya kusema haya aliingiza vidole vyake masikioni na kusema, "Kuwa kiziwi! Hakika haya nimeyasikia akisema Mtume wa Allah" (Ahamad, Baihaqi)*

Halikadhalika kutokana na Hadith mbali mbali, Zakat na Sadaq haitaswihi kutokana na chumo la haramu, Swaumu haitaswihi kwa mfungaji anayekula daku na futari ya haramu, hivyo hivyo kwa Hija na ibada nyingine za kibinafsi.

Hivyo waumini wanao wajibu mkubwa wa kuuangusha utwaaghuti na kusimika badala yake dola ya Kiislamu ambayo itawajengea mazingira ya kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo katika kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na kijamii.

**(f) Kuingia katika Biashara na Allah (s.w)**

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ آمَنُوا هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ تَجَارَةٍ تُنَجِّيكُمْ  
مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿١٠﴾

*“Enyi mlioamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuo kweni na adhabu iumizayo? (61:10)*

تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۖ وَتَجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ  
ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١١﴾

*(Basi biashara yenyewe ni hii):- Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, haya ni bora kwenu; ikiwa mnajua (61:11)*

يَغْفِرُ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلُكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا  
 الْأَنْهَارُ وَمَسَاكِنَ طَيِّبَةً فِي جَنَّاتٍ عَدْنٍ ذَلِكَ الْفَوْزُ  
 الْعَظِيمُ ﴿١٢﴾

(Mkifanya haya) Atakusameheni dhambi zenu na atakuingizeni katika Mabustani yapitayo mito mbele yake na (atakupeni) maskani mazuri mazuri katika Bustani za milele: huku ndiko kufuzu kukubwa. (61:12)

وَأُخْرَى تُحِبُّونَهَا نَصْرٌ مِّنَ اللَّهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ وَبَشِيرٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿١٣﴾

Na (atakupeni) kingine mnachokipenda: Nayo ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu na ushindi ulio karibu! Na wasashe habari njema waumini." (61:13)

Pamoja na kwamba tunaishi katika jamii ambayo Uislamu uko chini katika kiwango cha kibinafsi na Utwaaghuti ndio unaotawalia mifumo yote ya kijamii, bado Uislamu unanafasi ya kusimama na kutwaa utawala wa jamii endapo Waislamu wataitikia wito wakufanya **Biashara** na Allah (s.w). **Biashara** yenyewe kama ilivyoainishwa katika aya ya (61:11) ni kumuamini Allah (s.w) na Mtume wake ipasavyo kwa kutekeleza maamrisha na makatazo yote ya Allah (s.w) na Mtume wake katika kiwango cha binafsi na kisha kufanya jitihada za makusudi kiasi cha kujitua muhanga kwa mali na **nafsi**, katika **kuihuisha**, **kuisimamisha** na **kuihami** Dini ya Allah (s.w). Katika mwisho wa aya hii Allah anasisitiza "...haya ni bora kwenu, ikiwa mnajua!".

Faida ya biashara hii imebainishwa wazi kuwa ni:

- (i) Kuokolewa na adhabu kubwa itakayo wasibu watu wote wanaongozwa na Twaaghut kwa ridhaa yao hapa duniani (rejea Qur'an 8:25) na adhabu ya Motoni huko akhera (rejea Qur'an 2:257)



- (ii) Kusamehewa madhambi yetu yote
- (iii) Kustahiki pepo ya Allah (s.w)
- (iv) Kustahiki nusura ya Allah (s.w). Allah (s.w) ameahidi katika aya nyingi kuwanusuru wale wanaoinusuru dini yake.
- (v) Kupata ushindi hapa hapa duniani kwa kuweza kufikia lengo tarajiwa la kuudhihirisha Uislamu katika kila hatua ya mchakato wa kuliendea lengo kuu la kuutawalisha Uislamu katika jamii.

## **Wajibu wa waumini katika jamii kwa muhtasari Kama ulivyobainishwa katika Qur'an**

### **1. Al-Imraan (3:100-120)**

- (i) Kujiepusha kuwatii Mayahudi, Wakristo na viongozi wengine wa jamii kinyume cha kumtii Allah (s.w) na Mtume wake.
- (ii) Kumcha Allah (s.w) na kusimamia hilo mpaka mauti yatukute katika utii huo.
- (iii) Kushikamana na kushirikiana na waumini wengine popote walipo katika kusimamisha Dini ya Allah (s.w).
- (iv) Kuunda kundi la harakati za kuuhuisha na kuusimamisha Uislamu katika jamii.
- (v) Kujiepusha na faraka na ikhtilaaf zisizo za lazima zinazopelekea kuvunja udugu, kupoteza nguvu na kuharibikiwa mambo yetu (8:46).
- (vi) Kuamrisha mema na kukataza mabaya.
- (vii) Kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ipasavyo.
- (viii) Kutowafanya wasiri wetu watu wasiokatika sisi Mayahudi, Wakristo, Washirikina, Wanafiki, Makafiri n.k.
- (ix) Kujiepusha kuwapenda maadui wa Allah kwani wao hawatupendi na wala hawatatupenda abadan.
- (x) Kuwa na subira katika maudhi wanayotufanyia maadui wa Allah (s.w).

## **2. An-Nisaai (4:71-87)**

(i) Kushika tahadhari juu ya maadui kwa:

- ③ Kuwabaini maadui wa Uislamu na Waislamu.
- ③ Kujua mbinu na hila za maadui hao.
- ③ Kutowafanya maadui hao marafiki wa ndani.
- ③ Kuwa wasiri.
- ③ Kuwa wasalama na walinzi.
- ③ Kujiandaa kimazoezi na kivita.

(ii) Kupigana vita na maadui pale inapobidi ili:

- ③ Kuwaokoa wanyonge (watu madhaifu) wanaodhulumiwa katika jamii na mifumo kandamizi ya **kitwaghut**.
- ③ Kupigania Uhuru wa kuabudu (kuondoa fitna)

(iii) Kumtii Allah (s.w), Mtume (s.a.w) na Viongozi wa harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii.

(iv) Kujibu salaam na kulipiza visasi dhidi ya makafiri kwa kadiri wanavyotutendea, ama kuwazidishia kwa ajili ya kuzuia uovu wao na kuwatia adabu wasirudie.

## **3. Al-Anfaal (8:59-66)**

(i) Kuwaandalia makafiri nguvu kwa ajili ya kupambana nao, ambapo nguvu tuziwezazo ni

- ③ Elimu sahihi
- ③ Kuwa na mshikamano na
- ③ Kuwa na Iman thabit isiyotetereka.
- ③ Kuwa na tabia njema ya kiutendaji
- ③ Kujiandaa kisalama na kijeshi

(ii) Kuwa wepesi kutumia mali zetu, nguvu zetu, akili na vipaji vyetu kwa ajili ya Allah (s.w) kwani hiyo ni katika akiba tunayojiwekea, na pia ni amana tutakazoulizwa vipi tumezitumia.

(iii) Kukimbilia amani na salama zaidi kuliko malumbano na

mapambano.

- (iv) Kumtegemea Allah (s.w) katika yale tunayoyafanya.
- (v) Kujiepusha na kukimbia majukumu na wajibu wetu hata kama majukumu na wajibu huo utagharimu nafsi zetu na vile tuvipendavyo.
- (vi) Kuwa na subira kwa masaibu mbalimbali yatakayotukabili; Allah yupo pamoja na wanaovumilia (wanaosubiri).

#### **4. Al-Tawba (9:1-29, 38-42, 111-112)**

- (i) Kushikamana na ahadi na mikataba ya amani au mingineyo iliyo halali tuliyoiweka hata kama tumeiweka na makafiri.
- (ii) Waumini hawana haki ya kuanza wao kuvunja mikataba mpaka watangulie kuvunja wale walioweka nao.
- (iii) Kupigana na makafiri na washirikina na kuwazunguka katika kila pembe mpaka waukubali au kuuheshimu Uislamu.
- (iv) Kusimamia haki za madhaifu hata kama ni katika makafiri ua washirikina maadam tu wanadhulumiwa.
- (v) Kuwatafuta na kuwaangamiza wale wote wanaosimamia maovu na kumuasi Allah(s.w)
- (vi) Kumuogopa Allah (s.w) na kumcha ipasavyo bila kumchelea yeyote.
- (vii) Kushikamana na marafiki wa Allah (s.w) (watu wema, Mitume, Mashahidi) na kuwapiga vita maadui zake.
- (viii) Kusimamia nyumba za Allah (s.w) (misikiti) na kuzipa haki yake kama vituo vya harakati.
- (ix) Kusimamisha swala na kuwaamrisha watu katika hilo.
- (x) Kutoa katika vile Allah alivyoturuzuku na kuwaamrisha watu katika hilo.
- (xi) Kutowafanya maadui wa Allah kuwa marafiki (vipenzi vyetu) hata kama ni katika ndugu zetu wa karibu.

- (xii) Kupigania Dini ya Allah (s.w) kwa mali na nafsi zetu kwa hali zote katika dhiki au wasaa.
- (xiii) Kuamrisha mema.
- (xiv) Kukataza mabaya.
- (xv) Kuhifadhi mipaka ya Allah.
- (xvi) Kujipinda katika kufanya Ibada maalumu (kama vile kuswali, kufunga, kumdhukuru Allah (s.w), n.k.)

### **5. Al-Hajj (22:77-78)**

- (i) Kupigania Dini ya Allah katika haki ya kuipigania kwa kuweka mpango madhubuti wa kitaalam kupitia nyanja zote za maisha, uchumi, siasa, utamaduni, sheria, elimu, n.k.
- (ii) Kusimamisha swala.
- (iii) Kutoa Zakat (Sadaqat)na kutekeleza Ibada nyingine za faradhi na nasunnah.
- (iv) Kushikamana kwa udugu na upendo wa Kiislamu kwa ajili ya Allah (s.w).

### **6. As-Saaf (61:1-14)**

- (i) Kumtukua Allah (s.w) ipasavyo.
- (ii) Kuwa waumini watendaji.
- (iii) Kuwa na mshikamano madhubuti katika kupigania Dini ya Allah (s.w).
- (iv) Kumtii Allah (s.w) na Mtume (s.a.w) ipasavyo.
- (v) Kutomchelea yeyote katika kupigania Dini ya Allah (s.w).
- (vi) Kufanya juhudi za makusudi za kusimamisha Uislamu katika jamii kwa kutumia **mali na nafsi** kwa kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s.w).
- (vii) Kuinusuru Dini ya Allah (s.w) isianguke baada ya kusimamishwa.
- (viii) Kuwa na yakini kuwa ushindi katika kupigania Dini ya Allah uko kwa Waumini.

## **Maandalizi ya mwanaharakati wa kiislamu**

Mwanaharakati wa Kiislamu ni Muislamu Muumini anayepigania Uislamu katika haki ya kuupigania kwa lengo la kuusimamisha na kuudumisha katika jamii. Mtume Muhammad (s.a.w) aliyetumwa na Mola wake kwa lengo la kuusimamisha Uislamu katika jamii (rejea Qur'an 9:33, 61:9, 48:28), ndiye Mwanaharakati Mkuu na ndiye kiigizo cha harakati kwa Ummah huu wa mwisho.

### **Kuandaliwa Mtume (s.a.w)**

Mitume huzaliwa Mitume. Mitume wa Allah (s.w) wamekusudiwa kuwa waalimu na viigizo katika jamii zao. Hivyo Allah(s.w) Mjuzi Mwenye Hekima, aliwaandaa kuanzia mbali kabisa, ili kuwawezesha kufikia lengo makhsusi lililo kusudiwa na ili kuifanya kila hatua ya maisha yao iwe ni funzo kwa Umma zao na Umma zilizofuatia.

Tukirejea historia, tunaona kuwa Mtume (s.a.w) alipata maandalizi ya aina mbili, Maandalizi ya Ki-il-hamu na Maandalizi ya kufunzwa na kuelekezwa moja kwa moja.

#### **(1) Maandalizi ya Ki-il-hamu**

Maandalizi ya Ki-il-hamu ni maandalizi yaliyompitia Mtume (s.a.w) kabla ya kupewa Utume rasmi alipofikia umri wa miaka 40. Katika maandalizi haya hapana mafunzo rasmi yanayotolewa bali tunajifunza kutokana na matukio na mazingira mbali mbali kuwa palikuwa na mpango maalum uliopangwa kumuaanda Mtume(s.a.w). Ili tuone maandalizi haya hebu tuzingatie matukio mbali mbali katika maisha ya Muhammad (s.a.w) kabla ya kupewa Utume ikiwa ni pamoja na tabia yake njema isiyo na mfano wake.

## 1. Kuzaliwa katika kabila la Qurish

Mtume (s.a.w) kazaliwa Makkah katika kabila tukufu la Quraysh, chini ya ulezi wa Babu yake Abdul-Muttalib, aliyekuwa kiongozi wa Maquraysh, ni kielelezo kuwa alistahiki kuchaguliwa kuwa kiongozi wa watu wake. Kabila la Quraish ni katika kizazi cha Nabii Ibrahim (a.s) kupitia kwa Ismail (a.s). Mtume (s.a.w) kuwa Mtume na kiongozi wa Dola ya Kiislamu ni jibu la dua ya Nabii Ibrahimu baada ya kukamilisha kazi ya kujenga upya Ka'abah:

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ  
مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

*Na (kumbukeni khabari hii pia) Ibrahimu alipoinua kuta za nyumba (hii ya Al-Kaaba) na Ismaili (pia); (wakaomba wakasema) "Ee Mola wetu! Tutakabalie (amali yetu hii ya kujenga huu msikiti). Hakika wewe ndiye Mwenye kusikia, na Mwenye kujua." (2:127)*

رَبَّنَا وَأَبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ  
وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٢٨﴾

*"Ee, Mola wetu! Walettee Mtume anayetokana na wao, awesomee Aya Zako, na kuwafundisha Kitabu (chako) na hikima (nyingine) na awafundishe kujitakasa (na kila mabaya). Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, na ndiye Mwenye hikima. (2:129)*

## 2. Kuitwa jina la Muhammad

Kuzaliwa kwa Mtume (s.a.w) na kupewa jina la **Muhammad** na Babu yake, lililo na maana sawa na lile la **Ahmad** alilooteshwa mama yake ni jambo lingine linalothibitisha maandalizi haya. Jila la **Ahmad** lilitabiriwa katika Taurat na Injili kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَدْبِينِ اسْرِعِي لِي يَا رَسُولَ اللَّهِ  
إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ  
بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدٌ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ

*Na (wakumbushe) aliposema Issa bin Maryamu, 'Enyi wana wa Israil!  
Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisaidikishaye yaliyokuwa  
kabla yangu katika Taurat, na kutoa habari njema ya Mtume atakayekuja  
nyuma yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad. Lakini alipowajia kwa  
hoja zilizowazi walisema, 'huu ni udanganyifu uliodhahiri'. (61:6).*

### 3. Kupata malezi bora

Pamoja na kuwa Muhammad (s.a.w) alizaliwa akiwa yatima, alipata malezi bora na ya huruma kupitia kwa mama yake wa kunyonya - Bibi Halima bint Abi-Dhuaby, Mama yake Amina bint Wahhab, Babu yake Abdul-Muttalib na Ami yake Abu-Talib. Hii haikutoka tu kwa bahati nasibu, bali tunafahamishwa katika Qur-an kuwa ni maandalizi maalum aliyoyapanga Allah (s.w).

أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ ۖ وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ ﴿٧﴾

*Je! Hakukukuta yatima akakupa makazi (mazuri ya kukaa)? Na hakukuta hujui kuongoza njia akakuongoza! (93:6-7)!*

### 4. Tabia njema isiyo na mfano

Tabia yake njema isiyo na mfano wake kuanzia utotoni hadi utuuzima wake inaashiria wazi kuwa hakuwa zao la jamii yake, bali aliandaliwa na Mola wake awe vile ili awe kiigizo chema kwa watu wa Umma wake. Allah (s.w) anamsifu Mtume (s.a.w) kwa tabia yake njema katika Qur-an:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

*"Na bila shaka una tabia njema kabisa." (68:4)*

## 5. Ndoa yake na Bibi Khadija

Ndoa ya Mtume (s.a.w) na Mwanamke tajiri: Bibi Khadijah haikutokea kwa bahati nasibu tu, bali ulikuwa mpango madhubuti wa Allah (s.w) ili kumtajirisha Mtume ili aweze kutoa mchango wake katika kuwahurumia na kuwasaidia madhaifu katika jamii yake, na ili awe mfano wa kuigwa na matajiri katika kutoa mali kwa ajili ya Allah katika kuwahurumia wanajamii. Qur-an inatufahamisha:

وَوَجَدَكَ عَائِلًا فَأَغْنَى ﴿٨﴾

*Na akakukuta fakiri akakutajirisha?" (93:8)*

Pamoja na Bibi Khadija kutoa mali yake kwa familia, alimsaidia sana Mtume (s.a.w) katika kuendea lengo lake kabla na bada ya kupewa Utume.


## 6. Kuchukia maovu na kujitenga pangoni

Kuchukia maovu na kujitenga pangoni, ni tukio lingine linaloonyesha kuandaliwa kwa Mtume (s.a.w). Muhammad (s.a.w) tangu angali kijana alijihusisha mno na maisha ya jamii na alikuwa akikereka sana kuona wanyonge wakidhulumiwa. Akiwa na umri wa miaka 20 alijiunga na Chama cha kuwatetea wanyonge dhidi ya Madhalimu. Mtume (s.a.w) alikosa usingizi kwa Sababu ya matatizo ya wengine na alikuwa na shauku kubwa ya kutafuta njia ya kuitoa jamii yake kwenye uovu na upotofu na kuipeleka kwenye wema na uongofu. Katika hali hiyo ilibidi ajitenge pangoni ili kutafuta msaada kwa Muumba Wake na aliupata kwa njia ya ndoto na baadaye kutumiwa Malaika Jibril. Allah (s.w) anamkumbusha Mtume wake juu ya maandalizi haya:

أَلَمْ تَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ﴿١﴾ وَوَضَعْنَا عَنكَ وِزْرَكَ ﴿٢﴾ أَلَّذِي أَنْقَضَ ظَهْرَكَ ﴿٣﴾



*“Je! Hatukukupanulia kifua chako. Na tukakuondolea mzigo wako (mzito) uliovunja mgongo wako?” (94:1-3)*



*“Na akakukuta hujui kuongoza njia akakuongoza?” (93:7).*

Mzigo uliovunja mgongo wa Muhammad (s.a.w) kipindi kile si mwingine ila ile hali ya udhalimu na uovu iliyoshamiri katika jamii yake. Alikuwa na ari kubwa ya kuiondoa ile hali na kusimamisha uadilifu katika jamii lakini hakujua ni vipi atafanikisha hilo.

Kutokana na matukio haya yanayoashiria kuandaliwa kwa Mtume (s.a.w) kabla ya kupewa Utume rasmi, tunajifunza kuwa katika kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii hatuna budi kuzingatia haya yafuatayo:

**Kwanza**, hatunabudi kuwaandaa watoto wetu kuwa Makhaliifa wa Allah (s.w) mapema kabla hata hawajazaliwa. Maandalizi haya yanawezekana pale wazazi wote wawili watakapokuwa wanamtazamo huo wa Ukhalifa. Kisha baada ya watoto kuzaliwa tuwape majina mazuri, tuwalee kwa mapenzi na huruma na kuwafunza tabia njema tangu wangali wachanga. Tuwasomeshe watoto wetu katika shule na vyuo vyenye kufuata mfumo wa elimu wa Kiislamu wenye lengo la kuandaa Makhaliifa wa Allah(s.w)

**Pili**, hatunabudi kuandaa Waalimu na Madaiyah watakao ufundisha Uislamu na taaluma nyingine kwa lengo la kusimamisha Ukhalifa katika jamii.

**Tatu**, Mume na Mke (Baba na Mama) katika familia hawanabudi kushirikiana na kusaidiana kwa huruma na mapenzi ili kupata uwezo wa kuwalea watoto vilivyo na kupata wasaa wa kuyaandea masuala ya jamii.

**Nne**, Wanawake wa Kiislamu, hawanabudi kumfanya Bibi Khadijah, Mkewe Mtume (s.a.w), kuwa kiigizo chao katika kuwasaidia na kuwaliwaza waume zao hasa wanapokuwa katika harakati za kuuhiisha na kuusimamisha Uislamu katika jamii.

**Tano**, hatunabudi kuchukia maovu na dhulma wanazofanyiwa wanyonge na madhaifu katika jamii na kuwa tayari kuondoa maovu na dhulma kwa mikono yetu pale tunapoweza. Na pale ambapo hatuna uwezo wa kutumia mikono, tutoe makemeo, vinginevyo tuingie "**pangoni Hira**" tutafute msaada wa Allah (s.w).

**Sita**, hatunabudi kujipamba na tabia njema kwa kadiri iwezekanavyo. Mtu mwema hutambulika na kukubalika kwa watu kwa urahisi.

**Saba**, hatunabudi kuimarisha uchumi, kwani uchumi ndio nyenzo kuu ya kuusimamisha Uislamu katika jamii.

## (2) Maandalizi ya Kimafunzo

Maandalizi ya kimafunzo ni maandalizi yaliyompitia Mtume (s.a.w) pale alipoanza kuletewa wahyi na Malaika Jibril (a.s). Maandalizi haya tunayapata katika Qur-an katika wahay wa mwanzo mwanzo kumshukia Mtume (s.a.w) katika Suratul A'laq (96:1-5), Suratul-Muzzammil (73:1-10) na Suratul-Muddaththir (74:1-7).

### Suratul-A'laq (96:1-5)

أَقْرَأْ بِأَسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ① خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ② أَقْرَأْ وَرَبُّكَ  
الْأَكْرَمُ ③ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ④ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ⑤

*“Soma kwa jina la Mola wako aliyeeumba Aliyemuumba mwanaadamu kwa a'laq. Soma na Mola wako ni karimu sana.*

*Ambaye amefundisha kwa (msaada wa) kalamu. Amemfundisha mwanaadamu mambo aliyokuwa hayajui." (96:1-5)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa amri ya kwanza aliyopewa Mtume (s.a.w), na kwa hiyo waumini wote wa Ummah wake, ni kusoma au kutafuta elimu kwa ajili ya Allah (s.w). Kusoma kwa jina la Allah ni kusoma kwa lengo la kumuwezesha muumini kumjua na kumuabudu Mola wake vilivyo kisha kusimamisha Ukhalifa katika jamii.

Katika mazingira ya kupewa amri hii ya kwanza, pale pangoni katika kilima cha Hira (Jabal-Hira), Mtume (s.a.w) alishinikizwa kusoma na Malaika Jibril kwa kumbana (kumkumbatia kwa nguvu) mara tatu pale alipojitetea kuwa hajui kusoma. Kubanwa huku kwa Mtume (s.a.w) na Malaika Jibril kunaashiria kuwa elimu kwa waumini ni amri ya kwanza inayotakiwa itekelezwe kwa hima na kwa taklifu kubwa.

Elimu ni amri ya kwanza inayotakiwa itekelezwe kwa juhudi na bidii zote. Ndiyo silaha kuu itakayowawezesha waumini kupata ushindi wa kuusimamisha Uislamu katika jamii. Tukirejea nyuma katika historia, takrima ya kwanza aliyofanyiwa Adam (a.s) na Mola wake, ili kuandaliwa kuwa khalifa wa Allah (s.w) hapa duniani ni kufundishwa majina ya vitu vyote; ikimaanisha fani zote za Elimu anazohitajia binaadamu ili aweze kuwa kiongozi wa dunia kwa niaba ya Allah (s.w). Pia tunajifunza kuwa chanzo cha fani zote za elimu ni Allah (s.w).

### **Suratul-Muzzammil (73:1-10)**

يَتَأْتِيهَا الْمُرْمِلُ ﴿١﴾ فَمِ الْإِلَّهِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢﴾ نِصْفَهُ أَوْ أَنْقَضَ مِنْهُ قَلِيلًا

﴿٣﴾ أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلًا ﴿٤﴾

*“Ewe uliyejifunika maguo. Simama usiku kuacha (kuswali) ila muda mdogo (tu hivi). Nusu yake au upunguze kidogo au uzidishe na soma Qur-an vilivyo. (73:1-4)*

إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا ﴿٥﴾ إِنَّ نَاشِئَةَ اللَّيْلِ هِيَ  
 أَشَدُّ وَطْأًا وَأَقْوَمُ قِيْلًا ﴿٦﴾ إِنَّ لَكَ فِي النَّهَارِ سَبْحًا طَوِيلًا ﴿٧﴾ وَأَذْكُرِ  
 اسْمَ رَبِّكَ وَتَبَتَّلْ إِلَيْهِ تَبْتِيلًا ﴿٨﴾

*Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito. Hakika kuamka usiku kunawafikiana zaidi na moyo na maneno yake yanatuwa zaidi. Hakika mchana unashughuli nyingi. Na litaje jina la Mola wako na ujitupe kwake kwa kweli. (73:5-8)*

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٩﴾ وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا  
 يَقُولُونَ وَأَهْجُرْهُمْ هَجْرًا جَمِيلًا ﴿١٠﴾

*(Yeye Ndiye)Mola wa mashariki na magharibi. Hapana Mola ila yeye, basi mfanye kuwa mlinzi wako. Na subiri juu ya hayo wayasemayo na uwaepuke mwepuko mwema." (73:9-10)*

Aya ya kwanza ya sura hii inaashiria kuwa huu ni wahyi wa mwanzo mwanzo uliofuatia wahyi wa kwanza. Katika Hadith iliyosimuliwa na bibi Aysha (r.a), tunafahamishwa kuwa Mtume (s.a.w) alistushwa sana na lile tukio la Jabal Hira, la kulazimishwa kusoma na Malaika Jibril ambaye ilikuwa ni mara yake ya kwanza kukutana naye.

Mtume(s.w) alirudi nyumbani akiwa anayetemeka kama mtu mwenye homa kali. Alimuomba mkewe Khadija amfunike nguo. Baada ya muda hali ile ya khofu iliisha na kuweza kumhadithia mkewe yale yaliyomtokea. Alipomuona tena Jibril (a.s) anamjia kumletea wahay uliomo mwanzoni mwa sura hii (73:1-10) Mtume (s.a.w) alistuka tena na kujaribu kujihami asijefikwa na yale yaliyo mfika pangoni kwa kujifunika tena nguo. Lakini bado Jibril alimuendea Mtume (s.a.w) katika hali ile ile ya kujifunika na kumfikishia ujumbe huu wenye kumuamrisha kufanya yafuatayo:

- (i) Kusimama kwa swala ya usiku kwa kitambo kirefu - kati ya saa 4 (1/3) hadi 8(2/8) za usiku.
- (ii) Kusoma Qur-an kwa mazingatio.
- (iii) Kumdhukuru au kumkumbuka Allah (s.w) kila wakati.
- (iv) Kujitupa kwa Allah kikweli (kumcha Allah ipasavyo)
- (v) Kumfanya Allah kuwa mlinzi (wakili).
- (vi) Kufanya subira juu ya yale wayasemayo makafiri na kuwaepuka mwepuko mwema.

Imebainishwa wazi kuwa Mtume (s.a.w) amepewa amri hizi ili iwe maandalizi ya kupokea kauli nzito. Kauli nzito si nyingine ila lile lengo alioletwa kwalo la kusimamisha Uislamu katika jamii.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ  
عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

*Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki ili aijaalie kushinda (Dini hii) Dini zote, ijapokuwa watachukia hao washirikina. " (9:33)*

### Suratul-Muddaththir (74:1-7)

يَتَأْتِيهَا الْمُدَّثِّرُ ﴿١﴾ قُمْ فَأَنْذِرْ ﴿٢﴾ وَرَبِّكَ فَكَبِيرٌ ﴿٣﴾ وَتِيَابِكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾  
وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ﴿٥﴾

*Ewe uliyejifunika maguo. Simama uonye (viumbe). Na Mola wako umtukuze. Na nguo zako uzisafishe. Na Mabaya yapuuze, (endelea kuyapuza). (74:1-5)*

وَلَا تَمُنَّ بِتَسْتَكْبِرُ ﴿٦﴾ وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ﴿٧﴾

*Wala usiwafanyie ihsani (viumbe) ili upate kujikithirishia (wewe hapa duniani). Na kwa ajili ya Mola wako fanya subira (kwa kila yatakatayokufika). (74:6-7)*

Muda mfupi baada ya kupewa amri sita zilizomo katika

suratul-Muzzammil (73:1-10) na kuanza kuzitekeleza, Mtume (s.a.w) akiwa katika hali ile ile ya kujifunika funika aliamrishwa tena na Mola wake, ili kumaliza kazi ya maandalizi, kufanya yafuatayo:

- (i) Kusimama na kuonya - kulingania Uislamu.
- (ii) Kumtukuza Allah ipasavyo
- (iii) Kutakasa nguo(kuwa msafi kimwili na kitabia)
- (iv) Kupuuza mabaya.
- (v) Kufanya ihsani kwa ajili tu ya kutafuta radhi za Allah (s.w) tu.
- (vi) Kufanya subira kwa ajili ya Allah.

### **Mafunzo**

Kutokana na maandalizi haya ya awali aliyopewa Mtume (s.a.w) mwanzoni mwanzoni mwa Utume tunajifunza kuwa ili tuweze kusimamisha Uislamu katika jamii (kaulan thaqila) kama alivyofanikiwa Mtume (s.a.w) na maswahaba zake kuusimamisha, tunajifunza yafuatavyo:

- (1) **Elimu katika Fani zote**, ukiacha ila ya uchawi iliyoharamishwa,ndio nyenzo ya msingi ya kutuwezesha kusimamisha Uislamu katika jamii. Hivyo Waislamu hawanabudi kutilia mkazo suala la elimu na kuandaa mitaala na mazingira yatakayowezesha kuielimisha jamii kwa lengo la kusimamisha Ukhalifa katika ardhi.
- (2) **Kisimamo cha usiku**, ni nyenzo kuu ya pili inayofuatia katika maandalizi ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Allah (s.w) anatubainishia kuwa hekima ya kupewa amri ya kisimamo cha usiku (Qiyamullayl) ni ili tupate maandalizi ya **Ukomandoo** yatakayotuwezesha kukabiliana na suluba (misuko suko) ya kusimamisha Uislamu katika jamii. Allah (s.w) anabainisha pia kuwa maandalizi haya hayafai mchana ila usiku kwa Sababu kuna mazingira mazuri ya utulivu yatokayompelekea huyu askari wa Allah(s.w) kuwa na khushui (unyenyekavu) ya hali ya juu inayohitajika kuomba

hidaya na msaada kutoka kwa Allah (s.w).

Pia kuamka usiku na kukatisha utamu wa usingizi katika theluthi ya mwisho ya usiku, humpa Muislamu zoezi la uvumilivu na subira. Hivyo, ni wazi kuwa, **kisimamo cha usiku**, kikitekelezwa vilivyo, kinauwezo mkubwa wa kumfanya Muislamu awe **komandoo** na kusimamisha Uislamu katika jamii kwa hali yoyote iwayo. Hivyo kwa waumini wa kweli, wanaojua kuwa wanadhima ya kuusimamisha Uislamu katika jamii na kuuhami usiporomoke baada ya kusimama **kisimamo cha usiku**, si jambo la khiari kwao kama Mola wao anavyowatanabahisha:

أَمَّنْ هُوَ قَنْبِثٌ عَائِءٌ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا يَحْذَرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُو رَحْمَةَ رَبِّهِ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ  
إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولَئِكَ الْأَلْبَابِ ﴿٩﴾

*Je, afanyae Ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa Akhera na kutarajia rehema ya Mola wake (ni sawa na asiyefanya hayo)? Sema: "Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?" Wanaatanabahi ni wale wenye akili tu. "(39:9)*

- (3) **Kusoma Qur-an kwa mazingatio**, kwa lengo la kuifanya kuwa dira pekee ya maisha yetu ya kila siku, ni nyenzo nyingine itakayotuwezesha kusimamisha Uislamu katika jamii. Uislamu ni mfumo wa maisha wa kutii na kufuata utaratibu wa kuendesha maisha ya kibinafsi na ya kijamii anaouridhia Allah (s.w). Utaratibu huu wa maisha anaoridhia Allah (s.w) umeainishwa na Qur-an, kitabu chake cha mwisho. Hivyo, waumini wa kweli; ili waweze kusimamisha Uislamu katika jamii, hawanabudi kuisoma Qur-an kwa mazingatio kiasi cha kuweza kuielewa vilivyo na kuifanya

mwongozo wa kukiendea kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na kijamii. Vile vile jamii ya Waislamu hainabudi kuandaa mtaala wa kufundisha Qur-an kwa lengo la kuwaandaa wasomaji wa rika zote kuwa Makhaliifa wa Allah (s.w).

- (4) **Kumdhukuru na kumtukuza Allah (s.w)**, ni nyenzo nyingine muhimu itakayowawezesha waumini kusimamisha Uislamu katika jamii. Ili Waislamu wawe na msimamo thabiti, hawanabudi kuwa na yakini juu ya kuwepo Allah (s.w) na sifa zake tukufu. Imani ya kweli juu ya Allah (s.w) inathibitishwa na matendo ya Muumini ya kila siku pale atakapofuata maagizo na kuchunga mipaka ya Allah (s.w) katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake.
- (5) **Kujitupa kwa Allah kwa kweli au kumtii Allah (s.w) kwa unyenyekevu**, ni nyenzo nyingine ya kumuwezesha Muumini kusimamisha Uislamu katika jamii. Pamoja na kuwa kusimamsiha Uislamu ni **kauli nzito** (jambo zito), Muumini mwenye kujitupa kwa Allah kwa kweli, hatamchelea yeyote awaye au lolote zito liwalo, katika kutekeleza amri ya Allah (s.w) iliyombele yake.
- (6) **Kumfanya Allah kuwa Mlinzi Pekee**, ni nyenzo nyingine inayompa Muumini ujasiri wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Kuweka tegemezi kwa Allah (s.w) ambaye ni Al-qahharu (mwenye nguvu juu ya kila kitu) humfanya Muislamu asichelee kizuizi au nguvu yoyote inayozuia Uislamu kusimama.
- (7) **Kusimama na kuonya** ni amri ya kuwafahamisha watu juu ya upweke wa Allah (s.w) kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na kisha kuwafahamisha namna ya kumuabudu Allah (s.w) pekee katika kile kipengele cha maisha. Baada ya kufikisha ujumbe huu wa Tawhiid, kwa



hekima na mawaidha mazuri (rejea Qur-an 16:125), Mtume na Waumini kwa ujumla wanaamrisha kuwaonya watu juu ya adhabu kali itakayowafika wale wote watakaoshi kinyume cha Tawhiid, katika maisha ya akhera.

Pia amri hii ya kuwaonya watu inakwenda sambamba na kuwabashiria malipo mema watakatopata wasimamishaji wa Tawhiid katika maisha ya akhera. Kuufundisha Uislamu na kuweka wazi faida itakayopatikana kwa wale watakaoufuata vilivyo na hasara itakayowafika wale watakaoukanusha, ni hatua muhimu na ya msingi mno katika harakati za kusimaisha Uislamu katika jamii.

(8)**Kutakasa nguo**, ni amri inayoashiria kuwa mwenye kulingania Uislamu anatakiwa awe mfano wa kuigwa kwa tabia njema. Pamoja na mlinganiaji kutekeleza amri ya kutakasa nguo zake na mwili wake ili awe kivutio kwa watu atakaokutana nao katika harakati za kulingania Uislamu, anatakiwa awe na tabia njema itakayovuta usikivu wa watu. Katika kutekeleza amri hii Mtume (s.a.w) alikuwa akipendelea vazi jeupe na kujipaka manukato ili asiwe kero kwa watu kutokana na harufu mbaya inayotokana na nguo chafu na majasho.

Sambamba na usafi huu wa nguo na mwili, Mtume (s.a.w) alikuwa na tabia njema kabisa.

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

*"Na bila shaka una tabia njema kabisa." (68:4)*

Mlinganiaji kuwa kiigizo kwa tabia inasisitizwa katika aya zifuatazo:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبِيرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ  
 أَنْ تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾

*Enyi mlioamini! Mbona, (kwa nini) mnasema msiyoyatenda?  
 Ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema  
 msiyoyatenda. (61:2-3)*

- (9) **Kupuuza Mabaya**, ni pamoja na kutojali au kutokatishwa tamaa na mabaya unayofanyiwa na maadui wa Uislamu. Pia amri hii ya kupuuza mabaya ni pamoja na kujiepusha kuyafanya, kutoyathamini maovu hatakama yanafanywa na watu maarufu na kuyachukia. Kupuuza mabaya ni nyenzo nyingine muhimu katika kusimamisha Uislamu. Kama muumini hatakuwa na tabia ya kupuuza mabaya anayofanyiwa na maadui wa harakati za kusimamisha Uislamu, atafikishwa mahali pa kumkatisha tamaa na kususa harakati.
- (10) **Kufanya ihsani kwa ajili tu ya kutafuta radhi za Allah (s.w)**, ni amri inayowataka wanaharakati wa kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii wasitegemee malipo ya kazi hii kutoka kwa watu bali wategemee malipo yao kutoka kwa Allah (s.w). Kazi ya kusimamisha Uislamu katika jamii, Allah (s.w) ameifananisha na biashara kati yake na waumini ambapo waumini wanamuuzia Allah (s.w) mali zao na nafsi zao, naye Allah atawalipa malipo makubwa yanayobainishwa katika aya zifuatazo:

﴿إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَىٰ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِآنَ لَهُمُ الْجَنَّةُ  
 يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدًّا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَةِ  
 وَالْإِنجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبِشِرُوا بِبَيْعِكُمْ  
 الَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ وَذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١١﴾

*Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waislamu nafsi zao na mali zao (watoe nafsi zao na mali zao katika kupigania Dini) ili na yeye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu; wanaua na wanauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati na Injili na Qur-an. Na ni nani atokelezaye zaidi ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye (Mwenyezi Mungu). Na huko ndiko kufuzu kukubwa. "(9:111)*

يَتَّيَّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا هَلْ أَذُكُّمَ عَلَىٰ تَجَارَةٍ تُنَجِّيْكُمْ  
 مِنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿١١٠﴾

*Enyi mlioamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuoieni na adhabu iumizayo?(61:10)*

تُوْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ  
 ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١١١﴾

*Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganieni Dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na mali zenu. Haya ni bora kwenu ikiwa mnajuwa (61:10-11)*

**(11)Kufanya Subira kwa ajili ya Allah**, ni nyenzo nyingine ya msingi itakayowawezesha Waumini kusimamisha Uislamu katika jamii. Katika harakati za kusimamisha Uislamu katika

jamii, kuna kero na bughudha nyingi zinazoandaliwa na kusimamiwa na wapinzani wa Uislamu. Ukirejea historia ya Mtume (s.a.w), kero hizi huanza na kujenga mazingira ya kukatisha tamaa. Katika mazingira hayo, Mtume (s.a.w) aliitwa mwongo, mwenda wazimu, mtunga mashairi, mchawi, aliyepagawa, mkatikiwa na kheri (Abtari), n.k.

Katika mazingira ya sasa makafiri wanajitahidi kuwakatisha tamaa wanaharakati kwa kuwaita siasa kali (fundamentalist), mashabiki wa Kidini (fanatics), magaidi (terrorists), n.k. Allah (s.w) anatumrisha tusbiri juu ya hayo wayasemayo dhidi yetu na tuwaepuke mwepuko mwema. Kuwaepuka mwepuko mwema ni kuyapuza hayo wayasemayo dhidi yetu na tusilumbane nao wakajatutoa kwenye agenda yetu. Jibu la tusi kwa muungwana ni "hewala" na jibu la muumini kwa muumini ni "salama".

وَعِبَادُ الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ

الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا ﴿١٣﴾

*"Na waja wa Rahmani, ni wale wanaokwenda ulimwenguni kwa unyenyekevu; na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu (maneno ya) salama." (25:63).*

Tukirejea historia, baada ya makafiri kushindwa kuzuia harakati za kusimamisha Uislamu kwa maneno ya kukatisha tamaa, waliandaa nguvu za kuzuia Uislamu kwa matendo kama vile kutesa, kufunga gerezani, kufukuza nchini na kuua. Haya ndiyo mazingira halisi katika harakati za kusimamisha Uislamu na ndiyo sunnah ya harakati aliyoiweka Allah (s.w) kama anavyotukumbusha:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيْطِينِ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ  
إِلَى بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ فَذَرْهُمْ وَمَا  
يَفْتَرُونَ ﴿١١٢﴾

*Na namna hii tumemfanyia kila Nabii maadui; (nao ni)  
mashetani katika watu na (mashetani katika) majini. Baadhi  
yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupambapamba ili  
kuwadanganya. Na kama Mola wako angalipenda  
wasingalifanya hayo, (angewalazimisha kwa nguvu kutii).  
Basi waache na uwongo wao. (6:112)*

Hivyo waumini hawanabudi kuwa na subira ya hali ya juu ya  
kuhimili vitimbi vya maadui wa harakati za Uislamu. Tukumbuke kuwa kusimamisha Uislamu ni kazi ngumu (kauli  
nzito) yenye vikwazo na mitihani mingi kama  
tunavyokumbushwa.

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ  
مَسَّتْهُمُ الْبَأْسَاءُ وَالضَّرَّاءُ وَزُلْزِلُوا حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ آمَنُوا  
مَعَهُ مَتَى نَصْرُ اللَّهِ أَلا إِنَّا نَصْرُ اللَّهِ قَرِيبٌ ﴿١١٤﴾

*Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na  
mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu?  
Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana  
hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: "Nusura  
ya Mwenyezi Mungu itafika lini?" Jueni kuwa nusura ya  
Mwenyezi Mungu iko karibu. (2:214)*

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ  
وَيَعْلَمِ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٢﴾

*Je! Mnadhani mtaingia Peponi hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale waliopigania Dini ya Mwenyezi Mungu miongoni mwenu, na kuwapambanua waliofanya subira? (Sharti yaonekane kwanza haya hapa ulimwenguni). (3:142)*

## Zoezi la Pili

1. (a) Orodhesha sifa kumi (10) za waumini zilizoainishwa katika al-Muuminuun (23:1-11) na Al-Furqaan (25:63-76).
- (b) Orodhesha sifa za waumini zilizoainishwa katika sura zifuatazo:
  - (i) As-Sajdah (32:10-20).
  - (ii) Al-Ahzab (33:35).
  - (iii) Al-Ma'arij (70:19-35).
2. (a) Kwa mujibu wa Qur-an kafiri ni \_\_\_\_\_
- (b) Orodhesha sifa za makafiri kama zilivyoainishwa katika sura zifuatazo:
  - (i) As-Sajdah (32:10-22).
  - (ii) Al-Ma'arij (70:19-35).
3. (a) Kwa mujibu wa Qur-an wanafiki ni \_\_\_\_\_
- (b) Orodhesha sifa za wanafiki kama zilivyoainishwa katika sura zifuatazo:
  - (i) Al-Baqara (2:8-20).
  - (ii) Al-Ahzab (33:12-20).
  - (iii) Al-Munaafiquun (63:1-8).
4. Rejea surat bani Israil (17:23-40) Surat Luq-man (31:12-19) na Surat ul-Hujurat (49:1-13), kisha ujibu maswali yafuatayo:
  - (a) Orodhesha mambo mema anayotakiwa ayafanye mtu ili kujenga upendo na mshikamano katika jamii.

- (b) Orodhesha mambo mabaya anayotakiwa mtu ajiepushe nayo ili kuondoa chuki, uhasama na uadui katika jamii.
5. Orodhesha wajibu wa waumini katika jamii kama ulivyoainishwa katika sura zifuatazo:
- (a).Al-Imran (3:100-120)
  - (b).An-Nisaai (4:71-87)
  - (c).Al-Anfal (8:59-66)
  - (d).As-Saaf (61:1-14)
6. Tunajifuanza nini kutokanana kuandaliwa mtume (s.a.w)
- (a).Ki-il-ham?
  - (b).Kimafunzo?



## Sura ya Tatu

# MAFUNZO YA SURA ZILIZOCHAGULIWA KATIKA JUZUU AMMA

### Utangulizi:

Sura hizi zimechaguliwa ili kumwezesha msomaji kubaini ujumbe wa Qur'an na kisha kuingiza katika utekelezaji. Aidha sura hizi zimechaguliwa ili kukidhi mahitaji ya muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule za sekondari. Hivyo msomaji anatarajiwa:

- Kusoma kila sura kwa kuzingatia hukumu za usomaji wa Qur'an
- Kuhifadhi kila sura na tafsiri yake
- Kubaini ujumbe na mafunzo ya kila sura
- Kuingiza ujumbe na mafunzo katika utendaji wa maisha ya kila siku.

Katika sura hii tutapitia mafunzo ya sura zilizochaguliwa kutoka juzuu Amma kama ifuatavyo:-

1. Al-Fatiha	(1)
2. Al-A'ala	(87)
3. Adh-Dhuha	(93)
4. Alam-Nashrah	(94)
5. At-Tyn	(95)
6. Al-Bayyinah	(98)
7. A t- Takaathur	(102)
8. Al-A'sr	(103)
9. Al-Humazah	(104)
10 Al-Fyl	(105)

11. Quraysh	(106)
12. Al-Mau'un	(107)
13. Al-Kauthar	(108)
14. Al-Kaafiruun	(109)
15. An-Nasr	(110)
16. Al-Lahab	(111)
17. Al-Ikhlās	(112)
18. Al-Falaq	(113)
19. An-Naas	(114)

Sura hizi zimechaguliwa ili kumuwezesha msomaji kuubaini ujumbe wa Qur'an na kisha kuingiza katika utekelezaji. Aidha sura hizi zimechaguliwa pia ili kukidhi mahitaji ya muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule za sekondari.

Katika kuzipitia sura hizi msomaji anatarajiwa aweze kufanya yafuatayo:

- (i) Kusoma kila sura kwa ufasaha kwa kuzingatia hukumu ya usornaji wa Qur'an (Ah- kami)
- (ii) Kuhifadhi kila sura na tafsiri yake.
- (iii) Kubaini ujumbe na mafunzo yapatikanayo katika kila sura
- (iv) Kuingiza ujumbe na mafunzo haya ya Qur'an katika utendaji katika maisha ya kila siku yakibinafsi na kijami

Ilikufikia malengo haya, hasa lengo la (i) na (ii) msomaji anashauriwa ajiunge na Darasa duara au madarasa ya usomaji Qur'an. Katika sura hii tutajishughulisha tu na kubainisha ujumbe na mafunzo yatokanayo na kila sura.

# 1. Suratul-Fatihah

1. Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma Mwenye Kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ①

2. Sifa zote njema zinamstahikia  
Allah. Bwana na mlezi wa viumbe  
vyote.

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ②

3. Mwingi wa Rehma, mwenye  
kurehemu.

الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ③

4. Mwenye kumiliki siku ya malipo.

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ④

5. Wewe tu ndiye tunayekuabudu,  
na wewe tu ndiye tunayekuomba  
msaada.

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ⑤

6. Tuongoze katika njia iliyonyooka.

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ⑥

7. Njia ya wale uliowaneemesha,  
sio ya wale waliokasirikiwa,  
wala ya wale waliopotea.

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ

غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ⑦

## Maelezo juu ya Sura

Suratul-Faatihah ni katika surah za mwanzo mwanzo kushuka, ni sura ya tano kushuka na pia ni sura ya kwanza kushuka nzima. Kabla ya suratul-faatihah zilitangulia kushuka aya chache chache katika suratul-Alaq (1), suratul-Qalam (2), Suratul-Muzzammil (3) na Suratul-Muddaththir (4). Pia suratul-Faatihah ndiyo sura ya kwanza katika mpangilio wa sura za Qur'an (Al-Mushaf). Kutokana na nafasi yake katika Mushaf, ujumbe wake na

matumizi yake katika swala, suratul-faatihah imepewa majina yafuatayo:

**(i) Faatihatul-Kitaab**, yaani mwanzo wa kitabu. Kitabu hapa inakusudiwa Qur'an, yaani Suratul faatihah ndiyo sura ya kwanza ya Qur'an.

**(ii) Ummul-Kitaab**, yaani msingi au asili ya kitabu (Qur'an). Kutokana na maudhui yake, suratul-faatihah inasimama kama Utangulizi wa Qur'an. Maudhui ya suratul-fatihah ni dua, tunayoomba katika aya ya 6 na 7. Na dua hii Allah (sw) anajibu kwa kutuletea sura zote za Qur'an zilizobakia pale anapojibu mwanzoni mwa sura ya pili inayofuatia hii: -

ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾

*"Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake, ni uwongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu" (2:2)*

**(iii) Suratus-Swala**, yaani sura ya kuswalia. Suratul-faatihah ndiyo nguzo kubwa ya swala na swala haiswihi bila ya kusoma suratul-faatihah katika kila rakaa, kwa mujibu wa Hadithi ya Mtume (s.a.w).

**(iv) Assab'ul-Mathaani**, yaani aya saba ambazo husomwa mara kwa mara katika swala na katika ufunguzi wa shughuli mbalimbali. Hii ameirejea Allah (sw), kama tunu kwa Mtume (s.a.w) na umma wake kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَلَقَدْ آتَيْنَاكَ سَبْعًا مِّنَ الْمَثَانِي وَالْقُرْآنَ الْعَظِيمَ ﴿٨٧﴾

*"Na tumekupa (hizi aya) saba zisomwazo mara kwa mara na (tunakupa Qur'an) tukufu" (15:87)*

**(v) Surat-ul-Hamdu**, yaani sawa ambayo, baada ya Bismillah inaanza kwa kumuhimidi(kumsifu) allah (s.w)

### **Mafunzo**

Ukiipitia suratul-faatihah kwa makini utagundua kuwa kimafunzo, suratul-faatihah imegawanyika katika sehemu kuu tatu:

- (i) Kumsifu na kumtukuza Allah (sw) (aya 1-4)
- (ii) Kutoa ahadi ya kumuabudu Allah (sw) pekee na kumtegemea yeye pekee (aya ya 5).
- (iii)Kumuomba mwongozo wa maisha (aya ya 6-7)

Mafunzo tunayoyapata kutokana na kila sehemu ni kama ifuatavyo:

### **(i) Kumsifu na kumtukuza Allah (sw)**

"Allah" ni jina la dhati la Mungu muumba ambaye ni mpweke. Hapana wingi wa "Allah". Hivyo si sahihi kufasiri neno "Allah" kwa maana ya Mungu, kwani wingi wa Mungu ni miungu. Tafsiri ya Allah kwa kiswahili ni "Mwenyezi Mungu". Hapana wingi wa "Mwenyezi Mungu". Wafasiri wengi hupendelea kulibakisha neno "Allah" bila kulifasiri katika lugha husika.

**Aya ya kwanza** ya suratul-faatihah ni "Bismillahir Rahmaanir Rahiim" Sura hii ya kwanza kuanza kwa "Bismillahir Rahmaanir Rahiim" inatufunza kuwa tunapaswa kuanza kila jambo letu kwa kumtanguliza Allah (sw), Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Tukianza kila jambo letu kwa "Bismillahir Rahmaanir Rahiim" tunapata faida zifuatazo:

- (1)Kuomba msaada kwa Allah (sw) ili alifanikishe na alibariki lile tunaloanza kulifanya.

(2)Kujikinga na maovu. Muumini mwenye tabia ya kuanza kila jambo lake kwa "Bismillahir Rahmaanir Rahiim" hatathubutu kufanya maasi kwa kumtanguliza Allah (sw)

(3)Humzoesha muumini kubakia katika Ibada katika kila kipengele cha maisha yake.

**Aya ya pili** inatutaka tumuhimidi au tumsifu Allah (sw) kwa kila sifa njema. Kwani yeye ndiye Bwana Mlezi wa viumbe vyote. Allah (sw) pamoja na ukweli kuwa ndiye Muumba pekee wa viumbe vyote, pia ndiye pekee anayevilela mpaka kuvifikisha katika malengo yaliyokusudiwa katika maisha ya hapa duniani na huko akhera.

**Aya ya tatu** inatufahamisha kuwa Allah (sw) pamoja na kuwa **Rabbil-'Aalamiin**,pia yeye ni **Ar-rahmaanir** na **Ar-rahiim** sifa ya **Ar-rahmaan** huonesha kiwango cha hali ya juu cha ufadhili na huruma alichonacho kwa viumbe vyake. Katika kiwango hiki huvifadhili na kuvihurumia viumbe vyote - vidogo na vikubwa, vema na viovu bila ya ubaguzi wowote.

Sifa ya **Ar-rahiim** huonesha upendeleo maalumu katika kufadhili na kuhurumia. Yaani katika maisha ya akhera ufadhili na huruma zake zitakuwa juu ya watu wema tu.

**Aya ya nne** inatufahamisha kuwa Allah (sw) pia ndiye **Mmiliki** au **Mfalme** pekee katika maisha ya akhera. Pamoja na kwamba hapa duniani, Allah pekee ndiye anayestahiki kuwa mfalme wa walimengu wote, bado binadamu kwa uhuru aliopewa na yeye Mwenyewe Muumba, anaweza kutakabari na kujitangazia Ufalme dhidi ya ufalme wa Allah (sw). Mfalme Firauni wakati wa Nabii Mussa (a.s) alitangaza kifua mbele akasema "Mimi ndiye Bwana (Mola) wenu Mkuu" (79:24).

Na ni kawaida ya Wafalme wa Kitwaghuti wa zama zote kutakabari na kujisikia kuwa ufalme wao ni wa juu zaidia kuliko ule wa Allah (sw). Kinyume chake katika maisha ya akhera hapana yeyote atakayethubutu kujitangazia ufalme mbele ya ufalme wa Allah (sw). Kuthibitisha hilo siku hiyo katika hadhara

ya viumbe vyote, Allah (sw) atanadi, "Leo Ufalme ni wa nani?" Hapana yeyote atakayethubutu kunyanyua mdomo kujibu swali hili. Ndipo Allah (sw) mwenyewe atabainisha kwa viumbe vyote kuwa: "Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye nguvu" (40:16)

**(ii)Kutoa ahadi ya kumuabudu Allah (sw) na kumtegemea yeye pekee**

Baada ya mja kuyakinisha kuwa Allah (s.w) ni Bwana Mlezi pekee wa walimwengu wote, mwenye kurehemu viumbe kwa upeo wa pekee na Mmiliki (Mfalme) pekee wa maisha ya akhera, hutoa ahadi kwa uzito mkubwa kuwa hatamuabudu au kumtegemea yeyote kinyume na Allah (s.w). Kwa mtizamo wa Qur'an kumuabudu Allah (s.w), ni kumtii Allah (s.w) kwa kufuata kanuni na sharia alizotuwekea katika kukiendea kila kipengele cha maisha ya binafsi na maisha ya jamii. Kufanya kitendo chochote kile nje ya kanuni na sharia za Allah (s.w) zilizobainishwa katika vitabu vyake na sunnah ya Mitume wake ni kumuasi Allah (s.w) na kumuabudu shaitwani au yeyote yule aliyekuwekea na ukatii kanuni na sharia zake dhidi ya kanuni na sharia za Allah (s.w).

Ni muhali kumuabudu Allah (s.w) pekee bila ya kumtegemea yeye pekee. Kwa mfano kama mtu anahisi kuwa usalama wa maisha yake na uhai wake uko juu ya watu wenye mamlaka na nguvu juu yake itabidi aishi kwa kufuata kanuni na sharia atakazowekewa na watu hao hata kama ni dhidi ya kanuni na sharia za Allah (s.w). Hivyo mtu huyu, hata kama anaswali, anatoa zaka, anafunga Ramadhani na kuhiji Makka, hata kuwa ni mja wa Allah (s.w), bali atakuwa ni mja wa wale anaowategemea kwa usalama wa maisha yake na uhai wake; na hatakuwa ni mwenye kumuabudu Allah (sw) bali atakuwa anawaabudu wale anaowatii kwa kufuata kanuni na sharia walizomuwekea katika kuendea maisha yake ya kila siku ya binafsi na kijamii.

Hivyo mja mwenye yakini kuwa Allah (sw) ni "Rabbil-a'alamiin" na ni "Rrahmaani", na ni "Rrahiim" na ni "Maliki yawmidiin",

hanabudi kuamua kutii kanuni na sharia za Allah (sw) pekee katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii na hatomchelea yeyote akiwa na yakini kuwa hapana yeyote wa kumnufaisha au kumdhuru nje ya qadar ya Allah (sw)

**(iii) Kuomba mwongozo wa maisha**

Kwa mujibu wa Qur'an, njia iliyonyooka ni Uislamu (Al-Islaam). Uislamu ni utaratibu wa maisha aliouweka Allah (sw) unaomuwezesha binaadamu kuendea kila kipengele cha maisha yake kwa kufuata kanuni na sharia za Allah (sw). Uislamu ni njia iliyonyooka kwa sababu kwa kufuata kanuni na sharia alizozitwika Allah (sw) sambamba na kanuni na sharia zinazofuatwa na maumbile yote yaliyomzingira binaadamu ikiwa ni pamoja na umbile lake mwenyewe ndiyo njia pekee inayomuwezesha binaadamu kuishi kwa furaha na amani ya kweli hapa ulimwenguni na huko akhera.

أَفَغَيْرَ دِينِ اللَّهِ يَبِغُونَ وَلَهُ أَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ  
وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾

*Je! Wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii Yeye, kikipenda kisipende? Na Kwake watarejeshwa wote (3:83)*

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا  
تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا  
يَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

*Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawasawa - ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu; (yaani dini hii ya Kiislamu inawafikiana barabara na umbo la binadamu). Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini iliyo haki, lakini watu wengi hawajui (30:30)*



Hivyo Uislamu ndiyo njia ya hakika ya maisha ya binaadamu na njia nyingine zote ni za ubabaishaji tu, kama Allah (sw) anavyotutanabahisha

وَإِن تَطْعَ أَكْثَرَ مَن فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿١١٦﴾

*“Na kama ukiwatii wengi katika hawa waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kuzua (tu basi). (6:116)*

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ مَن يَضِلُّ عَن سَبِيلِهِ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١١٧﴾

*Bila shaka Mola wako ndiye anayewajuwa vyema wanaopotea na njia yake na ndiye anayewajuwa sana wanaoongoka” (6:117).*

### **Kwa nini binadamu anahitajia mwongozo kutoka kwa Allah (sw)**

Binadamu hanabudi kuhitajia mwongozo sahihi wa maisha yake kutoka kwa Allah (sw) kwa sababu kuu zifuatazo:

(1)Allah (sw) ndiye aliyemuumba binaadamu kwa lengo maalumu. Hivyo ndiye anayestahiki kumuwekea binaadamu mwongozo wa maisha utakaomfikisha kwa ufanisi na wepesi kwenye lengo tarajiwa. Ni katika ukweli huu Allah (sw) anasisitiza:

إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدَىٰ ﴿١١٨﴾

*“Ni juu yetu kutoa mwongozo (wa maisha) (92:12)*

(2)Binaadamu hana uwezo wa kujiundia utaratibu wa maisha utakaomuwezesha kuishi kwa furaha na amani ya kweli hapa ulimwenguni na huko akhera kutokana na mapungufu yafuatayo:

(a)Ametunukiwa na muumba wake kiasi kidogo sana cha elimu:

وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي وَمَا أُوتِيتُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِلَّا

قَلِيلًا ﴿٨٥﴾

*“Na wanakuuliza habari ya roho. Sema: Roho ni jambo lililohusika na Mola wangu. Nanyi hamkupewa elimu ila kidogo kabisa” (17:85)*

- (b) Anaathiriwa sana na mazingira yake.
- (c) Anaathiriwa sana na ubinafsi na uchoyo.
- (d) Milango ya fahamu anayoitumia kama zana za kupatia elimu ina udhaifu mwingi.

Katika kuomba dua hii ya mwongozo, mja anaweka bayana kuwa njia anayoihitajia ni ile itakayomuwezesha kupata neema za peponi kama wale walioneemeshwa na isiwe ile itakayompelekea kughadhibikiwa na Allah kama wale walioghadhibikiwa wala isiwe ile itakayompelekea kuishi nje ya kanuni na taratibu alizozianisha Allah (sw) kama wale waliopotea.

### **Walioneemeshwa**

Kwa mujibu wa Qur'an walioneemeshwa ni wale waliojitahidi kwa kadiri ya uwezo wao kuendesha maisha yao ya kila siku katika kila kipengele kwa kufuata kanuni na sharia ya Allah (sw) kisha wakajitahidi na kujitoa muhanga kwa mali zao na nafsi zao ili kuifanya njia hii iliyonyooka (Uislamu) itawale katika jamii ili kuhakikisha furaha na amani vinakuwepo na kudumu. Makundi ya watu walioneemeshwa yanabainishwa katika Qur'an kama ifuatavyo:

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ  
 وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا ﴿١٤﴾  
 ذَلِكَ الْفَضْلُ مِنَ اللَّهِ وَكَفَى بِاللَّهِ عَلِيمًا

*“Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao watakuwa pamoja na wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu, (ambao ni) Manabii, Masidiq, Mshahid na Maswalihi (watu wema). Na uzuri ulioje (kwa mtu) watu hao kuwa rafiki zake (4:69).*

Kwa ufafanuzi, **Manabii** ni Mitume wa Mwenyezi Mungu ambao walitekeleza wajibu wao kama walivyoagizwa na Mola wao. **Masidiq** ni maswahaba wa Mitume wa Mwenyezi Mungu, ambao waliwasadikisha mitume na wakashirikiana nao bega kwa bega katika kusimamisha Uislamu katika jamii. **Mashahidi** ni wale waumini waliokufa katika jihadi ya kusimamisha Uislamu katika jamii. **Maswalihi** ni wale wanaomtii Allah na Mtume wake katika kila kipengele cha maisha yao na wakawa wanajitahidi kwa kadri ya uwezo wao kuusimamisha Uislamu katika jamii kwa mali zao na nafsi zao.

### **Walioghadhikiwa na Allah (sw)**

Kwa mujibu wa Qur'an walioghadhikiwa na Allah (sw) ni Mayahudi ambao baada ya kuujua vyema ujumbe wa Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mitume na vitabu vyake, hawakuuifuata inavyotakikana. Kinyume chake waliamua kufuata baadhi ya muongozo wa Allah (sw) na kukanusha baadhi nyingine kutokana na msukumo wa matamano ya nafsi zao. Walikuwa wakichanganya haki na batili; walikuwa wakiamrisha mema na kujisahau nafsi zao; walikuwa wakirudia rudia makosa; walikuwa wakivunja ahadi zao; waliwauwa Mitume wa Mwenyezi Mungu pasi na haki; walikuwa wakibadilisha mwongozo wa Allah (sw) kwa ndimi zao na mikono yao, waliwadhihaki waumini wa kweli na

kuzifanyia stihizai aya za Mwenyezi Mungu na kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa namna mbalimbali. Kwa tabia yao hii, Mwenyezi Mungu aliwaghadhibikia Mayahudi na kuwalaani.

لُعِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَى لِسَانِ دَاوُدَ وَعِيسَى ابْنِ  
مَرْيَمَ ذَلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿٧٨﴾

*"Walilaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa Israil (Mayahud) kwa ulimi wa Daud na wa Isa bin Maryam. Hayo ni kwa sababu waliasi kupindukia mipaka. (5:78)*

كَانُوا لَا يَتَنَاهَوْنَ عَنْ مُنْكَرٍ فَعَلُوهُ لَبِئْسَ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٧٩﴾

*(Pia) hawakuwa wenye kukatazana mambo mabaya waliyokuwa wakifanya....." (5:79).*

## **Waliopotea**

Waliopotea ni washirikina na wakirsto (Watawa) ambao pamoja na kudai kwao kuwa wanamuamini Mwenyezi Mungu, hawafuati mwongozo wake kwa kutii kanuni na sharia zake katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Bali hutii kanuni na sharia zilizowekwa na binaadamu wenziwe dhidi ya kanuni na sharia za Allah (sw) huku wakiitakidi kuwa watapata uokovu (wa kiroho) katika maisha ya akhera kupitia uombezi wa miungu wa kati walio wabuni na kuwashirikisha na Allah (sw).

Makafiri wanaokanusha kuwepo kwa Allah (sw) na siku ya malipo, ni katika kundi hili la waliopotea. Huendesha maisha yao kwa kanuni na sharia walizozitunga kulingana na matashi ya watawala ambazo zinapingana na kanuni na sharia za Allah (sw)

Ili dua hii iwe kabuli waumini hawanabudi kujitahidi kujipamba na tabia ya wale walioneemeshwa na kujitahidi kujiepusha na tabia za wale walioghadhibikiwa na za wale waliopotea. Kama Waislamu wataomba dua hii katika kila swala na katika kila ufunguzi wa

shughuli zao lakini wakawa wanafuata kwa moyo mkunjufu, mifumo ya maisha iliyowekwa na makafiri, washirikina, Wayahudi na wakristo, wajue kuwa dua hii haitakuwa kabuli, bali wataghadhibikiwa na Allah (sw) kama walivyo ghadhibika Wayahudi

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

1. Suratul-fatiha ni dua na inatufunza adabu ya kuomba dua. Inatufunza kuwa tuwe na unyenyekevu wakati wa kumuomba Mwenyezi Mungu na tuanze dua yetu kwa kutanguliza majina yake matukufu.
2. Tuanze kila jambo letu kwa Bismillahir Rahmaanir Rahiim
3. Allah (sw) aliyemkamilifu wa sifa ndiye pekee anayestahiki kuabudiwa na kutegemewa.
4. Uislamu ndio njia sahihi ya maisha; njia iliyonyooka.
5. Mwongozo wa kuwapelekea watu kwenye njia sahihi ya maisha hauwezi kupatikana kwa yeyote ila kutoka kwa muumba aliye na hikima na ujuzi usio na mipaka.
6. Binaadamu hawezi kutoa mwongozo sahihi wa maisha kutokana na mapungufu mengi aliyonayo. Ana elimu ndogo sana, anaathiriwa sana na mazingira, ni mbinafsi mno na mchoyo.
7. Njia sahihi ya maisha ni moja tu (Al-Islaamu) na radhi za Mwenyezi Mungu hupatikana kwa yule tu atakayeifuata njia hiyo kwa ukamilifu.

## **ZOEZI 3:01**

1. Hifadhi kifuani Suratul-Faatihah na tafsiri yake.
2. Suratul-Faatihah imeitwa majina mengi. Ainisha majina manne (4) ya sura hii na kuyatolea maelezo kwa muhtasari.
3. Aya ya kwanza ya Suratul-Faatihah ni Bismillahir Rahmaanir Rahiim. Toa faida tatu zinazopatikana kwa muislamu kuanza kila jambo kwa jila la Allah (sw).
4. "Tuongoze katika njia iliyonyooka" (1:6).  
Kwa nini binaadamu anahitajia mwongozo kutoka kwa Allah (sw)?
5. Ainisha mafunzo makuu matano (5) yatokanayo na Suratul-Faatihah.

## 2. Suratul - A'ala (89)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

*1. Litukuze jina la Mola wako  
aliyemtukufu.*

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿١﴾

*2. Aliyeumba (kila kitu) na  
akakitengeneza.*

الَّذِي خَلَقَ فَسَوَّى ﴿٢﴾

*3. Na akakikadiria (kila kimoja  
jambo lake) na akakiongoza.*

وَالَّذِي قَدَّرَ فَهَدَى ﴿٣﴾

*4. Na aliyeotesha ndisha  
(malisho).*

وَالَّذِي أَخْرَجَ الْمَرْعَى ﴿٤﴾

*5. Kisha akaifanya mikavu  
yenyewe kupiga weusi.*

فَجَعَلَهُ وُغَاءً أَحْوَى ﴿٥﴾

*6. Tutakusomesha wala  
hutasahau.*

سَنُقْرِئُكَ فَلَا تَنْسَى ﴿٦﴾

*7. Ila akipenda Mwenyezi  
Mungu; Yeye anajua  
yaliyodhahiri na yaliyofichikana.*

إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ

وَمَا يَخْفَى ﴿٧﴾

*8. Nasi tutakusahilishia  
(kuitangaza) dini iliyo nyepesi  
(Uislamu).*

وَنُخِيسِرُكَ لِلْيُسْرَى ﴿٨﴾

9. Basi waidhisha ikiwa utafaa waadhi.

فَذَكِّرْ إِن نَّفَعَتِ الذِّكْرَىٰ ﴿٩﴾

10. Bila shaka atakumbuka mwenye kumuogopa Allah (s.w).

سَيَذَكِّرْ مَنْ يَخْشَىٰ ﴿١٠﴾

11. Na mwingi wa mateso atajitenga mbali nayo hayo (mawaidha).

وَيَتَجَنَّبُهَا الْأَشْقَىٰ ﴿١١﴾

### **Maelezo juu ya Sura**

Sura hii inapata jina lake kutokana na neno Al-a'laa lililomo katika aya ya kwanza. Sura hii ni ya 87 katika msahafu na katika historia ya kushuka ni ya 8. Hivyo sura hii ni katika sura za Makka iliyoshushwa katika kipindi cha mwanzo wa Utume pale Mtume (s.a.w) alipokuwa hajazoea kupokea wahyi na akikhofu kuwa atasahau kile alichosomewa na Jibril (a.s). Ndipo Allah (sw) akamliwaza katika aya ya 6 na 7

*“Tutakusomesha wala hutasahu, ila akipenda Mwenyezi Mungu...”*

Pamoja na maliwazo hayo, Mtume (s.a.w) kwa kujua uzito wa kutofikisha vilivyo kile alichogizwa na Mola wake afikishe kwa watu, alijisahau tena na kuufanyia haraka wahay; ndipo katika Suratul-Qiyaamah, ambayo ni ya 31 kushuka, Allah (sw) alimliwaza tena Mtume wake kwa kumuagiza:



لَا نُحَرِّكَ بِهِ لِسَانَكَ لِتَتَّعَجَلَ بِهِ ۗ (١١) إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ۗ (١٢)  
 فَإِذَا قَرَأَهُ فَاتَّبِعْ قُرْآنَهُ ۗ (١٣) ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ۗ (١٤)

*“Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi. Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha. Wakati tunapokusomea, basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu yetu kuubainisha” (75:16-19)*

Pamoja na Mtume (s.a.w) kuhakikishiwa uhibitaji wa ujumbe wa Qur'an na Mola wake, hakuacha kuwa na wasiwasi kutokana na unyeti wa dhima aliyopewa. Ndipo tena Allah (sw) akamliwaza katika Suratu Twaahaa, kama ifuatavyo:

فَتَعَالَى اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْآنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ  
 إِلَيْكَ وَحْيُهُ ۗ وَقُلْ رَبِّ زِدْنِي عِلْمًا (١١٤)

*“Ametukuka Mwenyezi Mungu. Mfalme wa haki, wala usiifanyie haraka (hii) Qur'an (kwa kusoma), kabla haujamalizika wahayi wake. Na (uombe) useme: "Mola wangu nizeidishie ilimu" (20:114)*

Baada ya hapo, haikumtokea tena Mtume (s.a.w) kuwa na wasiwasi katika kupokea wahayi.

### **Mafunzo**

Katika aya ya kwanza ya Sura hii tunaamrishwa kulitukuzwa jina la Mola wetu aliyemtukufu na katika aya ya 2 hadi ya 5, zinatolewa hoja kwanini Allah (sw) pekee ndiye anayestahiki kutukuzwa na si mwinginewe.

Katika aya hizi inabainisha wazi kuwa Allah (sw) ndiye muumbaji na mtengenezaji sura ya kila kitu pamoja na kukiumba kila kitu na kukipa sura yake, Allah (sw) amekikadiria kila kiumbe

jambo lake, akakiwekea mustakbali wake na akakiongoza kwa silka au kwa wahyi kufikia lengo lake lililokusudiwa. Kuongoza kwa Allah (sw) ni kwa namna mbili: kwa viumbe visivyo na hiari na kwa viumbe vyenye hiari (majini na watu).

Viumbe visivyo na hiari kama wanyama, mimea na kadhalika, huongozwa kwa silka (instincts) ambazo huwaelekeza namna ya kutafuta chakula, kujihifadhi na mazingira, kujilinda na maadui, kuzaliana na kadhalika. Viumbe vya kundi hili hufuata kanuni na sharia za maumbile alizozitwika Allah (sw) bila ya kuzikiuka. Tunathibitishiwa hili katika Qur'an:

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦١﴾

*“Vinamtukuza Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na ardhini, na yeye ni mwenye nguvu, mwenye hikima” (61:1).*

يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ الْمَلِكِ الْقُدُّوسِ الْعَزِيزِ

الْحَكِيمِ ﴿٦٢﴾

*Vinamtukuza Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini (Mwenyezi Mungu) aliye Mfalme, Mtakatifu, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima” (62:1)*

Majini na watu pamoja na kuongozwa kisilka (ndani kwa ndani) katika maumbile yao kama wanyama, wadudu na mimea, wametunukiwa akili na uwezo wa kufikiri, elimu na uwezo wa kujielimisha, utambuzi binafsi (self consciousness) na hiari ya kuchagua lipi la kufuata. Katika hali hiyo Allah (sw) amewaletea majini na watu mwongozo unawabainishia njia ya kheri (uongofo) itakayowafikisha kwenye lengo la maisha yao na ile ya shari (upotofu) itakayowakwamisha kufikia lengo tarajiwa. Na hili linathibitishwa katika Qur'an:

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا

*“Hakika sisi tumemuongoa (binadamu kwa kumbainishia) njia (zote mbili hizi kuwa hii ndiyo ya kheri na hii ndiyo ya shari). Basi (mwenyewe tena) atakuwa mwenye shukrani au awe mwenye kukufuru” (76:3).*

Uoteshaji wa malisho ya wanyama umetajwa kama mfano wa kuwakilisha sifa ya Allah (sw) ya ulishaji au utoaji rizki kwa viumbe vyote.

Pia umetajwa uwezo wa Allah (sw) wa kuyafanya malisho (majani na mimea mingine) kukauka kama mfano wa kuwakilisha sifa nyingine ya Allah (sw) ya kufisha vile alivyoviumba baada ya muda aliovikadiria kuisha.

Katika aya ya Sita hadi ya Nane, Allah (sw) anamliwaza Mtume (s.a.w) na kwahiyo, Waislamu wote kuwa atamfanyia wepesi kuifhamu Qur'an vilivyo na kumrahisishia kazi ya kuuhisha na kuusimamisha Uislamu katika jamii. Hii imekaririwa katika aya nyingi kuwa Allah (sw) ameifanya Qur'an kuwa nyepesi:

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ ﴿١٧﴾

*“Kwa yakini tumeifanya Qur'an iwe nyepesi kufahamika lakini yuko anayekumbuka?” (54:17,22,32,40)*

Pia Allah (sw) ametuhakikishia katika Suratul Hajj kuwa ameufanya Uislamu kuwa mwepesi:

..... وَمَا جَعَلْ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ .....

*“..... Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini.  
.....(22:78)*

Baada ya kuufahamu Uislamu na kuufuata tunalazimika kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa wale ambao haujawafikia, pia tunalazimika kuwakumbusha wale ambao tayari ujumbe

umeshawafikia, lakini wakawa wanasahau au kughafilika.

Waumini wa kweli wanapokumbushwa aya za Mwenyezi Mungu huzifuata kwa unyenyekevu, lakini wale waliokufuru, hawaonyeki kwa ukumbusho wa aya wala Hadithi, na Mwenyezi Mungu amewakamia adhabu kali ya motoni.

Katika aya ya 14 na 15 wametajwa wale waliofaulu kuwa ni wale wanaojitakasa na kujiepusha na mambo maovu na machafu na wakawa wanamkumbuka Mola wao kwa wingi, wakawa wanasimamisha swala na wakawa wanatii kanuni na sharia za Allah (sw) katika kukiendea kila kipengele cha maisha yao.

Katika aya ya 16 na 17 yanalinganishwa maisha ya **dunia** na maisha ya **akhera**. Maisha ya akhera yametajwa ni bora kwa mara nyingi zaidi na ya kudumu milele ambapo maisha ya dunia ni duni na ya muda mfupi sana.

Kuhusiana na muda mfupi wa maisha ya dunia ukilinganisha na ule wa maisha ya wa akhera, tunafahamishwa katika Qur'an kuwa watu watakapoulizwa kuwa waliishi muda gani humu duniani, watajibu,kuwa waliishi siku moja au sehemu ya sikuhata wale walioishi zaidi ya miaka elfu. Kuhusu ubora wa starehe za dunia na ule wa starehe za akhera, Allah (sw) anatufahamisha:

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ وَإِنَّمَا تُوَفَّقُونَ أُجُورَكُمْ يَوْمَ الْفِيئَةِ  
فَمَنْ زُحِرَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا  
مَتَاعُ الْعُرُورِ ﴿١٨٥﴾

*“Kila nafsi itaonja mauti. Na bila shaka mtapewa ujira wenu kamili siku ya kiyama. Na aliyewekwa mbali na Moto na akaingizwa peponi, basi amefuzu. Na maisha ya dunia si kitu ila starehe idanganyayo” (3:185)*

Kwa bahati mbaya binaadamu waliowengi pamoja na ujumbe huu ulio wazi, wamechagua kuchukua starehe za dunia na kukosa starehe za akhera. Ni ujinga na uzembe ulioje!

Aya ya 18 na 19 inahitimisha kuwa mafunzo yaliyomo ndani ya Qur'an kupitia kwa Mtume Muhammad (s.a.w) si mageni bali ni yale yale yaliyofundishwa na Mitume waliotangulia na kubainishwa katika vitabu vyao, akiwemo Mtume Ibrahim (as) na Musa (as). Kwa ujumla tunajifunza katika Qur'an kuwa Uislamu ni mfumo sahihi wa maisha kwa ajili ya walimwengu wote wa nyakati zote. Mitume wote kuanzia Adamu (as) hadi Muhammad (s.a.w) wameletwa kufundisha Uislamu na kuusimamisha katika jamii.

﴿ شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى وَعِيسَى أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ كَبُرَ عَلَى الْمُشْرِكِينَ مَا تَدْعُوهُمْ إِلَيْهِ اللَّهُ يَجْتَبِي إِلَيْهِ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ يُنِيبُ ﴾

*“Amekupeni sharia ya dini ile ile aliyomuusia Nuhu na tuliyokufunulia wewe na tuliyowausia Ibrahim na Musa na Issa, kwamba simamisheni dini wala msifarikiane kwayo. Ni ngumu kwa wenye kushirikisha (dini hii) unayowaitia...”*  
(42:13)

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kwa muhtasari kutokana na sura hii tunajifunza kuwa:

- (1) Mwenyezi Mungu pekee ndiye anayestahiki kutukuzwa na kusifiwa kwa sababu ndiye aliyeumba kila kituna kukitengeneza katika sura maridhawa kwa lengo maalumu, kisha akakipa mahitaji yake na akakilea na kukiongoza mpaka kikafikia lengo la kuumbwa kwake, kisha ndiye pekee atakayekifisha baada kumaliza muda wake aliokikadiria.

- (2) Qur'an imehifadhiwa na Mwenyewe Mwenyezi Mungu na ameijaalia kuwa nyepesi kwa yule anayetaka kuongoka na akatia juhudi ya kuisoma na kuifuata.
- (3) Uislamu ni dini nyepesi kujua na kuifuata.
- (4) Kila muislamu anawajibu kuujua Uislamu vilivyo na kuutekeleza.
- (5) Kila muislamu anawajibika kuufundisha na kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa wale ambao haujawafikia na kuwaonya na kuwakumbusha wale uliowafikia wakapuuzia au wakashau.
- (6) Wale watakaoupokea ujumbe wa Uislamu wakajitakasa na maovu na wakajizatiti kumtukua Mola wao katika kila kipengele cha maisha yao, wakawa wanasimamisha swala na kutekeleza Ibada nyingine mbalimbali walizopangiwa na Mola wao, watakuwa ni wenye kufuzu katika maisha ya dunia na akhera.
- (7) Wale watakaopuuzia mafundisho ya Uislamu, wakatakabari na kuendelea kufanya maovu watastahiki adhabu ya Mwenyezi Mungu iumizayo katika maisha ya akhera, japo hapa duniani wanaweza kuonjeshwa starehe ndogo.
- (8) Maisha ya akhera ndiyo bora kwani ni yenye starehe ya kweli yenye kudumu milele. Kinyume chake starehe ya hapa duniani ni ya uwongo na ni ya muda mfupi sana.
- (9) Uislamu ni dini pekee ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya walimwengu wote wa nyakati zote.

..... إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ

*Bila shaka dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu....." (3:19)*

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ

الْخَسِرِينَ ﴿٨٥﴾

*"Na anayetaka dini isiyokuwa Uislamu, haitakubaliwa kwake. Naye akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa)" (3:85)*

### **ZOEZI 3:02**

1. Hifadhi kifuni Suratul-A'ala na tafsiri yake.
2. Onesha kuwa aya ya 6 na 7 (87:6-7) ya Suratul-A'ala ni kiashiria kuwa sura hii ni miongoni mwa sura za Makka iliyoshushwa katika kipindi cha mwanzo cha Utume wa Muhammad (s.a.w).
3. Toa mafunzo makuu mawili (2) yatokanayo na aya ya 1 hadi ya 5 ya Suratul-A'ala (87:1-5).
4. "Nasi tutakusahilishia (kuitangaza) dini iliyo nyepesi" (87:8)  
  
Toa hoja tatu za msingi kuonesha kuwa Uislamu ni dini nyepesi kwa binaadamu.
5. Ainisha mafunzo makuu yatokanayo na aya ya 9 hadi ya 15 ya Suratul-A'ala (87:9-19)

### 3. Suratudh - Dhuhaa (93)

*Kwa jina la Allah Mwingi  
wa Rehma, Mwenye  
kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**1. Naapa kwa mchana.**

وَالضُّحَىٰ ﴿١﴾

**2. Na kwa usiku  
unapotanda.**

وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٢﴾

**3. Hakukuacha Mola wako  
wala hakukukasirikia (ewe  
Nabii Muhammad).**

مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ﴿٣﴾

**4. Na bila shaka (kila)  
wakati ujao (utakuwa)  
bora zaidi kuliko  
uliotangulia.**

وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ ﴿٤﴾

**5. Na Mola wako atakupa  
mpaka uridhike.**

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ﴿٥﴾

**6. Je, hakukukuta yatima  
akakupa makazi (mazuri  
ya kukaa)?**

أَلَمْ يَجِدَكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ ﴿٦﴾

**7. Na akakukuta hujui  
kuongoza njia,  
akakuongoza?**

وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ ﴿٧﴾



8. Na akakukuta fakiri  
akakutajirisha?

وَوَجَدَكَ عَابِلًا فَأَعْنَتُ ۝٨

9. Basi usimuonee Yatima.

فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ ۝٩

10. Wala usimkaripie  
aulizaye.

وَأَمَّا السَّائِلَ فَلَا تَنْهَرْ ۝١٠

11. Na Neema ya Mola wako  
usimulie (kwa kushukuru  
na kufanya amali njema).

وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ۝١١

### Maelezo juu ya Sura

Sura hii jina lake limetokana na neno **Wadh-dhuhaa**, ambalo ndilo neno na aya ya kwanza. Sura hii ni ya 93 katika Msahafu, ni sura ya Makka na ni sura ya 11 kushuka ikiashiria kuwa ni katika sura za mwanzo mwanzo kumshukia Mtume (s.a.w).

Tunafahamishwa katika Hadithi kuwa Wahay ulisitishwa kwa muda mrefu kidogo, kuliko kawaida aliyozoea Mtume (s.a.w), ikafuatiwa na Makafiri wa Kiquraish kudai kusomewa Wahayi kwa kejeli, huku wakimdhihaki kuwa Mola wake atakuwa amemkasirikia. Kibinaadamu, Mtume (s.a.w) naye akakumbwa na wasiwasi kuwa, huenda Mola wake amemkasirikia. Kila akijiuliza amekosea nini hapati jibu. Ndipo Mola wake akamshushia wahayi huu wa kumliwaza kuwa hakumkasirikia bali ni katika hekima yake kusitisha wahyi ili kumpumzisha.

Tukio hili la kusitishwa wahyi lilimtokea Mtume (s.a.w) katika kipindi cha mwanzo cha utume, pale alipokuwa bado hajazoea kuhimili mzigo mkubwa wa wahy. Kwa sababu hiyo kipindi cha mapumziko kilikuwa ni cha lazima kwake. Baadaye, Mtume (s.a.w) alipozoea kubeba mzigo wa wahyi hakukuwa tena na ulazima wa kupewa vipindi virefu vya mapumziko.

## Mafunzo

Maudhui makubwa ya sura hii ni kumliwaza Mtume ili kumuondolea dukuduku na huzuni iliyomsibu kutokana na kusitishwa wahyi kwa kipindi kirefu kidogo.

Allah (sw) amemliwaza Mtume, kwa kumhakikisha kwa kiapo kuwa Mola wake hakumuacha (hakumsusa) wala hakumkasirikia, kisha akampa bishara njema kuwa matatizo aliyokuwa akikabiliana nayo katika hiyo hatua ya mwanzo ya ujumbe wake hayatadumu kwa muda mrefu; na kila kipindi kijacho kitakuwa bora kwake na kwa Waislamu na Uislamu kuliko kilichopita.

Pia akambashiria kuwa baada ya muda si mrefu atamneemesha vilivyo, kwa kumuwezesha kusimamisha Uislamu, mpaka aridhike. Biashara hii ilipotolewa hapakuwa na dalili kabisa kuwa Mtume (s.a.w) pamoja na Waislamu wachache dhaifu aliokuwa nao kuwa watapata ushindi na kuufanya Uislamu uwe juu ya dini zote za ulimwengu wa wakati ule kwa kipindi cha muda mfupi uliofuatia. Baada ya mkataba wa Hudaybiyya, Mtume (s.a.w) aliwashinda maadui zake wote na Uislamu ukawa juu ya dini zote kama Qur'an inavyothibitisha

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظَاهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*"Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi" (48:28)*

Pamoja na bishara hii Allah (sw) anazidi kumliwaza Mtume wake kwa kumkumbusha kuwa haiwi Mola wake amkasirikie kwani alimteua kuwa Mtume wake kwa walimwengu wote na kumuandaa tangu utotoni mwake ili aweze kuchukua jukumu hili adhimu na kuweza kulitekeleza ipasavyo. Allah (sw) amemhakikishia Mtume

wake kuwa yuko radhi naye kwa kumkumbusha neema alizomtangulizia hata kabla ya neema hii kubwa ya utume:

"Je, hatukukuta yatima tukakupa makazi mema ya kukaa? Na tukakukuta hujui kuongoza njia, tukakuongoza kwa kukupa Utume? Na hatukukuta fakiri tukakutajirisha kupitia kwa Bibi Khadija?" Iweje tena hivi leo, ambapo ndio hasa unahitaji msaada zaidi kutoka kwetu ili uweze kufikia lengo lililokusudiwa, ndio tena tukususe na kukukasirikia?"

Baada ya maliwazo hayo, Allah (sw) anamfunza Mtume wake namna ya kushukuru neema. Akamuagiza Mtume kuwa awahurumie mayatima kama Mola wake alivyomhurumia na kumpa makazi mazuri, Asiwakaripie wale wanaotaka kuujua Uislamu na kuongoka bali awaangushie bawa la rehema na kuwaongoza kama Mola wake alivyomuongoza. Mwisho, Mtume (s.a.w) anaagizwa na Mola wake kuwa atangaze neema zake alizompa. Kusimulia neema ni kushukuru neema hizo kwa kuzitumia kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Neema kubwa aliyopewa Mtume pamoja na Waislamu wote ni Uislamu.

..... أَلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ

نِعْمَتِي وَرَضِيْتُ لَكُمْ الْإِسْلَامَ دِينًا.....

*"..... Leo nimekukamilishieni dini yenu na kukutimizieni neema yangu, na ninakupendeleeni Uislamu uwe Dini yenu....." (5:3)*

Hivyo kuisimulia neema hii kubwa ni kuishi kiislamu, kuufundisha Uislamu na kuusimamisha Uislamu katika jamii. Mtume (s.a.w) na maswahaba zake walitekeleza agizo hili na kuutawalisha Uislamu juu ya mifumo mingine yote ya maisha iliyokuwemo wakati wa zama zao, na Allah (sw) akawa ni shahidi juu ya hili.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*“Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi” (48:28)*

## **Mafunzo kwa Muhtasari**

Pamoja na kuwa sura hii imeelekezwa kwa mtume katika kumliwaza, mafunzo yake yanawahusu Waislamu wote wa zama zote mpaka siku ya mwisho. Kwa muhtasari kutokana na sura hii tunajifunza yafuatayo:

1. Mwenyezi Mungu huapia viumbe vyake, ili hivyo viumbe kwa namna vinavyojulikana viwe ni ushahidi au dalili ya wazi ili kuyakinisha jambo linaloelezwa baada ya kiapo hicho.
2. Hakuna kipindi chochote cha harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu ambacho Mtume (s.a.w) hakuwa na msaada wa Allah (sw). Hivyo Waislamu walioko katika harakati hizi za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii wasikatishwe tamaa na vikwazo mbalimbali vitakavyo wafika, bali wawe na yakini kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja nao na watashinda.
3. Pamoja na hali duni waliyonayo Waislamu hivi sasa, wakifanya jitihada za kuujua Uislamu, kuutekeleza na kuufundisha kama alivyofanya Mtume (s.a.w) na maswahaba zake katika kipindi kigumu cha Makka, Uislamu utapata nguvu kila muda unavyosogea na hatimaye utafikia kilele cha kutawala katika jamii kama Mtume (s.a.w) alivyoutawalisha.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*“Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi” (48:28)*

4. Muislamu anatakiwa awe na tabia ya kuwaangalia walio chini yake kihali na mali na asiwaangalie walio juu yake, ili aweze kukinai juu ya neema alizoneemeshwa na Mola wake na kuwahurumia wale walio chini yake. Tabia hii pia itamuwezesha kushukuru neema alizoneemeshwa na Mola wake.
5. Mwenyezi Mungu pekee ndiye mdhibiti wa mafanikio au shida. Huibadili hali moja hadi nyingine wakati wowote apendavyo. Wajibu wetu Waislamu ni kufanya jitihada za kuboresha hali zetu huku tukimuomba Mwenyezi Mungu na kufanya jitihada za makusudi za kusimamisha Dini yake kwa mali zetu na nafasi zetu. Tukifanya hivyo tutafanikiwa kwa ahadi ya Allah (sw)

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي

الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي

أَرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي

شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٥٥﴾

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote.*

*Na watakaokufuru baada ya hayo; basi hao ndio wavunjao amri zetu. (24:55)*

6. Hatunabudi kumshukuru Allah (sw) kwa kila neema tuiapatayo na njia bora ya kushukuru neema ni kuitumia neema hiyo kwa mujibu wa maagizo ya Mwenyezi Mungu na kuzidisha dhikiri na lbada za ziada kama vile kukithirisha swala za sunnah, visimamo vya usiku, funga za sunnah, kutoa sadaqa, n.k. Neema kubwa tuliyopewa ni kuwa Waislamu. Hivyo, ili tuwe waja wenye shukrani mbele ya Allah (sw), hatunabudi kuujua Uislamu vilivyo, kuishi kiislamu na kufanya jitihada za makusudi za kuusimamisha Uislamu katika jamii.

#### 4. Suratu - Alam - Nashrah (94)

Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehema, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Je, hatukukupanulia kifua  
chako.

أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ①

2. Na tukakuondolea mzigo  
wako (mzito).

وَوَضَعْنَا عَنْكَ وِزْرَكَ ②

3. Uliovunja mgongo wako?

الَّذِي أَنْقَضَ ظَهْرَكَ ③

4. Na tukatukuza utajo  
wako?

وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ④

5. Basi kwa hakika baada ya  
dhiki (huja faraja).

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ⑤

6. Hakika baada ya dhidi  
huja faraja.

إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ⑥

7. Basi ukisha maliza  
(kulingania) shughulika kwa  
lbada nyingine.

فَإِذَا فَرَغْتَ فَانصَبْ ⑦

8. Na jipendekeze kwa Mola  
wako.

وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَأَرْعَبْ ⑧

### **Maelezo juu ya Sura**

Sura hii imepata jina lake kutokana na neno la kwanza - **Alam-Nashrah**. Hii ni sura ya 94 katika msahafu na ni ya 12 katika utaratibu wa kushuka. Kwa mujibu wa maelezo ya Ibn Abbas (ra), sura hii iliteremshwa mara baada ya kuteremshwa Surat Dh-Dhuhaa.

### **Mafunzo:**

Lengo na madhumuni ya sura hii pia ni kumliwaza Mtume (s.a.w). Pamoja na wasiwasi aliokuwa nao Mtume (s.a.w), kuwa labda Mola wake alimkasirikia na kumsusa, kutokana na tukio la kuchelewesha wahyi lililoambatana na kejeli na dhihaka ya maadui zake, Mtume (s.a.w) alikuwa akikabilia na magumu mengi kuanzia pale alipoanza kulingania ujumbe wa Uislamu kwa watu wote. Mara tu alipoanza kulingania Uislamu, jamii ile ile iliyompa heshima ya pekee, iliyompa jina la **Aswadiq Al-Amiin**, ilianza kumtukana, kumkejeli, kumdhihaki na kumshutumu na kumpiga yeye pamoja na wafuasi wake wachache waliomuamini. Hali hii kibinaadamu ilikuwa inakatisha tamaa ya kufikiwa lengo lililokusudiwa la kuifanya Dini ya Allah kuwa juu ya dini zote.

Pamoja na kumliwaza Mtume (s.a.w) katika suratudh-Dhuhaa, katika sura hii, Allah (sw) amemliwaza mtume wake kwa kukumbusha neema kuu tatu alizomtunukia

- (i) Kupanuliwa kifua chake
- (ii) Kuondolewa mzigo mzito uliovunja mgongo wake
- (iii) Kukuzwa utajo wake.

Kupanuliwa kifua hapa inaashiria Mtume (s.a.w) kupewa uoni wa utume wa kuangalia maslahi ya jamii, hata kabla ya kupewa utume rasmi. Kifua chake kilizidi kupanuka pale alipopewa utume na kufundishwa Uislamu na Mola wake.



فَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يَهْدِيَهُ، يَشْرَحْ صَدْرَهُ، لِلْإِسْلَامِ

*“Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumuongoza humfungulia kifua chake Uislamu .....” (6:125)*

Mzigo mzito alioubeba Mtume (s.a.w) ni ile hali ya kuona watu wakifanya maovu na kudhulumu haki za wengine na akawa hana uwezo wa kuzuia uovu huo. Baada ya kushindwa kubeba mzigo huo alihamia pangoni katika mlima wa Hira, ndipo Allah (sw) akamuondolea mzigo huu kwa kumfanya Mtume wa kulingania Uislamu na kuusimamisha katika jamii. Utatuji wa matatizo yote ya jamii ni Uislamu.

Pamoja na kwamba, Muhammad (s.a.w) alitajwa kwa sifa nzuri na watu wa jamii yake kabla ya utume, walimuita **Aswadiq Al-Amiin**, utajo wake ulivuma kwa ulimwengu mzima wa wakati ule mpaka hivi sasa. Haikamiliki shahada mpaka atajwe Mtume na imekuwa ni amri ya Allah (sw) kwa waumini kumtakia Mtume Rehema na Amani mara kwa mara (katika kila swala) na kila atajwapo

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ

وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾

*“Hakika Mwenyezi Mungu anamteremshia rehema Mtume; na Malaika Wake (wanaomuomba dua) Basi; enyi mlioamini msalieni (muombeeni rehema) na amani” (33:56)*

Pia Mtume (s.a.w) pamoja na Waislamu aliokuwa nao, waliliwazwa na mola wao kuwa pamoja na dhiki waliokuwa nayo, faraja itafuatia si muda mrefu. Hivyo waendeleo kutekeleza wajibu wao na kusubiri. Baada ya bishara hii njema historia inashuhudia kukua kwa nguvu ya Uislamu wakati wa Mtume (s.a.w) na kuwa juu ya mifumo mingine yote ya maisha iliyokuwepo kwa kipndi kifupi cha miaka 23 tu.

Mwisho, baada ya kukumbushwa neema na kubashiriwa ushindi, Mtume (s.a.w) anaagizwa na kwa hiyo Waislamu wote, kuwa baada ya kutekeleza wajibu wake wa kulingania Uislamu, ajikurubishe kwa Mwenyezi Mungu kwa kuleta dhikr nyingi na kuzidisha Ibada za ziada (nafilah) na visimamo vya usiku.

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا

*“Na katika usiku jiondoshee usingizi kwa (kusoma) hiyo (Qur'an ndani ya swala) Hiyo ni (Ibada) ya ziada kwako. Huendea mola wako akakuinua cheo kinachosifika” (17:79)*

Katika kutekeleza agizo hili, Mtume (s.a.w) katika maisha yake yote alikuwa akimkumbuka Allah (sw) kila wakati katika kila jambo alilolifanya hata alipokuwa akiingia na kutoka chooni. Alikuwa akisimama usiku kwa swala, kwa kitambo kirefu mpaka miguu yake ikawa inavimba na alikuwa akisujudu kirefu katika swala ya usiku, mpaka siku moja mkewe Aysha (r.a) akamdhanika kuwa amekufa.

## **Mafunzo kwa Muhtasari**

Pamoja na kuwa sura hii imemlenga Mtume (s.a.w) moja kwa moja, bado mafunzo yake ni kwa ajili ya Waislamu wote wa nyakati zote. Kwa muhtasari kutokana na sura hii tunajifunza yafuatayo:

1. Hatunabudi kushukuru neema mbalimbali alizoturuzuku Allah (sw) kwa kujizatiti kuifundisha na kuisimamisha Dini yake katika jamii.
2. Yeyote yule atakayedhamiria kuujua Uislamu kwa usahihi na kuingiza katika utendaji katika kuendesha maisha yake ya kila siku, uoni wake wa maisha na wa masuala ya jamii utakuwa ni wa juu kuliko ule wa watu wengine. Lengo kuu la muumini ni kusimamisha Uislamu katika jamii na kupata radhi

za Mwenyezi Mungu zitakazompelekea kuingizwa peponi katika maisha ya akhera.

3. Muumini wa kweli anawajibu wa kuondoa maovu na dhuluma katika jamii na kusimamisha wema, haki na uadilifu. Wajibu huu wa umini wataweza kuutekeleza pale tu watakapoufahamu Uislamu vilivyo, kisha wakaufundisha na kuusimamisha katika jamii kama alivyofanya Mtume (s.a.w) baada ya kupewa mwongozo.
4. Kwa mtazamo wa Uislamu, mwenye kuheshimika mbele ya Allah (s.w) si yule mwenye hadhi kubwa katika jamii kicheo au kimali; bali yule aliyemstari wa mbele katika kuufuata Uislamu na kuusimamisha katika jamii.

..... إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقَى اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

*“...Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi katika nyinyi (49:13)*

5. Wakati wowote Waislamu watakapojitahidi kuufahamu Uislamu vilivyo, kuutekeleza na kuusimamisha katika jamii, na wakasubiri juu ya magumu yanayowafika, Allah (sw) atawafanyia wepesi kwa kila hatua wanayopiga kusonga mbele na hatimaye atawawezesha kusimamisha Uislamu katika jamii kama alivyomuwezesha Mtume (s.a.w) na maswahaba zake. Ahadi hii iko wazi katika Qur'an

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي  
 الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي  
 ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أُمَّتًا يُعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي  
 شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفٰسِقُونَ ﴿٥٥﴾

*“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa Atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo; basi hao ndio wavunjao amri zetu. (24:55)*

6. Hakuna wakati wa kupoteza kwa muislamu. Kama muislamu hana la maana la kufanya amkumbuke Mwenyezi Mungu kwa kuleta dhikri mbalimbali. Aidha Waislamu wanaoharaka kusimamisha Uislamu katika jamii, wanahimizwa kujipendekeza kwa Allah (sw) kwa kuzidisha dhikiri, Ibada za nyongeza (nawaafil) kama vile kuzidisha swala na funga za sunnah na kuzidisha na kurefusha visimamo vya usiku. Hizi ni nyenzo muhimu mno za kumuimarisha muislamu katika kazi hii aziz ya kusimamisha Uislamu katika jamii.

## **ZOEZI 3:03**

1. Hifadhi kifua ni Suratudh-Dhuhaa na Alam Nashrah na tafsiri.
2. Suratudh-Dhuhaa na Alam Nashrah zimeshushwa kumliwaza Mtume (s.a.w) na wale walioamini pamoja naye.
  - (a) Nini kisa na mkasa uliopelekea Mtume (s.a.w) aliwazwe na Mola wake?
  - (b) Ainisha maliwazo yaliyotolewa na sura hizi.
  - (c) Baada ya maliwazo Mtume (s.a.w) (na kwa hiyo waumini wote) alipewa majukumu ya kutekekeza. Ainisha majukuku hayo.
3. Toa mafunzo makuu matano (5) yatokanayo na
  - (a) Suratudh-Dhuhaa
  - (b) Surat Alam Nashrah

## 5. Suratut-tyn (95)

Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1.Naapa kwa Tini na Zaituni

وَالْتَيْنِ وَالزَّيْتُونِ ﴿١﴾

2.Na kwa mlima Sinai.

وَطُورِ سَيْنِينَ ﴿٢﴾

3.Na kwa mji huu (wa  
Makka) wenye amani.

وَهَذَا الْبَلَدِ الْأَمِينِ ﴿٣﴾

4.Bila ya shaka  
tumemuumba mwanaadamu  
kwa umbo lililo bora kabisa.

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ  
تَقْوِيمٍ ﴿٤﴾

5.Kisha tukamrudisha kuwa  
chini kuliko walio chini.

ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿٥﴾

### Maelezo juu ya Sura

Sura hii imepata jina lake kutokana na neno **Wat-tyn** ambalo ndilo neno lake la kwanza. Sura hii imeteremshwa Makka katika siku za mwanzo mwanzo za utume wa Muhammad (s.a.w). Ni sura ya 27 kuteremshwa na ni ya 95 katika Msahafu.

### Mafunzo

Sura hii imeanza kwa viapo katika aya ya kwanza hadi ya tatu. Katika viapo hivi Allah (sw) anaapia mazingira ambamo wametokea Mitume wa Allah (sw). Anaapia mimea ya Mitini na Mizaytuni inayostawi katika eneo la mashariki ya kati, katika makazi ya Mitume wengi wa Allah (sw). Pia ameapia Mlima wa

Sinai, sehemu ambayo Nabii Mussa (as) alikuwa akizungumza na Allah (sw) nyuma ya pazia wakati akipokea wahay. Kisha ameapia mji wa Makkah, kituo ambacho Mtume (s.a.w) alianza kuuhiisha Uislamu. Kama kawaida ya viapo vya Allah (sw), viapo hivi vimeletwa ili kumvuta msomaji atafakari juu ya ukweli unaobainishwa katika aya tatu zinazofuatia.

Kuhusu umbile la binaadamu, ni kweli kuwa binaadamu wenyewe hawajawa na hoja ya kuonesha kuwa kuna kiumbe mwengine wanaye mfahamu kwa dhahiri yake, mwenye sura na umbo lililo bora kuliko la binaadamu. Pia Allah (sw) anamtanabahisha binaadamu juu ya umbile lake katika aya zifuatazo:

يَتَأْتِيهَا الْإِنْسَانُ مَا غَرَّبَكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ ﴿٦﴾ الَّذِي خَلَقَكَ  
فَسَوْنَكَ فَعَدَلَكَ ﴿٧﴾ فَمِنْ أَيِّ صُورَةٍ مَا شَاءَ رَكَّبَكَ ﴿٨﴾

*“Ewe mwanaadamu! Nini kikudanganyacho na Mola wako mtukufu (hata ukamkanusha)? Aliyekuumba na akakutengeneza, kisha akakulinganisha sawa sawa, katika sura yoyote aliyoipenda amekutengeneza” (82:6-8)*

Binaadamu pamoja na kutengenezwa katika sura na umbo zuri ametunukiwa pia na Mola wake vipawa vikubwa vinayomuwezesha kuwa bora kuliko viumbe vyote. Vipawa hivi ni vinne vifuatavyo:

- (i) Akili na ufahamu wa hali ya juu unaomuwezesha kufikiri na kutafakari.
- (ii) Utambuzi binafsi (self consciousness) unaomuwezesha kuunganisha, kuchambua na kuhusisha kila kitu au kila jambo na kuliweka mahali pake.

- (iii)Elimu ambayo humuwezesha kutenda kwa ufanisi.
- (iv)Uhuria - anao uwezo wa kufanya mema akitaka na ana uwezo wa kufanya maovu akitaka.

Pamoja na vipawa hivi pia binaadamu ametukuzwa na kukirimiwa na Mola wake neema mbalimbali kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

﴿وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ

مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا﴾ (v)

*“Na hakika tumewatukuzwa binaadamu na tumewapa vya kupanda barani na baharini na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri na tumewatukuzwa kuliko wengi katika wale tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa (kabisa)” (17:70)*

Binaadamu akiwa na busara na kuamua kutumia uhuru wake vizuri kwa kutumia vipawa na neema mbalimbali alizotunukiwa na Mola wake kwa kumtambua vilivyo na kumuabudu ipasavyo, huzidi ubora wake kwa kustahiki cheo cha Ukhalifa wa Allah (sw) hapa ulimwenguni cheo kilicho kitukufu na bora kuliko kile cha malaika mbele ya Allah (sw) - Rejea Qur'an (2:30-34). Kwa kusimamisha ukhalifa katika ardhi, haki na uadilifu vitasimama na kustawisha furaha na amani ya kweli katika jamii.

Binaadamu akiwa mjinga na kuamua kutumia uhuru wake vibaya kwa kuamua kutumia vipawa na neema alizotunukiwa na Mola wake kwa kumkufuru na kumuasi, atashuka cheo na kudhalilika kuliko wanyama kama tunavyokumbushwa katika aya zifuatazo:

﴿وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ الْجِنَّةِ وَالْإِنسِ لَهُمْ قُلُوبٌ لَا يَفْقَهُونَ بِهَا

وَلَهُمْ أَعْيُنٌ لَا يُبْصِرُونَ بِهَا وَلَهُمْ آذَانٌ لَا يَسْمَعُونَ بِهَا أُولَئِكَ كَالْأَنْعَامِ

بَلْ هُمْ أَضَلُّ أُولَئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ﴾ (174)



*"Na bila shaka tumewaambia moto wa Jahannamu wengi katika majini na wanaadamu (kwa sababu hii): Nyoyo wanazo, lakini hawafahamu kwazo (Hawataki kufahamu kwazo), na macho wanayo, lakini hawaoni kwayo, na masikio wanayo, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama; bali wao ni wapotofu (wapotevu) zaidi. Hao ndio walioghafilika (7:179)*

﴿إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِنْدَ اللَّهِ الضُّمُّ الْبُكْمُ الَّذِينَ

لَا يَعْتَلُونَ﴾

*"Hakika vinyama viovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni hawa wanaojipa uziwi (wa kutosikia haki), wanaojipa ububu (wasikiri hiyo haki), ambao hawayatii akilini (wanayoambiwa, bali wanayakataa tu vivi hivi bila ya kuyapima kwanza)" (8:22)*

Binaadamu anapoamua kumkufuru na kumuasi Mola wake, hufanya uharibu mkubwa katika ardhi kuliko ule unaofanywa na wanyama waharibifu. Kwa mfano matatizo makubwa na majanga makubwa yanayokabili ulimwengu hivi leo kama vile maradhi mabaya ya Ukimwi, mauaji ya halaiki, utapia mlo, umaskini na ujinga kwa nchi zinazoitwa za dunia ya tatu, na kadhalika ni matokeo ya ukafiri na uasi wa binaadamu dhidi ya Mola wake.

Maswali yaliyoulizwa kwenye aya ya saba na ya nane yanatutaka tutafakari juu ya ukweli huu kuwa: "Wanaweza kuwa sawa katika malipo wale waliosimamisha uadilifu katika jamii na kuwawezesha watu kuishi kwa furaha na amani na wale waliofanya fisadi katika jamii na kuwadhalilisha watu kwa kuwakhofisha na kuwadhulumu?" Kwa kipimo cha kibinaadamu na kiuadilifu, mwema na muovu hawawezi kulipwa sawa. Mtu mwana anastahiki kupongezwa na kuzawadiwa na mtu muovu anastahiki kulaumiwa na kuadhibiwa. Pia rejea Qur-an (32:18,59:20)

Je, ikitokea muovu akawa mbabe asiyewezekana kuadhibiwa na yoyote, kama George W. Bush na serikali yake alivyoivamia Afghanistan na Iraq kwa dhuluma, au ikitokea mtu mwema muadilifu aliyejizatiti kuleta amani na furaha ya kweli katika jamii, akawa badala ya kupongezwa na kuzawadiwa akaitwa gaidi na kupigwa vita kama alivyoitwa Mohammed Mullah na serikali yake ya Taliban (Afghanistan), itakuwa ni uadilifu mambo yaishie hapo? Akili ya binaadamu haikubaliani na hili. Bali, kiuadilifu ni lazima pawe na maisha mengine baada ya haya (maisha ya akhera) ambapo kila mtu aliyefanya wema hapa duniani atapongezwa na kuzawadiwa ipasavyo na kila aliyefanya uovu hapa duniani ataadhibiwa ipasavyo. Atakayesimamia hukumu hii ni Allah (sw) ambaye ni hakimu muadilifu kuliko mahakimu wote.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

1. Allah (sw) ameapia mazingira walimotokea mitume wake mbalimbali, ili kwa kuzingatia ujumbe wa mitume hao, iwe ni chachu kwa msomaji kutafakari juu ya ujumbe unaofuatia.
2. Ubora wa binaadamu hupatikana kutokana na imani sahihi iliyoambatana na vitendo vizuri.
3. Mwanaadamu akiamua kufuata maisha ya kumkufuru na kumuasi Mola wake, huwa muharibifu katika jamii kuliko wanyama waharibifu.
4. Malipo ya kumuamini Allah (sw) na kufuata mwongozo wake hapa duniani ni kuishi kwa furaha na amani (maisha ya nuru)
5. Malipo ya kumkufuru na kumuasi Allah (sw) na kufuata miongozo iliyo dhidi na uongozi wake hapa duniani ni kuishi maisha ya khofu na dhuluma (maisha ya giza)
6. Lazima iwepo siku ya mwisho ili waumini waliotenda vitendo vizuri na makafiri waliofisi katika ardhi walipwe kwa uadilifu jaza ya vitendo vyao.

## **ZOEZI 3:4**

1. Hifadhi kifuani Suratut-Tyn na tafsiri yake.
2. "Bila shaka tumemuumba binaadamu kwa umbo lililo bora kabisa. Kisha tumemrudisha kuwa chini kuliko walio chini" (95:4-5)
  - (a) Onesha ubora wa binaadamu ukilinganisha na viumbe wote waliomzunguka.
  - (b) Kiutendaji onesha ni vipi binaadamu atabakia na ubora wake.
  - (c) Ni kwa vipi binaadamu pamoja na kuumbwa kwa umbo bora, hushuka na kuwa chini kuliko vyote vilivyo chini.
3. Ainisha mafunzo matano (5) yatokanayo na Suratut-Tyn.

## 6. Surat-ul-Bayyinah (98)

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa  
Rehma, Mwenye Kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

*1. Wale waliokufuru miongoni  
mwa watu wa kitabu na  
washirikina (waliotoa ahadi  
kuwa) hawataacha  
(waliyonayo) mpaka iwajie  
hoja (iliyodhahiri ya  
kuonyesha upotevu wa dini  
zao).*

لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا  
مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ

وَالْمُشْرِكِينَ مُنْفَكِينَ

حَتَّى تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ ﴿١﴾

رَسُولٌ مِنَ اللَّهِ يَتْلُو

*2. Ni Mtume aliyetoka kwa  
Allah anayewasomea kurasa  
zilizotakaswa.*

صُحُفًا مُطَهَّرَةً ﴿٢﴾

فِيهَا كُتِبَ قِيمَةٌ ﴿٣﴾

*3. Ndani yake mnasharia  
madhubuti.*

وَمَا تَفَرَّقَ الَّذِينَ أُوتُوا

الْكِتَابَ إِلَّا مِنْ بَعْدِ

*4. Wala hawakufarikiana wale  
waliopewa kitabu ila baada ya  
kuwajia hoja hiyo (waliyokuwa  
wakitaka).*

مَا جَاءَتْهُمْ الْبَيِّنَةُ ﴿٤﴾

وَمَا أَمْرٌ إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ

مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ

وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيؤْتُوا

*5. Na wala hawakuamrishwa  
ila kumuabudu Allah kwa  
kumtakasia dini, waache dini  
za upotofu na wasimamisha  
sala na kutoa Zakat hiyo ndiyo  
dini iliyo sawa (ambayo  
waowameikataa).*

الزَّكَاةَ وَذَلِكَ دِينُ الْقِيَمَةِ ﴿٥﴾

6.(Basi) bila shaka wale waliokufuru miongoni mwa watu waliopewa Kitabu na washirikina wataingia katika moto wa Jahannam wakae humo humo milele, nao ni waovu wa viumbe.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ  
الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ فِي نَارِ  
جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا أُولَئِكَ  
هُمْ شَرُّ الْبَرِيَّةِ ﴿٦﴾

7.Hakika wale walioamini na kutenda mema basi hao ndio wema wa viumbe.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا  
الصَّالِحَاتِ أُولَئِكَ  
هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ ﴿٧﴾

8.Malipo yao kwa Mola wao ni mabustani ya daima ambayo mito inapita mbele yake wakae humo milele (hali ya kuwa) Allah amewaridhia nao wameridhika. (malipo) hayo ni kwa yule anayemuogopa Mola wake.

جَزَاءُ لَهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنَّاتُ عَدْنٍ  
تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ  
فِيهَا أَبَدًا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا  
عَنْهُ ذَلِكَ لِمَنْ خَشِيَ رَبَّهُ ﴿٨﴾

## Maelezo juu ya Sura

Jina la sura hii linatokana na neno **al-bayyina** lililotumika katika aya yake ya kwanza. Ni sura ya 98 katika msahafu na ya 100 katika mpango wa kushuka. Imeshuka Madina.

## Mafunzo

Waliopewa kitabu ni Mayahudi na Wakristo wanaodai kuwa wanaishi kwa kufuata vitabu vya Mwenyezi Mungu miongoni mwa suhufi ya Ibrahim (a.s) na Taurati ya Musa (a.s), Zaburi ya Daud (as) na Injili ya Isa (as). Washirikina ni wale wanaoabudu mungu mwingine asiyekuwa Allah na kuishi kwa kufata yale ambayo Allah(s.w)

hakuyateremsha, na wala wanaofuata matamanio ya nafsi zao (5:44,45,47 na 25:43-44)

Muradi wa aya ya 1-4 ya sura hii ni kwamba kabla ya kuletwa Mtume Muhammad (s.a.w), Mayahudi na Wakrisito wa Madina waliokuwa wakipigana mara kwa mara na makabila ya washirikina wa mji huo, walikuwa wakiwatambia washirikina kuwa atakapokuja mtume wa Mwenyezi Mungu wanayemtarajia kutokana na utabiri wa vitabu vyao, watamfuata kisha atawaunganisha pamoja na kuwa na nguvu ya kuwapiga na kuwashinda. Walitarajia kuwa mtume huyo atatokana na wao. Washirikina wa Madina waliathiriwa na maneno haya, wakawa nao pia wanamngojea mtume huyo na kuweka azma ya kumuamini na kumfuata.

Mtume (s.a.w) alipokuja na Qur'an yenye sharia madhubuti, washirikina wa Madina walipodhihirikiwa na ujio wake walimuamini na kumuunga mkono katika kusimamisha Dola ya Kiislamu Madina. Mayahudi na Wakristo pamoja na kudhihirikiwa na ujio wa Mtume (s.a.w) wengi wao walimkataa kwa sababu ya husuda kwa vile hakuwa katika wao.

Katika aya ya 5 tunafahamishwa kuwa Mtume (s.a.w) hakuleta dini mpya bali alifundisha Dini ile ile moja ya Mwenyezi Mungu inayowataka watu wasimamishe swala, watoe zakat na watekeleze maamrisha yote mengine ya Mwenyezi Mungu na kujiepusha na makatazo yake yote kama yalivyobainishwa katika Qur'an na vitabu vingine vyote vya Mwenyezi Mungu vilivyoitangulia Qur'an ikiwa ni pamoja na Taurat, Zaburi na Injili wanavyodai kuvifuata Mayahudi na Wakristo.

Katika aya ya 6, Mwenyezi Mungu anatoa onyo kali kwa makafiri miongoni mwa Mayahudi, Wakristo na washirikina wanaoendesha maisha yao kinyume na mwongozo wa Qur'an na Sunnah ya Mtume Muhammad (s.a.w) kuwa watastahiki adhabu kali ya moto wa Jahannam na kudumu humo. Watastahili kupata adhabu kutokana na kufanya maovu na fisadi katika jamii.

Katika aya ya 7 na 8, Mwenyezi Mungu anawabashiria pepo wale waumini wakweli, walioendesha maisha yao kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah ya Mtume (s.a.w) na kufanya juhudi ya kusimamisha haki na uadilifu katika jamii.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

1. Katika zama zetu hizi muongozo pekee wa kumuongoza mwanaadamu ni Qur'an kama alivyokuja nayo Mtume Muhammad (s.a.w) na kuibainisha katika maisha ya kila siku ya kibinafsi, kifamilia na kijamii.
2. Makafiri miongoni mwa Mayahudi, Wakristo, Washirikina na Wanafiki wamehiari kuendelea kuwepo katika upotofu kwa jeuri tu na kwa ajili ya maslahi ya dunia kwani uongofu ameshakuja nao Mtume (s.a.w) na ni wenyekubakia katika (usahihi) wake. Mtume (s.a.w) katika Hija ya kuaga aliweka hili bayana:

*"Naondoka lakini nakuachieni vitu viwili ambavyo mkishikamana navyo hamtapotea abadan, navyo ni kitabu cha Allah (Qur'an) na Sunnah yangu"*

3. Wana adhabu kali huko akhera wale wanaofuata upotofu baada ya kuwajia haki na hapa duniani wataishi maisha ya khofu na huzuni za kila namna.
4. Wenye kumuamini Mtume (s.a.w) na yale yaliyoshushwa kwake na yale walioshushiwa Mitume kabla yake, na wakaishi kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah watalipwa malipo mazuri ya kudumu milele huko peponi na hapa duniani wataishi maisha ya heshima na amani ya kweli ya kimwili na kiroho.

## **ZOEZI 3:05**

1. Hifadhi kifuani Suratul-Bayyinah na tafsiri yake.
2. Ainisha mazingira ya historia ya kushushwa Suratul Bayyinah ukizingatia makundi yaliyotajwa katika aya yake ya kwanza.
3. Tunapata mazingatio gani kutokana na Suratul Bayyinah.



## 7. Surat-ul-Takaathur

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Kumekughafilisheni kutafuta  
wingi (wa vitu vya ulimwengu).

أَلْهَدِكُمْ التَّكَاثُرَ ①

2. Hata mumeingia makaburini  
(hamjafanya lolote la Akhera  
yenu).

حَتَّى زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ ②

3. Sivyo, karibuni hivi mtajua  
(kuwa sivyo hivyo).

كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ③

4. Kisha (nasema) sivyo hivyo,  
karibuni hivi mtajua (kuwa sivyo  
hivyo).

ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ④

5. Sivyo hivyo, lau kama (nyinyi)  
mnajua kwa ujuzi wa yakini  
(kuwa sivyo hivyo, basi  
msingefanya hivyo).

كَلَّا لَوْ تَعْلَمُونَ عِلْمَ الْيَقِينِ ⑤

6. Hakika mtauona moto.

لَتَرَوُنَّ الْجَحِيمَ ⑥

7. Kisha (nasema) mtamuona  
kwa yakini.

ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا عَيْنَ الْيَقِينِ ⑦

8. Kisha kwa hakika mtaulizwa  
siku hiyo juu ya neema  
(mlizopewa mlizitumiaje).

ثُمَّ لَتَسْأَلَنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ⑧

## Maelezo juu ya Sura

Sura hii imepata jina lake kutokana na neno **at-takaathur** lililomo katika aya ya kwanza. Ni katika sura za Makkah na ni ya 16 katika utaratibu wa kushuka. Ni sura ya 102 katika msahafu.

## Mafunzo

Katika aya ya 1-2 Allah (sw) anawatanabahisha watu kuwa wameghafilika na kutafuta wingi wa maslahi ya kidunia ikiwa ni pamoja na mali na watoto; starehe na anasa; umaarufu pamoja na madaraka mpaka uhai wao unaisha pasipo kufanya lolote katika kuliendea lengo halisi la maisha yao.

Binaadamu hakuletwa hapa duniani ili ajitafutie maslahi ya dunia yaliyoorodheshwa na kujinufaisha kwayo bali ana lengo maalumu alilowekewa na muumba wake analotarajiwa alifikie. Lengo hili linadhihirishwa katika Qur'an:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾ مَا أُرِيدُ مِنْهُمْ مِنْ رِزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَنْ يُطْعَمُوا ﴿٥٧﴾ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ ﴿٥٨﴾

*"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu. Sitaki kwao riziki wala sitaki wanilishie. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ndiye mtoaji wa riziki, Mwenye nguvu madhubuti" (51:56-58)*

Kumuabudu Mwenyezi Mungu ni kumtii kwa kufuata mwongozo wake kwa ukamilifu katika kila kipengele cha maisha ya binaadamu ya kibinafsi na kijamii. Mwenyezi Mungu hakutuwekea lengo la kumuabudu ili tumnufaishe kama wafalme wanavyonufaishwa na raiya zao. Binaadamu ndiye anayehitajia kwa Mwenyezi Mungu na neema zote alizonazo ametunukiwa na Yeye. Bali binaadamu ametakiwa amuabudu Mwenyezi Mungu katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii ili kusimamisha uadilifu katika jamii na kudumisha furaha na amani ya kweli.

Mali, watoto, madaraka na neema mbalimbali alizonazo ni dhamana aliyopewa na Mola wake ili imuwezesha kufikia lengo tarajiwa na kusimamisha uadilifu katika jamii. Hivyo binaadamu anawajibika kuchuma mali na kutafuta maslahi mbalimbali ya dunia kwa kuchunga mipaka ya muumba wake na pia anawajibika kutumia vitu hivyo kwa kuchunga mipaka yake. Akifanya hivyo atakuwa ameliendea vyema lengo la kuumbwa kwake na mola wake atamridhia maisha ya dunia na akhera.

Lakini endapo binaadamu atapupia kutafuta wingi wa mali na maslahi mbalimbali ya maisha ya dunia kwa kuchupa mipaka ya Allah (sw) na baada ya kuvipata vitu hivyo akajivuna na kuleta fisadi katika jamii atakuwa amepoteza dira ya lengo la kuumbwa kwake na atakuwa amekhini amana aliyopewa. Binaadamu wa sampuli hii, pamoja na kujiona na kuonekana machoni mwa watu hapa duniani kuwa amefaidi mali na madaraka makubwa aliyokuwa nayo, katika maisha ya akhera atakuwa dhalili kuliko waliodhalili katika adhabu ya moto wa Jahannamu.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

1. Pupa katika kutafuta mali na anasa za dunia ndiyo inayomshughulisha binaadamu hata akasahau lengo la kuumbwa kwake na hadhi yake hapa ulimwenguni.
2. Kuchuma mali na kutafuta maslahi mengine ya dunia si jambo baya iwapo itachungwa mipaka ya Allah (sw) na lengo likazingatiwa.
3. Kutumia mali, kustarehe na kufurahia maisha ya dunia si vibaya katika Uislamu iwapo utafuatwa mwongozo wa Allah (sw) na kuchunga mipaka yake.
4. Kuchuma mali na kuwahangaikia wake na watoto wetu kusitushughulishie kiasi cha kutusahaulisha na majukumu

yetu mbele ya Mwenyezi Mungu kama vile kuipigania dini yake na kuisimamisha katika jamii kwa mali zetu na nafsi zetu.

5. Kuwepo siku ya malipo ni jambo lisiloepukika ili kila mtu aoneshwe namna alivyotumia neema mbalimbali alizotunukiwa na Mola wake katika kuendea lengo la kuumbwa kwake. Wale waliotumia amana hii kama ilivyotakiwa kwa kusimamisha Uislamu katika jamii na kumuabudu Mola wao ilivyostahiki watazawadiwa starehe za peponi na wale waliohini amana hii kinyume na walivyoagizwa na Mola wao kwa kumuabudu twaghuti na kuifisidi jamii, wataadhibiwa kwa kuingizwa Motoni Jahannam.

### **ZOEZI 3:06**

1. Hifadhi kifuani Suratut-Takaathur na tafsiri yake.
2. Toa mafunzo makuu yatokanayo na Suratut-Takaathur

## 8. Suratul-'Asr (103)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa zama (wakati).

وَالْعَصْرِ ﴿١﴾

2. Kuwa binaadamu yumo katika  
hasara.

إِنَّ الْإِنْسَانَ لِفِي خُسْرٍ ﴿٢﴾

3. Ila wale walioamini na  
wakafanya mema. Wakahusiana  
haki na wakausiana  
kushikamana na subira.

إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا  
الصَّالِحَاتِ وَتَوَّصَوْا بِالْحَقِّ

وَتَوَّصَوْا بِالصَّبْرِ ﴿٣﴾

### Maelezo juu ya Sura

Jina la sura hii linatokana na neno **al-'asr** ambalo ndio aya yake ya kwanza. Hii ni sura ya Makkah iliyoteremka katika kipindi cha mwanzo mwanzo cha Utume. Ni sura ya 13 kushuka na ni ya 103 katika Msahafu.

### Mafunzo

Sura hii ni ya pekee katika ufupi wake na ukubwa wa maana yake. Ikitafsiriwa vilivyo kiutendaji inamuwezesha binaadamu kusimamisha Uislamu katika jamii. Sura hii ni muhtasari wa kuuendea Uislamu wote. Ni kwa msingi huu Imamu Shafii amethubutu kusema kuwa kama watu wataizingatia kwa makini sura hii peke yake ingeliwatosha kuwa mwongozo wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Kutokana na uzito wa ujumbe wa sura hii tunafahamishwa katika Hadithi ya Tabarani iliyopokelewa kwa 'Abdullah bin Hisn Ad-Darimi, kuwa kila

masahaba wawili walipokutana hawakufarikiana bila ya kusoma suratul 'Asr.

Sura inaanza kwa kiapo. Zipo sura nyingi katika msahafu (Qur'an) ambazo zimetanguliwa na kiapo kama hii. Viapo hivi vinatafsiri mbili:

**Kwanza**, ni kuwa Mwenyezi Mungu anasisitiza umuhimu wa ujumbe unaofuatia kiapo hicho. Kwamba msomaji asiuchukulie ujumbe huo kirahisi au kwa wepesi, bali aupe uzito na umuhimu mkubwa.

**Pili**, kila kilichoapiwa kinashuhudia ukweli wa ujumbe anaopewa mwanaadamu. Mwenyezi Mungu anahiari ya kuapia baadhi ya viumbe vyake kufikisha ujumbe kwa binaadamu.

Binaadamu haruhusiwi kuapia viumbe. Kama anataka kusisitiza ukweli wa jambo basi aape kwa jina la Mwenyezi Mungu. Na kiapo si kitu cha kufanyia mchezo na maskhara kama ilivyozoeleka. Kiapo kwa jina la Mwenyezi Mungu kitumike iwapo ni lazima na kuheshimiwa kwa maana kuwa jambo linaloapiwa ni la kweli na kama ni ahadi itatekelezwa.

Unapoapia majina ya watu au vitu, unavipa uwezo wa kighaibu wa kusikia, kushuhudia na kusimamia mambo yako. Au unavipa uwezo wa Mwenyezi Mungu wa kusaidia mambo yako. Hiyo ni Shirk!

Katika sura hii, Mwenyezi Mungu anaapia zama au wakati ('Asr). Mwenyezi Mungu ameapa kwa wakati ili kuthibitisha na kusisitiza umuhimu wa ujumbe uliokusudiwa umfikie binaadamu. Raslimali ya mwanaadamu hapa ulimwenguni ni umri wake. Hivyo, kila sekunde atakayoitumia katika mambo ya kheri hiyo itakuwa ndiyo faida yake na kila sekunde atakayoitumia vibaya katika mambo ya shari au pumbao, hiyo itakuwa ndiyo hasara

yake. Katika siku ya malipo, miongoni mwa neema atakazoulizwa mtu na Mola wake, ni namna gani mtu alitumia umri(uhai) wake.

Wakati ambao Mwenyezi Mungu anauapia katika sura hii unaweza kuwa:

- (a) Tokea pale alipoumbwa binaadamu wa kwanza hadi siku ya kiyama (mwisho wa dunia)
- (b) Kipindi cha maisha ya binaadamu, tokea kuzaliwa hadi kufa kwake.
- (c) Zama za ummah wa Nabii Muhammad hadi siku ya mwisho.

Vyovyote itakavyokuwa kuapiwa wakati ni msisitizo juu ya umuhimu wa muda. Mtume (s.a.w) anasema katika maneno yake yenye hekima kuwa:

*"Laiti kama patakuwa na jambo ambalo watu wa peponi watalijutia ni ule wakati ambao uliwapita bila ya kumtaja (kumkumbuka) Mwenyezi Mungu"*

Katika Qur'an (3:191) Allah (sw) anatumfahamisha kuwa watu wenye akili na busara ni wale wanaomkumbuka nyakati zote katika kukiendea kila kipengele cha maisha yao.

Katika aya ya 2 na 3 baada ya kiapo, ujumbe unaofuatia ni kuwa Binaadamu wote wako hasarani ila wale wenye kufanya kwa pamoja mambo manne yafuatayo:

- (1) Walioamini
- (2) Wakaambatanisha Imani yao na vitendo vizuri.
- (3) Wakausia Haki
- (4) Wakausia Subra

Imani thabiti juu ya Allah (sw) na vipengele vyote vya nguzo za imani vilivyobakia ndio msingi wa kutenda mema na kuacha maovu. Imani bila ya kufuatiwa na amali njema haitambuliki mbele ya Allah (sw) na ni unafiki kama tunavyojifunza katika Qur'an"

﴿٨﴾ وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ آمَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ

*"Na katika watu, wako (wanafiki) wasemao: Tumemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na hali ya kuwa wao si wenye kuamini (kiutendaji),*

يُخَادِعُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَمَا يَخْدَعُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ

﴿٩﴾ وَمَا يَشْعُرُونَ

*wanataka kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini (kivitendo) lakini hawadanganyi ila nafsi zao, nao hawatambui"*  
(2:8-9)

Hivyo, Imani bila kufuatiwa na matendo mema kama yalivyoinishwa katika Qur'an na Sunnah haisadii na haikubaliki na amali njema bila ya Imani haina mashiko na ni riyaa.

Katika Uislamu, baada ya mtu binafsi kuamini na kufanya amali njema, analazimika kuwasia wengine kuamini na kutenda mema akianza na watu wake wa karibu. Waumini kwa pamoja wanawajibika kushikamana na kushirikiana katika kusimamisha haki katika jamii. Haki haiwezi kupatikana katika jamii mpaka Uislamu usimamishwe na sharia ya Mwenyezi Mungu iwe ndiyo inayotawala. Uislamu ukisimama katika jamii patakuwa na uadilifu ambapo watu wote watatendewa haki, dhuluma itaondoka na watu wataishi kwa furaha na amani. Hivyo tunaweza kusema kuusia haki ni kuusia kufuatwa na kusimama kwa njia ya haki ya maisha ambayo ni Uislamu.

Subra ni jambo lingine la msingi katika kuusia haki na kusimamisha Uislamu katika jamii. Pana misukosuko na mitihani



mingi katika kufanya amali njema na kuusia haki. Mzee Luqman alimuusia mwanawe:

يَذُنُّنِي أَقِمِ الصَّلَاةَ وَأْمُرْ بِالْمَعْرُوفِ وَأَنْهَ عَنِ الْمُنْكَرِ  
وَأَصْبِرْ عَلَيَّ مَا أَصَابَكَ إِنَّ ذَلِكَ مِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿١٧﴾

“Ewe mwanangu! Simamisha swala na uamrishe mema na ukataze mabaya, na usubiri juu ya yale yatakayokusibu (kwani mwenye kuamrisha mema na kukataza mabaya lazima zitamfika taabu) na hakika hayo ni katika mambo yanayostahiki kuazimiwa” (31:17)

Pia Allah (sw) anatutanabaisha katika aya ifuatayo:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تُدْخَلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ  
وَيَعْلَمِ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٢﴾

“Je! Mnadhani mtaingia peponi, hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale waliopigania Dini ya Mwenyezi Mungu miongoni mwenu na kuwapambanua waliofanya subra? (3:142)

Katika kupigania Dini ya Mwenyezi Mungu (sw); hapana shaka ipo misukosuko mikubwa ambayo inahitaji subra kubwa. Na Mwenyezi Mungu anaahidi kuwatia binaadamu katika mitihani mbalimbali ili kuwapima imani zao.

وَلَتَبْلُؤَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ  
وَالْأَنْفُسِ وَالْثَّمَرَاتِ وَبَشِيرِ الصَّابِرِينَ ﴿١٥٥﴾

“Na tutakutieni katika msukosuko wa khofu na njaa na upungufu wa mali na watu na matunda. Na wapashe habari wanaosubiri, (2:155)

الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٦﴾

*Ambao uwapatapo msiba husema: "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake yeye tutarejea" (2:156).*

Kwa ajili ya ufafanuzi, subira yaweza kugawanyika ifuatavyo:

**Kwanza**, Subra katika kutenda mema, kudumu katika kutenda mambo mema si jambo jepesi. Yahitaji subra kubwa huku mtu akitarajia kuwa Mwenyezi Mungu atamlipa.

**Pili**, kufanya subra katika kujizuia na maovu. Mambo maovu na machafu mara nyingi yanavishawishi vikubwa. Kwa hiyo yahitaji subra kujizuia na mambo machafu.

**Tatu**, kufanya subra katika kupambana na misukosuko mbalimbali ya maisha.

**Nne**, Mtu anatakiwa pia awe na subra katika kuishi na wenzake. Watu wanatabia tofauti. Kwa hiyo kuishi pamoja panahitaji subra kubwa na kustahimiliana.

**Tano**, kutokuwa na haraka ya kupata matunda ya juhudi ulizozitia katika harakati za kusimamisha Uislamu katika jamii.

**Sita**, Subira katika kutoa maamuzi. Linapotokea tatizo, waumini hawatakiwi kuchukua mamuzi ya harakaharaka, bali wanatakiwa watulizane na kutafakari kabla ya kuchukua maamuzi

## **Mafunzo kwa Muhtasari**

1. Mwenyezi Mungu huapa kwa kutumia viumbe vyake ili kwa viumbe hivyo ambavyo vinafahamika kwa wazi viwe kielelezo cha kumthibitishia mwanaadamu hicho kinachoapiwa.

2. Muumini anatakiwa aape kwa jina la Mwenyezi Mungu (sw) kuapia kiumbe chochote kile ni shirk.
3. Kwa waumini si vizuri kufanyia mas-hara viapo. Kinachothibitishwa na kiapo lazima kiwe ni cha kweli. Kuleta viapo mara kwa mara ni dalili ya unafiki.
4. Wakati ni rasilimali muhimu sana inayotakiwa itumiwe kwa uangalifu mkubwa sana.
5. Imani ya kweli huambatana na vitendo vizuri.
6. Uislamu sio dini ya ubinafsi. Kwa hiyo ni lazima waumini wa kweli wausiane kufanya mema na kushirikiana kusimamisha haki na uadlilifu katika jamii. Waislamu wanaowajibu wa kuamrisha mema na kukataza maovu katika jamii.
7. Subra ni nyenzo muhimu na ya lazima katika kuishi kiislamu na kusimamisha Uislamu katika jamii.

### **ZOEZI 3:7**

1. Hifadhi kifuani Suratul-'Asr na tafsiri yake.
2. Ainisha maeneo makuu manne (4) ambamo mwanaadamu analazimika kufanya subra.
3. Ainisha mafunzo makuu matano (5) yatokanayo na Suratul-'Asr.

## 9. Surat-ul-Humazah (104)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma,  
Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

*1. Adhabu kali itamthibitikia kila  
mwenye kuramba kisogo,  
msengenyaji.*

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ﴿١﴾

*2. Ambaye amekusanya mali na  
kuyahesabu.*

الَّذِي جَمَعَ مَالًا وَعَدَّدَهُ ﴿٢﴾

*3. Anadhani ya kuwa mali yake  
yatadumisha milele.*

يَحْسَبُ أَنَّ مَالَهُ أَخْلَدَهُ ﴿٣﴾

*4. Hasha! Bila shaka atavurumizwa  
katika (moto unaoitwa) Hutama.*

كَلَّا لِيُبَدَّنَ فِي الْأَخْطَمَةِ ﴿٤﴾

*5. Na ni jambo gani litakalokujulisha  
(hata ukajua) ni nini Hutama?*

وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْأَخْطَمَةُ ﴿٥﴾

*6. (Huo) ni moto wa Allah  
uliowashwa (kwa ukali barabara).*

نَارُ اللَّهِ الْمَوْقُودَةُ ﴿٦﴾

*7. Ambao unapanda nyoyoni.*

الَّتِي تَطَّلِعُ عَلَى الْأَفْئِدَةِ ﴿٧﴾

*8. Hakika huo (moto) watafungiwa  
(wawemo ndani yake).*

إِنَّهَا عَلَيْهِمْ مُّوَصَّدَةٌ ﴿٨﴾

*9. Katika magogo marefu marefu.*

فِي عَمَدٍ مُمَدَّدَةٍ ﴿٩﴾

## **Maelezo juu ya Sura**

Sura hii imepata jina lake kutokana na neno **humazah** lililomo katika aya ya kwanza. Ni sura ya Makka, ya 32 kushuka na ya 104 katika msahafu.

## **Mafunzo**

Sura hii imeanza na makamio ya adhabu kali watakayopata wasengenyaji na wale wanaochuma mali na kuilimbikiza pasina kuitumia katika njia za kheri.

Ulimi ni katika neema za Mwenyezi Mungu (sw) kwa mwanaadamu ambayo kama haikutumika kwa kuchunga mipaka ya Mwenyezi Mungu ipasavyo ina uwezo mkubwa wa kuleta uharibifu na machafuko makubwa katika jamii. Miongoni mwa madhambi makubwa yanayochumwa na ulimi ni: kuzulia watu, kusengenywa, kusema uwongo, kushuhudia uwongo, kutukana, kuchochea na kufitinisha watu.

Kuhusiana na maana ya kusengenywa Mtume (s.a.w) anatuambia katika Hadithi iliyosimuliwa na Abu Hurairah kwamba, Mtume (s.a.w) aliuliza masahaba:

*“Je, mnajua maana ya kusengenywa? Masahaba wakamjibu: Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wajuao. Akasema (Mtume): Kumzungumza ndugu yako (asiyekuwepo) kwa jambo asilolipenda. Akaulizwa: Unaonaje ikiwa lile jambo analo? Akajibu: Ikiwa lile jambo ulisemalo analo, basi utakuwa umemsengenywa na ikiwa hanalo utakuwa umemzulia” (Muslim).*

Usengenyi unapoenea katika jamii hufitinisha watu, hujenga chuki na kuvunja umoja na mshikamano. Kwa ajili hiyo makemeo

makali yametolewa. Pia Allah (sw) katika kututanabahisha juu ya uovu wa usengenyi, amelifananisha ovu hili sawa na mtu kula nyama ya maiti ya ndugu yake, Qur'an (49:12)

Kuramba kisogo ni kusengenyi kwa kutumia ishara kwa macho, ulimi, midomo, mikono, miondoko na maandishi. Hata mwenye kusikiliza habari za kusengenyi naye anahesabiwa kuwa amesengenyi kama tunavyojifunza katika hadithi:

*Ibn 'Umar (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Msikilizaji naye ni mmoja wa wasengenyaji" (Tabarani)*

Kosa la usengenyaji limeunganishwa na kosa la kukusanya na kuhesabu mali bila ya kuchunga mipaka ya Mwenyezi Mungu katika kuchuma na katika kutumia. Mali inayomilikiwa na watu wasio wacha-Mungu imekuwa ndio sababu ya fitna na dhuluma katika jamii. Wenye mali hujisikia kuwa wao ndio wao na huwadharau wengine na kuwasengenyi kwa njia za kejeli na ishara za macho na ulimi.

Wenye kusengenyi na wenye kujilimbikizia mali pasina kuchunga mipaka ya Mwenyezi Mungu (s.w) katika kuchuma na kutumia, wote wamekamiwa kupata adhabu kali ya mto wa Hutama na watafungwa humo kwa minyororo katika magogo marefu marefu.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

1. Kusengenyi ni katika dhambi kubwa.
2. Ni makosa makubwa kuchuma mali na kuitumia pasi na kuchunga mipaka ya Mwenyezi Mungu na kufuata maagizo yake.

3. Ne.ema za Mwenyezi Mungu (sw) zikitumiwa kinyume na maagizo yake huwa ni sababu ya kuleta machafuko na uharibifu katika jamii.
4. Ni lazima iwepo siku ya malipo ili wale waliosababisha machafuko na uharibifu katika jamii wapate adhabu stahiki.

### **ZOEZI 3:8**

1. Hifadhi kifuani Suratul-Humazah na tafsiri yake.
2. "Adhabu kali itamthubutikia kila mwenye kuramba kisogo, msengenyaji" (104:1). Fafanua juu ya ovu lililokemewa katika aya hii.
3. Ainisha mafunzo yatoakanayo na Suratul-Humazah.

## 10. Suratul-Fyl (105)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

*1. Je! Huoni jinsi Mola wako  
alivyowafanya watu wenye  
ndovu?*

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ

بِأَصْحَابِ الْفِيلِ ﴿١﴾

*2. Je! Hakujaalia vitimbi  
vyao kuharibika?*

أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِي تَضْلِيلٍ ﴿٢﴾

*3. Na tukawapelekea ndege  
makundi kwa makundi.*

وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿٣﴾

*4. Wakawapiga kwa mawe ya  
udongo wa kuchoma.*

تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّن سِجِّيلٍ ﴿٤﴾

*5. Akawafanya kama majani  
yaliyoliwa (yakatapikwa).*

فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍ ﴿٥﴾

### Maelezo juu ya Sura

Jina la sura hii linatokana na neno **al-fyl** lililomo katika aya ya kwanza. Sura hii ni ya 105 katika msahafu na ni ya 19 katika mtiririko wa kushuka. Imeshuka katika kipindi cha mwanzo wa utume, Makka.

Ili kupata vizuri ujumbe wa sura hii hatunabudi kuirejea historia iliyojiri wakati huo mpaka kupelekea kutokea tukio hili la



**watu wenye ndovu** (as-hab al-fyl). Tukirejea katika tafsiri ya sheikh Abdullah Saleh al-Farsy, tunapata kisa hiki kutoka kwa wanahistoria mbalimbali kuwa mnamo karne ya 6 A.D dola ya Kikristo ya Kirumi, ilivamia Yemen na kuiweka chini ya utawala wake kwa lengo la kudhibiti biashara inayopitia bahari ya Sham (Red Sea). Pia Warumi walikuwa na azma ya kudhibiti misafara ya Waarabu ya biashara kati ya Yemen na Syria (Sham) na kueneza ukristo Bara Arab. Abraha aliyekuwa miongoni mwa makamanda wa Kihabeshi walioiteka Yemen, alifanywa kuwa Gavana.

Kwa mujibu wa maelezo ya Sheikh Al-Farsy, Abraha, baada ya kuimarisha utawala wake huko Yemen, alielekeza mawazo yake katika lile lengo la Warumi na marafiki zake wakristo wa Uhabeshi, la kueneza Ukristo Bara Arab kwa upande mmoja na kuidhibiti na kuitawala biashara iliyokuwa ikifanyika kupitia kwa Waarabu kati ya nchi za Mashariki na tawala za Kirumi kwa upande mwingine.

Hitajio la kufanikisha hayo liliongezeka kwa sababu mgogoro baina ya dola ya Kirumi na dola ya Kipeishia (Kiajemi) ulisababisha kuvurugwa kwa njia zote za biashara kati ya dola ya Kirumi na nchi za Mashariki.

Ili kufikia lengo hilo, Abraha alijenga kanisa kuu huko San'a ambalo wanahistoria wa Kiarabu wamelitaja kwa jina la al-Qalis au al-Qulais au al-Qullais neno hili ni la Kiarabu na Kigiriki chake ni Ekklesia, yaani kanisa. Baada ya kumaliza kulijenga, Abraha alimwandikia Najjash akimwambia: "Sitapumzika mpaka nimewageuzia mahujaji wa Kiarabu katika kanisa hili badala ya Al-Ka'aba". Ibn Kathir ameandika kuwa Abraha alitamka wazi dhamira yake hiyo huko Yemen na akaifanya itangazwe hadharani. Kusudio lake lilikuwa kuwachokoza Waarabu ili wafanye kitu ambacho kitampa sababu ya kuishambulia Makka na kuibomoa Ka'aba. Inasemekana Mwarabu mmoja wa Kikuraysh akiwa amekasirishwa na tangazo hilo la hadharani aliingia katika kanisa hili na kulitia najisi (kinyesi) na baadhi ya wanahistoria wanasema

kijana mwingine Mkureish alikasirika na kulitia moto kanisa hilo. Lakini pia baadhi ya wanahistoria wanaona kuwa iliwezekana kabisa kuwa Abraha mwenyewe alipanga hayo ya kulinajisi kanisa na kulichoma yakatendwa na mtu wake ili apate kisingizio na sababu ya kuivamia Makka na hivyo kufikia malengo yake ya kuwaangamiza Maqureysh na kuwatisha Waarabu kwa ujumla. Kwa hali yoyote, chochote kilichotokea pale habari zilipomfikia Abraha kuwa mmoja wa wale wenye kuithamini Al-Ka'aba amelitia najisi kanisa lake, aliapa kuwa hatapumzika mpaka ameibomoa Ka'aba.

Hivyo katika mwaka wa 570A.D Abraha, alikusanya jeshi la askari 60,000 na ndovu 13 (wengine wanasema ndovu 9) na kuelekea Makka. Njiani alikabiliiana na vikosi vya baadhi ya makabila ya Kiarabu lakini alivishinda na viongozi wake kujisalimisha mmoja wao akiwa Nufail bin Habib wa kabila la Khath'am. Alipojisalimisha, Nufail alifanywa mwongoza njia ya kuelekea Makka. Alipofika al-Mughammas (au al-Mughammis) sehemu ambayo ni maili tatu (kilomita 5 hivi) kutoka Makka, Abraha alituma askari wake watangulizi nao wakamletea ngawira kutokana na mashambulizi yao dhidi ya kabila la Tinamah na Quraish ambayo ilikuwa pamoja na ngamia mia mbili (200) za Abdul Muttalib, babu yake Mtume (s.a.w) na kiongozi wa Makka. Kisha Abraha akamtuma mjumbe wake huko Makka na ujumbe kwamba yeye hakuja kupigana na watu wa Makka, bali kuibomoa Ka'aba. Kama hawatafanya upinzani, basi hakuna sababu ya kumwaga damu. Abraha pia alimwambia mjumbe wake kuwa kama watu wa Makka wanataka mazungumzo basi arudi na chifu wao Mkuu. Chifu Mkuu wa Makka zama hizo alikuwa Abdul-Muttalib babu yake Mtume (s.a.w). Mjumbe wa Abraha alipomfikishia ujumbe ule, Abdul-Muttalib alijibu "Hatuna uwezo wa kupigana na Abraha. Hii ni nyumba ya Allah. Akipenda ataihami nyumba yake" Yule mjumbe alimwomba aende naye kwa Abraha na akakubali.

Abdul-Muttalib alikuwa mtu mtukufu, adhimu na mwenye kupendeza, kiasi ambacho Abraha alipomuona, alivutiwa sana naye, akateremka kutoka kitini akakaa naye pamoja juu ya zulia; kisha Abraha akamuuliza anataka nini. Abdul-Muttalib akajibu kuwa alimtaka mfalme amrudishie ngamia wake mia mbili aliowachukua. Abraha alisema: "Nilivutiwa sana nilipokuona, lakini jibu lako hili limekudunisha machoni mwangu; unadai ngamia wako tu, lakini husemi lolote kuhusu hii Nyumba (Al-Ka'aba) ambayo ndiyo Haram (pahala patakatifu) yako na ya wahenga wako!" Abdul-Muttalib alijibu: "Mimi ni mmiliki wa ngamia wangu, na nakusihi unirudishie. Ama kuhusu Al-Ka'aba hiyo ina Mola wake; Naye ataihami" Abraha aliposema eti Allah hataweza kuihami Al-Ka'aba, Abdul-Muttalib alisema kuwa hayo yapo baina ya Allah(s.w) na Abraha. Kwa maneno hayo Abdul-Muttalib alimwacha Abraha ila alirudi na ngamia wake.

Abdul-Muttalib baada ya kurudi toka kambi ya Abraha aliwaamrisha Maquraish kuondoka toka mji wa Makka waende majabalini pamoja na familia zao kwa khofu ya kuuawa kwa ujumla. Kisha Abdul-Muttalib alikwenda Al-Ka'aba pamoja na baadhi ya machifu wa Kiquraish na kumwomba Allah (s.w) ailinde nyumba yake pamoja na wahudumu wake (maquraish). Zama hizo kulikuwa na masanamu 360 ndani na kando kando ya Al-Ka'aba lakini katika hali ngumu kama hiyo, wakayasahau kabisa masanamu hayo, wakamwomba Allah (s.w) tu peke yake awanusuru. Dua zao zilizonakiliwa katika vitabu vya historia hazina jina lolote isipokuwa la Allah (s.w). Wanahistoria, Ibn Hisham, Suhail na Ibn Jarir wamenukuu beti za dua ya Abdul-Muttalib kama ifuatavyo:

*“O Allah, mtu hulinda nyumba yake,  
Nawe ilinde nyumba yako.  
Usiuachie msalaba na hila zao, kesho kuzishinda hila zako  
Kama utaamua kuwaachia waifanye watakavyo Qibla yetu, basi  
Wewe ni muweza wa kufanya uyapendayo.*

*Wanusuru leo watumishi wako dhidi ya watumishi wa msalaba  
na waabudu wake.*

*Ewe Mola wangu, sina matumaini yoyote toka kwa yeyote dhidi  
yao isipokuwa kwako*

*Ewe Mola wangu, ilinde nyumba yako dhidi yao*

*Adui wa nyumba hii ni adui yako.*

*Wazuie wasiiharibu nyumba yako"*

Baada ya kufanya maombi hayo, Abdul-Mutallib na machifu wa Kikuraish pia walielekea milimani. Asubuhi ya pili Abraha alijitayarisha kuingia Makka, lakini ndovu wake makhususi, Mahmud, ambaye alikuwa mstari wa mbele, alipiga magoti. Alipigwa kwa fimbo za chuma na akachomwa kwa vyuma vya moto, lakini katu hakuinuka. Walipomuelekeza kusini, kaskazini au mashariki mara moja alianza kutembea, lakini mara tu walipomwelekeza upande wa Makka alipiga magoti. Wakati huo huo makundi ya ndege waliobeba mawe midomoni na makuchani mwao yalijitokeza na kuwaangushia mawe hayo Abraha na askari wake. Yeyote aliyegongwa na vijiwe hivyo alianza kubomoka vipande vipande.

Ibn Abbas (r.a) asema kuwa kila aliyegongwa na changarawe hizo, alianza kujikuna hadi kuharibu ngozi yake na kudondosha nyama ya mwili wake. Katika Hadithi nyingine, Ibn Abbas, asema kuwa nyama na damu vilitiririka kama maji na mifupa mwilini ilionekana wazi wazi. Hayo yalimtokea Abraha pia. Nyama ya mwili wake ilidondoka vipande vipande na yakatokea majeraha mwilini mwake yaliyotoa usaha na damu. Hawakuangamia askari wote hapo hapo, bali baadhi walikufa hapo na wengine walifia njiani walipokuwa wakirudi kwao. Abraha naye alifia njiani.

Nufail bin Habib, ambaye walimleta kama mwongoza njia toka kabila la Kath'am alitafutwa na kuombwa awaongoze hadi Yemen, lakini alikataa na kusema: "Sasa mtu ataweza kukimbilia wapi, ikiwa Allah ndiye anayemfurusha? Mchanika-pua (Abraha) ameshindwa si mshindi"

Tukio hili lilitokea Muhassir karibu na bonde la Muhassab kati ya Muzdalifa na Mina. Kwa mujibu wa Sahihi Muslim na Abu Daud, katika kuielezea Hijjatul-Wada'a ya Mtume (s.a.w) kuwa Imamu Ja'far As-Sadiq amesimulia toka kwa babu yake, Imamu Muhammad Baqir, naye toka kwa Sayyidina Jabir bin 'Abdallah (r.a), asema kuwa mtume (s.a.w) alipotoka Muzdalifa kwenda Mina aliongeza mwendo katika bonde la Muhassir. Imamu Nawawi ameeleza kuwa tukio la watu wa ndovu lilitokea hapo; kwa hivyo mahujaji wameamrisha kupita hapo kwa haraka, kwani Muhassir ni pahali palipotemshwa adhabu. Imamu Malik katika al-Muwatta amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema kuwa Muzdalifa yote ni mahali pema pa kukaa, lakini mtu asikae katika bonde la Muhassir.

Tukio la "watu wa ndovu" lilikuwa kuu na lenye umuhimu mkubwa mno kiasi kwamba kwa haraka habari zake zilienea kote Bara Arab, na washairi wengi wakalifanya kuwa ndio mada ya kutungia mashairi yao. Katika mashairi hayo jambo moja ni dhahiri kuwa kila mmoja alilichukulia ni udhahirisho wa nguvu za kimiujiza za Allah (sw), na hamna yeyote hata kwa ishara tu, aliyesema kuwa ni yale masanamu 360 yaliyosaidia chochote katika tukio hilo.

Si hayo tu, bali kwa mujibu wa Ummu Hani (r.a) na Az-Zubair bin Al-Awwam (r.a) Mtume (s.a.w) amesema: "Maquraish hawakumuabudu yoyote isipokuwa Allah (s.w) peke yake kwa muda wa miaka kumi baada ya tukio la "watu wa ndovu".

Waarabu wanauita mwaka uliotokea tukio hilo kama 'Am al-Fyl (mwaka wa ndovu) na katika mwaka huo huo Mtume Muhammad (s.a.w) alizaliwa. Muhaddithina na wanahistoria karibu wote wanasema kuwa tukio la watu wa ndovu lilitokea Muharram na Mtume (s.a.w) alizaliwa Rabi'ul-Awwal. Na wengi wao wanasema kuwa alizaliwa siku 50 baada ya tukio hilo la watu wa ndovu.

## **Mafunzo:**

Ukizingatia historia hii ya Abraha na jeshi lake la ndovu, utaona mantiki ya Allah (s.w), kuanza sura na kuuliza swali juu ya vitimbi vya watu wenye ndovu. Wakati aya hizi zinashushwa Waarabu na hasa Maquraish walikuwa hadhiri mno juu ya tukio hilo la kihistoria. Maquraish na Waarabu wote kwa ujumla waliamini kuwa KI-Ka'aba ililindwa katika shambulio hilo si na yeyote bali Allah (.s.w). Ni Allah (s.w) peke yake aliyeombwa na machifu wa kiquiraish alete nusra yake, na kwa miaka kadhaa Maquraish wakiwa wamevutiwa na kupendezwa sana na tukio hilo, hawakumuabudu yoyote isipokuwa Allah (s.w). Kwa hivyo, hakukuwa na hoja ya kutoa maelezo marefu katika sura hii, bali kuliashiria tu tukio hilo la kihistoria kulitosha ili watu wa Bara Arab hususan Maquraish wazingatie vyema nyoyoni mwao ujumbe anaolingania Mtume Muhammad (s.a.w), kuwa wamuabudu Allah (s.w) peke yake aliye Mola wa Ka'aba.

Pia kukumbushwa Maquraish na Waarabu kwa ujumla juu ya tukio hili ni kuwatahadharisha kuwa na wao wakitumia nguvu kuukandamiza ujumbe wa Allah (sw) aliokuja nao Mtume (s.a.w), wanaikaribisha ghadhabu ya Allah (sw), aliyewaangamiza watu wa ndovu pamoja na maguvu waliyokuwa nayo.

## **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kutokana na kisa kilichoashiriwa katika Sura hii tunajifunza yafuatayo:

- (1) Uwezo wa Allah (s.w) ni mkubwa sana. Viumbe vyote vipo katika milki yake na ni majeshi yake yaliyotayari tayari kufanya kazi kwa ajili yake.
- (2) Nusura ya Allah (s.w) na msaada wake vinapatikana wakati wowote watu watakapokuwa wamemuamini na

- kumtegemea ipasavyo yeye pekee.
- (3) Kuhilikishwa Abraha na jeshi lake na jeshi asilolijua wala kulitegemea ni alama ya kuwepo Allah (s.w) ambaye ni muweza na mwenye nguvu juu ya kila kitu.
  - (4) Tukio la watu wa ndovu linawapa waumini ujasiri wa kuupigania Uislamu na kuusimamisha katika jamii wakiwa na yakini kuwa iwapo watafanya hivyo kwa kumtegemea Allah (s.w) hapana nguvu yoyote inayoweza kuwashinda.

### **ZOEZI 3:9**

1. Hifadhi kifuani Suratul-Fyl na tafsiri yake.
2. "Je! Huoni jinsi Mola wako alivyowafanya watu wenye ndovu?" (105:1)  
Kwa kurejea historia toa maelezo kwa muhtasari juu ya kisa cha As-habil-fyl.
3. Wanaharakati wa kusimamisha Uislamu hivi leo wanajifunza nini kutokana na tukio lililowafika As-habil-Fyl?

## 11. Suratul-Quraysh (106)

*Kwa jina la Allah, mwingi wa  
Rehma, Mwenye Kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

*1. Ili kuwafanya Makurayshi  
waendelee.*

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

*2. Waendelee na Safari zao  
za wakati wa kusi (kwenda  
Yemen) na wakati wa  
kaskazi (kwenda Shamu).*

إِلَّا إِلَهُهُمْ رِحْلَةَ الْشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ

*3. Basi nawamuabudu  
Bwana wa nyumba hii  
(Al-Kaaba).*

فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ هَذَا الْبَيْتِ

*4. Ambaye anawalisha  
(wakati Waarabu wenzao  
wamo) katika njaa, na  
anawapa amani (wakati  
wenzao wamo) katika khofu.*

الَّذِي أَطْعَمَهُمْ مِنْ جُوعٍ

وَأَمَّنَّهُمْ مِنْ خَوْفٍ

### Maelezo juu ya Sura

Jina la Sura hii linatokana na neno **Quraysh** lililomo katika aya ya kwanza. Ni sura ya 106 katika msahafu na ni ya 29 kushuka katika kipindi cha utume Makka.

Kuwepo Al-Ka'aba katika mji wa Makkah, imekuwa ni neema kubwa kwa wakazi wake. Al-Ka'aba ilijulikana kwa Waarabu wote tokea zama za Nabii Ibrahim (a.s) kuwa ni mahali patakatifu pa kufanyia Ibada ya Hija. Maquraish, kabila ambalo lilichukua dhima



ya ulinzi wa Al-Ka'aba na kutoa huduma mbalimbali kwa mahujaji, walijipatia umaarufu na heshima kubwa. Kwa nafasi yao hiyo ya ulinzi wa Al-Ka'aba na utoaji huduma kwa mahujaji, waliheshimiwa na kutukuzwa na makabila yote ya Bara Arab. Si tu kwamba waliishi kwa amani katika mji wa Makka, bali popote pale walipopita hapana mtu au kabila lolote lililowagusa kwa ubaya. Heshima na utukufu wao ulizidi mara dufu baada ya tukio la kuangamizwa Abraha na jeshi lake la ndovu.

Kwa hiyo japo palikuwa na maharamia waliokuwa wakivamia misafara ya biashara, Maquraish hawakuathirika. Waliweza kwenda kaskazini na kusini kufanya biashara kwa amani bila kubughudhiwa. Kwa hiyo, Maquraish waliweza kutajirika na kuwa na vyakula vya kutosha kutokana na misafara yao ya biashara wakati makabila mengine yana hali ya khofu na njaa.

## **Mafunzo**

Katika sura hii, Makuraysh wanakumbushwa kuwa heshima hiyo iliyowaletea amani na utajiri mkubwa imetokana na Al-Ka'aba ambayo wanaijua vyema kuwa ni nyumba ya Allah (s.w). Hivyo hawanabudi kumshukuru Allah (s.w), kwa kumuabudu ipasavyo kwa kumuamini na kumtii mjumbe wake, Muhammad (s.a.w).

Ujumbe wa sura hii hauishii tu kwa Maquraish, bali kwa walimwengu wote kuwa neema zote zilizomzunguka binaadamu zimetoka kwa Allah (s.w) kama inavyosisitizwa katika Suratul-Rahman:

قَبَائِلُ آلِ الْعَرَبِ رَبُّكُمْ مَا تُكَدِّبُونَ

*“Basi ipi katika neema za Mola wenu mnaikanusha (kuwa si neema yake?)(55:77).*

Swali hili Allah (s.w) ameliuliza kwa kurudia mara 31 ili kuweka

bayana kuwa neema zote zilizomzunguka binaadamu zimetoka kwake. Hivyo kila binaadamu mwenye akili timamu na busara, hanabudi kushukuru neema alizotunukiwa na Mola wake kwa kumuabudu ipasavyo. Tutaweza kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo kwa kufuata mwongozo wake ambao ni Qur'an na Sunnah ya Mtume (s.a.w)

## Mafunzo kwa Muhtasari

Kutokana na sura hii kwa muhtasari tunajifunza yafuatayo:

- (1) Neema zote zilizotuzunguka zinatoka kwa Allah (s.w).
- (2) Amani, usalama na ustawi wa kweli hupatikana kwa kumtii Allah (s.w) ipasavyo. Kwa mfano amani na ustawi wa Makka ulipatikana kutokana na dua ya Nabii Ibrahim (a.s) ambaye kwa kumtii Mola wake aliacha familia yake mahali pakavu na papweke pasipo na msaada wowote wa kibinaadamu. Wakati anatekeleza amri ya Allah (s.w) ya kuiacha familia yake pale, Nabii Ibrahim (a.s) aliomba:

رَبَّنَا إِنِّي أَسْكَنْتُ مِنْ ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيْرِ ذِي زَرْعٍ عِنْدَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ  
 رَبَّنَا لِيُقِيمُوا الصَّلَاةَ فَاجْعَلْ أَفْئِدَةً مِنَ النَّاسِ تَهْوِي إِلَيْهِمْ وَارْزُقْهُمْ مِنْ  
 الثَّمَرَاتِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ ﴿٣٧﴾

*"Mola wetu! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya kizazi changu (mwanangu Ismail na mama yake, Hajar) katika bonde (hili la Makka) lisilokuwa na mimea yoyote katika nyumba yako takatifu. Mola wetu! Wajaalie (wawe) wasimamishaji swala. Na ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao na uwaruzuku matunda ili wapate kushukuru" (14:37)*

- (3) Mahusiano, maingiliano na mawasiliano baina ya mataifa katika nyanja mbalimbali za kijamii ni katika neema za Allah (s.w)

## **ZOEZI 3:10**

1. Hifadhi kifua ni Suratul-Quraysh na tafsiri yake.
2. Kwa kurejea historia onesho mahusiano ya kabila la Quraysh na Al-Ka'aba.
3. Onesho mahusiano ya maudhui ya Suratul-fyl na Al-Qurysh.
4. Ainisha mafunzo makuu mawili (2) yatokanayo na Suratul-Quraysh.

## 12. Suratul- Ma'un (107)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehema, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Je, Unamjua yule  
anayekadhibisha dini  
(asiyeamini malipo ya  
Akhera)?

أَرَأَيْتَ الَّذِي يُكَذِّبُ بِالدِّينِ ﴿١﴾

2. Huyu ni yule  
anayemnyayasa yatima.

فَذَلِكَ الَّذِي يَدُعُّ الْيَتِيمَ ﴿٢﴾

3. Wala hajihimizi (yeye wala  
wengine) kuwalisha maskini.

وَلَا يَحِضُّ عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ﴿٣﴾

4. Basi adhabu itawathubutikia  
wanaoswali.

فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾

5. Ambao wanapuuza  
(Maamrishi) ya Swala zao.  
6. Ambao hufanya riyaa

الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾

7. Nao hunyima misaada  
(midogomidogo)

الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ ﴿٦﴾

وَيَمْتَعُونَ ﴿٧﴾

## **Maelezo juu ya Sura**

Jina la sura hii linatokana na neno **al-ma'un** lililomo katika aya yake ya mwisho. Ni sura ya 107 katika msahafu na ni ya 17 katika kushuka katika kipindi cha utume cha Makka, kwa mujibu wa tafsiri ya Sheikh 'Abdullah S. Al-farsy, lakini kimaudhui, inaonesha ni sura ya Madina. Katika mazingira ya Makka hapakuwa na uwezekano wa kuufuata Uislamu kwa riya kwani kuufuata Uislamu ilikuwa kama vile kuamua kushika kaa la moto. Katika mazingira ya Madina ambamo dola ya kiislamu ilidhihiri baada ya kusimama dola ya Kiislamu walitokea wanafiki waliofuata Uislamu kwa riya kwa ajili ya maslahi ya kidunia tu.

## **Mafunzo**

Sura inaanza kwa kuuliza swali "Je unamuona yule ananayekadhibisha dini?" jibu likafuatia kuwa ni yule :

- (1) Anaye wanyanyasa mayatima
- (2) Asiye waangalia maskini kwa jicho la huruma
- (3) Anayepuuza swala
- (4) Anayefanya riyaa
- (5) Anayenyima misaada midogomidogo.

Kwa kuzingatia swali hili na jibu lake lililofuatia, tunajifunza kuwa ili mtu awe muumini wa kweli wa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho hanabudi kuwa makini juu ya haya yafuatayo:

**Kwanza**, kuwahurumia na kuwafanyia wema mayatima. Yatima ni mtoto aliyefiwa na wazazi wake, hasa baba, kabla ya kufikia baleghe. Msisitizo wa kuwatendea wema mayatima tunaupata katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Huraira (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Kaya (familia), bora kuliko zote ni ile ambamo*

*anatendewa wema yatima; na kaya mbovu kuliko zote ni ile ambamo ananyanyaswa yatima" (Ibn Majah)*

**Pili**, kuwahurumia na kuwasaidia maskini na wale wote wenye upungufu wa mahitaji ya msingi ya maisha khususan chakula. Tunajifunza katika aya nyingi za Qur'an kuwa waumini wa kweli ni wale ambao wanasimamisha swala na kutoa yale Allah aliyowaruzuku kwa ajili ya kuwapa wale wanohitajia. Pia tunajifunza katika Qur'an kuwa mtu anayeiogopa akhera ni yule anayewalisha maskini pasina kutarajia malipo au shukrani kutoka kwao au kutoka kwa yeyote - Rejea Qur'an (76:5-11)

**Tatu**, kutopuuza swala. Kutopuuza swala ni kuisimamisha swala. Swala husimama kwa kutekeleza kwa ukamilifu **sharti zake zote**, kuiswali vilivyo kwa kutekeleza **nguzo zake zote** kwa ukamilifu na kuwa na **unyenyekavu (khushui)** wakati wa kuswali. Mtu akiswali bila ya kuyazingatia haya matatu atakua amepuuza swala na ni ishara kuwa haamini siku ya malipo.

**Nne**, kujiepusha na riya. Riya ni kufanya amali njema kwa makusudio ya kuonesha watu, ili uonekane kuwa ni mwema kuliko ulivyo. Riyaa ni aina ya shirk na pia ni aina ya wizi. Kinyume cha riyaa ni Ikhlas, yaani kufanya kila jambo kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w) na malipo kutoka kwake tu. Afanyaye riyaa haamini kuwa Allah (s.w) atamlipa kwa mema yake anayofanya. Anatarajia tu malipo kutoka kwa watu. Hivyo akiona kuwa hamna wakumlipa kwa wema atakaoufanya, hafanyi hata kama ni wajibu wake.

**Tano**, kuwa mwepesi wa kuwasaidia watu kwa kila msaada wanaohitajia na hasa ile misaada midogo midogo ambayo una uwezo nayo kama vile kumsaidia jirani yako chumvi, unjiti wa kiberiti, nauli ya daladala, kalamu ya kuandikia n.k. Mtu bakhili ni mwongo kwani kila anapombwa msaada wa kitu chochote hudai hana, huku anacho. Mtu mchoyo haamini kuwa kuna malipo ya akhera ambapo mtu atalipwa kwa kila wema alioufanya kwa ikhlas.

## **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kutokana na sura hii tunajifunza kwa muhtasari yafuatayo:

- (1) Imani katika Uislamu inadhihirishwa na matendo na si maneno au matamano tu.
- (2) Muumini wa kweli ni yule anayewajali binaadamu wenziwe wanapokuwa na matatizo hususan wale wasiojiweza.
- (3) Swala ni lazima itekelezwe kama ilivyoagizwa na Allah (s.w) kupitia kwa mtume (s.a.w) kwa kuchunga sharti, nguzo na khushui.
- (4) Kila muumini analolifanya katika kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi, kifamilia na kijamii ni ibada na atalipwa na Mola wake endapo atalifanya kwa ikhlas na kuchunga mipaka ya Allah (s.w) na Mtume wake.
- (5) Muumini wa kweli ni yule aliye mwepesi kutoa misaada kwa binaadamu wenziwe pale wanapohitajia, maadamu ana uwezo wa kusaidia.

## **ZOEZI 3:11**

1. Hifadhi kifuani Suratul-Ma'un na tafsiri yake.
2. Ainisha mafunzo makuu matano (5) yatokanayo na Suratul-Ma'un.

## 13. Suratul-Kawthar (108)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

*1.Hakika tumekupa kheri nyingi.*

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ﴿١﴾

*2.Basi Swali kwa ajili ya Mola  
wako na uchinje (kwa ajili yake).*

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْصَحْ ﴿٢﴾

*3.Hakika adui yako ndiye  
atakaekuwa mkiwa (atakatikiwa  
na kila kheri).*

إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ﴿٣﴾

### Maelezo juu ya Sura

Sura hii imepata jina lake kutokana na nano **Al-kawthar** lililomo katika aya yake ya kwanza. Hii ni sura ya 108 katika msahafu na ni sura ya 15 kushuka. Sura hii imeshuka Makka katika kipindi cha mwanzo mwanzo cha utume wa Muhammad (s.a.w)

Kama tulivyoona katika Suratudh-Dhuha na Alam-Nashrah, sura hii nayo imeshushwa kumliwaza Mtume (s.a.w) na Waislamu kutokana na kejeli, dhihaka, mabezo na maneno ya kukatisha tamaa ya kila aina kutoka kwa makafiri wa Kiquraish. Katika kumkejeli na kumdhihaki Mtume (s.a.w) makafiri wa Makka walimuita "**Abtar**" yaani aliyekatikwiwa na kheri au mkiwa. Walimpachika Mtume (s.a.w) jina hilo baada ya kufariki, 'Abdallah, mtoto wa pili wa kiume wa mtume (s.a.w) baada ya kufariki mtoto wake wa kwanza, Qasim. Abu Lahab, ami yake Mtume (s.a.w),



aliyekuwa adui mkubwa wa Uislamu, alikwenda kwa furaha kwa machifu wa Kiquraysh akitangaza kuwa Muhammad amekuwa "Abtar" yaani amekuwa bila mrithi wala ukumbusho wa kuachwa nyuma.

Muhammad (s.a.w), baada ya kumuoa Bibi Khadija yeye na mkewe waliinukia kuwa miongoni mwa matajiri wakubwa katika mji wa Makka; lakini baada ya kupewa utume, Mtume (s.a.w) hakuwa na wasaa tena wa kufanya biashara na mali yao nyingi waliitumia kuwasaidia masikini, kuwagombooa watumwa na kuwasaidia Waislamu waliokuwa wakinyanyaswa na kudhulumiwa haki zao na jamaa zao makafiri kutokana na kusilimu kwao. Hivyo hali yao kiuchumi ilishuka.

Makafiri wa Makka walipoona mtume (s.a.w) ameshuka kiuchumi na ikatokea tena amefiwa na watoto wake wawili pekee wa kiume, walisherehekea wakipita huku na kule wakitangaza kuwa Muhammad (s.a.w) amekuwa "**Abtar**"

Sura hii imeshushwa kumliwaza mtume (s.a.w) na Waislamu, kuwa mtume (s.a.w) amepewa kheri nyingi na wale wanaopinga ujumbe wake ndio waliokatikiwa na kheri, bali hawajui tu kutokana na uoni wao mfinyu wa kutazama mambo kihalisia. Kheri nyingi alizopewa mtume (s.a.w) ni pamoja na kupewa utume, mwongozo wa Qur'an, wafuasi wengi, ushindi na kuifanya dini ya Allah kuwa juu ya dini zote. Pamoja na maliwazo hayo, mtume (s.a.w) na Waislamu kwa ujumla, wanaamrisha kuchinja kwa ajili ya Allah (s.w) na kufanya kila jambo kwa ikhlas.

## **Mafunzo**

Tunajifunza kutokana na sura hii kuwa kwa mtazamo wa Uislamu, mafanikio au kheri haipimwi kwa kiasi cha mali mtu alichohodhi au kiasi cha watoto wa kiume au jeshi lililochini ya milki yake. Hiki ni kipimo cha makafiri. Kwa mtazamo wa kiislamu kheri

nyingi au mafanikio ya kweli ni yale yatakayompelekea mtu kupata radhi za Allah (sw) na kustahiki kuwa miongoni mwa watu wa peponi. Mtu atastahiki kupata radhi za Allah (sw) pale atakapoufahamu Uislamu vizuri akautekeleza ipasavyo na kufanya juhudi za makusudi za kuusimamisha katika jamii.

Pia tunajifunza, kutokana na sura hii kuwa, maadui wa Uislamu, pamoja na maguvu mengi waliyonayo hivi sasa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, Waislamu wakifuata vilivyo nyayo za Mtume (s.a.w) na kupita mle alimopita hatua kwa hatua, hawana uwezo katu wa kuuzuia Uislamu kusimama katika jamii. Katika kipindi kile cha Mtume (s.a.w), makafiri wa Makka walijiona kuwa wao ndio "Abtar" baada ya muda mfupi tu, hasa baada ya kukombolewa Makka (Fat-h Makka) na kuwa chini ya uongozi wa Mtume (s.a.w). Ushindi huu unashuhudiwa katika Qur'an:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظَاهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*Yeye Mwenyezi Mungu ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote (mifumo yote ya maisha). Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi." (48:28)*

## **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kutokana na sura hii kwa muhtasari tunajifunza yafuatayo

- (1) Mafanikio hayapimwi kwa wingi wa mali na watu bali hupimwa kwa kiasi gani mtu amepata ridhaa ya Mola wake aliyemuumba kwa ajili ya lengo maalum. Mtu atapata ridhaa ya Allah (s.w) pale atakapoishi kulingana na lengo la kuumbwa kwake ambalo ni: "Kumuabudu Allah (sw) ipasavyo" - Rejea Qur'an (51:56).

- (2) Hakuna neema kubwa aliyotunukiwa mja na mola wake kuliko ile ya kuupokea Uislamu, kuujua kwa usahihi, kuufuata vilivyo, kuufikisha kwa wengine na kushirikiana nao katika kuusimamisha katika jamii. Neema hii Allah (s.w) anaidhirisha katika Qur'an:

الْيَوْمَ يَئِسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنَ الْيَوْمَ  
أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتِمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيْتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

*".....Leo waliokufuru wamekata tamaa katika Dini yenu, basi msiwaogope, bali niogopeni mimi. Leo nimekukamilishieni dini yenu, na kukutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini yenu...." (5:3)*

- (3) Hatimaye maadui na wapinzani wa Uislamu ni wenye kupata khasara na kufedheheka na Waislamu daima watakuja juu endapo watafuata mafundisho ya Uislamu vilivyo.

### **ZOEZI 3:12**

1. Hifadhi kifuani Suratul-Kawthar na tafsiri yake.
2. Suratul-Kawthar kama ilivyo Suratudh-Dhuhaa na Nashrah, ilishushwa kumliwaza Mtume (s.a.w) na waumini waliokuwa pamoja naye. Toa maelezo ya kihistoria juu ya hali iliyojiri dhidi ya Mtume (s.a.w) wakati inashushwa sura hii.
3. "Hakika tumekupa kheri nyingi" (108:1).  
Ainisha kheri nyingi alizopewa Mtume (s.a.w)
4. Toa mafunzo makuu yatokanayo na Suratul-Kawthar.

## 14. Suratul-Kafiruun (109)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma, Mwenye Kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Sema, Enyi makafiri.

قُلْ يَتَّيِّبُهَا الْكٰفِرُونَ ﴿١﴾

2. Siabudu Mnachoabudu.

لَا اَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٢﴾

3. Wala nyinyi hamuabudu  
ninayemuabudu.

وَلَا اَنْتُمْ عٰبِدُونَ مَا اَعْبُدُ ﴿٣﴾

4. Wala sitaabudu  
mnachoabudu.

وَلَا اَنَا عٰبِدُ مَا عٰبَدْتُمْ ﴿٤﴾

5. Wala nyinyi hamtaabudu  
ninayemuabudu.

وَلَا اَنْتُمْ عٰبِدُونَ مَا اَعْبُدُ ﴿٥﴾

6. Nyinyi mna dini yenu nami  
nina dini yangu.

لَكُمْ دِيْنِكُمْ وَلِيَّ دِيْنٍ ﴿٦﴾

### Mafunzo juu ya Sura

Sura hii imepata jina lake kutokana na neno **al-kaafiruuna** lililomo katika aya yake ya kwanza. Ni sura ya 109 katika msahafu na ni sura ya 18 katika utaratibu wa kushuka. Ni katika sura za Makka.

Sura hii ilishuka katika kipindi ambacho makafiri wa Kigureish walikuwa wakifanya juhudi mbalimbali ili kuzuia ujumbe wa Uislamu aliokuwa akiulingania Nabii Muhammad (s.a.w) usienee. Miongoni mwa jitihada zao za kutaka kuzima nuru ya Allah (sw), ni ile ya kutaka

kumlaghai Mtume (s.a.w) akubali kushirikiana na makafiri katika ibada kwa zamu; mwaka mmoja Waislamu waabudu masanamu pamoja na makafiri na mwaka unaofuata makafiri nao wamuabudu Mungu mmoja pamoja na Waislamu, ili makafiri na Waislamu wakae kwa amani bila ya kubughudhiana.

Kuna Hadithi nyingi zinazosimulia sababu ya kushushwa sura hii, miongoni mwa hizo ni ile aliyosimulia 'Abdullah bin Abbas (ra) kuwa Maquraish walimwambia mtume (s.a.w) "Kama tu ungekubali kujizuia kuongea dhidi ya miungu yetu, tungelikufanya uwe tajiri kuliko watu wote wa Makka, tungekuoza mwanamke wa chaguo lako na juu ya hayo, tungekufanya kiongozi wetu. Kama hayo hayakubaliki kwako, basi tunakupa shauri lingine ambalo ni la faida kwako na kwetu pia". Mtume (s.a.w) akauliza "Ni lipi shauri hilo? Wakajibu: "Kwa zamu, mwaka mmoja uiabudu miungu yetu, Lat na Uzza, na mwaka mmoja tutamwabudu Mungu wako, Allah". Mtume (s.a.w) akasema: "Vema, ngojeni nitaangaalia amri gani itakuja toka kwa Mola wangu". Hapo akateremshiwa Suratul-kaafiruun na ile aya ya 64 katika suratul-Zumar (39:64)

*Yaani "Sema Je! Mnaniamrisha niabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu enyi majahili" (Ibn Jarir, Ibn Abi Hatim, Tabarani)*

## **Mafunzo:**

Kwa kuzingatia mnasaba huo wa kihistoria, tunajifunza kuwa sura hii haikuteremshwa kuja kufundisha kuvumilia dini nyingine kama wadhaniavyo baadhi ya watu wa leo, bali iliteremshwa kutangaza waziwazi kutokubaliana na makafiri. Dini ya Uislamu ni tofauti na dini ya Ukafiri na katu hakuna uwezekano wa kuziunganisha. Japokuwa hapo mwanzoni msimamo huu ulielekezwa kwa makafiri wa Kiqureish kama jibu kwa mashauri yao ya suluhu na Mtume (s.a.w), msimamo huu unawahusu makafiri wote wa nyakati zote mpaka siku ya kiyama maadamu umewekwa ndani ya Qur'an.

Kwa upande mwingine Waislamu wameaamrisha kuwa mahali popote na katika zama zozote wajitenge na kujiepusha kushirikiana na makafiri katika mifumo ya maisha (dini) inayopingana na mfumo wa maisha (dini) wa Allah (s.w). Kwa maana nyingine umoja wa Waislamu na Wakristo (UWAWARU) unaopigiwa debe na nchi nyingi za kitwaghuti leo umeharamishwa kwa mujibu wa sura hii kwani ni sawa na ule ule ulaghai wa makafiri wa Kiqureish kwa Mtume (s.a.w). Waislamu wa kweli hawanabudi kudhihirisha kwa uwazi kwa maneno na matendo kuwa Uislamu haukubaliani au kuchanganyika na ukafiri hata chembe.

Tunajifunza katika Hadith mbalimbali kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akisoma sura hii mara kwa mara na kuwahimiza Waislamu kuisoma. Hebu turejee Hadith zifuatazo:

1. *Abdullah bin Umar (r.a) anasimulia kuwa mara nyingi alimsikia mtume (s.a.w) akisoma "Qul-yaa ayyuhal-kaafiruun" na "Qul-Huwallaahu Ahad" katika rakaa mbili za Sunnah kabla ya swala ya Alfajir na katika rakaa mbili za sunnah baada ya swala ya Magharibi. (Hadithi nyingi kama hiyo zikiwa tofauti kidogo kwa maneno zimenakiliwa na Tirmidh, Ahmad, Nasai, Ibn Majah, Ibn Hibbaan na Ibn Marduyah toka kwa Ibn Umar).*
2. *Amesimulia Khabbaab (r.a) "Mtume (s.a.w) amemuusia kusoma "Qul yaa ayyuhal-kaafiruun" wakati wa kulala na ilikuwa tabia ya Mtume (s.a.w) kuisoma sura hii wakati wa kulala" (Bazzar, Tabaran, Ibn Majah)*
3. *Ibn 'Abbas (r.a) amesema kuwa Mtume (s.a.w) aliwaambia watu: "Je, niwafundisheni jambo ambalo litawalinda kutokana na shirk? Jambo hilo ni kusoma "Qurl-yaa ayyuhal kaafiruun" wakati wa kulala. (Abu Ya'ala, Tabaran)*

4. *Anas bin Malik (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alimuusia Mu'adh bin Jabal (r.a) kusoma "Qul-yaa ayyuhali-kaafiruun" wakati wa kulala kwani hili ni tangazo dhidi ya shirk. (Baihaqi)*

## **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kwa muhtasari tunajifunza kutokana na sura hii kuwa:

1. Dini kwa mtazamo wa Qur'an ni mfumo wa maisha anaoufuata binaadamu katika kuendea maisha yake ya kila siku ya kibinafsi, kifamilia na kijamii. Kwa maana hii ukafiri nao ni dini kama ulivyo Uislamu.
2. Hapana uwezekano wa binaadamu kufuata dini mbili kwa wakati mmoja kwa mfano huwezi kuwa muislamu na wakati huo huo ukaishi kwa kufuata mifumo mingine ya maisha inayopingana na Uislamu.
3. Ili Waislamu wabakie katika msimamo huu wa kuukanusha mfumo wa maisha wa kikafiri, hawanabudi kujihimiza kufuata sunnah ya Mtume (s.a.w) ya kuisoma sura hii kabla ya kulala na katika swala za sunnah zilizotajwa.

## **ZOEZI 3:13**

1. Hifadhi kifuaani Suratul-Kaafiruun na tafsiri yake.
2. Kwa kurejea historia, toa sababu ya kushushwa Suratul-Kaafiruun.
3. Ainisha mafunzo makuu manne (4) yatokanayo na Suratul-Kaafiruun.

## 15. Suratun-Nasr (110)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehema, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

*1.Itakapofika nusura ya Allah  
(s.w) na kushinda.*

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١﴾

*2.Na utakapowaona watu  
wakiingia katika dini ya Allah  
makundi makundi.*

وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي  
دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا ﴿٢﴾

*3.Basi hapo mtakase Mola  
wako pamoja na kumsifu,  
Umuombe msamaha, hakika  
yeye ndiye apokeye toba.*

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَأَسْتَغْفِرْهُ  
إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ﴿٣﴾

### Maelezo juu ya Sura

Jina la sura hii linatokana na neno Nasr lililomo katika aya ya kwanza, na si jina tu, bali pia ndio kichwa cha habari cha sura hii. Ibn Abbas (r.a) anasema kuwa hii ndiyo sura ya mwisho ya Qur'an kuteremshwa, yaani baada ya sura hii hakuna sura kamili iliyoteremshwa tena kwa mtume (s.a.w) (Muslim, Nasai, Tabarani, Ibn Abi Shaibah)

Naye Abdullah bin 'Umar (r.a) asema kuwa sura hii iliteremshwa katika siku ya kati ya siku ya Tashrik katika tukio la Hijatul - Wi'daa' huko Mina, baada ya hapo Mtume (s.a.w) akatoa hutuba yake maarufu juu ya mgongo wa ngamia (Tirmidh, Bazzar, Baihaq, Ibn Abi Shaibah)



Hivyo, kwa mujibu wa Hadithi hizo sura hii ni ya 114 katika utaratibu wa kushuka na ni sura ya 110 katika msahafu. Kwa mujibu wa Hadithi mbalimbali sura hii ilimbashiria Mtume (s.a.w) kuwa amemaliza kazi yake na muda wake wa kufariki dunia umewadia.

*“Ibn 'Abbas (ra) amesema kuwa sura hii ilipotemshwa, Mtume (s.a.w) alisema kuwa kufariki kwake kumbashiriwa na kwamba wakati wake umewadia (Ahmad, Ibn Marduyah). Hadithi nyingi toka kwa Ibn Abbas zinasema kuwa kwa kuteremshwa sura hii Mtume (s.a.w) alielewa kuwa amebashiriwa kufariki kwake dunia (Musnad Ahmad, Ibn Jarir, Tabarani, Nasai, Abi Halim, Ibn Marduyah)*

Mtume (s.a.w) alifariki miezi mitatu na siku chache baada ya Hijjatul Wi'daa'.

Nusura na ushindi unaokusudiwa katika sura hii ni ule ushindi mkubwa Mtume (s.a.w) aliupata dhidi ya maadui wa dola ya kiislamu hususan baada ya mkataba wa Hudaibiyya. Mara baada ya mkataba kutiwa saini, Mtume (s.a.w) alishushiwa wahyi uliombashiria ushindi uliodhahiri.

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ﴿١﴾ لِيُغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿٢﴾ وَيَنْصُرَكَ اللَّهُ نَصْرًا عَزِيمًا ﴿٣﴾

*“Bila shaka tumekwisha kupa kushinda kuliko dhahiri. ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yanayokuja na kukutumizia neema zake na kukuongoa katika njia iliyonyooka. na akunusuru Mwenyezi Mungu nusura yenye nguvu kabisa" (48:1-3)*

Mkataba wa Hudaibiyya ulifanyika mwaka wa 6 A.H. Kabla ya mkataba wa Hudaibiyya, maadui walioisonga dola ya Kiislamu ni Maquraysh na makabila mengine ya Waarabu, Mayahudi, Warumi na Wanafiki. Baada ya mkataba wa Hudaibiyya na khususan baada ya kukombolewa Makka (Fat-h Makka) katika mwaka 8 A.H, Waislamu waliwashinda maadui zao wote na katika mwaka wa 9 A.H makabila ya Waarabu kutoka Bara Arab kote yalimiminika Madina makundi kwa makundi kuja kwa Mtume (s.a.w) kusilimu. Uislamu ulidhihiri kuwa juu ya mifumo yote ya maisha ya ushirikina iliyokuwepo wakati huo, hivyo Mtume (s.a.w) kufikia lengo la kuletwa kwake Mwenyezi Mungu akiwa shahidi:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*“Yeye (Mwenyezi Mungu) Ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na Dini iliyo ya haki, ili aishindishe (aidhihirishe) juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi (kuwa mtume wake amefikia lengo hilo) (48:28)*

Hivyo, wakati sura hii inashushwa lengo la kuletwa Mtume (s.a.w) lilishafikiwa na yale yote yaliyo bashiriwa, yaani nusura, ushindi na watu kuingia katika Dini ya Uislamu makundi kwa makundi, yalishapatikana. Ndio maana Mtume (s.a.w) akadhihirisha wazi kuwa muda wake wa kufariki dunia umeshawadia.

Tunajifunza katika Hadithi mbalimbali kuwa baada ya kushushwa sura hii Mtume (s.a.w) alizidisha kumsabihi Mola wake na kuleta maghira.

## **Mafunzo**

Kutokana na sura hii tunajifunza kuwa Waislamu hawana budi kufanya juhudi za makusudi za kuusimamisha Uislamu katika jamii

kwa mali zao na nafsi zao wakiwa na yakini kuwa watapata nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi uliokaribu. Rejea Qur'an (61:10-14).

Jambo lingine tunalojifunza kutokana na sura hii ni kuwa Uislamu hautashindwa kusimama katika jamii kutokana na nguvu au uwingi wa maadui zake, bali utashindwa kusimama pale Waislamu watakapokuwa hawajawa tayari kuusimamisha, wakawa wanaridhika kuwa chini ya mifumo ya maisha ya kitwaghuti na kutosheka na kule kutekeleza kwao baadhi ya vipengele vilivyo vyepesi kama vile kuswali, kufunga, kutekeleza baadhi ya sunnah, n.k.

Wakati wa Mtume (s.a.w) Waislamu walianza wakiwa wachache na wanyonge, ambapo maadui zao wakati huo walikuwa wengi na wenye nguvu kisiasa na kiuchumi. Lakini baada ya kuamua kupigania dini ya Allah (s.w) kwa mali zao na nafsi zao, huku wakimtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kumtegemea Mwenyezi Mungu vilivyo, walipata nusura na ushindi na dini ya Allah (s.w) ikawa juu ya dini zote katika kipindi cha miaka 23 tu.

Aya ya mwisho ya sura hii inatufunza kuwa mafanikio yoyote tutakayoyapata tujue kuwa hayatokani na uwezo wetu ila kwa uwezo wa Allah (s.w). Kilicho ndani ya uwezo wetu ni uamuzi wa kutenda mema na kufanya juhudi kadiri atakavyotuwezesha Allah (sw). Matokeo ya jitihada zetu yamo mikononi mwa Allah (s.w). Hivyo tukipata mafaniko yoyote kutokana na juhudi zetu, tushukuru na kumhimidi Allah (sw) kwa kusema

*"Al-Hamdulillah" na ikiwa hatujafanikiwa kama tulivyotarajia pia tumuhimid Allah (s.w) kwa kusema Al-Haamdulillah alaa kulli haali".*

Pia tunajifunza katika aya hii ya mwisho kuwa baada ya kupata ushindi au mafaniko yoyote, tuzidishe kuleta Is-tigh-far, tuombe msamaha kwa Allah, kwa sababu binaadamu si mkamilifu;

huenda katika kupata ushindi au mafanikio fulani, akajivuna na kujisikia kuwa kayapata hayo kwa uwezo wake bila ya msaada wa Allah (s.w).

Pia tunajifunza kuwa muislamu kila wakati ajiandae kuifariki dunia kwa kutopoteza muda katika kutekeleza wajibu wake kama khalifa wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni na kutoakhirisha mambo. Kila linalotekelezeka leo lifanywe lisingoje kesho. Kesho hatuna muamana nayo. Pia kila mara tuwe tunaleta stighfar na kumsabih Allah kwa kumingiza Mtume kwa kuleta dhikiri au dua kwa kila tunachokifanya - Rejea sura ya tano ya juzuu hii.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kutokana na sura hii kwa muhtasari tunajifunza:

- (1) Nusura na mafanikio hutoka kwa Allah (s.w).
- (2) Nusura na mafanikio huja baada ya kufanya juhudi kwa kadiri ya uwezo wa kibinaadamu.
- (3) Pamoja na kufanya juhudi za kibinaadamu katika kutafuta mafaniko au ushindi hatunabudi kumtegemea Allah (s.w) na kuchunga mipaka yake na ya Mtume wake ipasavyo.
- (4) Baada ya kupata mafaniko au ushindi muislamu hanabudi kumsabihi Allah (s.w) kwa wingi, kuzidisha kufanya wema kwa kutoa sadaqa, kufunga, kuswali swala ya kushukuru na kuzidisha kuleta stighfar.
- (5) Kufanikiwa kwa kweli sio kule kwa kuwa na mali nyingi na vitu vingi kwa ajili ya starehe za maisha ya dunia, bali mafanikio kwa mtazamo wa Uislamu ni kusimama kwa Uislamu katika jamii; ambalo ndilo lengo la muislamu anayemfuata Mtume (s.w) na kumfanya kiigizo chake. Lengo la kuletwa Mtume

(s.a.w) na kwa hiyo, lengo la wale wote wanomfuata Mtume (s.a.w) limebainishwa katika Qur'an.

*Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote, ijapokuwa washirikina watachukia" (9:33, 61:9)*

## **ZOEZI 3:14**

1. Hifadhi kifuani Suratun-Nasr na tafsiri yake.
2. Kwa kurejea Historia na Hadith Sahihi oneshwa kuwa kushushwa kwa Suratun-Nasr kuliashiria kukamilika kwa kazi ya Mtume (s.a.w).
3. Ainisha mafunzo makuu matano (5) yatokanayona Suratun-Nasr.

## 16 Suratul-Lahab (111)

Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehema, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1.Pana kuangamia mikono  
miwili ya Abu-lahab! Naye  
ameshakwisha angamia.

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ ①

2.Hayatamfaa mali yake wala  
alivyovichuma.

مَا أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ ②

3.(Atakapokufa) Ataingia moto  
wenye mwako (mkubwa  
kabisa).

سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ③

4.Na mkewe mchukuzi wa  
kuni (za fitina).

وَأْمَرَ أُنثَىٰ وَحَمَلَةَ الْخَطَبِ ④

5.(Kana kwamba) Shingoni  
mwake iko kamba iliyosokotwa  
(anayechukulia kuni za fitina  
hizo).

فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍ ⑤

### Maelezo juu ya Sura

Jina la sura hii linatokana na neno **Lahab** lililomo katika aya ya kwanza. Sura hii ni ya 111 katika msahafu na katika utaratibu wa kushuka ni sura ya 6. Ni sura ya pili kushuka nzima.

Sura hii imeshushwa kama apizo kwa Abu Lahab na mkewe

Ummu - Jamil, kutokana na vitendo vyao vya kuupinga Uislamu na kumpiga vita Mtume (s.a.w). Abu Lahab alikuwa ami yake Mtume (s.a.w) na miongoni mwa machifu wa Makka na tajiri mkubwa. Chuki yake dhidi ya Mtume (s.a.w) ilikuwa kubwa sana kiasi cha kukiuka hata mila ya Waarabu iliyojiri nyakati hizo. Waarabu pamoja na ujahili waliokuwa nao walikuwa na kanuni moja nzuri, ya mtu kuwahurumia na kuwatendea wema watu wa ukoo wake. Kanuni hii ndiyo iliyowafanya Bani Hashim na Bani Muttalib wamtetee Mtume (s.a.w) asiuliwe na Maquraish mpaka ikabidi watengwe pamoja na Waislamu katika bonde la Shi'b Abi Talib. Lakini Abu Lahab bin Abdul-Muttalib peke yake alijitenga na ukoo wake na kusimama na koo nyingine dhidi ya ndugu zake wa Bani Hashim kwa sababu tu wamemtetee Muhammad (s.a.w) mtoto wa ndugu yake, Abdullah bin Abdul-Muttalib.

Katika jamii ya Waarabu nyakati zile, ilitegemewa toka kwa ami kumwangalia na kumsaidia mtoto wa ndugu yake kama awafanyiavyo watoto wake, hasa pale huyo mtoto wa ndugu yake awapo yatima, lakini Abu Lahab alizivunja desturi zote hizo kwa sababu ya uadui wake dhidi ya Uislamu na kuipenda kwake kufuru. Alipofariki Abdullah, mtoto wa pili wa kiume wa Mtume (s.a.w), baada ya kufariki mtoto wa kwanza, Qasim, Abu Lahab badala ya kushiriki katika huzuni za Mtume (s.a.w) ambaye ni mtoto wa ndugu yake, yeye kwa furaha kubwa alikimbilia kwa machifu wa Kiquraish na kuwaarifu kuwa Muhammad amekuwa "Abtar" yaani amekuwa bila mrithi wala ukumbusho wa kuacha nyuma yake. Hayo yote ni kenda na kumi ni pale alipomuapiza Mtume (s.a.w) hadharani pale alipoamrisha na Mola wake autangaze ujumbe wa Uislamu kwa watu wake wa karibu kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Abbas (ra) anasimulia kuwa Mtume (s.a.w) alipoamrisha kulingania uislamu kwa watu wote kwa ujumla, na ile amri ya kuwaonya kwanza jamaa zake wa karibu dhidi ya adhabu ya Allah (sw) ilipotaremka, alipanda juu ya kilima cha Safa mapema asubuhi na akanadi: "Ee*

*Balaa ya asubuhi (ya Sabah)" Arabuni ukelele huu ulipigwa na mtu ambaye ameona jeshi la maadui likitaka kushambulia kabila lake alfajiri. Waliposikia ukelele wa Mtume (s.a.w) watu waliuliza nani aliyekuwa akipiga ukelele huo. Waliambiwa kuwa alikuwa Muhammad (s.a.w). Hapo watu wa koo zote za Quraish walikimbilia alikokuwa Mtume (s.a.w). Yeyote asiyeweza kwenda alituma mtu wa kumwakilisha. Wote walipokusanyika karibu yake, Mtume (s.a.w) aliuita kila ukoo wa Quraish, mmoja baada ya mwingine kwa jina. "Ee Bani Hashim, Ee Bani Abdul-Muttalib, Ee Bani Fihri, Ee Bani fulani (mpaka koo zote zikaisha) ningewaambieni kuwa nyuma ya mlima huu kunajeshi tayari kuwashambulieni, je, mngeniadini? Watu wakajibu kwa sauti moja. "Naam, katu hatujakusikia kusema uongo" kisha Mtume(s.a.w) akaendelea: "Basi nawaonyeni kuwa adhabu kali inawakurubieni." Hapo, kabla ya yeyote kuweza kusema Abu Lahab alipayuka: "Mwana kulaanika! Hivi hayo ndiyo uliyotuitia? Katika Hadith moja kuna ziada kuwa aliokota jiwe kumtupia Mtume (s.a.w) (Musnad Ahmad, Bukhar, Muslim, Tirmidh, Ibn Jarir)*

Amesimulia Ibn Jariri toka kwa Ibn Zaid: "Siku moja Abu Lahab alimuuliza Mtume (s.a.w) "Nikiikubali Dini yako, nitapa nini?" Mtume (s.a.w) alijibu: "Vyote ambavyo Waislamu watapata." Akaendelea kuuliza: "Hamna neema makhusus kwa ajili yangu? Mtume (s.a.w) akamuuliza: "Nini kingine ukitakacho" Hapo akayoyoma" Ilaaniwe dini ambayo ndani yake mimi nitasawazishwa na watu hawa."

Baada ya Abu Lahab kufikia hatua hii ya kumuapiza Mtume na kuulani Uislamu, Allah (sw) alimshushia Mtume (s.a.w) sura hii ili kumliwaza Mtume (s.a.w) na Waslamu kuwa watashinda na Abu Lahab ndiye atakayeangamia.

Miaka minane hivi baada ya kushuka sura hii Waislamu



walipata ushindi mkubwa katika vita vya Badr ambapo machifu wote wa maquraish waliokuwa vitani waliuliwa. Abu Lahab hakwenda vitani lakini baada tu ya vita vya Badr alipata maradhi mabaya ambapo mwili wake ulikuwa ukioza na watu wanyumbani kwake wakamkimbia. Alipokufa watu walimzika kwa kumsukumiza kwa miti; kumtupia mawe, miti na mchanga ili kumfukia wakiwa mbali, kukimbia harufu ya uozo na kuambukizwa ugonjwa.

Mkewe, Ummu jamil, naye pia alikuwa katika watu waliomchukia sana Mtume (s.a.w) na Uislamu. Alikuwa akifanya visa vingi vya kuudhi na kutaka kumdhuru Mtume (s.a.w). Alikuwa akiwashinikiza makafiri wamuue Mtume (s.a.w). Kutajwa kwake kama mchukuzi wa kuni kuna tafsiri mbili:

**Kwanza**, ni kuwa alikuwa akichukua maneno ya huku na kule kuwafitinisha watu ili wauchukie Uislamu. Mtu wa namna hii Waarabu humshabihisha na "mchukuzi wa kuni"

**Pili**, yapo pia maelezo kuwa mkewe Abu Lahab alikuwa akiweka miba na takataka katika njia aliyoibaini kuwa ataipitia Mtume (s.a.w) ili kumuudhi.

Sura hii inamuapiza Abu Lahab; kuwa ataangamia na wala mali yake na vile alivyovichuma havitamfaa. Na kweli Abu Lahab aliangamia kweli, alikufa bila kusilimu na kifo chake kikawa kibaya.

Pamoja na chuki aliyokuwa nayo dhidi ya Mtume (s.a.w) Abu Lahab hakuweza kumshushua Mtume (s.a.w) japo kusilimu kiuongo, ili Mtume (s.a.w) aonekane muongo na Qur'an yake. Bali aling'ang'ania ukafiri wake mpaka akafa kwa udhalili na watoto wake hawakumfaa wala mali yake.

## **Mafunzo**

Kutokana na sura hii tunajifunza kuwa kila zama kuna Abu

Lahab wake.

Yeyote yule anayeuchukia Uislamu na kufanya jitihada ya kuuzuia Uislamu usisimame kwa kuwakandia viongozi wake na kuwafitinisha Waislamu atakuwa amechukua nafasi ya Abu Lahab na mkewe, Ummu Jamil.

Kwa upande mwingine tunajifunza kuwa Waislamu daima wasitetemeshwe na vitimbi na hila za akina Abu Lahab bali waendeleo kushikilia uzi wa kusimamisha Uislamu, kwani si muda mrefu watapata ushindi dhidi ya maadui zao.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kutokana na sura hii kwa muhtasari tunajifunza yafuatayo:

- (1) Mwenye kuuchukia Uislamu na kuupiga vita usisimame kwa jeuri na kibri, ajue kuwa mwisho wake utakuwa mbaya. Historia ni shahidi juu ya hili.
- (2) Mali, watoto na vyote alivyovichuma binaadamu havisadii kitu ijapo adhabu ya Allah (sw)
- (3) Kuchochea fitna na uasi ni makosa makubwa yenye kuangamiza.
- (4) Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya wale wanaokanusha Uislamu na kuupiga vita kwa kibri na jeuri.

### **ZOEZI 3:15**

1. Hifadhi kifuni Suratul-Lahab na tafsiri yake.
2. Suratul-Lahab ilishushwa ili kumliwaza Mtume (s.a.w) na Waislamu. Kwa kurejea historia, eleza mazingira yaliyojiri dhidi ya Mtume (s.a.w) yaliyopelekea kushushwa kwa sura hii.

3. Ainisha mafunzo makuu yatokanayo na Surat-ul-Lahab.

## 17. Surat-ul-Khlas (112)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Sema, Yeye ni Allah moja (tu).

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ①

2. Allah tu ndiye anayestahiki  
kukusudiwa.

اللَّهُ الصَّمَدُ ②

3. Hakuzaa wala Hakuzaliwa.

لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ③

4. Wala hana anayefafanana  
naye hata mmoja.

وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ ④

### Maelezo juu ya Sura

**Al-Ikhlās** si jina tu la sura hii, bali pia ni kichwa cha habari cha mafundisho yake kwani Tawhiid imefafanuliwa vizuri ndani yake. Sura nyingine za Qur'an kwa ujumla zinapata majina yake kutokana na neno lipatikanalo ndani ya sura husika, lakini sura hii imepata jina lake kutokana na maudhui ya sura yenyewe.

Suratul Ikhlas ni sura ya 112 katika msahafu na ni sura ya 22 kushuka. Kulingana na maudhui ya sura hii inaonesha iliteremshwa katika kipindi cha mwanzo kabisa cha utume huko Makka, wakati ambapo aya zenye maelezo ya kutosha kuhusu sifa za Allah (sw) zilikuwa bado kuteremshwa, na watu baada ya kusikia da'awah ya Mtume (s.a.w) ya kuwalingania watu kumuabudu Mungu Mmoja aliye mpweke - Allah (sw), walitaka kujua sifa za huyo Allah. Haya yanathibitishwa na ukweli kwamba

pale Bilal (r.a) alipokuwa akiteswa katika jua kali baada ya kukandamizwa kifuni mwake na jiwe zito kwenye mchanga wa moto, yeye daima na kwa mfululizo alikuwa akisema: "Ahad", "Ahad" (Mmoja, Mmoja) Neno hili alilipata katika sura hii. Zifuatazo ni baadhi ya Hadithi kuhusu kushuka kwa sura hii:

1. *Abdullah bin Mas'us (r.a) amesema: "Maquraish walimuuliza Mtume (s.a.w) kuwa vipi ilikuwa nasaba au ukoo wa Mungu wake (Allah). Hapo sura hii iliteremshwa" (Tabarani)*
2. *Jabir bin 'Abdullah (r.a) amesema: Bedui mmoja alimuuliza Mtume (s.a.w) kuhusu nasaba na jadi ya Mungu wake. Hapo Allah(s.w) akaiteremsha sura hii (Abu Ya'la, Ibn Jarir, Ibn al-Mundhir, Tabarani, Baihaq, Abu Nu'aim)*
3. *Ikramah amesimulia toka kwa Ibn 'Abbas (r.a) "Kundi la Mayahudi ambamo Ka'b bin Ashraf na Huyayy bin Akhtab na Wayahudi wengine mashuhuri pia walikuwemo, lilimwendea Mtume (s.a.w) na kumuuliza: Ewe Muhammad, tuambie ni Mungu wa aina gani aliyekutuma? Hapo sura hii ikateremshwa" (Ibn Abi Hatim, Ibn Addiyy, Baihaqi)*
4. *Anas bin Malik (r.a) amesema: "Baadhi ya Wayahud wa Khaiybar walikuja kwa Mtume (s.a.w) na kumuuliza: Ewe Abdul Qasim, Allah amewaumba malaika kutokana na nuru iliyojificha, Adam kutokana na udongo uliooza, Iblis kutokana na ulimi wa moto, mbingu kutokana na moshi, ardhi kutokana na mapovu ya maji yanayochemka. Sasa tuambie kuhusu Mungu wako (ametengenezwa na nini?) Mtume (s.a.w) hakujibu. Kisha Jibril (as) alikuja na kumwambia Mtume (a.a.w) asome: "Qul Huwallahu Ahad ..... " (tafsiri ya Ibn Taimiyyah)*

5. *Amesimulia Ibn Abbas (r.a) "Ujumbe wa kikiristo toka Najran ulikuja kwa Mtume (s.a.w) na ukamuuliza: Tuambie Mungu wako ni wa aina gani, na ametengenezwa kwa kitu gani? Mtume (s.a.w) akajibu Mungu wangu hakutengenezwa kwa chochote. Yeye ni tofauti na hahusiani na kitu chochote. Hapo Allah (sw) akaiteremsha sura hii. (Tafsiri ya Ibn Taimiyyah)*

Kutokana na Hadith hizi chache, tunajifunza kuwa katika matukio tofauti watu walimuuliza Mtume (s.a.w) kuhusu asili ya Allah (s.w) ambaye yeye Mtume(s.a.w) alikuwa akiwalingania wamuabudu. Katika Hadith hizo, yale maneno kuwa sura hii iliteremshwa katika tukio hilo, yasilite kueleweka vibaya kuwa Hadithi hizi zinapingana. Ukweli ni kuwa inapokuwa aya au sura fulani ya Qur'an kuhusu swali au tatizo fulani tayari imeshateremshwa, basi baadaye kila litokeapo swali au tatizo hilo hilo, maelekezo yalikuja kwa Mtume (s.a.w) toka kwa Allah (s.w) kuwa jibu lipo katika aya au sura fulani, au soma aya au sura fulani.

## **Mafunzo**

Mtume (s.a.w) kuulizwa juu ya nasaba au asili ya Allah na Waarabu, Wayahud na Wakristo, inaashiria kina cha ushirikina uliokuwemo katika kipindi hicho cha jahiliya. Waarabu waliabudu masanamu ya kike na ya kiume yaliyotengenezwa na mbao, mawe, fedha, dhahabu n.k Wamajusi (Waajemi) waliabudu moto, Wasabai waliabudu nyota, Wayahudi pamoja na kudai kwao kuwa walimuamini Mungu mmoja, walimfanya "Uzair" mwana wa Allah(s.w) na Wakirsto nao walimfanya Isa bin Mariyam kuwa mtoto wa Allah(s.w) na mama yake kuwa mama wa Mungu.

Sura hii imeweka wazi kuwa Mungu wa Waislamu,

Wanayemuamini na kumuabudu kwa unyenyekevu katika kila kipengele cha maisha yao, ni Allah aliye mmoja tu na mpweke, anayetegemewa na viumbe vyote kwa kila jambo, asiye na mwanzo (asili), asiye na nasaba na asiyeshabihiana na chochote.

Mtume (s.a.w) alikuwa akionesha sana umuhimu wa sura hii kwa Waislamu kwa njia tofauti ili waisome mara kwa mara, wautangaze ujumbe uliomo ndani yake kwa watu. Kwani sura hii inauelezea msingi wa kwanza wa Uislamu (Tawhiid) katika aya nne fupi ambazo ni rahisi kuzihifadhi na kuzisoma. Katika hadithi za Mtume (s.a.w) ameilinganisha suratul-Ikhlās na Thuluth moja ya Qur'an, katika Hadith zilizonukuliwa katika Tirmidh Bukhar, Muslim, Abu Daud, Nisai, Tirmidh, Ibn Majah, Musnad Ahmad, Tabarani n.k Hadithi nyingi kuhusu jambo hili zimesimuliwa na Abu Sai'a Al-Khuadri, Abu Hurairah, Jabiri bin 'Abdullah, Ubayy bin Ka'b, Ibn 'Umar 'Abdullah bin Mas'ud, Qatadal, Anas bin Malik na Ibn Mas'ud (r.a).

Wafasiri wametoa maelezo mengi kuhusu usemi na msisitizo huu wa Mtume (s.a.w), lakini kwetu sisi maelezo yaliyowazi zaidi ni kwamba njia ya maisha (dini) iliyofundishwa na Qur'an imeasisiwa juu ya misingi mitatu ya imani. Kwanza Tawhiid, (Umoja na upweke wa Allah), pili Risalah (Utume) na tatu Akhera (maisha baada ya kufa). Kwa vile sura hii inafafanua Tawhiid Khalis, hiyo ndiyo maana Mtume (s.a.w) amesema sura hii tu peke yake ni sawa na thuluthi ya Qur'an yote.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kutokana na suratul-Ikhlās tunajifunza kwa muhtasari yafuatayo:

1. Jina la dhati la Mungu Mmoja na ni Allah (sw).

2. Allah (sw) ndiye muumba wa kila kitu, hivyo ndiye pekee anayestahiki kukusudiwa kwa kuombwa, kuabudiwa na kutegemewa na kila kitu. Ni utovu wa shukrani na wizi wa fadhila kwa binaadamu kukusudia Miungu wasio umbwa na kumpuuza yule aliyemuumba.
3. Allah (sw) hana nasaba wala asili, alikuwepo na atakuwepo milele, yaani Allah hana mwanzo wala mwisho. Kwa muhtasari miongoni mwa sifa za Allah zinazoambatana na aya ya 3 ya sura hii ni hizi zifuatazo:
  - ⦿ Al- Badiu - Asili au mwanzilishi wa kila kitu
  - ⦿ Al- Awwalu - Wa mwanzo
  - ⦿ Al-Aakhir - Wa mwisho
  - ⦿ Al-Hayyu - Mwenye uhai wa milele
  - ⦿ Al-Baaqy - Mwenye kubakia milele
4. Allah (sw) hashabihiani na chochote kwa namna yoyote ile, yaani yeye ni mpweke asiyefanana na chochote kwa hali yoyote ile.

### **ZOEZI 3:16**

1. Hifadhi kifuani Suratul-Ikhlās na tafsiri yake.
2. Toa mafunzo makuu manne (4) yatokanayo na Suratul-Ikhlās.
3. Katika Hadith kadhaa Mtume (s.a.w) ameilinganisha Suratul-Ikhlās na theluthi moja ya Qur-an. Ninimantiki yake?

## 18. Suratul-Falaq (113)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehema, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Sema Najikinga kwa Mola wa  
Ulimwengu wote.

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْقَلْقِ ۝١

2. Na shari ya alivyoviumba.

مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ۝٢

3. Na shari ya giza la usiku  
liingiapo.

وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ۝٣

4. Na shari ya wale wanaopi  
mafundoni.

وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ ۝٤

5. Na shari ya hasidi  
anapohusudu.

وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ۝٥

### Maelezo ju ya Sura

Jina la sura hii linatokana na neno **al-falaq** lililomo katika aya yake ya kwanza. Sura hii ni ya 113 katika msahafu na ni ya 20 katika mfululizo wa kushuka. Sura hii imeshuka kwa mfululizo mmoja na sura inayofuatia, Suratun - Nas, (sura ya 21 kushuka) na maudhui ya sura hizi mbili yake ni mamoya ya kujikinga kwa Allah (sw) na shari mbalimbali kama zinavyoainishwa katika aya hizo. Hivyo sura hizi zimepewa jina moja la jumla, **Al-Mu'awwidhatain** yaani sura mbili za kujilinda kwa Allah.



Ili kupata vizuri mafunzo ya sura hizi mbili, Al-falaq na An-Naas ni vyema turejee historia ya Mtume (s.a.w) katika mwanzo wa kazi yake ya kuulingania Uislamu Makka.

Mazingira ambamo sura mbili hizi ziliteremshwa huko Makka yalikuwa magumu kwa Mtume (s.a.w). Mtume (s.a.w) alipoanza kulingania Tawhiid (umoja na upweke wa Allah), alioenekana wazi kuwa amejiingiza katika hatari kubwa. Kadri wito wa Tawhiid ulivyozidi kusambaa uadui wa makafiri wa Kiquraish uliendelea kuzidi ila maadamu walikuwa na matumaini kuwa labda kwa kufanya maafikiano na Mtume (s.a.w) kwa kumbembeleza na kumrairai huenda wakafaulu kumwachisha kazi yake ya kulingania Uislamu, uadui wao ulibakia katika kiwango cha chini; lakini pale Mtume (s.a.w) alipowakatisha tamaa kabisa ya kuwafikiana nao katika jambo la dini kwa kuwasomea suratul - kaafiruun, uadui wa makafiri ulishtad na kufikia kielele chake. Khususan zile familia ambazo watu wake (wanaume, wanawake na watoto) walisimu, dumu daima familia hizo zilikuwa dhidi ya Mtume (s.a.w). Takriban katika nyumba zote, Mtume (s.a.w) alikuwa akitukanwa. Mikutano ya siri ilifanyika ili kupika njama ya kumuua Mtume (s.a.w), ili Bani Hashim, ukoo wake Mtume (s.a.w) usimjue muuaji na hivyo ushindwe kufanya kisasi. Uchawi ulitumika dhidi yake ili kumuua au kumfanya awe mgonjwa sana au kichaa. Mashetani ya kijini na kiinsi yalisambaa kueneza wasiwasi, urongo na mashaka dhidi ya Mtume (s.a.w), dini yenyewe ya kiislamu pamoja na Qur'an katika nyoyo za watu ili wamwepuke Mtume (s.a.w) na wawe dhidi yake.

Watu wengi nyoyo zao ziliunguzwa na moto wa hasadi kwani wasingeweza kuvumilia kutukuka kwa yoyote mwingine isipokuwa tu wao wenyewe au watu wa makabila yao. Kwa mfano, sababu iliyomfanya Abu Jahal apindukie mipaka ya uadui dhidi ya Mtume (s.a.w) imeelezwa naye mwenyewe."Ilikuwa mashindano kati yetu na 'Abdul Manaf, yaani ukoo wa Mtume (s.a.w). Walifanyia watu karamu na kuwashibisha nasi tukafanya. Waliwapatia watu

wanyama wa kupanda nasi tukafanya. Walitoa zawadi nasi tukatoa. Baada ya kuwa sawa nao kwa hadhi na heshima, sasa wanadai kuwa miongoni mwao wana Mtume ambaye anateremshiwa wahyi toka mbinguni. Angalieni, vipi tutaweza kushindana nao katika jambo hili? Wallah, katu hatuamwamini wala kuushuhudia ukweli wake" (Ibn Hisham, Juzuu 1 kur. 337-338)

Katika mazingira hayo, Mtume (s.a.w) aliambiwa awaambie watu hao kuwa yeye anajilinda kwa Mola wa mapambazuko kutokana na shari ya vyote Alivyoviumba, shari ya giza la usiku, shari ya wachawi na shari ya watu walioghilibiwa na hasadi na wivu, na kwamba alikuwa anajilinda kwa Mola wa watu, mfalme wa watu, Mungu wa watu kutokana na shari ya mwenye kutia wasiwasi mwenye kurejea nyuma, awe miongoni mwa majini au binaadamu. Usemi (du'a) huu wa Mtume (s.a.w) mbele ya wakuu wa Makafiri wa Makka unashabihiana na ule usemi wa Nabii Musa (as), pale Firauni, mbele ya mawaziri wake alipodhihirisha dhamira yake ya kumuua:

وَقَالَ مُوسَىٰ إِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ مِّنْ كُلِّ مُتَكَبِّرٍ لَا يُؤْمِنُ بِيَوْمِ

الْحِسَابِ ﴿٢٧﴾

*“Na Musa akasema: "Mimi najikinga kwa Mola wangu na Mola wenu Anilinde na kila mwenye jeuri, asiye amini siku ya Hisabu" (40:27).*

وَإِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ أَنْ تَرَجُمُونِ ﴿٢٠﴾

*“Nami najikinga kwa Mola wangu na (ndiye) Mola wenu (pia) ili msinipige mawe" (44:20).*

Katika matukio yote mawili ya mapambano ya hawa mitume wa Allah (s.w), nao wakiwa na nguvu dhaifu kabisa, mapambano yao yalikuwa dhidi ya watu wenye uwezo mkubwa wa kimali na kijeshi. Katika matukio yote mawili, mitume hao walisimama imara dhidi ya maadui zao wenye nguvu kubwa, japo wao hawakuwa na

nyenzo za kimada za kupigana nao; na katika matukio yote mawili, waliyadharau na kutoyajali matisho, njama hatari na uadui mkuu wa wapinzani wao kwa kusema kuwa walijilinda kwa Mola wa ulimwengu dhidi yao. Ni dhahiri kuwa uithibati na uimara huo unaweza tu kuoneshwa na yule mtu ambaye kwa yakini anaamini kuwa nguvu za Mola wake ndizo kubwa kuliko zote, na nguvu za viumbe zikifananishwa na nguvu za Allah(s.w), si chochote si lolote. Hamna awezaye kumdhuru alindwaye na Allah. Hivyo ni mtu aliyejilinda kwa Allah(s.w) tu ndiye awezaye kusema kuwa hajali chochote duniani, kitakachotaribu kumzuia asilinganie Haki.

### **Mafunzo**

Sura hii inatufundisha tuombe ulinzi wa Mwenyezi Mungu (sw), dhidi ya shari ya vitu vinne:

**Kwanza**, shari ya vitu mbalimbali Alivyoviumba akavipa nafasi na uwezo tofauti. Mwanadamu kuna vitu avijuavyo na vingine vingi asivyovijua. Miongoni mwa hivyo vipo vyenye kheri na yeye na vipo vyenye shari na yeye. Lakini vyote hudhibitiwa na Allah (s.w). Hivyo ni Allah (s.w) pekee anayeweza kutoa ulinzi dhidi ya shari ya viumbe hivyo.

**Pili**, kuna shari ya giza la usiku liingiapo. Giza la usiku linafuatana na vitu na mambo mengi ambayo binaadamu pekee hana namna ya kujikinga nayo yakimtokea. Mashetani, wezi, wanyama wabaya, n.k hutumia kiza kama blanketi la kufichia uovu na unyama wao. Kwa Allah (s.w) kinadhihirika kila kitu hatakiwa ndani ya giza totoro ndani ya kitu cheusi tii. Hivyo ni Allah (s.w) pekee mwenye uwezo wa kumkinga mja wake dhidi ya shari za giza la usiku.

سَوَاءٌ مِّنْكُمْ مَّنْ أَسْرَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ

وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ ﴿١٦﴾

*"Ni sawa (kwake Mwenyezi Mungu) anayeficha kauli yake miongoni mwenu na anayeidhirisha; na (pia) ajifichaye usiku na aendaye mchana. (Wote Awajua)" (13:10)*

**Tatu**, shari ya uchawi, uchawi upo na umeharamishwa katika Uislamu - Rejea Qur'an (2:102). Uchawi ni aina ya kiini macho ambacho hufanywa na mtu mwenye elimu hiyo kiasi cha kuyazuga macho ya wale wasio na elimu hiyo. Hayo yalimkuta Nabii Musa (as) kama tunavyosoma katika Qur'an:

قَالُوا يَمْوَسَىٰٓ اٰمَّآ اَنْ تُلْقَىٰ وَاٰمَّآ اَنْ نَّكُوْنَ  
 اَوَّلَ مَنْ اَلْقَىٰ ﴿١٥﴾

*"Wakasema: Ewe Musa! Je! Utatupa wewe (kwanza uchawi wako) au tutakuwa sisi wa kwanza kutupa?(20:65)*

قَالَ بَلْ اَلْقَوْا فَاِذَا حَبَالُهُمْ وَعَصِيَّتُهُمْ يَخِيْلُ اِلَيْهِ مِنْ  
 سِحْرِهِمْ اَنَّهُمْ تَسْعَىٰ ﴿١٦﴾ فَاَوْجَسَ فِي نَفْسِهِ خِيفَةً مُّوسَىٰ ﴿١٧﴾

*(Musa) akasema: Bali tupeni (nyinyi kwanza)! Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake (musa) kwa uchawi wao, inakwenda mbio mbio. Basi Musa akatia khofu katika nafsi yake. (20:66-67)*

قُلْنَا لَا تَخَفْ اِنَّكَ اَنْتَ الْاَعْلَىٰ ﴿١٨﴾ وَاَلْقَىٰ مَا فِي يَمِيْنِكَ تَلْقَفْ مَا  
 صَنَعُوْٓا اِنَّهُمْ صَنَعُوْٓا كَيْدُ سَحِرٍ وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ اَتَىٰ

*Tukasema: 'Usiogope! Hakika wewe ndiye utakayekuwa mwenye kushinda. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kuume; kitavimeza walivyovitengeneza. Hakika wao wametengeneza hila za mchawi tu, wala mchawi hafaulu popote afikapo" (20:68-69).*

Hivyo ndivyo ulivyo uchawi. Uchawi huweza kuathiri akili ya mtu na kumfanya afikiri na kutenda atakavyo yule mchawi. Uovu wa aina hii hapana shaka unahitaji ulinzi wa Allah (s.w).

**Nne**, shari ya hasidi anapohusudu. Husuda ni uovu ambao huja baada ya mtu mmoja kuona kwanini mwenziwe ametunukiwa neema fulani na Mola wake. Hasidi hutamani au kufanya jambo ili neema aliyotunukiwa mtu iondoke ijapokuwa asiipate yeye. Katika Hadith iliyosimuliwa na Abu Hurairah, Mtume (s.a.w) amehadharisha juu ya husuda kwa kusema:

*"Jihadharini sana na husuda kwani hasuda hula mema ya mtu kama moto unavyokula kuni" (Abu Daud)*

Kwa kuhitimisha mafunzo ya sura hii, hatunabudi Waislamu kufahamu vyema kuwa anayelinda au kuelekewa kwa ulinzi ni Allah (s.w) na siyo hii sura au Qur'an. Kuna baadhi ya Waislamu wanafanya kinyume kwa kuziandika sura hizi na kuzibandika ukutani au kuzining'iniza mlangoni au garini au kuzivaa kama hirizi. Kufanya hivyo ni shirki.

Mtume (s.a.w) amesema kuwa mwenye kutundika hirizi amemshirikisha mwenyezi Mungu. Hivyo Qur'an kama ilivyo siyo mlinzi wako, bali anayelinda ni Mwenyezi Mungu. Qur'an ni mwongozo wa kutuelekeza namna ya kuendea kila kipengele cha maisha yetu, ikiwa ni pamoja na hiki cha kujikinga kwa Allah kutokana na shari mbalimbali.

## **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kutokana na sura hii tunajifunza kwa muhtasari yafuatayo:

- (1) Binaadamu ni sehemu ndogo ya maumbile ya Mwenyezi Mungu na katika maumbile hayo kuma mengi yenye shari

kwa binaadamu. Katika hali kama hiyo binaadamu siku zote awe ni mwenye kutaka ulinzi wa Mwenyezi Mungu ambaye ndiye muumba na mmiliki wa viumbe vyote.

- (2) Ili tuweze kujikinga kwa Allah (s.w) pekee ni lazima tuwe na yakini juu ya kuwepo kwake na juu ya uwezo wake juu ya kila kitu.
- (3) Waislamu wa kweli hawatamchelea yeyote katika kusimamisha haki katika jamii, bali watatawakali kwa Allah (s.w) na kumuomba awakingie shari za makafiri. Allah (s.w) anasisitiza katika Qur'an:

..... الْيَوْمَ يَبْسُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنَ .....  
.....

*“.... Leo waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu basi msiwaogope bali niogopeni mimi .....” (5:3)*

- (4) Kila wakati tusome kwa mazingatio hizi sura za kinga kama alivyokuwa akifanya Mtume (s.a.w) - Rejea sura ya tano ya juzuu hii.

## 19. Suratun-Naas (114)

Kwa jina la Allah, Mwingi wa  
Rehma, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1.Sema, Najikinga kwa  
Bwana mlezi wa watu.

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿١﴾

2.Mfalme wa watu.

مَلِكِ النَّاسِ ﴿٢﴾

3.Muabudiwa wa Watu.

إِلَهِ النَّاسِ ﴿٣﴾

4.Na shari ya mwenye kutia  
wasiwasi,mwenye kurejea  
nyuma.

مِن شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ﴿٤﴾

5.Atiaye wasiwasi nyoyoni  
mwa Watu.

الَّذِي يُوسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ ﴿٥﴾

6.(Ambaye) ni katika majini  
na watu.

مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ﴿٦﴾

### Maelezo juu ya Sura

Jina la sura hii linatokana na neno **An-naas** lililomo katika aya yake ya kwanza. Ni sura ya mwisho katika msahafu, sura ya 114. Pia ni sura ya 21 kushuka. Sura hii ilishuka pamoja na suratul-Falaq na zote kwa pamoja zinajumuishwa na jina moja la **Al-Mu'awwidhatain**, yaani sura mbili za kujilinda kwa Allah (sw). Maelezo juu ya sura hizi mbili tumeshapata kwa urefu katika maelezo ya suratul-Falaq yaliyotangulia.

## Mafunzo

Pamoja na kujikinga kwa Allah (sw) na zile shari nne katika suratul-Falaq, shari ya vyote alivyoviumba, shari ya giza la usiku liingiapo, shari ya wachawi na shari ya mahasidi, katika aya hii tunatakiwa kujikinga kwa Allah (sw) na shari ya wasiwasi wa shetani.

Kabla ya kuomba kinga hii tunakumbushwa uwezo wa huyo tunayemuomba atukinge na shari hiyo kuwa yeye Allah (sw) ni Bwana mlezi wa watu, Mfalme wa watu na Mola wa watu. Kwa sifa hizi, Allah (sw) ndiye pekee mwenye uwezo wa kumlinda binaadamu.

Kwa upande mwingine shetani ametajwa katika sura hii kuwa ni mwenye shari ya kutia wasiwasi katika nyoyo za watu. Shetani huweza kumtia mtu wasiwasi mpaka akatilia shaka uwezo wa Allah (sw) katika kutoa rizk, kulea, kulinda, kuhuisha n.k na huweza kumshawishi mtu na kumhadaa mpaka akatoka nje kabisa ya njia sahihi ya maisha ya Uislamu. Kwa ajili hiyo shetani kwa binaadamu ni adui mkubwa.

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ  
أَصْحَابِ السَّعِيرِ ①

*Kwa yakini shetani ni adui yenu; basi mfanyeni adui (yenu hivyo msimtii), kwani analiita kundi lake liwe katika watu wa motoni." (35:6)*

Katika sura hii shetani ametajwa kuwa ni katika majini na watu. Shetani hamjii mtu katika sura ya kumpotosha na njia ya haki, bali humjia kwa kumshawishi; kumlaghai, na kumhadaa kuwa anamuelekeza kwenye njia nzuri yenye manufaa, kama Allah (s.w) anavyodhihirisha.



وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيْطِينَ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ  
إِلَى بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا .....

*“Na namna hii tunamfanyia kila Nabii maadui, (hao ni) mashetani katika watu na majini. Baadhi yao wanawafunulia wenzi wao maneno ya kupamba-pamba ili kuwadanganya ....” (6:112).*

Ni kwa namna hii ya tashawishi, Iblis (jinni) aliwatelezesha wazee wetu, Adamu (a.s) na Hawwa, wakala lile tunda walielokatazwa:

فَوَسَّوَسَ لَهُمَا الشَّيْطَانُ لِيُبْدِيَ لَهُمَا مَا وُورِيَ عَنْهُمَا مِنْ سَوْآتِهِمَا  
وَقَالَ مَا نَهَاكُمَا رَبُّكُمَا عَنْ هَذِهِ الشَّجَرَةِ إِلَّا أَنْ تَكُونَا مَلَكَيْنِ  
أَوْ تَكُونَا مِنَ الْخَالِدِينَ ﴿٢٠﴾

*“Basi shetani, naye ni yule (iblis) aliwatia wasiwasi ili kuwadhihirishia aibu zao walizofichiwa, akasema: Mola wenu hakukukatazeni mti huu ila (kwa sababu hii) msije kuwa malaika au kuwa miongoni mwa wakaao milele (msife). (7:-20)*

وَقَاسَمَهُمَا إِنِّي لَكُمَا لَمِنَ النَّاصِحِينَ ﴿٢١﴾

*Naye akawaapia (kuwaambia) kwa yakini mimi ni mmoja wa watoa shauri njema kwenu ” (7:-21)*

Shetani hashughulishwi na mtu ambaye ameshaamua kumuasi Mwenyezi Mungu (s.w) bali yeye hushughulishwa zaidi na waliomo misikitini, wafanyao kazi za halali, wanaokaa na kupanga vipi wataisimamisha dini ya Allah (s.w) n.k. Hata hivyo mashetani huendelea kuwazuia wale waliokwisha zama kwenye maasi

wasitoke humo na wakati huo huo wakiendelea kupotosha watu wema.

Ni nadra shetani wa kijini kujitokeza kwa umbo bali hufanya tashawish za hisia tu. Tukipata tetesi za kuingiwa na wasiwasi wa kishetani tunamuelekea Mola wetu na kujikinga kwake kwa kusoma sura hii, pia tunaweza kuleta dua ifuatayo:

..... رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ هَمَزَاتِ الشَّيْطَانِ ﴿٣٧﴾

وَأَعُوذُ بِكَ رَبِّ أَنْ يَحْضُرُونِ ﴿٣٨﴾ .....

*"... Mola wangu! Najikinga kwako na wasiwasi wa shetani, na najikinga kwako, Mola wangu ili wasinihudhuri" (23:97-98)*

Kwa ujumla shetani awe binaadamu au jinni si wengi wanaoweza kumng'amua kwani ni mwenye kurejea nyuma, yaani mwenye kuja kwa uficho wa kitashawish. Jambo la msingi tunalotakiwa tulifahamu, ni kwamba pale ambapo hapana mwongozo wa Allah (s.w) pana mwongozo wa shetani; na pale ambapo hatajwi Allah (s.w) anatajwa shetani. Pale penye mambo ya upuuzi (lagh-wi) shetani huwa mgeni rasmi.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kutokana na sura hii tunajifunza kwa muhtasari yafuatayo:

- (1) Shetani hana uwezo wa kutumia nguvu na kuitenza nafsi ya mtu kumuasi Mwenyezi Mungu (s.w), bali yeye hutumia tashwishi tu na kutia wasisi nyoyoni.
- (2) Tunapojiwa na wasiwasi wowote katika nafsi zetu unaotaka kutupelekea kumuasi Allah (s.w), tuombe msaada wa kinga toka wa Allah (s.w) na tujiepushe na maasi hayo.
- (3) Shetani ni adui yetu mkuu, lakini ni dhaifu iwapo tuta mcha-Allah (s.w) ipasavyo, na kuomba ulinzi wa Allah dhidi ya

shetani. Shetani (Iblis) alipochukua azma ya kuwapotosha binaadamu alikiri na Allah (s.w) akathibitisha hivyo kuwa hataweza kuwapotosha wacha-Mungu:

قَالَ رَبِّ بِمَا أَغْوَيْتَنِي لَأُزَيِّتَنَّ لَهُمُ فِي الْأَرْضِ  
وَلَأُغْوِيَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٣٩﴾ إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِينَ ﴿٤٠﴾

“Akasema (Iblis): Mola Wangu! Kwa sababu umenihukumu kupotea basi nitawapambia (waja wako upotofu) katika ardhi na nitawapoteza wote. Isipokuwa wale waja wako waliosafika kweli kweli. (15:39-40).

قَالَ هَذَا صِرَاطٌ عَلَيَّ مُسْتَقِيمٌ ﴿٤١﴾ إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ  
إِلَّا مَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغَاوِينَ ﴿٤٢﴾

(Mwenyezi Mungu) akasema: "Hii njia yao ya (kuja) kwangu imenyooka. Hakika waja wangu, wewe hutakuwa na mamlaka juu yao, isipokuwa wale wenye kukufuata (kwa hiari zao) katika hao wapotofu" (15:41-42).

- (4) Wasaidizi wa shetani ni wengi na mara zote huwakilishwa na majini na binaadamu waovu.

## ZOEZI 3:17

1. Hifadhi Suratul-Falaq na An-Naas pamoja na tafsiri za sura hizi.
2. Kwa nini Suratul-Falaq na An-Naas kwa pamoja zimepewa jina la "Al-Mu'awwidhatin" ?
3. Ainisha mafunzo yatokanayo na Suratul-Falaq.
4. Toa mafunzo yatokanayo na Suratun-Naas.

## Sura ya Nne

# SUNNAH NA HADITH

### Maana ya Sunnah

**Kilugha:** Neno sunnah katika lugha ya Kiarabu lina maana ya mwenendo au mila. Hivyo ukisema "**Sunnat Muhammad (s.a.w)**" ina maana ya **mwenendo** au tabia au **mila** aliyokuwa akiifuata Mtume Muhammad (s.a.w) katika maisha yake ya kila siku. Na ikisemwa, "**Sunnatullah**" kama ilivyotumika katika Qur-an, ina maana ya desturi au kawaida au mila ya Allah (s.w) katika kufanya mambo ya Uungu wake kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

سُنَّةَ اللَّهِ فِي الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلُ وَلَنْ تَجِدَ لِسُنَّةِ اللَّهِ تَبْدِيلًا

*"Hii ni kawaida (sunnah) ya Allah (ya kuwaadhibu wakorofi) iliyokuwa kwa waliopita zamani, hutapata mabadiliko katika kawaida (sunnah) ya Allah." (33:62)*

**Kisheria**, sunnah ni mwenendo au matendo ya Mtume (s.a.w) ambayo ni sehemu ya Utume wake. Waislamu wanalazimika kuyaiga na kuyafuata katika uendeshaji wa maisha yao ya kila siku ili kupata radhi za Allah (s.w). Mwenendo wa Mtume (s.a.w) haukutokana na matashi yake bali ulikuwa ni wahyi kutoka kwa Allah (s.w) kama inavyohibitika katika Qur-an:

وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ۗ إِن هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ۗ

*"Na hazunguzi (Muhammad) kwa matamania ya nafsi yake. Isipokuwa (anayozungumza ni) wahyi uliofunuliwa kwake." (53:3-4)*

**Kiutendaji**, sunnah ya Mtume (s.a.w) ni yale matendo ya msingi aliyoyafanya, aliyoyaagiza na yaliyofanywa mbele yake asiyakemee au kuyakataza.

### **Maana ya Hadith**

**Kilugha:** maana ya Hadith katika lugha ya Kiarabu ni **jambo jipya au kitu kipya**", **hutuba, taarifa**, maelezo au **mapokezi**. Katika Qur-an neno "Hadith" limetumiwa kwa maana hizi kama ilivyo katika aya ifuatayo:

﴿فَبِأَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَهُ يُؤْمِنُونَ﴾

*Basi simulizi gani baada ya hizi (simulizi za Qur-an) wataziamini?" (77:50)*

**Kisheria**, Hadith za Mtume (s.a.w) ni simulizi (mapokeo) au taarifa juu ya yale yote aliyoyafanya Mtume (s.a.w) katika kuufundisha Uislamu kinadharia na kimatendo au juu ya yale yaliyotendwa mbele yake akayakataza au akayaridhia au maelezo juu ya mwenendo na tabia ya Mtume (s.a.w). Ifuatayo ni mifano ya Hadith za Mtume (s.a.w):

#### **(i) Maelezo au maelekezo ya Mtume (s.a.w)**

Amesema Mtume (s.a.w) "Mwenye kumueleza mwenzake jambo la kheri anapata malipo sawa na mtendaji wa kheri hiyo."

#### **(ii) Vitendo vya Mtume (s.a.w)**

Amesema Bibi Aysha (r.a): "Mtume (s.a.w) alikuwa akiswali swala ya Dhuha rakaa nne na mara nyingine huzidisha atakazo."

#### **(iii) Kukubali (kuridhia)**

Amesema Bibi Aysha (r.a): "Mtume (s.a.w) aliwapeleka askari kwenye vita, kiongozi wao alikuwa akipendelea sana kusoma suratul-lkhlas katika swala. Waliporejea waliripoti kwa Mtume (s.a.w) jinsi Imamu wao alivyokuwa anafanya, Mtume (s.a.w) akasema: "Muulizeni kwanini alifanya hivyo." Wakamuuliza naye akajibu kwamba suratul-

Ikhlas ni sifa za Mwenyezi Mungu na yeye anapenda kuzisema. Mtume (s.a.w) akasema: "Mwambieni kwamba na yeye Mwenyezi Mungu anampenda."

**(iv) Sifa au Mwenendo wa Mtume (s.a.w)**

*"Amesema Sayidna Ali (r.a), Mtume (s.a.w) alikuwa mwenye elimu, mpole na mkarimu. Mwenye kumuona Mtume (s.a.w) huvutiwa naye na kumfuata."*

## Nafasi ya Sunnah katika Uislamu

Mtume Muhammad (s.a.w) kama ilivyokuwa kwa Mitume waliomtangulia, alikuwa ni mjumbe wa Allah (s.w) aliyeteuliwa ili aufundishe Uislamu na kuusimamisha katika jamii, yeye mwenyewe akiwa ni kiigizo chema. Hivyo ili watu waweze kuufahamu Uislamu vilivyo na kuweza kuusimamisha katika jamii hawana budi, pamoja na kuisoma Qur-an kwa mazingatio, kumfuata Mtume, kumtii na kumfanya kuwa kiigizo chao kitabia na kimwenendo. Qur-an inasisitiza jambo hili katika aya nyingi na baadhi ya hizo ni hizi zifuatazo:

**Amri ya Kumtii Mtume (s.a.w)**

Utii kwa Allah (sw) umesisitizwa sambamba na utii kwa Mtume (s.a.w) kama tunavyojfinza katika aya zifuatazo:

وَاطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٣٢﴾

*"Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa." (3:132)*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَاطِيعُوا اللَّهَ وَاطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولَى  
الْأَمْرِ مِنْكُمْ ۗ فَإِن تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن  
كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥١﴾

“Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu nyenu, walio katika nyie (Waislamu wenzenu). Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lo lote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hiyo ndiyo kheri, nayo ina matokeo bora kabisa.” (4:59)

وَاطِيعُوا اللَّهَ وَاطِيعُوا الرَّسُولَ وَأَحْذَرُوا فَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَأَعْلَمُوا أَنَّمَا عَلَىٰ

رَسُولِنَا الْبَلَّغُ الْمُبِينُ ﴿٤٩﴾

Na mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na tahadharini (na kukhalifu amri zao). Na mkikengeuka basi jueni ya kwamba juu ya Mtume wetu ni kufikisha tu (ujumbe) waziwazi. (Na akishafikisha hana lawama; lawama juu yenu). (5:92)

وَاطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٥١﴾ .....

.....Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ikiwa nyinyi ni katika wanaoamini (kweli). (8:1)

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَا تَوَلَّوْا عَنْهُ وَأَنْتُمْ

تَسْمَعُونَ ﴿٥٢﴾

“Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msijiepushe naye na hali mnasikia.” (8:20)

قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ فَإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْهِ مَا حُمِّلَ وَعَلَيْكُمْ

مَا حُمِّلْتُمْ وَإِن تُطِيعُوهُ تَهْتَدُوا وَمَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلَّغُ الْمُبِينُ ﴿٥٣﴾

Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume, na kama mkikengeuka, basi ni juu yake huo (mzigo) aliotwika; (kazi aliyopewa kufikisha ujumbe). Na juu yenu (huo mzigo) mliotwikwa (kutii). Na mkimtii mtaongoka; hapana juu ya

*Mtume ila kufikisha (ujumbe wake) wazi wazi. (24:54)*

﴿يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا ءَأَطِيعُوا ٱللَّهَ وَءَأَطِيعُوا ٱلرَّسُولَ وَلَا تُبْطِلُوا

ءَأَعْمَلَكُمْ﴾

*Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu. ( 47:33)*

وَءَأَطِيعُوا ٱللَّهَ وَءَأَطِيعُوا ٱلرَّسُولَ فَاِن تَوَلَّيْتُمْ فَاِنَّمَا عَلٰى رَسُوْلِنَا ٱلْبَلٰغُ

ٱلْمُبِيْنُ﴾

*Na mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume. Mkipuuzwa (hapana lawama juu yake). Juu ya Mtume wetu ni kufikisha tu kuliko wazi wazi. (Naye amekwisha kukufikishieni). (64:12)*

## **Amri ya Kumfuata Mtume (s.a.w)**

قُلْ اِن كُنْتُمْ تُحِبُّوْنَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُوْنِى يُحِبِّبْكُمْ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوْبَكُمْ

وَٱللَّهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ﴾

*Sema, "Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni, (hapo) Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye maghufira (na) mwenye rehema." (3:31)*

ءَأْمِنُوْا بِٱللَّهِ وَرَسُوْلِهِ ؕ وَءَأَنْفِقُوْا مِمَّا جَعَلَكُمْ مُّسْتَخْلِفِيْنَ فِيْهِ ؕ فَاَلَّذِيْنَ

ءَأْمِنُوْا مِنْكُمْ وَءَأَنْفَقُوْا لَهُمْ ءَأَجْرٌ كَبِيْرٌ﴾

*"Na anachokupeni Mtume basi pokeeni na anachokukatazeni jiepusheni nacho". (57:7)*



## Amri ya Kumfanya Mtume (s.a.w) Kiigizo

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ  
الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٦١﴾

"Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana." (33:21)

## Kutomfuata Mtume (s.a.w) ni Uasi

وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَتَعَدَّ حُدُودَهُ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيهَا وَلَهُ  
عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿٤٤﴾

Na anayemwasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kuiruka mipaka yake, (Mwenyezi Mungu) atamwingiza Motoni, humo atakaa milele, na atapata adhabu zifedheheshazo. (4:14)

يَوْمَئِذٍ يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَعَصُوا الرَّسُولَ لَوْ تُسَوَّىٰ بِهِمُ الْأَرْضُ وَلَا  
يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا ﴿٤٢﴾

Siku hiyo wale waliokufuru na kumwasi Mtume watatamani ardhi isawazishwe juu yao (yaani lau kuwa wamefukiwa tu kaburini bila ya kufufuliwa). Wala hawataweza kumficha Allah Hadith yo yote (katika ambo waliyoyafanya). (4:42)

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّهُ مَن يُحَادِدِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَأَنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا فِيهَا  
ذَٰلِكَ الْخِزْيُ الْعَظِيمُ ﴿٦٣﴾

"Je, hawajui ya kwamba anayeshindana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake kuwa yeye atapata moto wa Jahannam kukaa humo daima? Hiyo ndiyo hizaya kubwa." (9:63)

وَمَنْ يَعِصِ اللَّهَ .....

وَرَسُولَهُ فَإِنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا فِيهَا أَبَدًا ﴿٧٢﴾

“... Na watakao muasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi bila shaka watapata moto wa Jahanam, wakae humo milele.” (72:23)

Aya hizi zote kwa ujumla zinatunyeshwa wazi kuwa kufuata sunnah, ya Mtume (s.w) si jambo la hiari kwa Muislamu. Hivyo ule uoni walionao baadhi ya Waislamu kuwa sunnah ni jambo la hiari, ukilifanya unapata thawabu na ukiliacha hupati dhambi ni uoni potofu kama tutaizingatia pia aya ifuatayo:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا لِمُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ

الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika wamepotea upotofu ulio wazi (kabisa). (33:36)

## Historia fupi ya uandishi wa Hadith za Mtume (s.a.w)

Tofauti na Qur-an, ambayo iliandikwa mara tu baada ya kushushwa chini ya malekezo na usimamizi wa Mtume (s.a.w) mwenyewe, Hadith za Mtume (s.a.w) ambamo ndani yake ndio tunapata sunnah yake, zimeandikwa na watu kulingana na walivyomuona, au walivyomsikia. Historia ya uandishi wa Hadith za Mtume (s.a.w) katika vitabu vya Hadith, imechukua takriban muda wa karne tatu. Kwa kurahisisha tutaigawa historia ya kuhifadhiwa Hadith katika maandishi katika hatua nne zifuatazo:

- Wakati wa Mtume (s.a.w).
- Wakati wa Maswahaba wa Mtume (s.a.w).
- Wakati wa Tabi'iina.
- Wakati wa Tabii Tabi'iina.

### **Wakati wa Mtume (s.a.w)**

Wakati wa Mtume (s.a.w), hapakuwa na uandishi mkubwa wa Hadith kwa sababu:

**Kwanza**, Mtume mwenyewe alikuwepo, hivyo kilichokuwa muhimu kwa Masahaba ni kufuata mafundisho ya Mtume(s.a.w) na kuigiza mwenendo wake, kila walipokwama katika utendaji au kila walipotatizwa na tatizo lolote, walimwendea Mtume(s.a.w) na aliwakwamua au kuwatatulia tatizo lolote walilokuwa nalo.

**Pili**, Masahaba katika kipindi hiki walijishughulisha sana na kuandika, kusoma na kuhifadhi Qur-an moyoni na kuitekeleza katika maisha yao ya kila siku.

**Tatu**, kwa kuwa mwanzoni Mtume (s.a.w) aliwakataza Masahaba wake kuandika Hadith, walizoea kutoandika Hadith hata wakati waliporuhusiwa kuandika na walipendelea kutoandika kuliko kuandika Hadith.

**Nne**, katika wakati huu wa Mtume (s.a.w) Masahaba walishughulika sana katika harakati za kuuhami Uislamu ambao ulikuwa umesongwa sana na maadui wake ambao walipania sana kumuua Mtume, Uislamu na Waislamu.

Kutokana na sababu hizi nne na nyinginezo, uandishi wa Hadith haukupewa nafasi nzito katika kipindi hiki cha Mtume (s.a.w). Hivyo, Hadith nyingi zilibakia katika matendo na vifua vya Masahaba. Masahaba waliokuwa karibu sana na Mtume (s.a.w) kwa muda mrefu wa maisha yao, walihifadhi Hadith nyingi zaidi

kuliko wale waliokaa mbali na Mtume (s.a.w). Miongoni mwa Masahaba waliofahamika kuwa mashuhuri kwa kuhifadhi Hadith nyingi ni Abu Hurairah, bibi Aysha (mkewe Mtume (s.a.w)) 'Abdullah bin 'Umar, 'Abdullah bin 'Abbas, na Abdullah bin 'Amr na Abdallah bin Masu'ud (r.a)

### **Wakati wa Masahaba wa Mtume (s.a.w)11-100. A.H**

Kipindi hiki ambacho kimechukua kama karne moja hivi kuanzia pale alipotawafu Mtume (s.a.w) mpaka kutawafu kwa sahaba wa mwisho. Sahaba wa mwisho, Anas bin Malik alifariki 91 A.H. Hiki ni kipindi cha Makhalfi wanne waongofu na Masahaba mashuhuri wa Mtume (s.a.w).. Ni katika kipindi hiki ambapo Dola ya Kiislamu ilitanuka sana. Matatizo mengi ya wakati huu yalitatuhiwa kwa kutegemea hukumu za Hadith zilizohifadhiwa vifuani mwa Masahaba. Kwa mfano, baada ya kutawafu Mtume (s.a.w),zilijitokeza kesi ambazo zilionesha umuhimu wa kuhifadhiwa Hadith kama vile:

"Mtume azikwe wapi - Makka au Jerusalem?" Ikatolewa Hadith ya Mtume isemayo: "Mtume azikwe afiapo." Hadith ikamaliza tatizo.

Katika kipindi cha Makhalfi wanne waongofu kazi ya uandishi ilikuwepo, lakini haikuwa katika kiwango kikubwa. Kazi kubwa ya kwanza ya uandishi wa Hadith iliyoonekana katika kipimdi hiki ni ile ya kitabu cha Hadith - "Alqatadaya cha 'Ali (r.a) aliyefariki 40 A.H. Pia palikuwa na Juzuu (Pamphlet) ya Hadith ya Ibn 'Abbas (r.a) aliyoiandika muda mrefu baada tu ya kutawafu Mtume (s.a.w). Ibn 'Abbas (r.a) alifariki 61 A.H. Hazrat 'Ali na Ibn 'Abbas japo walikuwa wanazuoni wakubwa, kazi yao hii ndogo, haikuwa inatosheleza mahitaji ya wakati huo.

Katika kipindi hiki haja kubwa ya kuhifadhi Hadith katika maandishi ilijitokeza baada ya kutokea matatizo ya kisiasa,

palipotokea makundi mawili: Kundi la 'Ali na kundi la Mu'awiayh. Hadith zilianza kutumiwa vibaya kwa maslahi ya kikundi. Kila kikundi kilikubaliana tu na Hadith zile zinazotetea upande wake. Vile vile kulizuka Hadith nyingi za uongo. Ikumbukwe pia katika wakati huu wa Historia, dola ya Kiislamu ilikuwa imepanuka sana na kwa hiyo ulikuwepo uwezekano mkubwa wa kuzusha Hadith za uongo. Hii ndio sababu iliyomsukuma kiongozi aliyekuja baadaye kabisa 'Umar bin 'Abdul-Azizi (101 A.H.) achukuwe dhima ya kuchuja na kuandika Hadith zilizo sahihi. Chini ya uongozi wake vitabu kadhaa viliandikwa na ziliwekwa sheria za kutambua asili ya Hadith na maisha ya wapokezi hasa kuhusu mwenendo na msimamo wao. Watu wawili walifanya kazi hii, Ibn Shihab Al-Zuberi na Abu Bakr al-Hazm.

### **Wakati wa Wafuasi wa masahaba (Tabi'ina)101-200 A.H**

Hiki ni kipindi cha wafuasi wa Masahaba wa Mtume (s.a.w) katika karne ya pili Hijriyyah 101-200 A.H. Katika kipindi hiki walitokea wanazuoni wengi waliojizatiti katika kazi ya ukusanyaji wa Hadith kutoka katika vituo mbali mbali vya mafunzo (Centres of Learning). Wafuatao ni baadhi ya wanazuoni wa Hadith (Muhaddithina) waliojitokeza kutoka miji mbali mbali. Ma'mar bin Rashi wa Baghdadi; Said bin Abi Ubadah na Rabia bin Sabin wa Basra; Ibn Harith wa Baghdad; Abdul Malik bin Juraiji wa Makka; Walid bin Mubarrak wa Khurasan; Abu Bakr Shyaban wa Kufa na Sufyan bin Uyaina wa Madina.

Japo wanazuoni hawa walijitahidi sana katika hii kazi ya ukusanyaji Hadith, kazi zao bado hazikuwa zenye kutosheleza; isitoshe sehemu kubwa ya vitabu vyao ilihusu ripoti ya vituo vyao.

Baada ya kazi hizi, kilitokea kitabu cha "**al-Muwatta**" cha **Imam Malik bin Anas** aliyeshi Madina kati ya 95 A.H na 179 A.H. Kazi ya Imam Malik ndiyo ya kwanza iliyowekwa katika mpango mzuri na kuwa kitabu cha kutegemewa na Umma. Imam Malik

alifutu mas-ala ya Uislamu kwa kutegemea Qur-an na Hadith tu. Alianzisha umoja wa "Ahli Hadith" ambao kazi yake ilikuwa ni kukusanya Hadith na kuzitekeleza katika matendo.

Katika wakati huo huo alitokea Imam **Abu Hanifa al-Numan bin Thabit** (80-150) aliyefutu mas-ala mbali mbali ya Kiislamu kwa hoja na Qiyasi (deductions) baada ya kuzingatia Qur-an, Hadith na Ijma'i (makubaliano ya wanavyuoni). Hakuandika kitabu chochote cha Hadith lakini alikuwa mwanazuoni mkubwa wa "Qur-an na Hadith na alikuwa Muj-tahid na Mcha-Mungu.

Katika kipindi hiki hiki palitokea Maimamu wengine wawili mashuhuri. **Imam Muhammad bin Idris al-Shafii** (150-240 A.H.) aliyezaliwa Palestine mji wa Ghazza, na mwingine ni **Imam Ahmad bin Hambal** (164-241 A.H.) aliyezaliwa Baghdad na kujulikana sana kwa kitabu chake cha **Isnad ya Ibn Hambali** kilichokuwa na Hadith zaidi ya 30,000 alizokusanya.

## **Wakati wa Wafuasi wa Masahaba (Tabi'i Tabi'ina) 201-300 A.H**

Hatua ya nne ya ukusanyaji na uandishi wa Hadith ni ile iliyopitiwa katika karne ya Tatu Hirjiriyah (201-300 A.H.). Kazi ya karne ya pili au hata ya tatu ya uandishi wa Hadith tuliyoiona, Hadith zake hazikutosheleza yote yanayohitajika katika utekelezaji wa Uislamu katika kila kipengele cha maisha ya kila siku. Kwa mfano kitabu cha Imamu Malik kilichokuwa mashuhuri sana kilitumiwa au kupatikana sana huko Hijaz na kiligusia baadhi ya mambo tu yakiwemo ya lbada kama kufunga, kuhiji, Sala na Zakat.

Hivyo kulikuwa na haja kubwa ya kueleza mambo mengine yaliyohusu Uislamu katika nyanja zote za maisha. Kwa hiyo kipindi hiki kilikuwa cha kazi nzito ya kukusanya na kuhifadhi Hadith na kuziweka katika hali zilivyo hivi sasa. Katika kipindi hiki walitokea wanazuoni mashuhuri sita waliojitahidi na kutumia sehemu kubwa

ya maisha yao katika kukusanya Hadith. Walisafiri masafa marefu kwa ajili ya kazi hii ya ukusanyaji wa Hadith na ilibidi wajifunze tabia za watu kadhaa kabla ya kuandika Hadith moja. Sio kila Hadith waliyoambiwa waliandika bali kulikuwa na utaratibu wa kuchambua Hadith iliyo sahihi na isiyo sahihi. Ndio maana vitabu sita vya Hadith walivyoandika vilijulikana kwa jina la "Sahihu-Sitta." Vitabu hivi sita ni vile vya:

### **(a) Sahihi ya al-Bukhari**

Kitabu cha **Muhammad bin Isma'il Abu 'Abdallah al'Ju'fi** anayejulikana kwa jina la "Imamu al-Bukhari." Alizaliwa 13 Shawwal, 194 A.H./21 Julai, 810 A.D. katika mji wa Bukhara huko Urusi, na alifariki 30 Ramadhan, 256 A.H./31 Agosti 870 .D.

Hamu yake ya kuhifadhi Hadith aliipata bado akiwa mtoto wa umri wa miaka kumi na moja. Alipofikia umri wa miaka kumi na sita alikwenda kuhiji Makka na kubakia humo humo kujifunza Hadith kwa wanazuoni mbali mbali. Baada ya kutoka Makka alikwenda Misr kisha Basra na sehemu nyingine za Asia ambapo alitembea huku na huku katika kujifunza na kukusanya Hadith kwa muda wa miaka kumi na sita.

Kazi yake ya miaka kumi na sita inaonekana katika kitabu chake mashuhuri kijulikanacho kwa jina la "**Al-Jami'u al-Sahih au Sahihi al-Bukhari**". Kitabu hiki ndio kitabu cha kwanza cha Hadith kinachotemgemewa na Umma wa Waislamu baada ya Qur-an, kwa sababu ya uangalifu mkubwa uliochukuliwa na Imamu Bukhari katika ukusanyaji na uchambuaaji wa Hadith zake. Jumla ya Hadith alizokusanya ni 600,000 na katika hizo alihifadhi Hadith 200,000.

Lakini kutokana na uangalifu na tahadhari kubwa aliyoichukua katika kuhakiki usahihi wa Hadith alizozipokea, ni Hadith 7,275 tu zilizotokea katika kitabu cha sahihi al-Bukhari. Kabla hajaikubali

Hadith kuwa ni sahihi, ilibidi kwanza achunguze historia ya maisha ya kila mpokeaji wa Hadith hiyo kutokea kwa Mtume (s.a.w) mpaka kumfikia.

Imamu Bukhari amezipanga Hadith katika kitabu chake kufuatana na mada za fiq-h. Ameigawanya kazi yake katika juzuu tisini na saba na katika milango (sura) 3,450.

### **(b)Sahihi ya Muslim**

Ni kitabu cha Hadith sahihi kinachofuatia sahihi al-Bukhari kilichokusanywa na Abul Husain Muslim bin al-Hajjaj anayejulikana kwa jina la Imamu Muslim. Imamu Muslim alizaliwa katika mji wa Misabur, 202 A.H./817 A.D. na alifariki 261 A.H./875 A.D. katika mji huo huo. Kama alivyokuwa Imamu Bukhari, naye alisafiri sana huku na huko katika nchi za Uarabuni, Misr, Syria (Sham) na Iraq ambapo alipata fursa ya kusoma kwa wanazuoni wengi waliokuwa mashuhuri. Miongoni mwa wanazuoni mashuhuri ambao alisoma kwao ni Ahmad bin Hambal, mwanafunzi wa Imam Shafii.

Imam Muslim alikusanya Hadith 300,000 na katika hizo ni Hadith 9,200 alizoziandika katika kitabu chake kinachojulikana kwa jina mashuhuri "Sahihi Muslim". Alimpenda sana Imam Bukhari na kazi yake. Kama imam Bukhari, Muslim naye amekifuma kitabu chake kulingana na mada za fiq-h. Naye alichukua uangalifu mkubwa mno katika kuchagua Hadith zilizo sahihi kwa kiasi ambacho Hadith zake nyingi zimekubaliana na zile za Al-Bukhari. Alikuwa mwangalifu sana katika kuchambua sehemu ya upokezi (isnad) kwa kiasi ambacho Hadith moja ilikuwa na isnad nyingi (misururu mingi ya wapokeaji). Kwa msomaji, Sahihi Muslim imekuwa katika mpango mzuri zaidi kuliko ule wa Sahihi al-Bukhari.



### **(c)Sunnan ya Abu Dawud**

Ni kitabu cha Hadith cha Abu Dawud. Alizaliwa 203 A.H. na akafiriki 275 A.H. Elimu yake ya mwanzo aliipata Khurasan. Alisafiri sehemu mbali mbali ambazo zilikuwa mashuhuri kwa kuwa na wanazuoni wa Hadith. Ni miongoni mwa wanafunzi wa Imam Ahmad bin Hambali. Alikusanya Hadith 500,000 na alizoziandika katika kitabu chake cha Hadith kinachojulikana kwa jina la "**Sunnah**" ni Hadith 48,000 tu.

Japo hakuwa mkali sana katika uchambuzi na uhakiki wa Hadith zake kama walivyokuwa Bukhari na Muslim, Sunan yake imekuwa ni kitabu cha Hadith mashuhuri sana kwa Umma wa Kiislamu na imeshika daraja la 2 kwa usahihi baada ya sahihi mbili. Hapana shaka kitabu hiki kimejaza mapengo ya mambo yale ambayo hayakugusiwa na Imam Bukhari na Imamu Muslim. Pia Abu Dawud naye alipanga Hadith zake kulingana na vichwa vya habari vya mada mbali mbali.

### **(d)Jami'u ya at-Tirmidh**

**Abu Isa Muhammad bin 'Issa bin Sarwa bin Shaddad** anayejulikana kwa jina la at-Tirmidh alisoma kwa Imamu Bukhari, Ahmad bin Hambali na Abu Dawud al-Sijistani. Alizaliwa katika mji wa Tirmidh mnamo 209 A.H. na akafariki mwaka wa 279 A.H.

**Imamu Tirmidh** alikuwa mwanazuoni mkubwa. Pamoja na kitabu chake cha Hadith aliandika vitabu vingine vya Sharia na Tarekh. Alisafiri sana katika kukusanya Hadith katika nchi za Khurasan, Iraq na Hijaz.

Kitabu chake cha Hadith kinachojulikana kwa jina la **Jamiu** kimemfanya kuwa maarufu sana. Alikuwa mwanazuoni wa kwanza kuchambua Hadith kutokana na majina ya wasimulizi. Alizingatia majina yao, majina yao ya ukoo, majina ya utani, n.k. Jami'u ina Hadith chache zaidi ukilinganisha na **Sahihi Bukhari** na **Sahihi Muslim**.

### **(e) Sunan ya Ibn Majah**

Hiki ni miongoni mwa vitabu sita vya Hadith sahihi kilichoandikwa na **Muhammad bin Yazid** anayejulikana kwa jina la Ibn Majah aliyezaliwa 209 A.H. na akafariki 295 A.H. Katika kukusanya Hadith alisafiri nchi mbali mbali palimokuwa na vituo vya elimu kama Basra, Kufa, Baghdad, Makka, Syria (Sham) na Misr.

Kitabu chake cha Hadith kinachojulikana kwa jina la "**Sunan**" kimejishughulisha na Hadith zinazohusu sharia zinazoonyesha halali na haramu. Katika uchambuzi wa Hadith sahihi hakuwa makini sana kama walivyokuwa Maimam wawili wa mwanzo. Hivyo Hadith zake zimewekwa kwenye daraja la pili la usahihi. Hadith za daraja la kwanza ni Hadith za Bukhari na Muslim.

### **(f) Sunan ya an-Nasai**

An-Nasai ambaye jina lake kamili ni Abu 'Abdur-Rahman Ahmad bin an-Nasai alizaliwa katika mwaka 214 A.H na kufariki 303 A.H./315 A.D. An-Nasai alikuwa mwanafunzi wa Abu Dawud na Hadith za kitabu chake kinachojulikana kwa jina la "**Sunan**" amezipanga katika muundo alioutumia mwalimu wake. Kazi ya an-Nasai katika ukusanyaji Hadith imekuwa ni kazi muhimu sana kwa Uma wa Kiislamu lakini kwa kuwa hakuwa mwangalifu sana katika uchujaji wa Hadith sahihi, kazi yake imeangukia katika kundi la Hadith za daraja la pili. Baadhi ya Hadith za kitabu hiki ni dhafu na zenye kutiliwa mashaka zilizo simuliwa na watu wanaotiliwa mashaka.

Hivi ndivyo vitabu sita mashuhuri vilivyodhibiti Hadith katika maandishi katika kipindi hiki cha nne cha historia ya uandishi wa Hadith. Vitabu hivi vimeitwa Sahihi kutokana na uangalifu uliochukuliwa na waandishi katika kuzikusanya Hadith na kuzidhibiti katika maandishi. Kila waandishi walivyochukua tahadhari ya hali ya juu katika kuzichuja Hadith ndivyo Hadith zao

zilivyopanda daraja la usahihi. Ni kwa msingi huu Hadith za Imam Bukhari na Muslim zimekuwa daraja la kwanza na zinajulikana kwa jina la "Sahihain"(Sahihi mbili), na Hadith za Maimamu wanne waliofuatia zimekuwa katika daraja la pili la Usahihi. Vipimo au vigezo vya Hadith sahihi tutaviona katika kipengele kinachofuatia.

Hata hivyo, pamoja na vitabu hivi sita mashuhuri, pana vitabu vingine vya Hadith vilivyoandikwa katika karne hii ya tatu Hijiriyah ambavyo pia hutegemewa na Waislamu na ambavyo imetubidi tuvitaje hapa ili kuonyesha jinsi kazi ya uandishi wa Hadith ilivyopamba moto katika karne ya tatu Hijiriyah. Kwa hiyo, pamoja na "**Sahihi Sita**" tulizozitaja, vifuatavyo pia viliandikwa na vilikuwa mashuhuri kwa kiasi chake.

**(g) Kitabu cha al-Waqidi**

- Wa Baghdad aliyefariki 207 A.H.

**(h) Masnad ya Imam Ahmad**

- Kitabu cha Hadith cha Imam Ahmad bin Hambali aliyezaliwa 164 A.H. na kufariki 241 A.H. kilikuwa kitabu mashuhuri sana kwa wakati wake.

**(i) Kitabu cha 'Abdullah bin Hakam**

- Aliyezaliwa 221 A.H. na alifanyia kazi yake Basra.

**(j) Kitabu cha Yahya bin Mayum**

- aliyezaliwa 233 A.H. na kufanyia kazi yake Madina.

**(k) Sunan ya Darimi:**

- Ni kitabu cha Abu Muhammad 'Abdulah bin Ad-Darimi aliyezaliwa 181 A.H. na kufariki 255 A.H. Baada ya kitabu hiki ndipo vikafuata vitabu vya "Sahihi Sita".

### **(I)Kitabu cha Bayhaqi:**

- Kilichoandikwa na Imamu Abu bakr Ahmad al-Bayhaqi aliyelizaliwa 348 A.H. na akafariki 456 A.H. Kitabu hiki ni miongoni mwa kazi za mwanzo za karne ya nne Hijiriyah.

### **Uhakiki wa Hadith za Mtume (s.a.w)**

Kwa kuwa Hadith hazikuwa na ahadi ya Allah (s.w) ya hifadh kama ilivyo kwa Qur-an - "*Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya (Qur-an) na hakika sisi ndio tutakaoyalinda*". (15:9) - walitokea watu waovu wakamzulia Mtume (s.a.w) mambo mengi yaliyokinyume kabisa na Uislamu wenyewe. Hili lililwastua wanazuoni wacha-Mungu na kuwafanya wawajibike kuweka utaratibu maalumu wa kuchambua Hadith za Mtume (s.a.w). Katika harakati za uchambuzi wa Hadith, wanazuoni wa Hadith waliigawa Hadith katika sehemu kuu mbili - **Isnad** na **Matin**.

**Isnad** ni sehemu ya Hadith inayoonyesha msururu wa wapokezi wa Hadith hiyo tokea kwa yule aliyemsikia Mtume (s.a.w) akieleza jambo au aliyemuoma Mtume akifanya jambo, au aliyemuona Mtume akiridhia au akithibitisha jambo lililofanyika mbele yake au akieleza tabia ya Mtume (s.a.w) kama alivyoiona.

### **Mfano wa Isnad:**

*AmetuHadithia Abdallah bin Yusuf toka kwa Malik toka kwa Abizinadi toka kwa A'araji toka kwa Abu Hurairah ambaye amesema: Hakika ya Mtume wa Allah (s.a.w) amesema: .....*" (Bukhari)

Kwa hiyo msururu wa watu wote hao kuanzia yule aliyemsikia Mtume (s.a.w), Abu Hurairah (r.a) ambaye ni sahaba wa Mtume, hadi kumfikia Bukhari ambaye ni Imamu wa Hadith aliyepokea na kuiandika ndio **Isnad**.

**Matin** ni kauli ya Mtume au matendo yake.

Mfano wa Matin:

Mtume (s.a.w) amesema:

*"Yule ashikaye silaha dhidi yetu si pamoja na sisi." (Muslimu)*

Maneno aliyosema Mtume (s.a.w) yaliyofungiwa kwenye "....." ndio matin ya Hadith hii.

### **Riwaya**

Matin moja ya Hadith inaweza kuripotiwa na msururu wa wapokezi (Isnaad) zaidi ya moja.

### **Kwa mfano:**

Mtume (s.a.w) amesema "Yule ashikaye silaha dhidi yetu si pamoja sisi." (Muslimu)

Maneno haya aliyosema Mtume (s.a.w) yamesimuliwa katika **riwaya** tatu zifuatazo:

1. *"Abdullah bin Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yule ashikaye silaha dhidi yetu si pamoja na sisi." (Muslimu)*
2. *Ilyas bin Salama ameHadith a kutoka kwa baba yake kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yule ashikaye upanga (silaha) dhidi yetu si pamoja na sisi." (Muslimu)*
3. *Abu Musa Ashiari amesema kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yule ashikaye silaha dhidi yetu si pamoja na sisi." (Muslimu)*

### **Uhakiki wa Isnad**

Katika harakati za kuchuja Hadith zilizosahihi na zisizo sahihi; wanazuoni wa Hadith walikuwa wakifuatilia kwa undani historia ya wale wote waliomo kwenye msururu wa wapokezi wa Hadith na kumchunguza mtu wa kwanza kuHadith a Hadith hiyo

kuwa kweli alikuwa Swahaba balegh na Mkalafi aliyekuwa na uwezo wa kumsikia au kumuona Mtume (s.a.w). Kwa ujumla, ili Hadith iwe sahihi, kila msimulizi katika Isnad alitakiwa awe Muislamu mwaminifu, mwenye kumbukumbu nzuri, mwenye tabia njema na mcha-Mungu.

### **Uhakiki wa Matin**

Pamoja na kuwa na usahihi katika upokezi wa Hadith, "**Matin**" ya Hadith inaweza isiwe sahihi. Hivyo Hadith itakuwa shihi iwapo sehemu zote kwa pamoja - **Isnad** na **Matin** vitakuwa sahihi. **Matin** ya Hadith itakuwa sahihi iwapo itatekeleza masharti yafuatayo:

- (i) Isipingane na Qur-an.
- (ii) Isipingane na Hadith nyingine iliyothibitishwa kuwa ni sahihi.
- (iii) Isimzulie Mtume (s.a.w) kufanya jambo ambalo ni kinyume na Uislamu.
- (iv) Isipingane na hakika (fact)
- (v) Isipingane na ukweli unaothibitishwa na historia.
- (vi) Isiwe na maneno ya uongo ndani yake.
- (vii) Isiwe inaahidi adhabu kali sana kwa kosa dogo sana na isiwe imeahidi malipo makubwa sana kwa wema mdogo sana.

### **Tanzu za Hadith**

#### **(1) Tanzu ya Usahihi**

Kulingana na kiwango cha usahihi wa Hadith, Hadith zimegawanywa katika makundi makuu manne:

- (a) Sahihi (b) Hasan/Nzuri. (c) Dhaifu. (d) maudhu'u

### **(a) Sahihi**

Hadith sahihi ni zile Hadith zenye wasimulizi wote wenye sifa zilizokamilika kutokea mpokezi wa mwisho mpaka kufikia kwa Mtume (s.a.w). Kwa ufupi mambo yafuatayo ni muhimu yapatikane yote kwa pamoja ndio Hadith iitwe sahihi.

1. Pawepo Muungano wa Wapokezi wa Hadith. Kila mpokezi awe amepokea moja kwa moja kutoka kwa yule aliyeko juu yake kutoka mwanzo wa Isnadi mpaka mwisho wake.
2. Uadilifu wa Mpokezi. Kila mpokezi wa Hadith awe ni Muislamu, balegh, mwenye akili na asiwe fasiki na mwenye kufanya mambo ya ovyo ovyo.
3. Udhhibitifu wa Mpokezi. Ni kuwa kila mpokezi awe amekamilika katika udhibitifu wake, ama awe mdhibitifu wa kifua (kuhifadhi) au awe mdhibitifu wa kuandika.
4. Kutokwenda kinyume na aliyekuwa mdhibitifu zaidi. Asimukhalifu ambaye anajulikana kuwa mdhibitifu zaidi kuliko yeye.
5. Kutokuwa na Ila. Isiwe Hadith yenye ila wala sababu iliyojificha ambayo inasababisha kutokusihi kwa Hadith ijapokuwa nje yake haina wasi wasi.

### **Mfano wa Hadith Sahihi**

Hadith aliyoipokea Bukhari katika kitabu chake kasema:

*Ametuadithia 'Abdallah bin Yusuf akasema: Ametupa habari Malik kutoka kwa Ibn Shihab kutoka kwa Muhammad bin Ubair bin Mut-'im kutoka kwa baba yake kwamba: "Nimemsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anasoma Wat-tur katika swala ya Maghrib."*

Hadith hii ni sahihi kwa sababu: Wapokezi wake wameshikamana na wapokezi wake ni wadhibitifu.

1. 'Abdullah bin Yusuf ni mdhibitifu.
2. Malik bin Anas ni Imamu Hafiidh.
3. Ibn Shihab ni Faqihi Hafidh.
4. Muhammad bin Jubair ni mdhibitifu.
5. Jubair bin Mut-im-Sahaba.

### **Hadith Sahihi ziko katika daraja saba:**

- (i) Hadith iliyokubaliwa kwa pamoja na Imamu Bukhari na Muslim, huwekwa katika daraja la juu kabisa ya usahihi - na Hadith hii huelekezwa kwa: "Makubaliano (ya Bukhari na Muslim)."
- (ii) Hadith iliyopokelewa na Bukhari mwenyewe huchukua nafasi ya pili ya Usahihi.
- (iii) Hadith iliyosimuliwa na Muslimu mwenyewe huchukua daraja la Tatu ya Usahihi.
- (iv) Hadith iliyokubaliwa kwa kufuata masharti ya kuchambua Hadith aliyoweka Muslim na Bukhari, huwa katika daraja la nne ya Hadith Sahihi.
- (v) Hadith yenye kufuata masharti aliyoweka Bukhari mwenyewe huchukua nafasi ya tano ya Usahihi.
- (vi) Hadith iliyochambuliwa kwa masharti aliyoyaweka Muslim mwenyewe huchukua nafasi ya sita ya Usahihi.
- (vii) Hadith iliyokubaliwa na Muhaddithina wote isipokuwa Bukhari na Muslim huchukua nafasi ya saba ya Usahihi.

### **(b) Hasan/Nzuri**

Ni Hadith iliyofanana na Hadith sahihi bali kasoro yake ni kwamba wasimulizi wake wote au baadhi yao wamekuwa dhaifu katika udhibitifu wao ukiwalinganisha na wale wasimulizi wa Hadith sahihi.



### **(c)Dhaifu**

Ni Hadith ambayo miongoni mwa wasimulizi wake wana kasoro zilizojitokeza. Hadith za namna hii si zenye kuaminika na kwa hiyo si za kutegemea.

### **(d)Maudhu'u**

Hii ni Hadith ya uongo ambapo Mtume (s.a.w) amezuliwa na wapakachikwa wapokezi wa kughushi. Ni Hadith ambayo hupingana na Qur'an na Hadith nyingine iliyo sahihi.

## **(2.) Tanzu ya umashuhuri(umaarufu)**

Pia Hadith zimegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo ili kuonyesha uzito wa kukubalika au kutokubalika kwake.

(a) **Mutawatir** - ni Hadith yenye kusimuliwa na watu wengi, wanne au zaidi wote wakiwa wanasifa zilizokamilika na wakawa wameisimulia kwa nyakati mbali mbali kwa kiasi ambacho huifanya Hadith hiyo iwe ni muhali kuwa na tone la doa la uwongo ndani yake. Pia Hadith Mutawatir ni zile zinazokubalika na watu wote wa nyakati zote tangu wakati wa Mtume Muhammad (s.a.w). Kwa mfano Hadith ifuatayo imesimuliwa na Masahaba wengi na imekubaliwa na watu wote.

*Mtume (s.a.w) amesema: "Mwenye kunizulia uwongo makusudi, atarajie (angojee) makazi ya Motoni."*

Hadith hii ni Mutawatir - yaani ni yenye kukubalika pasina tone la shaka.

(b)**Ahad** ni Hadith ambayo japo wasimulizi wake ni wenye sifa zilizokamilika, hawana mfungamano yaani msururu wa wasimulizi una mapengo mapengo katikati (Isnad haikukamilika). Pia Hadith Ahad ni ile isiyokubaliwa na watu wengi. Hadith za namna hii ni za mashaka mashaka na si zenye kuaminika na si vizuri kuzitegemea.

## **Aina za Hadith**

Kuna aina kuu mbili za Hadith - (a) Hadith Nabawiyyi. (b) Hadith Qudusiyyi.

### **(a)Hadith an-Nabawiyyi**

Ni usemi au habari aliyoitoa Mtume (s.a.w) kwa watu kwa maneno yake. Utazikuta Hadith za aina hii zikianza na: Amesema Mtume (s.a.w) "Mfano wa Hadith an-Nabawiyyi:

*Aysha (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah (Rehema na amani iwe juu yake) amesema: "Yoyote atakayeingiza jambo jipya katika mambo yetu (dini yetu) lisilokuwa la humu, litakataliwa." (Wamekubaliana Bukhari na Muslim)*

### **(b)Hadith Qudusiyyi:**

Ni usemi au habari aliyoitoa Mtume (s.a.w) kama alivyoipokea kutoka kwa Allah (s.w) lakini iliyo nje ya Qur-an. Hadith hizi huanza na: Amesema Mtume (s.a.w) kuwa Allah (s.w) kasema: "....." Mfano wa Hadith Qudusiyyi:

*Abu Huraira (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah (rehema na amani iwe juu yake) amesema: Allah (s.w) amesema: "Ni mwingi wa kujitoshleza kwa kiasi kwamba sihitaji mshiriki yeyote. Kwa hiyo yeyote yule atakaye fanya amali (atakayefanya jambo) kwa ajili ya mtu mwingine pamoja na Mimi Nitaikataa hiyo amali na kuipeleka kwa yule aliyenishirikisha naye." (Imesimuliwa na Muslim, hali kadhalika Ibn Majah).*

Hadith Qudusiyyi ni chache sana ukizilinganisha na Hadith Nabawiyyi. Idadi yake ni Hadith mia mbili na kidogo tu.

## Zoezi la 4

1 (a) Ainisha maana ya sunnah kilugha na kisheria.

(b) Ainisha maana ya Hadith kilugha na Kisheria.

(c) Kiutendaji kufuata sunnah ya Mtume (s.a.w) ni kufanya yafuatayo:

(i) \_\_\_\_\_ (ii) \_\_\_\_\_.

(iii) \_\_\_\_\_ (iv) \_\_\_\_\_.

2. (a) Kazi ya uandishi wa Hadith mpaka kupata vitabu sita sahihi vinavyotegemewa na Waislamu, imepitiwa na vipindi vine vya historia vifuatavyo:

(i) \_\_\_\_\_ (ii) \_\_\_\_\_.

(iii) \_\_\_\_\_ (iv) \_\_\_\_\_.

(b) Taja sababu nne zilizopelekea uandishi wa Hadith usishamiri wakati wa Mtume (s.a.w).

3. (a) Isnad ya Hadith ni \_\_\_\_\_

(b) Matin ya Hadith ni \_\_\_\_\_

(c) Nukuu Hadith yoyote kisha uoneshe Isnad na Matini ya Hadith hiyo.

(d) Matin ya Hadith itakuwa sahihi iwapo itatekeleza masharti yafuatayo:

(i) \_\_\_\_\_ (ii) \_\_\_\_\_.

(iii) \_\_\_\_\_ (iv) \_\_\_\_\_.

(v) \_\_\_\_\_

4. Toa maelezo mafupi juu ya:

(a) Hadith Nabawiyyi.

(d) Hadith Mutawatir.

(b) Hadith Dhaifu.

(e) Hadith Qudusiyyi.

(c) Hadith Maudhuu.

## Sura ya Tano

# MWENENDO WA MUISLAMU

### Utangulizi

Muislamu anatakiwa kwa muda wote wa maisha yake kuwa katika Ibada.

Muislamu atakuwa katika Ibada kwa muda wote wa saa 24 endapo atamtii Allah (s.w) katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii. Ili kuweza kumtii Allah (s.w) ipasavyo katika kila kipengele cha maisha yetu ya saa 24 hatuna budi kudumu katika mzunguko wa kuipitia Qur-an yote kwa mazingatio na kuiigiza katika matendo ya pamoja na kuigiza mwenendo wa siku nzima wa Mtume(s.a.w). Pamoja na utekelezaji wa Ibada maalumu kama vile kusimamisha swala za faradhi na sunnah, Mtume (s.a.w) alikuwa na tabia ya kuleta dhikr katika kila jambo alilolifanya. Katika sura hii tumerejea baadhi ya dua na dhikr alizoleta Mtume(s.a.w) katika kuendea vipengele mbalimbali vya maisha ya saa 24

### 1. Dhikri ya kuleta wakati wa kuamka kutoka usingizini

Mtume (s.a.w) alipoamka kutoka usingizini alikuwa akisema:

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَحْيَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا وَإِلَيْهِ النُّشُورُ.

*Al-hamdulillahilladhy ahyanaa ba'adamaa amaataanaa wailayhi nmushuuru"*

*"Sifa zote njema anastahiki Allah ambaye ametupa uhai baada ya kutufisha na ni kwake tu ufufuo."*

Mtume (s.a.w) amesema: "atakaye amka usiku kisha akasema:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ  
وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ.

*Laaillahailallaahu wah-dahu laa shariika lahu, lahulmulku  
walahul-hamdu wahuwa a'laa kulli shay-in qadiiru,*

*"Hapana Mola ila Allah, Mpweke asiye na mshirika, ni wake  
ufalme na ni zake sifa njema, ni muweza juu ya kila kitu;*

Kisha akasema

رَبِّ اغْفِرْ لِي.

"Rabbigh-fir-ly"

*"Ee, Mola nisamehe"*

Basi atasamehewa. Na kama atasimama akaenda kutawadha kisha akaswali basi swala yake itakubaliwa."

## 2.Dhikri ya kuleta wakati wa kuvaa nguo

لَحْمَدُ لِلَّهِ الَّذِي كَسَانِي هَذَا (الثَّوْبَ) وَرَزَقَنِيهِ مِنْ غَيْرِ حَوْلٍ مِنِّي وَلَا قُوَّةَ.

*Al-hamdulillaahi lladhy kasaany hadha (thawba) warazaqaniihi  
min ghairi hawlin minny walaquwwat"*

*"Sifa zote njema ni za Allah ambaye amenivisha nguo hii na  
kuniruzuku pasina uwezo wala nguvu kutoka kwangu."*

### 3. Dua ya Kuvua Nguo

بِسْمِ اللَّهِ .

"Bismillah"

"Kwa jina la Allah (nina vua)."

### 4. Dua ya Kuingilia Chooni

Muislamu akiingia chooni atangulize mguu wa kushoto na kusema:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْخُبْثِ وَالْخَبَائِثِ .

(Bismillah) "*Allahumma inni a'uudhubika minal-khubuth wal-khabaaithi*"

(Kwa jina na Allah). Ee, Allah najikinga kwako na maovu yote na wafanya maovu"

### 5. Dua ya Kutoka Chooni

Muislamu akitoka chooni hutanguliza mguu wa kulia na kusema:

غُفْرَانَكَ .

"Ghuf-raanaka"

"Nakuomba msamaha (Ee Allah)

### 6. Dhikri wakati wa kutoka Nyumbani

بِسْمِ اللَّهِ ، تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ .

*Bismillahi tawakkal-tu 'alallaahi walaahawla walaaquwwata illaabillaahi*

*Kwa jina la Allah, ninajitegemeza kwa Allah, na hapana uwezo wala nguvu ila vyote vinatokana na Allah"*

## 7. Dhikri wakati wa kurejea nyumbani

بِسْمِ اللَّهِ وَلَجْنَا، وَبِسْمِ اللَّهِ خَرَجْنَا، وَعَلَى رَبِّنَا تَوَكَّلْنَا.

*Bismillahi walaj-naa, wabismillaah kharaj-naa wa'alaah Rabanaa tawakkal-naa.*

*"Kwa jina la Allah tunaingia na kwa jina la Allah tunatoka, na kwa Mola wetu tunategemea."*

## 8. Dua ya Kuingia Msikitini

Tukiingia msikitini tunatanguliza mguu wa kulia na kusema:

أَعُوذُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ وَبِوَجْهِهِ الْكَرِيمِ وَسُلْطَانِهِ الْقَدِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ  
الرَّجِيمِ، [بِسْمِ اللَّهِ، وَالصَّلَاةُ] [وَالسَّلَامُ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ]،  
اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ.

*"A'udhubillaahil-'adhiim wabiwajhi-hil-kariim.*

*'Wasul-Twaanihil-qadiimi minash-shaytwaanir rajiim  
Bismillaah wasw-swallatu wassalaam a'laa rasuulillah ,  
Allaahummaf-tahaly ab-waaba rah-matika".*

*"Najikinga kwa Allah aliye mtukufu, na kwa uso wake mtukufu, na kwa utawala wake wa kale, kutokana na sheitwani aliyeepushwa na rehema za Allah, Kwa jina la Allah na Rehema na Amani ziwafikie Mtume wa Allah Ee! Allah nifungulie milango ya rehema zako."*

## 9. Dua ya kutoka Msikitini

Tukitoka msikitini tunatangeliza mguu wa kushoto na kusema:

بِسْمِ اللَّهِ وَالصَّلَاةِ وَالسَّلَامِ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ ،  
اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ ، اللَّهُمَّ اعْصِمْنِي  
مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ .

*"Bismillahir wasw-swalaatu was-salaamu 'alaa rasuulillaahi,  
Allaahumma inny as-aluka min fadh-lika, Allaahumma  
A'iswimniy, minash-shaytwaanir-rajiimi."*

*"Kwa jina la Allah na rehema na amani zimfikie Mtume wa  
Allah; Ee! Allah, nakuomba katika fadhila zako, Ee! Allah nilinde  
kutokana na shetani aliyeepushwa na rehema zako (aliye  
laaniwa)."*

## 10. Dhikri za Kuleta Asubuhi na Jioni

اللَّهُمَّ عَافِنِي فِي بَدَنِي ، اللَّهُمَّ عَافِنِي فِي سَمْعِي ،  
اللَّهُمَّ عَافِنِي فِي بَصَرِي ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ . ( ثلاثا )

*"Allahumma 'aafiniy fiy badaniy, Allahumma 'aafiniy fiy sam-'iy.  
Allahumma 'aafiniy fiy baswariy, Laailaha illaa anta. (Mara tatu)*

*Ee! Allah nipe afya ya mwili wangu, Ee! Allah nipe afya ya  
usikivu wangu (masikio yangu), Ee! Allah nipe afya ya uoni  
wangu (macho yangu). Hapana Mola ila wewe (mara tatu).*

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْكُفْرِ ، وَالْفَقْرِ ، وَأَعُوذُ بِكَ  
مِنَ عَذَابِ الْقَبْرِ ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ . ( ثلاثا )

*Allahumma inniy a'uudhubika minal-kufri, walfaq-ri, waa'uudhubika*



*min'adhaabil-qabri, Laailaha illa anta. (mara tatu)*

*Ee! Allah hakika mimi najilinda kwako kutokana na ukafiri; na ufakiri; na najilinda kwako kutokana na adhabu ya kabri; Hapana Mola ila wewe." (Mara 3)*

حَسْبِيَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَهُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ.  
( سبع مرات حين يصبح و يمسي )

*"Has-biyallahu laailaha illaahuwa 'alayhi tawakkal-tu wahuwa rabbul-'arshil-adhiimi. (Mara saba asubuhi na jioni).*

*Allah ananitosha, hapana Mola ila yeye. Kwake yeye ninategemea, na yeye ni Mola wa arshi tukufu (mara saba asubuhi na jioni).*

أَعُوذُ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ. (ثلاثا إذا أمسى)

*"A'uudhubikalimaatillaahi ttaammaati min-sharri maa khalaqa." (mara tatu jioni)*

*"Najikinga kwa maneno timilifu ya Allah kutokana na shari ya alivyoviumba" (mara tatu jioni).*

بِسْمِ اللَّهِ الَّذِي لَا يَضُرُّ مَعَ اسْمِهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ  
وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ. (ثلاثاً)

*"Bismillahi lladhii laayadhurru ma'asmih shay-un fiyl-ardhi walaa fissanamaai wahuwas-samii'ul-'aliimu. (mara tatu).*

*"Kwa jina la Allah ambaye hakidhuru kwa jina lake kitu chochote kile kilichoko ardhini wala mbinguni, naye ni Msikivu Mjuzi.*

سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ عَدَدَ خَلْقِهِ وَرِضَا نَفْسِهِ وَزِنَةَ عَرْشِهِ وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ. (ثلاثاً)

"Sub-haanallahi wabihamdihi, 'adadakhalqih, waridhwaa nafsih wazinata 'arshih wamidaada kalimatih, (Mara tatu)

"metakasika Allah na sifa zote njema ni zake kwa hisabu ya viumbe vyake, na radhi yake (mara tatu kila asubuhi)

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ عِلْمًا نَافِعًا وَرِزْقًا طَيِّبًا، وَعَمَلًا مُتَقَبَّلًا.  
(بعد السلام من صلاة الفجر)

"Allahumma inni as-aluka 'il-man-naafiaa, wariz-qan twayiba, wa-'amalan mutaqabbala".

"Ee! Allah nakuomba unipe elimu yenye manufaa, na riziki iliyo nzuri na amali (ibada) yenye kukubaliwa."

سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ

Sub-hanallahi wabihamdihi."  
(mara mia)

Ametakasika Allah na sifa zote njema ni zake.

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَكَهُ الْحَمْدُ  
وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ. (مائة مرة)

"Laailaha illallahu, wah-dahu laa sharikalahu, lahul-mul-ku walahul-hamdu wahuwa 'alaa kulli shay-in qadiiru" (mara mia)

"Hapana Mola ila Allah, mpweke, asiye na mshirika, ni wake ufalme na ni zake sifa njema zote, na yeye yuko juu ya kila kitu.

Mwenye kusoma Ayatul-Kurisiyy (2:255) pindi anapoamka atalindwa kutokana na mashetani (majini) mpaka jioni, na atakayesoma jioni atalindwa nayo mpaka asubuhi.

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لَا تَأْخُذُهُ سِنَّةٌ وَلَا نَوْمٌ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ ﴿٢٥٥﴾

*Mwenyezi Mungu hakuna Mola ila Yeye, (na) ndiye Mwenye uhai wa maisha, Msimamia kila jambo. Kusinzia hakumshiki wala kulala. Ni Vyake (peke yake vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi. Na nani huyo awezaye kuombea mbele Yake (Allah) bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao (viumbe) na (yajayo) nyuma yao; wala (hao viumbe) hawalijui lo lote katika yaliyo katika ilimu Yake (Mwenyezi Mungu) ila kwa alipendalo (Mwenyewe). Enzi yake imeenea mbingu; na ardhi; wala kuvilinda hivyo hakumshindi; na Yeye (peke yake) ndiye aliye juu na ndiye aliye Mkuu. (2:255)*

Mwenye kuzisoma mara tatu asubuhi na jioni sura zifuatazo zinamtosheleza na kila kitu:

**Suratul-Ikhlās (112:1-4)**

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ① اللَّهُ الصَّمَدُ ② لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ③ وَلَمْ يَكُن لَّهُ ④ كُفُوًا أَحَدٌ ⑤

*Sema, Yeye ni Allah aliye mmoja tu Allah ndiye anayestahiki*

*kukusudiwa (na viumbe vyote). Hakuzaa wala hakuzaliwa. Hakuna hata mmoja anayefanana naye." (112:1-4)*

### **Suratul-Falaq (113:1-5)**

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴿١﴾ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ﴿٢﴾ وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ﴿٣﴾  
وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ ﴿٤﴾ وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ﴿٥﴾

*Sema: Ninajikinga kwa Mola wa ulimwengu wote. Na shari ya Alivyoviumba. Na shari ya giza la usiku liingiapo. Na shari ya wale wanaopulizia mafundoni. Na shari ya hasidi anapohusudu. (113:1-5)*

### **Suratun-Naas (114:1-6)**

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿١﴾ مَلِكِ النَّاسِ ﴿٢﴾ إِلَهِ النَّاسِ ﴿٣﴾ مِنْ شَرِّ  
الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ﴿٤﴾ الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ ﴿٥﴾ مِنَ الْجِنَّةِ  
وَالنَّاسِ ﴿٦﴾

*Sema: Ninajikinga kwa Bwana Mwenye kuwalea watu. Mfalme wa watu. Muabudiwa wa watu. Na shari ya mwenye kutia wasiwasi mwenye kurejea nyuma. Atiaye wasi wasi nyoyoni mwa watu. (Ambaye ni) katika majini na watu." (114:1-6)*

## **Kumswalia Mtume Asubuhi na Jioni**

Mtume (s.a.w) amesema: Mwenye kuniombea rehema asubuhi mara kumi na jioni mara kumi, nitamuombea shufaa (masamaha) siku ya kiyama.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ  
وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ  
مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ.

*"Allahumma swali'ala Muhammad wa'ala aali Muhammad, kama swallayta 'ala Ibraahiima wa'ala aali Ibraahiim, Innaka hamidun majiidu, allahumma baarik-'ala Muhammad wa-'ala aali Muhammad, kama barak-ta 'ala Ibraahiima wa-'ala aali Ibraahiima, Innaka hamidun-majiidu."*

*Ee Allah! Mrehemu Muhammad na jamaa zake (wafuasi wake) Muhammad kama ulivyo mrehemu Ibrahiim na jamaa zake (wafuasi wake) Ibrahiim, hakika wewe ni mwenye kusifika mtukufu. Ee Allah! Mbariki Muhammad na jamaa zake Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na jamaa zake Ibrahiim, Hakika wewe ni Mwenye kusifika Mtukufu.*

Mtume (s.a.w) amesema:

*"Anayeniswalia mara moja, Allah (s.w) humswalia mara kumi." (Muslimu)*

Pia Mtume (s.a.w) amesema:

*"Bahili ni yule ninapotajwa, haniswalii (haniombei rehema na amani kwa Allah)." (Tirmidh)*

Kumswalia Mtume (s.a.w) kumeamrishwa kwa waumini kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ  
وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾

*"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamswalia Mtume (wanamtakia rehema na amani). Basi, enyi mlioamini mswalieni (muombeeni Mtume) rehema na amani." (33:56)*

## **11. Kuomba Msamaha na Kutubia**

**Amesema Mtume (s.a.w):**

*"Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika mimi ninamtaka msamaha Mwenyezi Mungu na ninatubia kwake katika kila siku zaidi ya mara sabini." (Al-Bukhari).*

أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ .

*"Astagh-firu llaha waatuubu ilahi." (mara mia)*

*"Namuomba msamaha Allah na ninatubia kwake."*

Pia Mtume (s.a.w) amesema: "Yeyote anayesoma maneno yafuatayo, Mwenyezi Mungu atamsamehe hatakama anamakosa ya kukimbia vitani:

أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ الْعَظِيمَ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ

*"Astagh-firu llaahal-'adhiimal-ladhii laaillaha illahuwal-hayyul qayyuumu wa-atuubu ilayhi."*

*"Namuomba msamaha Allah, Mtukufu ambaye hapana Mola ila yeye, aliye Hai, aliyesimama kwa dhati yake na ninatubia kwake."*

Amesema Mtume (s.a.w):

*"Hakuna mja yeyote yule anayefanya dhambi kisha akatawadha vizuri na akaswali raka mbili, kisha akamtaka Mwenyezi Mungu msamaha ila atasamehewa". (Abu Daud na Tirmidh)*

## **12. Dhikri ya kuleta baada ya kupatwa na janga au balaa**

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ الْعَظِيمُ الْحَلِيمُ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ،  
لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَرَبُّ الْأَرْضِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ.

*"Laailaha illa llahul-'adhwimul-haliimu, laa ilaha illa llahu rabbul-'ar-shil 'adhwimi, Laailaha illallahu rabbussamaawaat warabbul-ardhwi, warabbul-'ar-shil-kariimi.*

*"Hapana Mola ila Allah, aliye mtukufu mpole, Hapana Mola ila Allah, Mola wa arshi tukufu, Hapana Mola ila Allah, Mola wa mbingu na ardhi na Mola wa arshi tukufu.*

لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ.

*"Laailaha illaa-anta Sub-hanaanaka inny kuntuminal Dhw-Dhwaalimiina."*

*Hapana Mola ila Wewe, Utukufu ni wako, hakika mimi ni miongoni mwa waliodhulumu nafsi zao.*

## **13. Unapokutana na adui au mtawala dhalimu**

حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ.

*"Hasbunallahu wani'imal-wakiilu"*

“Allah anatutosheleza Naye ni mbora wa kutegemewa.

#### 14. Dua ya Kulipa Deni

اللَّهُمَّ اكْفِنِي بِحَلَالِكَ عَنْ حَرَامِكَ وَأَغْنِنِي بِفَضْلِكَ عَمَّنْ سِوَاكَ.

"Allahummak-finiy bihalaalika'an haraamika wa-agh-niy bifadhw-lika 'amman siwaaka."

Ee Allah! Nitosheleze na halali yako na Uniepushe na haramu yako, na Unitosheleze kwa fadhila zako nisiwahitaji wengine asiye wewe.

#### 15. Dua anayoleta yule aliyefikwa na jambo gumu

اللَّهُمَّ لَأَسْهَلَ إِلَّا مَا جَعَلْتَهُ سَهْلًا وَأَنْتَ تَجْعَلُ الْحَزْنَ إِذَا شِئْتَ سَهْلًا.

“Allahumma laasah-la illaa maaja-'al-tahu sah-laa, wa anta taj-'alul-haz-na idhaashi-ita sah-laa.

Ee Allah hakuna jepesi ila ulilolifanya jepesi, nawe unalifanya gumu kuwa jepesi ukitaka.

#### 16. Dua ya kuomba unapotokewa na jambo usiloliridhia au unaposhindwa kufanya jambo

Amesema Mtume (s.a.w) (katika Sahihi Bukhari): "Muumini mwenye nguvu (qawiyyu) ni bora na anapendeza zaidi kwa Allah (s.w) kuliko muumini dhaifu, na wote wanakheri. Fanya pupa kwa kile kitakacho kunufaisha na taka msaada wa Allah wala usichoke, na kikikupata kitu chochote kibaya basi usiseme lau kama ningelifanya kadha na kadhaa yasingenitokea haya, lakini sema:

قَدَّرَ اللَّهُ وَمَا شَاءَ فَعَلَ.

"Qaddarallahu wamaa shaa-af-a'la.

“Amepanga Allah na analolitaka anafanya.”



Hakika Allah analaumu mwenye kukata tamaa, lakini usivunjike moyo, na ukishindwa na jambo kabisa sema:

حَسْبِيَ اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ.

"Has-biya llahu wani-i'mal-wakiilu"

"Allah ananitosheleza, Naye ni mbora wa kutegemewa."

### 17. Dua ya Kumuomba mgonjwa wakati wa kumtembelea

لَا بَأْسَ طَهْرٌ إِنْ شَاءَ اللَّهُ.

"Laa ba-asa twahuurun in-shaa-allahu."

"Hakuna neno, (ugonjwa) ni kusafishwa na dhambi anapopenda Allah." (Al-Bukhari)

Anasema Mtume wa Allah: "Hapana yeyote Muislamu anayemtembelea mgonjwa ambaye wakati wake wa kufa bado haujafika na anamuomba mara saba.

أَسْأَلُ اللَّهَ الْعَظِيمَ رَبَّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ أَنْ يَشْفِيكَ (مربع مرات).

"As-ahullaah l-a'dhiima rabal-a'r-shi l-a'dhiimi an-yash-fiyaka.

"Namuomba Allah Mtukufu, Mola wa arshi tukufu akuponyeshe."

Isipokuwa Allah humponyesha mgonjwa huyo."

(At-Tirmidh na Abu Daud)

### 18. Dua anayoomba mgonjwa aliyekata tamaa na kupona

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَأَلْحِقْنِي بِالرَّيِّطِ الْأَعْلَى

"Allahumma gh-fir-liy war-hamniy wa-alhiq-niy birrafiq il-a-a'laa"

*Ee! Allah, nisamehe na unirehemu na unikutanishe na waja walio katika daraja za juu".*

### **19. Dua ya kuomba mvua**

اللَّهُمَّ أَسْقِنَا غَيْثًا مُغِيثًا مَرِيئًا مَرِيئًا، نَافِعًا غَيْرَ ضَارٍّ، عَاجِلًا غَيْرَ آجِلٍ.

*"Allahumma asqinaa ghaythan mughiithan mariian marii-a'a, naafia'an ghayradhwaarrin, a'ajilanghayra aajilin.*

*Ee! Allah tunyeshenze mvua yenye kuokoa, nyingi, yenye kustawisha, yenye manufaa isiyodhuru.*

### **20. Dua ya kuleta wakati unapovuma upepo**

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَهَا وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا.

*Allahumma inniy as-aluka khayrahaa wa-au'udhubika min-sharrihaa.*

*Ee, Allah! Ninakuomba unipe kheri ya upepo huu na uniepushe na shari yake.*

### **21. Dua ya kuleta wakati mvua inanyesha**

اللَّهُمَّ صَيِّبًا نَافِعًا.

*"Allahumma Swayyiban naafia'n*

*"Ee Allah ijaalie iwe mvua yenye manufaa."*

### **22. Dua ya kuleta baada ya mvua kunyesha**

مُطِرْنَا بِفَضْلِ اللَّهِ وَرَحْمَتِهِ.

*Mutwir-haa bifadh-lillahi warah-matihi.*

*Tumepata mvua kwa msaada na rehema ya Allah."*

### 23. Dua ya kusema unapoanza kula

Unapoanza kula hunabudi kusema:

بِسْمِ اللَّهِ

*"Bismillaahi"*

*"Kwa jina la Allah"*

Na ukisahau kusema hivyo wakati wa kuanza, ukikumbuka wakati unaendelea kula sema:

بِسْمِ اللَّهِ فِي أَوَّلِهِ وَآخِرِهِ.

*"Bismillahi fiy awwalihi wa-aakhirih"*

*"Kwa jina la Allah katika mwanzo wake na mwisho wake"*

### 24. Dua ya kushukuru baada ya kula

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَطْعَمَنِي هَذَا وَرَزَقَنِيهِ مِنْ غَيْرِ حَوْلٍ مِنِّي وَلَا قُوَّةٍ.

*"Al-hamdulillahilladhii atw-a'maniy hadhaa warazaqaniyhi min khayri hawlin minniy walaa quwwatin"*

*"Shukurani zote anastahiki Allah ambaye amenilisha chakula hiki bila ya uwezo wala nguvu yoyote kutoka kwangu."*

### 25. Dua ya mgeni kumuomba mwenyeji aliye mlisha chakula

اللَّهُمَّ بَارِكْ لَهُمْ فِيْمَا رَزَقْتَهُمْ، وَاغْفِرْ لَهُمْ وَارْحَمْهُمْ.

*"Allahumma baarik-lahum fiymaa razaq-tahum, wagh-fir lahum war-hamhum."*

*Ee Allah, wape baraka kwa hicho ulicho wapa, wasamehe na warehemu."*

## **26. Dua ya kuleta baada ya kupiga chafya**

Unapopiga chafya hunabudi kusema:

الْحَمْدُ لِلَّهِ.

*"Al-hamdulillaahi"*

*"Sifa zote anastahiki Allah."*

Kisha ndugu zako Waislamu watasema:

يَرْحَمُكَ اللَّهُ

*"Yar-hamuka (ki\*) llahu."*

*"Allah akurehemu."*

Kisha utajibu kwa kusema:

يَهْدِيكُمْ اللَّهُ وَيُصْلِحُ بِالْكُم

*"Yah-diykumullahu wayusw-lihi baalakum."*

*"Allah akuongozeni na kuwasahilishia mambo yenu."*

## **27. Dua ya kuwaombea maharusi (waliooana)**

بَارَكَ اللَّهُ لَكَ، وَبَارَكَ عَلَيْكَ،  
وَجَمَعَ بَيْنَكُمَا فِي خَيْرٍ.

*"Baarakallahulaka, wabaaraka a'layka, wajama-a'baynakumaa fiy khayrin"*

*"Allah akubariki wewe na yeye (mkeo/mumeo) na awaunganishe katika kheri."*

## 28. Dua ya kuleta unapoanza kufanya tendo la ndoa

بِسْمِ اللَّهِ اللَّهُمَّ جَنِّبْنَا الشَّيْطَانَ  
وَجَنِّبِ الشَّيْطَانَ مَا رَزَقْتَنَا.

*"Bismillahi Allahumma jannib-nashshay-twaana wajannibish-shytwaana maarazaq-tanaa".*

*"Kwa jina la Allah, Ee Allah muweke shetani mbali nasi na muweke shetani mbali na hicho ulichoturuzuku."*

## 29. Dua ya kuleta unapopandwa na hasira

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ.

*"Au'udhubillaahi minash-shaytwaani rrajiimi"*

*"Najikinga kwa Allah na shetani aliyelaaniwa."*

## 30. Dua ya kuleta mwisho wa kikao (mkutano)

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ أَشْهَدُ أَنْ  
لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُوبُ  
إِلَيْكَ.

*"Sub-haanaka lllahumma wabihamdika, ash-hadu an-laa ilaha illa anta as-taghfiruka wa-atuubu ilayka."*

*"Utukufu ni wako, Ee Allah, nakutukuza. Ninashuhudia kuwa hapana Mola ila wewe. Nakuomba msamaha na ninatubia kwako."*

### 31. Dua unayomuomba yule aliyekufanyia jambo zuri

جَزَاكَ اللَّهُ خَيْرًا.

*"Jazaka llahu khayran"*

*"Allah akulipe kheri."*

### 32. Dua ya kuomba kuepushwa na shirk

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ أَنْ أُشْرِكَ بِكَ  
وَأَنَا أَعْلَمُ وَأَسْتَغْفِرُكَ لِمَا لَا أَعْلَمُ.

*"Allahumma inniy au'udhubika an-ush-rika bika waanaa-aa'lamu, wa-astagh-firuka limaa laa-aa'lamu."*

*"Ewe Allah, najikinga kwako nisikushirikishe huku nikijua na naomba unisamehe kwa lile (baya) nitakalolifanya bila kujua."*

### 33. Dua ya kupokelea sadaqa au zawadi

بَارَكَ اللَّهُ فِيكُمْ.

*"Baarakallahu fiyikum."*

*"Baraka za Allah ziwe juu yenu."*

و فِيهِمْ بَارَكَ اللَّهُ.

*Na aliyetoa zawadi/swadaqa na akaombewa hivi atajibu*

*"Wafiyhim baarakallahu."*

*"Pia Allah awabariki."*



mnyama), na hatukuwa sisi kwako ni wenye uwezo, na sisi kwa Mola wetu tutarejeshwa. Ee Allah, hakika sisi tunakuomba katika safari yetu hii wema na ucha Mungu, na katika matendo unayoridhia, Ee, Allah ifanye nyepesi safari yetu hii na ufupishe umbali wake. Ee Allah, wewe ndie mwenzangu katika safari na mchungaji wa familia yangu.

### 36. Dua ya kupokea habari ya kufurahisha

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي بَعَثَنِي فِي الْمَوَالِكِ

“Al-hamdulillahilladhiy bina-a'matihi tatimmu sw-swaalihaatu.”

“Shukurani zote anastahiki Allah ambaye kwa neema yake hizi nzuri imekamilika.”

### 37. Dua ya kupokea habari za kuhuzunisha

الْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى كُلِّ حَالٍ.

“Al-hamdulillahi a'laa kulli haali”

“Shukurani zote anastahiki Allah kwa hali zote.”

### 38. Dua ya kuingia sokoni

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ يُحْيِي  
وَيُمِيتُ وَهُوَ حَيٌّ لَا يَمُوتُ بِيَدِهِ الْخَيْرُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Laa illaaha illa Ilaahu wah-dahu laashariikalahu, lahul-mulku walahul-hamdu, yuh-yi' wayumiitu wahuwa hayyun laa yamuutu wahuwa a'laa kullishay-in qadiiru.”

“Hakuna Mola ila Allah aliye mpweke, hana mshirika, ni wake ufalme, na ni zake sifa njema, anahuisha na anafisha, naye ni hai asiyekufa, kheri iko mikononi mwake, na yeye juu ya kila kitu ni muweza.”



### 39. Uhora wa kusalimiana

Mtume (s.a.w) amesema

*"Hamtoingia peponi mpaka muamini na hamtaweza kuamini mpaka mpendane. Je, nikufahamisheni jambo ambalo mkilifanya mtapendana? Jambo hili ni kutoleana salaamu."*

*(Muslim)*

*Ukamilifu wa salaamu ya Kiislamu ni*

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

*"Assalaamu a'laykumu Warahmatullahi wabarakaatuhu."*

*"Amani ya Allah, Rehema zake na Baraka zake ziwe juu yenu."*

*Anayesalimiwa analazimika kujibu kwa kusema:*

وَعَلَيْكُمْ السَّلَامُ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

*"Waa'laykumu ssalaamu warahmatullahi wabarakaatuhu."*

*"Nanyi pia amani ya Allah, Rehema zake na Baraka zake ziwe juu yenu."*

### 40. Uhora wa kumkumbuka na Kumtukuza Allah wakati wa mapumziko

*A'bdullaah Ibn Qays (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) alimuuliza: "Ee 'Abdullah Ibn Qays, ni kufahamishhe hazina miongoni mwa hazina za Peponi? Kisha Mtume (s.a.w) akamwambia sema:*

لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ.

*"Laa haula walaquwwata illaabillahi."*

*"Hapana uwezo wala nguvu ila kutoka kwa Allah."*

*(Bukhari na Muslimu)*

Mtume (s.a.w) amesema, maneno anayopenda Allah kuliko yote ni manne

سُبْحَانَ اللَّهِ، وَ الْحَمْدُ لِلَّهِ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ.

*“Sub-hanallahi, Wal-hamdulillahi, Walaa ilaaha illallaahu, Wallaahu Akbaru.”*

*“Utukufu ni wa Allah, shukurani zote anastahiki Allah, Hapana Mola ila yeye, Allah ni Mkubwa.” (Muslimu)*

*Abu Hurayrah (r.a) ameeleza kuwa: Mtume (s.a.w) amesema, "Kuna maneno mawili (2) ambayo ni mepesi katika ulimi na mazito katika mizani na anayopenda Allah, nayo ni:*

سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ وَسُبْحَانَ اللَّهِ الْعَظِيمِ.

*“Sub-haanallahi wabihamdihi, wasubuhaana llaahil-a'dhiim.”*

*“Utukufu ni wa Allah na shukrani zote anastahiki yeye. Utukufu ni wa Allah aliye mkuu.” (Bukhari na Muslimu)*

*Jabir Ibn Abdullah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Hakika dua kubwa ni kusema:*

الْحَمْدُ لِلَّهِ

*“Al-hamdulillaahi”*

*“Shukurani zote anastahiki Allah.”*

Na hakika namna bora ya kumkumbuka Allah (dhikri) ni kusema:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

*“Laailahailla llaaha.”*

*“Hapana Mola ila Allah.” (Ahmad)*

Mtume (s.a.w) amesema, amali njema ya kudumu ni kusema:

سُحَانَ اللَّهِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ  
وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ.

*“Sub-haanallahi, wal-hamdulillaahi, walaailaha illallaahu walaahu akbaru walaahawla walaaquwwata illaabillaahi.”  
Utukufu ni wa Allah na shukurani zote anastahiki Allah, na Hapana Mola ila Allah na Allah ni mkubwa. Hapana uwezo wala nguvu ila kutoka kwa Allah.”*

#### **41.Dhikri ya kuleta wakati wa kulala**

Alikuwa Mtume (s.a.w) akienda kulala usiku, akiweka pamoja viganja vyake kisha akivipulizia na akivisomea suratul-Ikhlis, suratul Falaq na Suratun-Naas, kisha akipangusa kwa hivyo viganja vyake kiasi anachoweza katika mwili wake, akianza kichwani, usoni na mbele (akifanya hivyo mara tatu.) (Bukhari na Muslimu)

*Mtume (s.a.w) amesema: "Ukienda kulala soma Ayatul-kursiyyu kwani Allah ataendelea kukuhifadhi, wala hakukaribii shetani mpaka asubuhi." (Al-Bukhari)*

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لَا تَأْخُذُهُ سِنَّةٌ وَلَا نَوْمٌ لَهُ مَا فِي  
السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ  
مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ  
وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيُّ  
الْعَظِيمُ

*Mwenyezi Mungu, hakuna Mola ila yeye, ndiye mwenye uhai wa milele, msimamia kila jambo. Kusinzia hakumshiki wala*

*kulala. Ni vyake (peke yake vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao (viumbe) na (yaliyo) nyuma yao; wala (hao viumbe) hawalijui lolote katika ilimu yake ila kwa alipendalo. Enzi yake imeenea mbinguni na ardhini, wala kuvilinda hivyo hakumshindi; Na yeye (pekee) ndiye aliye juu na ndiye aliye mkuu." (2:255)*

Alikuwa Mtume (s.a.w) akitaka kulala, anaweka mkono wake wa kulia chini ya shavu lake, kisha anasema:

اللَّهُمَّ قِنِي عَذَابَكَ يَوْمَ تَبْعَثُ عِبَادَكَ. ( ثلاثاً )

***"Allahumma qiniy a'dhaabaka yaumatab-a'thu i'baadaka."***

***"Ee! Allah nikinge mimi kwa adhabu yako siku utakapowafufua waja wako."***

Pia Mtume (s.a.w) wakati wa kulala alikuwa akisema:

بِسْمِكَ اللَّهُمَّ أَمُوتُ وَأَحْيَا.

*"Allahumma Bismika amuutu wa-ahyaa.*

*"Kwa jina lako, Ee Allah ninakufa na nina kuwa hai."*

## Zoezi la 5

1. Eleza umuhimu wa kuleta dhikiri/dua katika kila jambo unalolifanya.
2. Hifadhi dhikiri/dua tatu kila siku na ziingize katika utekelezaji.

---

---

سُبْحَانَكَ لَا عِلْمَ لَنَا إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ

*Utukufu ni wako! Hatuna elimu isipokuwa  
ile uliyotufundisha; bila shaka  
wewe (Allah) ndiye  
Mjuzi na ndiye  
Mwenye hikima (2:32)*

---